

SAUTI KATIKA USEMI NA WIMBO



- 

1 Sikiliza, Sikiliza, Sikiliza
- 

2 Weka umakini
- 

3 Ondoa vurugu
- 

4 Lugha ya maneno
- 

5 Lugha ya mwili na mwonekano
- 

11 Jali mahusiano
- 

12 Je, Unazungumza mbele ya umati wa watu?
- 

13 Usizungumze kwa haraka sana
- 

10 Usihukumu watu kabla ya kutoa ombi moyoni
- 

9 Usimalizie sentensi za wengine
- 

8 Je, ni nani unayezungumza naye?
- 

7 Uliza maswali
- 

6 Changamka-Ucheshi
- 

14 Fikiri kabla ya kuzungumza.



MaarifaMtandaoni.com | SamaritanLaymenMinistries.Org

SAUTI KATIKA USEMI NA WIMBO

Formatted: Centered

Nhandi Masunga na Grace Momadi Masaka-Jersey 2026 July

Shukurani Kwa Mwenyezi Mungu, Watafsiri, Waombezi,
Wahariri, Wahakiki Washauri, Wataalamu wa Teknolojia, na Watia Moyo Wote

Formatted: Font: 10 pt

1. Grace Momadi-Masaka-Jersey, Marekani
2. Nhandi Masunga, Mpwapwa, Tanzania
3. Sharon Ondieki, Nairobi, Kenya
4. E Masige-Nairobi, Kenya
5. Daudi na Denis Masaka-Carolina, Marekani
6. Daniel Masaka-Kisii, Kenya
7. Sandra Barron-Carolina, Marekani
8. Judi Mmari Mugane-Boston, Marekani
9. John Mugane-Boston, Marekani

Nhandi Masunga na Grace Momadi Masaka-Jersey 2026 July

|

Formatted: Normal (Web), Left, Indent: Left: 0.91",
Line spacing: At least 24.9 pt, Pattern: Clear (White)

Utangulizi

Elimu rasmi ya Ellen White ilikoma alipokuwa na umri wa miaka tisa tu; hivyo hakuwahi kupata fursa ya kufundishwa na wataalamu wa usemi na sauti wa wakati wake. Hata hivyo, akiwa amefundishwa na Bwana, alikuja kuwa mmoja wa wanawake wahubiri mashuhuri zaidi nchini Amerika. Kwa zaidi ya miaka sabini, muda mrefu kabla ya kuwapo kwa vipaza sauti na mifumo ya matangazo ya hadhara, alihutubia hadhira zenye watu wapatao 20,000. {VSSsw 5.2}

Akiwa tayari sikuzote kuzungumza, hasa kuhusu mada ya kiasi, alisema, “Ninapombwa kuzungumza kuhusu kiasi, sijawahi kusita.” (MS 31, 1911). Wakati mmoja alikutana na ushindani kutoka kwa circus/Sarakasi ya Barnum huko Battle Creek, Michigan, kwa kutoa hotuba ya dakika tisini kuhusu kiasi mbele ya wasikilizaji 5,000 waliokuwa na shauku. Alihutubia katika ukumbi wa jiji huko Haverhill, Massachusetts; katika gereza huko Salem, Oregon; juu ya jukwaa la muda lililoundwa kwa meza za bia nchini Norway; na katika mikutano ya wazi, makanisani, kumbi za mikutano, na mahema katika mabara matatu. Alikuwa akialikwa mara kwa mara kuwa mnenaji katika mikutano ya kambi. Ellen White alikuwa mhubiri wa injili mwenye uwezo mkubwa- [Sarakasi ya marekani enzi zile ilikuwa waigizaji, watumbuizaji ambao wana wachekeshaji waliovaa na kwa namna ya vituko hivi, na wanasarakasi, na wanyama waliofunzwa, na vyuma vya kupanda, miziki, wacheza dansi, waruka viunzi, watembeaji kwenye kamba, watu wa mazingaombwe yaani wachawi, watu wanaotupa vitu kadhaa na kudaka, wanyama walioshonwa ambao wanazungumza, Waendesha baiskeli, na wataenda sehemu mbali mbali na kupiga kambi na kulipwa kwa huduma zao, watumbuizaji hawa, hii ndiyo ilikuwa kazi au taaluma yao ya maisha/A circus is a company of

performers who put on diverse entertainment shows that may include clowns, acrobats, trained animals, trapeze acts, musicians, dancers, hoopers, tightrope walkers, jugglers, magicians, ventriloquists, and unicyclists as well as other object manipulation and stunt-oriented artists. The term "circus" also describes the field of performance, training, and community which has followed various formats through its 250-year modern history. who put on diverse entertainment shows that may include clowns, acrobats, trained animals, trapeze acts, musicians, dancers, hoopers, tightrope walkers, jugglers, magicians, ventriloquists, and unicyclists as well as other object manipulation and stunt-oriented artists. The term "circus" also describes the field of performance, training, and community which has followed various formats through its 250-year modern history.]{VSSsw 5.3}

Isingekuwa kwa vitabu vyake, bila shaka Ellen White angekumbukwa zaidi leo kwa huduma yake ya mimbarani. Lakini hakufanya kazi ya kuhubiri tu; aliandika pia—kwa wingi. Takriban vitabu 70 vinavyochapishwa kwa sasa vinabeba jina lake kama mwandishi. Karibu vyote vimeuzwa kwa makumi ya maelfu ya nakala, na baadhi yake hata kwa mamilioni ya nakala. Kitabu hiki kinajiunga na orodha hiyo ndefu ya vitabu vilivyopata mafanikio makubwa katika mauzo. **Kitakaribishwa na wachungaji, walimu, wanamuziki, na wengine wote wanaojishughulisha kwa namna ya pekee na matumizi sahihi ya sauti.** {VSSsw 5.4}

Mashauri yaliyochapishwa humu yametolewa na Mungu; ni ya kuaminika na yanastahili kutegemewa. Kitabu hiki kinatolewa pamoja na maombi kwamba kitawaletea baraka wote wanaotafuta kuboresha kipawa chao cha sauti kwa utukufu wa Mungu na kwa manufaa ya wanadamu. {VSSsw 6.1}

Nhandi Masunga na Grace Momadi Masaka-Jersey 2026 July



Ulimwengu wa Kiswahili una uhaba wa vitabu ambavyo ni msaada kwa maisha ya siku kwa siku, jiunge kutafsiri au kuandika, maana sasa ndiyo ulimwengu wa watu wanaomwamini Mungu wa Mbinguni, kuliko mahali pengine duniani, yaani Afrika ni bara la watu wanaomwamini Mwenyezi Mungu, kuliko

bara lolote duniani sasa! Tunaitaji kulishwa kwa Neno, na pia kuishi mtindo wa maisha unaoendana na wito huu!

Wadhamini wa Hazina ya Ellen G. White

YALIYOMO

SURA YA 1—KIPAWA CHA MBINGUNI.....	7
SURA YA 2—KUSUDI LA MAWASILIANO.....	10
SURA YA 3—CHOMBO CHA UINJILISTI.....	14
SURA YA 4—UMUHIMU WA ELIMU YA USEMI.....	19
SURA YA 5—WAJIBU WA WAZAZI.....	21
SURA YA 6—WAJIBU WA WALIMU.....	23
SURA YA 7—WANAFUNZI NA USEMI.....	27
SURA YA 8—USHAWISHI WA MANENO.....	31
SURA YA 9—USHAWISHI KUPITIA USEMI.....	39
SURA YA 10—KUTUMIA VIBAYA KIPAWA CHA USEMI.....	42
SURA YA 11—ASILI YA SAUTI YAKE.....	45
SURA YA 12—UFANISI WA UWASILISHAJI.....	48
SURA YA 13—UPENDO, HURUMA, NA FADHILI.....	51
SURA YA 14—UTULIVU WA SUBIRA.....	53
SURA YA 15—URAHISI.....	54
SURA YA 16—NGUVU, MAMLAKA, NA BIDII.....	57
SURA YA 17—MANENO YA KWELI.....	61
SURA YA 18—HAKUNA HOJA CHANGAMANO WALA MIJADALA MIREFU.....	63
SURA YA 19—KRISTO ALIVYOCHUNGUZA NYUSO ZA WATU.....	64

SURA YA 20—KUZOEWA MAHITAJI YA WASIKILIZAJI WAKE.....	66
SURA YA 21—MIFANO, ISHARA, NA TAMATHALI ZA USEMI.....	68
SURA YA 22—KIELELEZO CHA MTENDAKAZI.....	71
SURA YA 23—UFUNUO WA KRISTO.....	73
SURA YA 24—UNYENYEKEVU, UKWELI, NA BUSARA.....	77
SURA YA 25—AINA ZA USEMI HASI.....	79
SURA YA 26—UPENDO NA FADHILI.....	85
SURA YA 27—ATHARI ZA MANENO JUU YA MWENYEWWE.....	88
SURA YA 28—UTAMBUZI KATIKA KUKEMEA.....	91
SURA YA 29—SIFA NA SHUKRANI.....	97
SURA YA 30—UANGALIFU KATIKA KUSEMA JUU YA WENGINE.....	99
SURA YA 31—TUMAINI NA KUTIA MOYO.....	102
SURA YA 32—IMANI IWE MADA YA MAZUNGUMZO.....	107
SURA YA 33—UNYENYEKEVU KATIKA USEMI WETU.....	109
SURA YA 34—UMUHIMU WA MADA HII.....	113
SURA YA 35—UWAZI NA USAFI WA MATAMSHI.....	118
SURA YA 36—UMUHIMU WA AFYA YA JUMLA.....	125
SURA YA 37—MATUMIZI SAHIHI YA SAUTI.....	127
SURA YA 38—UPENDO NA WEMA.....	133
SURA YA 39—URAHISI NA UWAZI.....	138
SURA YA 40—LUGHA SAFI.....	144
SURA YA 41—BIDII NA UHAKIKA.....	146
SURA YA 42—MTINDO WA MAZUNGUMZO.....	151
SURA YA 43—HAKUNA MANENO MAKALI WALA ROHO YA MABISHANO.....	155

SURA YA 44—UFUPI.....	161
SURA YA 45—KASI NA MKUNJO WA SAUTI.....	169
SURA YA 46—VISA NA UCHESHI.....	177
SURA YA 47—MIFANO NA VIFAA VYA KUONEKANA.....	182
SURA YA 48—UWASILISHAJI WA HOTUBA ZA UFASAH NA MAONYESHO YA KIMAIGIZO.....	187
SURA YA 49—HATARI YA HISIA ZILIZOZIDI KIASI.....	192
SURA YA 50—KUSIKIKA, LAKINI SI KWA KUPAZA SAUTI.....	195
SURA YA 51—USTAARABU NA UZITO WA MWENENDO.....	198
SURA YA 52—KILA MTU NI WA PEKEE.....	199
SURA YA 53—USHAHIDI HALISI WA MAHUBIRI.....	200
SURA YA 54—KRISTO NDIYE JUMLA NA KIINI.....	206
SURA YA 55—AHADI YA ROHO MTAKATIFU.....	210
SURA YA 56—KWELI YA MILELE.....	212
SURA YA 57—KWELI ZINAZOJARIBIWA.....	216
SURA YA 58—KUJA KWA YESU HIVI KARIBUNI.....	223
SURA YA 59—NJIA YA WOKOVU.....	225
SURA YA 60—UCHAJI WA MUNGU UNAOTUMIKA KATIKA MAISHA.....	230
SURA YA 61—WANAUME NA WANAWAKE WA BIBLIA	233
SURA YA 62—WANAMATENGENEZO WA ZAMA ZA KATI.....	253
SURA YA 63—WAANZILISHI WA KIADVENTISTA.....	259
SURA YA 64—NGUVU YA WIMBO.....	272
SURA YA 65—UIMBAJI WA KRISTO.....	276
SURA YA 66—MALEZI YA SAUTI NA UIMBAJI.....	278
SURA YA 67—MATUMIZI MABAYA YA SAUTI KATIKA MUZIKA.....	280

Nhandi Masunga na Grace Momadi Masaka-Jersey 2026 July

SURA YA 68—UIMBAJI UNAOMTUKUZA MUNGU.....	287
SURA YA 69—WIMBO NI SEHEMU YA IBADA.....	291
SURA YA 70—UIMBAJI KAMA NJIA YA USHUHUDA.....	297
SURA YA 71—UIMBAJI KATIKA UZOEFU WA ISRAELI.....	299
SURA YA 72—WIMBO KATIKA UFUFUO NA KUPAA KWA KRISTO.....	308
SURA YA 73—WIMBO KATIKA PAMBANO KUU LA MWISHO.....	310
SURA YA 74—NYIMBO ZA WALIOKOMBOLEWA.....	312

SEHEMU YA 1—KARAMA ITOKAYO KWA MUNGU

SURA YA 1—KIPAWA CHA MBINGUNI

Baraka Kuu kwa Ajili ya Mema—Uwezo wa kusema au kuzungumza, ni kipawa ambacho kinapaswa kukuzwa/kupaliliwa kwa bidii. Miongoni mwa karama zote tulizopokea kutoka kwa Mungu, hakuna inayoweza kuwa baraka kubwa zaidi kuliko hii. Kwa sauti tunasadikisha na kuwashawishi wengine; kwa sauti hiyo tunamtolea Mungu maombi na sifa; na kwa sauti hiyo tunawaeleza wengine kuhusu upendo wa Mkombozi. Basi, ni muhimu jinsi gani sauti zetu/hiyo ifundishwe na kukuzwa ili itumike kwa ufanisi mkubwa zaidi kwa ajili ya mema. —*Mifano ya Masihi*, uk. 335. {VSSsw 13.1}

Sauti na Ulimi ni Karama za Mungu—Sauti na ulimi ni karama zitokazo kwa Mungu, na zikitumiwa ipasavyo, huwa nguvu katika kazi ya Mungu. Maneno yana maana kubwa sana. Yanaweza kueleza upendo, kujitoa wakfu, kujitolea, sifa, na nyimbo za kumsifu Mungu, au chuki na visasi. Maneno hufunua hisia za moyo. Yaweza kuwa harufu ya uzima iletayo uzima, au harufu ya mauti iletayo mauti. Ulimi ni ulimwengu wa baraka, au ulimwengu wa uovu. —*The SDA Bible Commentary*, juzuu la 3, uk. 1159. {VSSsw 13.2}

Nguvu Katika Kuwasilisha Maarifa—Tunaweza kuwa na maarifa, lakini tusipojua jinsi ya kuitumia sauti kwa usahihi, kazi yetu haitafanikiwa. Tusipoweza kuyavika mawazo yetu katika lugha inayofaa, elimu yetu itakuwa na faida gani? Maarifa hayatakuwa na manufaa makubwa kwetu isipokuwa tukikuza kipawa cha usemi; lakini huwa nguvu ya ajabu yanapounganishwa na uwezo wa kusema maneno ya hekima na yenye msaada, na kuyasema kwa namna itakayovuta usikivu wa wasikilizaji. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juzuu la 6, uk. 380. {VSSsw 13.3}

Mvuto wa Hisia za Ndani na Mguso wa Moyo—Haidhuru maarifa ya mtu ni makubwa kiasi gani, hayana faida yoyote ikiwa hawezi kuyawasilisha kwa wengine. Achia hisia za ndani za sauti yako ziguse mioyo ya wasikilizaji. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juzuu la 7, uk. 268. {VSSsw 14.1}

Amana Takatifu—Karama ya usemi ni kipawa cha thamani. Kamwe usiidharau wala usiipuuze karama hii. Mshukuru Mungu kwa kukuaminisha karama hiyo. Ni kipawa cha thamani kinachopaswa kutakaswa, kuinuliwa, na kupewa hadhi

inayostahili. Kwa kuwa ni amana takatifu, sauti inapaswa kutumiwa kwa kumheshimu Mungu. Kamwe sauti isitamke maneno makali, machafu, au ya kulaumu. Injili ya Kristo inapaswa kutangazwa kwa sauti. {VSSsw 14.2}

Kutumia Kipawa cha Usemi Kuwasilisha Ukweli—Kwa kipawa cha usemi tunapaswa kuwasilisha ukweli kila tupatapo fursa. Kipawa hiki kinapaswa kutumiwa daima katika utumishi wa Mungu; lakini kinatumiwa vibaya sana. Maneno yanayosemwa husababisha madhara makubwa. Kristo alisema, “*Basi, nawaambia, Kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu. Kwa kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa.*” (Mathayo 12:36, 37). —*Manuscript* 21, 1899. {VSSsw 14.3}

Nguvu ya Roho Mtakatifu Katika Kukuza Sauti—Watie moyo wote watumie lugha rahisi, safi, na yenye hadhi. Usemi, matamshi, na sauti—vikuzeni vipawa hivi, si chini ya mafunzo ya mtaalamu wa sanaa ya usemi wa ulimwengu huu [elocutionist], bali chini ya uweza wa Roho Mtakatifu wa Mungu. —*Letter* 83, 1898. {VSSsw 14.4}

Ujasiri, Uchangamfu, na Tumaini—Zungumzeni juu ya wema na upendo wa Yesu. Mimi na wewe tumepewa baraka ya usemi, ambayo ni kipawa chenye thamani kubwa. Kitumieni kuzungumzia mambo yanayokuza upendo kwa Yesu. Na tuzungumzie rehema Zake na maneno ya neema aliyoyasema ili kutia moyo, kufariji, na kuleta tumaini, furaha, na upendo mioyoni mwetu. ... Na tuyapambe maisha yetu yaliyosalia kwa maneno yanayoleta ujasiri, uchangamfu, na tumaini. Adui ataweka kivuli chake kati ya Kristo na nafsi zetu. Atatujaribu tuzungumze kwa mashaka na kwa kukosa imani. Lakini mawazo yasiyofaa yanapotafuta kutamkwa, msiyaruhusu yatoke. Semeni kwa imani. Zungumzeni juu ya neema ya Bwana na Mwokozi wetu, juu ya upendo Wake na rehema Zake, na juu ya uzuri wa tabia Yake. Midomo yenu na izoe kutamka mawazo yenye thamani na yenye kutia moyo. —*Letter* 14, 1900. {VSSsw 15.1}

Uongofu wa Ulimi—Ulimi ni kiungo kisichotawalika, lakini haupaswi kuwa hivyo. Unapaswa kuongoka, kwa maana kipawa cha usemi ni kipawa chenye thamani kubwa sana. Kristo daima Yuko tayari kutushirikisha utajiri Wake, nasi

tunapaswa kukusanya vito vitokavyo Kwake, ili tunapozungumza, vito hivyo vidondoke kutoka midomoni mwetu. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juzuu la 6, uk. 173–174. {VSSsw 15.2}

Chombo Katika Kuendeleza Ufalme Wake—Usemi ni kipawa, na unaweza kutumiwa kumheshimu au kumvunjia Mungu heshima. Tunawajibika kwa matumizi yetu ya kipawa cha maneno. ... Kipawa cha usemi, cha kumbukumbu, na cha mali—vyote vinapaswa kutumiwa kwa ajili ya utukufu wa Mungu na kuendeleza ufalme Wake. —*Letter* 44, 1900. {VSSsw 16.1}

SURA YA 2—KUSUDI LA MAWASILIANO

Maneno ni Udhihirisho wa Mawazo—Maneno yetu hudhihirisha hali ya mioyo yetu; na iwe watu wanazungumza sana au kidogo, maneno ya watu huonyesha tabia ya mawazo yao. Tabia ya mtu inaweza kutambuliwa kwa usahihi mkubwa kutokana na mazungumzo yake. Maneno yaliyo mema na ya Kweli husikika kuwa ya Kweli. —*Wana na Binti za Mungu*, uk. 180. {VSSsw 17.1}

Mawasiliano na Mungu na Wanadamu—Usemi ni mojawapo ya karama kuu za Mungu. Ni njia ambayo mawazo ya moyoni huwasilishwa. Ni kwa ulimi tunamtolea Mungu maombi na sifa. Ni kwa ulimi tunasadikisha na kuwashawishi wengine. Ni kwa ulimi tunafariji na kubariki, tukituliza nafsi zilizochubuka na kujeruhiwa. Ni kwa ulimi tunaweza kutangaza maajabu ya neema ya Mungu. Lakini pia kwa ulimi tunaweza kutamka mambo yaliyopotoka, tukisema maneno yanayong’ata kama nyoka. {VSSsw 17.2}

Ulimi ni kiungo kidogo, lakini maneno yanayoundwa nao yana nguvu nyingi. Bwana anasema, “*Ulimi hakuna mwanadamu awezaye kuudhibiti.*” Umechochea taifa dhidi ya taifa, na umesababisha vita na umwagaji wa damu. Maneno yamewasha moto ambao umekuwa vigumu kuuzima. Pia yameleta furaha na shangwe katika mioyo ya wengi. Na maneno yanaposemwa kwa sababu Mungu amesema, “*Waambie maneno Yangu,*” mara nyingi huleta huzuni iletayo toba. {VSSsw 17.3}

Ulimi Usiotakaswa—Mtume Yakobo anaandika hivi kuhusu ulimi usiotakaswa: “*Ulimi ni moto; ule ulimwengu wa uovu, ule ulimi, umewekwa katika viungo vyetu, nao huutia mwili wote unajisi, nao huuchoma mwendo wote wa maisha ya mwanadamu, nao huwashwa moto na jehanamu.*” Shetani huingiza akilini mawazo ambayo Mkristo hapaswi kamwe kuyatamka. Majibu ya dharau, maneno makali na yenye hasira, shutuma za kikatili na za kutilia mashaka, hutoka kwake. Ni maneno mengi kiasi gani yanayosemwa ambayo huleta madhara tu kwa wale wanaoyatamka na kwa wale wanaoyasikia! Maneno makali huutandika moyo, yakiamsha hisia mbaya zaidi ndani yake. Wale wanaotenda uovu kwa ndimi zao,

wanaopanda mifarakano kwa maneno ya ubinafsi na wivu, wanamhuzunisha Roho Mtakatifu; kwa maana wanafanya kazi kinyume na Mungu. —*The Review and Herald*, Mei 12, 1910. {VSSsw 18.1}

Nguvu kwa Ajili ya Mema—Mtume, alipoona tabia ya kutumia vibaya kipawa cha usemi, alitoa maelekezo kuhusu matumizi yake. Anasema: “*Neno lolote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji.*” Neno “*ovu*” hapa linamaanisha kila neno ambalo lingelea athari inayodhuru kanuni takatifu na dini isiyo na unajisi; kila mawasiliano yanayoficha mtazamo wa Kristo na kuondoa akilini huruma ya kweli na upendo. Linajumuisha dokezo zisizo safi, ambazo, zisipopingwa mara moja, huongoza kwenye dhambi kubwa. Kila mtu ana wajibu wa kuyazuia mawasiliano maovu yasipate nafasi.... {VSSsw 18.2}

Linda kwa uangalifu kipawa cha usemi; kwa maana ni nguvu kubwa kwa uovu na vilevile kwa wema. Huwezi kuwa mwangalifu kupita kiasi kuhusu yale unayosema; kwa maana maneno unayotamka yanaonyesha ni nguvu gani inayotawala moyo wako. Ikiwa Kristo anatawala humo, maneno yako yatafunua uzuri, usafi, na harufu nzuri ya tabia iliyoumbwa na kufinyangwa kwa mapenzi Yake. Lakini ikiwa uko chini ya uongozi wa adui wa kila jema, maneno yako yataakisi hisia zake. {VSSsw 19.1}

Wajibu mkuu ulioambatana na matumizi ya kipawa cha usemi umewekwa wazi katika Neno la Mungu. Kristo alisema: “*Kwa kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa.*” Naye mtunga zaburi anauliza: “*Bwana, ni nani atakayekaa Katika hema Yako? Ni nani atakayefanya maskani yake Katika kilima chako kitakatifu? Ni mtu aendaye kwa ukamilifu, Na kutenda haki. Asemaye kweli kwa moyo wake, Asiyekingizia kwa ulimi wake. Wala hakumtenda mwenziwe mabaya, Wala hakumsengenya jirani yake. Machoni pake mtu asiyefaa hudharauliwa, Bali huwaheshimu wamchao Bwana Ingawa ameapa kwa hasara yake, Hayabadili maneno yake. Hakutoa fedha yake apate kula riba, Hakutwaa rushwa amwangamize asiye na hatia. Mtu atendaye mambo hayo Hataondoshwa milele.*” (Zaburi 15:1–5). {VSSsw 19.2}

“*Uuzuie ulimi wako na mabaya, Na midomo yako na kusema hila.*” (Zaburi 34:13). Mnyama mkali wa porini anaweza kufugwa, “*Bali ulimi hakuna awezaye kuufuga; ni uovu usiotulia, umejaa sumu iletayo mauti.*” (Yakobo 3:8). Ni kwa njia ya Kristo pekee tunaweza kupata ushindi juu ya mwelekeo wa kusema maneno ya

haraka yasiyofanana na Kristo. Tunapokataa, kwa nguvu Zake, kutoa nafasi kwa mawazo ya Shetani, mmea wa uchungu ulio ndani ya mioyo yetu hunyauka na kufa. Roho Mtakatifu anaweza kuufanya ulimi kuwa harufu ya uzima iletayo uzima. — *The Review and Herald*, Mei 12, 1910. {VSSsw 19.3}

Kielelezo cha Tabia—Maneno yako ni kiashiria cha tabia yako, nayo yatashuhudia juu yako. Hapa tunaona umuhimu wa kuwa waangalifu katika matumizi ya usemi. Kipawa hiki ni nguvu kubwa kwa mema kinapotumiwa kwa usahihi, lakini ni nguvu kubwa vilevile kwa uovu wakati maneno yanayosemwa yanapokuwa yenye sumu. Kipawa hiki kinapotumiwa vibaya, mambo mabaya hutoka moyoni. Maneno huwa ama harufu ya uzima iletayo uzima au ya mauti iletayo mauti.... {VSSsw 20.1}

Je, sisi sote, wazee kwa vijana, hatutajifunza kuzungumza lugha inayozungumzwa na wale watakaotwaliwa katika ufalme wa Mungu? Je, maneno yetu hayatakuwa yale ambayo yatasikika kwa furaha na Baba yetu wa mbinguni? {VSSsw 20.2}

Kwa kuwa tunajiita Wakristo, tuko chini ya wajibu mtakatifu wa kudhihirisha ukweli wa imani yetu kwa maneno yetu. Ulimi ni kiungo kidogo, lakini unaweza kufanya mema makubwa kiasi gani ikiwa moyo ni safi! Ikiwa moyo umejaa mambo mema, ikiwa umejaa upole, huruma, na adabu kama za Kristo, jambo hilo litaonekana katika maneno yanayosemwa na matendo yanayofanywa. Nuru ing'aayo kutoka katika Neno la Mungu ndiyo mwongozo wetu. Hakuna kitu kinachodhoofisha kanisa kama matumizi mabaya ya kipawa cha usemi. Tunamvunja heshima Kiongozi wetu wakati maneno yetu si yale yanayopaswa kutoka katika midomo ya Mkristo. {VSSsw 20.3}

“Utimizezi wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka. Kwa maana Ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi Lake jema.” Ubora wa matendo yetu unaonekana katika maneno yetu. Wakati maneno yetu na matendo yetu yanapopatana ndani ya Kristo, tunaonyesha kwamba tumejiweka wakfu kwa Mungu, tukikamilisha utakatifu katika kumcha Mungu. Tunapojitoa Kwake, nafsi, mwili, na roho, Yeye hufanya kazi ndani yetu, kutaka kwetu na kutenda kwetu kwa mapenzi Yake mema. (Wafilipi 2:12, 13). {VSSsw 21.1}

Upendo wa Kristo ulio moyoni hudhihirishwa kwa njia ya maneno ya sifa. Wale waliojiweka wakfu kwa Mungu wataonyesha jambo hilo kupitia mwenendo wao na mazungumzo yao yaliyotakaswa. Ikiwa mioyo yao ni safi, maneno yao yatakuwa safi, yakionyesha kanuni ya juu inayofanya kazi katika njia iliyotakaswa. Akili itajishughulisha na kutafakari mambo matakafifu, na kutakuwa na ufahamu wa uwepo wa Mungu. —*The Review and Herald*, Januari 18, 1898. {VSSsw 21.2}

Njia ya Kutangaza Upendo wa Mungu—Usemi ni kipawa. Miongoni mwa vipawa vyote alivyokabidhiwa mwanadamu, hakuna kinachopaswa kuthaminiwa zaidi kuliko kipawa cha usemi. Kinapaswa kutumiwa kutangaza hekima ya Mungu na upendo Wake wa ajabu. Kwa njia hiyo, hazina za neema na hekima Yake zinapaswa kuwasilishwa kwa wanadamu. —*Mashauri kwa Uwakili*, uk. 115. {VSSsw 21.3}

Maneno Yenye Kukolezwa na Hekima na Usafi—Kwa maneno yetu tutahesabiwa haki au kuhukumiwa. Wakati wa hukumu ya mwisho tutakapokuwa mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu, maneno yetu ndiyo yatakayotuthibitisha au kutuhukumu. Kuna mambo mengi zaidi yanayohusika katika suala la usemi kuliko tunavyotambua. Acha midomo yako iguswe kwa kaa la moto kutoka madhabahuni pa Mungu. Tamka maneno ya kweli pekee. Kesheni na kuomba, ili maneno na matendo yenu yawe daima ushuhuda wa Kristo. Hebu maneno yako yakolezwe kwa hekima na usafi. —*Letter* 283, 1904. {VSSsw 21.4}

Kuwasilisha Neema ya Kristo—Utajiri wa neema ya Kristo, ambao daima yuko tayari kutujalia, tunapaswa kuuwasilisha kwa maneno ya Kweli na yenye tumaini. “*Furahini katika Bwana sikuzote; tena nasema, Furahini.*” Ikiwa tungeyalinda maneno yetu, ili yasitoke midomoni mwetu isipokuwa maneno ya wema, tungetoa ushahidi kwamba tunajiandaa kuwa washiriki wa familia ya mbinguni. Kwa maneno na matendo yetu tutaonyesha sifa Zake Yeye aliyetuita kutoka gizani kuingia katika nuru Yake ya ajabu. Ni ushawishi mkubwa kiasi gani wa mabadiliko ungetokea ikiwa sisi kama watu tungelithamini kipawa cha usemi kwa thamani yake halisi na kutambua ushawishi wake juu ya nafsi za wanadamu! —*Medical Ministry*, uk. 213. {VSSsw 22.1}

Kushauri, Kutia Moyo, na Kukemea—Kipawa cha usemi tulipewa ili tuzungumze, si maneno ya kulaumu, bali maneno ya kushauri, maneno ya kutia

moyo, na maneno ya kukemea. —*The Review and Herald*, Julai 20, 1905. {VSSsw 22.2}

SURA YA 3—CHOMBO CHA UINJILISTI

Usemi kwa Ajili ya Ushuhuda—Mungu ametupatia kipawa cha usemi ili tuweze kuwaeleza wengine jinsi alivyotutendea, ili upendo na huruma Yake viguse mioyo mingine, na ili sifa pia zipande kutoka katika nafsi za wengine kwenda Kwake Yeye aliyetuita kutoka gizani kuingia katika nuru Yake ya ajabu. Bwana amesema: “Ninyi ni mashahidi Wangu.” (Isaya 43:10). Lakini wote walioitwa kuwa mashahidi wa Kristo wanapaswa kujifunza kutoka Kwake, ili wawe mashahidi wenye ufanisi. Kama watoto wa Mfalme wa mbinguni, wanapaswa kujielimisha ili kutoa ushuhuda kwa sauti iliyo wazi na yenye kueleweka, na kwa namna ambayo hakuna mtu atakayepata wazo kwamba wanasita kueleza rehema za Bwana. —*Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi*, uk. 243. {VSSsw 23.1}

Kuwasilisha Ukweli—Injili ya Kristo inapaswa kutangazwa kwa njia ya sauti. Kwa kipawa cha usemi tunapaswa kuwasilisha Ukweli kila tunapopata nafasi. Kipawa hiki kinapaswa kutumiwa daima katika utumishi (huduma) wa Mungu. —*The Review and Herald*, Septemba 12, 1899. {VSSsw 23.2}

Lugha Sahihi na Sauti Zilizoboreshwa—Laiti wote wangetafuta kwa bidii kuijua kweli, na kujifunza kwa dhati ili wawe na lugha sahihi na sauti zilizoboreshwa, kusudi waweze kuuwasilisha ukweli katika uzuri wake uliotukuka na wenye kuinua. —*Misingi ya Elimu kwa Kila Mwanadamu*, uk. 256. {VSSsw 23.3}

Njia ya Kuwasilisha Maarifa ya Mungu—Uwezo wa usemi ni kipawa cha thamani, na ikiwa uwezo wetu mkuu zaidi, yaani akili, utaelekezwa katika kumjua Mungu, basi kipawa cha usemi kinaweza kuwa njia ya neema kwa wengine, na njia ambayo kupitia hiyo maarifa ya Mungu yanaweza kuwasilishwa. —*Letter 59*, 1895. {VSSsw 24.1}

Njia ya Kumwasilisha Kristo—Mungu aliwapa wanadamu macho ili waweze kuona mambo ya ajabu yaliyomo katika sheria Yake. Aliwapa masikio ya kusikia ili waweze kusikiliza ujumbe Wake unaotolewa na mhubiri aliye hai. Aliwapa wanadamu kipawa cha usemi ili waweze kumwasilisha Kristo kama Mwokozi anayesamehe dhambi. Kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa

kinywa hukiri hata kupata wokovu. —*Nyumba Imngojeayo Masihi*, uk. 401. {VSSsw 24.2}

Njia ya Kukuza Mada Takatifu—Yeye anayefundisha Neno la Mungu anapaswa kukuza uwezo wake wa usemi, ili mada takatifu anazozitungumzia ziwasilishwe kwa namna bora kabisa, ili mafuta ya thamani ya dhahabu yaifanye taa yake kuangaza kwa miale iliyo wazi na dhahiri. Ukweli haupaswi kupoteza nguvu yake wala uzuri wake wa kuvutia kwa sababu ya chombo kinachotumiwa kuuwasilisha. Tunapaswa kutafuta kukuza sifa safi zaidi, za juu zaidi, na za heshima zaidi, ili tuweze kuwakilisha kwa usahihi tabia takatifu na iliyo safi ya kazi na kusudi la Mungu. —*The Review and Herald*, Aprili 20, 1897. {VSSsw 24.3}

Kuendeleza Utukufu Wake—Usemi wako ni kipawa ulichopewa na Mungu, si kwa ajili ya kujifurahisha kwako, bali kwa ajili ya utumishi wa Mungu, ili kitumike kuendeleza utukufu wake kwa matumizi sahihi. —*Letter* 89, 1897. {VSSsw 25.1}

Nguvu Katika Kuwavuta Watu kwa Kristo—Kuna mvuto mkubwa wa hisia na uzuri wa muziki katika sauti ya mwanadamu, na ikiwa mwanafunzi atafanya juhudi za dhati na za kudumu/endelevu, atapata ustadi wa kuzungumza na kuimba utakaokuwa nguvu kwake katika kuwavuta watu kwa Kristo. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 504. {VSSsw 25.2}

Fursa ya Kutumia Usemi—Wakristo wanapaswa kuwa kama Kristo katika shauku yao ya kweli ya kuokoa nafsi. Wanapaswa kuona kuwa ni heshima kuu zaidi kuandikishwa katika jeshi la Kristo. Wanapaswa kumshukuru Mungu kwa fursa ya kutumia kipawa cha usemi katika kuwavuta watu kwa Kristo. Hawapaswi kuona fursa nyingine yoyote kuwa ya thamani zaidi kuliko ile ya kuwashirikisha wanadamu wengine maarifa waliyoyapokea. —*The Review and Herald*, Desemba 24, 1901. {VSSsw 25.3}

Wokovu kwa Ajili ya Majirani Zako—Washiriki wa kanisa, iacheni nuru ing'ae. Hebu sauti zenu zisikike katika maombi ya unyenyekevu, katika ushuhuda dhidi ya kutokuwa na kiasi, mambo ya kipumbavu, na anasa za ulimwengu huu, na katika kutangaza ukweli wa wakati huu. Sauti zenu, ushawishi wenu, na wakati wenu—vyote hivi ni vipawa kutoka kwa Mungu na vinapaswa kutumiwa katika kuwavuta watu kwa Kristo. {VSSsw 25.4}

Watembelee majirani zako na uonyeshe kujali wokovu wa nafsi zao. Amsheni kila nguvu ya kiroho ili itende kazi. **Waambie wale unaowatembelea kwamba mwisho wa mambo yote umekaribia.** Bwana Yesu Kristo atafungua mlango wa mioyo yao na ataacha katika akili zao mvuto wa kudumu.... Maneno yako yenye uchangamfu na moyo wa dhati yatawasadikisha kwamba umepata Lulu ya thamani kuu. Acha maneno yako yenye furaha na kutia moyo yaonyeshe kwamba hakika umeipata njia iliyo bora zaidi. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juzuu la 9, uk. 38. **{VSSsw 26.1}**

Usafi wa Lugha—Unapotafuta kuwavuta wengine katika upeo wa upendo Wake, acha usafi wa lugha yako, kutokuwa na ubinafsi katika huduma yako, na uchangamfu wa mwenendo wako viwe ushuhuda wa nguvu ya neema Yake. Mwakilishe kwa ulimwengu kwa namna safi na ya haki kiasi kwamba watu watamwona katika uzuri Wake. —*Huduma ya Uponyaji*, uk. 156. **{VSSsw 26.2}**

Namna ya Kuzungumza ni Uwakilishi wa Kristo—Kutokana na nuru niliyoipokea, huduma ya kichungaji ni nafasi takatifu na yenye hadhi kuu, na wale wanaokubali nafasi hii wanapaswa kuwa na Kristo mioyoni mwao na kudhihirisha shauku ya kweli ya kumwakilisha kwa kustahili mbele ya watu katika matendo yao yote, katika mavazi yao, katika maneno yao, na hata katika mtindo wao wa kuzungumza. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juzuu la 2, uk. 615. (*Msisitizo umeongezwa.*) **{VSSsw 26.3}**

Kinywa cha Mungu—Mjumbe anayewasilisha Neno la uzima kwa ulimwengu unaoangamia ana wajibu wa kusema kweli. Bwana Yesu Yuko pamoja naye, tayari kupanua mipaka finyu ya maarifa ya kibinadamu, ili wote waweze kuona kwamba mwalimu anawasilisha zawadi ya utajiri usioharibika kwa wote watakaomwamini Kristo. Kuna nguvu ndani ya Kristo ya kuokoa tabia ya kiakili na kimaadili, na kumchonga/kumfinyanga mwanadamu kulingana na mfano wa Mungu. —*The Review and Herald*, Julai 19, 1898. **{VSSsw 26.4}**

Umuhimu wa Busara Katika Kumweleza Mwokozi—Popote tulipo, tunapaswa kutafuta fursa za kuwaeleza wengine kuhusu Mwokozi. Tukifuata mfano wa Kristo katika kutenda mema, mioyo itatufungukia kama ilivyomfungukia Yeye. Si kwa njia ya ghafla, bali kwa hekima na busara vitokanavyo na upendo wa Mungu, tunaweza kuwaeleza habari Zake Yeye aliye “Mkuu kuliko elfu kumi” na ambaye ni “anayependeka kabisa.” Hii ndiyo kazi ya juu kabisa ambayo tunaweza kutumia

kipawa cha usemi kuitimiza. Kipawa hiki tulipewa ili tumwasilishe Kristo kama Mwokozi anayesamehe dhambi. —*Mifano ya Masihi*, uk. 339. {VSSsw 27.1}

Uwasilishaji Sahihi Katika Maneno ya Ukweli—Kujifunza kueleza kwa ushawishi na mguso wa moyo yale anayoyajua mtu ni jambo la thamani ya pekee kwa wale wanaotamani kuwa watenda kazi katika huduma ya Mungu. Kadiri tunavyoweza kuweka nguvu zaidi ya uwasilishaji katika maneno ya ukweli, ndivyo maneno hayo yatakavyokuwa na ufanisi zaidi kwa wale wanaoyasikia. Kuwasilisha kwa usahihi ukweli wa Bwana ni jambo linalostahili juhudi zetu za juu kabisa. —*Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi*, uk. 217. {VSSsw 27.2}

Tumaini kwa Nafsi—Jirani yako ndiye anayepaswa kutafutwa kwa bidii na kuhudumiwa kwa juhudi. Je, hana ufahamu? Acha mawasiliano yako yamfanye awe na ufahamu zaidi. Je, amevunjika moyo na kukata tamaa? Acha maneno yako yalete tumaini katika nafsi yake.... Kwa mvuto wa maneno yanayotoka katika moyo uliojaa upendo, wale waliokata tamaa wanaweza kuwa ushuhuda hai wa ushindi wa neema—warithi wa Mungu, na warithi pamoja na Kristo Yesu. —*The Review and Herald*, Februari 16, 1897. {VSSsw 27.3}

Mawazo Yanayotolewa na Mungu—Ikiwa utaendelea kumjua Bwana na kutenda mapenzi Yake, utajua kwa uzoefu wako kwamba Mungu atakutia mawazo unapojaribu kuzungumza na wale walio karibu nawe, ili kuwazuia wasifanye yaliyo mabaya na kuwaonyesha njia ya uzima. —*Manuscript* 61, 1907. {VSSsw 28.1}

Maneno ya Upole, Yasiyo Makali—Zungumza na nafsi zilizo katika hatari na uzisaidie kumtazama Yesu msalabani, akifa ili iwezekane Kwake kuwasamehe. Zungumza na mwenye dhambi huku moyo wako ukiwa umejaa upendo wa Kristo wenye upole na huruma. Acha kuwe na uzito mkubwa wa moyo na bidii ya kweli; lakini kamwe sauti kali wala ya kelele isisikike kutoka kwa yule anayejitahidi kumvuta mtu amtazame Kristo na kuishi.... {VSSsw 28.2}

Kristo aliyesulubiwa—mzungumzieni, mwombeni, mwimbieni, Naye atavunja ugumu wa mioyo na kuivuta mioyo. Hii ndiyo nguvu na hekima ya Mungu ya kuwakusanya watu kwa Kristo. Misemo iliyokaririwa na iliyowekwa tayari, pamoja na uwasilishaji wa mada kwa mtindo wa hoja za mabishano pekee, huleta manufaa machache sana. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juzuu la 6, uk. 67. {VSSsw 28.3}

Sheria ya Wema Midomoni Mwako—Tafuta njia ya kuwafikia watu wanaoishi katika eneo lako. Unapowaeleza ukweli, tumia maneno yenye huruma ya Kristo.... Usitamke hata neno moja lisilo la fadhili. Acha upendo wa Kristo uwe moyoni mwako, na sheria ya wema iwe midomoni mwako. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juzuu la 9, uk. 41. {VSSsw 28.4}

Maneno ya Upole Kama Manyunyu Madogo—Tunahitaji kuwa na ushirika wa karibu na Mungu, ili ubinafsi usije ukainuka ndani yetu kama ulivyokuwa kwa Yehu, nasi tukatoa mafuriko ya maneno yasiyofaa, yasiyo kama umande wala kama manyunyu ya utulivu yanayohuisha mimea inayonyauka. Maneno yetu na yawe ya upole tunapotafuta kuokoa nafsi. Mungu atakuwa hekima kwa yule anayetafuta hekima kutoka katika chanzo cha Mungu. Tunapaswa kutafuta fursa kila upande. Tunapaswa kukesha katika maombi na kuwa tayari sikuzote kutoa jibu kwa kila mtu anayetaka kujua sababu ya tumaini lililo ndani yetu. Ili tusije tukatoa mvuto usiofaa kwa mtu yeyote ambaye Kristo alimfia, tunapaswa kuinua mioyo yetu kwa Mungu, ili fursa inapojitokeza, tupate neno linalofaa la kusema kwa wakati unaofaa. —*The Review and Herald*, Oktoba 7, 1902. {VSSsw 29.1}

Matendo Yakiambatana na Maneno—Mungu anatamani kwamba baraka nyingi alizowapa kwa hiari watoto Wake ziwafikie wale ambao hawana baraka nyingi za maisha haya. Kupitia kuwashirikisha wengine mambo haya, yaani kwa kutamka maneno ya wema yanayoambatana na matendo ya upendo, wale wanaomtumikia Mungu watapata njia ya kuingia mioyoni mwa watu na kuwavuta wengine kwa Kristo. Sehemu hii ya maisha ya dini hatupaswi kuisahau; “kwa maana sadaka za namna hiyo Mungu hupendezwa nazo.”—*The Review and Herald*, Februari 18, 1902. {VSSsw 29.2}

SURA YA 4—UMUHIMU WA ELIMU YA USEMI

Tawi Muhimu Zaidi—Kipawa cha usemi kinapaswa kujifunzwa na kulindwa kwa uangalifu mkubwa. Hili ndilo tawi muhimu zaidi la elimu, lakini kwa masikitiko limepuuzwa sana katika jumuiya zetu zote. Uwezo wa kuwasiliana na wale tunaoshirikiana nao unaweza kuwa baraka kubwa au laana kubwa. —*Manuscript 77*, 1897. {VSSsw 30.1}

Somo Muhimu Katika Shule Zetu—Elimu ya usemi haipaswi kupuuzwa katika shule zetu. Wale wanaoingia katika jamii wakiwa na shauku na azimio la kuwa vile Kristo alivyowaamuru wawe, hawatakubali kushiriki katika mazungumzo yasiyo ya Kikristo. Watatafuta kumwakilisha Kristo kwa mwenendo wao na kwa maneno yao. —*The Review and Herald*, Januari 25, 1898. {VSSsw 30.2}

Mazungumzo Yaliyotakaswa—Nuru niliyopewa kupitia Neno la Mungu ni kwamba usemi unahitaji kuongolewa na kutakaswa. Bwana anahitaji kwamba watu wafundishwe ustadi wa kuzungumza. Uwezo huu umetumiwa vibaya sana na kupotoshwa. Haujathaminiwa kama kipawa cha thamani kutoka kwa Mungu, kinachopaswa kutumiwa kulitukuza jina Lake. Maneno ni nguvu kwa mema au kwa uovu; ni harufu ya uzima iletayo uzima au ya mauti iletayo mauti. Maneno yaliyochaguliwa kwa uangalifu yanapaswa kusemwa na wale wanaotaka kumtumikia Kristo. Maneno yasiyopangwa, ya haraka-haraka, ya kawaida, na kuzungumza kwa ajili tu ya kuzungumza, wakati ambapo ukimya ungekuwa bora zaidi, ni dhambi. Wale walio na maneno mengi kupita kiasi hawatoi ushawishi wenye afya katika jamii wanamoishi na kushirikiana nayo. Dini ya Biblia haipaswi kuonyeshwa kwa kujisifu, bali inapaswa kudhihirishwa kwa utulivu kupitia maneno mazuri na matendo mema. —*Manuscript 74*, 1897. {VSSsw 30.3}

Usemi Mbaya ni Kosa Linalostahili Nidhamu ya Kanisa—Zingatia maneno haya: “*Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwenu.*” Mkifanya jambo hili, wingi wa maneno yasiyo na wema wala faida hayatatoka midomoni mwenu. “*Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwenu; ndiyo mliyoitiwa katika mwili mmoja; tena iweni watu wa shukrani. Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwambia Mungu kwa neema mioyoni mwenu. Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye.*” **Wakolosai 3:15-17** {VSSsw 31.1}

Haya ndiyo mafunzo tunayohitaji katika shule zetu. Matumizi ya haraka-haraka na yasiyo ya uangalifu ya kipawa cha usemi ndiyo chanzo cha karibu matatizo yote yaliyopo katika makanisa. Usemi mbaya unapaswa kushughulikiwa kama kosa la kinidhamu linaloweza kupelekea kesi ya kanisa na kutengwa na ushirika wa kanisa ikiwa mtu ataendelea katika mwenendo huo; kwa maana kanisa haliwezi kuwekwa katika utaratibu kwa njia nyingine yoyote. —*Manuscript* 74, 1897. {VSS^{sw} 31.2}

Sayansi ya Mazungumzo Inayohusiana na Kujifunza Neno la Mungu—Elimu yetu kuhusu sayansi ya mazungumzo itaboreshwa kwa kila namna ikiwa tutalifanya Neno la Mungu kuwa somo letu. Tawi hili la elimu limepuuzwa sana. Wengi hupokea vyeti kutoka vyuoni bila kuwa wamevipata kwa kupata elimu kamili na yenye uwiano katika nyanja zote. Walimu na wanafunzi mara nyingi hupuuza jambo muhimu la elimu ya usemi. Kwa kukosa mafunzo katika eneo hili, wanafunzi hupoteza mengi. Hutoka shuleni wakiwa na upungufu huo unaoendelea kuonekana katika uzoefu wao wote wa maisha. —*Manuscript* 74, 1897. {VSS^{sw} 31.3}

SURA YA 5—WAJIBU WA WAZAZI

Nyumbani ni Shule ya Kukuza Usemi—Ni kazi ya wazazi kuwafundisha watoto wao mazoea yanayofaa ya usemi. Shule bora kabisa ya kujifunzia ustadi huu ni maisha ya nyumbani. Tangu wakiwa wadogo kabisa, watoto wanapaswa kufundishwa kuzungumza kwa heshima na upendo kwa wazazi wao na wao kwa wao. Wanapaswa kufundishwa kwamba ni maneno ya upole, ya kweli, na yaliyo safi pekee yanayopaswa kutoka midomoni mwao. Wazazi wenyewe na wawe wanafunzi wa kila siku katika shule ya Kristo. Kisha, kwa mafundisho na kwa mfano, wataweza kuwafundisha watoto wao matumizi ya “maneno yenye uzima, yasiyoweza kulaumiwa.” (**Tito 2:8**). Huu ni mojawapo ya wajibu wao mkubwa na wenye uzito zaidi. —*Mifano ya Masihi*, uk. 337–338. {VSS^{sw} 33.1}

Wajibu wa Wazazi na Wajibu wa Mungu—Akina baba na akina mama, mna kazi takatifu na yenye uzito mkubwa ya kufanya. Wokovu wa milele wa watoto wenu unategemea mwenendo wenu. Mtafauluje kuwaelimisha watoto wenu? Si kwa kuwakemea kila wakati, kwa maana jambo hilo halitawaletea manufaa. Zungumzeni na watoto wenu kana kwamba mnauamini uwezo wao wa kufikiri. Shughulikeni nao kwa wema, upole, na upendo. Waambieni yale ambayo Mungu anataka wayafanye. Waambieni kwamba Mungu anataka wafundishwe na kulelewa ili wawe watenda kazi pamoja Naye. Mkitekeleza sehemu yenu, mnaweza kumtumaini Bwana atekeleze sehemu Yake. —*Mwongozo wa Malezi kwa Mtoto na Mzazi*, uk. 33. {VSS^{sw} 33.2}

Kufundisha Mazoea Sahihi ya Usemi—Maelekezo yanapaswa kutolewa daima ili kuwahimiza watoto kujenga mazoea sahihi ya usemi, matumizi ya sauti, na mwenendo. —*Misingi ya Elimu ya Kwa Kila Mwanadamu*, uk. 267. {VSS 34.1}

Mwanga wa Jua au Vivuli—Ni muhimu watoto na vijana wafundishwe kulinda maneno na matendo yao; kwa maana mwenendo wao huleta mwanga wa jua au vivuli, si nyumbani mwao tu, bali pia kwa wote wanaokutana nao. —*Nyumba Inayomngojea Masihi*, uk. 437. {VSS 34.2}

Viungo vya Usemi ni Chombo Hai—Mojawapo ya matawi bora na yenye kuinua zaidi ya elimu ni kujifunza jinsi ya kuzungumza na watu wa nyumbani, ili ushawishi wa maneno yanayosemwa uwe safi na usio na upotovu. Mazungumzo yanayofaa kwa Mkristo ni yale yanayomwezesha kubadilishana mawazo na

wengine. Maneno ya sauti ya juu yasiyomsaidia wala kumbariki mtu yeyote yangukuwa afadhali yabadilishwe na maneno mema, yenye hadhi, na yanayoonyesha hekima yenye kiasi. Sehemu hii ya kazi ndiyo huduma kubwa zaidi ya umishonari ambayo Mkristo yeyote anaweza kuifanya. Wale wanaotumia viungo vyao vya usemi kama chombo hai cha Mungu huwa mawe yaliyo hai katika hekalu Lake, yakitoa nuru na maarifa. **{VSS 34.3}**

Maonyo na mafundisho ya Neno la Mungu kuhusu usemi ndiyo yanayopuuzwa zaidi. Ikiwa wanafunzi wangeishi kulingana na kanuni za Biblia, utukufu wa Mungu ungekuwa lengo lao katika matumizi ya kipawa cha usemi walichopewa na Mungu. Wangeufundisha ulimi wao kwa bidii ili usitamke maneno yasiyofaa wala yaliyopotoka. Kwa njia hiyo wangukuwa washindi katika eneo hili, ambalo ni gumu sana kulidhibiti. Hatua kubwa zingepigwa katika kuilinda ngome ya nafsi, ili Shetani asiingie na kuitawala. —*Manuscript* 74, 1897. **{VSS 34.4}**

SURA YA 6—WAJIBU WA WALIMU

Ujumbe Wenye Umuhimu wa Milele—Kila Mkristo ameitwa kuwafahamisha wengine utajiri usiochunguzika wa Kristo; kwa hiyo anapaswa kujitahidi kufikia ukamilifu katika usemi. Anapaswa kuliwasilisha Neno la Mungu kwa namna itakayowavuta wasikilizaji kulikubali. Mungu hokusudii kwamba vyombo Vyake vya kibinadamu viwe duni au visivyositawi. Si mapenzi Yake kwamba mwanadamu audhalilishe au aushushe mkondo wa mbinguni unaosafiri kupitia mwanadamu na kwenda ulimwenguni. **{VSS 36.1}**

Tunapaswa kumtazama Yesu, Kielelezo Kikamilifu. Tunapaswa kuomba msaada wa Roho Mtakatifu, na kwa nguvu Zake kujitahidi kukifundisha kila kiungo cha mwili kifanye kazi kwa ukamilifu. **{VSS 36.2}**

Hili ni muhimu hasa kwa wale walioitwa katika utumishi wa hadharani/umma. Kila mhudumu wa Injili na kila mwalimu anapaswa kukumbuka kwamba Bwana anawapa watu ujumbe unaohusu masilahi ya milele. Ukweli anaouhubiri utawahukumu watu katika siku ile kuu ya hukumu ya mwisho. Kwa baadhi ya watu, namna anavyowasilisha ujumbe ndiyo itakayoamua ikiwa wataupokea au wataukataa. Basi, Neno na lisemwe kwa namna itakayoufikia ufahamu na kuugusa mioyo. Linapaswa kutamkwa polepole, kwa uwazi, na kwa uzito unaostahili, lakini pia kwa dhati na

bidii yote inayolingana na umuhimu wake. —*Mifano ya Masihi*, uk. 336. **{VSS 36.3}**

Utii kwa Neno la Mungu—Katika kila eneo la mafundisho, walimu wanapaswa kujitahidi kutoa nuru kutoka katika Neno la Mungu na kuonyesha umuhimu wa kutii kauli **“Bwana asema hivi.”** Elimu inapaswa kuwa ya namna ambayo itawafanya wanafunzi kuzifanya kanuni sahihi kuwa mwongozo wa kila tendo lao. Hii ndiyo elimu itakayodumu milele. —*Misingi ya Elimu kwa Kila Mwanadamu*, uk. 516. **{VSS 37.1}**

Maisha Yaliyotakaswa ni Mfano Wenye Nguvu—Mwalimu ambaye nafsi yake imemtegemea Kristo atanena na kutenda kama Mkristo. Hatatosheka mpaka Ukweli utakapoyatakasa maisha yake na kuyaondolea mbali kila jambo lisilo la lazima. Hatatosheka isipokuwa akili yake iumbwe/ifyinyangwe siku kwa siku na mvuto mtakatifu wa Roho wa Mungu. Ndipo Kristo ataweza kusema na moyo wake,

na sauti Yake isemayo, “**Njia ndiyo hii, ifuateni,**” itasikiwa na kutiiwa. —*Misingi ya Elimu kwa Kila Mwanadamu*, uk. 526. {VSS 37.2}

Maneno ya Kutia Moyo—Onyesha huruma na upole unaposhughulika na wanafunzi wako. Dhihirisha upendo wa Mungu. Maneno unayosema na yawe ya fadhili na yenye kutia moyo. Kisha, unapowafanyia kazi wanafunzi wako, kutakuwa na badiliko kubwa katika tabia za wale ambao hawakupata malezi yanayofaa nyumbani. Bwana anaweza kuwafanya hata walimu vijana kuwa njia za kudhihirisha neema Yake, ikiwa watajiweka wakfu Kwake. —*Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi*, uk. 152. {VSS 37.3}

Nguvu na Shauku—Mwalimu anapaswa daima kulenga unyenyekevu na ufanisi katika ufundishaji wake. Anapaswa kufundisha kwa kutumia mifano kwa wingi, na hata anapowafundisha wanafunzi waliokomaa zaidi, anapaswa kuhakikisha kwamba kila ufafanuzi ni wazi na rahisi kueleweka. Wanafunzi wengi walioendelea katika umri bado ni watoto katika ufahamu wao. {VSS 38.1}

Jambo muhimu katika kazi ya elimu ni shauku/ari [enthusiasm]. Kuhusu jambo hili, kuna funzo muhimu katika kauli iliyowahi kutolewa na mwigizaji mmoja mashuhuri. Askofu Mkuu wa Canterbury*, wa Uingereza, alimwuliza kwa nini waigizaji wa jukwaani huwagusa watazamaji wao kwa nguvu wanapozungumzia mambo ya kubuni, ilhali wahudumu wa Injili mara nyingi huwagusa wasikilizaji wao kwa kiwango kidogo wanapozungumzia mambo halisi. Mwigizaji huyo akajibu, “Kwa heshima yote kwa Ukarimu au neema yako, niruhusu niseme kwamba sababu iko wazi. Iko katika nguvu ya shauku/ari. Sisi jukwaani huzungumza kuhusu mambo ya kubuni kana kwamba ni halisi, lakini ninyi mimbarini huzungumza kuhusu mambo halisi kana kwamba ni ya kubuni.” [Askofu Mkuu wa Canterbury*, wa Uingereza, ni mkuu wa kanisa la Anglikani au Episcopal] {VSS 38.2}

Mwalimu, katika kazi yake, hushughulika na mambo halisi; kwa hiyo anapaswa kuyazungumzia kwa nguvu na ari/shauku yote ambayo ujuzi wa uhalisi wake na umuhimu wake unaweza kumpa. —*Elimu*, uk. 233. {VSS 38.3}

Maneno Machache, Si Hotuba Ndefu—Wale wanaowafundisha watoto wanapaswa kuepuka maelezo marefu yasiyo ya lazima. Maneno mafupi

yanayoelekea moja kwa moja kwenye jambo yatakuwa na matokeo mazuri. Ikiwa kuna mengi ya kusema, yafidiwe kwa kuyatoa kwa vipindi vifupi lakini vya mara kwa mara. Maneno machache yenye kuvutia yanayotolewa mara kwa mara yatakuwa na manufaa zaidi kuliko kusema yote kwa wakati mmoja. Hotuba ndefu huchosha akili changa za watoto. Maneno mengi kupita kiasi yatawafanya wachoke hata mafundisho ya kiroho, kama vile kula kupita kiasi kunavyoelekea tumbo na kupunguza hamu ya kula, hata kufikia hatua ya kuchukia chakula. Vivyo hivyo, akili za watu zinaweza kushibishwa kwa hotuba nyingi kupita kiasi. Kazi kwa ajili ya kanisa, na hasa kwa ajili ya vijana, inapaswa kuwa “*amri juu ya amri, kanuni juu ya kanuni, hapa kidogo na pale kidogo.*” Wapeni watu muda wa kuyeyusha Kweli mnazowalisha. Watoto wanapaswa kuvutwa kuelekea mbinguni, si kwa pupa, bali kwa upole, fadhili, na kujali au upendo mwanana. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juzuu la 2, uk. 420. {VSS 38.4}

Kila Neno Litamkwe kwa Uwazi—Mwalimu wa Ukweli anapaswa kuwa mwangalifu kuhusu namna anavyowasilisha Ukweli {Neno la Mungu}. Anapaswa kutamka kila neno kwa uwazi na kwa matamshi yaliyo sahihi, akiwa na usadikisho wa dhati unaobeba ushawishi unaogusa mioyo. Maneno yanapotamkwa kwa haraka kiasi kwamba yanabana, matokeo yaliyokusudiwa kugusa moyo hupotea. Kipawa cha usemi kinapaswa kukuzwa, ili Ukweli usizungumzwe kwa msisimko usiofaa, bali polepole na kwa uwazi, kusudi hata silabi moja isipotee. —*Kazi ya Kusini Mwa Marekani kwa Watumwa Weusi*, Oktoba 27, 1903. {VSS 39.1}

Matumizi Sahihi ya Lugha—Mojawapo ya sifa muhimu zaidi za mwalimu ni uwezo wa kuzungumza na kusoma kwa uwazi na kwa nguvu. Yeye anayejua kutumia lugha kwa ufasaha na kwa usahihi anaweza kuwa na ushawishi mkubwa zaidi kuliko yule asiyeweza kueleza mawazo yake kwa urahisi na kwa uwazi. —*Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi*, uk. 216. {VSS 39.2}

Utamkaji Wenye Uelewa—Mwalimu anapaswa kukuza uwezo wake wa usemi ili azungumze kwa uwazi, akitamka maneno kwa usahihi na kwa uelewa-umahiri. —*Mashauri kuhusu Kazi ya Shule ya Sabato*, uk. 97. {VSS 40.1}

Urahisi wa Maneno ya Kristo—Mafarisayo walimdhahiki Kristo; waliukosoa urahisi wa lugha Yake, ambao ulikuwa wazi sana kiasi kwamba watoto, wazee, na

watu wa kawaida walimsikiliza kwa furaha na kuvutiwa na maneno Yake. Masadukayo pia walimdhiki kwa sababu mafundisho Yake hayakuwa kama yale yaliyotolewa na watawala wao na waandishi. Walimu hao wa Kiyahudi walizungumza kwa sauti ya mkazo mmoja isiyobadilika, na hata Maandiko yaliyo wazi na yenye thamani kubwa yalifanywa yasivutie wala yasieleweke, yakifunikwa chini ya wingi wa mapokeo na elimu ya wanazuoni. Baada ya marabi kumaliza kuzungumza, watu walielewa maana ya Maandiko kwa kiwango kidogo zaidi kuliko walivyoielewa kabla ya kuwasikiliza. Kulikuwa na nafsi nyingi zilizokuwa na njaa ya Mkate wa Uzima, naye Yesu akawalisha kwa Ukweli safi na rahisi. Katika mafundisho Yake alitumia mifano kutoka katika maumbile na shughuli za kawaida za maisha walizozifahamu. Hivyo, Ukweli ukawa kwao uhalisia ulio hai. Mandhari za maumbile na shughuli za kila siku ziliendelea kuwakumbusha mafundisho ya thamani ya Mwokozi. Namna ya Kristo ya kufundisha ndiyo hasa anayotaka watumishi Wake waifuata. —*Misingi ya Elimu kwa Kila Mwanadamu*, uk. 242–243.

{VSS 40.2}

Fadhili Katika Kukemea—Mwalimu na alete amani, upendo, na uchangamfu katika kazi yake. Asijiruhusu kukasirika wala kuchokozwa au kuhamaki kirahisi. Bwana anamtazama kwa makini sana ili kuona kama anafinyangwa na Mwalimu wa Kiungu/Mbinguni. **{VSS 40.3}**

Mtoto anayeshindwa kujitawala anastahili kusamehewa zaidi kuliko mwalimu anayejiruhusu kukasirika na kukosa subira. Inapolazimu kutoa karipio kali, linaweza kutolewa kwa fadhili. Mwalimu na ajihadhari asimfanye mtoto kuwa mkaidi kwa kuzungumza naye kwa ukali. Kila karipio na lifuatwe na matone ya mafuta ya fadhili. Mwalimu asisahau kamwe kwamba anashughulika na Kristo katika nafsi ya mmoja wa watoto Wake wadogo. **{VSS 41.1}**

Na iwe kanuni isiyobadilika kwa ukubwa, kwamba katika nidhamu yote ya shule, uaminifu na upendo vitawale. Mwanafunzi anaporekebisha kwa namna ambayo haimfanyi ahisi kuwa mwalimu anataka kumwaibisha, upendo kwa mwalimu huanza

kuchipuka moyoni mwake mwanafunzi. —*Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi*, uk. 212. {VSS 41.2}

SURA YA 7—WANAFUNZI NA USEMI

Usemi Unavyoathiriwa na Ukweli Uliomo Ndani ya Moyo—Ikiwa wanafunzi watakuwa na ujasiri wa kimaadili wa kuishi kulingana na Ukweli siku baada ya siku, nguvu yake ya kutakasa itakuwa na ushawishi wa ajabu juu ya usemi wao. Wanaweza kufanya mabadiliko fulani katika tabia na mwenendo wao, lakini hakuna tunda litakaloonekana mpaka usemi wao utakapotakaswa. Wanaweza kuusikia Ukweli, lakini hawatafanya badiliko la kweli isipokuwa wajilishe kwa Neno la Mungu. Mpaka Ukweli uwe sehemu ya maisha yao, wanaweza kuukubali maadamu haupingwi; lakini unapopingwa, maneno yao yataonyesha kwamba Neno la Mungu si mkate wa uzima kwao. Mungu amempa kila mtu nafasi/upendeleo na fursa ya kuwa mshiriki wa asili ya Uungu, na hivyo kuwa mmoja na Yesu Kristo. Lakini wengi huonyesha kwa maneno yao kwamba hawamli Kristo; kwa hiyo hawawezi kung’aa wala kuwashirikisha wengine kile ambacho hakijawa chakula na kinywaji chao. Matumizi yao ya kipawa cha usemi yanaonyesha kwamba wamekusanya makapi tu. —*Manuscript* 74, 1897. {VSS 42.1}

Kukuza Sauti—Vijana wa kiume na wa kike, je, Mungu ameweka mioyoni mwenu shauku ya kumtumikia Yeye? Basi, kwa vyovyote vile, ikuzeni sauti yenu kadiri ya uwezo wenu wote, ili mpate kuwaeleza wengine kwa uwazi Ukweli wa thamani. Msijenge mazoea ya kuomba kwa sauti isiyoeleweka au kwa sauti ya chini

sana kiasi kwamba maombi yenu yawe yahitaji mfasiri. Ombeni kwa urahisi, lakini kwa uwazi na kwa kutamka maneno kwa dhahiri. Kushusha sauti kiasi kwamba haisikiki sio uthibitisho wa unyenyekevu. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 89. {VSS 42.2}

Uwezo wa Kuwasilisha—Kiwango cha manufaa ya Mkristo hupimwa kwa uwezo wake wa kuwasilisha yale aliyoyapokea na ambayo yamekuwa uzoefu wake binafsi. Elimu huwa haijakamilika ikiwa wanafunzi hawapati maarifa ya jinsi ya kutumia kipawa cha usemi na jinsi ya kutumia kwa manufaa makubwa zaidi elimu waliyoipata. Vijana wanapaswa kuanza tangu wakiwa wadogo kujifunza namna sahihi ya kuzungumza. —*Manuscript* 74, 1897. {VSSw 43.1}

Mafunzo Kamili katika Matumizi Sahihi ya Lugha— Ikiwa wanafunzi wako, pamoja na kujifunza Neno la Mungu, watajifunza pia kutumia kwa usahihi lugha ya Kiingereza katika kusoma, kuandika, na kuzungumza, basi kazi kubwa itakuwa imekamilika. Wale wanaofundishwa kwa ajili ya huduma katika kazi ya Bwana wanapaswa pia kufundishwa jinsi ya kuzungumza kwa usahihi katika mazungumzo ya kawaida na mbele ya makutano. Mara nyingi manufaa ya mhudumu hupunguzwa kwa sababu ya kutofahamu jinsi ya kupumua kwa usahihi na kuzungumza kwa uwazi, kwa nguvu, na kwa msisitizo unaofaa. Wengi hawajajifunza kuweka mkazo unaostahili katika maneno wanayosoma na wanayosema. Mara nyingi matamshi yao si wazi. Mafunzo ya kina katika matumizi ya lugha ya Kiingereza yana thamani kubwa zaidi kwa kijana kuliko kujifunza kwa juujuu lugha za kigeni huku akiipuuza lugha yake mama-lugha ya asili. —*Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi*, uk. 207, 208. {VSS 43.2}

Kusoma na Kuzungumza kwa Ufasaha—Mara nyingi vijana wetu hudhuriwa sana kwa kuruhusiwa kuanza kuhubiri kabla hawajapata ujuzi wa kutosha wa Maandiko ili waweze kuwasilisha imani yetu kwa njia yenye kueleweka na ya busara. Baadhi ya wanaoingia katika uwanja wa kazi ni kwamba wameanza tu katika kuyafahamu Maandiko-siyo wazoefu. Hata katika mambo mengine hawana ustadi wala uwezo

wa kutosha. Hawawezi kusoma Maandiko bila kusitasita, wakitamka vibaya maneno, au kuita majina isivyo na kuyachanganya kwa namna ambayo hulidhalilisha Neno la Mungu. Wale ambao hawajafuzu kuwasilisha Ukweli kwa namna inayofaa hawapaswi kuhangaishwa kuhusu wajibu wao. Nafasi yao ni kuwa wanafunzi, si walimu. Vijana wanaotamani kujiandaa kwa ajili ya huduma ya injili hufaidika sana kwa kuhudhuria chuo chetu; hata hivyo, bado wanahitaji mafunzo ya ziada ili waweze kupata stahiki za wasemaji wanaokubalika. Mwalimu anapaswa kuajiriwa ili kuwafundisha vijana jinsi ya kuzungumza bila kuchosha viungo vya sauti. Pia adabu, mijongo na mwenendo wao hupaswa kuzingatiwa kwa makini. — *Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 4, uk. 405, 406. {VSS 44.1}

Ukamilifu wa Usemi na Sauti—Walimu katika shule zetu hawapaswi kuvumilia wanafunzi kuwa na mijongo isiyofaa, ishara zisizo za ustaarabu katika jamii, sauti zisizofaa katika kusoma, wala lafudhi au msisitizo usio sahihi. Ukamilifu wa usemi na sauti unapaswa kusisitizwa kwa kila mwanafunzi. Kwa sababu ya uzembe na mafunzo duni au mabaya, mara nyingi watu hujenga mazoea ambayo huwa vikwazo vikubwa katika kazi ya m hudumu ambaye, mbali na hayo, ana kipawa cha elimu nzuri. Mwanafunzi anapaswa kushawishiwa kwamba anao uwezo wa kujijenga na kuwa mtu mwenye ustadi kwa kuunganisha neema ya Mungu na juhudi zake mwenyewe. Uwezo wa akili na wa mwili ambao Mungu amemjalilia unaweza, kwa kufundishwa ipasavyo na kwa juhudi za dhati, kuwa nguvu yenye manufaa makubwa kwa wanadamu wenzake. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 668, 669. {VSS 44.2}

Hitaji la Kuboresha Sauti ya Usemi—Wanafunzi, Mungu amewapa kipawa cha kuzungumza. Yeye Anatamani mkiendeleze kipawa hicho. Mnaweza kuboresha ubora wa sauti zenu. Azimieni, kwa neema ya Mungu, kujiwezesha kuwa wakamilifu kadiri iwezekanavyo. Ikiwa mtakuwa na usahihi katika usemi na matendo yenu, wale wanaoshirikiana nanyi watabarikiwa kwa ushirika huo. Wale

wanaosema kwa haraka na kwa pupa hutamka mambo mengi ambayo hawatatamani kuyakabili siku ya hukumu. **{VSS 45.1}**

Msiruhusu neno lolote litoke midomoni mwenu ambalo litachochea ugomvi katika moyo wa mwingine. Mungu anatamani maneno yenu yawe ya namna ambayo yataleta mwanga wa furaha badala ya huzuni, na upatanifu badala ya uadui. — *Manuscript 65, 1901.* **{VSS 45.2}**

Uwezo wa Kuzungumza kwa Uwazi— Ikiwa wanafunzi wanaojiandaa kwa ajili ya kazi ya Mungu hawatafundishwa kuzungumza kwa uwazi na kwa unyofu, watapoteza nusu ya uwezo wao wa kutenda mema. Bila kujali wito wao utakuwaje, kila mwanafunzi anapaswa kujifunza kuidhibiti sauti yake. Uwezo wa kuzungumza kwa uwazi na kwa matamshi yanayoeleweka, kwa sauti kamili, nzito, na yenye mwangwi mzuri, una thamani kubwa katika kazi yoyote ile; nao ni wa lazima kwa wale wanaotamani kuwa wahudumu wa injili, wainjilisti, watendakazi wa Biblia, au wasambazaji wa vitabu vya injili. —*Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi*, uk. 217. **{VSS 45.3}**

Kuwa Makini katika Mwenendo, Sauti, na Lugha— Mtenda kazi wa Mungu anapaswa kujitahidi kwa dhati kuwa mwakilishi wa Kristo, akiacha ishara zisizofaa na usemi usio na ustaarabu. Anapaswa kujitahidi kutumia lugha sahihi. Kuna watu wengi ambao hawajali jinsi wanavyozungumza; hata hivyo, kwa uangalifu na bidii, wanaweza kuwa wawakilishi wa Ukweli. Kila siku wanapaswa kuendelea kupiga hatua mbele. Hawapaswi kupunguza manufaa na ushawishi wao kwa kudumisha kasoro katika mwenendo, sauti, au lugha yao. Misemo ya kawaida iliyozoeleka na ya ovyo inapaswa kubadilishwa na maneno yaliyo safi, yenye staha, na yenye maana. Kwa kujichunga daima na kwa nidhamu ya dhati, kijana Mkristo anaweza kuuzuia ulimi wake usinene mabaya/maovu, na midomo yake isinene hila. **{VSS 46.1}**

Tunapaswa kuwa waangalifu tusiyatamke maneno yetu kwa namna isiyo sahihi. Kuna watu miongoni mwetu ambao, kwa nadharia, wanajua vyema kwamba si vema kutumia lugha isiyo sahihi, lakini katika utendaji hufanya makosa mara kwa mara. —*Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi*, uk. 238, 239. **{VSS 46.2}**

Kuzungumza kwa Heshima kwa Watu Wote—Kipawa cha usemi ni kipawa cha thamani sana, na hakipaswi kamwe kutumiwa vibaya. Ulimi ni kiungo kisichotawalika kwa urahisi, lakini haupaswi kubaki hivyo. Kiungo ambacho kimetumiwa vibaya katika usemi mchafu kinapaswa kubadilishwa kitumike kumtolea Mungu sifa. Ikiwa wanafunzi wote wangejitahidi kwa dhati kubadili namna yao ya kufikiri, ya kuzungumza, na ya kutenda; ikiwa, katika mazingira ya familia, wangejizuia kusema maneno yasiyo ya fadhili na heshima, na badala yake wakizungumza kwa heshima na kila mtu; ikiwa wangekumbuka kwamba hapa wanajiandaa kuwa washiriki wa familia ya mbinguni, mvuto wa matengenezo ungeenea kwa nguvu kutoka katika kila nyumba! —*Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi*, uk. 239. {VSS 46.3}

Mielekeo ya Asili na Matokeo Yake— Mielekeo ya asili ikifuatwa itasababisha kutokuwa na uthabiti katika mwenendo, usemi usiofaa, kupuuza Neno la Mungu, matumizi ya lugha chafu, na mawazo yasiyofaa. —*Manuscript 77, 1897*. {VSS 47.1}

Kiwango cha Manufaa—Vijana wa kiume na wa kike wanaojiunga na kanisa wanapaswa kupewa mafunzo maalumu kwa ajili ya kazi inayowafaa kulingana na vipawa vyao. Lakini ikiwa mtu ataendelea kutumia mazungumzo ya kiwango cha chini na yasiyo na staha, asikubalike kuwa mtenda kazi. Ataleta madhara makubwa kwa wafanyakazi wengine kuliko yanavyoweza kurekebishwa.... Maneno, roho, na mwenendo wa mtu ndivyo vinavyoamua kiwango cha manufaa yake. —*The Review and Herald*, Machi 22, 1898. {VSS 47.2}

SURA YA 8—USHAWISHI WA MANENO

Kuutawala Ulimi kwa Neema ya Mungu—Ndugu zangu wanaume na wanawake, mnakitumiaje kipawa cha usemi? Je, mmejifunza kuudhibiti ulimi wenu ili daima utii maelekezo ya dhamiri iliyoangaziwa na hisia takatifu? Je, mazungumzo yenu hayana mzaha usiofaa, kiburi, uovu, udanganyifu, wala uchafu? Je, hamna hila mbele za Mungu? Maneno yana nguvu kubwa ya ushawishi. Shetani atafanya kila awezalo kuufanya ulimi utumike katika huduma yake. Kwa nguvu zetu wenyewe hatuwezi kuudhibiti ulimi, kiungo hicho kisichotawalika. Neema ya Mungu ndiyo tumaini letu pekee. —*Testimonies for the Church*, juz. 5, uk. 175. {VSS 48.1}

Ushawishi wa Kuongoza Nafsi Kwenye Njia Iliyo Sahihi—Maneno yanayonenwa kwa wakati unaofaa ni mema jinsi gani! Neno la tumaini, la kutia moyo, na la kuhimiza kudumu katika njia iliyo sahihi humtia nguvu nyingi mtu anayeelekea kuingia katika mazoea yanayoharibu tabia. Azimio thabiti ulilonalo la kushikamana na kanuni njema litakuwa na ushawishi wa kuzielekeza nafsi katika njia iliyo sahihi. —*Messages to Young People*, uk. 125. {VSS 48.2}

Kuchagua Maneno kwa Kuzingatia Hukumu—Ikiwa utaendelea kuwa na utambuzi wa kudumu kwamba Mungu huona na husikia yote unayofanya na kusema, na kwamba huweka kumbukumbu ya uaminifu ya maneno na matendo yako yote, na kwamba siku moja utawajibika kwa hayo yote, basi katika kila jambo utakalofanya au kusema utatafuta kufuata maelekezo ya dhamiri iliyoangaziwa na iliyo macho. Hivyo ulimi wako utatumika kwa utukufu wa Mungu na utakuwa chanzo cha baraka kwako mwenyewe na kwa wengine. Lakini ikiwa utajitenga na Mungu, kama ambavyo umekuwa ukifanya, jihadhari usije ukauacha ulimi wako ukathibitika kuwa ulimwengu wa uovu na kujiletea hukumu ya kutisha; kwa maana nafsi (roho) zitapotea kwa sababu yako. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 4, uk. 244. {VSS 48.3}

Viungo katika Mnyororo wa Matukio ya Maisha ya Wanadamu—Unaweza kudhani kwamba unachofanya au unachosema si jambo la maana, kumbe kuna hatima ya matokeo makubwa sana, kwa mema au ya mabaya, ambayo hutokana na maneno na matendo yetu. Maneno na matendo yanayoonekana kuwa madogo na

yasiyo na umuhimu ni viungo katika mnyororo mrefu wa matukio ya maisha ya wanadamu. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 3, uk. 542. {VSS 49.1}

Njia ya Kristo—Watumishi wa Mungu katika kizazi hiki wamekabidhiwa Kweli zilizo nzito sana ili wazitangaze; kwa hiyo matendo yao, mbinu zao, na mipango yao lazima iendane/ilingane/itoshane na umuhimu wa ujumbe wao. Ikiwa mnaliwasilisha Neno kwa njia ya Kristo, wasikilizaji wenu wataguswa sana na Kweli mnazowafundisha. Watafikia usadikisho kwamba hakika hili ni Neno la Mungu Aliye hai. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 9, uk. 143. {VSS 49.2}

Umuhimu wa Kila Neno—Kila neno linalotamkwa huwa na ushawishi, na kila tendo hubeba mlolongo wa jukumu au wajibu wake. Hakuna mtu anayeweza kuishi kwa ajili yake mwenyewe tu katika ulimwengu huu, hata kama angetamani kufanya hivyo. Kila mmoja ni sehemu ya mtandao mkubwa wa ubinadamu, na kupitia nyuzi-nyuzi za ushawishi wetu binafsi, tumeunganishwa na ulimwengu wote au sayari zote (universe). Kristo alitumia ushawishi Wake kuwavuta watu kwa Mungu, Naye ametuachia mfano wa jinsi tunavyopaswa kusema na kutenda. Mtu anayefinyangwa na Roho wa Mungu atajua jinsi ya kusema “neno kwa wakati wake kwa yeye aliyechoka,” naye atatambua baraka kuu zaidi ambayo mwanadamu anaweza kuipata—furaha ya kuwagawia wengine hazina za thamani za hekima na neema ya Kristo. Lakini wale wanaojiruhusu kuthibitiwa/kutawaliwa na adui wa mema yote watasema maneno ambayo hayakupaswa kamwe kutamkwa. —*The Review and Herald*, Februari 16, 1897. {VSS 49.3}

Athari ya Kila Neno na Kila Tendo— “Sisi tu watenda kazi pamoja na Mungu.” (1 Wakorintho 3:9). Bwana Atakutumia wewe, atanitumia mimi, na atamtumia kila mtu anayeingia katika huduma Yake, ikiwa tutajisalimisha chini ya uongozi Wake. Kila mmoja anapaswa kusimama katika mnara au kituo chake cha ulinzi, akisikiliza kwa makini yale ambayo Roho anamwambia, huku akikumbuka kwamba kila neno na kila tendo lake huacha athari, si tu katika tabia yake mwenyewe, bali pia katika tabia za wale anaoshirikiana nao. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 8, uk. 172. {VSSw 50.1}

Maneno ya Upendo—Wajibu wetu ni kuishi katika mazingira ya upendo wa Kristo, kuuvuta ndani kabisa upendo Wake, na kuakisi joto Lake kwa wale wanaotuzunguka. Lo, ni uwanja mpana kiasi gani wa ushawishi ulio wazi mbele yetu! Tunapaswa kuzipalilia/kuzilima kwa uangalifu bustani ya nafsi zetu, ili zizae maua yaliyo safi, matamu, na yenye harufu nzuri. Maneno ya upendo mwanana, huruma nyororo, kujali na hisani, fadhila, wema hutakasa ushawishi wetu kwa wengine. —*Mwito Wetu Mkuu*, uk. 175. {VSS 50.2}

Harufu ya Uzima au ya Mauti—Maneno tunayoyasema leo masikioni mwa watu, kazi tunazozifanya, na roho ya ujumbe tunaoubeba vitakuwa harufu ya uzima iletayo uzima au harufu ya mauti iletayo mauti. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 5, uk. 716. {VSS 51.1}

Baraka au Laana—Siku baada ya siku tunapanda mbegu kwa ajili ya mavuno ya wakati ujao. Hatuwezi kuwa waangalifu kupita kiasi kuhusu mbegu tunazopanda kwa maneno yetu. Mara nyingi maneno husemwa kwa uzembe na baadaye husahaulika, lakini maneno hayo, yawe ya mema au ya mabaya, yatazaa mavuno. Panda neno moja lisilo la fadhili au lenye ukali, na mbegu hiyo, ikipata udongo katika akili za wanaolisikia, itaota na kuzaa matunda yanayofanana nayo. Panda mbegu moja kwa maneno ya upendo, ya upole, fadhila na yanayofanana na ya Kristo, nayo itakuletea mavuno tele. Na tujihadhari, tujilinde ili tusije tukazungumza maneno ambayo hayawi baraka, bali laana. —*Mwito Wetu Mkuu*, uk. 294. {VSS 51.2}

Ni Nguvu Ipi Inayokutawala?—Huwezi kuwa mwangalifu kupita kiasi kuhusu unayosema, kwa maana maneno unayoyatamka huonyesha ni nguvu gani inayotawala akili na moyo wako. Ikiwa Kristo anatawala moyoni mwako, maneno yako yatafunua usafi, uzuri, na harufu nzuri ya tabia iliyofinyangwa na kuumbwa kulingana na mapenzi Yake. Lakini tangu kuanguka kwake, Shetani amekuwa mshtaki wa ndugu; kwa hiyo ni lazima uwe macho usije ukaidhihirisha roho iyo hiyo ya Adui. —*Akili, Tabia na Haiba*, juz. 2, uk. 579, 580. {VSS 51.3}

Maisha na Usemi Wenye Ushawishi—Kwa utulivu wa mazungumzo yetu tunaweza kutoa ushuhuda mzuri kwa ajili ya Mungu. Mtindo wa maisha ulio sahihi na usemi ulio sahihi vina ushawishi mkubwa zaidi kwa mema kuliko mahubiri yote yanayoweza kuhubiriwa. —*Manuscript 65, 1901*. {VSS 51.4}

Maneno na matendo ya haki yana ushawishi wenye nguvu zaidi kwa mema kuliko mahubiri yote yanayoweza kuhubiriwa. —*Maisha Yangu Leo*, uk. 114. {VSS 52.1}

Mazungumzo ya Busara—Mazungumzo ya busara na matendo yaliyo sahihi huleta ushawishi wenye nguvu wa kuwaelekeza watu katika njia iliyo sahihi. Lakini kwa ujumla, wale wanaozungumza sana ndio wanaoshinikiza au kuleta kwa watu fikira chache sana zenye kina na za dhati na ari, nao hufanya kazi ndogo sana kwa ajili ya Bwana. Wanafikiri kwamba kwa kuzungumza wanaweza kufidia mapungufu yao. Lakini ni watendaji wa Neno ndio wanaohesabiwa haki mbele za Mungu. —*Manuscript 53, 1899*. {VSS 52.2}

Uhusiano Kati ya Mioyo Yetu na Maneno Yetu—Tutaonyesha yaliyo ndani ya mioyo yetu kupitia maneno tunayoyasema. Uhusiano kati ya moyo na maneno ya vinywa vyetu ni wa karibu sana; na kwa maneno yetu tutahukumiwa mmoja mmoja katika siku ya mwisho.... Mawazo yetu huzaa maneno yetu, na maneno yetu nayo huathiri tena mawazo yetu. —*Letter 16a, 1895*. {VSS 52.3}

Dalili ya Tabia—Maneno ni zaidi ya ishara ya tabia; yana uwezo wa kuathiri tena tabia yenyewe. Wanadamu huathiriwa na maneno yao wenyewe. Mara nyingi, kwa msukumo wa muda mfupi unaochochewa na Shetani, mtu hutamka wivu au mashaka mabaya, akisema mambo ambayo kwa kweli hayaaamini; lakini maneno hayo huathiri tena mawazo yao. Wanadanganywa na maneno yao wenyewe na hatimaye huamini kuwa ni kweli kile kilichosemwa kwa msukumo wa Shetani. Mara tu wanapokuwa wametoa maoni au kufanya uamuzi fulani, mara nyingi huwa na kiburi kiasi cha kushindwa kurudisha nyuma tamko hilo au kusahihisha mambo, nao hujitahidi kujithibitisha wenyewe kuwa wako sahihi, mpaka hatimaye wanafikia hatua ya kuamini kwamba kweli wako sahihi. {VSS 52.4}

Ni hatari kutamka neno la mashaka; ni hatari kuhoji na kukosoa nuru ya Mungu. Mazoea ya kukosoa bila uangalifu na bila kicho au heshima huathiri tabia kwa kukuza kutomheshimu Mungu na kutokuamini. Watu wengi wanaojiruhusu kuendelea na tabia hii wameendelea bila kutambua hatari iliyopo, mpaka walipofikia hatua ya kuwa tayari kukosoa na kuikataa kazi ya Roho Mtakatifu.—*Tumaini la Vizazi Vyote*, uk. 323. {VSS 53.1}

Ushawishi Nje ya Kanisa—Wafuasi wanaodai kuwa wa Kristo wanapaswa kutambua kwamba ushawishi wa maneno na matendo yao hauwaathiri wao wenyewe tu, bali pia huenea nje ya kanisa. Ikiwa wangeweza kuona madhara yanayosababishwa na maneno yao ya uzembe, kurudia-rudia taarifa zisizo na msingi, na lawama zisizo za haki, kungekuwa na mazungumzo machache zaidi na maombi mengi zaidi wakati Wakristo wanapokusanyika pamoja.—*The Review and Herald*, Oktoba 19, 1886. {VSS 53.2}

Athari kwa Wasioamini—Maisha, maneno, na mwenendo ni hoja yenye nguvu zaidi na rufaa yenye uzito zaidi kwa wale wasiojali, wasiomcha Mungu, na wenye mashaka. Hebu maisha na tabia viwe hoja kuu yenye nguvu ya Ukristo; ndipo watu watalazimika kutambua kwamba mmekuwa pamoja na Yesu na kwamba mmejifunza kutoka Kwake. —*Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi*, uk. 478. {VSS 53.3}

Ushawishi Hata Baada ya Kifo— Ni watu wachache wanaotambua jinsi ushawishi wa maneno na matendo yao unavyoweza kufika mbali. Mara nyingi makosa ya wazazi huleta madhara makubwa sana kwa watoto wao na wajukuu wao, hata muda mrefu baada ya wale walioyafanya kulala kaburini. Kila mtu anaacha ushawishi juu ya wengine, na atawajibika kwa matokeo ya ushawishi huo. Maneno na matendo yana nguvu kubwa ya kuleta matokeo, na wakati ujao wa mbali utaonyesha athari ya maisha yetu ya hapa duniani. Athari inayotokana na maneno na matendo yetu hakika itaturudia sisi wenyewe, iwe kwa baraka au kwa laana. Wazo hili linaupa uzima uzito wa kutisha, na linapaswa kutuongoza kumkaribia Mungu katika maombi ya unyenyekevu, tukimwomba atuongoze kwa hekima Yake. —*Wazee wa Imani na Manabii*, uk. 556. {VSS 54.1}

Neno Litamkwalo bila la Kufikiri na Hatima ya Milele ya Nafsi—Mtu yeyote asithubutu kusema kwa wepesi juu ya maonyo yanayotolewa na wale ambao wajibu wao ni kulinda ustawi wao wa kimaadili na kiroho. Maneno hayo yanaweza kuonekana kuwa hayana umuhimu mkubwa, yakiacha tu athari ya muda mfupi katika akili za wasikilizaji. Lakini si hivyo tu. Mara nyingi maneno hayo hupata mwikio katika mioyo ya vijana isiyotakaswa, ambao hawajawahi kujisalimisha kwa maonyo wala kujitiisha kwa nidhamu au makatazo. Ushawishi wa neno lisilofikiriwa unaweza kuathiri hatima ya milele ya nafsi. Kila mtu anaacha

ushawishi katika maisha ya wengine.—*Shuhuda Kwa Kanisa*, juz. 4, uk. 654. {VSS 54.2}

Maneno Yanayosemwa kwa Wakati Unaofaa—Kwa kweli, ulimwengu umejaa haraka, kiburi, ubinafsi, tamaa, na vurugu; na huenda ikaonekana kwetu kwamba ni kupoteza muda na nguvu kuendelea kuwa tayari kila wakati, katika msimu na nje ya majira/msimu, na katika kila hali kuwa tayari kusema maneno yenye fadhila, upole, safi, yenye kuinua, yenye heshima, na matakatifu, katikati ya kimbunga cha vurugu na machafuko, pilikapilika, na ugomvi. Hata hivyo, maneno yanayosemwa kwa wakati unaofaa, yanayotoka katika mioyo na midomo iliyotakaswa, na yanayoungwa mkono na mwenendo wa Kikristo wenye kumcha Mungu na ulio thabiti, yatakuwa kama **matufaha ya dhahabu katika mapambo ya fedha....** {VSS 54.3}

Hupaswi kusubiri nafasi kubwa, wala kutazamia uwezo wa pekee, kabla ya kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya Mungu. Hupaswi hata kufikiria watu wa ulimwengu watakufikiriaje. Ikiwa ushirika wako nao na mazungumzo yako ya kumcha Mungu ni ushuhuda hai kwao wa usafi na unyofu wa imani yako, na wakitambua kwamba unatamani kuwanufaisha au kuwatendea mema, maneno yako hayatapotea bure mbele yao, bali yatazaa matunda mema.—*Shuhuda Kwa Kanisa*, juz. 3, uk. 247. {VSS 55.1}

Tabia Inayopatana na Maneno—Ikiwa tunatamani kuwabadilisha wengine, ni lazima sisi wenyewe tutekeleze kanuni tunazotaka wao wazifuate. Maneno, hata yawe mazuri kiasi gani, hayatakuwa na nguvu ikiwa yanapingana na maisha ya kila siku. Wahudumu wa Kristo, nawasihi: **“Jitunze nafsi yako na mafundisho yako.”** Usizitolee udhuru dhambi zilizo ndani yako mwenyewe ambazo unazikemea kwa wengine. Ikiwa unahubiri juu ya upole, unyenyekevu, na upendo, acha neema hizo zionekane katika maisha yako mwenyewe. Ikiwa unawahimiza wengine kuwa wema, wenye adabu, uungwana, staha na wenye kujali na umakini nyumbani, acha mfano wako mwenyewe uyatie nguvu maonyo yako. —*Shuhuda Kwa Kanisa*, juz. 5, uk. 160. {VSS 55.2}

Kumkana Kristo kwa Kuzungumza Mabaya—Yeye anayetaka kumkiri Kristo lazima awe na Kristo anayekaa ndani yake. Hawezi kuwapa wengine kile ambacho yeye mwenyewe hajapokea. Wanafunzi wangeweza kuzungumza kwa ufasaha kuhusu mafundisho Yake; wangeweza kurudia Maneno ya Kristo

Mwenyewe; lakini kama hawangekuwa na unyenyekevu, fadhila na upendo unaofanana na wa Kristo, wasingekuwa wanamkiri Kristo. Roho iliyo kinyume na Roho ya Kristo humkana Kristo, hata kama mtu anadai kuwa ni mfuasi Wake. Wanadamu wanaweza kumkana Kristo kwa kusema mabaya juu ya wengine, kwa mazungumzo ya kipumbavu, au kwa maneno yasiyo ya kweli na yasiyo na fadhili. —*Tumaini la Vizazi Vyote*, uk. 357. {VSS 56.1}

Chanzo cha Sehemu Tisa Kati ya Kumi za Matatizo Kanisani—Usemi usio wa Kikristo ndio chanzo cha sehemu tisa kati ya kumi za matatizo yote yaliyopo kanisani [9/10]. Mawakala wa Shetani wanafanya kazi kwa bidii kuwafanya wale wanaodai kuwa Wakristo wazungumze bila kufikiri. Wanapofanikiwa, Shetani hushangilia, kwa sababu wafuasi wa Mungu wameuharibu mvuto wao wenyewe. —*The Review and Herald*, Novemba 24, 1904. {VSS 56.2}

Maneno ya Kudharau—Wengi leo wanajipa uhuru wa kutumia kipawa cha usemi bila tahadhari, bila kufikiria ushawishi ambao maneno yao yatakuwa nao juu ya wengine. Bwana hutuma ujumbe Wake kupitia watu anaowachagua, na wale wanaotoa maneno ya kudharau wajumbe na ujumbe huo wanapaswa kukumbuka kwamba, hakika wangemsema Kristo kwa namna hiyo hiyo ikiwa angekuja kwao kama alivyokuja kwa Wayahudi, akiwa na ujumbe ambao haukumatana na mioyo yao ambayo haijafanywa upya. Wale wanaotumia usemi wao kumdhihaki au kumwigiza mtu anayesema maneno ya Mungu wanahesabiwa kuwa wamemfanyia Kristo jambo hilo; kwa maana jambo hilo hufanywa kwake katika nafsi za watakatifu wake. —*The Review and Herald*, Januari 18, 1898. {VSS 56.3}

Ushawishi wa Maneno ya Hasira—Laiti wale wanaotangaza ujumbe mzito zaidi kuwahi kutolewa kwa ulimwengu wangetambua jinsi ushawishi wao unavyodhoofishwa sana wanapokuwa na kushuku/mashaka juu ya ndugu zao na wanaporuhusu maneno ya hasira kutoka midomoni mwao! Hasira ya Mungu inamjia kila mtu anayezungumza maneno makali na yasiyo na fadhili. —*The Review and Herald*, Julai 21, 1903. {VSS 57.1}

Kuwa na Imani kwa Ndugu—Kwa kupanda uovu katika akili za walio watu dhaifu, ambao hawana uhusiano hai na Mungu, na kuwaambia jinsi ulivyo na imani ndogo kwa wengine, unavunja tegemeo ambalo ndugu zao walikuwa nalo juu yao; kwa sababu unaharibu imani yao kwa ndugu zao. Lakini usimruhusu adui autumie ulimi wako kwa namna hiyo; kwa maana katika siku ya hukumu ya mwisho, Mungu

atakuita utoe hesabu ya maneno yako. Usitumie ushawishi wako kwa njia ambayo itamfanya mtu aache kushikilia mkono wa Mungu na hivyo amwache Mungu. Hata kama hujatendewa kama unavyodhani ulipaswa kutendewa, usiruhusu mzizi wa uchungu uchipuke; kwa maana kwa njia hiyo wengi watatiwa unajisi. Kupitia maneno yako unaweza kuwafanya wengine waanze kuwa na mashaka. —*The Review and Herald*, Agosti 24, 1897. {VSS 57.2}

Kuangusha au Kuwaletea Uharibifu Wale Walio Dhaifu Katika Imani—Usimruhusu Shetani autumie ulimi wako na sauti yako kuwaangusha au kuwaangamiza wale walio dhaifu katika imani; kwa maana katika siku ya hukumu ya mwisho, Mungu atakuita utoe hesabu ya kazi yako. —*The S.D.A. Bible Commentary*, juz. 3, uk. 1161. {VSS 57.3}

Madhara ya Kudumu ya Maneno ya Kipumbavu—Kama Wakristo wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo, tunapaswa kuzingatia ushawishi ambao maneno yetu huwa nao kwa wale tunaoshirikiana nao, wawe waumini au wasio waumini. Maneno yetu huzingatiwa, na madhara hutokea kwa sababu ya maneno yanayotamkwa bila kufikiri. Hakuna ushirika wa baadaye wa waumini au wasio waumini utakaoweza kuondoa kabisa ushawishi usiofaa wa maneno yasiyofikiriwa na ya kipumbavu. Maneno yetu yanaonyesha aina ya chakula ambacho nafsi hujilisha nacho. —*The S.D.A. Bible Commentary*, juz. 3, uk. 1159, 1160. {VSS 58.1}

Nguvu ya Mfano—Wakati jaribu au kipindi cha shida kinapomfikia mtu yeyote katika maisha yake, na unapojaribu kumpa ushauri au maonyo, maneno yako yatakuwa na uzito wa ushawishi kwa mema kwa kadiri tu ambayo mfano wako mwenyewe na roho yako vimekujengea na kukupatia uwezo huo.—*Mlima wa Baraka*, uk. 127. {VSSw 58.2}

SURA YA 9—USHAWISHI KUPITIA USEMI

Usemi Uliotakaswa ni Baraka Kuu Zaidi—Kati ya vipawa vyote ambavyo Mungu amempa mwanadamu, hakuna kilicho bora zaidi wala chenye baraka kubwa zaidi kuliko kipawa cha usemi, ikiwa kimetakaswa na Roho Mtakatifu. Kwa ulimi tunashawishi na kuwavuta wengine; kwa huo tunamtolea Mungu maombi na sifa; na kwa huo tunawasilisha mawazo yenye thamani kuhusu upendo wa Mkombozi. —*Shuhuda kwa Kanisa*, uk. 316, 317. **{VSS 59.1}**

Amani Moyoni—Tunapaswa kuonyesha kwa maisha yetu ya kila siku kwamba tuna amani na pumziko ndani ya Mungu. Amani Yake iliyo moyoni itaonekana katika uso wetu. Itaipa sauti yetu uwezo wa kushawishi. Ushirika na Mungu utauinua mwenendo wa tabia yetu kimaadili na kuathiri maisha yetu yote. —*Shuhuda Kwa Kanisa*, juz. 6, uk. 47. **{VSS 59.2}**

Ukaribisho wa Upole na Furaha—Wakaribieni watu kwa namna yenye ushawishi, yenye fadhili/wema, iliyojaa furaha na upendo kwa Kristo. Hakuna ulimi wa mwanadamu unaoweza kueleza thamani ya huduma ya Neno na Roho Mtakatifu. Hakuna usemi wa mwanadamu unaoweza kueleza kwa akili yenye mipaka thamani

ya kuelewa na kupokea kwa imani hai baraka inayotolewa wakati Yesu wa Nazareti anapopita. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 444. {VSS 59.3}

Ushawishi kwa Ajili ya Kuleta Roho—Nguvu ya kushawishi ni kipawa cha ajabu. Ina maana kubwa sana kwa wale wanaotamani kuleta roho kwa Kristo. —*Letter 32, 1911*. {VSS 60.1}

Nguvu ya Uzoefu Binafsi—Mtu anapokuwa ameipokea kweli kwa upendo wake, ataidhihirisha katika namna yake ya kushawishi na katika sauti yake. Atatangaza yale ambayo yeye mwenyewe ameyasikia, kuyaona, na kuyashika kuhusu Neno la uzima, ili wengine waweze kuwa na ushirika pamoja naye katika kumjua Kristo. Ushuhuda wake, unaotoka katika midomo iliyoguswa kwa kaa la moto kutoka madhabahuni, huwa kweli kwa moyo unaopokea, na hufanya kazi ya utakaso katika tabia. —*Tumaini la Vizazi Vyote*, uk. 142. {VSS 60.2}

Upendo na Huruma—Ufasaha wenye nguvu zaidi wa kushawishi ni maneno yanayosemwa kwa upendo na huruma. Maneno kama hayo yataleta nuru katika akili zilizochanganyikiwa na tumaini kwa waliokata tamaa, yakifanya matarajio yao yawe yenye nuru zaidi. Wakati tunaoishi unahitaji nguvu hai na iliyotakaswa; unahitaji bidii, juhudi, unyofu, na huruma nyororo pamoja na upendo mwanana; unahitaji maneno ambayo hayataongeza huzuni, bali yatachochea imani na tumaini. Tunaelekea nyumbani, tukitafuta nchi iliyo bora zaidi, yaani nchi ya mbinguni. Badala ya kusema maneno yatakayochoma mioyo ya wale wanaotusikia, je, hatutasema kuhusu upendo ambao Mungu ametupenda nao? Je, hatutajaribu kuwafariji wale wanaotuzunguka kwa maneno ya huruma kama ya Kristo? —*Mwito Wetu Mkuu*, uk. 295. {VSS 60.3}

Kisima cha Ushawishi—Dhamiri isiyo na kosa mbele za Mungu na wanadamu, pamoja na moyo wenye huruma kuu kwa wanadamu, hasa kwa kusudi la kuwavuta kwa Kristo, vitakuwa na sifa zile alizokuwa nazo Kristo. Watu wa namna hiyo watajazwa na Roho Wake, na watakuwa na hazina ya ushawishi pamoja na ghala la ufasaha rahisi. —*Shuhuda kwa Wachungaji na Watendakazi wa Injili*, uk. 120. {VSS 61.1}

Uzito wa Ushahidi—Mungu anaviwasilisha katika akili za wanadamu vito vya thamani vya Kweli vilivyowekwa na Mungu, vinavyofaa kwa wakati wetu. Ameziokoa Kweli hizi kutoka katika mchanganyiko wa makosa na kuziweka katika mpangilio wake unaofaa. Wakati Kweli hizi zinapopewa nafasi yake inayostahili katika mpango mkuu wa Mungu, na zinapowasilishwa kwa uelewa, kwa bidii, na kwa heshima kuu ya kumcha Mungu na watumishi wa Bwana, wengi wataamini kwa dhamiri zao kwa sababu ya uzito wa ushahidi, bila kusubiri kila tatizo linalodhaniwa kuwa lipo katika akili zao liondolewe. —[Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti](#), uk. 122. **{VSS 61.2}**

Kemeo Kuu Zaidi kwa Kosa—Watu hawawezi kutarajiwa kuona mara moja ubora wa Kweli juu ya kosa ambalo wamelithamini na kulishikilia. Njia bora zaidi ya kufichua udanganyifu wa kosa ni kuwasilisha ushahidi wa Kweli; hili ndilo kemeo kuu zaidi linaloweza kutolewa dhidi ya kosa. Ondoa wingu la giza linalotanda juu ya akili kwa kuangaza nuru angavu ya Jua la Haki. —[Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti](#), uk. 170. **{VSS 61.3}**

Kutoa Hoja Kutoka Katika Maandiko—Si msisimko tunaotamani kuleta, bali ni tafakari ya kina na ya dhati, ili wale wanaosikia wafanye kazi imara, kazi halisi, yenye msingi na ya kweli, itakayodumu milele. Hatutamani msisimko wala mambo ya kushangaza; kadiri tunavyokuwa na mambo hayo machache, ndivyo inavyokuwa bora zaidi. Hoja tulivu, ya dhati, na yenye msingi katika Maandiko ni ya thamani na yenye kuzaa matunda. Hapa ndipo siri ya mafanikio ilipo: kumhubiri Mwokozi aliye hai na binafsi kwa namna rahisi na yenye bidii, ili watu waweze kuishikilia imani, nguvu ya Neno la uzima. —[Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti](#), uk. 170. **{VSS 62.1}**

Jambo Moja kwa Wakati Mmoja—Ingawa mwalimu wa Kweli anapaswa kuwa mwaminifu katika kuwasilisha injili, asimwage kamwe mbele ya watu wingi wa mambo ambayo hawawezi kuyaelewa kwa sababu ni mapya kwao na magumu kufahamu. Shughulikia jambo moja kwa wakati mmoja, na ulifanye jambo hilo lieleweke wazi kwa kuzungumza polepole na kwa sauti inayoeleweka-wazi. Zungumza kwa namna ambayo watu wataona uhusiano wa jambo hilo moja na

Kweli zingine muhimu za msingi.—[Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti](#), uk. 202. **{VSS 62.2}**

Mtenda Kazi wa Shule ya Sabato—Mtenda kazi wa Shule ya Sabato, utakutana na kiwango kipi—kiwango cha Kristo au kiwango cha ulimwengu? Je, utasema: “Nitauinua msalaba na kumfuata Yesu”? Je, hutakuza upole Wake katika ushawishi, bidii Yake katika maonyo, na kuonyesha kanuni kuu za Kweli kwa kudhihirisha katika maisha na tabia yako kile ambacho dini ya Kristo imekufanyia? Je, sisi sote hatutazingatia maonyo ya mtume: “*Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo, wala msiuangalie mwili, hata kuwasha tamaa zake.*”? **Warumi 13:14** —[Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi](#), uk. 95. **{VSS 62.3}**

Ujumbe, Siyo Mtu Mwenyewe—Mhudumu ambaye amejifunza kutoka kwa Kristo daima atatambua kwamba yeye ni mjumbe wa Mungu, aliyekabidhiwa kufanya kazi yenye hatima/matokeo kwa wakati huu na kwa umilele. Haipaswi kuwa sehemu ya kusudi lake kuelekeza umakini wa watu kwake mwenyewe, elimu au kisomo chake, au uwezo wake. Badala yake, lengo lake lote linapaswa kuwa kuwaongoza wenye dhambi watubu, akiwaelekeza kwa mafundisho na kwa mfano wake kwa **Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu**. Nafsi yake mwenyewe inapaswa kufichwa ndani ya Yesu. Watu wa namna hiyo watazungumza wakiwa na ufahamu kwamba wanamiliki nguvu na mamlaka kutoka kwa Mungu, wakiwa kinywa Chake. Mahubiri yao yatakuwa ya dhati na bidii na nguvu ya ushawishi itakayowaongoza wenye dhambi kuona hali yao ya kupotea na kukimbilia kwa Kristo ili kupata wokovu.—[Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti](#), uk. 134. **{VSS 63.1}**

SURA YA 10—KUTUMIA VIBAYA KIPAWA CHA USEMI

Ushawishi wa Maneno Makali—Je, wewe haupendi kuambiwa maneno makali? Kumbuka kwamba unaposema maneno kama hayo, wengine huhisi uchungu wake. Acha mfano wako unaostahili kuigwa, maneno yako ya amani, na matendo yako yasiyo ya ubinafsi yawe harufu ya uzima iletayo uzima. **{VSS 64.1}**

Kipawa cha usemi kilitolewa ili kitumike kwa manufaa ya wote. Maneno mazuri na yenye uchangamfu hayagharimu zaidi kuliko maneno yasiyopendeza na yenye huzuni. Maneno makali hujeruhi na kuumiza nafsi. Katika maisha haya kila mtu ana matatizo anayopaswa kupigana nayo mieleka. Kila mtu hukutana na malalamiko, maudhi na masikitiko. Je, hatutaleta mwanga wa furaha badala ya giza katika maisha ya wale tunaokutana nao? Je, hatuzungumza maneno yatakayowasaidia na kuwabariki wengine? Maneno hayo yatakuwa baraka kwetu kama yalivyo kwa wale wanaoyasikia au wale watakaozungumziwa au kuambiwa hayo.—*Manuscript 93, 1901*. {VSS 64.2}

Maneno Yanayochochea Hasira—Kipawa cha usemi ni cha thamani. Unaweza kutumia ulimi wako kwa maneno ya malalamiko au kwa maneno ya upole na yenye furaha. Kumbuka kwamba kusema kwa upole hakutapunguza ushawishi wako; bali kutaufanya ushawishi wako uwe wenye mvuto zaidi. Ikiwa utaambiwa maneno yanayochochea hasira, usijibu hata neno moja. Kemeo bora zaidi unaloweza kumpa mtu aliyesema neno la kukukasirisha ni kunyamaza mpaka utakapoweza kuzungumza kwa sauti tulivu na yenye upole.—*The Review and Herald*, Julai 6, 1905. {VSS 64.3}

Maneno Yasiyo na Faida—Kwa kipawa cha usemi tunapaswa kuwasilisha ile Kweli kwa wengine kila tunapopata nafasi. Kipawa hiki kinapaswa kutumiwa daima katika huduma ya Mungu. Lakini kwa huzuni, kipawa hiki kinatumiwa vibaya sana. Maneno husemwa ambayo husababisha madhara makubwa. Kristo alisema: “Basi, nawaambia, Kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu. Kwa kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa **Mathayo 12:36-37**.”—*The Review and Herald*, Septemba 12, 1899. {VSS 65.1}

Mazungumzo Yasiyo na Maana na Yasiyo na Faida—Kipawa cha usemi ni zawadi kutoka kwa Mungu; kwa hiyo tunaposikia mazungumzo mengi yasiyo na faida wala maana, tunaweza kuwa na hakika kwamba wale wanaotumia vibaya kipawa hiki cha thamani si Wakristo. Hawakai ndani ya Kristo, wala Kristo hakai ndani yao. Kila mti hujulikana kwa matunda yake. “Mtu mwema katika hazina njema ya moyo wake hutoa yaliyo mema, na mtu mwovu katika hazina mbovu ya moyo wake hutoa yaliyo maovu. **Luka 6:45**” Ni mafuriko makubwa kiasi gani ya uovu na

mambo yasiyo na thamani yanayotoka kwa sababu ya kipawa cha usemi! Na ni wangapi wanaomkana Kristo kwa usemi wao! Badala ya kutoa ushuhuda mzuri wa Kristo kupitia mazungumzo yao, wao husema kwa matendo yao: “*Simjui Mtu huyu.*” Ni rahisi kuwa na sura ya utauwa; lakini kutoa ushuhuda kamili wa imani yetu katika Kristo kunamaanisha kwamba maneno yetu, mavazi yetu, na roho yetu vitashuhudia Ukweli huo.—*Letter 19, 1897. {VSS 65.2}*

Mazungumzo ya Ujinga na Mzaha—Kuza kipawa hiki cha thamani cha usemi kama chombo ulichokabidhiwa na Mungu. Usianzishe mada za mzaha usio na maana wala mazungumzo ya kipumbavu. Zungumza kwa namna ambayo watu wasio wa imani yetu watapata ushahidi kwamba umefundishwa katika usemi wenye afya na kanuni zilizo sahihi. “*Ninyi ni nuru ya ulimwengu.*” Ni akina nani wanaoheshimiwa kwa namna hiyo? Ni wale wote waliotumia vizuri nafasi zao kujifunza jinsi ya kumtumikia Bwana kupitia kipawa cha usemi.—*Manuscript 74, 1897. {VSS 66.1}*

Kuzungumza kwa Mizaha na Utani—Ni wajibu wa vijana kuhimiza uzito wa tabia na kiasi katika mwenendo. Uzembe, mizaha, na utani vitasababisha ukavu wa kiroho na kupoteza kibali cha Mungu. Wengi wenu hamtoi ushawishi mbaya kwa wengine, na kwa hiyo kwa kiasi fulani mnajiona mmeridhika; lakini je, mnatoa ushawishi kwa mema? Je, kupitia mazungumzo na matendo yenu mnatafuta kuwaongoza wengine kwa Mwokozi, au, ikiwa wanamkiri Kristo, mnatafuta kuwaongoza katika kutembea Naye kwa ukaribu zaidi?—*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 2, uk. 236, 237. **{VSS 66.2}**

Mazungumzo Yasiyo na Thamani—Rafiki zangu vijana, je, mtayaanza maisha yenu ya Kikristo mkiwa watu ambao mioyo yenu imewashwa na upendo wa Yesu? Kamwe hamtajua ni mema kiasi gani mnayoweza kutenda au kutimiza kwa kusema maneno ya upole, kujali, upendo, yenye busara, na yenye makini/uzito kuhusu wokovu wa nafsi kwa wale ambao hawadai kuwa watoto wa Mungu; lakini kwa upande mwingine, huenda msijue mpaka siku ya hukumu ni nafasi ngapi mlizozipoteza au ambazo hamkuboresha ambazo zingewafanya kuwa mashahidi wa Kristo, wala madhara mliyoyasababisha kwa nafsi fulani kupitia mwenendo wenu wa michezo-michezo na mzaha, au mambo yasiyo na maana, mazungumzo yenu

yasiyo na thamani, na mwenendo wenu wa masihara ambayo hayakupatana kabisa na imani yenu takatifu.—*Jumbe kwa Vijana*, uk. 201. **{VSS 66.3}**

Maneno Makali ya Kukera—Mwokozi anayekaa ndani ya moyo hujidhihirisha kupitia maneno, lakini Roho Mtakatifu hakai katika moyo wa mtu anayeudhika-udhika kwa sababu wengine hawakubaliani na mawazo na mipango yake; kutoka midomo ya mtu wa namna hiyo hutoka maneno makali yanayochoma, ambayo humhuzunisha Roho Mtakatifu na kukuza tabia za kishetani badala ya tabia za Kiungu/mbinguni. Bwana anatamani wale walionganisha katika kazi Yake wazungumze daima kwa upole wa Kristo; ikiwa utachokozwa, usiwe na haraka ya kukasirika na kukosa ustahimilivu, bali onyesha upole ambao Kristo alituwekea mfano katika maisha Yake. **{VSS 67.1}**

Kama Wakristo, tunapaswa kuzungumza kama Kristo ambavyo angezungumza ikiwa angekuwa katika nafasi yetu. Tunatamani kuona matengenezo yakifanyika, lakini mara nyingi mambo yasipotokea jinsi tunavyotaka, roho mbaya huweka matone ya uchungu katika kikombe chetu, na nafsi nyingine hutiwa sumu. Kwa maneno yetu yasiyofikiriwa vizuri, tunawachokoza na kuwachochea wengine kuwa na roho ya uasi. Fanya kusudi lako kuwa kusema Kweli kwa upendo; ndipo Bwana Yesu, kwa Roho Wake, atatoa nguvu na uwezo unaohitajika. Usichanganye ubinafsi wako na jambo lolote linalofanywa kwa ajili ya Mungu. Daima dhihirisha roho ya upole na unyenyekevu ya Bwana wako.—*The Review and Herald*, Aprili 9, 1901. **{VSS 67.2}**

SEHEMU YA 2—KRISTO, MZUNGUMZAJI BORA

SURA YA 11—ASILI YA SAUTI YAKE

Matamshi Yaliyo Wazi—Yesu Ndiye mfano wetu. Sauti Yake ilikuwa yenye mvuto wa kimuziki, wala hakuwahi kuinua sauti Yake kwa nguvu nyingi au kwa mlio wa juu uliokazwa alipokuwa akizungumza na watu. Hakuzungumza kwa haraka kiasi cha kufanya maneno Yake yashonane au kufuatana bila nafasi, jambo ambalo lingefanya iwe vigumu kuelewa maana yake. Alitamka kila neno kwa uwazi, na wale walioisikia sauti Yake walitoa ushuhuda kwamba: “*Hajanena kamwe mtu yeyote kama huyu anavyonena. Yohana 7:46.*”—*The Review and Herald*, Machi 5, 1895. {VSS 71.1}

Sauti Tulivu, Yenye Bidii na Kimuziki—Kwa maneno ya upendo na matendo ya rehema, Kristo alishinda mapokeo ya zamani na amri zilizotungwa na wanadamu, na akaonyesha upendo wa Baba katika utimilifu Wake usio na mwisho. Sauti Yake tulivu, yenye bidii, na yenye mvuto wa kimuziki ulisikika juu ya roho zilizojeruhiwa kama dawa ya uponyaji.—*The Review and Herald*, Machi 5, 1901. {VSS 71.2}

Upendo Katika Mlio wa Sauti Yake—Huruma Yake nyororo iligusa mioyo iliyochoka na yenye taabu kwa mguso wa uponyaji. Hata katikati ya ghasia za maadui wenye hasira, alizungukwa na mazingira ya amani. Uzuri wa uso Wake, mvuto wa tabia Yake, na zaidi ya yote, upendo ulioonyeshwa katika mtazamo Wake na katika mlio wa sauti Yake, uliwavuta Kwake wote ambao mioyo yao haikuwa imefanywa migumu na kutokuamini. Kama si kwa roho ile ya upole na huruma iliyodhihirika katika kila mtazamo na kila Neno Lake, asingevutia makutano makubwa kama yale yaliyomkusanyikia.—*Tumaini la Vizazi Vyote*, uk. 254. {VSS 71.3}

Kama Muziki Masikioni—Sauti ya Mwokozi ilikuwa kama muziki masikioni mwa wale waliokuwa wamezoea mahubiri yasiyo na mvuto, jotojoto, na yasiyo na nguvu ya kiroho ya waandishi na Mafarisayo, ambayo yalikuwa hayavutii kwani yalikuwa yale yale kila kila siku, bila ya kubadilisha sauti au kuweka msisitizo. Alizungumza polepole, kwa mguso na kwa msisitizo, akisisitiza maneno yale ambayo alitaka wasikilizaji Wake wayape umakini wa pekee. Wazee kwa vijana, wasio na elimu

kwa wasomi, wote waliweza kufahamu kikamilifu maana ya Maneno Yake. Jambo hilo lisingewezekana ikiwa angezungumza kwa haraka, akiharakisha kusema sentensi moja baada ya nyingine kwa kufuatana bila mapumziko. Watu walimsikiliza kwa makini sana, na ilisemekana juu Yake kwamba hakuzungumza kama waandishi na Mafarisayo, kwa maana maneno Yake yalikuwa kama ya mtu mwenye mamlaka.—*Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi*, uk. 240. {VSS 72.1}

Mlio wa Asili wa Sauti— Kama angeinua sauti Yake kwa kiwango kisicho cha kawaida, ... mvuto wa hisia na uzuri wa sauti ya mwanadamu ungepotea, na sehemu kubwa ya nguvu ya Kweli ingepungua.—*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 56. {VSS 72.2}

Muziki Mtamu Katika Sauti Yake— Katika siku zangu za ujana nilikuwa nikizungumza kwa sauti ya juu sana. Bwana alinionyesha kwamba nisingeweza kutoa mvuto unaofaa kwa watu kwa kuiinua sauti yangu kufikia kiwango kisicho cha kawaida. Kisha Kristo alionyesha mbele yangu pamoja na namna Yake ya kuzungumza; na niliona kwamba kulikuwa na muziki mtamu katika sauti Yake. Sauti Yake, ilipokuwa ikizungumza kwa utulivu na polepole, iliwafikia wale waliokuwa wakimsikiliza, na Maneno Yake yaliingia moyoni mwao kiasi kwamba waliweza kuelewa kikamilifu kile alichokuwa akisema kabla hata hajaanza sentensi iliyofuata. Wengine huonekana kufikiri kwamba ni lazima wazungumze kwa haraka sana, vinginevyo watapoteza msukumo/ari/uvuvio na watu nao watapoteza mguso au hamasa. Ikiwa huo ndio mguso au ari kwa wanaodai kuwa nao, basi ni bora wauache upotee; na kadiri unavyopotea haraka ndivyo itakavyokuwa bora zaidi.—*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 670. {VSS 72.3}

Kristo, Mwalimu wa Usemi kwa Wanafunzi Wake—Ikiwa sauti itaratibiwa vizuri, ikiwa itabeba uzito au adhima, na ikiwa itabadilishwa kwa namna inayogusa hisia za moyo, italeta mvuto mkubwa zaidi. Hii ndiyo ilikuwa namna ya sauti

ambayo Kristo aliitumia alipowafundisha wanafunzi Wake. Aligusa mioyo kwa uzito wa mada na unyenyekevu; alizungumza kwa namna iliyogusa hisia zao za ndani za huruma, sikitiko na huzuni.—*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 2, uk. 615. **{VSS 73.1}**

Machozi Katika Sauti Yake—Aliukemea bila woga unafiki, kutokuamini, na uovu; lakini machozi yalikuwa katika sauti Yake alipokuwa akitoa makaripio Yake makali.—*Tumaini ya Vizazi Vyote*, uk. 353. **{VSS 73.2}**

Sauti Kama Tarumbeta ya Mungu—Katika ulimwengu wenye shughuli nyingi, uliojaa kelele za biashara na mabishano ya shughuli za kibiashara, ambamo wanadamu walikuwa wakijitahidi kwa ubinafsi kujipatia kila walichoweza kwa ajili yao wenyewe, Kristo alikuja; na juu ya vurugu hiyo yote, sauti Yake kama tarumbeta ya Mungu ilisikiwa ikisema: **“Mtu atafaidika nini akiupata ulimwengu wote, akipata hasara ya nafsi yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake?”**—*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 559. **{VSS 73.3}**

Sauti Safi na Yenye Mlio wa Nguvu Katika Hekalu—Macho Yake yalitazama juu ya umati mkubwa wa watu, akimwona kila mtu mmoja mmoja. Mwonekano Wake ulionekana kuinuka juu yao kwa heshima yenye mamlaka, na nuru ya Kiungu/mbinguni ikaangaza katika uso Wake. Alizungumza, na sauti Yake safi yenye mlio wa nguvu—ile ile iliyotangaza sheria juu ya Mlima Sinai ambayo makuhani na watawala walikuwa wakiivunja—ilisikika ikirudia ndani ya matao ya hekalu: **“Yaondoeni haya; msiiifanye nyumba ya Baba Yangu kuwa nyumba ya biashara.”** Yohana 2:16—*Tumaini ya Vizazi Vyote*, uk. 158. **{VSS 73.4}**

Sauti Isiyo na Mfano—Walitazama mikono na miguu Yake iliyotiwa alama na misumari ya kikatili. Waliitambua sauti Yake, sauti ambayo hawakuwa wamewahi kuisikia kutoka kwa mtu mwingine yeyote. **“Basi walipokuwa hawajaamini kwa furaha, huku wakistaajabu, aliwaambia, Mna chakula cho chote hapa?”** Luka 24:41 —*Tumaini ya Vizazi Vyote*, uk. 803. **{VSS 74.1}**

SURA YA 12—UFANISI WA UWASILISHAJI

Kila Neno Likiwa Harufu ya Uzima—Popote alipokuwa—iwe katika sinagogi, kando ya njia, ndani ya mashua iliyosukumwa nje kidogo ya ufukoni, kwenye karamu ya Farisayo, au mezani kwa mtoza ushuru—Kristo aliwaambia watu mambo yaliyohusu uzima wa juu zaidi; mambo ya asili na matukio ya maisha ya kila siku aliyafungamanisha na Maneno ya Kweli, hivyo mioyo ya wasikilizaji Wake ilivutwa Kwake kwa sababu alikuwa amewaponya wagonjwa wao, kuwafariji waliokuwa na huzuni, na kuwachukua watoto wao mikononi Mwake na kuwabariki, na alipofungua midomo Yake kuzungumza, umakini wao ulimwelekea kabisa, na kila Neno Lake lilikuwa kwa nafsi fulani harufu ya uzima iletayo uzima.—*Mifano ya Masihi*, uk. 338. **{VSS 75.1}**

Usemi wa Kristo Akiwa Mtoto—Mara tu alipoanza kuzungumza, Kristo alitumia kipawa cha usemi ndani ya duru la familia,, na miongoni mwa marafiki na watu aliofahamiana nao, kwa namna isiyo na kosa lolote, na hakuna hata neno moja lisilo safi lililoropokwa kutoka katika midomo Yake. —*Huduma ya Ustawi*, uk. 286, 287. **{VSS 75.2}**

Mvuto kwa Wasomi—Baada ya Yusufu na Mariamu kumtafuta Yesu kwa siku tatu, walimpata katika ua wa hekalu akiwa ameketi katikati ya walimu, akiwasikiliza na kuwauliza maswali; na wote waliomsikia walishangazwa na

ufahamu Wake na majibu Yake, kwa maana aliuliza maswali Yake kwa neema iliyowavutia sana watu hao wenye elimu, na mama Yake hakuweza kujizuia kutambua maneno Yake, roho Yake, na utiifu Wake wa hiari kwa kila hitaji Lake. — *Wana na Binti za Mungu*, uk. 134. {VSS 75.3}

Wasikilizaji Wake Walivutiwa Kabisa—Wakulima wasio na elimu na wavuvi kutoka maeneo ya jirani, askari wa Kirumi kutoka ngome za Herode, viongozi waliokuwa na panga pembeni mwao tayari kukomesha jambo lolote lililoonekana kuwa na dalili za uasi, watoza ushuru wenye tamaa kutoka vibandani mwao vya kukusanyia kodi, na makuhani waliovaa vifuko vya maandiko kutoka katika Baraza Kuu la Wayahudi-Sanhedrin, wote walimsikiliza [Yohana Mbatizaji] kana kwamba walikuwa wamenaswa na nguvu ya maneno yake; na wote, hata Mafarisayo na Masadukayo, wale waliokuwa na mioyo migumu na waliodharau mambo ya kiroho, waliondoka wakiwa wameacha dhihaka zao, huku mioyo yao ikiwa imekatwakatwa/imechomwa kwa kutambua dhambi zao, na Herode katika jumba lake la kifalme aliusikia ujumbe huo, naye mtawala huyo mwenye kiburi na aliyeufanya moyo wake kuwa mgumu kwa dhambi alitetemeka aliposikia mwito wa toba.—*Watenda Kazi wa Injili*, uk. 55. {VSS 76.1}

Mamlaka Katika Sauti Yake—Aliweza kumwambia mtu yeyote aliyemtaka: “*Nifuate*,” naye aliyeitwa alisimama na kumfuata; nguvu ya mvuto wa ulimwengu ilivunjwa, na kwa kusikia sauti Yake, roho ya tamaa na kiburi cha kutafuta makuu iliondoka moyoni mwao, nao watu wakasimama wakiwa wamewekwa huru ili kumfuata Mwokozi. —*Huduma ya Uponyaji*, uk. 25. {VSS 76.2}

Maisha Yake Yakiwa Mfano wa Maneno Yake—Alifundisha kile alichoiishi, na aliwaambia wanafunzi Wake: “*Nimewapa kielelezo; ili kama Mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo.*” “*Kama vile Mimi nilivyoziishika amri za Baba yangu.*” (*Yohana 13:15; 15:10*). Hivyo, katika maisha Yake, maneno ya Kristo yalikuwa na mfano na uthibitisho mkamilifu katika kutenda-Yalipatana na maneno; zaidi ya hayo, kile alichofundisha Yeye Mwenyewe alikuwa, na maneno Yake hayakuwa tu maelezo ya uzoefu Wake binafsi wa maisha, bali yalikuwa pia udhihirisho wa tabia Yake mwenyewe. —*Elimu*, uk. 78, 79. {VSS 76.3}

Roho Yake Ilikuwa Ufunuo wa Mafundisho Yake—Mafundisho ya Kristo hayakugusa mioyo ya wasikilizaji Wake kwa ishara zozote za nje, bali kwa maneno

Yake, matendo ya maisha Yake ya kila siku, na kwa roho aliyodhihirisha. —
Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi, uk. 399. {VSS 77.1}

Mafundisho Yenye Nguvu na Mvuto—Kuna ufasaha wenye nguvu zaidi kuliko ufasaha wa maneno katika maisha tulivu, thabiti, endelevu, na safi ya Mkristo wa kweli; kwa maana mtu alivyo ana ushawishi mkubwa zaidi kuliko asemavyo. {VSS 77.2}

Maafisa waliotumwa kwa Yesu walirudi na ushuhuda kwamba: Kamwe *“Hajanena kamwe mtu ye yote kama huyu anavyonena.” Yohana 7:46* Lakini sababu ya jambo hilo ilikuwa kwamba hakuna mwanadamu aliyewahi kuishi kama Yeye alivyoishi; kwa maana kama maisha Yake yangekuwa tofauti na yalivyokuwa, Asingeliweza kusema kama alivyosema. Maneno Yake yalikuwa na nguvu ya kushawishi kwa sababu yalitoka katika moyo safi na mtakatifu, uliojaa upendo, huruma, wema, ukarimu na Kweli. —*Huduma ya Uponyaji*, uk. 469. {VSS 77.3}

Maneno Yenye Neema—Mafarisayo walijawa na wendawazimu wa chuki kali dhidi Yake, kwa sababu waliona kwamba mafundisho Yake yalikuwa na nguvu na mvuto ambao maneno yao hayakuwa nayo hata kidogo. Waliamua kwamba njia pekee ya kukomesha ushawishi Wake ilikuwa kutoa hukumu ya kifo juu Yake, na hivyo wakawatuma maafisa wamkamate; lakini maafisa hao walipofika mahali ambapo wangeweza kusikia sauti Yake, na waliposikiliza maneno Yake yenye neema, walivutwa na kuguswa sana, kiasi kwamba wakasahau kabisa kusudi la utume wao. —*Manuscript 33, 1911*. {VSS 77.4}

Mvuto wa Mwonekano na Maneno Yake—Mwonekano wa Yesu na maneno Yake wakati wa kesi Yake yaliacha mvuto mkubwa katika akili za wengi waliokuwapo wakati huo. —*Maandiko ya Awali*, uk. 174. {VSS 78.1}

Nguvu Hai—Uso wa Mwokozi uliangazwa kwa nuru ya mbinguni; Alionekana kana kwamba alikuwa katika uwepo wa Yule asiyeonekana, na kulikuwa na nguvu hai katika Maneno Yake, kama ya mtu anazungumza akiwa pamoja na Mungu.—*Mlima wa Baraka*, uk. 102. {VSS 78.2}

SURA YA 13—UPENDO, HURUMA, NA FADHILI

Busara, Siyo Ukali—Mwokozi hakuwahi kuzuia Kweli, bali aliutamka daima kwa upendo. Katika mahusiano Yake na wengine alionyesha busara kuu, na sikuzote alikuwa mwenye fadhili na mwenye kujali wengine. Hakuwahi kuwa mkali au asiye na adabu; hakuwahi kusema neno kali bila sababu, wala kusababisha maumivu yasiyo ya lazima kwa mwenye kuguswa kwa urahisi. Hakukemea udhaifu wa kibinadamu, bali aliushutumu bila woga unafiki, kutokuamini, na uovu. Hata hivyo, machozi yalikuwa katika sauti Yake alipokuwa akitoa makaripio Yake makali. Hakuwahi kuifanya Kweli kuwa ya kikatili, bali daima alionyesha huruma kuu kwa wanadamu. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 117. {VSS 79.1}

Maneno Kama Dawa ya Uponyaji—Makutano mengi ambayo hayakupendeza na hotuba za marabi yalivutwa na mafundisho Yake. Waliweza kuyaelewa maneno Yake, na mioyo yao ilipata joto na faraja. Alimzungumzia Mungu, si kama hakimu mwenye kulipiza kisasi, bali kama Baba mwenye huruma; Naye alifunua sura ya Mungu kama ilivyoakisiwa ndani Yake Mwenyewe. Maneno Yake yalikuwa kama dawa ya uponyaji kwa roho zilizojeruhiwa. Kwa Maneno Yake na matendo Yake ya rehema, alikuwa akivunja nguvu ya ukandamizaji ya mapokeo ya kale na amri zilizotungwa na wanadamu, na kuonyesha upendo wa Mungu katika ukamilifu wake usio na mwisho. —*Tumaini la Vizazi Vyote*, uk. 205. {VSS 79.2}

Huruma Katika Kuzungumza na Kusikiliza—Maisha ya Kristo yalijaa maneno na matendo ya wema, ukarimu, fadhila, huruma, na upendo. Sikuzote alikuwa tayari kusikiliza na kupunguza huzuni za wale waliomjia. Makutano mengi yalibeba ndani ya nafsi zao wenyewe ushahidi wa nguvu Yake ya Kiungu. Hata hivyo, baada ya kazi hiyo kukamilika, wengi waliona aibu kwa sababu ya Mwalimu huyo mnyenyekevu lakini Mwenye nguvu. Kwa kuwa watawala hawakumwamini, watu hawakuwa tayari kumpokea Yesu. Alikuwa mtu wa huzuni, aliyezoea masikitiko. Hawakuweza kuvumilia kuongozwa na maisha Yake ya kiasi, kujikana nafsi, na kujitoa. Walitamani kufurahia heshima ambayo ulimwengu huwapa wanadamu. Hata hivyo, wengi walimfuata Mwana wa Mungu na kusikiliza mafundisho Yake, wakijilisha na kufaidi Maneno yaliyotoka midomoni Mwake kwa neema nyingi. Maneno Yake yalikuwa yamejaa maana, lakini yalikuwa wazi kiasi kwamba hata walio dhaifu waliweza kuyaelewa. —*Maandiko ya Awali*, uk. 160. **{VSS 80.1}**

Uhakikisho wa Kweli—Maneno ya Bwana yalikuwa wazi na yenye kutamkwa kwa usahihi, na yalisemwa kwa huruma nyororo, kujali, upendo mwanana na upole. Yalibeba ndani yake uhakikisho kwamba hapo palikuwa na Kweli. Ilikuwa ni usahihi, unyenyekevu na bidii ambayo Kristo alionyesha katika kufanya kazi na kuzungumza iliyowavuta wengi Kwake. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 53. **{VSS 80.2}**

Faraja na Upole—Hata katika utoto Wake, Kristo alisema Maneno ya faraja na upole kwa vijana na wazee. Alikuwa mfano wa kile ambacho watoto wote wanaweza kujitahidi kuwa. Katika maneno na matendo Yake alionyesha huruma nyororo na kujali kwa wote. Ushirika Wake ulikuwa kama dawa ya uponyaji na utulizaji kwa waliokata tamaa na waliovunjika moyo. —*Wana na Binti za Mungu*, uk. 151. **{VSSw 80.3}**

SURA YA 14—UTULIVU WA SUBIRA

Yasiwepo Maneno ya Haraka Wala ya Hasira—Kwa msaada ambao Kristo anaweza kutupatia, tutaweza kujifunza kuutawala ulimi wetu. Ingawa alijaribiwa sana katika suala la kusema kwa haraka na kwa hasira, hakuwahi hata mara moja kutenda dhambi kwa midomo Yake. Kwa utulivu wa subira, alivumilia dhihaka, kejeli, na maneno ya kudharau kutoka kwa wafanyakazi wenzake katika karakana ya useremala. Badala ya kujibu kwa hasira, alianza kuimba mojawapo ya zaburi nzuri za Daudi; na wenzake, kabla hawajatambua walichokuwa wakifanya, waliungana Naye katika wimbo huo. Ni mabadiliko makubwa kiasi gani yangetokea katika ulimwengu huu ikiwa wanaume na wanawake leo wangeufuata mfano wa Kristo katika matumizi yao ya maneno! —*The S.D.A. Bible Commentary*, juz. 7, uk. 936. **{VSS 82.1}**

Upole wa Tabia—Upendo utafanya jambo ambalo mabishano au hoja haziwezi kulitimiza. Lakini kukasirika kwa muda mfupi, jibu moja lenye ukali, au ukosefu wa adabu, uungwana na staha ya Kikristo katika jambo dogo kunaweza kusababisha kupotea kwa marafiki na ushawishi. **{VSS 82.2}**

Kile ambacho Kristo alikuwa alipokuwa duniani, ndivyo mtendakazi Mkristo anapaswa kujitahidi kuwa. Yeye ni mfano wetu, sio tu katika usafi Wake usio na doa, bali pia katika uvumilivu Wake, upole Wake, na tabia Yake yenye kuvutia. Maisha Yake yalikuwa mfano wa uungwana na staha ya kweli. Siku zote alikuwa na mtazamo wa fadhili na neno la faraja kwa wahitaji na wanadamu waliokandamizwa. Uwepo Wake ulileta mazingira safi zaidi ndani ya nyumba. Maisha Yake yalikuwa

kama chachu inayofanya kazi katikati ya jamii. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 121. {VSSw 82.3}

SURA YA 15—URAHISI

Lugha Rahisi Zaidi—Kristo daima alitumia lugha rahisi zaidi, lakini Maneno Yake yalipokelewa na watu wenye fikra za kina na akili zilizo wazi, na zisizo na ubaguzi kwa sababu yalikuwa maneno yaliyopima na kujaribu hekima yao. Mambo ya kiroho yanapaswa sikuzote kuwasilishwa kwa lugha rahisi, hata wakati wanafunzi wenye elimu wanapofundishwa; kwa maana mara nyingi watu wenye elimu hawana uelewa wa kutosha kuhusu mambo ya kiroho. Lugha rahisi zaidi ndiyo yenye ufasaha mkubwa zaidi. Wenye elimu na wasio na elimu wanapaswa kuzungumziwa kwa namna iliyo wazi na rahisi zaidi, ili Kweli iweze kueleweka na kukaa makazi ndani ya moyo. Hivyo ndivyo Kristo alivyowafundisha makutano makubwa yaliyomzunguka; na wote, wenye elimu na wasio na elimu, waliweza kuelewa mafundisho Yake. —*The Review and Herald*, Mei 18, 1897. {VSSw 84.1}

Unyenyekevu kwa Wenye Elimu na Watu wa Kawaida—Mwalimu mkuu kuliko wote ambaye ulimwengu umewahi kumjua aliheshimiwa kwa sababu ya unyenyekevu wake; kwa maana aliwasilisha Kweli ya Mungu kwa namna ambayo hata watoto waliweza kuelewa Maneno Yake, na wakati huohuo aliweza kuvuta fikira za watu wenye elimu bora zaidi na wenye fikra za kina zaidi duniani. Kwa kutumia mifano iliyokuwa ya kawaida kwao, aliifanya Kweli iwe wazi katika akili za watu wa kawaida. Kwa urahisi, alipanda mbegu ya Kweli ya Injili katika akili na mioyo ya wasikilizaji Wake, nayo ikaota na kuzaa mavuno ya uzima wa milele. —*Wana na Binti za Mungu*, uk. 86. {VSSw 84.2}

Mifano Inayofaa—Alizungumza nao kwa lugha rahisi kiasi kwamba hawangeweza kushindwa kuelewa. Kwa njia zilizokuwa Zake pekee, aliwasaidia wote waliokuwa katika huzuni na mateso. Kwa neema nyororo, uungwana na

heshima, Aliwahudumia watu waliokuwa wagonjwa wa dhambi rohoni, akiwaletea uponyaji na nguvu. **{VSS 85.1}**

Akiwa Mkuu wa walimu, alitafuta njia ya kuwafikia watu kupitia mambo waliyoyazoea katika maisha yao ya kila siku. Aliwasilisha Kweli kwa namna ambayo tangu wakati huo ilifungamana na kumbukumbu zao takatifu zaidi na hisia zao za ndani na huruma. Alifundisha kwa namna iliyowafanya wahisi kwamba alihusika kikamilifu na masilahi yao pamoja na furaha yao. Mafundisho Yake yalikuwa ya moja kwa moja, mifano Yake ilikuwa yenye kufaa sana, na maneno Yake yalikuwa yenye huruma na uchangamfu kiasi kwamba wasikilizaji Wake walivutiwa sana. Urahisi na bidii aliyokuwa nayo alipowahutubia wahitaji vilifanya kila neno Lake liwe lenye uzito na utakatifu. —*Huduma ya Uponyaji*, uk. 23, 24. **{VSS 85.2}**

Kweli ya Kiroho Ikiwasilishwa kwa Urahisi—Kristo hakuwahi kujipendekeza kwa wanadamu au kuwadanganya kwa kuwasifia kwa kutia chumvi. Hakusema kamwe jambo ambalo lingekuza mawazo yao ya kujiona au mawazo yao ya kubuni, wala hakuwasifu kwa uvumbuzi wao wa werevu; bali watu wenye fikra za kina na wenye akili zilizo wazi walipokea mafundisho Yake na kugundua kwamba yalikuwa yakijaribu hekima yao. Walistaajabia Kweli za kiroho zilizowasilishwa kwa lugha rahisi zaidi. —*Tumaini la Vizazi Vyote*, uk. 254. **{VSS 85.3}**

Kweli Iliyo Wazi Hata kwa Mtoto—Maneno ya uzima yaliwasilishwa kwa urahisi kiasi kwamba hata mtoto angeweza kuyaelewa. Wanaume, wanawake, na watoto walivutiwa sana na namna Yake ya kueleza Maandiko kiasi kwamba walishika/walidaka hata namna ya matamshi ya sauti Yake, wakaweka msisitizo uleule katika maneno yao, na kuiga ishara Zake. —*Mashauri kwa Afya*, uk. 498, 499. **{VSS 86.1}**

Maneno Rahisi Zaidi na Mifano Iliyo Wazi Zaidi—Mwokozi alikuja “*kuwahubiria maskini habari njema.*” (*Luka 4:18*). Katika mafundisho Yake alitumia maneno rahisi zaidi na mifano iliyo wazi zaidi. Na imeandikwa kwamba “*watu wa kawaida walimsikiliza kwa furaha.*” (*Marko 12:37*). Wale wanaotafuta kufanya kazi Yake katika wakati huu wanahitaji ufahamu wa kina zaidi wa mafundisho ambayo ametoa. —*Huduma ya Uponyaji*, uk. 443. **{VSS 86.2}**

Kama Dawa ya Gileadi—Watu walisikiliza maneno ya rehema yaliyotiririka kwa wingi kutoka midomoni mwa Mwana wa Mungu. Walisikia maneno yenye neema, rahisi, na yaliyo wazi kiasi kwamba yalikuwa kama uponyaji/dawa ya Gileadi kwa roho zao. —*Tumaini la Vizazi Vyote*, uk. 365. {VSS 86.3}

Lugha Yenye Nguvu/msukumo Lakini Rahisi—Kristo aliwafikia watu katika hali waliyokuwa nayo. Aliwasilisha Kweli iliyo wazi kwa akili zao kwa lugha rahisi lakini yenye nguvu kubwa. Maskini wanyenyekevu na watu wasio na elimu waliweza kuelewa, kwa njia ya imani Kwake, Kweli za juu na kuu zaidi. Hakuna mtu aliyelazimika kwenda kuwauliza walimu wenye elimu ili kupata maana ya Maneno Yake, kwa kuwa hakuwachanganya watu wasio na ujuzi kwa mafumbo yasiyoeleweka wala kutumia maneno magumu ya kielimu ambayo hawakuwa na ufahamu nayo. Mwalimu mkuu kuliko wote ambaye ulimwengu umewahi kumjua alikuwa mwenye kueleza kwa uwazi zaidi, kwa urahisi zaidi, na kwa matumizi ya moja kwa moja zaidi katika mafundisho yake. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 49, 50. {VSS 86.4}

Kweli Kuu za Maadili Zikiwa na Uhai na Nguvu Mpya—Yesu, Mwalimu mkuu, alifunua Kweli kuu za maadili kwa lugha rahisi zaidi, akizivisha uzuri wa uhai mpya na nguvu. —*The Review and Herald*, Machi 21, 1893. {VSS 87.1}

Kweli Rahisi na Zenye Kulenga Moja kwa Moja—Yeye [Yesu] alifanya kazi daima kwa kusudi moja; nguvu Zake zote zilitumika kwa ajili ya wokovu wa wanadamu, na kila tendo la maisha Yake lilielekezwa kwenye kusudi hilo. Alisafiri kwa miguu, akiwafundisha wafuasi Wake alipokuwa akiendelea na safari. Mavazi Yake yalikuwa yamefunikwa na vumbi na alama za safari, na mwonekano Wake haukuwa wa kuvutia kwa macho ya wanadamu. Lakini Kweli rahisi na zenye kulenga moja kwa moja zilizotoka katika midomo Yake ya Kiungu, ziliwafanya wasikilizaji Wake wasahau upesi mwonekano Wake; nao walivutiwa, sio kwa sura ya mtu huyo, bali na mafundisho aliyoyatoa. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 4, uk. 373. {VSS 87.2}

Hakuna Jambo Lisilo la Lazima—Maneno ya Kristo hayakuwa na jambo lolote lisilo la lazima. Mahubiri ya Mlimani ni kazi ya ajabu sana, lakini ni rahisi kiasi kwamba hata mtoto anaweza kuyasoma bila kupotosha maana yake. Mlima wa Baraka/Heri ni ishara ya hali ya juu ya kiroho ambayo Kristo alikuwa amesimama

juu yake daima. Kila Neno alilotamkalilitoka kwa Mungu, Naye alizungumza kwa mamlaka ya mbinguni. Alisema: “*Maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima.*” (Yohana 6:63). —**Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi**, uk. 439. {VSS 87.3}

Hakuna Gwaride la Kujionyesha kwa Ufasaha wa Kibinadamu—Katika Maneno haya yaliyosemwa na Mwalimu mkuu kuliko wote ambaye ulimwengu umewahi kumjua, hakuna kujionyesha kwa ufasaha wa kibinadamu. Lugha Yake ni wazi, na mawazo pamoja na hisia Zake vina sifa ya urahisi mkubwa sana. Maskini, wasio na elimu, na wale wenye ufahamu mdogo kabisa waliweza kuyaelewa. Bwana wa mbingu alikuwa akizungumza kwa rehema na fadhili kwa nafsi alizokuja kuziokoa. Aliwafundisha kama mtu mwenye mamlaka, akisema Maneno ya uzima wa milele. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 5, uk. 254. {VSS 88.1}

SURA YA 16—NGUVU, MAMLAKA, NA BIDII

Mamlaka Thabiti—Kweli za kivitendo alizozisema Kristo zilikuwa na nguvu ya kushawishi na zilivuta umakini wa watu, kiasi kwamba makutano mengi yalika karibu Naye yakistaajabia hekima Yake. Namna Yake ya kuzungumza ililingana na Kweli kuu alizozitangaza, kwa kuwa hakukuwa na kuomba msamaha, kusita, wala hata kivuli cha shaka au kutokuwa na uhakika kwamba jambo hilo lingeweza kuwa tofauti na alivyolitangaza. Alizungumza kuhusu mambo ya duniani na ya mbinguni, kuhusu mambo ya kibinadamu na ya Kiungu, akiwa na mamlaka thabiti; na watu “walishangazwa na mafundisho Yake, kwa maana Neno Lake lilikuwa na nguvu.” —*The Review and Herald*, Julai 6, 1911. {VSS 89.1}

Mamlaka Iliyokuwa Yake Pekee—Kristo alifundisha kwa mamlaka. Mahubiri ya Mlimani ni kazi ya ajabu sana, lakini ni rahisi kiasi kwamba hata mtoto anaweza kuyasoma bila kupotoshwa. Mlima wa Heri ni mfano wa hali ya juu ya kiroho ambayo Kristo alikuwa amesimama juu yake daima, Naye alizungumza kwa

mamlaka ambayo yalikuwa Yake pekee. —*Misingi ya Elimu kwa Kila Mwanadamu*, uk. 407. {VSS 89.2}

Mamlaka ya Kifalme Juu ya Makuhani wa Hekalu— Kristo alizungumza kwa mamlaka ya kifalme, na katika mwonekano Wake pamoja na toni ya sauti Yake kulikuwa na nguvu ambayo hawakuwa na uwezo wa kuipinga. Kwa Neno Lake la amri, walitambua, kama ambavyo hawakuwahi kutambua hapo awali, hali yao halisi ya kuwa wanafiki na wanyang’anyi. —*Tumaini la Vizazi Vyote*, uk. 162. {VSS 89.3}

Nguvu Isiyoweza Kuzuiwa— Kwa uwazi na nguvu, Kristo alisema Maneno ambayo yangeshuka na kuja hadi kwenye wakati wetu kama hazina ya wema. Maneno hayo yalikuwa ya thamani jinsi gani, na yalijaa faraja kwa kiwango gani! Kutoka katika midomo Yake ya Kiungu yalitiririsha kwa wingi na kwa uhakika mkubwa baraka zilizomdhihirisha kuwa Yeye ndiye chemchemi ya wema wote, na kwamba ilikuwa haki Yake kuwabariki na kugusa akili za wote waliokuwapo. {VSS 90.1}

Kulikuwa na nyakati ambapo Kristo alizungumza kwa mamlaka iliyofanya Maneno Yake yafikie mioyo kwa nguvu isiyoweza kuzuiwa, pamoja na hisia kuu ya ukuu wa Mzungumzaji ilifanya watu watekewe; na wanadamu waliokuwa mbele Yake walionekana kuwa wadogo kabisa walipolinganishwa na Yule aliyekuwa mbele yao. Waliguswa sana, na akili zao zilivutwa na kuguswa, hata kutambua kwamba alikuwa akirudia amri kutoka katika utukufu mkuu wa mbinguni. Alipoiita dunia imsikilize, walivutiwa kabisa na kunaswa na mvuto huo, na usadikisho ukaingia ndani ya mioyo yao. Kila Neno lilijipatia nafasi yake ndani yao, na wasikilizaji waliamini na kuyapokea maneno ambayo hawakuwa na uwezo wa kuyapinga. Kila neno alilolinena liliwaonekana wasikilizaji Wake kuwa kama uzima wa Mungu. —*The S.D.A. Bible Commentary*, juz. 5, uk. 1084, 1085. {VSS 90.2}

Nguvu Kama Dhoruba Kuu—Kristo alizungumza kwa nguvu iliyowatikisa watu kama dhoruba kuu aliposema: *“Imeandikwa, Nyumba Yangu itaitwa nyumba ya sala; lakini ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang’anyi.”* Mathayo 21:13 Sauti Yake ilisikika kama tarumbeta ndani ya hekalu, na hasira ya haki iliyonekana katika uso Wake ilifanana na moto unaoteketeza. Kwa mamlaka akaamuru: *“Yaondoeni haya.”* (Yohana 2:16). —*Tumaini la Vizazi Vyote*, uk. 591. {VSS 90.3}

Mfano kwa Baba, Kielelezo kwa Watoto—Yesu alikuwa mfano kwa watoto, na pia alikuwa kielelezo kwa baba. Alizungumza kama mtu mwenye mamlaka, na neno Lake lilikuwa na nguvu; hata hivyo, katika mahusiano Yake yote na watu wakorofi na wenye jeuri, hakutumia hata kauli moja isiyo na fadhili wala isiyo ya heshima. —*Tumaini la Vizazi Vyotes*, uk. 515. {VSS 91.1}

Miito Iliyojaa Huruma na Kujali—Kulikuwa na mamlaka ya pekee katika matakwa Yake na ahadi Zake, na miito Yake ilikuwa imejaa huruma na kusihi kwa upole. Kwa upendo wa namna gani aliwaambia watu waliokuwa wakitaabika kwa kazi: “*Njoni Kwangu ninyi nyote msumbukao na kulemewa na mizigo, Nami nitawapumzisha.*” Mathayo 11:28 Kwa nguvu na huruma kubwa kiasi gani Yesu alipaza sauti Yake akisema: “*Mtu akiona kiu, na aje Kwangu anywe.*”—*The Review and Herald*, Februari 21, 1893. {VSS 91.2}

Hakuna Kusita Wala Kutokuwa na Uhakika—Alizungumza kama mtu mwenye mamlaka, wala si kama waandishi waliokuwa wakizungumza kwa kusita na bila uhakika. Kwa utulivu na nguvu, alitangaza kanuni hai za Kweli, akizifanya ziwe na mvuto mkubwa zaidi kupitia namna Yake ya kuziwasilisha. —*The Review and Herald*, Agosti 20, 1903. {VSS 91.3}

Hakuna Kivuli cha Shaka—Kristo alikuja kuifunua Kweli ya Mungu kwa ulimwengu. Alifundisha kama mtu mwenye mamlaka. Alisema kwa namna ambayo hakuna mwanadamu mwingine aliyewahi kusema. Hakukuwa na kusita katika mwenendo Wake, wala kivuli chochote cha shaka katika maneno Yake. Alizungumza kama mtu aliyeielewa kila sehemu ya jambo alilokuwa akilifundisha. —*Misingi ya Elimu kwa Kila Mwanadamu*, uk. 236, 237. {VSSw 92.1}

Ujuzi Binafsi wa Kristo—Kristo alizungumza kwa mamlaka. Kila Kweli muhimu ambayo watu walipaswa kujua aliitangaza kwa uhakika usiotetereka unaotokana na maarifa ya hakika. Hakusema mambo ya kubuni au ya hisia tu. Hakuwasilisha hoja za udanganyifu wala mawazo ya kibinadamu. Hakuna hadithi zisizo na maana wala nadharia za uongo zilizofunikwa kwa lugha nzuri zilizotoka midomoni Mwake. Kauli Zake zilikuwa Kweli zilizothibitishwa na ujuzi Wake binafsi. Aliona mapema mafundisho ya upotoshaji ambayo yangeujaza ulimwengu, lakini hakuyafafanua. Katika mafundisho Yake alikazia kanuni zisizobadilika za

Neno la Mungu. Aliinua Kweli rahisi na za kivitendo ambazo watu wa kawaida wangeweza kuzielewa na kuzitumia katika maisha yao ya kila siku. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 8, uk. 201. {VSSsw 92.2}

Bidii, Ari na Uhakika—Yesu alipozungumza, hakuzungumza kwa kusita au kwa kutokuwa na uhakika, wala kwa kurudia maneno bila sababu au kutumia mifano iliyozoeleka tu. Kweli ilitoka midomoni Mwake ikiwa imewasilishwa kwa maelezo mapya na yenye kuvutia, yaliyoiweka katika hali mpya kana kwamba ilikuwa ufunuo mpya. {VSSsw 92.3}

Sauti Yake haikuwahi kuinuliwa kwa kiwango kisicho cha kawaida, bali Maneno Yake yalitoka kwa udhati/bidii na uhakika uliolingana na umuhimu wake pamoja na matokeo makubwa yaliyohusika katika kuyakubali au kuyakataa. Mafundisho Yake yalipopingwa, aliyatetea kwa bidii na uhakika mkubwa kiasi kwamba wasikilizaji Wake waliona kwamba angekuwa tayari hata kufa ili kulinda mamlaka ya mafundisho Yake. Alipofundisha, maneno Yake yalikuja kwa mamlaka, kwa maana alisema akiwa na ujuzi thabiti kuhusu Kweli hiyo. —*The Review and Herald*, Januari 7, 1890. {VSSsw 92.4}

Kweli Ikiwa na Uhai Mpya Kama Ufunuo Mpya—Kweli haikuwahi kudhoofika midomoni Mwake, wala haikuwahi kupoteza nguvu yake kwa sababu ya kutokutimiza matakwa yake. Kristo alisema: “*Mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya, na kwa ajili ya haya Mimi nalikuja ulimwenguni, ili niishuhudie Kweli.*” Yohana 18:37 Na kanuni kuu za Kweli zilitoka midomoni Mwake zikiwa na uzuri mpya kama wa ufunuo mpya. Kweli ilitamkwa Naye kwa bidii iliyolingana na umuhimu wake usio na mwisho na matokeo makubwa yaliyotegemea kuikubali au kuikataa. —*The S.D.A. Bible Commentary*, juz. 5, uk. 1148. {VSSsw 93.1}

Bidii/Udhati na Nguvu—Maneno ya Kristo, ingawa yalitamkwa kwa utulivu, yalitolewa kwa bidii na nguvu iliyogusa mioyo ya watu. Walimsikiliza wakitarajia kusikia marudio ya mapokeo yasiyo na uhai na masharti magumu ya marabi, lakini hawakuyapata. {VSSsw 93.2}

“**Makutano walishangaa mno kwa mafundisho yake; kwa maana alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi wao.**” (*Mathayo 7:28, 29*). —*Mlima wa Baraka*, uk. 46, 47. {VSSsw 93.3}

Faraja Katika Upendo na Upole—Walimsikia akizungumza kwa upendo na huruma, akiwatia moyo wale waliokuwa dhaifu na wenye mateso. Pia walimsikia akikemea kwa sauti yenye mamlaka nguvu ya Shetani na kuwaamuru mateka wake waachiliwe. Waliyasikiliza Maneno ya hekima yaliyotoka midomoni Mwake, na walivutiwa sana kiasi kwamba hawakuweza kumkamata. —*Maandiko ya Awali*, uk. 160. {VSSsw 93.4}

SURA YA 17—MANENO YA KWELI

Kweli Ikiwa Imefafanuliwa Kwa Uwazi—Mwana wa pekee wa Mungu alikuja katika ulimwengu wetu ili kuifunua Kweli kwa kuitofautisha na kosa. Kweli hii iokoayo, tunapaswa kuidhihirisha katika usemi wetu na katika mwenendo wetu unaofanana na Kristo. Kweli haikuwahi kudhoofika midomoni mwa Kristo, bali ilidhihirishwa kwa uwazi katika maneno Yake, matendo Yake, na roho Yake. —*Letter 222, 1908*. {VSSsw 95.1}

Upole, kujali, Katika Mlio wa Sauti Yake—Katika mafundisho Yake yote, Kristo aliwasilisha kanuni safi zisizochanganywa na upotoshaji wowote. Hakutenda

dhambi, wala hila haikuonekana kinywani Mwake. Sikuzote Maneno matakatifu na yenye kuinua yalitiririka kutoka midomoni Mwake. Alisema kama ambavyo hakuna mwanadamu mwingine hakuwahi kusema, akiwa na huruma yenye kugusa mioyo ya watu. Alijawa na hasira takatifu alipowaona viongozi wa Kiyahudi wakifundisha amri za wanadamu kuwa mafundisho ya Mungu, Naye aliwaambia kwa mamlaka ya ukuu wa Kweli. Kwa nguvu kuu alikemea kila hila ya ujanja na kila tendo la udanganyifu. Alilitakasa hekalu kutokana na uchafu wake, kama vile anavyotamani kuitakasa mioyo yetu kutokana na kila kitu kinachofanana na udanganyifu. Kweli haikuwahi kudhoofika midomoni Mwake. Bila woga aliufunua unafiki wa makuhani na watawala, Mafarisayo na Masadukayo. —*The Review and Herald*, Mei 12, 1910. {VSSw 95.2}

Kweli Katika Nuru Yake Halisi—Maneno ya Kristo hayakuwa mapya, lakini yalikuja na nguvu kama ya ufunuo; kwa maana yaliwasilisha Kweli katika nuru yake halisi, na si katika nuru ambayo walimu walikuwa wameiwasilisha mbele ya watu. —*The Review and Herald*, Novemba 28, 1893. {VSSw 96.1}

Kutenganisha Kosa na Kweli—Kristo angeweza kufunua siri ambazo wazee wa zamani na manabii walitamani kuzichunguza, na ambazo udadisi wa kibinadamu ulikuwa ukitamani sana kuzielewa. Lakini ikiwa wanadamu hawakuweza kutambua Kweli rahisi zilizoelezwa waziwazi, wangeweza kuelewa siri zilizofichwa kutoka kwa macho ya wanadamu? Yesu hakudharau kurudia kweli za zamani na zilizojulikana, kwa maana Yeye Ndiye mwandishi wa Kweli hizo. Yeye Ndiye utukufu wa hekalu. Kweli ambazo zilikuwa zimepuuzwa, zilizowekwa mahali pasipofaa, zilizotafsiriwa vibaya, na kutenganishwa na nafasi yake halisi, aliziondoa katika mchanganyiko wa makosa; kisha akazionyesha kama vito vya thamani vinavyong’aa kwa uzuri Wake wenyewe, akazipanga tena katika mfumo Wake unaofaa, na kuziamuru zidumu imara milele. {VSSw 96.2}

Hii ilikuwa kazi kubwa kiasi gani! Ilikuwa kazi ya namna ambayo hakuna mwanadamu mwenye ukomo au mipaka angeweza kuelewa wala kuifanya. Ni mkono wa kimungu pekee ulioweza kuichukua Kweli ambayo, kwa sababu ya kuchanganywa kwake na kosa, ilikuwa ikitumika kuendeleza kazi ya adui wa Mungu na mwanadamu, na kuiweka mahali ambapo ingemtukuza Mungu na kuwa wokovu kwa wanadamu. Kazi ya Kristo ilikuwa kuipa tena dunia Ukweli katika uchangamfu

Nhandi Masunga na Grace Momadi Masaka-Jersey 2026 July

na uzuri wake wa asili. —*The Review and Herald*, Novemba 28, 1893. {VSSw
96.3}

SURA YA 18—HAKUNA HOJA TATA/NGUMU au CHANGAMANO WALA MIJADALA MIREFU

Moja kwa Moja Kwenye Jambo Kuu—Kristo mara chache alijaribu kuthibitisha kwamba Kweli ni Kweli. Aliieleza kweli katika vipengele vyake vyote, kisha aliwaacha wasikilizaji Wake wawe huru kuikubali au kuikataa kulingana na uchaguzi wao. Hakumlazimisha mtu yeyote kuamini. Katika Mahubiri ya Mlimani, aliwafundisha watu uchaji wa Mungu unaotumika katika maisha ya kila siku,

akieleza waziwazi wajibu wao. Alizungumza kwa namna iliyoipeleka Kweli moja kwa moja kwenye dhamiri zao. Nguvu iliyoonyeshwa na wanafunzi Wake ilidhihirishwa katika uwazi, unyofu na bidii ambayo kwayo waliwasilisha Kweli. **{VSSsw 97.1}**

Katika mafundisho ya Kristo hakukuwa na hoja ndefu, za kuvutia toka mbali, wala hoja changamano zisizoeleweka. Alifika moja kwa moja kwenye kiini cha jambo. Katika huduma Yake, aliisoma kila mioyo ya watu kama kitabu kilicho wazi, na kutoka katika hazina yake isiyokwisha alitoa mambo mapya na ya zamani ili kueleza na kusisitiza mafundisho Yake. Aligusa mioyo na kuamsha hisia zao za ndani za huruma. —[Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti](#), uk. 171. **{VSSsw 97.2}**

Akili Inayotafuta Uelewa—Kristo hakuwasilisha mkusanyiko mkubwa wa kweli ambao ulipaswa kukubaliwa wote kwa wakati mmoja. Aliiongoza akili iliyokuwa ikitafuta kuelewa kutoka Kweli moja hadi nyingine, na kutoka fundisho moja hadi jingine, akifunua maana ya Maandiko kadiri walivyoweza kustahimili. Katika kila kizazi, Kweli inayohusika na wakati husika na iliyo muhimu kwa tabia na maisha, lazima ifunuliwe kwa namna hii. —*The Review and Herald*, Oktoba 14, 1890. **{VSSsw 97.3}**

Utii Haujatikani Kwa Hoja Pekee—Kristo alikuja ulimwenguni ili kuleta upinzani wote na mamlaka zote chini ya utawala Wake, lakini hakudai utii kwa nguvu ya hoja wala kwa sauti ya amri. Aliendelea kufanya mema na kuwafundisha wafuasi Wake mambo yaliyohusu amani yao. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 4, uk. 139. **{VSSsw 98.1}**

SURA YA 19—KRISTO ALIVYOCHUNGUZA NYUSO ZA WATU

Mionekano ya Nyuso—Mkombozi wa ulimwengu aliendelea kufanya mema kila mahali alipokwenda. Alipokuwa mbele ya watu, akiwatamkia maneno ya Kweli ya uzima wa milele, alizitazama kwa umakini mkubwa nyuso za wasikilizaji Wake

zilivyobadilika. Nyuso zilizoonyesha shauku kubwa na furaha waliposikiliza maneno Yake zilimletea kuridhika sana. Lakini Kweli iliposemwa waziwazi na kugusa dhambi fulani waliyokuwa wameishikilia moyoni au sanamu fulani waliyokuwa wamezipa thamani kubwa, aliona mabadiliko katika nyuso zao—mwonekano wa baridi, ukali, na kutokukubali, uliodhihirisha kwamba Kweli hiyo haikupokelewa kwa furaha. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 48. {VSS 99.1}

Kristo Ni Mfano kwa Walimu—Kristo alipokuwa akifundisha duniani, alitazama nyuso za wasikilizaji Wake. Macho yao yaliyowaka kwa shauku na mwonekano wao wenye uhai vilimwonyesha mara moja wakati mtu alipokubaliana na Kweli. Vivyo hivyo, walimu wa watu leo wanapaswa kujifunza kuchunguza nyuso za wasikilizaji wao. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 158. {VSS 99.2}

Watu Wenye Tumaini Katika Ufalme Wake—Yesu alizitazama kwa dhati na umakini mkubwa nyuso za wasikilizaji Wake zilizokuwa zikibadilika. Nyuso zilizoonyesha shauku na furaha zilimletea kuridhika sana. Mishale ya Kweli ilipoingia ndani ya nafsi, ikavunja vizuizi vya ubinafsi, ikazalisha toba, na hatimaye ikaleta shukrani, Mwokozi alifurahi. Alipotazama umati wa wasikilizaji na kutambua miongoni mwao nyuso alizokuwa ameziona hapo awali, uso Wake uliangaza kwa furaha. Aliwaona kuwa watu wenye tumaini kwa ajili ya ufalme Wake. Lakini Kweli iliposemwa waziwazi na kugusa sanamu fulani waliyokuwa wameishikilia moyoni, aliona mabadiliko katika nyuso zao—mwonekano wa baridi na wa kutoa ilani ya kukataa, uliodhihirisha kwamba nuru hiyo haikukaribishwa. Alipoona watu wakikataa ujumbe wa amani, moyo Wake ulichomwa kwa huzuni kuu kabisa. —*Tumaini la Vizazi Vyote*, uk. 255. {VSS 99.3}

Mwitikio wa Kila Mtu Binafsi—Hata ule umati mkubwa uliokuwa ukimfuata mara nyingi Kristo hakuuona kama kundi lisilo na tofauti la wanadamu. Alizungumza moja kwa moja na kila akili na kuufikia kila moyo. Alizitazama nyuso za wasikilizaji Wake, akaona nuru ya furaha ikiongezeka katika nyuso zao na mtazamo wao wa haraka wenye kuitikia, uliodhihirisha kwamba Kweli ilikuwa

Nhandi Masunga na Grace Momadi Masaka-Jersey 2026 July

imefikia nafsi zao. Ndani ya moyo Wake kulikuwa na mwitikio wa furaha yenye huruma kwao. —*Elimu*, uk. 231. **{VSS 100.1}**

SURA YA 20—KUZOEWA MAHITAJI YA WASIKILIZAJI WAKE

Kweli Kadiri Watu Walivyoweza Kustahimili—Kristo alivuta mioyo ya wasikilizaji Wake Kwake kwa kudhihirisha upendo Wake, kisha, hatua kwa hatua, kadiri walivyoweza kustahimili, aliwafunulia Kweli kuu za ufalme Wake. Vivyo hivyo, nasi tunapaswa kujifunza kuoanisha kazi zetu na hali ya watu, tukikutana nao pale walipo. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 57. {VSS 101.1}

Ujumbe Anuwai/Mbalimbali kwa Wasikilizaji Tofauti—Ujumbe wa Yesu wa rehema uliwasilishwa kwa namna mbalimbali kulingana na hali ya wasikilizaji Wake. Alijua *“jinsi ya kumtegemeza kwa maneno yeye aliyechoka” (Isaya 50:4)*; kwa maana neema ilimiminwa midomoni Mwake ili aweze kuwafikishia watu hazina za Kweli kwa namna yenye mvuto mkubwa zaidi. Alikuwa na busara ya kukabiliana na akili zilizokuwa na chuki, na aliweza kuwashangaza kwa kutumia mifano iliyovuta usikivu wao. Kupitia uwezo wa mawazo, aliufikia moyo wa mwanadamu. —*Tumaini la Vizazi Vyote*, uk. 254. {VSS 101.2}

Lugha ya Maisha ya Kawaida—Jifunzeni kutoka kwa Yesu. Alikuwa Mwalimu mkuu kuliko wote ambao ulimwengu umewahi kuwajua; hata hivyo, alizungumza kwa lugha ya maisha ya kawaida na alikidhi mahitaji ya watu wote. Alibadilisha mafundisho Yake kulingana na nyakati na mahali mbalimbali, akiwafikia matajiri na maskini, wenye elimu na wasio na elimu. Sikuzote alikazia mada kuu na tukufu zinazoweza kuvuta fikira za wanadamu, na aliziwasilisha kwa namna fulani na kwa kutumia mifano ambayo hata akili dhaifu zaidi zingeweza kuelewa maana yake, huku akili zenye uwezo mkubwa zaidi zikivutiwa na kufundishwa. —*The Review and Herald*, Julai 22, 1884. {VSS 101.3}

Kuwafikia Watu wa Makundi Yote—Kristo alikidhi mahitaji ya kila kundi la watu kupitia mada na namna ya mafundisho Yake. Alikula na kulala pamoja na matajiri na maskini, na akajifanya kufahamu shauku, masilahi pamoja na shughuli zao ili apate njia ya kuifikia mioyo yao. Watu wenye elimu na wenye akili nyingi walifurahia na kuvutiwa na mafundisho Yake; lakini wakati huohuo, mafundisho hayo yalikuwa wazi na rahisi kiasi kwamba hata watu wa hali ya chini zaidi waliweza kuyaelewa. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 3, uk. 214. {VSS 102.1}

Mafundisho Yanayolingana na Mahitaji—Heshima aliyoonyeshwa Kristo katika karamu alizohudhuria ilikuwa tofauti sana na namna Waandishi na Mafarisayo walivyotendewa, jambo lililowafanya wawe na wivu. Kristo alitoa mafundisho yaliyolingana na mahitaji ya wasikilizaji Wake. —*Manuscript 19, 1899.* {VSS 102.2}

Si kwa Matendo ya Ghafla Wala Kanuni Zilizowekwa Bila Kubadilika—Yesu alipata njia ya kufikia akili za watu kupitia njia ya mahusiano yao ya kawaida na mambo waliyoyazoea zaidi. Aliingilia kwa kiasi kidogo iwezekanavyo mtiririko wao wa kawaida wa mawazo kwa matendo ya ghafla au kwa kanuni zilizowekwa bila kuzingatia hali zao. Aliwaheshimu wanadamu kwa kuwaamini, na hivyo aliwaweka katika nafasi ya kuwajibika kwa heshima. Aliwasilisha Kweli za zamani katika mwanga mpya na wa thamani zaidi. Kweli ilitoka midomoni Mwake ikiwa nzuri katika urahisi wake, lakini ikiwa imevikwa heshima na nguvu. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 140. {VSS 102.3}

Njia Mbalimbali za Kuvuta Usikivu—Kutokana na mbinu za Kristo za kufanya kazi tunaweza kujifunza masomo mengi yenye thamani. Hakutumia njia moja pekee; bali kwa namna mbalimbali alitafuta kuvuta usikivu wa makutano, na baada ya kufanikisha hilo, aliwatangazia Kweli za injili. —*Mashauri kwa Afya*, uk. 387. {VSS 103.1}

SURA YA 21—MIFANO, ISHARA, NA TAMATHALI ZA USEMI

Mifano Iliyochaguliwa Vizuri—Yesu alikuwa Mwalimu mkuu kuliko wote ambao ulimwengu umewahi kuwajua. Aliwasilisha Kweli kwa kauli zilizo wazi na zenye nguvu, na mifano aliyotumia ilikuwa ya kiwango cha juu kabisa na yenye usafi mkubwa. Hakuwahi kuchanganya mifano isiyo na thamani wala tamathali zisizofaa katika mafundisho Yake ya Kiungu; wala hakutafuta kuridhisha udadisi wa watu au kuwafurahisha wale waliomsikiliza kwa kusudi la kuburudishwa tu. Hakushusha Kweli takatifu hadi kwenye kiwango cha mambo ya kawaida yasiyo na heshima; na mifano ya kuchekesha au ya kutumbuiza ambayo baadhi ya wahubiri wa Injili hutumia haikuwahi kutoka katika midomo Yake ya Kiungu. Kristo hakutumia mifano iliyokusudiwa kuleta burudani au kuchochea kicheko. —*The Review and Herald*, Agosti 6, 1895. {VSSsw 104.1}

Si kwa Mifano ya Kuchekesha kwa Kusudi la Kuvuta Usikivu—Katika mafundisho ya Mwalimu wa Kiungu, hakukuwa na mfano wowote ambao ungeacha hata kivuli kidogo kwenye vibao vya moyo wa mwanadamu. Maneno Yake yalikuwa na usafi wa hali ya juu na yalikuwa yamejaa heshima. Hakuwahi kushuka hadi kutumia maneno ya kuchekesha kwa kusudi la kuvutia umati wa watu. —*The Review and Herald*, Agosti 6, 1895. {VSSsw 104.2}

Mifano Kutokana na Mambo ya Kawaida—Yesu alieleza utukufu wa ufalme wa Mungu kwa kutumia uzoefu na matukio ya maisha ya duniani. Kwa upendo wenye huruma na upole, aliwatia moyo, aliwafariji, na kuwafundisha wote waliomsikiliza; kwa maana neema ilimiminwa midomoni Mwake ili aweze kuwafikishia watu hazina za Kweli kwa namna yenye mvuto mkubwa zaidi. —*Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi*, uk. 240. {VSSsw 104.3}

Mafundisho ya Kiroho Kutokana na Asili—Mwalimu Mkuu aliwaunganisha wasikilizaji Wake na asili, ili waweze kusikiliza sauti inayozungumza kupitia vitu vyote vilivyumbwa. Mioyo yao ilipokuwa laini na akili zao zikiwa tayari kupokea mafundisho, aliwasaidia kutambua na kufasiri mafundisho ya kiroho yaliyokuwa yamefunuliwa kupitia mandhari waliyoyaona kwa macho yao. Mifano ambayo alipenda kutumia kufundishia Kweli inaonyesha jinsi moyo Wake ulivyokuwa wazi kwa mvuto wa asili, na jinsi alivyofurahia kupata mafundisho ya kiroho kutoka katika mazingira ya maisha ya kila siku. {VSSw 105.1}

Ndege wa angani, maua ya kondeni, mpanzi na mbegu, mchungaji na kondoo—kwa vitu hivi Kristo alifafanua Kweli za milele. Pia alitoa mifano kutokana na matukio ya maisha na mambo halisi ya uzoefu yaliyokuwa yakijulikana kwa wasikilizaji Wake, kama vile chachu, hazina iliyofichwa, lulu ya thamani, wavu wa kuvulia samaki, sarafu iliyopotea, mwana mpotevu, na nyumba iliyojengwa juu ya mwamba pamoja na ile iliyojengwa juu ya mchanga. Katika mafundisho Yake kulikuwa na jambo la kuvutia kila akili na kugusa kila moyo. —*Elimu*, uk. 102. {VSSw 105.2}

Maeneo Yaliyochaguliwa kwa Uangalifu kwa Ajili ya Mafundisho—Mkombozi wa ulimwengu alitafuta kufanya mafundisho Yake yawe wazi na rahisi, ili kila mtu aweze kuyaelewa. Mara nyingi alichagua maeneo ya wazi kwa ajili ya kutoa mafundisho Yake. Hakukuwa na kuta ambazo zingeweza kuzuia umati mkubwa uliomfuata; lakini kulikuwa na sababu maalumu iliyomfanya aende kwenye mapori na kando ya bahari ili kufundisha. Katika maeneo hayo angeweza kuona mandhari iliyokuwa mbele Yake kwa upana, na kutumia vitu pamoja na matukio ambayo watu wa hali ya kawaida walivifahamu ili kufafanua Kweli muhimu alizokuwa akiwafunulia. {VSSw 105.3}

Pamoja na mafundisho Yake, aliunganisha kazi za Mungu katika asili. Aliwaelekeza wasikilizaji Wake kwenye ndege waliokuwa wakiimba nyimbo zao bila hofu wala wasiwasi; maua ya kondeni yaliyong'aa kwa uzuri wake; yungiyungi lililolala katika usafi wake juu ya uso wa ziwa; miti mirefu; mashamba yaliyolimwa; nafaka zilizokuwa zikipeperushwa na upepo; udongo usiozaa; mti usiozaa matunda; vilima vya milele; vijito vinavyobubujika; na jua lililokuwa likitua, likipaka rangi na kuyafanya mawingu ya mbingu yang'ae. Vitu hivi vyote alivitumia kuwajengea

wasikilizaji Wake uelewa wa Kweli za Mungu. Aliunganisha kazi za vidole vya Mungu katika mbingu na duniani pamoja na Maneno ya uzima aliyotaka kuyaweka ndani ya akili zao, ili kila walipotazama kazi za ajabu za Mungu katika asili, mafundisho Yake yawe mapya katika kumbukumbu zao. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 2, uk. 579, 580. {VSSsw 106.1}

Kutoka Katika Kinachojulikana Kwenda Katika Kisichojulikana—Katika mafundisho Yake, Kristo alichota mifano kutoka katika hazina kubwa ya mahusiano ya kifamilia na upendo wa nyumbani, pamoja na ulimwengu wa asili. Alifafanua mambo yasiyojulikana kwa kutumia yale yaliyokuwa yanajulikana; na Kweli takatifu na za Kiungu alizifafanua kwa kutumia mambo ya kawaida ya duniani ambayo watu walikuwa wameyazoea zaidi. Hivyo ndivyo vitu hivyo vilivyoweza kuzungumza na mioyo yao na kuacha alama ya mguso wa kina katika akili zao. {VSSsw 106.2}

Maneno ya Kristo yaliweka mafundisho ya asili katika mtazamo mpya na kuyafanya yawe kama ufunuo mpya. Aliweza kuzungumza kuhusu vitu ambavyo mikono Yake mwenyewe ilikuwa imeviumba, kwa sababu vilikuwa na sifa na tabia zilizokuwa za kipekee. Katika asili, kama vile katika kurasa takatifu za Maandiko ya Agano la Kale, kweli za kimungu na zenye uzito mkuu zinafunuliwa; na katika mafundisho Yake, Yesu aliziweka wazi mbele ya watu, akizifungamanisha na uzuri wa vitu vya asili. —*Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi*, uk. 178, 179. {VSSsw 107.1}

Tamathali na Ishara—Kwa kusudi Lake lenye hekima, Bwana hufunika Kweli za kiroho kwa kutumia mifano na ishara. Kupitia matumizi ya tamathali za usemi, mara nyingi aliwapa washitaki na maadui Zake makaripio yaliyo wazi na yenye nguvu, lakini hawakuweza kupata katika Maneno Yake jambo la kumshtaki. Katika mifano na ulinganisho, alipata njia bora zaidi ya kuwasilisha Kweli za Mungu. Kwa lugha rahisi, akitumia vielelezo vilivyotokana na ulimwengu wa asili, aliwafunulia wasikilizaji Wake Kweli za kiroho na kueleza kanuni za thamani ambazo zingepita katika akili zao bila kuacha athari kubwa, kama asingeyaunganisha maneno Yake na matukio yenye kugusa ya maisha, uzoefu, au asili. Kwa njia hii aliwachochea

wasikilizaji Wake kuwa na shauku, akaamsha udadisi na maswali ndani yao; na baada ya kuhakikisha kwamba alikuwa amevuta usikivu wao kikamilifu, aliweka ndani yao ushuhuda wa Kweli kwa uthabiti. Kwa njia hii aliweza kuacha alama ya kudumu moyoni, kiasi kwamba baadaye walipotazama kitu kile alichokihusianisha na fundisho Lake, waliweza kukumbuka tena Maneno ya Mwalimu wa Kiungu/mbinguni. —*Misingi ya Elimu kwa Kila Mwanadamu*, uk. 236. {VSSsw 107.2}

SURA YA 22—KIELELEZO CHA MTENDAKAZI

Kristo Ni Mfano Wetu—Kile ambacho Kristo alikuwa duniani hapa, ndicho mtendakazi Mkristo anapaswa kujitahidi kuwa. Yeye ni mfano wetu, si katika usafi Wake usio na doa pekee, bali pia katika uvumilivu Wake, upole Wake, na mvuto wa tabia Yake inayowaleta watu karibu. Maisha Yake yalikuwa kielelezo cha adabu ya kweli. Sikuzote alikuwa na mtazamo wa fadhili na Neno la faraja kwa wahitaji na waliokandamizwa. Uwepo Wake ulileta hali safi zaidi ndani ya nyumba. Maisha Yake yalikuwa kama chachu iliyokuwa ikifanya kazi katikati ya jamii. Akiwa safi na asiye na unajisi, alitembea katikati ya watu wasiojali mambo ya kiroho, wakorofi, wenye jeuri, na wasio na adabu; katikati ya watoza ushuru wasio wa haki, Wasamaria wasio waadilifu, askari wa mataifa, wakulima wenye tabia ngumu, na makutano ya watu wa aina mbalimbali. Aliwatamkia wengine neno la huruma hapa, na wengine neno la faraja pale. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 121. {VSSsw 109.1}

Uwakilishi wa Mbinguni—Mwokozi wa ulimwengu anatamani kwamba watenda kazi wenzake wamwakilishe Yeye; na kadiri mtu anavyotembea karibu zaidi na Mungu, ndivyo mwenendo wake wa kusema, tabia yake, mkao wake, na ishara zake vitakavyokuwa visivyo na dosari zaidi. Tabia mbaya, na ukali havikuonekana katika mkao na mjongeo wake au ukosefu wa ustaarabu havikuwahi

kuonekana katika Kielelezo chetu, Kristo Yesu. Yeye alikuwa mwakilishi wa mbingu, na wafuasi Wake wanapaswa kufanana Naye. —*Shuhuda kwa Kanisa, juz. 4, uk. 405. {VSS 109.2}*

Mahubiri ya Mfano—Mahubiri ya Mlimani ni mfano wa namna tunavyopaswa kufundisha. Ni juhudi kubwa kiasi gani Kristo alizofanya ili kufanya mambo ya siri yasiendele kuwa siri, bali yawe Kweli zilizo wazi na rahisi! Katika mafundisho Yake hakuna jambo lisiloeleweka, lenye utata wala gumu kufahamu. **{VSS 110.1}**

“Akafunua kinywa chake, akawafundisha.” (Mathayo 5:2). Maneno Yake hayakutamkwa kwa sauti ya kunong’ona, wala usemi Wake haukuwa mkali au usiovutia. Alizungumza kwa uwazi na msisitizo, akiwa na nguvu, adhima na kushawishi. —*Shuhuda kwa Kanisa, juz. 7, uk. 269. {VSS 110.2}*

Mfano kwa Kila Mtendakazi—Katika kazi Yake ya huduma kwa wagonjwa na wenye mateso, Kristo anasimama mbele ya ulimwengu kama Mmishonari Mkuu wa Tiba kuliko wote waliowahi kujulikana, na kama kielelezo kwa kila mtendakazi Mkristo wa kimisionari. Alijua Neno sahihi la kusema kwa kila mtu aliyekuwa katika mateso, na hakusema tu yale yaliyoleta uponyaji wa mwili, bali pia yale yaliyoleta usadikisho wa nafsi na mwangaza wa kiroho. Aliwasaidia wale waliomtafuta, maarifa ya kuelewa hali yao wenyewe na kutambua hitaji kuu zaidi la nafsi. **{VSS 110.3}**

Mafundisho au Mahubiri ya Kristo yalikuwa maelezo ya kiroho ya huduma Yake kwa walioteseka. —*Huduma ya Tiba, uk. 194. {VSS 110.4}*

Si Kuhubiri Tu Kwa Maneno—Kristo Ndiye Mfano wa mhudumu wa injili. Maneno Yake yalifika moja kwa moja kwenye kiini cha jambo, yalilingana vizuri na kusudi na mazingira yaliyokuwapo, na mifano Yake ilikuwa wazi na yenye nguvu kiasi gani! Mtindo Wake ulitambulishwa kwa urahisi na uzito. Katika mafundisho yote ya Kristo hakuna jambo lolote linaloweza kumpa mhudumu sababu ya kutumia hadithi za kuchekesha madhabahuni. Mafundisho ya Kristo yanapaswa kujifunzwa kwa makini, na mada, namna, na muundo wa mahubiri vinapaswa kuigwa kutokana na Kielelezo cha Kiungu. Maonyesho ya ufasaha wa kusema, maneno ya kuvutia yasiyo na msingi, na mkao au ishara nzuri za mwili haviwezi kufanya mahubiri yawe bora. Kristo hakuhubiri kwa mtindo ambao wanadamu wengi hutumia leo. Kwa sauti

yenye bidii kubwa na uzito, aliwahakikishia watu Kweli kuhusu uzima ujao na njia ya wokovu. —*The Review and Herald*, Juni 23, 1891. {VSS 110.5}

SEHEMU YA 3—MITAZAMO YA KIKRISTO KATIKA USEMI

SURA YA 23—UFUNUO WA KRISTO

Mwokozi Wetu Kuwa Mada ya Mazungumzo

Msizungumzie sana uovu na dhambi zilizomo ulimwenguni, bali inueni mawazo yenu na mzungumzie Mwokozi wenu. Mnapoona uovu ukiwazunguka kila mahali, jambo hilo linapaswa kuwafanya mzidi kufurahi kwa sababu Yeye Ndiye Mwokozi wenu, nanyi ni watoto Wake. —*Akili, Tabia na Haiba*, juz. 2, uk. 582. {VSS 115.1}

Mada Kuu: Kristo Aliyesulubiwa

Kristo aliyesulubiwa—zungumzieni jambo hilo, ombeeni jambo hilo, na liimbeni jambo hilo; nalo litavunja na kuvuta mioyo ya watu. Misemo iliyowekwa kwa mtindo wa kawaida na rasmi, pamoja na uwasilishaji wa mada zinazolenga mabishano pekee, huleta manufaa machache sana. —*The Review and Herald*, Juni 2, 1903. {VSS 115.2}

Malisho Mabichi kwa Kondoo wa Zizi la Mungu—Sauti nyingi zinatetea kosa; kwa hiyo sauti yenu na itetee Kweli. Wasilisheni mada ambazo zitakuwa kama malisho mabichi kwa kondoo wa zizi la Mungu. Msiwaongoze wasikilizaji wenu katika maeneo makavu yasiyo na uzima, ambako watakuwa hawajakaribia chemchemi ya maji ya uzima zaidi ya walivyokuwa kabla ya kuwasikiliza. Iwasilisheni Kweli kama ilivyo ndani ya Yesu, mkifafanua wazi matakwa ya sheria na injili. Mwasilisheni Kristo, ambaye Ndiye Njia, Kweli, na Uzima, na elezeni nguvu Yake ya kuwaokoa wote wanaomjia. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 154. {VSSsw 115.3}

Neema ya Kristo na Wokovu—Ni jambo gani linalostahili zaidi kutawala na kusheheni mawazo ya mwanadamu kuliko mpango wa ukombozi? Hili ni jambo lisiloweza kumalizika kuchunguzwa. Upendo wa Yesu, wokovu unaotolewa kwa mwanadamu aliyeanguka kupitia upendo Wake usio na mwisho, utakatifu wa moyo, Kweli ya thamani iokoayo kwa ajili ya siku hizi za mwisho, na neema ya Kristo—haya ni masomo yanayoweza kuhuisha nafsi na kuwafanya walio safi moyoni wapate furaha ileile ambayo wanafunzi walipata Yesu alipokuja na kutembea pamoja nao walipokuwa wakisafiri kuelekea Emau. {VSSsw 116.1}

Yeye ambaye ameuwelekeza moyo wake kwa Kristo atafurahia ushirika huu mtakatifu na atapata nguvu ya Kiungu kupitia mazungumzo kama hayo. Lakini yule asiye na ladha kwa mazungumzo ya aina hii, na anayefurahia zaidi kuzungumza mambo ya kihisia na kufikirika yasiyo na maana, amekwenda mbali na Mungu na anazidi kupoteza hamu ya mambo mtakatifu, bora na yenye heshima. Mambo ya kimwili na ya kidunia hutafsiriwa na mtu wa namna hiyo kana kwamba ni mambo ya mbinguni. —*Testimonies for the Church*, juz. 5, uk. 600. {VSSsw 116.2}

Mwakili wa Neema ya Kristo—Kwa nini wengi wanaodai kuwa watoto wa Mungu wanatumia uwezo waliokabidhiwa na Mungu kwa ajili ya mambo ya ubinafsi? Wao ni mawakili wa neema ya Kristo, na wanapaswa kumwinua Yesu mbele ya ulimwengu. Wanapaswa kumzungumzia Kristo, kwa maana sifa Zake zinapaswa kuwa midomoni mwao, kwa sababu Jua la Haki linawaangazia ndani ya mioyo yao. Kupitia wao Jina Lake takatifu linapaswa kuinuliwa/kutukuzwa duniani. —*The Review and Herald*, Agosti 16, 1898. {VSSsw 116.3}

Njia Bora Zaidi ya Mawasiliano—Msizungumzie sana kuhusu nafsi zenu, kwa maana hilo halitamwimarisha mtu yeyote. Msijifanye kuwa kitovu cha mambo,

mkifikiri kwamba lazima daima mjihudumie wenyewe na kuwafanya wengine wawajali na kuwashugulikia. Ondoeni mawazo yenu kutoka kwenu wenyewe na kuyaelekeza katika njia iliyo bora zaidi. Mzungumzieni Yesu, na muuache ubinafsi; nafsi yenu izamishwe ndani ya Kristo. Hebu maneno ya moyo wenu na yawe: ***“Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu.” (Wagalatia 2:20).*** Yesu atakuwa msaada wenu wa sasa katika kila wakati wa uhitaji. Yeye Hatawaacha mpambane peke yenu dhidi ya nguvu za giza. La hashah!; amemweka msaada juu ya Yule aliye na uwezo wa kuokoa kabisa. —***Shuhuda kwa Kanisa, juz. 2, uk. 320, 321. {VSSw 116.4}***

Lugha ya Kanaani—Tunapaswa kuwa mashahidi wa Kristo, na tutakuwa hivyo tunapokua kila siku hadi kufikia kimo kamili cha wanaume na wanawake ndani ya Kristo. Ni upendeleo na fursa yetu kufanana Naye zaidi na zaidi kila siku. Ndipo tutakapopata uwezo wa kueleza upendo wetu Kwake kwa maneno yaliyo bora zaidi na safi zaidi; mawazo yetu yatapanuka na kuongezeka kwa kina, na maamuzi/hukumu yetu itakuwa thabiti na yenye kuaminika zaidi, huku ushuhuda wetu ukiwa na uhai na uhakika mkubwa zaidi. Hatupaswi kuzoea lugha ya kidunia na kufahamiana sana na mazungumzo ya wanadamu kiasi kwamba lugha ya Kanaani iwe jambo geni na lisiloeleweka kwetu. —***Wana na Binti za Mungu, uk. 72. {VSS 117.1}***

Mfumo wa Mashine Unaosimamiwa na Mkono Mkuu—Kila moyo ulioguswa na miale angavu ya Jua la Haki utaonyesha kazi ya Roho wa Mungu katika sauti, akili, na tabia. Mfumo huo utafanya kazi kana kwamba umetiwa mafuta na kuongozwa na mkono wa ustadi mkuu. Kutakuwa na msugurano mdogo zaidi wakati roho ya mtendakazi inapopokea mafuta kutoka katika yale matawi mawili ya mzeituni. Mvuto mtakatifu utawasilishwa kwa wengine kupitia maneno ya fadhili, upole, upendo, na kutia moyo Zek 4. —***Shuhuda kwa Kanisa, juz. 7, uk. 195, 196. {VSS 117.2}***

Mbegu za Upendo na Fadhili—Baadhi ya watu huonekana kutoka katika ushirika wao wa kila siku na Mungu wakiwa wamevikwa unyenyekevu wa Kristo. Maneno yao hayafanani na mvua ya mawe yenye kuharibu na kupondaponda kila kitu mbele yake; bali hutoka midomoni mwao kwa utamu na upole. Hutawanya mbegu za upendo na fadhili katika njia yao yote bila hata kutambua, kwa sababu

Kristo anaishi ndani ya mioyo yao. Ushawishi wao huhisiwa zaidi kuliko unavyoonekana. **{VSS 118.1}**

Maneno ya fadhili, upole, kujali na huruma nyororo yatatoka katika mioyo na midomo iliyotakaswa. —*Wana na Binti za Mungu, uk. 180. {VSS 118.2}*

Maneno Yenye Uzito na Busara—Wale walio na Roho huyo [wa Kristo] ni watenda kazi wenza wa dhati na bidii pamoja na Mungu; akili za mbinguni hushirikiana nao, nao huendelea wakiwa wamebeba roho ya ujumbe wanaoutangaza. Husema maneno yenye uzito na busara, na kutoka katika hazina ya mioyo yao hutoa mambo safi na matakatifu, kwa mfano wa Kristo. —*Watendakazi wa Injili, uk. 288. {VSS 118.3}*

Usemi Rahisi, Wazi, na wa Kweli—Wale ambao wamejifunza kutoka kwa Kristo “*hawatahirikiana na matendo yasiyozaa ya giza.*” (*Waefeso 5:11*). Katika usemi wao, kama vile katika maisha yao, watakuwa wanyenyekevu, sahili, wazi, na wa kweli, kwa maana wanajiandaa kwa ushirika wa watakatifu wale ambao vinywani mwao hamna hila. —*Manabii na Wafalme, uk. 252. {VSS 118.4}*

Upole, Kujisalimisha—Wale wanaokaa ndani ya Yesu watakuwa na furaha, uchangamfu, na shangwe katika Mungu; upole, utulivu na kujisalimisha vitaonekana katika sauti yao, heshima kwa mambo ya kiroho na ya milele itaonyeshwa katika matendo yao, na muziki—muziki wa furaha—utasikika kutoka midomoni mwao, kwa maana hutiririka kutoka katika kiti cha enzi cha Mungu. —*Shuhuda kwa Kanisa, juz. 4, uk. 626. {VSS 119.1}*

SURA YA 24—UNYENYEKEVU, UKWELI, STAHA, UUNGWANA NA BUSARA

Lugha ya Unyenyekevu na Iliyoinuliwa—Usemi wetu unapaswa kuwa wa staha, uungwana, unyenyekevu na wenye heshima ya juu. Roho ambayo tumeilea ndani yetu imeacha alama yake katika sura zetu. Kristo anapoketi katika kiti cha enzi cha hekalu la nafsi, ataondoa mwonekano ule wa huzuni, manung'uniko, na kutokuwa na furaha; na jeshi la mashahidi litakapomtazama mtu anayeakisi sura ya Kristo, litatambua kwamba amezungukwa na mazingira yenye kupendeza. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 4, uk. 348. {VSS 120.1}

Mazungumzo Yanayoinua na Bora—Mazungumzo yetu yanapaswa kuwa ya kiwango cha juu na yenye kuinua, kiasi kwamba baadaye yaweze kukumbukwa kwa hisia za furaha kuu. —*Counsels on Diet and Foods*, uk. 88. {VSS 120.2}

Wema wa Mungu—Mazungumzo ya kila mmoja wetu yanapaswa kuwa ya kiwango cha juu, yenye kusudi la kuyaelekeza mawazo ya wengine katika njia iliyo sahihi. Kutajwa kwa uchache kwa wema wa Mungu na upendo Wake kunaonyesha wazi kutokuwa na shukrani, na kwamba Kristo hajatawazwa moyoni. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 4, uk. 456. {VSS 120.3}

Mvuto Safi wa Kweli—Mvuto safi wa kweli utamwinua mtu mzima. Katika shughuli zake za kibiashara na mahusiano yake na wanadamu wenzake, atakuwa na hofu ya Mungu mbele yake, atampenda jirani yake kama nafsi yake mwenyewe, na atawatendea wengine jinsi anavyotamani kutendewa. Mazungumzo yake yatakuwa ya kweli, safi, na yenye tabia ya kuinua kiasi kwamba wasioamini hawataweza kuyatumia vibaya wala kusema jambo baya juu yake na hivyo kutotenda haki; wala hawatachukizwa na mwenendo wake usio na staha/adabu au usemi wake usiofaa. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 1, uk. 415, 416. {VSS 120.4}

Maneno Yenye Nguvu za Kiroho—Hata alipokuwa ameketi mezani wakati wa chakula, Kristo alifundisha kweli zilizowaletea faraja na ujasiri mioyoni mwa wasikilizaji Wake. Upendo Wake unapokaa ndani ya nafsi kama kanuni hai, kutoka katika hazina ya moyo yatatoka maneno yanayofaa kwa wakati husika; si maneno mepesi na yasiyo na maana, bali maneno ya kuinua na yenye nguvu za kiroho. —*Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi*, uk. 554. {VSS 121.1}

Ushuhuda Chanya—Ni wajibu wetu kuwa na wivu na waangalifu sana kuhusu utukufu wa Mungu na tusilete ushuhuda mbaya juu Yake hata kwa huzuni ya uso wetu au kwa maneno yasiyofikiriwa vizuri, kana kwamba matakwa ya Mungu ni kizuizi kwa uhuru wetu. Mtu mzima amepewa nafasi ya kutoa ushuhuda ulio wazi katika kila jambo—katika sura yake, tabia yake, haiba yake, maneno yake, na mwenendo wake—kwamba kumtumikia Bwana ni jambo jema. Kwa maisha yao wanatangaza: *“Sheria ya Bwana ni kamilifu, huiburudisha nafsi.” Zaburi 19:7* Maneno yenu na yawe yenye kusimama upande wa Bwana. —*Manuscript 70, 1897.* **{VSS 121.2}**

Maneno Machache, Maombi Mengi—Tuwe waangalifu kuhusu maneno yetu. Loo, kuna usemi mwingi sana ambao haumletei Mungu utukufu. Je, haingekuwa bora zaidi kama tungenema machache na kuomba zaidi? —*Manuscript 39, 1908.* **{VSS 121.3}**

Maneno Yaliyochaguliwa Vizuri—Tunapokuwa katika kazi, hebu tulinde mawazo yetu, tuyatulize kwa Mungu, tuseme machache, na tutafakari zaidi. Tukumbuke: *“Kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu.”* Mathayo 12:36 Hebu maneno yetu na yawe yale yaliyochaguliwa kwa uangalifu; jambo hili litafunga mlango dhidi ya adui wa nafsi. —*Shuhuda kwa Kanisa, juz. 4, uk. 588.* **{VSS 122.1}**

Kristo Aseme Kupitia Kwetu—Tufanye agano na Mungu kwamba tutayalinda vizuri maneno yetu. *“Mtu asiyejikwaa katika kunena, huyo ni mtu mkamilifu, awezaye kuuzuia na mwili wake wote.” (Yakobo 3:2).* Tukumbuke kwamba maneno ya kulipiza kisasi hayamfanyi mtu ahisi kwamba ameshinda. Tumruhusu Kristo aseme kupitia kwetu. Tusipoteze baraka inayotokana na kuondoa mawazo mabaya mioyoni mwetu. —*Shuhuda kwa Kanisa, juz. 7, uk. 243.* **{VSS 122.2}**

SURA YA 25—AINA ZA USEMI HASI

Mbegu Zenye Thamani Zaidi—Hebu tuwe waangalifu kuhusu yale tunayosema, kwa maana mbegu inayotoka katika akili moja na kupandwa katika akili nyingine inapaswa kuwa mbegu yenye thamani kubwa zaidi, wala isiwe mbegu ya manung'uniko na malalamiko. —*Manuscript 18, 1895. {VSS 123.1}*

Maoni Yasiyo Sahihi—Huwezi kuwa mwangalifu kupita kiasi kuhusu maneno unayosema, kwa sababu maneno unayoyatamka yanaonyesha nguvu inayotawala akili na moyo wako. Kama Kristo anatawala moyoni mwako, maneno yako yatafunua usafi, uzuri, na harufu njema ya tabia iliyoubwa na kufinyangwa kulingana na mapenzi Yake. *{VSS 123.2}*

Bwana anataka maneno yetu yawe ya kiwango cha juu kabisa na kwamba ndimi zetu ziwe za Kweli sikuzote. Kila dalili ya udanganyifu ni kosa mbele Zake. Kila neno tunalolisema linahitaji kufikiriwa kwa uangalifu mkubwa, ili lisije likawapotosha wale walio dhaifu katika imani. Kutokana na nuru ambayo Mungu amenipa, najua kwamba kupitia maneno yako yasiyofikiriwa vizuri umeacha maoni yasiyo sahihi katika akili za baadhi ya watu huko Sydney; na itahitaji muda mwingi kurekebisha athari za maoni hayo. Mambo hayo uliyoyaeleza kwa maneno hayakuwa ya kweli, bali yalitokana na mawazo yako mwenyewe ya kufikirika. Usiendelea tena kutegemea hali ya kiroho isiyo ya kweli. —*Letter 69, 1896. {VSS 123.3}*

Urithi Wenye Thamani—Mungu anataka watu Wake, kwa maneno yao na mwenendo wao, wautangazie ulimwengu kwamba hakuna mvuto wa kidunia wala mali za dunia zilizo na thamani inayoweza kulinganishwa au kufidia, kupoteza urithi wa mbinguni. Wale ambao kwa kweli ni watoto wa nuru na wa mchana hawatakuwa watu wa majivuno wala wepesi katika mazungumzo yao, mavazi yao, au mwenendo wao; bali watakuwa wenye kiasi, wenye kutafakari, na wanaotumia daima mvuto wao kuwavuta watu kwa Mwokozi. *{VSS 124.1}*

Mungu anawaagiza wafuasi Wake wote kutoa ushuhuda hai kwa lugha iliyo wazi na isiyo na utata kupitia mwenendo wao, mavazi yao, na mazungumzo yao katika kila shughuli ya maisha; yaani, kwamba nguvu ya uchaji Mungu wa Kweli ni

yenye manufaa katika maisha haya na katika maisha yajayo, na kwamba hii pekee ndiyo inayoweza kuridhisha nafsi ya anayeipokea. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 4, uk. 580, 581. {VSS 124.2}

Maisha Safi na Usemi Safi—Hakuna neno lolote linalopaswa kusemwa bila kufikiriwa. Hakuna usemi mbaya, mazungumzo ya kipuuzi, manung'uniko ya kukasirika, wala mapendekezo machafu yatakayotoka katika midomo ya mtu anayemfuata Kristo. Mtume Paulo, akiandika kwa uongozi wa Roho Mtakatifu, anasema: Hebu *“Neno lolote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu.”* (Waefeso 4:29). Usemi mchafu haumaanishi tu maneno yaliyo waziwazi machafu; bali unahusisha kila kauli iliyo kinyume na kanuni takatifu na dini safi isiyo na unajisi. Pia unajumuisha dokezo chafu na kauli za kificho zinazoashiria uovu. Ikiwa mambo haya hayatapingwa mara moja, yanaweza kuongoza katika dhambi kubwa. {VSS 124.3}

Juu ya kila familia na kila Mkristo binafsi kuna wajibu wa kuzuia njia ya usemi mchafu. Tunapokuwa katika kundi la watu wanaojihusisha na mazungumzo ya kipumbavu, ni wajibu wetu kubadilisha mada ya mazungumzo ikiwa inawezekana. Kwa msaada wa neema ya Mungu, tunapaswa kwa utulivu kusema maneno machache au kuanzisha mada itakayolielekeza mazungumzo katika njia yenye manufaa. —*Mifano ya Masihi*, uk. 337. {VSS 124.4}

Kuheshimu Sheria na Utaratibu—Hatutakiwi kukaidi mamlaka zilizowekwa. Maneno yetu, yawe yamesemwa au yameandikwa, yanapaswa kufikiriwa kwa uangalifu, ili tusijiweke katika hali ya kuonekana kuwa tunapinga sheria na utaratibu. Hatupaswi kusema wala kufanya jambo lolote litakalofunga njia yetu bila sababu. Tunapaswa kusonga mbele katika Jina la Kristo, tukitetea Kweli tulizokabidhiwa. —*Matendo ya Mitume*, uk. 69. {VSS 125.1}

Mambo Yaliyo Sahihi—Tafadhali someni sura ya hamsini na nane ya Isaya, kwa maana sura hii imetolewa nuru kubwa. Ombi la dhati linalotoka katika moyo mnyenyekevu na uliovunjika litasikilizwa na kujibiwa. *“Amebarikiwa mtu yule anayemtegemea Bwana, Ambaye Bwana ni tumaini lake. Maana atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, Uenezao mizizi yake karibu na mto; Hautaona hofu wakati wa hari ujapo, Bali jani lake litakuwa bichi; Wala hautahangaika mwaka wa uchache wa mvua, Wala hautaacha kuzaa matunda.”* Yeremia 17:7-8 Hili ndilo tunaloweza kutarajia ikiwa tutashirikiana na Mungu kwa kujitoa wakfu

wenyewe—nafsi, mwili, na roho—chini ya ulinzi Wake. Ndipo hakutasikika tukisema mazungumzo ya kipuuzi wala usemi wa uovu; bali ulimi utasema mambo yaliyo sahihi. —*The Review and Herald*, Januari 25, 1898. {VSS 125.2}

Maneno ya Kusengenya—Kazi ya Adui

Tunapaswa kuwa waangalifu sana ili maneno yetu na matendo yetu vipatane na Kweli takatifu ambazo Mungu ametukabidhi. Tunapokuwa pamoja, tunapaswa kulinda sana maneno yetu; mazungumzo yetu yanapaswa kuwa ya namna ambayo hayatatusababisha kujuta baadaye. Ikiwa neno lolote litasemwa ambalo linaharibu tabia ya rafiki au ndugu, kamwe tusihamasishe au kutia moyo usemi huo mbaya, kwa maana huo ni kazi ya adui. Badala yake, tumkumbushe msemaji kwamba Neno la Mungu linakataza mazungumzo ya aina hiyo. —*The Review and Herald*, Februari 25, 1904. {VSS 126.1}

Madhara ya Mazungumzo Yasiyofaa—Dhambi ya kusema maneno ya kipuuzi imeenea miongoni mwa wale wanaodai kuamini Kweli zenye uzito mkubwa zaidi ambazo zimewahi kutolewa kwa ulimwengu. Kwa sababu ya mazungumzo haya ya kawaida, mepesi, na yasiyo na maana, Roho wa Bwana huhuzunishwa na kuondoka. Mazungumzo yasiyofaa ndiyo chanzo cha ukosefu wa imani na nguvu unaoonekana miongoni mwa watu wa Mungu. —*Letter 47*, 1897. {VSS 126.2}

Hakuna Uzembe, Michezo Wala Mambo Yasiyo na Maana—Kila aina ya uzembe, mazungumzo rahisi, utani, na masihara hudhoofisha nafsi na kuutenga moyo na roho ya maombi. Kama mtume Paulo, wafuasi wa Kweli wa Kristo daima hubeba ndani ya miili yao kufa kwa Bwana Yesu; hawawezi kuyaweka mawazoni mateso ya Kristo kwa ajili yao na bado wakaendelea kuwa watu wepesi na wasiojali mambo ya kiroho. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 233, toleo la 1892. {VSS 126.3}

Mazungumzo ya Kipumbavu—Ni wachache sana wanaotambua kwamba kwa mawazo na hisia zao za ubinafsi, pamoja na mazungumzo yao ya kipuuzi na yasiyo na maana, wanaweza kumfukuza Roho wa Mungu. Ikiwa neema ya Kristo ingepandwa ndani ya mioyo yao na kuotesha mizizi yake ndani ya udongo mzuri, wangezaa matunda ya tabia tofauti kabisa. Ni nguvu ya Mungu ibadilishayo pekee inayoweza kuweka kanuni safi ndani ya moyo, kiasi kwamba yule mwovu asipate jambo la kushambulia. Usafi katika usemi na staha/adabu ya kweli ya Kikristo na

Kielelezo chetu? Sikilizeni zaidi—je, Yesu anatajwa? Je, Kweli ndiyo mada kuu ya mazungumzo? Je, wanaozungumza wanajisifu katika msalaba wa Kristo? — ***Shuhuda kwa Kanisa, juz. 1, uk. 505. {VSS 128.2}***

Usemi Uliotiwa Chumvi—Mawazo yetu huzaa maneno yetu, na maneno yetu nayo huathiri mawazo yetu tena. Ikiwa mtu atajenga mazoea ya kutumia maneno matakatiifu kwa heshima, atazoea kuwa mwangalifu katika usemi wake, akijua kwamba kuna Shahidi anayesikia kila neno linalotamkwa. Hisia zinapochochewa na maneno yanapotiliwa chumvi, namna ya kuzungumza huwa ya kupindukia. Hali hiyo humwathiri mtu mwenyewe, nayo huendelea kuathiri wengine pia. **{VSS 128.3}**

Neno la Mungu linasema: ***“Kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa.” (Mathayo 12:37).*** Ikiwa maneno yetu yana athari juu yetu wenyewe, yana nguvu kubwa zaidi ya kuwaathiri wengine. Madhara makubwa husababishwa na maneno yanayosemwa bila uangalifu na kwa kutia chumvi. Mungu pekee Ndiye anayejua na kupima matokeo ya usemi kizembe, usio wa tahadhari na uliotiwa chumvi. Kuna kuapa kwingi kunakofanywa kwa nia ya moyoni. —***That I May Know Him, uk. 137. {VSS 128.4}***

Misemo Isiyo na Maana na Maneno ya Kujazia—Neno la Mungu pia linakataza matumizi ya misemo isiyo na maana na maneno ya kujazia yanayokaribia lugha ya kukufuru. Linakataza pia pongezi za udanganyifu, kukwepa ukweli, kutia chumvi, na kupotosha mambo katika biashara, mambo ambayo yameenea katika jamii na katika ulimwengu wa kibiashara. ***“Bali maneno yenu yawe: Ndiyo, ndiyo; siyo, siyo; kwa kuwa yanayozidi hayo yatoka kwa yule mwovu.” (Mathayo 5:37). {VSS 129.1}***

“Kama mtu mwenye wazimu atupaye mienge, Na mishale, na mauti; Ndivyo alivyo amdanganyaye mwenzake, Na kusema, Je! Sikufanya mzaha tu?” (Mithali 26:18, 19). {VSS 129.2}

Kinachohusiana kwa karibu na kusengenya ni dokezo la kificho, kauli ya hila, au ishara ya ujanja ambayo watu wenye mioyo michafu hutumia kuingiza uovu ambao hawathubutu kuusema waziwazi. Vijana wanapaswa kufundishwa kuepuka

kila namna ya mazoea haya kama wanavyoepuka ukoma. —*Education*, uk. 236. {VSS 129.3}

Kiapo cha Kisheria—Niliona kwamba Maneno ya Bwana wetu: “*Msiape kabisa*” hayahusiani na kiapo kinachotolewa mahakamani. “*Bali maneno yenu yawe: Ndiyo, ndiyo; siyo, siyo; kwa maana yanayozidi hayo yatoka kwa yule mwovu.*” Haya yanahusu mazungumzo ya kawaida. Baadhi ya watu hutia chumvi katika usemi wao. Wengine huapa kwa maisha yao wenyewe; wengine huapa kwa vichwa vyao, wakisema: “Kwa hakika *kama niishivyo*,” au “Kwa hakika kama *nilivyo na kichwa*.” Wengine huita mbingu na dunia kuwa mashahidi kuthibitisha kwamba jambo fulani ni kweli. Wengine hutoa kiapo cha kutamani kwamba Mungu awaondoe duniani ikiwa wanachosema si kweli. Ni aina hii ya kuapa katika mazungumzo ya kawaida ambayo Yesu aliwaonya wanafunzi wake dhidi yake. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 1, uk. 201. {VSS 129.4}

SURA YA 26—UPENDO NA FADHILI

Maneno ya Fadhili na Faraja—Wakati roho maskini, zilizojeruhiwa na kuumizwa zinapokuja kwako zikitafuta maneno ya tumaini, unapaswa kuwaambia

maneno ya Kristo. Je, utakataa kuwapa maneno mazuri, yenye adabu na fadhili? Wale wanaosema kama Kristo alivyosema kamwe hawatapanda maneno machungu kama mishale yenye ncha katika nafsi iliyojeruhiwa. “Bwana alisikiliza na akasikia.” Je, utakumbuka kwamba Bwana husikia maneno tunayosema na anajua roho inayochochea matendo yetu? Je, si jambo linalolingana na tabia ya Kristo kusema maneno ya fadhili na ya faraja, hata kama ndani yako unahisi kutaka kufanya kinyume chake? —*The Review and Herald*, Mei 26, 1896. {VSS 131.1}

Sheria ya Fadhili Midomoni Mwetu—Fanyeni kazi bila ubinafsi, kwa upendo na uvumilivu, kwa ajili ya wote mnaokutana nao. Msionyeshe kukosa subira. Msitamke hata neno moja lisilo la fadhili. Upendo wa Kristo na uwe mioyoni mwenu, na sheria ya fadhili iwe midomoni mwenu. —*Huduma ya Ustawi*, uk. 76. {VSS 131.2}

Kufikiria Fadhili kwa Makini—Kila nafsi tunayokutana nayo imenunuliwa kwa damu ya Kristo, hivyo maneno ya fadhili na matendo ya kujali yanapaswa kutolewa kwa wale wanaokuja miongoni mwetu. Vijana wanahitaji msaada unaotokana na maneno na matendo ya fadhili. —*Manuscript 33, 1911*. {VSS 131.3}

Kweli Katika Upendo—Kama vile umande na mvua nyepesi zinavyonyesha juu ya mimea inayonyauka, vivyo hivyo maneno yetu yanapaswa kushuka kwa upole tunapotafuta kuwatoa watu katika makosa. Mpango wa Mungu ni kuufikia moyo kwanza. Tunapaswa kusema Kweli katika upendo, tukimtumaini Yeye ili alipe nguvu neno hilo la kubadilisha maisha. Roho Mtakatifu atalitia moyoni neno lililosemwa kwa upendo. —*Huduma ya Upanyaji*, uk. 157. {VSS 132.1}

Ukosoaji Kidogo, Mvuto Mkubwa wa Wema—Katika kazi ya kuwasaidia wengine, tunaweza kupata ushindi wa thamani sana. Tunapaswa kujitoa kwa bidii isiyochoka, uaminifu wa dhiti, kujikana nafsi, na uvumilivu katika kazi ya kuwasaidia wale wanaohitaji kukua. Maneno ya fadhili na ya kutia moyo yatafanya maajabu makubwa. Wapo wengi ambao, ikiwa wataonyeshwa juhudi za kudumu na zenye furaha bila kulaumiwa wala kukemewa, wataonyesha uwezo wa kubadilika na kuwa bora. Kadiri tunavyowakosoa wengine kidogo, ndivyo ushawishi wetu wa kuwasaidia utakavyokuwa mkubwa zaidi. Kwa wengi, maonyo mengi ya mara kwa mara yanaweza kuleta madhara kuliko manufaa. Fadhili ya Kristo na ionyeshwe kwa wote. —*Huduma ya Tiba*, uk. 208, 209. {VSS 132.2}

Tiba ya Ugonjwa na Huzuni—Bwana Yesu anatamani tuwe na uso wenye kupendeza na kusema maneno ya fadhili na huruma. Hata tunapokuwa wagonjwa au tunapojisikia vibaya, si lazima kuwaeleza wengine hali yetu kila mara. Tukizungumza juu ya wema wa Bwana, jambo hilo litakuwa tiba ya huzuni na masikitiko. —*Manuscript 39, 1908. {VSSsw 132.3}*

Neno la Mungu Ni Mwongozo wa Usemi wa Kila Siku—Maneno yetu, iwe tuko nyumbani au tunaposhirikiana na watu walio nje ya familia, yanapaswa kuwa ya fadhili, ya upendo/mapenzi, na safi. Ikiwa tutalichunguza Neno la Mungu na kulifanya sehemu ya maisha yetu, kama inavyoonyeshwa katika usemi “kulila Neno,” tutakuwa na uzoefu wenye afya ya kiroho ambao daima utadhihirisha Kweli. Tunapaswa kuchunguza mioyo yetu kwa bidii, tukilinganisha usemi wetu wa kila siku na mwenendo wa kazi zetu pamoja na Neno la Mungu, ili tusikosee. —*Manuscript 3, 1906. {VSSsw 133.1}*

Udhihirisho wa Nje wa Neema ya Ndani—Hitaji kuu la lugha ni kwamba iwe safi, yenye fadhili, na ya kweli—yaani, “udhihirisho wa nje wa neema ya ndani.” Shule bora zaidi ya kujifunza lugha hii ni nyumbani. *{VSSsw 133.2}*

Maneno ya fadhili ni kama umande na mvua nyepesi kwa nafsi. Maandiko yanasema juu ya Kristo kwamba neema ilimiminwa midomoni Mwake, ili aweze “*kujua jinsi ya kumtegemeza kwa maneno yeye aliyechoka.*” Naye Bwana anatuagiza: “*Maneno yenu na yawe na neema sikuzote,*” ili “*yawape neema wasikiao.*”—*Nyumba Inayomngojea Masihi, uk. 435. {VSS 133.3}*

Wakristo Wenye Staha/Uungwana—Wakristo huinuliwa katika mazungumzo yao; na ingawa wanaamini kwamba kujihusisha na sifa za kinafiki ni dhambi, wao ni watu wenye adabu, fadhili, na ukarimu. Maneno yao yana sifa ya unyofu na Ukweli. —*Jumbe kwa Vijana, uk. 349. {VSS 133.4}*

Furaha Aliyoitoa Mungu—Mungu amempa kila mtu furaha inayoweza kufurahiwa na matajiri pamoja na maskini. Hii ni furaha inayopatikana katika kukuza mawazo safi na matendo yasiyo ya ubinafsi; furaha inayotokana na kusema maneno ya huruma na kutenda matendo ya fadhili. Kutoka kwa wale wanaotekeleza huduma hiyo, nuru ya Kristo huangaza na kuyatia nuru maisha yaliyotiwa giza na huzuni nyingi. —*Shuhuda kwa Kanisa, juz. 9, uk. 57. {VSS 134.1}*

Maneno ya Fadhili na Matendo ya Upendo—Mungu anatamani kwamba baraka alizowapa watoto Wake kwa wingi zifikishwe kwa wale walio na mahitaji. Kupitia ushirika huo, kupitia maneno ya fadhili yanayoambatana na matendo ya upendo, wale wanaomtumikia Mungu watapata mpenyo wa kuingia miyoyoni mwa watu na kuwavuta wengine kwa Kristo. —*The Review and Herald*, Desemba 14, 1897. {VSS 134.2}

Roho ya Upole na Unyenyekevu—Unapomwendea mtu unayefikiri amekosea, hakikisha kwamba unazungumza naye kwa roho ya upole na unyenyekevu; kwa maana hasira ya mwanadamu haitendi haki ya Mungu. Mtu aliyekosea hawezi kurejeshwa kwa njia nyingine isipokuwa kwa roho ya upole, unyenyekevu, na upendo wa huruma. Kuwa mwangalifu katika mwenendo wako. Epuka jambo lolote katika sura, ishara, neno, au sauti linaloonyesha kiburi au kujiona kuwa bora na uliyejitosheleza. Jilinde dhidi ya neno au mtazamo wowote unaoweza kukuinua wewe mwenyewe au kulinganisha wema na haki yako na mapungufu ya mwingine. Jihadhari na dalili yoyote ya dharau, na kujiweka mbali, ukali, au kubeza. Epuka kwa makini kila mwonekano wa hasira; na ingawa unapaswa kusema waziwazi, usitumie lawama, mashtaka makali, wala ishara yoyote ya ukali isipokuwa ule unaotokana na upendo wa dhati. Zaidi ya yote, pasiwepe kivuli chochote cha chuki au nia mbaya, uchungu, ugwadu, wala ukali wa usemi. Hakuna kitu isipokuwa fadhili na upole kinachopaswa kutoka katika moyo wenye upendo. {VSS 134.3}

Hata hivyo, matunda haya ya thamani yasikuzuie kusema kwa namna yenye uzito na umakini mkubwa, kana kwamba macho ya malaika yanakutazama na kwamba unatenda ukiwa mbele ya hukumu inayokuja. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 2, uk. 52. {VSS 135.1}

SURA YA 27—ATHARI ZA MANENO JUU YA MWENYEWE

Ukosoaji Usio wa Uangalifu na Usio na Heshima—Mazoea ya kukosoa bila uangalifu na bila kicho/heshima huathiri tabia kwa kukuza ukosefu wa uchaji na kutokuamini. Watu wengi wanaojihusisha na tabia hii wameendelea bila kutambua

hatari iliyopo, mpaka wakafikia hatua ya kuwa tayari kukosoa na kuikataa kazi ya Roho Mtakatifu. Yesu alisema: *“Kila neno lisilo maana watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu yake siku ya hukumu. Kwa kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa.”*—*Tumaini za Vizazi Vyote*, uk. 323. {VSS 136.1}

Afya ya Akili na Mwili—Kila neno la fadhili na huruma linalosemwa kwa mtu mwenye huzuni, kila tendo linalofanywa ili kuwasaidia waliokandamizwa, na kila zawadi inayotolewa ili kukidhi mahitaji ya wanadamu wenzetu, ikiwa vimetolewa au kufanywa kwa ajili ya utukufu wa Mungu, vitamletea baraka yule anayetoa. Wale wanaofanya kazi hiyo wanatii sheria ya mbinguni na watapokea kibali cha Mungu. Furaha ya kuwafanyia wengine, mema huleta uchangamfu katika hisia, unaopita katika mishipa ya fahamu, kuharakisha mzunguko wa damu kwa njia bora, na kuchochea afya ya akili na mwili. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 4, uk. 56. {VSS 136.2}

Uchangamfu na Amani—Uchangamfu, utulivu wa moyo, na amani vinapowafanya wengine kuwa na furaha na afya njema, mambo hayo pia humletea mtu mwenyewe manufaa makubwa sana. Huzuni na kuzungumza juu ya mambo ya kuhuzunisha huchochea kumbukumbu za matukio yasiyofurahisha na kurudisha tena juu ya mtu mwenyewe athari zake mbaya. Mungu anataka tusahau mambo hayo yote—tusiangalie chini, bali juu; juu! —*Akili, Tabia na Haiba*, juz. 2, uk. 662. {VSS 137.1}

Msaada kwa Wengine Ni Msaada Kwako Mwenyewe—Wengi wako katika hali ya giza na mkanganyiko. Wamepoteza mwelekeo wao na hawajui ni njia gani wanayopaswa kufuata. Hebu wale waliochanganyikiwa na watafute wengine walio katika hali hiyo hiyo, kisha wazungumze nao maneno ya tumaini na kutia moyo. Wanapoanza kufanya kazi hii, nuru ya mbinguni itawaonyesha njia wanayopaswa kufuata. Kwa maneno yao ya faraja kwa walioteseka, wao wenyewe watafarijiwa. Kwa kuwasaidia wengine, wao wenyewe watasaidiwa kutoka katika matatizo yao. Furaha itachukua nafasi ya huzuni na kukata tamaa. Moyo uliojawa na Roho wa Mungu hung’aa kwa uchangamfu wa upendo kwa kila mwanadamu mwenzake. Kila mtu wa namna hiyo hatabaki tena gizani; kwa maana “giza” lake litakuwa “kama adhuhuri.”—*The S.D.A. Bible Commentary*, juz. 4, uk. 1151. {VSS 137.2}

Huruma kwa Wengine, Siyo Kujihurumia Mwenyewe—Maisha ya baadhi ya watu hayana amani wala furaha kwa sababu hawajawahi kutoka katika mzunguko wa kujifikiria wenyewe. Daima wanatafuta huruma kutoka kwa wengine. Ikiwa wangejitahidi kuona jinsi wanavyoweza kuwa msaada kwa wengine na kusema maneno ya upendo na ujasiri, nafsi zao ambazo sasa ni kavu na zenye huzuni zingekuwa kama bustani iliyotiwa maji. —*Wana na Binti za Mungu*, uk. 88. {VSS 137.3}

Maneno ya Hasira Kali—Neno moja la hasira linaweza kumpa Shetani nafasi na mara nyingi huijeruhi nafsi yako mwenyewe na kuwafanya wengine waondoke katika nuru. —*The Review and Herald*, Mei 3, 1887. {VSS 138.1}

Hasira Kama Ulevi—Mtu anapoiruhusu roho ya hasira imtawale, ni kana kwamba amelewa sawa na mtu aliyekiweka kikombe kinywani mwake. Jifunze ustadi wa ukimya na tambua kwamba Mungu anawaheshimu wale walionunuliwa kwa damu ya Kristo. Jifunzeni; tunapaswa kujifunza kila siku. Tunapaswa kupanda juu zaidi na zaidi na kusogea karibu zaidi na Mungu. Ondoeni takataka katika njia ya Mfalme. Tengenezeni njia ili Mfalme aweze kutembea katikati yetu. Ondoeni maneno machafu vinywani mwenu (*tazama Wakolosai 3:8*). —*Akili, Tabia na Haiba*, juz. 2, uk. 582. {VSS 138.2}

Ukali wa Maneno Ni Jeraha Linalokuumiza Mwenyewe—Majaribu makali yatakujia. Weka tumaini lako kwa Bwana Yesu Kristo. Kumbuka kwamba kwa ukali wa maneno utajijeruhi mwenyewe. Ikiwa katika kila hali utakaa katika mahali pa mbinguni pamoja na Kristo, maneno yako hayatakuwa kama risasi zinazojeruhi mioyo na zinazoweza kuharibu maisha. —*Akili, Tabia na Haiba*, juz. 2, uk. 578. {VSS 138.3}

Maneno matupu na mabaya—Onyo la Kristo kuhusu dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu linahusiana kwa karibu na onyo dhidi ya maneno yasiyo na manufaa na maovu. Maneno ni dalili ya kile kilicho ndani ya moyo. “*Kwa kuwa kinywa hunena yaujazayo moyo.*” Lakini maneno ni zaidi ya dalili ya tabia; yana nguvu ya kuathiri tena tabia yenyewe. Wanadamu huathiriwa na maneno yao wenyewe. Mara nyingi, kwa msukumo wa muda mfupi unaochochewa na Shetani, hutamka wivu au kushuku mabaya, wakisema mambo ambayo kwa kweli hawaamini; lakini

maneno hayo huathiri tena mawazo yao. Hupotoshwa na maneno yao wenyewe na hatimaye huanza kuamini jambo lile lililosemwa kwa msukumo wa Shetani. Baada ya kutoa maoni au uamuzi fulani, mara nyingi huwa na kujiona/kiburi cha kuyakataa, hivyo hujaribu kujithibitisha kuwa wako sahihi mpaka wanaishia kuamini kwamba ni kweli. Ni hatari kutamka neno la mashaka; ni hatari kuhoji na kukosoa nuru ya Mungu. —*Tumaini za Vizazi Vyote*, uk. 323. {VSS 138.4}

Matukano Ni Laana Mara Mbili—Ni nani asiyependa maisha na kutamani kuona siku njema? Lakini ni wachache kiasi gani wanaotimiza masharti ya kuuzuia ulimi wao usiseme mabaya na midomo yao isitamke hila. Ni wachache walio tayari kufuata mfano wa Mwokozi katika upole na unyenyekevu. Wengi humwomba Bwana awanyenyekeze, lakini hawako tayari kukubali nidhamu inayohitajika. Jaribu linapokuja, matatizo yanapotokea, au hata mambo madogo yanapowakasirisha, mioyo yao huasi, na ndimi zao hutamka maneno yaliyo kama mishale yenye sumu au mvua ya mawe yenye kuangamiza. {VSS 139.1}

Kuzungumza uovu kuhusu wengine ni laana mara mbili, kwa maana humwangukia zaidi msemaji kuliko msikilizaji. Yeye anayesambaza mbegu za mafarakano na ugomvi huvuna ndani ya nafsi yake mwenyewe matunda mabaya yenye kuua. Jinsi alivyo mwenye huzuni msengenyaji na yule anayeshuku mabaya ya wengine! Yeye ni mgeni kwa furaha ya kweli. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 5, uk. 176. {VSS 139.2}

SURA YA 28—UTAMBUZI KATIKA KUKEMEA

Ujumbe wa Kweli

Ikiwa kuna wakati ambapo watu wanahitaji kutembea mbele za Mungu kama Henoko alivyotembea, basi ni sasa. Waadventista wa Sabato wanapaswa kuonyesha unyofu wao kwa maneno safi, usemi ulio safi, na maneno yaliyojaa huruma, upole, na upendo. **{VSS 140.1}**

Kuna nyakati ambazo maneno ya kukemea na kuonya yanahitajika. Wale waliopotoka kutoka katika njia iliyo sahihi wanapaswa kuamshwa ili watambue hatari inayowakabili. Ujumbe unapaswa kutolewa ambao utawatikisa kutoka katika usingizi wa kiroho unaofunga fahamu zao. Lazima kuwe na matengenezo ya maadili; la sivyo nafsi zitapotea katika dhambi zao. Acha ujumbe wa Kweli, kama upanga mkali wenye makali kuwili, upenye mpaka moyoni. Toeni miito itakayowaamsha wasiojali na kuyarudisha kwa Mungu mawazo ya wapumbavu na waliopotoka. —*Shuhuda kwa Kanisa, juz. 7, uk. 155.* **{VSS 140.2}**

Kukemea Katika Upendo—Tunapotafuta kuwarekebisha au kuwabadilisha wengine, tunapaswa kuwa waangalifu katika matumizi ya maneno yetu. Maneno hayo yanaweza kuwa harufu ya uzima iletayo uzima au harufu ya mauti iletayo mauti. Katika kutoa karipio au ushauri, wengi hutumia maneno makali na kama sindano, yasiyofaa kuponya nafsi iliyojeruhiwa. Kwa sababu ya maneno hayo yasiyofikiriwa vizuri, roho huchafuka, na mara nyingi waliokosea huchochewa kuasi. Wote wanaotetea kanuni za kweli wanapaswa kupokea mafuta ya mbinguni ya upendo. Katika kila hali, karipio linapaswa kutolewa kwa upendo. Ndipo maneno yetu yataleta matengenezo badala ya kuamsha uchungu na hasira. Kristo, kwa njia ya Roho Wake Mtakatifu, atatoa nguvu na uwezo. Hiyo ndiyo kazi Yake. —*Mifano ya Masihi, uk. 337.* **{VSS 140.3}**

Uwazi Unaodaiwa, Aina ya Ubinafsi—Baadhi ya watu hujivunia kuwa wazi sana katika kusema, wakali, na wasio na maneno ya upole; nao huliita jambo hilo unyofu wa kusema jambo kama lilivyo-frankness. Lakini hilo si jina linalofaa; huo ni ubinafsi wa kiwango cha juu kabisa. Watu hawa wanaweza kuwa na sifa njema; wanaweza kuwa wakarimu na kuwa na nia nzuri, lakini mwenendo wao usio na adabu huwafanya karibu wasivumilike. Wanakosoa, wanaumiza, na kusema mambo yasiyopendeza. Je, tabia wanayoikuza itawapendekeza kwa Yesu? Je, itawaandaa kwa ajili ya ushirika wa mbinguni? Ni vema tujichunguze ili kuona ni aina gani ya roho tunayokuza ndani yetu. Hebu tujifunze kusema kwa upole na utulivu hata

katika mazingira magumu zaidi. Tudhibiti si maneno yetu pekee, bali pia mawazo na fikira zetu. Hebu tuwe wema na wenye adabu katika maneno yetu na mwenendo wetu. Kuna upungufu mkubwa katika jambo hili. —*The Review and Herald*, Aprili 29, 1884. {VSS 141.1}

Wakristo Wenye Ukali na Uchungu—Sifa njema ambazo wengi wanazo hufichwa, na badala ya kuwavuta watu kwa Kristo, zinawafukuza. Ikiwa watu hawa wangeona athari ya mwenendo wao usio na adabu na maneno yao yasiyo ya fadhili kwa wasioamini, na jinsi mwenendo huo unavyomchukiza Mungu, wangebadili mazoea yao; kwa maana ukosefu wa adabu ni mojawapo ya vikwazo vikubwa vinavyowazuia wenye dhambi. Wakristo wenye ubinafsi, walalamikaji, na wenye uchungu huzuia njia, kiasi kwamba wenye dhambi hawatamani kumkaribia Kristo. —*Mwito Wetu Mkuu*, uk. 229. {VSS 141.2}

Maneno Makali—Maneno makali hupiga moyo kupitia masikio, na kuamsha tamaa mbaya kabisa za nafsi, huku yakimshawishi mwanadamu kuvunja amri za Mungu. —*Nyumba Inayomngojea Masihi*, uk. 439. {VSS 142.1}

Kuwarekebisha Watoto—Maneno makali na yenye hasira hayatokani na mbingu. Kukemea kwa ukali, kuudhika na kulalamika hakusaidii kamwe; badala yake, huchoea hisia mbaya zaidi ndani ya moyo wa mwanadamu. Watoto wako wanapokosea na kujazwa na roho ya uasi, nawe unapojaribiwa kusema na kutenda kwa ukali, subiri kabla hujawarekebisha. Wape nafasi ya kutafakari, na ruhusu hasira yako itulie. —*Mwongozo wa Mtoto na Mzazi*, uk. 246. {VSS 142.2}

Pembe Kali na Sehemu Zenye Ukali—Pembe kali na zisizo laini katika tabia zetu, pamoja na udhihirisho wa ubinafsi katika maneno na matendo yasiyo ya fadhili, hulipasua vazi laini la upendo na furaha ya kibinadamu. —*The Review and Herald*, Julai 18, 1893. {VSS 142.3}

Watumishi wa Mwovu—Yeye anayepokea Roho ya Kristo kwa moyo wake ataonyesha kupitia maneno ya fadhili na mwenendo wenye adabu. Lakini wale wanaodai kuwa na kweli huku wakiwa wakali, rafu-wenye mikwaruzo, wenye uchungu, na wasio na fadhili katika maneno na mwenendo wao, hawajajifunza kutoka kwa Yesu. Maonyesho hayo yote yanaonyesha kwamba bado ni watumishi wa yule mwovu. —*Mwito Wetu Mkuu*, uk. 238. {VSS 142.4}

Kuelimisha Midomo Yetu—Na tufanye agano na Mungu kwamba hatutasema neno lolote la wivu au lisilo la fadhili. Midomo yetu isimvunjie Mungu heshima kwa maneno ya kulalamika na kutoridhika. Izoeshie midomo yako kumsifu Yeye ambaye Kwake hutoka baraka zote. —*The Review and Herald*, Mei 1, 1888. {VSS 143.1}

Mabishano Yasiyo ya Lazima

Isipokuwa jambo muhimu sana linahusika, uwe tayari kuacha/kusaliisha maoni yako mwenyewe kuliko kuanzisha mabishano. Hata kama kwa hoja unaweza kushinda msimamo wako, unaweza kumwekea mtu mwingine mzigo unaozidi sana faida unayoona utaipata. Ni vigumu kuponya majeraha yaliyosababishwa na maneno makali. {VSS 143.2}

Mara nyingi unaweza kulinda amani kwa kuuzuia ulimi wako. Kamwe usilete katika mazungumzo yako mambo yatakayozalisha ugomvi, yakiumiza nafsi yako na nafsi za wengine. —*Manuscript 60, 1903*. {VSS 143.3}

Usemi wa Haraka na Usio na Subira

Katika matumizi ya lugha, labda hakuna kosa ambalo vijana na wazee hulipuuza zaidi kuliko kusema kwa haraka na bila subira. Hufikiri kuwa ni kisingizio cha kutosha kusema: “Nilikuwa sijajitawala na nikawa nje ya kituo changu cha ulinzi, na sikumaanisha nilichosema.” Lakini Neno la Mungu halilichukulii jambo hilo kuwa dogo. Maandiko yanasema: “*Je! Umemwona mtu mwenye kuhamaki katika maneno? Afadhali kumtumaini mpumbavu kuliko yeye.*” (Mithali 29:20). Mtu “*Asiyetawala roho yake ni mfano wa mji uliobomolewa usio na kuta.*” (Mithali 25:28). {VSS 143.4}

Kwa muda mfupi tu, kupitia ulimi wa haraka, wenye hasira, na usio wa uangalifu, uovu unaweza kutendeka ambao hata maisha yote ya kutubu hayawezi kuurekebisha. Lo! Ni mioyo mingapi imevunjika, marafiki wametengana, na maisha yameharibiwa kwa sababu ya maneno makali na ya haraka ya wale ambao wangeweza kuleta msaada na uponyaji! —*Elimu*, uk. 236, 237. {VSS 144.1}

Tabia Iliyotawaliwa na kuratibiwa Vizuri

Ni “jibu la upole” ndilo “linalogeza hasira.” Kulipiza kisasi hakujawahi kumshinda adui. Tabia iliyoratibiwa vizuri huleta ushawishi mwema kwa wote

wanaotuzunguka; lakini *“asiyetawala roho yake ni mfano wa mji uliobomolewa usio na kuta.”*—*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 4, uk. 367, 368. {VSS 144.2}

Maneno ya Kukasirika na Kuapa

Sehemu kubwa ya furaha ya maisha hutegemea mwenendo wetu na matendo yetu kwa wengine. Neno kali linapaswa kuachwa lisitamkwe. Maneno ya hasira yanapaswa kuzimwa katika upendo wa Yesu Kristo; kwa maana ikiwa uchafu huu hautaondolewa katika nafsi, hakuna tumaini la uzima wa milele. Tabia ya ubinafsi na mlipuko wa maneno ya hasira vimewekwa katika orodha ile ile ya giza pamoja na kuapa. —*Letter 6a, 1893*. {VSS 144.3}

Kuwaza na Kusema Mabaya

Hakuna jambo ambalo Kristo analihitaji zaidi kuliko kuwa na watenda kazi wanaohisi wajibu wa kumwakilisha. Kusema mabaya na kuwaza mabaya ni uharibifu kwa nafsi. —*Manuscript 8a, 1888*. {VSS 144.4}

Hakuna Maneno ya Kuudhi

Mungu anatamani maneno yako yawe yenye kutoa uzima. Lisitamkwe neno lolote la kuudhi au la kuchochea hasira. Hata kama umechokozwa kiasi gani, zuia kila neno ambalo lingeamsha uovu katika moyo wa mwingine. Usemi ni kipawa kikubwa; na Mungu anatamani kila mmoja afikie kiwango cha kufanana na Kristo. Kila neno unalosema na liwe la kubariki na kuinua. —*Manuscript 65, 1901*. {VSS 144.5}

Kuwakosoa Wengine

Mara nyingi kuna jaribu kubwa la kuzungumza juu ya mambo ambayo hayana faida kwa msemaji wala msikilizaji, bali huleta uovu na utasa kwa wote wawili. Muda wetu wa mlango wa rehema kufungwa ni mfupi sana kuutumia katika kutafakari mapungufu ya wengine. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 4, uk. 135. {VSS 145.1}

Midomo Iliyotakaswa—Mtu aliyeongoka kweli hana mwelekeo wa kufikiri wala kusema juu ya makosa ya wengine. Midomo yake imetakaswa, na akiwa shahidi wa Mungu hushuhudia kwamba neema ya Kristo imeubadilisha moyo wake. Ni wale tu ambao wameshinda jaribu la kuwaza na kusema mabaya ndio watakaolingia mbinguni. —*Wana na Binti za Mungu*, uk. 348. {VSS 145.2}

Wala Watu wa Leo—Maneno ya kashfa, ambayo kwa kweli ni aina ya kula nyama ya mwanadamu (cannibalism), hayatasemwa na wale wanaojilisha kwa Mkate wa Uzima, yaani Neno la Mungu aliye hai, na wanaofurahia utajiri wa ahadi Zake kuu mno na za thamani. Kupitia kwa Yesu Kristo, nafsi hushirikiana na malaika wa mbinguni; kwa hiyo, haina tamaa ya kujihusisha na porojo za kipuuzi zisizo na maana wala kuketi mezani pamoja na wachongezi (wala watu). Yesu Kristo anataka watoto Wake wawe “watenda kazi pamoja Naye,” watu wa maombi, wenye fadhili, wakarimu, na wenye bidii katika kutenda mema. —*Letter 14a, 1893. {VSS 145.3}*

Mbegu za Mashaka na Kutokuaminiana

Hebu wale wanaomcha Mungu na kuiamini kweli na waweke ulinzi midomoni mwao. Na waazimie kuto sema maneno yatakayodhuru kazi ya Mungu au kutoa taswira isiyo sahihi kuhusu kazi inayofanywa katika taasisi Zake zozote. Hebu na wawe waangalifu wasiseme maneno yatakayomshawishi mtu mwingine kuwanyima watumishi wa Mungu imani na maneno ya kutiwa moyo wanayostahili kupewa, hasa wale waliopitia majaribu makali na ambao huenda wamekuwa wakifanya kazi tangu asubuhi hadi usiku kutimiza majukumu mengi yanayokuja kwao, hata kufikia hatua ambayo akili zao zinakaribia kulemewa na mzigo huo na kuanguka. Mara nyingi, katika nyakati kama hizo, watu hujenga mawazo yasiyo sahihi kuhusu watumishi hao kwa sababu ya maneno ya kikatili yaliyojaa dhana na mashaka. Mbegu za mashaka na kutokuaminiana, kama mbegu za mmea wa miiba zinazopeperushwa na upepo, husambaa mbali na kote, wala haziwezi kukusanywa tena. —*Manuscript 94, 1904. {VSS 146.1}*

Maneno Yanayokubaliwa na Roho Mtakatifu

Upendo wa Mungu ndani ya moyo siku zote utatuongoza kusema maneno ya upole. *“Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo haujivuni wala kujitakabirisha; hautendi yasiyopasa; hautafuti yaliyo yake; haukasiriki upesi; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu, bali hufurahia pamoja na kweli; huvumilia yote, huamini yote, hutumaini yote, hustahimili yote. Upendo haupungui kamwe.” {VSS 146.2}*

Je, hatupaswi kukumbuka jambo hili? Ikiwa upendo wa Mungu umo mioyoni mwetu, hatutafikiri mabaya, hatutafadhaishwa kwa urahisi, wala hatutamruhusu hasira itutawale. Badala yake, tutaonyesha kwamba tumefungwa nira pamoja na

Nhandi Masunga na Grace Momadi Masaka-Jersey 2026 July

Kristo na kwamba nguvu ya kuzuia ya Roho Wake inatuongoza kusema maneno ambayo Yeye anaweza kuyakubali. Nira ya Kristo ndiyo kifungo kinachowekwa na Roho Mtakatifu ili kutudhibiti. Hasira inapoanza kutuchochea, na tuseme, “La! Kristo yuko kando yangu, nami sitamwaibisha kwa kusema maneno makali na yenye ghadhabu.”—*Manuscript 73, 1897. {VSS 146.3}*

SURA YA 29—SIFA NA SHUKRANI

Kumtukuza Mungu kwa Sifa

Ndugu zangu, Bwana Ndiye Mungu wetu. Ikiwa Kristo amefanyika ndani yetu, tumaini la utukufu, tunakuwa na tumaini katika Mungu ambalo haiwezekani

kulificha ndani yetu wenyewe. Tutamsifu Yeye. Hatumsifu kwa kiwango kinachostahili. Kila ampaye Mungu sifa humtukuza. Basi, badala ya kusema maneno ya huzuni na kusimulia majaribu na mateso yetu, na tumshukuru Mungu kwa kuwa ametujalia uwezo wa kusema, tena tuamue kwamba tutajitahidi kulitukuza jina Lake. —*Manuscript 39, 1908. {VSS 148.1}*

Sifa za Daima—Sauti zetu zinapaswa kusikika mara nyingi zaidi zikimsifu na kumshukuru Mungu. Sifa Zake zinapaswa kuwa daima mioyoni mwetu na midomoni mwetu. —*The Review and Herald, Mei 22, 1900. {VSS 148.2}*

Sehemu za Thamani Katika Uzoefu Wetu—Zaidi sana kuliko tunavyofanya sasa, tunapaswa kusimulia sura za thamani za uzoefu wetu. Baada ya kumiminwa kwa namna ya pekee kwa Roho Mtakatifu, furaha yetu katika Bwana na ufanisi wetu katika kumtumikia ungeongezeka sana ikiwa tungekuwa tukisimulia wema Wake na matendo Yake ya ajabu aliyowatendea watoto Wake. —*Mifano ya Masihi, uk. 299–300. {VSS 148.3}*

Furaha Mbinguni— “*Ndipo wale waliomcha Bwana waliposemezana wao kwa wao. Naye Bwana akasikiliza, akasikia; na kitabu cha ukumbusho kikaandikwa mbele Zake, kwa ajili ya hao waliomcha Bwana, na kulitafakari Jina Lake.*” **Malaki 3:16** Je, maneno waliyosema yalikuwa ya kulalamika, ya kulaumu, au ya kujihurumia? La. Kinyume chake, tofauti na wale wanaomnenea Mungu mabaya, wale wanaomcha Mungu huzungumza maneno ya kutia moyo, ya shukrani, na ya sifa. Maneno kama hayo huifanya mbingu yote kushangilia. Wanaoyasema wanaweza kuwa maskini kwa mali za dunia, lakini kwa kumrudishia Mungu kwa uaminifu sehemu anayodai, hukiri kwamba wanamwia deni. Kujitafutia faida hakutawali historia ya maisha yao. Kwa upendo na shukrani, wakiwa na nyimbo za furaha midomoni mwao, humletea Mungu sadaka zao wakisema, kama alivyosema Daudi: “*Kwani vitu vyote vyatoka kwako na katika vitu vyako mwenyewe tumekutolea.*” **1 Mambo ya Nyakati 29:14** —*The Review and Herald, Januari 5, 1897. {VSS 149.1}*

Kutoka Katika Hazina ya Mioyo Yetu—Ikiwa tunaufurahia upendo wa Mungu mioyoni mwetu, tutakuwa na jambo la kusema. Kutoka katika hazina ya mioyo yetu tutatoa mambo mema. Tutamtotea Mungu matunda ya midomo yetu. Maneno yetu yatakuwa maneno ya sifa na shukrani. —*Manuscript 74, 1897. {VSS 149.2}*

Rehema na Kweli ya Mungu—Niliona kwamba Mungu amekuwa Mwenye rehema kwa kutupa uwezo wa kusema. Ametupa ulimi, nasi tutawajibika Kwake kwa jinsi tunavyoutumia. Tunapaswa kumtukuza Mungu kwa vinywa vyetu kwa kusema maneno yanayoiheshimu Kweli Yake na rehema Zake zisizo na mipaka. Nasi tutashinda kwa neno la ushuhuda wetu na kwa damu ya Mwana-Kondoo. — *Maandiko ya Awali*, uk. 114. {VSS 149.3}

Sifa Ni Bora Kuliko Malalamiko—Ni afadhali kumsifu Bwana kuliko kulalamika. Hebu ndimi zetu zisitamke maneno ambayo tutayaonea aibu Kristo atakapokuja katika utukufu Wake pamoja na malaika Wake wote watakatifu. Tunapaswa kuwa safi katika midomo na mioyo yetu; tunapaswa kutakaswa na kusafishwa, kama Kristo alivyokuwa. —*Manuscript 95, 1909*. {VSS 150.1}

SURA YA 30—UANGALIFU KATIKA KUSEMA JUU YA WENGINE

Sifa Njema za Wengine—Jizoeshe kusema mema kuhusu wengine. Zingatia sifa njema za wale unaoshirikiana nao, na uone makosa na mapungufu yao kwa kiwango kidogo iwezekanavyo. Unapojaribiwa kulalamikia jambo ambalo mtu fulani amesema au ametenda, sifia au taja jambo jema katika maisha au tabia yake. Jizoeshe kuwa na moyo wa shukrani, na umsifu Mungu kwa upendo Wake wa ajabu

uliomfanya amtote Kristo afe kwa ajili yetu. —*Huduma ya Uponyaji*, uk. 492. {VSS 151.1}

Njia ya Wokovu kwa Wanaojaribiwa—Hakuna mtu anayekuwa bora kwa kulaumiwa au kushutumiwa. Kumwambia mtu anayepitia majaribu juu ya hatia yake hakumhamasishi kuazimia kufanya yaliyo mema zaidi. Badala yake, mwelekeze aliyekosea na aliyekata tamaa kwa Yeye awezaye kuwaokoa kabisa wote wanaomjia. Mwonyeshe kile anachoweza kuwa, na umwambie kwamba ndani yake mwenyewe hakuna jambo linalomfanya akubalike mbele za Mungu, bali Kristo alikufa kwa ajili yake ili akubalike ndani ya Mpendwa. —*Akili, Tabia na Haiba*, juz. 2, uk. 453. {VSS 151.2}

Hakuna Maneno ya Kujivuna Wala ya Mashtaka—Usemi ni kipawa cha ajabu. Mungu hutukuzwa zaidi kwa maneno ya upole kuhusu urithi Wake ulionunuliwa kwa damu ya Kristo kuliko kwa maneno ya kulaumu na kukosoa. Mawingu yatakuja, na maneno mabaya yatatoka kwa maadui wa Kweli ili kuwatesa wenye haki; lakini kamwe isiwe kwamba waumini wawasemee waumini wenzao maneno ya kiburi au ya mashtaka. Je, hatuna uthibitisho wa kutosha wa wema wa Mungu na baraka Zake wa kuijaza midomo yetu shukrani na sifa, na hivyo kumtukuza? {VSS 151.3}

Je, tutahesabiwa kuwa na haki kwa kutamka maneno ya chuki na ya kuharibu sifa za wale tunaodhani wamekosea? Je, sisi wenyewe hatujawahi kukosea? Je, hatujawahi kupita katika bonde la kukata tamaa? Mungu atusaidie kukumbuka jinsi ilivyo vigumu mtu anapojaribiwa na Shetani, halafu ndugu zake wenyewe wakasimama upande wa Shetani na kujaribu kumuumiza na kumwangamiza. Kwa hiyo, unapojaribiwa kusema maneno ya kulaumu, anza kuimba, "Msifuni Bwana." —*Manuscript 129, 1901*. {VSS 152.1}

Sifa za Kujipendekeza Hupotosha Akili—Kila namna ya sifa za kujikomba inapaswa kuondolewa, kwa maana hiyo ni kazi ya Shetani. Wanadamu maskini, dhaifu, na walioanguka kwa kawaida hujiona kuwa wa maana vya kutosha; hivyo hawahitaji kutiwa moyo kwa namna hiyo. Kuwasifu watumishi wa injili kwa namna ya kujipendekeza au kuwapaka mafuta kwa chupa ya mgongo si jambo linalofaa, kwa kuwa jambo hilo hupotosha akili na haliongozi kwenye upole na unyenyekevu.

Hata hivyo, wanaume na wanawake hupenda kusifiwa, na mara nyingi hata watumishi wa injili hulifurahia jambo hilo. Majivuno yao huridhishwa kwa sifa hizo, lakini zimekuwa laana kwa wengi. Kwa hiyo, karipio lina thamani zaidi kuliko sifa za udanganyifu tu ili ujikombe kwao. —*Shuhuda kwa Kanisa, juz. 2, uk. 338. {VSS 152.2}*

Matumaini Yasiyotimia—Maneno ya kujipendekeza ni matamu kwa moyo ambao haujatakaswa. Wengine wanaodhani kwamba wamesimama imara hudanganywa, huvutwa, na kulewa kwa matumaini ambayo kamwe hayatatimia. Kwa njia hiyo madhara makubwa yamefanyika. Kwa hiyo, kila mmoja anapaswa kufikiri na kusema kwa unyenyekevu kuhusu uwezo wake mwenyewe, huku akiwa mwangalifu asichochee kiburi na kujithamini kupita kiasi kwa wengine. —*Shuhuda kwa Kanisa, juz. 5, uk. 478. {VSS 152.3}*

Sifa za Wanadamu Ni Hatari—Wapo watu ambao daima huzungumza, husengenya, na kutoa ushuhuda wa uongo. Hawa hupanda mbegu za mafarakano na kuchochea ugomvi, na mbingu huwaona kuwa watumishi hodari zaidi wa Shetani na wenye ufanisi. Hata hivyo, mtu anayedhuriwa yuko katika hatari ndogo zaidi kuliko yule anayebembelezwa na kusifiwa kwa sababu ya mafanikio machache yanayoonekana, kwa kuwa sifa kutoka kwa marafiki wanaojifanya kuwa waaminifu ni hatari zaidi kuliko lawama. *{VSS 153.1}*

Kila mtu anayejisifu mwenyewe hupunguza uzuri wa matendo yake bora. Tabia iliyo ya kweli na yenye heshima haitashuka hadi kulipiza kisasi kwa mashtaka ya uongo kutoka kwa maadui; badala yake, kila neno linalosemwa dhidi yake hupita bila kumduru, kwa maana humtia nguvu katika yale ambayo maadui hawawezi kubomoa. —*Shuhuda kwa Kanisa, juz. 4, uk. 607. {VSS 153.2}*

Kweli Moyoni, Kweli Midomoni—Tunapaswa kuwa waangalifu kwa kiasi gani ili maneno na matendo yetu yapatane kikamilifu na Kweli takatifu ambayo Mungu ametukabidhi! Tunapokuwa pamoja, na tuwe waangalifu katika maneno yetu, na mazungumzo yetu yawe ya namna ambayo hayatatufanya tujute baadaye. Ikiwa upendo wa kweli umo moyoni mwako, utazungumza juu ya kweli na juu ya tumaini lenye baraka ulilo nalo katika Yesu. Ikiwa una upendo moyoni mwako, utajitahidi kumtia nguvu na kumjenga ndugu yako katika imani iliyo takatifu sana. Ikiwa neno lolote litatamkwa linaloharibu sifa ya rafiki au ndugu yako, usiunge mkono usemi huo mbaya au mazungumzo hayo yenye uovu, kwa maana hiyo ni kazi ya adui.

Nhandi Masunga na Grace Momadi Masaka-Jersey 2026 July

Badala yake, kwa upole mkumbushe msemaji kwamba Neno la Mungu linakataza mazungumzo ya namna hiyo. —*The Review and Herald*, Juni 5, 1888. {VSS 153.3}

SURA YA 31—TUMAINI NA KUTIA MOYO

Zeri ya Uponyaji—Wapo watu wanaokosea na kutambua aibu na upumbavu wao. Wana kiu ya kusikia maneno ya kuwatia moyo, lakini huendelea kutafakari makosa na mapungufu yao mpaka wanakaribia kukata tamaa kabisa. Badala ya kuwakemea, kuwahukumu, na kuzima nuru ya mwisho ya tumaini ambayo Jua la Haki huwaangazia mioyoni mwao, acha maneno yako yawe kama zeri ya uponyaji kwa

nafsi iliyojeruhiwa. Usiwe kama mvua ya mawe iharibuyo na kuangamiza tumaini changa linalochipuka miyoni mwao. Usimwache mtu mwenye njaa ya kiroho aangamie katika hali yake ya kutokuwa na msaada kwa sababu umeshindwa kusema maneno ya upole, yenye kujali, na nyororo na ya kutia moyo. —*Mwito Wetu Mkuu*, uk. 295. {VSS 155.1}

Kutia Moyo Kunawafurahisha Malaika—Maneno ya faraja na ya kutia moyo yanayosemwa wakati nafsi imechoka na nguvu ya ujasiri imepungua, Mwokozi huyahesabu kana kwamba yamesemwa Kwake Mwenyewe. Mioyo inapotiwa moyo, malaika wa mbinguni hulitazama jambo hilo kwa furaha na kulikubali. —*Huduma ya Uponyaji*, uk. 159. {VSS 155.2}

Maneno ya Ujasiri na Matumaini—Wapo watu wengi wenye ujasiri ambao wameelemewa sana na majaribu, kiasi cha kuwa karibu kuzimia katika mapambano dhidi ya nafsi na nguvu za uovu. Usimvunje moyo mtu wa namna hiyo katika pambano lake gumu. Badala yake, mtie moyo kwa maneno ya ujasiri na matumaini yatakayomsukuma kuendelea mbele. Kwa njia hiyo nuru ya Kristo itaangaza kupitia kwako. “*Kwa sababu hakuna mtu miongoni mwetu aishiye kwa nafsi yake, wala hakuna afaye kwa nafsi yake.*” (*Warumi 14:7*). Kwa ushawishi wetu, hata tusipoutambua, tunaweza kuwatia wengine moyo na kuwapa nguvu, au tukawavunja moyo na kuwaweka mbali na Kristo na Kweli. —*Ngazi ya Kufika Mbinguni-Njia Salama*, uk. 120. {VSS 155.3}

Bila Mashaka Wala Kukatisha Tamaa—Jifanyie kanuni ya kutotamka hata neno moja la mashaka wala la kukatisha tamaa. Kwa maneno ya matumaini na uchangamfu mtakatifu unaweza kufanya mengi kuangaza maisha ya wengine na kuimarisha juhudi zao. —*Ngazi ya Kufika Mbinguni-Njia Salama*, uk. 119–120. {VSS 156.1}

Hakuna Maneno Duni Wala ya Kawaida—Na tuufundishe ulimi kusema maneno yaliyo mema—maneno yatakayowatia moyo na kuwaimarisha wanadamu wenzetu. Na tuzungumze juu ya wema, rehema, na upendo wa Mungu. Ondoeni maneno yote ya kutokuamini, pamoja na maneno yote duni na ya kawaida. —*The Review and Herald, Machi 28, 1899*. {VSS 156.2}

Ujasiri Mtakatifu Unaotia Moyo—Acha ulimi uongozwe na ujasiri mtakatifu kusema maneno ya kutia moyo, maneno yatakayowaamsha na kuwaimarisha watu

ili wavunje vifungo vya uvivu na hali ya kujiona salama vinavyowafunga katika hali ya kutokuwa na uhakika. —*Letter 151, 1903. {VSS 156.3}*

Kurudia Maneno Kama Kasuku—Huwezi kuifikia mioyo ya watu kwa kutumia maneno ya mazoea au kwa kurudia-rudia misemo iliyokaririwa kama kasuku. Maneno unayosema yanapaswa kuwa udhihirisho wa uzoefu wako binafsi. Ikiwa utaitia mioyo ya watu ujasiri na matumaini, itakuwa kwa sababu neema na upendo wa Mungu ni uhalisia ulio hai katika maisha yako. Kinachopaswa kuonekana ndani yao ni chapa ya Mungu, si chapa yako mwenyewe. Lakini ikiwa mtenda kazi mwenyewe hajasafishwa na kubadilishwa, hataweza kuiwasilisha kweli kwa upya na kuburudisha, kwa nguvu na uwezo unaoamsha mwikio katika mioyo ya wale wanaolisikia Neno la uzima. —*The Review and Herald, Aprili 12, 1892. {VSS 156.4}*

Maneno ya Kutia Moyo—Vilio vya ulimwengu wenye huzuni vinasikika pande zote zinazotuzunguka. Dhambi imetanda kama kivuli juu yetu; kwa hiyo akili zetu zinapaswa kuwa tayari kwa kila neno jema na tendo jema. Tunajua kwamba Yesu yuko pamoja nasi. Ushawishi mtamu wa Roho Wake Mtakatifu hufundisha na kuyaongoza mawazo yetu, ukituongoza kusema maneno yatakayowatia watu moyo na kuangaza njia ya wengine. —*Shuhuda kwa Kanisa, juz. 6, uk. 115. {VSS 157.1}*

Sauti za Upole na Zenye Kupendeza—Tunapaswa kusema maneno yatakayofariji na kutia moyo. Ndugu zangu, jizoezeni kusema kwa sauti za upole na zenye kupendeza. Kusema kwa fadhili hakudhuru kamwe; huleta mema. Lakini kusema kwa ukali na bila adabu huwafanya malaika watakatifu waondoke wakiwa na huzuni. —*The Review and Herald, Juni 15, 1905. {VSS 157.2}*

Kama Msumari Uliopigiliwa Mahali Imara—Mawazo makuu, matarajio yenye heshima na bora, ufahamu ulio wazi wa Kweli, makusudi yasiyo ya ubinafsi, na shauku ya uchaji na utakatifu vitaonekana katika maneno yanayofunua hazina iliyomo moyoni. *{VSS 157.3}*

Watu tunaoshirikiana nao kila siku wanahitaji msaada na mwongozo wetu. Huenda wakawa katika hali ambayo neno linalosemwa kwa wakati unaofaa litakuwa kama msumari uliopigiliwa mahali imara. —*Manabii na Wafalme, uk. 348. {VSS 158.1}*

Mbegu za Mashaka ni Kumtumikia Shetani—Hebu na tujilinde tuiseme maneno yanayokatisha tamaa. Hebu na tuamue kutoshiriki kamwe katika kusema mabaya au kusengeny. Hebu na tukatae kumtumikia Shetani kwa kupanda mbegu za mashaka. Na tujilinde tusikuze kutokuamini mioyoni mwetu wala kukukiri mbele ya wengine. Mara nyingi sana nimetamani kuwepo kwa ahadi iliyoandikwa yenye nadhiri ya kusema maneno yale tu yanayompendeza Mungu. Ahadi ya namna hiyo ni ya lazima kwa kadiri ile ile ambayo ilivyo ahadi ya kujiepusha na matumizi ya vileo vinavyoleweshwa. Na tuanze kuufundisha ulimi wetu nidhamu, tukikumbuka daima kwamba tunaweza kufanya hivyo tu kwa kuitia nidhamu akili, kwa maana *“kwa kuwa kinywa hunena yaujazayo moyo.” (Mathayo 12:34).* —*Mwito Wetu Mkuu, uk. 291. {VSSsw 158.2}*

Kumwasilisha Mwokozi—Lo, lisitamkwe neno lolote litakaloongeza maumivu! Kwa mtu aliyechoshwa na maisha ya dhambi, lakini asiyejua mahali pa kupata nafuu/afueni, mwelekeze kwa Mwokozi Mwenye huruma. Mshike mkono, mwinue, na useme naye maneno ya ujasiri na matumaini. Msaidie kuushika mkono wa Mwokozi. —*Huduma ya Uponyaji, uk. 168. {VSSsw 158.3}*

Ngazi ya Mbinguni—Yeye anayemjia Yesu anaweka miguu yake juu ya ngazi inayounganisha dunia na mbingu. Fundisha Ukweli huu kwa kalamu na kwa sauti kwamba Mungu Yuko juu ya ngazi hiyo, na kwamba miale yenye kung'aa ya utukufu Wake inaangazia kila hatua ya ngazi. Anawatazama kwa neema wote wanaopanda kwa taabu ili awapelekee msaada—msaada wa Kiungu—wakati mikono yao inanza kulegea na miguu yao kutetemeka. Naam, waambie; waambie kwa maneno yatakayoyeyusha moyo kwamba hakuna yeyote atakayeshindwa kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo ikiwa ataendelea kupanda kwa uvumilivu. Wale wanaomwamini Kristo hawatapotea kamwe, wala hakuna atakayewanyakua kutoka mkononi Mwake. *{VSS 158.4}*

Waambie watu kwa lugha iliyo wazi na yenye matumaini jinsi wanavyoweza kutoroka kutoka katika urithi wa aibu ambao kwa haki ndio sehemu yetu. Lakini kwa ajili ya Kristo, usiwaelezee mawazo yatakayowakatisha tamaa au kuwafanya njia ya kwenda mbinguni ionekane kuwa ngumu kupita kiasi. —*Jumbe Teule, juz. 1, uk. 181–182. {VSS 159.1}*

Dawa ya Kushinda Kuvunjika Moyo—Hatuwezi kumudu kuwa kikwazo kwa wengine kwa namna yoyote. Kila mmoja ana majaribu na mitihani yake ya pekee,

nasi tunapaswa kusimama mahali ambapo tunaweza kuwasaidia na kuwaimarisha wanadamu wanaojaribiwa. Tunapaswa kuwatia moyo na, ikiwezekana, kuwainua wale walio dhaifu katika imani. Kwa kuzungumza juu ya ahadi za Mungu, wakati mwingine tunaweza kuondoa huzuni/sonona na kukata tamaa katika mawazo ya wale wanaopitia majaribu na shida. —*Akili, Tabia na Haiba*, juz. 2, uk. 435.

{VSS 159.2}

Mazungumzo Kuhusu Mbinguni—Tunapoweza kushirikiana ili kusaidiana kuelekea mbinguni, na mazungumzo yetu yakawa juu ya mambo ya Mungu na ya mbinguni, ndipo kuzungumza kunakuwa na thamani ya Kweli. Lakini mazungumzo yanapojikita katika nafsi, mambo ya dunia, na mambo yasiyo na maana, kimya huwa dhahabu/bora kuliko kusema-silence is golden. Sikio linalotii litapokea karipio kwa unyenyekevu, uvumilivu, na moyo wa kufundishika. Hapo ndipo mawasiliano yetu sisi kwa sisi huwa yenye manufaa na kutimiza yote ambayo Mungu anakusudia. Pande zote mbili za maagizo ya Mungu zinapotimizwa, yule anayekaripia kwa hekima hutekeleza wajibu wake, naye anayesikiliza kwa utii husikia kwa kusudi na kufaidika. —*Wana na Binti za Mungu*, uk. 166. **{VSS 159.3}**

Mawazo Yenye Uchungu na Yasiyopendeza—Ni kazi ya Shetani kuzungumzia mambo yanayomhusu yeye mwenyewe, naye hufurahi wanadamu wanapozungumza juu ya uwezo wake na jinsi anavyotenda kazi kupitia kwa wanadamu. Kwa kuzoea mazungumzo ya namna hiyo, akili huwa yenye huzuni, uchungu, na isiyopendeza. Tunaweza kuwa mikondo ambayo Shetani huitumia kuwasilisha maneno yasiyoleta nuru katika moyo wowote. Lakini na tuamue kwamba haitakuwa hivyo. Na tuamue kutokuwa njia ambazo Shetani atazitumia kueneza mawazo ya huzuni na yasiyopendeza. Maneno yetu yasiwe harufu ya mauti iletayo mauti, bali ya uzima iletayo uzima. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 6, uk. 62–63. **{VSS 160.1}**

Udhaifu Wetu Usiwe Mada ya Mazungumzo—Si jambo la kusifiwa kuzungumzia udhaifu wetu na kukata tamaa kwetu. Badala yake, kila mmoja na aseme, “Ninahuzunika kwa sababu ninashindwa ninapojaribiwa, maombi yangu ni dhaifu sana, na imani yangu ni haba.” —*In Heavenly Places*, uk. 276. **{VSS 160.2}**

Hakuna Fadhila Katika Kukumbuka Dhambi—Kila mara tunapozungumza mambo ya giza, humfurahisha adui, kwa maana hataki furaha ya Kristo ikae mioyoni

Nhandi Masunga na Grace Momadi Masaka-Jersey 2026 July

mwetu kwa njia ya imani. Kristo kwetu ni chemchemi isiyokauka ya furaha na burudisho. Mungu haoni kuwa ni fadhila kwetu kuendelea kutazama na kuzungumzia makosa na dhambi zetu. —*Letter 42, 1896. {VSS 161.1}*

SURA YA 32—IMANI IWE MADA YA MAZUNGUMZO

Sheria ya Asili—Ni sheria ya asili kwamba mawazo na hisia zetu huchochewa na kutiwa nguvu tunapozieleza kwa maneno-tunapozitamka. Ingawa maneno huonyesha mawazo yetu, ni kweli pia kwamba mawazo hufuata maneno. Kama tungeizungumza imani yetu mara nyingi zaidi na kufurahia zaidi baraka tunazojua kuwa tunazo—yaani rehema kuu na upendo wa Mungu—tungekuwa na imani iliyo kubwa zaidi na furaha iliyo tele zaidi. Hakuna ulimi unaoweza kueleza, wala akili yenye mipaka haiwezi kufahamu kikamilifu, baraka zinazotokana na kuthamini wema na upendo wa Mungu. Hata tukiwa duniani tunaweza kuwa na furaha kama chemchemi isiyokauka, kwa kuwa hulishwa na mito inayotiririka kutoka katika kiti cha enzi cha Mungu. —*Huduma ya Uponyaji, uk. 251–253. {VSS 162.1}*

Mavuno Yasiyoepukika—Wale wanaonena juu ya imani na kuikuza watakuwa na imani; lakini wale wanaopenda na kukuza mashaka mioyoni mwao na kuyaonyesha kwa maneno watakuwa na mashaka. —*Shuhuda kwa Kanisa, juz. 5, uk. 302. {VSS 162.2}*

Chanzo cha Nguvu—Kama tungeizungumza imani yetu mara nyingi zaidi na kufurahia zaidi baraka tunazojua kuwa tunazo—reheba kuu, ustahimilivu, na upendo wa Mungu—kila siku tungekuwa na nguvu zaidi. Je, maneno yale ya thamani aliyoyasema Kristo, Mwana wa Mungu, hayatupi uhakika na nguvu zinazopaswa kuwa na ushawishi mkubwa juu yetu, kwamba Baba yetu wa mbinguni Yuko tayari zaidi kuwapa Roho Mtakatifu wale wanaomwomba kuliko wazazi walivyo tayari kuwapa watoto wao vipawa vyema? —*Jumbe Teule, juz. 2, uk. 243. {VSS 162.3}*

Mbegu za Mashaka Huzaa Mavuno ya Kutokuamini—Hebu na tuyalinde maneno yetu. Na tunene imani, nasi tutakuwa na imani. Kamwe tusikubali mawazo ya kukatisha tamaa kuhusu kazi ya Mungu, wala tusitamke neno lolote la mashaka. Neno la mashaka ni kama mbegu inayopandwa mioyoni mwa msemaji na wasikilizaji wake, nayo huzaa mavuno ya kukata tamaa na kutokuamini. —

Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, uk. 633. {VSS 163.1}

Nafasi au Faida Kubwa ya Shetani—Hata tunapopitia majaribu, lugha yetu inaweza kuwa ya imani, tumaini, na ujasiri. Lakini tusijiachie katika mzaha usiofaa wala masihara ya kipuuzi yenye maadili mabaya, ambayo twataka kuwaonyesha kwamba tuna akili zenye ujanja wa maneno (witticism); maneno ya namna hiyo yasitoke midomoni mwetu, kwa maana humpa Shetani nafasi kubwa ya kutupinga. —*The Review and Herald, Mei 13, 1884. {VSS 163.2}*

Fungua Madirisha Yanayoelekea Mbinguni—Kadiri unavyonena juu ya imani, ndivyo imani yako itakavyozidi kuongezeka. Kadiri unavyoendelea kukazia na kukaa katika fikira mambo ya kukatisha tamaa, na kuwaeleza wengine majaribu yako, na kuyakuza ili upate huruma unayoitamani, ndivyo utakavyokuwa na majaribu na mambo ya kukatisha tamaa zaidi. Kwa nini tuomboleze juu ya mambo ambayo hatuwezi kuyaepuka? Mungu anatumia sisi tuyafunge madirisha ya nafsi yanayoelekea duniani na tuyafungue yanayoelekea mbinguni, ili ajaze mioyo yetu

utukufu unaong'aa kutoka kwenye kizingiti cha mbinguni. —*Akili, Tabia na Haiba*, juz. 2, uk. 579. {VSS 163.3}

Hata Magumu Yawe Sababu ya Kushukuru—Mtu anapokuuliza hali yako, usitafute kufikiria jambo la kuhuzunisha ili upate huruma. Usizungumzie ukosefu wako wa imani, huzuni zako, wala mateso yako. Mjaribu hufurahia kusikia maneno ya namna hiyo. Unapozungumza mambo ya huzuni, wewe unamtukuza yeye. Hatupaswi kukazia katika fikira, nguvu kubwa ya Shetani ya kutushinda, kwa maana mara nyingi tunajiweka mikononi mwake kwa kuendelea kuzungumzia uwezo wake. {VSS 164.1}

Badala yake, na tuzungumzie nguvu kuu ya Mungu ya kuunganisha masilahi yetu yote na mapenzi Yake. Simulia juu ya nguvu za Kristo zisizo na kifani, na uzungumze juu ya utukufu Wake. Mbingu yote inajishughulisha na wokovu wetu. Malaika wa Mungu, maelfu kwa maelfu na makumi elfu mara makumi elfu, wametumwa kuwahudumia wale watakaourithi wokovu. Wanatulinda dhidi ya uovu na kuyasukuma nyuma majeshi ya giza yanayotafuta kutuagamiza. Je, sisi hatuna sababu ya kumshukuru Mungu kila wakati, hata pale ambapo inaonekana kuna magumu katika njia yetu? —*Huduma ya Uponyaji*, uk. 253–254. {VSS 164.2}

SURA YA 33—UNYENYEKEVU NA USAHILI KATIKA USEMI WETU

Siri za Mafanikio ya Injili—Mafanikio ya ujumbe wa Injili hayategemei hotuba za kitaalamu, ushuhuda wenye ufasaha, wala hoja nzito, bali hutegemea urahisi wa ujumbe wenyewe na jinsi unavyowasilishwa na kuratibiwa ili kuwafikia watu walio na njaa ya Mkate wa Uzima. “*Nifanye nini ili nipate kuokolewa?*” Hicho ndicho kilio na hitaji kubwa la nafsi. —*Mifano ya Masihi*, uk. 231. {VSS 165.1}

Usafi na Unyenyekevu—Kazi yetu ni kutumia kila fursa inayopatikana kuuwasilisha ukweli katika usafi na urahisi wake popote penye hamu au shauku ya kusikiliza sababu za imani yetu. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 3, uk. 214. {VSS 165.2}

Kazi Katika Miji—Bwana anawaambia watu Wake wakati huu: Ingieni katika miji, mkaihubiri Kweli kwa unyenyekevu na kwa imani. Roho Mtakatifu atafanya kazi

kupitia juhudi zenu ili kugusa mioyo ya watu. Msiingize mafundisho ya Imani ya kigeni katika ujumbe wenu, bali semeni maneno rahisi ya Injili ya Kristo ambayo yanaweza kueleweka na watu wa kila umri. Wasio na elimu pamoja na walioelimika wanapaswa kuifahamu kweli ya ujumbe wa malaika wa tatu, nao wanapaswa kufundishwa kwa unyenyekevu. Ikiwa mnataka kuwafikia watu kwa njia inayokubalika, nyenyekezeni mioyo yenu mbele za Mungu na kujifunza njia Zake. — *Huduma ya Tiba*, uk. 299. {VSS 165.3}

Kufungua Mioyo Iliyofungwa—Maneno ya Kweli na ya uaminifu kutoka kwa mwana au binti wa Mungu, yanayosemwa kwa unyenyekevu wa kawaida, yatafungua mlango wa mioyo ambayo imekuwa imefungwa kwa muda mrefu. — *Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 6, uk. 115. {VSS 166.1}

Maneno Rahisi Hufungua Mioyo Iliyofungwa—Mara nyingi watu wenye akili nyingi au mahiri zaidi, wanaohesabiwa na kusifiwa kuwa wenye vipawa vikubwa duniani, huburudishwa na maneno rahisi yanayotoka katika moyo wa mtu anayempenda Mungu na anayezungumza juu ya upendo huo kwa urahisi, kama vile mtu wa dunia anavyozungumza juu ya mambo yanayojaza akili yake. Mara nyingi maneno yaliyotayarishwa kwa uangalifu na kufikiriwa sana huwa na ushawishi mdogo. Lakini maneno ya Kweli na ya uaminifu/uadilifu kutoka kwa mwana au binti wa Mungu, yanayosemwa kwa unyenyekevu wa kawaida, yatafungua mlango wa mioyo ambayo imekuwa imefungwa kwa muda mrefu. — *Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 6, uk. 115. {VSS 166.2}

Uthibitisho Usiopitiliza Kiasi—Katika kizazi hiki, ambapo hadithi zinazovutia lakini zisizo za kweli zinaenea na kuvutia mawazo ya watu, Ukweli unaowasilishwa kwa mtindo rahisi na kuungwa mkono na hoja chache lakini zenye nguvu ni bora kuliko kutafuta na kuleta mkusanyiko mkubwa wa ushahidi; kwa maana mara nyingi jambo kuu halionekani wazi katika mawazo ya wengi baada ya kuletwa kwa pingamizi na ushahidi mwingi kuliko lilivyokuwa hapo mwanzo. Kwa watu wengi, kauli iliyo wazi hufanya kazi kubwa kuliko hoja ndefu. Wao huchukua mambo mengi kuwa ya Kweli bila kuhitaji maelezo marefu; hivyo ushahidi mwingi hauongezi uzito wa hoja katika mawazo yao. — *Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 3, uk. 36. {VSS 166.3}

Alama Wazi za Njiani—Dunia inahitaji watenda kazi sasa. Wito unatoka kila upande kama ule wa Makedonia: “Vuka uje utusaidie.” Hoja zilizo wazi, za moja

kwa moja, na zenye kuelekeza kama vingi vya kilomita au alama za njiani zitawashawishi watu wengi zaidi kuliko mlolongo mrefu wa hoja unaogusa mambo mengi, lakini ambao ni wachache tu wenye tabia ya kuchunguza mambo kwa kina watakaokuwa na hamu ya kuufuatilia. —*Shuhuda kwa Kanisa, juz. 3, uk. 39. {VSS 167.1}*

Maelezo Machache Lakini Yenye Nguvu—Maelezo machache lakini yenye nguvu kuhusu fundisho fulani yataikaza Kweli hiyo katika akili kwa uthabiti zaidi kuliko kuwasilisha habari nyingi kiasi kwamba hakuna jambo linalobaki wazi na dhahiri katika mawazo ya wale wasioifahamu imani yetu. Pamoja na mafundisho ya unabii, yapaswa kuingizwa pia mafundisho ya vitendo yanayotokana na mafundisho ya Kristo. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, uk. 171–172. {VSS 167.2}*

Mbegu za Kweli Zisipandwe Kina Kupita Kiasi—Baadhi ya watu wamejizoesha kuelekeza nguvu zao zote katika jambo moja pekee. Uwezo wa kuelekeza akili katika jambo moja bila kukengeushwa na mengine ni mzuri kwa kiwango fulani, lakini wale wanaotumia nguvu zote za akili katika mkondo mmoja wa mawazo mara nyingi huwa dhaifu katika mambo mengine. Katika mazungumzo, watu wa namna hiyo huchosha wasikilizaji. Maandishi yao hukosa mtindo mwepesi na wenye mtiririko mzuri. Wanapozungumza hadharani, mada waliyo nayo huwavutia sana kiasi kwamba huendelea kuichambua kwa undani zaidi na zaidi. Kadiri wanavyozidi kujikita ndani ya somo hilo, ndivyo wanavyoona maarifa na nuru zaidi, lakini ni wachache wanaoweza kuwafuata. *{VSS 167.3}*

Kuna hatari ya watu wa namna hiyo kupanda mbegu ya kweli kwa kina sana kiasi kwamba mche mchanga hautaweza kamwe kuchomoza juu ya uso wa ardhi. Hata Kweli zilizo wazi kabisa na muhimu zaidi zinaweza kufunikwa na maneno mengi kiasi cha kufanya zionekane zenye ukungu na zisizoeleweka. —*Watendakazi wa Injili, uk. 169. {VSS 168.1}*

Maneno ya Kristo Yalieleweka—Kwa kuzingatia yote yaliyo mbele ya muumini, uchaji-Mungu wake unapaswa kuzidi daima. Anapaswa kufanya kazi kwa ajili ya wokovu wa watu kwa kutumia akili na uwezo wake wote. Asijitahidi kupata sifa kwa ufasaha wa kusema au heshima ya wanadamu, bali ajitahidi kuwa na unyenyekevu

wa maisha na unyenyekevu wa usemi. Kristo hakuhitaji kufafanua neno lolote alilotumia. Maneno Yake yote yalikuwa rahisi, na hata watu wote walio wa kawaida na duni kabisa waliyaelewa. —*The Review and Herald*, Januari 7, 1909. {VSS 168.2}

Tofauti za Mawazo ya Wanadamu—Akili za wanadamu hutofautiana. Watu wenye viwango tofauti vya elimu na namna tofauti za kufikiri, hupokea maana tofauti kutokana na maneno yale yale, na ni vigumu kwa mtu mmoja kuwasilisha kwa mwingine mwenye tabia, elimu, na mazoea tofauti ya kufikiri wazo lilelile analoliona wazi katika akili yake mwenyewe. Hata hivyo, kwa watu waadilifu/waaminifu na wenye nia njema, anaweza kutumia maneno rahisi na ya wazi kiasi cha kuwafikishia maana yake kwa madhumuni yote ya vitendo. —*Jumbe Teule*, juz. 1, uk. 19. {VSS 168.3}

Ufasaha wa Juu Zaidi—Unapaswa kuwa chombo ambacho kupitia kwacho Mungu atazungumza na mioyo ya watu; mambo ya thamani yataletwa kwenye kumbukumbu, na kwa moyo uliojaa upendo wa Yesu utasema maneno yenye umuhimu na yenye kuleta uzima. Unyenyekevu wako na unyofu wako vitakuwa ufasaha wa juu zaidi, na maneno yako yataandikwa katika vitabu vya mbinguni kuwa maneno yanayofaa, yaliyo kama matufaha ya dhahabu katika vyombo vya fedha. —*Wana na Binti za Mungu*, uk. 274. {VSS 168.4}

Nuru Katika Kila Neno—Katika mkutano wa kambi wa Queensland mwaka 1898, nilipewa maagizo kwa ajili ya watenda kazi wetu wa Biblia-**Bible Workers**. Katika maono ya usiku, wahudumu na watenda kazi walionekana wakiwa katika mkutano ambapo mafundisho ya Biblia yalikuwa yakitolewa. Tulisema, “Leo tunaye Mwalimu Mkuu pamoja nasi,” nasi tulisikiliza maneno Yake kwa shauku. Alisema: “Kuna kazi kubwa iliyo mbele yenu mahali hapa. Mtahitaji kuwasilisha Ukweli katika urahisi wake. Waongozeni watu kwenye maji ya uzima. Waambieni mambo yanayohusu zaidi mema yao ya sasa na ya milele. Msifanye kujifunza kwenu Maandiko kuwa kwa juu juu, hovyoyote au kwa uzembe. Katika kila jambo mnalosema, tambueni kwamba mnacho kitu kinachostahili muda mtakaotumia kukisema na muda wa wasikilizaji wenu kukisikiliza. Zungumzieni mambo yale yaliyo ya msingi au muhimu, mambo yatakayofundisha, mkileta nuru katika kila neno. {VSS 169.1}

Jifunzeni kukutana na watu katika hali waliyonayo. Msiwasilishe mada zitakazoamsha mabishano. Hebu ,mafundisho yenu yasiwe ya namna ya kutatanisha akili. Msiwafanye watu wahangaika juu ya mambo mnayoyaelewa ninyi lakini wao hawayaoni, isipokuwa kama mambo hayo yana umuhimu na hatima kubwa kwa ajili ya wokovu wa nafsi. Msiwasilishe Maandiko kwa namna itakayoinua nafsi zenu au kuchochea majivuno kwa yule anayelifungua Neno la Mungu. Kazi ya wakati huu ni kuwazoeza na kuwafunza wanafunzi na watenda kazi kushughulikia mada kwa namna iliyo wazi, yenye uzito, na ya heshima.” —*Shuhuda kwa Kanisa, juz. 6, uk. 58–59. {VSS 169.2}*

Ugonjwa wa Kiroho—Hali yote ya ubaridi wa hisia na kutokuwa na uzito wa kiroho (*sang-froid*) ambayo imeenea sana, miondoko ya kuigiza (theatrical gestures), mambo ya mzaha na uzembe, utani na masihara yote, vinapaswa kuonekana na mtu aliyevaa nira ya Kristo kuwa “havifai”—ni kosa mbele za Mungu na ni kumkana Kristo. **{VSS 170.1}**

Mambo hayo huifanya akili ishindwe kujikita katika mawazo mazito na kazi yenye msingi; humfanya mtu asiwe na ufanisi, awe wa juu juu, na awe mgonjwa kiroho. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, uk. 644. {VSS 170.2}*

SEHEMU YA 4—MALEZI YA SAUTI

SURA YA 34—UMUHIMU WA MADA HII

Ufanisi Kama Watenda Kazi wa Kristo

Kwa juhudi ya dhati, wote wanaweza kupata uwezo wa kusoma kwa ufasaha, na akili mahiri na kueleweka, na kuzungumza kwa sauti iliyo kamili, wazi, yenye

nguvu, na yenye kuvutia. Kwa kufanya hivyo, tunaweza kuongeza kwa kiwango kikubwa ufanisi wetu kama watenda kazi wa Kristo. {VSS 173.1}

Kila Mkristo ameitwa kuwajulisha wengine utajiri usiochunguzika wa Kristo; kwa hiyo anapaswa kutafuta ukamilifu katika usemi. Anapaswa kulihubiri Neno la Mungu kwa namna itakayolifanya likubalike kwa wasikilizaji. Mungu hakusudii vyombo Vyake vya kibinadamu viwe visivyo na ustadi, vyenye uchafu au mvuto mbaya katika mawasiliano. Si mapenzi Yake kwamba mwanadamu apunguze au ashushie hadhi ule mkondo wa mbinguni unaopita kupitia kwake kwenda kwa ulimwengu. {VSS 173.2}

Tunapaswa kumtazama Yesu, Mfano mkamilifu; tunapaswa kuomba msaada wa Roho Mtakatifu, na kwa nguvu Zake, tutafute kuzoeza kila kiungo ili kitimize kazi yake kwa ukamilifu. {VSS 173.3}

Jambo hili ni la muhimu hasa kwa wale walioitwa katika huduma ya hadhara/umma. Kila mhudumu na kila mwalimu anapaswa kukumbuka kwamba anawapelekea watu ujumbe unaohusu hatima ya milele. Ukweli unaonenwa utawahukumu siku ile kuu ya hesabu ya mwisho. Kwa baadhi ya watu, namna mjumbe anavyowasilisha ujumbe itaamua kama wataupokea au kuukataa. Kwa hiyo, neno linapaswa kusemwa kwa namna litakayofikia ufahamu na kugusa moyo. Neno linapaswa kusemwa polepole, kwa uwazi, kwa heshima, na kwa uzito unaostahili umuhimu wake, lakini pia kwa bidii yote inayotokana na thamani yake. {VSSsw 173.4}

Malezi sahihi na matumizi yanayofaa ya uwezo wa kuzungumza yanahusiana na kila sehemu ya kazi ya Kikristo; yanaingia katika maisha ya nyumbani na katika mahusiano yetu yote na wengine. Tunapaswa kujizoesha kusema kwa sauti zenye kupendeza, kutumia lugha safi na sahihi, pamoja na maneno yenye fadhili, staha, uungwana na adabu. Maneno matamu na yenye upole ni kama umande na manyunyu laini kwa nafsi. Maandiko yanasema juu ya Kristo kwamba neema ilimiminwa midomoni Mwake ili aweze *“kujua jinsi ya kumtegemeza kwa maneno yeye aliyechoka.”* (Zaburi 45:2; Isaya 50:4). Naye Bwana anatuagiza: *“Maneno yenu yawe na neema siku zote”* (Wakolosai 4:6) *“ili liwape neema wanaosikia.”* (Waefeso 4:29). —Mifano ya Masihi, uk. 335–336. {VSSsw 174.1}

Kupuuza Malezi ya Sauti—Malezi na matumizi sahihi ya sauti yamepuuzwa sana, hata na watu wenye akili na wanaojihusisha na shughuli za Kikristo. Wapo wengi wanaosoma au kuzungumza kwa sauti ya chini sana au kwa haraka mno kiasi kwamba hawawezi kueleweka kwa urahisi. Wengine wana matamshi mazito yasiyo wazi; wengine huzungumza kwa sauti ya juu, kali, na yenye kupenya masikioni kama kingora, kiasi kwamba huwaumiza wasikilizaji. Maandishi ya Maandiko, nyimbo, na taarifa mbalimbali zinazosomwa mbele ya mikusanyiko ya watu wakati mwingine husomwa kwa namna ambayo hazieleweki, na mara nyingi nguvu na mvuto wake hupotea. —*Mifano ya Masihi, uk. 335. {VSS 174.2}*

Wajibu wa Mwalimu—**Palizi au** Malezi ya sauti yanapaswa kufundishwa katika masomo ya kusoma; na katika masomo mengine mwalimu anapaswa kusesitiza kwamba wanafunzi wazungumze kwa uwazi na watumie maneno yanayoeleza mawazo yao kwa usahihi na kwa nguvu. Wanafunzi wanapaswa kufundishwa kutumia misuli ya tumbo wakati wa kupumua na kuzungumza. Jambo hili litafanya sauti zao ziwe nzito, kamili, na wazi zaidi. —**Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi, uk. 216. {VSS 175.1}**

Somo la Msingi Katika Elimu—Wakati mafunzo ya sauti, kusoma, kuandika, na tahajia vitakapopewa nafasi yake inayostahili katika shule zetu, kutakuwa na mabadiliko makubwa yenye manufaa. Masomo haya yamepuuzwa kwa sababu walimu hawajatambua thamani yake. Lakini masomo haya ni muhimu zaidi kuliko Kilatini na Kigiriki. Sisemi kwamba kusoma Kilatini na Kigiriki ni jambo baya, bali nasema kwamba ni kosa kupuuza masomo yaliyo msingi wa elimu ili kuilemea akili kwa masomo ya matawi ya juu zaidi. —**Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi, uk. 218. {VSS 175.2}**

Muziki wa Sauti—Wale wanaopata uelewa sahihi kuhusu suala la malezi ya sauti wataona umuhimu wa kujielimisha na kujizoeza ili wamtukuze Mungu na kuwabariki wengine. Watajitia chini ya walimu wenye subira na uwezo, na ufanisi na kujifunza kusoma kwa namna itakayodumisha uzuri wa muziki wa sauti. Wakiwa na nia moja ya kumtukua Mungu, watatumia kikamilifu uwezo wao wa asili. Kwa kutawala vipawa vyao wenyewe, hawataaibishwa na kasoro za usemi, na manufaa yao katika kazi ya Mungu yataongezeka. —**Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi, uk. 247. {VSS 175.3}**

Mtiririko Laini na Wenye Mdundo wa Sauti—Yule anayesoma Biblia mbele ya kusanyiko au katika familia anapaswa kuwa na uwezo wa kusoma kwa mwendo wa sauti laini, wenye melodi nzuri ya muziki na unaovutia, ambao utawavutia wasikilizaji. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 6, uk. 380. {VSS 176.1}

Nguvu Kuu—Wale wanaohudumu katika neno na mafundisho wanapaswa kujitahidi kujikamilisha katika matumizi ya lugha. Sauti ni nguvu kuu, lakini wengi hawajajiozea sauti zao kwa namna ambayo ingeziwezesha kutumika kwa kiwango chake cha juu kabisa. —*The Review and Herald*, Machi 5, 1895. {VSS 176.2}

Uelewa Wazi kwa Kila Mtu—Yeye aliyetupatia vipawa vyote vinavyotuwezesha kuwa watenda kazi pamoja na Mungu, Anatarajia watumishi Wake wazitunze na kuzilea sauti zao ili waweze kuzungumza na kuimba kwa namna ambayo kila mtu ataweza kuelewa. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 9, uk. 144. {VSS 176.3}

Matamshi Yasiyo Kamili Humvunjia Mungu Heshima—Kila mmoja na atumie kwa kiwango cha juu kipawa cha usemi alichopewa. Mungu anahitaji huduma iliyo bora zaidi na yenye ukamilifu zaidi. Yeye Anavunjiwa heshima na matamshi yasiyo kamili ya mtu ambaye, kwa juhudi ya kudumu, angeweza kuwa chombo kinachokubalika cha kuwasilisha ujumbe Wake. Mara nyingi Ukweli huharibiwa kwa mkondo unaofikisha habari hizo. {VSS 176.4}

Bwana anawaita wote wanaohusika katika huduma Yake kuzingatia malezi ya sauti, ili waweze kutamka kwa namna inayokubalika Kweli kuu na takatifu alizowakabidhi. Mtu yeyote asiharibu ukweli kwa matamshi yenye kasoro. Wale ambao wamepuuza kukuza kipawa cha usemi wasidhani kwamba wamehitimu kwa huduma, kwa maana bado wanahitaji kupata uwezo wa kuwasilisha ujumbe. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 6, uk. 382–383. {VSS 176.5}

Sauti Zenye Kasoro za Wahudumu—Wachungaji na wahudumu wa Injili wanapaswa kujua jinsi ya kuzungumza kwa nguvu na kwa mvuto, wakifanya maneno ya uzima wa milele yawe yenye maana na yenye kushawishi kiasi kwamba wasikilizaji wahisi uzito wake. Ninaumia ninaposikia sauti zenye kasoro za wachungaji wetu wengi. Wahudumu wa namna hiyo wanamnyang'anya Mungu utukufu ambao angeupata kama wangukuwa wamejiozea kulitangaza Neno kwa nguvu. {VSS 177.1}

Hakuna mtu anayepaswa kujiona kuwa anastahili kuingia katika huduma ya kichungaji/kuhubiri mpaka, kwa juhudi ya kudumu, awe ameshinda kila kasoro katika matamshi yake. Anapojaribu kuzungumza na watu bila kujua jinsi ya kutumia kipawa cha usemi, nusu ya ushawishi wake hupotea, kwa maana huwa hana uwezo wa kutosha wa kushikilia usikivu wa kusanyiko. —*Shuhuda kwa Kanisa, juz. 6, uk. 381. {VSS 177.2}*

Matumizi Mabaya ya Kipawa cha Usemi—Kipawa cha usemi kimetumiwa vibaya sana na kimepotoka kutoka katika kusudi lake lililokusudiwa; lakini wale wanaodai kuwa watoto wa Mfalme wa mbinguni na waamke kutambua wajibu wao, na wakitumie kwa kiwango cha juu kipawa hiki. Mtu yeyote asiseme: “Hakuna faida kwangu kujaribu kuomba, kwa sababu wengine hawanisikii.” Badala yake aseme: “Nitafanya juhudi ya dhati na bidii, ili kushinda tabia hii isiyomtukuza Mungu ya kuzungumza kwa sauti ya chini na isiyoieleweka. Nitajiweka katika nidhamu mpaka sauti yangu isikike hata kwa wale walio na usikivu mdogo.”—**Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi, uk. 245–246. {VSS 177.3}**

Kristo Kama Kielelezo Chetu—Mafundisho ya Kristo yalikuwa yenye mvuto na uzito; sauti Yake ilikuwa yenye kupendeza kama muziki. Je, sisi nasi, kama Kristo, hatupaswi kujifunza kuwa na muziki katika sauti zetu? Yeye Alikuwa na ushawishi mkubwa kwa sababu alikuwa Mwana wa Mungu. Sisi tuko chini sana kuliko Yeye na tuna upungufu mwingi kiasi kwamba, hata tukifanya yote tuwezayo, juhudi zetu zitakuwa dhaifu. Hatuwezi kupata wala kuwa na ushawishi aliokuwa nao Yeye; lakini kwa nini basi tusijifunze kumkaribia Kielelezo hicho kadiri iwezekanavyo, ili tupate ushawishi mkubwa zaidi tunaoweza kuwa nao kwa watu? **{VSS 178.1}**

Maneno yetu, matendo yetu, mwenendo wetu, mavazi yetu, na kila jambo linalotuhusu linapaswa kuwa mahubiri. Si kwa maneno yetu pekee tunapaswa kuwafikia watu, bali kila kitu kinachohusiana na maisha yetu kinapaswa kuwa ujumbe na hubiri kwao, ili waone picha sahihi na Ukweli unaosemwa uwafikie na kuupeleka majumbani mwao. Kwa njia hiyo imani yetu itaonekana katika nuru bora zaidi mbele ya jamii. —*Shuhuda kwa Kanisa, juz. 2, uk. 617–618. {VSS 178.2}*

Wajibu wa Vijana—Vijana wa kiume na wa kike, je, kama watu binafsi, mlionunuliwa kwa gharama isiyo na kikomo, mmejithahidi kujionyesha kuwa mmekubaliwa na Mungu, kuwa watenda kazi wasio na sababu ya kuona aibu-

kutahayari? Je, mmemletea Mungu kipawa cha thamani cha sauti zenu, na kufanya juhudi ya bidii kuzungumza kwa uwazi, kwa kutamka vizuri, na kwa urahisi? Hata kama namna yenu ya kutamka si kamilifu, mnaweza kurekebisha kasoro zenu na kukataa kuendelea kuwa na sauti ya puani au kuzungumza kwa kubana na bila uwazi. Ikiwa matamshi yenu yatakuwa wazi na yanayoeleweka, manufaa yenu yataongezeka sana. Kwa hiyo msiachie tabia yoyote yenye kasoro katika usemi bila kuirekebisha. —*Misingi ya Elimu kwa Kila Mwanadamu*, uk. 215. {VSS 178.3}

Lugha Sahihi na Sauti Iliyolelewa—Kitabu kikuu cha elimu ni Biblia, lakini ni wachache wanaoisoma au kuitekeleza katika maisha. Laiti kila mtu angejitahidi kuwa yote anayoweza kuwa, akitumia fursa zake kwa kiwango bora kabisa, na kudhamiria kutumia kila uwezo ambao Mungu amempa, si kwa ajili ya maendeleo ya mambo ya duniani pekee, bali pia kwa ajili ya maendeleo ya mambo ya kiroho. Laiti wote wangetafuta na kuchunguza kwa dhati na bidii kujua Ukweli na kujifunza kwa juhudi ili wawe na lugha sahihi na sauti zilizoratibiwa, ili waweze kuwasilisha Ukweli katika uzuri wake wa hali ya juu na wenye kuinua. {VSS 179.1}

Hebu mtu yeyote asifikiri kwamba ataingia tu kwa kubahatisha katika nafasi ya manufaa bila maandalizi. Ikiwa watu wanataka kutumiwa katika kazi ya Mungu, wanapaswa kutumia nguvu zao zote na kuelekeza akili zao kwa bidii katika kujifunza. Ni Shetani anayetaka kuwaweka watu katika ujinga na kutokuwa na uwezo, ili wakue kwa upande mmoja tu ambao baadaye hawawezi kurekebisha mambo kwa kuwa na msawaziko mzuri. Adui anataka watu watumie uwezo mmoja wa vitivo/uwezo huku wakipuuza mingine, kiasi kwamba akili inapoteza nguvu zake na inapohitajika wakati wa dharura ishindwe kuitikia. Mungu anataka watu wafanye yote wawezayo; wakati Shetani anavuta akili upande mmoja, Yesu anaivuta upande mwingine. —*Misingi ya Elimu kwa Kila Mwanadamu*, uk. 256. {VSS 179.2}

Watenda Kazi Pamoja na Roho Mtakatifu—Baadhi ya watu hudhani kwamba Bwana atamwezesha mtu kwa Roho Wake kuzungumza kwa namna Anayotaka bila juhudi yoyote kutoka kwake. Lakini Bwana hakisudii kufanya kazi ambayo amempa mwanadamu kuifanya. Yeye Ametupatia uwezo wa kufikiri, kudadavua na nafasi za kuelimisha akili na kuboresha mwenendo. Baada ya kufanya yote tunayoweza kwa ajili yetu wenyewe, tukitumia vizuri faida na fursa tulizo nazo, ndipo tunaweza kumwomba Mungu kwa bidii afanye kwa Roho Wake kile ambacho sisi wenyewe hatuwezi kufanya. —*The Review and Herald*, Februari 5, 1880. {VSS 180.1}

SURA YA 35—UWAZI NA USAFI WA MATAMSHI

Uwezo Unaofaa wa Kuzungumza au Stahiki ya Kuzungumza—Kwa maombi ya dhati na juhudi za bidii, tunapaswa kupata uwezo unaofaa wa kuzungumza. Uwezo huu unahusisha kutamka kila silabi kwa uwazi na kuweka mkazo na msisitizo mahali panapostahili. Zungumza polepole. Watu wengi huzungumza kwa haraka, wakiharakisha neno moja baada ya jingine kiasi kwamba athari ya maneno yao hupotea. Katika yote unayosema, weka roho na uzima wa Kristo. —**Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi**, uk. 254–255. {VSS 181.1}

Mafunzo ya Sauti—Yeye aliyetupatia vipawa vyote vinavyotuwezesha kuwa watenda kazi pamoja na Mungu, anatarajia watumishi Wake wazipalilie na kuziratibu sauti zao ili waweze kuzungumza na kuimba kwa namna ambayo kila mtu ataweza kuelewa. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 9, uk. 144. {VSS 181.2}

Kuwa Msemaji wa Mungu—Mtu anayekubali nafasi ya kuwa msemaji wa Mungu anapaswa kuona kuwa ni jambo la muhimu sana kuwasilisha Ukweli kwa neema na akili yote anayoweza kuwa nayo, ili Ukweli usipoteze chochote katika namna anavyowasilisha kwa watu. Wale wanaodhani kuwa ni jambo dogo kuzungumza kwa matamshi yasiyo kamili wanamvunjia Mungu heshima. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 665. {VSS 181.3}

Kushinda Matamshi Yasiyoeleweka—Katika kusoma au kukariri, matamshi yanapaswa kuwa wazi. Sauti ya puani au mkao usiofaa unapaswa kurekebisha mara moja. Kila ukosefu wa uwazi katika matamshi unapaswa kutambuliwa kuwa ni kasoro. Watu wengi wamejizoesha kuzungumza kwa namna nzito na isiyoeleweka, kana kwamba ulimi wao ni mkubwa kuliko nafasi ya kinywa chao. Tabia hii imezuia sana manufaa yao. **{VSS 182.1}**

Ikiwa wale walio na kasoro katika namna yao ya kutamka watakubali kukosolewa na kurekebisha, wanaweza kuzishinda kasoro hizo. Wanapaswa kufanya mazoezi kwa uvumilivu ya kuzungumza kwa sauti ya chini lakini iliyo wazi, wakitumia misuli ya tumbo katika kupumua kwa kina na kulifanya koo kuwa mkondo wa kutoa sauti. Wengi huzungumza kwa haraka na kwa sauti ya juu isiyo ya kawaida. Mazoea hayo yataumiza koo na mapafu. Kwa sababu ya matumizi mabaya ya muda mrefu, viungo hivyo vilivyo dhaifu na vilivyovimba vinaweza kupata ugonjwa, na hatimaye kusababisha ugonjwa wa kifua kikuu. —**Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi, uk. 239. {VSS 182.2}**

Sauti Laini na Yenye Kushawishi—Uwe safi katika usemi wako. Jizoeshe kutumia sauti laini na yenye kushawishi, si sauti kali na ya kuamuru. Wafundishe watoto malezi ya sauti. Zoesha tabia zao za usemi mpaka maneno makali, ya mkwaruzo au yasiyo na upole yasitoke midomoni mwao kwa urahisi wanapokutana na majaribu. —**Nyumba Inayomgonjea Masihi, uk. 435. {VSS 182.3}**

Kudhibiti Nguvu ya Sauti—Wahudumu wanapaswa kuzungumza kwa heshima. Baadhi yao huharibu athari ya utulivu na uzito waliokuwa wameleta kwa watu kwa kuinua sauti zao kupita kiasi, kupiga kelele, na kupiga mayowe wanapowasilisha Ukweli. Ukweli unapowasilishwa kwa namna hii, hupoteza sehemu kubwa ya utamu/uzuri wake, nguvu yake, na uzito wake. Lakini ikiwa sauti itadhibitiwa vizuri, ikiwa itakuwa yenye heshima na kupangwa kwa namna inayogusa moyo na hisia za ndani za sikitiko, italeta athari bora zaidi. **{VSS 182.4}**

Hii ndiyo ilikuwa sauti ambayo Kristo alitumia alipowafundisha wanafunzi Wake. Aliwajaza hisia ya uzito; alizungumza kwa namna iliyogusa mioyo. Lakini kupiga kelele huku kwa sauti kubwa kunaleta nini? Hakuwapi watu mtazamo wa juu

zaidi kuhusu Ukweli wala hakuwagusi kwa kina zaidi. Kunawapa wasikilizaji hisia zisizofurahisha tu na kuchosha viungo vya sauti vya msemaji. Toni za sauti ina nafasi kubwa katika kuathiri mioyo ya wale wanaosikia. —*Shuhuda kwa Kanisa, juz. 2, uk. 615. {VSS 183.1}*

Usemi Usio na Uhai—Tumehuzunika tunapohudhuria mikutano ya makonferensi/makongamano, mikutano ya mashirika ya machapisho, na mikutano ya aina mbalimbali ambako taarifa husomwa kwa sauti isiyosikika vizuri, kwa namna ya kusitasita, au kwa sauti iliyofichika na isiyo wazi. Nusu ya mvuto wa mkutano hupotea wakati washiriki wanapotekeleza wajibu wao kwa namna ya kutojali na isiyo na ari. Wanapaswa kujifunza kuzungumza kwa namna itakayowajenga wale wanaowasikiliza. Hebu kila mtu anayehusika katika kazi ya umisionari ajipatie stahiki kwa kujitayarisha ili aweze kuzungumza kwa uwazi, kwa mvuto, na kwa kutamka kila neno kwa usahihi. —**Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi, uk. 246–247. {VSS 183.2}**

Mafunzo ya Sauti Nyumbani—Mafundisho kuhusu malezi ya sauti yanapaswa kutolewa nyumbani. Wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto wao kuzungumza kwa uwazi kiasi kwamba wasikilizaji waweze kuelewa kila neno. Wanapaswa pia kuwafundisha kusoma Biblia kwa matamshi yaliyo wazi na sahihi, kwa namna itakayomtukuza Mungu. Wale wanaopiga magoti katika madhabahu ya familia wasiinamishe nyuso zao mikononi mwao karibu na kiti wanapozungumza na Mungu; bali wainue vichwa vyao na kwa heshima takatifu wazungumze na Baba yao wa mbinguni, wakitamka maneno yao kwa sauti inayoweza kusikika. **{VSS 183.3}**

Wazazi, jifunzeni kuzungumza kwa namna itakayokuwa baraka kwa watoto wenu. Wanawake wanahitaji kuelimishwa katika jambo hili pia. Hata akina mama wenye shughuli nyingi wanaweza, ikiwa watajitahidi, kukuza kipawa chao cha usemi na kuwafundisha watoto wao kusoma na kuzungumza kwa usahihi. Wanaweza kufanya hivyo wanapoendelea na shughuli zao za kila siku. Kamwe hatujachelewa kuboresha uwezo wetu. Mungu anawaita wazazi kuleta kiwango cha

juu zaidi cha ukamilifu kinachowezezekana katika mazingira ya familia. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 6, uk. 381–382. {VSS 184.1}

Sauti Zenye Mvuto wa Muziki—Wale wanaolifungua Neno la Mungu mbele ya watu wanapaswa kuboresha namna yao ya kuwasilisha Ukweli, ili uweze kutolewa kwa ulimwengu kwa njia inayokubalika. Wanapaswa kuweka mkazo unaofaa katika maneno yanayopaswa kuvutia zaidi na kuzungumza polepole. Sauti yao inapaswa kuwa na uzuri wa kimuziki kadiri inavyowezezekana. {VSS 184.2}

Mungu anataka wahudumu Wake watafute ukamilifu ili wawe vyombo vya heshima. Wanapaswa kuongozwa na Roho Mtakatifu; na wanapozungumza, wanapaswa kuonyesha nguvu inayolingana na umuhimu wa mada wanayoiwasilisha. Wanapaswa kuonyesha kwamba nguvu wanayoihubiri imeleta mabadiliko katika maisha yao. Wanapounganishwa kwa kweli na Kristo, watatoa mwaliko wa mbinguni kwa dhati na bidii itakayogusa mioyo. Wanapoonyesha juhudi katika kutangaza ujumbe wa Injili, bidii inayolingana nayo itazalishwa ndani ya wasikilizaji, na athari za kudumu za wema zitafanyika ndani yao. —*The Review and Herald*, Januari 14, 1902. {VSS 184.3}

Kweli Kama Manna Kutoka Mbinguni—Kweli inapaswa kusemwa kwa uwazi, polepole, na kwa nguvu, ili iweze kugusa msikilizaji. Wakati Ukweli katika eneo lolote unapowasilishwa, ni muhimu kwamba ueleweke, ili chakula chake cha thamani—mkate wa uzima, mana kutoka mbinguni—kiweze kupokelewa. —*Shuhuda kwa Wachungaji na Watendakazi wa Injili*, uk. 257. {VSS 185.1}

Uharibifu wa Viungo vya Mwili—Watu wengi ambao wangeweza kuwa watenda kazi wenye manufaa wanatumia vibaya nguvu zao za uhai na kuharibu mapafu pamoja na viungo vya sauti kwa sababu ya namna yao ya kuzungumza. Baadhi ya wachungaji wamejenga tabia ya kutamka haraka haraka yale wanayotaka kusema, kana kwamba wana somo la kukariri na wanataka kulimaliza kwa kasi iwezekanavyo. Hii siyo njia bora ya kuzungumza. Kwa kutumia uangalifu unaofaa, kila mhudumu anaweza kujifunza kuzungumza kwa uwazi na kwa mvuto, badala ya kusongamanisha maneno kwa haraka bila kuchukua muda wa kupumua. Anapaswa kuzungumza kwa mwendo wa wastani ili watu waweze kuyaweka mawazo anayowasilisha katika akili zao. Lakini ujumbe unapoharakishwa kupita kiasi, watu hawawezi kuyafahamu mambo muhimu au pointi za maana, wala hawapati muda wa kupokea athari ambayo walipaswa kuipata; na Ukweli haupati nafasi ya

kuwagusa kama ambavyo ungeweza kufanya. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 2, uk. 615–616. {VSS 185.2}

Hatari ya Usemi wa Msisimko—Wakati baadhi ya watu wanapojaribu kuzungumza kwa utulivu, bila msisimko na bila kutumia ishara za mwili kupita kiasi, huhisi aibu na kukosa uhuru kwa sababu wanajizuia kufuata mazoea yao ya zamani. Lakini hebu hisia zote za namna hiyo, ambazo ni msisimko wa kibinadamu tu, zinapaswa kuachwa kabisa, zipotee na upepo. Uhuru wa hisia unaoweza kumpeleka mtu katika kujiharibu haujatakaswa. —*The Review and Herald*, Februari 5, 1880. {VSS 186.1}

Shauku Katika Uwasilishaji Si Ushahidi wa Nguvu ya Mungu—Sauti inapaswa kuratibiwa/kupaliliwa ili kuboresha ubora wake wa kimuziki, ili iweze kupendeza masikioni na kugusa moyo. {VSS 186.2}

Bwana anamtaka mtumishi Wake wa kibinadamu asiendeshwe na msukumo wa ghafla anapozungumza, bali azungumze kwa utulivu, polepole, na kumruhusu Roho Mtakatifu kuipa Kweli nguvu ya kufanya kazi. Kamwe msifikiri kwamba kwa kujichochea katika shauku kubwa ya uwasilishaji, kuzungumza kwa msukumo wa hisia usiodhibitiwa, na kuruhusu hisia zenu kuinua sauti zenu kufikia kiwango kisicho cha kawaida, mnatoa ushahidi wa nguvu kuu ya Mungu juu yenu. {VSS 186.3}

Ushawishi wenu unapaswa kufikia mbali, na uwezo wenu wa kusema unapaswa kuwa chini ya udhibiti wa akili. Mnapolazimisha viungo vya usemi, mabadiliko ya mdundo wa sauti hupotea-kuratibiwa kwa sauti kunakosekana. Tabia ya kuzungumza haraka inapaswa kushindwa kabisa. Mungu anadai kutoka kwa chombo cha kibinadamu huduma yote ambayo mwanadamu anaweza kutoa. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 668. {VSS 186.4}

Usemi Sahihi Katika Kusoma Kwa Sauti—Sayansi ya kusoma kwa usahihi na kwa kuweka mkazo unaofaa ina thamani kubwa sana. Haijalishi umejipatia maarifa kiasi gani katika maeneo mengine; ikiwa umepuuza kuipalilia na kuiratibu sauti yako na kuboresha namna yako ya kuzungumza ili uweze kusema na kusoma kwa uwazi na kwa uelewa, elimu yako yote itakuwa na manufaa madogo sana, kwa

maana bila malezi ya sauti au kuiratibu huwezi kuwasilisha kwa urahisi na kwa uwazi yale uliyojifunza. **{VSS 187.1}**

Kujifunza kueleza kwa ushawishi na kwa mvuto kile mtu anachojua ni jambo la thamani hasa kwa wale wanaotamani kuwa watenda kazi katika kazi ya Mungu. Kadiri unavyoweka msisitizo na hisia zaidi katika maneno ya kweli, ndivyo maneno hayo yatakavyokuwa na nguvu zaidi kwa wale wanaoyasikia. Uwasilishaji unaofaa wa Kweli ya Bwana unastahili juhudi zetu kubwa zaidi. Hebu, wanafunzi wanaojiandaa kwa ajili ya huduma ya Bwana wanapaswa kufanya juhudi thabiti kujifunza kuzungumza kwa usahihi na kwa nguvu, ili wanapozungumza na wengine kuhusu ile Kweli au wanaposhiriki katika huduma ya hadhara/umma, waweze kuwasilisha kwa namna inayofaa kweli zitokazo mbinguni. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 666. **{VSS 187.2}**

Uwazi Katika Kila Neno—Unapozungumza, kila neno linapaswa kutamkwa kwa ukamilifu na kwa sauti iliyojaa, na kila sentensi inapaswa kuwa wazi na yenye kueleweka hadi neno la mwisho. Wengi wanapokaribia mwisho wa sentensi hushusha sauti zao na kuzungumza kwa namna isiyoeleweka kiasi kwamba nguvu ya wazo hupotea. Maneno yanayostahili kusemwa, hakika yanastahili kusemwa kwa sauti iliyo wazi, yenye mkazo na yenye mvuto unaofaa. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 6, uk. 383. **{VSS 187.3}**

Sauti za Malaika Zikiungana na Sauti za Wanadamu—Acheni sauti za wafuasi wa Kristo zinapaswa kulelewa kiasi kwamba, badala ya kubanana maneno na kuyatamka kwa namna nzito na isiyoeleweka, matamshi yao yawe wazi, yenye nguvu, na yenye kujenga watu. Hawapaswi kuruhusu sauti ishuke baada ya kila neno, bali wanapaswa kuiendeleza kwa namna itakayofanya kila sentensi iwe kamili na yenye maana. Je, haitastahili kujitia katika nidhamu ikiwa kwa kufanya hivyo wataweza kuongeza mvuto katika huduma ya Mungu na kuwajenga na kuwaboresha watoto Wake? Sauti za shukrani, sifa, na furaha zinasikika mbinguni. Sauti za malaika wa mbinguni huungana na sauti za watoto wa Mungu duniani

wanapomtolea Mungu na Mwana-Kondoo heshima, utukufu, na sifa kwa ajili ya wokovu mkuu uliotolewa. —**Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi, uk.**

246. {VSS 188.1}

Ishara Zisizofaa na Usemi Usiofaa au Matusi na Maneno Machafu—Mtenda kazi wa Mungu anapaswa kufanya juhudi ya dhati ili awe mwakilishi wa Kristo, akiondoa ishara zote zisizofaa na usemi usio na ustaarabu au mchafu. Anapaswa kujitahidi kutumia lugha sahihi. Kuna kundi kubwa la watu ambao hawazingatii namna wanavyozungumza, lakini kwa uangalifu wa kudumu na juhudi ya makusudi, watu hawa wanaweza kuwa wawakilishi wa Kweli. Kila siku wanapaswa kufanya maendeleo. Hawapaswi kupunguza manufaa yao wala ushawishi wao kwa kushikilia kasoro katika mwenendo, sauti, au matumizi ya lugha. Maneno ya kawaida yasiyo na thamani, na ya hovyoyavyo yanapaswa kubadilishwa na maneno yenye uzito, safi, na yenye maana. Kwa uangalifu wa kudumu na nidhamu ya dhati, vijana Wakristo wanaweza kuilinda ndimi zao dhidi ya uovu na midomo yao dhidi ya kusema hila [uncooth talks or expression kwenye jamii yetu inaweza kuwa ni kukonyeza, kucheza dansi,. {VSS 188.2}

Tunapaswa kuwa waangalifu tusitamke maneno yetu kwa namna isiyo sahihi.

Miongoni mwetu kuna watu ambao, kwa nadharia, wanajua kwamba matumizi mabaya ya lugha si jambo linalofaa; lakini katika vitendo bado hufanya makosa

hayo mara kwa mara. —**Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi, uk. 238.**

{VSS 189.1}

Msaada wa Roho Katika Kuzungumza kwa Uwazi—Mwalimu wa Kweli anapaswa kuzingatia kwa makini namna anavyowasilisha Ukweli. Anapaswa kutamka kila neno kwa uwazi na kwa usahihi, akiwa na usadikisho wa dhati unaoweza kugusa mioyo ya watu. {VSS 189.2}

Ikiwa maneno yanabanwa na kutamkwa kwa haraka haraka, mvuto unaopaswa kupatikana hupotea. Kipawa cha usemi kinahitaji kulelewa/kupaliliwa ili ukweli usemwe si kwa msisimko usiodhibitiwa, bali kwa utulivu na uwazi, ili hata silabi moja isipotee. Kasi ya kuzungumza inaweza na inapaswa kurekebisha. Ikiwa maneno ya Kweli yana umuhimu wa kutosha kusemwa mbele ya wasikilizaji, basi

yana umuhimu wa kutosha kusemwa kwa uwazi. Uongozi wa Roho hauwezi kamwe kumwongoza mtu katika usemi usioeleweka. Roho huchukua mambo ya Mungu na kuyawasilisha kupitia chombo cha kibinadamu kwa watu. Kwa hiyo, maneno hayo yanapaswa kutoka midomoni mwetu kwa namna bora na kamilifu iwezekanavyo. — ***Kazi ya Kusini- Miongoni mwa Watu Weusi Watumwa, Oktoba 27, 1903. {VSS 189.3}***

Maneno Yetu Ni Njia ya Kuwasilisha Ukweli—Tunapaswa kupata elimu inayohitajika katika eneo la mawasiliano, ili tujue jinsi ya kutumia maneno yanayofaa na toni inayostahili, ili maneno yetu yawe nguvu ya kuleta mema. Ukweli hauwi kweli kwetu isipokuwa umefikia sehemu za ndani kabisa za nafsi zetu. Hilo linapotokea, maneno yetu huwa ni mikondo ambayo kupitia kwayo Ukweli huwasilishwa kwa wengine. Panda mbegu kando ya maji yote, bila kujua ni ipi itakayostawi, iwe hii au ile. Lakini endelea kujielimisha daima katika namna ya kutumia kwa usahihi kipawa cha usemi. Unapozungumza na wengine, inua moyo wako kwa Mungu, ukimwomba aandae mioyo yao kupokea mbegu ya mbinguni. Hakuna mwanaume wala mwanamke anayeweza kuwa kile anachopaswa kuwa kama mtenda kazi pamoja na Mungu katika kueneza mbegu ya kweli bila kufanya juhudi ya dhati na ya uangalifu katika kuratibu/malezi ya sauti na matumizi sahihi ya maneno. —***Manuscript 74, 1897. {VSS 189.4}***

SURA YA 36—UMUHIMU WA AFYA YA JUMLA

Ili tuwe na damu yenye afya, tunapaswa kupumua vizuri. Kuvuta pumzi kwa kina na kwa ukamilifu kwa hewa safi, ambayo hujaza mapafu kwa oksijeni, na huisafisha damu. Hufanya damu iwe na rangi ang’avu na kuipeleka kama mkondo wenye kuleta uhai katika kila sehemu ya mwili. Kupumua vizuri hutuliza mishipa ya fahamu, huchochea hamu ya kula, huboresha mmeng’enywa wa chakula, na huleta usingizi mzuri wenye kuburudisha. **{VSS 191.1}**

Mapafu yanapaswa kupewa nafasi kubwa iwezekanavyo ili yafanye kazi kwa uhuru. Uwezo wake huongezeka yanapofanya kazi bila kizuizi; lakini hupungua yanapobanwa au kukandamizwa. Hivyo ndivyo madhara yanavyotokea kutokana na tabia iliyozoeleka sana, hasa miongoni mwa watu wanaofanya kazi za kukaa muda mrefu, ya kuinama wanapofanya kazi. Katika hali hii haiwezekani kuvuta pumzi kwa kina. Hatimaye, kupumua kwa juu juu huwa mazoea, na mapafu hupoteza uwezo wake wa kujitanua. Athari kama hiyo pia husababishwa na mwili kubanwa kwa mavazi yanayobana sana. Nafasi ya kutosha haitolewi katika sehemu ya chini ya kifua; misuli ya tumbo, ambayo iliundwa kusaidia katika kupumua, haipati nafasi ya kufanya kazi kikamilifu, na mapafu huzuiwa katika utendaji wake. **{VSS 191.2}**

Kwa hiyo, mwili hupokea kiasi kisichotosha cha oksijeni. Damu huzunguka kwa udhaifu. Uchafu na sumu zinazopaswa kutolewa nje kupitia hewa inayotolewa na mapafu hubaki ndani ya mwili, na damu huwa chafu. Si mapafu pekee yanayoathirika, bali pia tumbo, ini, na ubongo. Ngozi huwa na rangi iliyofifia, mmeng'enywa wa chakula hupungua, moyo hudhoofika, ubongo huwa mzito, mawazo huchanganyikiwa, huzuni huingia moyoni, na mfumo mzima wa mwili huwa dhaifu na usiotenda vizuri. Hali hiyo huufanya mwili uwe katika hatari zaidi ya kushambuliwa na magonjwa. —*Huduma ya Uponyaji*, uk. 272–273. **{VSS 192.1}**

Kuwa na Ugavi Endelevu wa hewa mpya: Mapafu huendelea daima kutoa uchafu kutoka mwilini, hivyo yanahitaji kupewa hewa safi kila wakati. Hewa chafu haitoi kiasi kinachohitajika cha oksijeni, na damu huenda kwenye ubongo na viungo vingine bila kupata nguvu na uhai unaotokana na oksijeni ya kutosha. Kwa hiyo, kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na uingizaji hewa mzuri. Kuishi katika vyumba vilivyofungwa na visivyo na hewa ya kutosha, ambavyo hewa yake imetulia na imechafuliwa, hudhoofisha mfumo mzima wa mwili. Mwili huwa dhaifu na kuathirika kwa urahisi na baridi, kiasi kwamba hata kukutana kidogo na mazingira ya baridi kunaweza kusababisha ugonjwa. —*The Huduma ya Uponyaji*, uk. 274. **{VSS 192.2}**

Oksijeni Kwenye Mapafu: Ni jambo la muhimu kwa afya kwamba kifua kiwe na nafasi ya kutosha kujitanua kwa kiwango chake kamili, ili mapafu yaweze kuvuta pumzi kikamilifu. Mapafu yanapobanwa, kiasi cha oksijeni kinachoingia ndani yake hupungua. Damu haipati uhai unaostahili, na uchafu pamoja na sumu

zinazopaswa kutolewa nje kupitia mapafu hubaki mwilini. Zaidi ya hayo, mzunguko wa damu huzuiwa, na viungo vya ndani hubanwa na kusongamana kiasi kwamba haviwezi kufanya kazi zake kwa usahihi. —*Huduma ya Uponyaji*, uk. 292. {VSS 192.3}

Mafunzo ya Sauti ni Sehemu ya Kuratibu Mwili au Elimu ya Mwili wa Binadamu: Baada ya kuwa na mkao sahihi wa mwili, jambo la muhimu linalofuata ni kupumua na malezi ya sauti. Mtu anayekaa na kusimama wima ana uwezekano mkubwa zaidi wa kupumua kwa usahihi kuliko wengine. Lakini mwalimu anapaswa kuwafundisha wanafunzi wake umuhimu wa kupumua kwa kina. Anapaswa kuwaonyesha jinsi utendaji mzuri wa viungo vya kupumua unavyosaidia mzunguko wa damu, kuimarisha mwili mzima, kuchochea hamu ya kula, kuboresha mmeng'enywa wa chakula, na kuleta usingizi mzuri wenye kuburudisha. Kwa njia hiyo, kupumua vizuri hakuburudishi mwili pekee, bali pia hutuliza na kuipa akili hali ya amani. Wakati umuhimu wa kupumua kwa kina unapofundishwa, zoezi hilo linapaswa kuisitizwa na kufanywa kwa vitendo. Mazoezi yanayosaidia jambo hili yanapaswa kutolewa mpaka tabia hiyo ijengeke. {VSS 193.1}

Angalia mada kama Deep breathing videos

https://youtu.be/acUZdGd_3Dg?si=QENa_VGjLiEBm4pD

Mafunzo ya sauti yana nafasi muhimu katika malezi ya mwili, kwa sababu husaidia kupanua na kuimarisha mapafu, na hivyo kusaidia kuzuia magonjwa. Ili kuhakikisha usomaji na usemi wenye usahihi, hakikisha kwamba misuli ya tumbo inafanya kazi kikamilifu wakati wa kupumua, na kwamba viungo vya kupumua havizuiwi. Nguvu ya kupumua itokane zaidi na misuli ya tumbo kuliko misuli ya koo. Kwa njia hii, uchovu mkubwa na magonjwa makubwa ya koo na mapafu yanaweza kuzuiwa. Uangalifu mkubwa unapaswa kutolewa katika kuhakikisha matamshi yaliyo wazi, sauti laini yenye mabadiliko mazuri ya mdundo, na kasi ya kuzungumza isiyozidi kiasi. Hili halitasaidia afya tu, bali pia litaongeza kwa kiwango kikubwa uzuri na ufanisi wa kazi ya mwanafunzi. —*Elimu*, uk. 198–199. {VSS 193.2}

SURA YA 37—MATUMIZI SAHIHI YA SAUTI

Kanuni za Afya—Matumizi sahihi ya viungo vya sauti huleta manufaa kwa afya ya mwili na huongeza manufaa pamoja na ushawishi wa wafuasi wa Kristo. Ni kwa kuingia katika mazoea mabaya ya kuzungumza ndipo watu huwa wasomaji na wasemaji wanaochosha na kuchoka wenyewe au hata wanaoboa [monotonous]. Lakini wale wanaonekana kuwa na akili ya kutosha kuwa watenda kazi wa umisionari au kushughulikia shughuli za kibiashara wanapaswa pia kuwa na uelewa wa kutosha wa kurekebisha namna yao ya kuzungumza. Kwa kufanya mazoezi yanayofaa na yenye busara, wanaweza kupanua kifua na kuimarisha misuli yao. Kwa kuzingatia maelekezo sahihi na kufuata kanuni za afya kuhusu upanuzi wa mapafu na malezi ya sauti, vijana wa kiume na wa kike wanaweza kuwa wasemaji wenye sauti inayosikika vizuri. Mazoezi yanayohitajika ili kufikia uwezo huu pia yataongeza muda wa maisha yao. —*Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi*, uk. 247. {VSS 195.1}

Kupumua kwa Kina—Ikiwa wale walio na kasoro katika namna yao ya kutamka watakubali kukosolewa na kurekebisha, wanaweza kushinda kasoro hizo. Wanapaswa kufanya mazoezi kwa uvumilivu ya kuzungumza kwa sauti ya chini lakini iliyo wazi, wakiipa misuli ya tumbo mazoezi katika kupumua kwa kina na kulifanya koo kuwa njia ya kupitisha sauti. Wengi huzungumza kwa haraka na kwa sauti ya juu isiyo ya kawaida. Mazoea hayo huumiza koo na mapafu. Kwa sababu ya matumizi mabaya ya muda mrefu, viungo hivyo vilivyo dhaifu na vilivyovimba vinaweza kupata ugonjwa, na hatimaye kusababisha kifua kikuu. —*Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi*, uk. 239. {VSS 195.2}

Matumizi Sahihi ya Misuli ya Tumbo—Malezi ya sauti ni jambo linalohusiana kwa karibu na afya ya wanafunzi. Vijana wanapaswa kufundishwa namna ya kupumua kwa usahihi na namna ya kusoma ili mkazo usio wa kawaida usiwe katika koo na mapafu, bali kazi ya kutoa sauti ibebwe na misuli ya tumbo. Kuzungumza

kwa kutumia koo, yaani kuruhusu sauti itoke katika sehemu ya juu ya viungo vya sauti, hudhoofisha afya ya viungo hivyo na kupunguza uwezo wake wa kufanya kazi. Misuli ya tumbo inapaswa kufanya sehemu kubwa ya kazi, huku koo likitumika kama njia ya kupitisha sauti. Watu wengi wamepoteza maisha ambao wangeweza kuishi ikiwa wangepfundishwa namna ya kutumia sauti zao kwa usahihi. Matumizi sahihi ya misuli ya tumbo katika kusoma na kuzungumza yatakuwa msaada mkubwa katika matatizo mengi ya sauti na kifua, na yatasaidia kurefusha maisha. —*Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi*, uk. 297. {VSSsw 196.1}

Kuhifadhi Nguvu Katika Maombi—Niliona kwamba baadhi ya wachungaji wetu hawaelewi namna ya kuhifadhi nguvu zao ili waweze kufanya kazi nyingi zaidi bila kuchoka. Wahudumu hawapaswi kuomba kwa sauti kubwa na kwa muda mrefu kiasi cha kumaliza nguvu zao na kujichakaza. Si lazima kuchosha koo na mapafu katika maombi. Sikio la Mungu daima liko wazi kusikia maombi ya moyoni ya watumishi Wake wanyenyekevu, na Yeye hahitaji wachoshe viungo vyao vya sauti wanapozungumza Naye. Kinachompendeza Mungu ni tumaini kamili kwa Bwana, utegemezi thabiti, kudai kwa uthabiti ahadi Zake, na imani rahisi kwamba Yeye Yupo na kwamba huwapa thawabu wale wanaomtafuta kwa bidii. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 1, uk. 645. {VSSsw 196.2}

Ushawishi wa Mafundisho Sahihi—Taasisi zetu za elimu zinapaswa kuwa na vifaa na miundombinu yote inayohitajika kwa ajili ya kufundisha kuhusu muundo na utendaji wa mwili wa mwanadamu. Wanafunzi wanapaswa kufundishwa namna ya kupumua, namna ya kusoma, na namna ya kuzungumza ili mkazo usiwe katika koo na mapafu, bali katika misuli ya tumbo. Walimu wanahitaji kujielimisha katika eneo hili. Wanafunzi wetu wanapaswa kupata mafunzo kamili, ili waweze kuingia katika maisha ya utendaji wakiwa na ujuzi sahihi kuhusu mwili ambao Mungu amewapa kuwa makao yao. Wafundisheni watu kwamba wanapaswa kuendelea kuwa wanafunzi maisha yao yote. Na wakati mnawafundisha, kumbukeni kwamba wao pia watawafundisha wengine. Somo lenu litarudiwa kwa manufaa ya wengi

zaidi kuliko wale wanaokaa mbele yenu kila siku. —*Misingi ya Elimu kwa Kila Mwanadamu*, uk. 147–148. {VSSsw 197.1}

Matumizi ya Kupita Kiasi ya Viungo vya Sauti—Matumizi ya muda mrefu na yenye nguvu kupita kiasi ya viungo vya sauti yameleta madhara ya kukera katika koo na mapafu yake (Ndugu D), na yameharibu afya yake kwa ujumla zaidi kuliko ambavyo kanuni zake maalumu za kula na kupumzika zimemsaidia. Matumizi ya nguvu kupita kiasi au mkazo mkubwa katika viungo vya sauti, hata kama yatatokea mara moja tu, yanaweza yasipone haraka na yanaweza hata kugharimu maisha ya msemaji. Namna ya kuzungumza kwa utulivu, kwa dhati na bila haraka, lakini kwa bidii na uzito, huwa na ushawishi mkubwa zaidi kwa kusanyiko kuliko kuruhusu hisia kuchocheka na kutawala sauti pamoja na mwenendo wa msemaji. Kadiri inavyowezekana, msemaji anapaswa kudumisha sauti yake ya asili. Ni Ukweli unaowasilishwa ndio unaogusa moyo. Ikiwa msemaji ataifanya Kweli hiyo kuwa halisi katika maisha yake, kwa msaada wa Roho wa Mungu ataweza kuwagusa wasikilizaji na kuwathibitishia kwamba anazungumza kwa moyo wa dhati, bila kuvilazimisha na kuvikera viungo dhaifu vya koo wala mapafu. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 2, uk. 672. {VSSsw 197.2}

Njia ya Kupitisha Sauti—Ndugu A, upendo wako wa kusoma na kutopenda kwako kutumia nguvu za mwili unapozungumza na kutumia koo lako, vinakuweka katika hatari ya kupata magonjwa ya koo na mapafu. Unapaswa kuwa mwangalifu na usizungumze kwa haraka, ukimwaga maneno yako kana kwamba unasoma somo la kukariri. Haupaswi kuruhusu kazi yote ya kutoa sauti ifanywe na sehemu ya juu ya viungo vya sauti, kwa sababu kufanya hivyo kutavichosha na kuvikera daima, na hatimaye kuweka msingi wa ugonjwa. Nguvu ya kutoa sauti inapaswa kutoka katika misuli ya tumbo. Mapafu na koo yanapaswa kuwa njia ya kupitisha sauti, lakini havipaswi kubeba kazi yote. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 3, uk. 311. {VSSsw 198.1}

Mazoezi Baada ya Kula—Kuna wanaume na wanawake wenye uwezo mkubwa wa asili ambao hawatimizi hata nusu ya kile wanachoweza kutimiza kwa sababu hawajifunzi kujizuia, kujikana nafsi katika kuridhisha hamu ya kula. {VSSsw 198.2}

Waandishi wengi na wasemaji wengi hukosea katika jambo hili. Baada ya kula chakula kingi, hujishughulisha na kazi za kukaa kwenye kiti bila kufanya mazoezi

ya mwili; husoma, hujifunza, au huandika. Matokeo yake ni kwamba mtiririko huru wa mawazo na maneno huzuiwa. Hawawezi kuandika wala kuzungumza kwa nguvu na msukumo unaohitajika ili kufikia mioyo ya watu; juhudi zao huwa dhaifu na zisizo na matokeo-matunda. —*Huduma ya Uponyaji*, uk. 308–309. {VSS 198.3}

Msaada kwa Wagonjwa—Mipango inapaswa kufanywa ili kuwasaidia wagonjwa kutumia muda wao wakiwa nje katika hewa ya wazi. Kwa wale wanaoweza kufanya kazi za mikono, wapewe shughuli rahisi na zenye kupendeza. Waonyeshwe jinsi kazi za nje zinavyoweza kuwa za kufurahisha na zenye manufaa. Wahimizwe kuvuta hewa safi. Wafundishwe kupumua kwa kina na, wanapopumua na kuzungumza, watumie misuli ya tumbo. —*Huduma ya Uponyaji*, uk. 264–265. {VSS 199.1}

Kuzungumza kwa Usahihi Ni Zoezi Lenye Afya—Kutumia sauti katika kuzungumza ni zoezi lenye afya. Fundisheni na kuishi kwa uangalifu. Shikeni kwa uthabiti kanuni kwamba wote, hata viongozi wetu wakuu, wanahitaji kuzoesha akili ya kawaida katika kutunza afya zao, kuhakikisha kwamba mwili na akili vinapata mazoezi yenye uwiano unaofaa. —*Huduma ya Tiba*, uk. 264–265. {VSS 199.2}

Matumizi Sahihi ya Viungo vya Sauti—Uangalifu mkubwa na mafunzo maalumu yanapaswa kutolewa kwa viungo vya sauti. Viungo hivyo huimarishwa vinapotumiwa kwa usahihi, lakini hudhoofika vinapotumiwa vibaya. Matumizi yake kupita kiasi, kama vile kuhubiri mahubiri marefu mara kwa mara, si tu kwamba huumiza viungo vya usemi, bali pia huleta mkazo usiofaa katika mfumo mzima wa mishipa ya fahamu. Kinubi maridadi na nyeti, chenye nyuzi elfu moja huchakaa, huharibika, na badala ya kutoa sauti nzuri huanza kutoa mlio usio na mpangilio. {VSS 199.3}

Ni jambo la muhimu kwa kila msemaji kuyazoeza viungo vya sauti kwa namna itakayoviweka katika hali nzuri ya afya, ili aweze kuwatangazia watu Maneno ya uzima. Kila mtu anapaswa kupata uelewa mahiri kuhusu namna bora zaidi ya kutumia uwezo aliopewa na Mungu, na kisha kufanya mazoezi kulingana na kile alichojifunza. Si lazima kuzungumza kwa sauti kubwa au ya juu au kwa mlio wa juu sana, kwa maana kufanya hivyo humdhuru sana msemaji. Badala yake kuzungumza kwa haraka huharibu sehemu kubwa ya nguvu ya hotuba, kwa sababu maneno hayawezi kutamkwa kwa uwazi na usahihi kama yanavyoweza kutamkwa

ikiwa yatasemwa kwa utulivu, na kumpa msikilizaji muda wa kuelewa maana ya kila neno. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 667. {VSS 200.1}

Kulinda Maisha—Msemaji anapozungumza kwa njia sahihi, akivuta pumzi ndefu na kamili, na kutoa sauti kwa namna iliyo wazi na inayoeleweka, mwili wake wote hupata manufaa. Matumizi ya mapafu yangu katika kupumua kwa kina nilipokuwa nikihubiri mbele ya watu yamekuwa njia ya kunihifadhi hai. {VSS 200.2}

Uangalifu unapaswa kuchukuliwa daima ili kutovitia mkazo viungo vya sauti. Vinapaswa kuwekwa katika hali nzuri na laini kadiri iwezekanavyo. Unapozungumza mbele ya kusanyiko, acha misuli ya tumbo ibebe sehemu kubwa zaidi ya kazi. Ujumbe au nuru niliyopewa kwa ajili yako ni kwamba unapaswa kufanya zaidi kazi ya kuzungumza hadharani, na unapozungumza hakikisha unatumia misuli ya tumbo. Ubongo wako umechoka kwa kutumiwa kwa kupitiliza - matumizi makubwa. Zingatia mambo ninayokuandikia, nawe utaona kwamba maneno yangu ni ya kweli. Unapojihusisha na kazi ambayo Bwana amekuonyesha, Roho wa Mungu atagusa akili za watu kupitia maneno utakayosema. Neno linalosemwa kwa kinywa litafanya mvuto mkubwa zaidi mioyoni kuliko Neno lililoandikwa. —*Letter 92, 1910*. {VSS 200.3}

Malezi Sahihi ya Sauti Si Jambo la Kupuuzwa—Mwanadamu anapaswa kujitawala na kujisimamia mwenyewe. Mungu amempa uwezo wa kimwili na wa kiroho, na uwezo huo unapaswa kuelewa na kuboreshwa daima. Kwa kiwango kikubwa, uchovu wa mwili unaweza kuepukwa kwa kuzungumza polepole, kwa utulivu, na bila msisimko. {VSS 201.1}

Katika kuzungumza, watu wengi wamekuwa wakiweka mzigo wa kudumu juu ya viungo vyao vya sauti. Mapafu yao yameathirika, na kifo cha mapema kimekatiza kazi yao. Mwili hauwezi kuvumilia daima matumizi mabaya yanayokiuka kanuni zake. Watu wengi huzipuuza kanuni hizo, lakini hatimaye mwili hutoa onyo lake na kumwadhibu anayezivunja sheria hizo. Ikiwa watenda kazi hawa wangejifunza kwamba Mungu hahitaji wajichoshe kwa mkazo huu wa kupita kiasi, na kwamba kwa kuvitia mkazo viungo vya thamani vya mwili na kufupisha muda wa manufaa yao wanamvunjia heshima Mungu, wasingejenga mazoea yanayodhuru afya yao. {VSS 201.2}

Kisingizio kinachotolewa ni: *“Hii ndiyo tabia yangu; hivi ndivyo nilivyo, na siwezi kuishinda.”* Je, ndugu zangu watazingatia namna wanavyovitumia viungo vyao vya usemi katika huduma ya Neno? Wanapaswa kufuata njia ya Mungu, wala si mapenzi yao wenyewe. Kristo hakuonyesha mfano wa namna hiyo katika mafundisho Yake. Wafuasi Wake wanapaswa kufanya juhudi kubwa kushinda mazoea yao ya kuzungumza kwa muda mrefu na kwa sauti kubwa au ya juu. Mazoea hayo hugaribu sana uzuri na mvuto wa sauti ya mwanadamu. **{VSS 201.3}**

Mungu anakusudia kwamba wale wanaohudumu katika Neno na mafundisho wawe wafundishaji/walimu wanaoonyesha namna sahihi ya kufundisha. Wanapaswa kusimama mbele ya watu kama wawakilishi wa Mungu, wakionyesha kwamba wanathamini vipawa vya thamani walivyopewa na Mungu. Wanapaswa kutumia viungo vyao vya sauti, lakini wasivinyanyase vibaya. Hawapaswi kutoa kisingizio kisicho na msingi na cha kipumbavu: *“Hii ndiyo tabia yangu; siwezi kuondoa kasoro hizi.”* Hawapaswi kuendelea kutumia vibaya uwezo waliopewa na Mungu kwa ajili ya kuukuza kwa kiwango cha juu, wala kuruhusu mazoea yao yasiyo kamili na kisha yapunguze mema ambayo wangeweza kuyafanya. Bwana atawasaidia wote watakaozimia kushinda tabia hizi zisizofaa wanapowasilisha ujumbe Wake kwa ulimwengu. **{VSS 202.1}**

Jambo hili limechukuliwa kwa muda mrefu kana kwamba ni hekaya isiyo na maana na haina utafiti wa kuiunga mkono. Lakini ni jambo zito sana, na linapaswa kuongeza hisia ya wajibu kwa kila mtu anayekuwa msemaji wa Mungu [mdomo wa Mungu, anayewasilisha kwa watu neno la uzima. Wahudumu wa Mungu wanapaswa kujifunza ili wajionyeshe kuwa wamekubaliwa na Mungu katika kuwasilisha Kweli takatifu; wawe watenda kazi wasio na sababu ya kuona aibu. **{VSS 202.2}**

Kweli inayozungumzwa, iwe imesemwa kwa namna inayopendeza au isiyopendeza, itamhukumu msikilizaji katika siku kuu ya hesabu ya mwisho. Itakuwa harufu ya uzima iletayo uzima au harufu ya mauti iletayo mauti. Katika hali yoyote ile, msemaji atakosolewa na wale wanaogeza masikio yao wasisikie Kweli; lakini kila juhudi inapaswa kufanywa ili kuwafikia watu. Mchungaji ni mwalimu wa kweli takatifu na yenye uzito. Kwa hiyo, anapaswa kutafuta ukamilifu katika tabia na katika namna yake ya kuwasilisha ujumbe, ili kutoa nafasi ndogo iwezekanavyo kwa lawama. Mwanadamu anaheshimiwa kwa kuitwa mtenda-kazi pamoja na Mungu. Kwa hiyo, anapaswa kufanya kazi kulingana na mfano wa Kristo, akiipokea

Kweli katika usafi wake kutoka katika Neno la Mungu na kuiwasilisha kwa namna itakayomvutia msikilizaji na kuifanya ipokelewe kwa moyo. —*Manuscript 4, 1897.*
{VSS 202.3}

SEHEMU YA 5—MBINU BORA ZA HOTUBA ZA HADHARANI

SURA YA 38—UPENDO NA WEMA

Ufasaha wa Upendo wa Mungu—Ufasaha wenye ushawishi mkuu zaidi ni neno linalonewa kwa upendo na huruma. Maneno kama hayo yataleta nuru kwa akili zilizochanganyikiwa na tumaini kwa waliokata tamaa, yakiangaza matarajio yao ya wakati ujao. Wakati tunaoishi unahitaji nguvu hai zilizotakaswa; unahitaji bidii, unyofu/udhati, juhudi, na huruma pamoja na upendo wa hali ya juu kabisa; unahitaji maneno ambayo hayataongeza huzuni, bali yatakayochochea imani na tumaini. Tunasafiri kuelekea nyumbani mbinguni, tukitafuta nchi iliyo bora zaidi, yaani, nchi ya mbinguni. Badala ya kusema maneno yatakayochoma mioyo ya wanaotusikia, je, hatupaswi kusema juu ya upendo ambao Mungu ametupenda nao? Je, hatupaswi kujitahidi kuifariji mioyo ya wale wanaotuzunguka kwa maneno ya huruma ya Kikristo? Je, hatupaswi kuwaambia kuhusu pumziko lililowekwa akiba kwa ajili ya watu wa Mungu? “*Neno linenwalo kwa wakati ufao ni kama tufaha za*

dhahabu katika vyombo vya fedha.”—*The Review and Herald*, Februari 16, 1897. {VSS 207.1}

Vizuizi vya Kiburi na Ubinafsi—Roho wa Yesu anapaswa kuijaza nafsi ya mtendakazi; ni maneno ya upole na ya huruma, pamoja na udhihirisho wa upendo usio na ubinafsi kwa nafsi zao, yatakayobomoa vizuizi vya kiburi na ubinafsi, na kuwaonyesha wasioamini kwamba tunao upendo wa Kristo. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 636. {VSS 207.2}

Mwangaza na Hekima Vitokavyo kwa Mungu—Wale wanaofanya kazi katika neno na mafundisho wana kazi kubwa mbele yao ya kung'oa kutoka katika akili za wale wanaowahudumia udanganyifu wa mauti wa Shetani, na kuwafanya watambue umuhimu wa kujitahidi kuufikia kiwango cha juu cha Mungu cha haki. Wanapaswa kuomba kwa dhiti ili wapate mwangaza wa Mungu na hekima ya kuuwasilisha Ukweli kama ulivyo katika Yesu. Huruma, upole, na upendo, vikifumwa katika mahubiri yao na kudhihirishwa katika maisha yao, vitapokonya nguvu ya upinzani, vitadhoofisha chuki, na kufungua njia ya kuifikia mioyo mingi. —*Historical Sketches of the Foreign Missions of the Seventh-day Adventists*, uk. 121. {VSS 208.1}

Kumwiga Kristo Katika Kazi Zake—Inasikitisha kwamba wengi hawatambui kuwa namna ambayo Ukweli wa Biblia unavyowasilishwa ina athari kubwa katika hisia zinazojengeka katika akili za watu, na katika tabia ya Kikristo inayokuja kukuzwa baadaye na wale wanaoupokea Ukweli. Badala ya kumwiga Kristo katika namna Yake ya kufanya kazi, wengi ni wakali, wakosoaji, na wenye kutawala kwa mabavu. Wanawafukuza watu badala ya kuwavuta kwa Kristo. Watu wa namna hiyo hawatajua kamwe ni watu wangapi walio dhaifu ambao wamejeruhiwa na kukatishwa tamaa kwa sababu ya maneno yao makali. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 168. {VSSsw 208.2}

Mahubiri Mengi Kupita Kiasi—Mahubiri yanapaswa kutoka, si katika moyo wa kimazoea, bali katika moyo uliojaa upendo wa Mungu, uliotiishwa na kulainishwa kwa neema Yake; ili unapozungumza, malaika wa Mungu washirikiane nawe, na Kristo awe upande wako, naye Kristo Ndiye anayefanya ujumbe uguse mioyo ya watu. Hata hivyo, mambo haya yamepuuzwa katika makambi yetu ya

mikutano. Tumepoteza thuluthi mbili ya yote ambayo makambi hayo yalikusudiwa kutimiza. Inaonekana kwamba wazo limejikita katika akili za baadhi ya watu kwamba kazi yao ni kuhubiri tu, kuhubiri tu. Ingawa mahubiri yana nafasi yake, mahubiri yanatolewa mfululizo kwa watu kiasi kwamba hawawezi kuyahifadhi akilini mwao—haiwezekani kufanya hivyo—na hatimaye wanachoshwa na mahubiri hayo. —*Manuscript 19b*, 1890. {VSSsw 208.3}

Wachungaji Waliovaa Viatu vya Injili—Kila mhudumu ajifunze kuvaa viatu vya injili Efeso 6. Yeye aliyevaa maandalio ya Injili ya amani atatembea kama Kristo alivyotembea. Ataweza kunena maneno yafaayo, na kuyasema kwa upendo. Hatajaribu kulazimisha ujumbe wa Mungu wa Kweli kwa ukali. Ataitendea kila moyo kwa upole, kujali, na upendo, akitambua kwamba Roho Mtakatifu ndiye atakayefanya ukweli uguse wale walio tayari kupokea mivuto ya Roho wa Mungu. Kamwe hatakuwa mkali katika mwenendo wake. Kila neno atakalolisema litakuwa na mvuto wa kulainisha na kunyenyekeza mioyo.... {VSSsw 209.1}

Tunaponena maneno ya karipio, na tuweke ndani ya sauti yetu upole na upendo wote unaofanana na wa Kristo unaowezekana. Kadiri nafasi ya mhudumu ilivyo ya juu, ndivyo anavyopaswa kuwa mwangalifu zaidi katika maneno na matendo yake.—*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 174. {VSSsw 209.2}

Mguso wa Kudumu Kupitia Upendo—Katika majaliwa Yake, Mungu huwavuta watu kuhudhuria mikutano yetu ya hema na ibada za kanisani. Wengine huja kwa sababu ya udadisi, wengine ili kukosoa au kudhihaki. Mara nyingi hushawishika kuhusu dhambi zao. Neno linalonenwa katika roho ya upendo, huacha mguso wa kudumu ndani yao. Basi, mikutano hii inapaswa kuendeshwa kwa uangalifu mkubwa kiasi gani! Maneno yanayonenwa yanapaswa kuwa na mamlaka, ili Roho Mtakatifu ayatie katika akili za wasikilizaji. Mnenaji anayetawaliwa na Roho wa Mungu huwa na hadhi takatifu, na maneno yake huwa harufu ya uzima iletayo uzima. Hebu vielelezo au visa visivyofaa visiingizwe katika hotuba. Hebu Maneno yote yanayonenwa yawe kwa ajili ya kuwajenga wanaosikia. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 207–208. {VSSsw 209.3}

Ukweli Ndio Ukate, Si Maneno Yetu—Katika kuuwasilisha ukweli usiopendwa na wengi, unaohusisha kubeba msalaba mzito, wahubiri wanapaswa kuwa waangalifu kwamba kila neno liwe kama Mungu anavyotaka liwe. Maneno yao yasikate kamwe. Wanapaswa kuuwasilisha Ukweli kwa unyenyekevu, kwa upendo wa ndani kabisa kwa ajili ya roho za watu, na kwa shauku ya dhati ya kuwaona wakipata wokovu; kisha wauache Ukweli wenyewe ukate. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 3, uk. 218. {VSS 210.1}

Matengenezo, Si Kuchochea Uchungu—Mungu anawaita wahamasishaji wa matengenezo watakaonena maneno yenye nguvu na yenye kuinua kutoka mimbarini mwetu. Wakati watu wanaponena maneno yao wenyewe kwa nguvu zao wenyewe, badala ya kuhubiri Neno la Mungu katika uweza wa Roho Mtakatifu, huumia na kukasirika wanapooni maneno yao hayapokelewi kwa shauku. Ndipo wanapojaribiwa kusema maneno yatakayochochea roho ya uchungu na upinzani miongoni mwa wanaowasiliza. Ndugu zangu, pokeeni ushauri. Maneno ya namna hiyo hayapaswi kutoka katika midomo ya mabalozi wa Kristo. Midomo iliyotakaswa itanena maneno yanayoleta matengenezo, wala si yanayochochea uchungu. Ukweli unapaswa kuwasilishwa kwa upole na upendo wa Kristo. —*Jumbe Teule*, kit. 1, uk. 159. {VSS 210.2}

Kutoka Katika Mioyo Iliyovunjika/iliyopondeka na Yenye Toba—Ndugu zangu, mioyo yenu ivunjike na kuwa na toba ya kweli. Maneno ya huruma na upendo, yasiyochoma ulimi, na yatiririke kutoka katika midomo yenu. —*The S.D.A. Bible Commentary*, Vol. 3, uk. 1164. {VSS 211.1}

Ucha Mungu Katika Kuhubiri-Ukiroho—Mahubiri ya Ndugu B hayakuwa na uthibitisho wa Roho wa Mungu. Anaweza kuzungumza kwa ufasaha na kufafanua hoja kwa wazi, lakini mahubiri yake yamekosa hali ya kiroho. Rai zake hazijaigusa mioyo kwa hisia mpya za upole na unyororo. Kumekuwa na wingi wa maneno, lakini mioyo ya wasikilizaji wake haijahuishwa wala kuyeyushwa kwa hisia ya upendo wa Mwokozi. —*Shuhuda kwa Kanisa*, kit. 3, uk. 31. {VSSw 211.2}

Kwa Walimu: Upole wa Kristo—Ninatamani kwa dhati kwamba kila siku mjifunze kutoka kwa Mwalimu Mkuu. Mkimkaribia kwanza Mungu, kisha mkawakaribia wanafunzi wenu, mtaweza kufanya kazi yenye thamani kubwa sana. Ikiwa mtakuwa wenye bidii na wanyenyekevu, Mungu atawapa kila siku maarifa,

mwelekeo na uwezo wa kufundisha. Jitahidini kwa kadiri ya uwezo wenu kuwashirikisha wengine baraka ambazo amewajalia. **{VSSsw 211.3}**

Kwa shauku ya dhati na ya kina ya kuwasaidia wanafunzi wenu, waongozeni hatua kwa hatua katika nyanja za maarifa. Jengeni ukaribu nao kadiri mwezavyo.

Isipokuwa walimu wawe na upendo na uungwana na upole wa Kristo ukiwajaa mioyoni mwao, wataudhihirisha kupita kiasi roho ya mwalimu mkali na mwenye kutawala. *“Jilindeni katika upendo wa Mungu, huku mkingojea rehema ya Bwana wetu Yesu Kristo, hata mpate uzima wa milele. Wahurumieni wengine walio na shaka, na wengine waokoeni kwa kuwanyakua katika moto; na wengine wahurumieni kwa hofu, mkilichukia hata vazi lililotiwa uchafu na mwili.”* (Yuda 1:21–23). —**Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi, uk. 253. {VSS 211.4}**

Bila Neno Wala Kitendo cha Hasira—Katika kuwaelimisha watoto na vijana, walimu hawapaswi kuruhusu hata neno moja la hasira/harara* wala ishara yoyote ya hasira iharibu kazi yao, kwa maana kwa kufanya hivyo wanawapandikiza wanafunzi roho ileile waliyo nayo wao wenyewe. —**Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi, uk. 170** [passion au kupitiliza kwenda kwenye hasira au furaha inayopitiliza]. **{VSS 212.1}**

Walimu Wasiwe Wenye Kukasirisha—Walimu walio chini ya nidhamu ya Mungu hupokea neema, ukweli, na nuru kwa njia ya Roho Mtakatifu ili wawashirikishe watoto. Wako chini ya Mwalimu Mkuu kuliko wote ambaye ulimwengu umewahi kumjua; basi, ingekuwa jambo lisilofaa kiasi gani kwao kuwa na roho isiyo na fadhili, sauti kali iliyojaa ukali na kukereka! Kwa kufanya hivyo wangeyaendeleza mapungufu yao wenyewe ndani ya watoto. —**Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi, uk. 171. {VSS 212.2}**

Hakuna Kukosa Wema, Hata Kwa Watenda Mabaya—Ikiwa mwalimu, kwa neema ya Kristo, anajitawala na kushika uongozi kwa mkono thabiti na wenye subira, atautuliza ujeuri, atahifadhi heshima yake mwenyewe, na kupata heshima ya wanafunzi wake. Mara tu utaratibu unapokuwa umerejeshwa, wema, upole, na upendo vidhihirishwe. Huenda uasi ukajitokeza tena na tena, lakini asiruhusu hasira ya ghafula ionekane. Usiseme kwa ukali kwa mtenda mabaya, wala usimvunje moyo mtu anayepambana na nguvu za giza. —*Mashauri Kuhusu Kazi ya Shule ya Sabato*, uk. 173. **{VSS 212.3}**

SURA YA 39—URAHISI NA UWAZI

Maneno Machache, Lakini Yenye Dhati—Mwelimishaji wa kweli ataziongoza akili za wasikilizaji wake kufuatana naye. Maneno yake yatakuwa machache, lakini yenye dhati. Yakitoka moyoni, yatakuwa yamejaa huruma na yenye uchangamfu wa upendo kwa ajili ya roho zenye thamani. —*Mashauri Kuhusu Kazi ya Shule ya Sabato*, uk. 167. **{VSS 214.1}**

Hatari ya Kutumia Maneno Marefu [bombastic misamiati]—Katika kila shule, mafundisho yanayotolewa yanapaswa kuwa rahisi kueleweka kama yale aliyoyatoa Kristo. Matumizi ya maneno marefu huchanganya akili na kufifisha uzuri wa wazo linalowasilishwa. Kuna haja ya walimu watakaowakaribia wanafunzi wao na kuwapa mafundisho yaliyo wazi na yenye kueleweka, wakieleza mambo ya kiroho kwa kutumia vitu vya asili na matukio yanayofahamika ya maisha ya kila siku. —*Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi*, uk. 261. **{VSS 214.2}**

Matumizi ya Wavu wa Injili—Bwana anataka ujifunze jinsi ya kutumia wavu wa Injili. Wengi wanahitaji kujifunza ustadi huu. Ili ufanikiwe katika kazi yako, matundu ya wavu wako—yaani, matumizi ya Maandiko—yanapaswa kuhusiana kwa karibu na jambo linalozungumziwa, na maana yake iwe rahisi kueleweka. Kisha uvute wavu kwa ustadi wote uwezavyo. Nenda moja kwa moja

kwenye hoja kuu. Vielelezo vyako vijieleze vyenyewe. Haidhuru mtu ana maarifa makubwa kiasi gani, hayana manufaa ikiwa hawezi kuyawasilisha kwa wengine. Mguso wa hisia katika sauti yako na hisia zake za ndani viache athari katika mioyo. Wahimiza wanafunzi wako wajisalimishe kwa Mungu.... **{VSS 214.3}**

Fanya maelezo yako yawe wazi, kwa maana ninajua kwamba wako wengi wasioelewa mambo mengi wanayoambiwa. Mruhusu Roho Mtakatifu aumbe na kuutengeneza usemi wako, akiutakasa na kuuondolea uchafu wote. Nena kama watoto wadogo, ukikumbuka kwamba wako wengi walioendelea sana kwa umri, lakini ni watoto wadogo katika ufahamu. —**Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi, uk. 253–254. {VSS 215.1}**

Kujituma kwa Dhati na Kujifunza kwa Bidii—Kujifunza jinsi ya kuyafungua Maandiko kwa wengine kwa namna inayokubalika kunahitaji kujituma kwa dhati na kujifunza kwa bidii. Hili ni muhimu ili kutoa hotuba iliyopangiliwa vizuri, kwa uwazi na nguvu, huku ukiziweka wazi hoja zote muhimu ili zisiweze kueleweka vibaya. —*Letter 185*, 1899. **{VSS 215.2}**

Mpangilio wa Kimantiki wa Mawazo—Baadhi ya akili zinafanana zaidi na duka la vitu vya kale linaloleta udadisi, kuliko kitu kingine chochote. Vipande vingi vya Ukweli visivyo na mpangilio vimeokotwa na kuhifadhiwa humo; lakini wenye akili hizo hawajui jinsi ya kuviwasilisha kwa namna iliyo wazi na yenye muunganiko. Uhusiano wa mawazo hayo kati yao ndio unaoyapa thamani. Kila wazo na kila kauli vinapaswa kuunganishwa kwa karibu kama viungo vya mnyororo. Mhudumu anapowatupia watu wingi wa mambo ili wayakusanye na kuyapangilia wenyewe, juhudi zake huwa bure; kwa maana ni wachache sana watakaoweza kufanya hivyo. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, **uk. 648–649. {VSS 215.3}**

Hoja Chache Muhimu kwa Wakati Mmoja—Ukweli ni tofauti sana katika tabia na utendaji wake ukilinganishwa na mafundisho ya upotovu maarufu yanayohubiriwa kutoka mimbarini, kiasi kwamba unapowekwa mbele ya watu karibu huwastaajabisha. Ni chakula kigumu, hivyo unapaswa kutolewa kwa busara.

Mnapowasilisha kiasi kinachofaa na mkiacha kuzungumza wakati unaofaa, wale wanaosikiliza watakuwa na hamu ya kusikia zaidi. **{VSS 216.1}**

Mungu amewafanya wajumbe Wake kuwa hazina/wahifadhi wa Ukweli Wake, ulio mzito na wenye umuhimu wa milele. Nuru inapaswa kung'aa katikati ya giza la kimaadili ili kufunua dhambi na kosa. Ukweli unapaswa kutolewa hoja baada ya hoja. Unapaswa kunenwa kwa uwazi na kwa matamshi yaliyo dhahiri, ukitoa hoja chache muhimu; ndipo utakuwa kama msumari uliogongolemewa mahali pake salama na Bwana wa makusanyiko. **{VSS 216.2}**

Mhubiri anapaswa kujitahidi kuvuta uelewa na hisia za watu pamoja naye. Usiweke chakula cha kiroho juu sana kiasi kwamba watu wasiweze kukifikia. Huo si mpango wa hekima katika kufundisha Ukweli. —*Letter 7*, 1885. **{VSS 216.3}**

Mambo Mapya na Mambo ya Kale Kutoka Katika Hazina ya Mungu—Wachungaji wanahitaji kuwa na namna iliyo wazi zaidi na rahisi zaidi ya kuuwasilisha ukweli kama ulivyo katika Yesu.... Wale wanaopuza sehemu hii ya kazi wanahitaji kuongoka wao wenyewe kabla ya kuthubutu kutoa hotuba. Wale ambao mioyo yao imejaa upendo wa Yesu na Kweli za thamani za Neno Lake wataweza kupakua kutoka katika hazina ya Mungu mambo mapya na mambo ya kale. Hawatapoteza muda kusimulia visa; wala hawatajitaabisha kutafuta kuwa wahubiri hodari wanaojiinua juu sana kiasi kwamba hawawezi kwenda pamoja na watu; bali kwa lugha rahisi na kwa bidii yenye kugusa moyo, watauwasilisha Ukweli kama ulivyo katika Yesu. —*Jumbe Teule*, Vol. 1, uk. 157. **{VSS 216.4}**

Ubatili wa Hotuba za Kitaaluma—Wachungaji wanapaswa kuuwasilisha Ukweli kwa namna iliyo wazi na rahisi. Miongoni mwa wanaowasiliza wako wengi wanaohitaji maelezo ya wazi kuhusu hatua zinazohitajika ili kupata uongofu. Idadi kubwa ya watu hawajui mambo haya kwa kiwango kinachozidi vile wengi wanavyodhani. Miongoni mwa wahitimu wa vyuo, wanenaji mahiri, viongozi wa serikali, na watu wenye nyadhifa za juu za uaminifu, wako wengi waliotumia uwezo wao katika mambo mengine na kupuuza mambo yaliyo ya umuhimu mkuu. Watu wa namna hiyo wanapokuwa sehemu ya kusanyiko, mnenaji mara nyingi hujitahidi kutumia uwezo wake wote kutoa hotuba ya kitaaluma, na hivyo hushindwa kumdhahirisha Kristo. Haonyeshi kwamba dhambi ni uasi dhidi ya sheria ya Mungu. Hafafanui wazi njia ya wokovu. Kile ambacho kingeigusa mioyo ya wasikilizaji

wake ni kuwaelekeza kwa Kristo aliyekufa ili kuwaletea ukombozi ulio ndani ya uwezo wao kuupokea. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 170. {VSS 217.1}

Umuhimu wa Kutii Amri za Mungu—Ukweli unapaswa kuwasilishwa kwa uwazi mkubwa kiasi kwamba hakuna mvunjaji wa sheria atakayekuwa na udhuru, baada ya kuusikia, kwa kushindwa kutambua umuhimu wa kuzitii amri za Mungu. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 148. {VSS 217.2}

Mahubiri Yaliyo Wazi na Yenye Mpangilio—Ikiwa una neema ihuishayo ya Kristo inayotia nguvu katika utendaji wako, utaweka bidii katika mahubiri yako. Mada yako itakuwa wazi na yenye mipaka dhahiri akilini mwako. Hutakuwa mrefu kupita kiasi katika maelezo yako, wala hutanena kwa kusitasita kana kwamba wewe mwenyewe huamini unayoyasema. Ni lazima uushinde mwendo wa kusitasita, kutokuwa na uamuzi, na uzembe, na ujifunze kuwa mtu anayethamini kila dakika kwa kuwa na utayari saa yoyote. {VSS 217.3}

Masomo ambayo wengi wa wahudumu wetu huwasilisha mbele ya watu hayana hata nusu ya muunganiko, uwazi, na nguvu za hoja kama yanavyopaswa kuwa. —*The Review and Herald*, Aprili 6, 1886. {VSS 218.1}

Bila Mapambo ya Kujitengenezea/feki -artificial embellishment—Mungu anawaita wahudumu wa Injili wasiotafuta kujitanua kupita kiasi kwa kutumia mapambo ya kujitengenezea katika hotuba zao, wakitafuta sifa na makofi ya wanadamu, na kutamani kujionyesha kwa akili na ufasaha wao.... Kadiri wahudumu wanavyomwona Kristo kwa uwazi zaidi na kupokea Roho Wake, ndivyo watakavyohubiri kwa nguvu zaidi Ukweli rahisi ambao Kristo ndiye kiini chake. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 181. {VSS 218.2}

Kuomba Kidogo Sana, Kujifunza Sana—Wao [wahudumu] huiharibu kazi na kudhoofisha athari ya Ukweli wanaotaka kuutetea kwa kusongamanisha mambo mengi sana katika hotuba moja na kwa kuwasilisha hoja nyingi kiasi kwamba akili za wasikilizaji haziwezi daima kuzielewa wala kuzifuata. Wangefanikiwa zaidi kama wangesisitiza hoja moja au mbili katika akili za wasikilizaji, wakizifanya kuwa za umuhimu mkuu, wakazikazia moyoni, na kuwaonya juu ya hatari ya kuikataa

nuru inayohusiana na hoja hizo. Hebu akili za wasikilizaji zinapaswa kuelewa wazi maana ya kila hoja, kisha wahimizwe kufanya uamuzi. {VSS 218.3}

Nilionyeshwa kwamba muda unaotumika katika kusoma na kujifunza kupita kiasi mara nyingi hupotezwa bure-ni muda uliotumiwa vibaya zaidi ya muda uliopotea. Sehemu kubwa ya muda unaotumiwa katika vitabu na kujifunza inapaswa kutumiwa mbele za Mungu, tukimwomba hekima ya mbinguni, nguvu, na uwezo ili Ukweli wanaoelewa vizuri uangaze mbele ya watu katika uwazi wake na uzuri wake wenye upatano. Muda mdogo sana hutumiwa katika sala ya siri na kutafakari mambo matakatifu. Kilio cha watumishi wa Mungu kinapaswa kuwa kuomba kutiwa mafuta na Roho Mtakatifu na kuvikwa vazi la wokovu, ili yale wanayohubiri yaguse mioyo. Wakati ni mfupi sana, na wahudumu wa siku hizi za mwisho ni wachache sana, hivyo wanapaswa kutumia nguvu zao zote katika kazi na kudumisha uhusiano wa karibu na Mungu pamoja na malaika watakatifu, ili mahubiri yao yawe na nguvu za ajabu—nguvu ya kushawishi itakayomvuta kila mtu mwaminifu na anayependa Ukweli na kuendelea kuumbatia daima. —*Manuscript 7*, 1863. {VSS 219.1}

Mafundisho ya Mchungaji Mkuu—Siku ya Jumapili, saa tano asubuhi, Ndugu Wilson wa New Zealand alitoa hotuba yenye manufaa makubwa, nzuri katika urahisi wake, na isiyodhihirisha kwa namna yoyote hali ya juu juu au hovy ovyo. Kadiri hotuba inavyokuwa rahisi na wazi zaidi, ndivyo mafundisho ya wachungaji walio chini ya Mchungaji Mkuu yanavyozidi kuwakilisha mafundisho ya Mchungaji Mkuu. —*Letter 82*, 1895. {VSS 219.2}

Hatari ya Kupaa Juu Kupita Kiasi—Mhubiri anapaswa kujitahidi kuuvuta uelewa na hisia za watu pamoja naye. Asipae juu sana kiasi kwamba watu wasiweze kumfuata; bali awasilishe Ukweli hoja baada ya hoja, polepole na kwa uwazi, akitoa hoja chache muhimu. Ndipo Ukweli utakuwa kama msumari uliogongomewa mahali pake salama na Bwana wa makusanyiko. Akiacha kuzungumza wakati unaofaa, bila kuwapa mara moja zaidi ya yale wanayoweza kuelewa na kunufaika nayo, watakuwa na hamu ya kusikia zaidi, na hivyo shauku yao itaendelea kudumu. —*Evangelism*, uk. 177. {VSS 219.3}

Mada Muhimu Zinazoeleweka kwa Urahisi—Wahudumu wetu wanapaswa kujitahidi kuuwasilisha Ukweli kwa namna iliyo bora na yenye kibali zaidi. Kadiri inavyowezekana, na wote wanene mambo yaleyale. Mahubiri yawe rahisi na

yashughulikie mada muhimu zinazoweza kueleweka kwa urahisi. —*Jumbe Teule*, kit. 1, uk. 167. {VSS 220.1}

Njia za Kutosha na Sahihi za Kuwafikia Watu—Enyi wahudumu, katika mahubiri yenu msipae juu sana kiasi kwamba watu wasielewe mnayosema. Nimeagizwa kwamba mara nyingi sana tunapaa juu mno katika namna tunavyowasilisha Ukweli wa Biblia. Tunapoteza mengi kwa kutoshuka hadi kwenye usahili wa uchaji wa kweli. Mungu ametupatia kila kitu tunachohitaji ili kutuwezesha kuwafikia watu wanaotuzunguka; lakini matengenezo yaliyotokea katika siku za Kristo kutokana na kuhubiriwa kwa Injili ni nadra sana leo. Tunahitaji nguvu za Mungu ziletazo uongofu mioyoni mwetu zitufundishe urahisi katika maneno na matendo. —*Manuscript 85*, 1909. {VSS 220.2}

Neno la Mungu, Si la Mwanadamu—Hubirini Ukweli kwa upole wa unyenyekevu, mkikumbuka kwamba si maneno yenu, bali Neno la Mungu ndilo linalopaswa kupenya na kukata-kata hadi moyoni. —*The Review and Herald*, Juni 13, 1912. {VSS 220.3}

Chakula kwa Wakati Wake—Uwasilisheni Ukweli kama ulivyo katika Yesu, kwa upole wote na unyenyekevu, yaani, kwa urahisi na kwa unyofu, mkitoa chakula kwa wakati wake, na kumpa kila mtu sehemu yake ya chakula. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 432. {VSS 221.1}

Usahili wa Watoto wa Mungu—Wanaume na wanawake wanatangatanga katika ukungu na giza la upotovu. Wanataka kujua Ukweli ni nini. Waambieni, si kwa lugha ya kujikweza, bali kwa urahisi unaowapasa watoto wa Mungu. —*Huduma ya Uinjilisti wa Vitabu*, uk. 72. {VSS 221.2}

SURA YA 40—LUGHA SAFI

Midomo Iliyoguswa na Bwana—Kwa wale wanaojitoa wakfu kikamilifu kiasi kwamba Bwana anaweza kuigusa midomo yao, neno hili hunenwa: “*Nendeni katika shamba la mavuno. Nami nitashirikiana nanyi.*” {VSS 222.1}

Mhudumu aliyepokea maandalizi haya atakuwa nguvu ya kutenda mema duniani. Maneno yake yatakuwa safi, ya Kweli, na yaliyojaa huruma na upendo; matendo yake yatakuwa mema, yakiwaletea msaada na baraka walio dhaifu. Kristo atakuwa kwake uwepo wa kudumu, akiutawala moyo, maneno, na matendo yake. — *Watendakazi wa Injili*, uk. 23. {VSS 222.2}

Kuwa Waangalifu Katika Maneno na Matendo—Kuliko watu wengine wote, wale ambao Bwana amewaamini na kuwaheshimu, na ambao wamekabidhiwa utumishi maalumu, wanapaswa kuwa waangalifu katika maneno na matendo yao. Wanapaswa kuwa watu waliojitoa kwa Mungu ambao, kwa matendo ya haki na kwa maneno safi na ya Kweli, wanaweza kuwainua wanadamu wenzao kufikia kiwango cha juu zaidi. — *Watendakazi wa Injili*, uk. 124. {VSS 222.3}

Kutakaswa kwa Maneno kwa Njia ya Roho Mtakatifu—Ni uwepo wa Roho Mtakatifu wa Mungu unaowaandaa watendakazi, wanaume kwa wanawake, kuwa wachungaji wa kundi la Mungu.... Watajizoeza staha/uungwana/adabu ya kweli ya Kikristo, wakikumbuka kwamba Kristo, Aliye Mwenzake wao, hawezi kuyakubali maneno makali, yasiyo na fadhili, wala hisia zisizo na upendo. Maneno

yao yatatakaswa. Kipawa cha kusema kitahesabiwa kuwa talanta ya thamani waliyoazimwa ili waitumie katika kazi iliyo kuu na takatifu. Chombo cha kibinadamu kitajifunza jinsi ya kumwakilisha Mwenzake wa Kiungu ambaye hushirikiana nacho. Kwa Yule Mtakatifu asiyeonekana kitaonyesha heshima na kicho, kwa sababu a/kimevaa nira Yake na kinajifunza njia Zake safi na takatifu. Wale walio na imani katika Msaidizi huyu wa Kiungu wataendelea kukua. Watapewa karama na uwezo wa kuuvika ujumbe wa Ukweli uzuri mtakatifu.—*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 6, uk. 322. {VSS 222.4}

Maneno ya Hekima na Utakatifu—Sauti ya Bwana inaposema, “*Nimtume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili Yetu?*” Roho wa Mungu huiwezesha mioyo kuitikia: “*Mimi hapa, nitume mimi.*” (Isaya 6:8). Lakini kumbuka kwamba kwanza kaa la moto litokalo madhabahuni linapaswa kuigusa midomo yako. Ndipo maneno utakayonena yatakuwa maneno ya hekima na utakatifu. Ndipo utakuwa na hekima ya kujua la kusema na la kuacha bila kulisema. Hutajaribu kuonyesha umahiri wa akili yako kama mwanatheolojia. Utakuwa mwangalifu usije ukachochea roho ya mabishano au kuamsha chuki kwa kuanzisha mafundisho yenye mabishano au maliumbano. Utapata mambo ya kutosha ya kuzungumzia ambayo hayatazua upinzani, bali yatafungua mioyo ili itamani kupata ujuzi wa kina zaidi wa Neno la Mungu. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 6, uk. 325. {VSS 223.1}

Si Maneno ya Kubahatisha—Wawakilishi wa Mungu duniani wanapaswa kuwa katika ushirika wa kila siku pamoja Naye. Maneno yao yanapaswa kuchaguliwa kwa uangalifu, na usemi wao uwe sahihi na wenye uzima. Maneno ya kubahatisha au pata-potea ambayo mara nyingi hutumiwa na wahudumu wasiomhubiri Injili kwa uaminifu yanapaswa kuachwa kabisa. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 2, uk. 707. {VSS 223.2}

Usemi wa Busara Usioweza Kukosolewa—Kila mhudumu wa Kristo anapaswa kutumia usemi ulio mzuri na wa hekima, usioweza kukosolewa. *Shuhuda kwa Kanisa* juz. 2, uk. 709. {VSS 224.1}

Maandalizi ya Wanafunzi Kuwa Wanenaji wa Hadhara/Umma—Wanafunzi wanapaswa kuandaliwa ili waweze kunena kwa namna inayokubalika mbele ya makutaniko; kwa hiyo wanapaswa kujizoeza kutumia lugha safi na rahisi, na kufuata mbinu bora za kunena. Uangalifu mkubwa unapaswa kutolewa katika

kujizoeza kusoma kwa sauti iliyo wazi, yenye nguvu, na matamshi yaliyo sahihi, huku wakitilia mkazo unaofaa kila neno.... {VSSw 224.2}

Wote wanaweza kuwasilisha Kweli kuu lakini rahisi kuhusu utume na kazi ya Kristo, ikiwa watapenda kufanya hivyo. Wakimtafuta Bwana kila siku kwa sala ya dhiti, na bidii, wataelewa jinsi ya kuwafikia watu kama Kristo alivyowafikia, wakiyalinganisha mafundisho yao na hali mbalimbali pamoja na kiwango cha ufahamu wa wasikilizaji wao. Mafundisho ya kiroho kuhusu ufalme wa Mungu, haya wanapaswa kuyafafanua kwa kutumia vitu vya asili ambavyo wasikilizaji wao wanavifahamu. Kisha vitu hivyo vya asili vitakapoonekana siku baada ya siku, fundisho la Ukweli litarudi tena akilini mwao. —*The Review and Herald*, Oktoba 4, 1898. {VSSw 224.3}

SURA YA 41—BIDII, DHATI NA UHAKIKA

Uhakika Katika Kuwasilisha Ukweli wa Thamani—Neno la Mungu linapaswa kuhubiriwa kwa Roho na kwa uzima. Kwa wote wanaolipokea, lina maana ya uzima wa milele. Kulihubiri kwa ulegevu, kusitasita, na bila uhai hakutakuwa na manufaa yoyote. Jiboreshe katika namna ya kuwasilisha, sauti, bidii, na uhakika, kana kwamba unajua vyema kile unachokishughulikia. Laiti imani ingeshikwa kwa uthabiti zaidi—naam, zaidi sana kuliko ilivyo sasa. Tunaweza kuwa na Kweli za thamani kuu, lakini tukaziwasilisha kwa namna ya ulegevu, woga, ubaridi, kusitasita, na bila uhai kiasi kwamba nguvu yake ya kuigusa mioyo na kuamsha dhamiri hupotea, kwa sababu mioyo yetu wenyewe haijapokea maonyo yake mazito. Je, tunaamini Biblia? Ikiwa tunaamini, basi tutalidhihirisha hilo. —*Letter 1a*, 1896. {VSSw 225.1}

Uhai Katika Kuhubiri na Kuomba—Kumbukeni kwamba kuwa mhudumu hakumaanishi kuhubiri sana tu. Ndugu zangu, nawasihi mazitunze nafsi zenu katika upendo wa Mungu, wala msiruhusu kamwe chemchemi ya uzima ikauke. Hotuba baridi isiyo na furaha italiangamiza kanisa. Leteni uhai katika maneno na sala zenu. Kusiwe na mahubiri hafifu ya ovyo, yasiyo na imani. Ukweli unaokaa moyoni na kuitakasa nafsi utawapa hamu ya kujilisha Kristo, aliye Mkate wa Uzima. Mnapokula mana ya mbinguni, mtaweza kusema: “*Njoni mle yaliyo mema, na nafsi*

zenu zijiburudishe kwa unono.” Wakeni uwezo wenu wote wakfu, kwa Mungu. Bwana anataka muuwakilishe, Kweli kama ulivyo katika Yesu. Kusiwe na jambo lolote linalofanywa kwa kusudi la kutafuta ukuu kuliko wengine. —Letter 1a, 1896. {VSSw 225.2}

Uhakika Unaotokana na Kusadiki Moyoni—Msiuwasilishe Ukweli kwa namna ya kimazoea, bali acha moyo uhuishwe na Roho wa Mungu, na maneno yenu yanenwe kwa uhakika kiasi kwamba wanaowasikia wajue kuwa Ukweli ni halisi kwenu. Namna yenu ya kuwasilishe inaweza kufundishwa, na Maneno yenu yanaweza kuwa kama yale ya Petro: *“Maana hatukufuata hadithi zilizotungwa kwa werevu, tulipowajulisha ninyi nguvu Zake Bwana wetu Yesu Kristo na kuja Kwake; bali tulikuwa tumeuona wenyewe ukuu Wake.”* (2 Petro 1:16). Kwa uhakika huo huo mnaweza kutangaza ujumbe wa Ukweli wa Mungu. Wale wanaouamini Ukweli mtakatifu na wa milele wanapaswa kuuwekeza moyo wao wote katika juhudi zao. Tunapaswa kuguswa sana mioyoni tunapooni unabii ukitimia katika matukio ya mwisho ya historia ya dunia hii. Na maono yetu yanapoelekezwa zaidi katika utukufu wa umilele—kuja kwa Kristo kwa uweza na utukufu mwingi, pamoja na matukio ya siku kuu ya hukumu—hatupaswi kubaki bila hisia, wala bila msukumo. Yohana asema: *“Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao.”* —Letter 8, 1895. {VSS 226.1}

Shauku Katika Mambo Halisi na ya Kufikirika—Siku moja, mwigizaji maarufu Betterton alipokuwa akila chakula pamoja na Dk. Sheldon, Askofu Mkuu wa Canterbury, askofu huyo alimwuliza: “Bw. Betterton, tafadhali niambie kwa nini ninyi waigizaji mnawavutia na kuwaathiri wasikilizaji wenu kwa nguvu sana mnazozungumza kuhusu mambo ya kufikirika?” Betterton akajibu: {VSS 227.1}

“Bwana wangu, kwa heshima yote kwa Neema yako, niruhusu niseme kwamba sababu yake ni rahisi: yote yanategemea nguvu ya shauku/enthusiasm. Sisi jukwaani tunazungumza mambo ya kufikirika kana kwamba ni halisi; lakini ninyi mimbari mnazungumza mambo halisi kana kwamba ni ya kufikirika.” —

Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi, uk. 255. {VSS 227.2}

Mhudumu ni Mjumbe wa Mungu—Mhudumu aliyejifunza kutoka kwa Kristo atakuwa na ufahamu wa daima kwamba yeye ni mjumbe wa Mungu, aliyepeleka utume na Yeye kufanya kazi ambayo athari yake itadumu milele. Lengo lake halipaswi kuwa kujitafutia sifa kwa sababu ya elimu au uwezo wake. Kusudi lake kuu linapaswa kuwa kuwaongoza wenye dhambi kwenye toba, akiwaelekeza kwa mafundisho na kwa mfano wake kwa Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Anapaswa kunena kama mtu anayejua kwamba amepewa nguvu na mamlaka kutoka kwa Mungu. Mahubiri yake yanapaswa kuwa ya dhati na bidii, ari, na nguvu ya ushawishi itakayowaongoza wenye dhambi kukimbilia kwa Kristo ili wapate kimbilio. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 172–173. **{VSS 227.3}**

Nguvu Isiyozuilika yenye Kugusa Mioyo—Hata sauti yenyewe, mwonekano wa uso, na maneno yanapaswa kuwa na nguvu isiyozuilika ya kuigusa mioyo na kutawala fikra za watu. Yesu anapaswa kukaa moyoni mwa mchungaji. Ikiwa Yesu Yuko katika maneno na sauti yake, na ikiwa sauti hiyo imejaa upendo Wake mwororo, hilo litakuwa baraka yenye thamani kuliko utajiri wote, anasa, na utukufu wa dunia; kwa maana baraka hizo hazitapita bila kutimiza kazi yake. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 3, uk. 32. **{VSS 228.1}**

Bidii Hai na Dhati—Mungu anahitaji bidii iliyo hai. Wachungaji wanaweza kuwa na elimu ndogo ya vitabuni; lakini wakitumia kwa uaminifu vipawa walivyo navyo, wakifanya kazi kadiri wanavyopata nafasi, wakivika ujumbe wao kwa lugha rahisi na wazi kabisa, na wakiwa watu wanyenyekevu wanaotembea kwa uangalifu na unyenyekevu, wakitafuta hekima ya mbinguni, wakimumikia Mungu kwa moyo wote, na wakiongozwa na kusudi moja kuu—upendo kwa Kristo na kwa roho ambazo Yeye alizifia—watasikilizwa hata na watu wenye uwezo na vipawa vikubwa zaidi. Kutakuwa na mvuto na uchangamfu katika urahisi wa Kweli wanazozihubiri. Kristo ndiye Mwalimu Mkuu ambaye ulimwengu umewahi kumjua. —*Jumbe Teule*, Vol. 2, uk. 152. **{VSS 228.2}**

Nguvu Katika Kuwasilisha Biblia—Ni lazima tuendeleze hisia ya kudumu ya kutambua udhaifu na kutoweza kwetu, na kumtegemea Yesu kabisa. Hilo litatuwezesha kubaki watulivu na thabiti katika maneno na mwenendo wetu. Msimko wa mnenaji si nguvu, bali ni udhaifu. Bidii na nguvu ni mambo ya lazima katika kuwasilisha Ukweli wa Biblia, yaani Injili iliyo uweza wa Mungu uletao wokovu. —*Jumbe Teule*, kit. 2, uk. 59. **{VSSw 228.3}**

Ukubwa wa Kusanyiko Si Jambo Muhimu Zaidi—Kumbukeni kwamba mnashirikiana na mawakala wa mbinguni—mawakala wasiowahi kushindwa. Neneni kwa bidii, dhiti, imani, na shauku ileile kana kwamba maelfu ya watu wapo wakisikiliza sauti zenu. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 167. {VSSsw 229.1}

Sauti Zenye Uamuzi na Zinazogusa Moyo—Kwa kila taifa, kabila, lugha, na watu, habari njema za msamaha kupitia Kristo zinapaswa kupelekwa. Ujumbe huu haupaswi kutolewa kwa usemi legevu na usio na uhai, bali kwa maneno yaliyo wazi, yenye uamuzi, na yanayogusa moyo. Mamia ya watu wanangojea onyo litakalowawezesha kuokolewa- ili waweze kutoroka. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 29. {VSS 229.2}

Uwasilishaji Wenye Uhakika—Jizoezeni kuwa na bidii na msimamo thabiti mnapowahutubia watu. Maudhui ya ujumbe wenu yanaweza kuwa bora sana na kuwa hasa kile ambacho watu wanahitaji, lakini mtakuwa mnafanya vyema mkichanganya uthabiti huo na maombi yenye ushawishi.... {VSS 229.3}

Wasilisheni wazi maneno haya: “*Bwana asema hivi*,” kwa mamlaka, na kuinua hekima ya Mungu iliyo katika Neno Lake lililoandikwa. Waongozeni watu wafikie uamuzi; daima waweke mbele yao sauti ya Biblia. Waambieni kwamba mnazungumza yale mnayoyajua na mnashuhudia yale yaliyo Kweli, na mnayoyajua kwa sababu Mungu Ndiye aliyesema hayo. Hebu mahubiri yenu yawe mafupi na yaelekee moja kwa moja kwenye hoja kuu; kisha, kwa wakati unaofaa, waalike watu kwa mwito, kufanya uamuzi. Msiuwasilishe Ukweli kwa namna ya kimazoea, bali acha moyo uhuishwe na Roho wa Mungu, na maneno yenu yanenwe kwa uhakika kiasi kwamba wanaowasikia wajue kuwa Ukweli ni halisi kwenu.—*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 296. {VSS 229.4}

Madhara ya Mahubiri Yasiyo na Hamasa—Mhudumu ambaye hajajiweka wakfu kwa Mungu, anapowasilisha ukweli bila ari wala msukumo, huku nafsi yake yenyewe ikiwa haijaguswa na Kweli anazowahubiria wengine, atafanya madhara tu. Kila jitihada anayofanya huzidi kushusha kiwango.—[Shuhuda ka Kanisa, 2:344](#). {VSS 230.1}

Ulegevu Katika Namna ya Kuhubiri—Baadhi yao huhubiri Kweli hizi zenye umuhimu mkubwa sana kwa namna isiyo na ari, kiasi kwamba haziwezi kuwagusa watu. *“Lolote mkono wako utakalolipata kulifanya, lifanye kwa nguvu zako.”*—[Shuhuda ka Kanisa, 2:504. {VSS 230.2}](#)

Kudunisha Ujumbe wa Mungu—Uwezo zaidi, ustadi na ekima vinahitajika katika kuwasilisha Neno na kuwalisha watu wa Mungu kiroho kuliko wengi wanavyodhani. Kuwasilisha uUkweli kwa namna kavu na isiyo na uhai huidunisha ujumbe mtakatifu zaidi ambao Mungu amewapa wanadamu.—[Shuhuda kwa Kanisa, 6:47, 48. {VSS 230.3}](#)

Walaji, Si Wazalishaji—Wale wanaohubiri Injili bila kuweka nafsi yao yote—moyo, akili, roho na nguvu zao—katika kazi hiyo ni walaji, wala si wazalishaji [consumers and not producers]. Mungu anawaita watu wanaotambua kwamba wanapaswa kufanya juhudi ya dhati; watu wanaoweka mawazo, bidii, busara, uwezo na sifa za tabia ya Kristo katika kazi yao. Kuokoa roho ni kazi kubwa sana, inayohitaji kutumiwa kwa kila kipawa na kila karama ya neema. Wale wanaojishughulisha na kazi hii wanapaswa daima kuongeza ufanisi wao. Wanapaswa kujazwa na shauku ya dhati ya kuongezewa uwezo wa kutumika, wakitambua kwamba watakuwa dhaifu bila kuendelea kuongezewa neema. Wanapaswa kutafuta kupata matokeo makubwa zaidi, na makubwa zaidi bado, katika kazi yao. Watenda kazi wetu wanapokuwa na uzoefu huu, matunda yataonekana. Nafsi nyingi zitaletwa katika Kweli.—[Manuscript 90, 1904. {VSS 230.4}](#)

Hakuna Ujumbe wa Kusinzia Wakati Huu—Wakati wa kuja kwa Kristo mara ya kwanza, malaika walivunja ukimya wa usiku kwa sauti za sifa, wakitangaza: “Utukufu kwa Mungu juu mbinguni, na amani duniani; kwa wanadamu nia njema.” Bwana Yu karibu kuja tena akiwa na nguvu na utukufu mkuu. Wale ambao hawajafungamana na ulimwengu watatambua kwamba wakati huu unahitaji zaidi ya hotuba dhaifu, isiyo na nguvu na ya kimazoea. Wataona kwamba lazima kuwe unyofu na bidii na nguvu zinazoambatana na Neno, kiasi cha kuyachochea majeshi ya kuzimu kuupinga ujumbe wa maonyo. Mungu anakusudia kuwafikia watu ili kuwaamsha wanadamu kutoka katika hali yao ya usalama wa kimwili, ili wapate kujitayarisha kwa ajili ya tukio kuu lililo karibu sana kutokea. Ahadi ni hii: *“Mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa*

mashahidi Wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.” Mungu hata kubali ujumbe wowote wa kusinzia na usio na nguvu wakati huu.—[Letter 27, 1894](#). {VSS 231.1}

SURA YA 42—MTINDO WA MAZUNGUMZO

Mahubiri Machache, Mafundisho Zaidi—Kazi haipaswi kuwa kuhubiri pekee. Mahubiri yanahitajika kupunguzwa sana. Muda mwingi zaidi unapaswa kutolewa katika kuwafundisha wengine kwa uvumilivu, huku tukiwapa wasikilizaji nafasi ya kujieleza. Wengi wanahitaji mafundisho—mstari juu ya mstari, kanuni juu ya kanuni; hapa kidogo na pale kidogo. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 338. {VSS 232.1}

Maneno Kutoka Katika Mioyo Iliyojaa Upendo—Bidii yenu isiwe ya kuhubiri tu, bali iwe ya kuhudumu. Semeni maneno yanayotoka katika mioyo iliyotiwa joto na upendo wa Yesu. —*Letter 1a*, 1896. {VSS 232.2}

Watendakazi Pamoja na Yesu Kristo—Katika mikutano ya makambi, mnapaswa kujitahidi kufundisha katika nyanja mbalimbali kama Kristo alivyofanya. Kristo alitoa mahubiri machache sana. Yeye Alikuwa Mwalimu Mkuu, na makutano yalikusanyika kila alipokwenda ili kusikiliza mafundisho Yake. Alifundisha kama mtu mwenye mamlaka, akijua kwamba alikuwa akifundisha Kweli. Alinena kama ambavyo mwanadamu mwingine hakuwahi kunena. {VSS 232.3}

Wahudumu wanapaswa kuelimishwa kufanya kazi kulingana na Kielelezo cha Kiungu. Wengi wenu mnapenda kufundisha, lakini hamjaanza kazi ya kufundisha

kwa urahisi wa Injili ya Kristo. Watu husikiliza mahubiri ambayo mara nyingi huwa marefu mara mbili ya urefu unaopaswa kuwa nao; lakini wanaweza kukumbuka mambo machache tu ya hotuba hiyo, kwa sababu mawazo yao muda wote yamekuwa yakishughulishwa na mambo ya kidunia na ya maisha haya. Kwa hiyo husikiliza wakiwa na mawazo ya kidunia kiasi kwamba Ykweli wa Mungu hauachi athari yoyote ndani ya mioyo yao. Hauingii mpaka ndani kabisa ya nafsi, wala jembe la Ukweli halipenyezi ndani vya kutosha. Kisha hutoka kwenye mkutano na kurudi katika hali yao ya awali. Kwa kuwa mahubiri mara nyingi huwa marefu kuliko inavyopaswa, maneno hupoteza nguvu yake katika akili za wasikilizaji. Mambo mengine huingia na kuzisonga mbegu za Ukweli. {VSS 232.4}

Ukweli wa Mungu lazima ufanywe kuwa wenye mvuto na kugusa myo kwa kuwasilishwa hoja baada ya hoja. Ni kwa manufaa yao ya milele kuujuu Ukweli huo. Mbegu ya Ukweli lazima ipandwe kwa kina kiasi kwamba ishike mizizi imara na iza matunda kwa utukufu wa Mungu. {VSS 233.1}

Sasa Ukweli unapowasilishwa, kuna haja ya kutoa matumizi yake na kutoa miito itakayoupeleka moja kwa moja moyoni ili watu wafanye uamuzi, kwa maana huo ni uamuzi muhimu. Je, ni nani yupo wakati Ukweli huu unawasilishwa? Kuna mwingine zaidi yenu. Shetani na malaika zake wapo ili kuinyakua mbegu ya ukweli. Je, hao ndio wote waliopo? Hapana. Malaika wa Mungu na Yesu Kristo pia wapo. Basi matokeo yake ni nini? Mnapojitahidi kuugusa moyo kwa Ukweli, mtakuwa watendakazi pamoja na Yesu Kristo. —*Manuscript 11*, 1891. {VSS 233.2}

Si Kutoa Mahubiri Pekee, Bali Kufunza na Kuelekeza—Watu wanateseka kwa kukosa maarifa ya ukweli. Hawafahamu wanachopaswa kufanya ili waokolewe. Ikiwa Injili haitahubiriwa kwa uwazi, kwa urahisi, na kurudiwa tena na tena—mstari juu ya mstari, kanuni juu ya kanuni—Shetani atatupa kivuli chake kati ya mwenye dhambi na Mungu. Mungu ataonyeshwa kama Hakimu mkali asiye na rehema wala msamaha. Kristo hakutoa mahubiri tu; alitoa mafundisho kama Mwalimu wa Kiungu. Alifundisha kwa urahisi, na hivyo ndivyo mabalozi Wake wanavyopaswa kuwasilisha Ukweli, wakifanya kila jambo linalohusiana na wokovu wa nafsi liwe wazi na rahisi kueleweka. Ujumbe lazima upelekwe kwa ulimwengu kwamba njia ya toba na imani sasa imewekwa wazi kupitia Yeye aliyekuwa na uwezo wa kuutoa uhai Wake na kuuchukua tena. *"Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi."*—*Manuscript 147*, 1897. {VSS 233.3}

Mafundisho ya Biblia kwa Mtindo wa Mazungumzo au Mjadala Katika Mikutano ya Makambi—(Mazungumzo haya ya ghafla kati ya Ellen White na mwanawe, W. C. White, yalifanyika alipokuwa akitoa hotuba mbele ya Kamati ya Konferensi Kuu huko Lake Goguwac, karibu na Battle Creek, Michigan, Julai 14, 1890.) Mzee White alisema: "Mama, nimekusikia ukisema kwamba tunapaswa kuwa na mafundisho zaidi na mahubiri machache; mahubiri machache na mafundisho zaidi. Ninapozungumzia jambo la kuwakusanya watu pamoja na kufanya masomo ya Biblia..." {VSS 234.1}

Ellen White akajibu: "Hiyo ndiyo ilikuwa njia katika siku za Kristo. Angezungumza na watu, nao wangemuuliza swali kuhusu maana ya jambo fulani. Yeye alikuwa Mwalimu wa watu." {VSS 234.2}

Mzee White akaendelea: "Nakumbuka vizuri uliposema kwamba kadiri tunavyokaribia mwisho, nimeona mikutano yetu ya makambi ikiwa na mahubiri machache na masomo mengi zaidi ya Biblia; makundi madogo yakiwa katika maeneo mbalimbali, yakiwa na Biblia mikononi mwao, na watu tofauti wakiongoza masomo ya Maandiko kwa uhuru katika mtindo wa mazungumzo." {VSS 235.1}

Ellen White akasema: "Hiyo ndiyo kazi niliyoonyeshwa kwamba itafanya mikutano yetu ya makambi iongeze mafanikio na shauku. Wapo wanaohitaji nuru iliyo dhahiri zaidi. Wengine huchukua muda mrefu zaidi kuelewa mambo na kufahamu hasa kile mnachomaanisha. Kama wangepata nafasi ya kufafanuliwa kwa uwazi zaidi, wangeona na kulipokea. Na lingekuwa kama msumari uliogongomewa mahali pake salama, na lingeandikwa katika mbao za mioyo yao." {VSS 235.2}

"Makutano makubwa yalipomzunguka Kristo, aliwapa mafundisho Yake. Kisha wanafunzi, katika maeneo na nafasi mbalimbali baada ya hotuba hiyo, walirudia yale Kristo aliyosema. Watu walikuwa wameelewa vibaya maneno ya Kristo; hivyo wanafunzi waliwaeleza watu yale Maandiko yalisema na yale Kristo alisema Maandiko yalisema. Walikuwa wakijifunza kuwa waelimishaji. Walikuwa karibu na Kristo, wakipokea masomo kutoka Kwake na kuwapelekea watu." — *Manuscript 19b*, 1890. {VSS 235.3}

Mafundisho Katika Nyumba za Watu—Watumishi wa Mungu wana kazi kubwa ya kufanya zaidi ya kuhubiri mimbarani. Katika kazi ya huduma kuna mahubiri mengi mno na mafundisho halisi ya Biblia machache sana. {VSS 235.4}

Wahudumu wetu wanapaswa kuwatembelea washiriki wa kanisa zaidi kuliko wanavyofanya sasa, ili kuzungumza na kuomba pamoja nao. Mioyo yao inapaswa kujazwa upendo kwa wale waliokabidhiwa chini ya uangalizi wao. Wachungaji wanapotembelea familia, wanapaswa kujitahidi kufanya saa ya ibada iwe baraka kubwa; na wanapokuwa mezani wakati wa chakula, wajitahidi kufanya mazungumzo kuwa chanzo cha faraja na kujengwa kiroho. Hebu wazungumzie mambo ya Biblia na kusimulia uzoefu wao katika kuendesha mikutano na kuwatembelea watu. Wazazi watanufaika, watoto wataathiriwa mioyo, na kadiri joto na neema ya Kristo vinavyohisiwa, nguvu za kiroho zitaongezeka. **{VSS 236.1}**

Mara nyingi mchungaji hulazimika kuzungumza katika chumba chenye msongamano wa watu na joto jingi. Wasikilizaji huanza kusinzia, akili zao hudhoofika, na huwa vigumu sana kufahamu mambo yanayowasilishwa. Badala ya kuwahubiria tu, ikiwa mnenaji angejaribu kuwafundisha kwa kuwauliza maswali na kuzungumza kwa mtindo wa mazungumzo, akili zao zingechochewa kufanya kazi, na wangeweza kuelewa kwa uwazi zaidi Kweli zinazofunuliwa mbele yao. Uelewa wao ungeyashika mafundisho hayo yaliyo hai, ambayo ni muhimu kwa kuamsha utambuzi na kukua katika maarifa. Anapopitia hotuba yake hoja baada ya hoja, akiwapa wasikilizaji wake nafasi ya kuuliza maswali na kutoa mapendekezo, yeye mwenyewe atapata uelewa bora zaidi wa somo lake. Pasipo kuweka Kweli kuu za Neno la Mungu wazi mbele ya ufahamu, haziwezi kueleweka na akili wala kutekelezwa katika maisha. —*Manuscript 41*, 1903. **{VSS 236.2}**

SURA YA 43—HAKUNA MANENO MAKALI WALA ROHO YA MABISHANO

Kutumia Ukweli Kama Mjeledi—Katika siku zilizopita, uliwasilisha ukweli kwa ukali, ukiutumia kana kwamba ulikuwa mjeledi. Jambo hilo halikumtukuza Bwana. Uliwapa watu hazina nyingi za thamani kutoka katika Neno la Mungu, lakini namna yako ya kuuwasilisha ilikuwa ya kukemea na kuhukumu kiasi kwamba waliugeukia mbali ukweli huo. Hukuwafundisha Ukweli kwa namna ambayo Kristo aliufundisha; badala yake, uliwasilisha kwa njia iliyoharibu mvuto wake. Moyo wako unahitaji kujazwa neema ya Kristo ibadilishayo. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 173–174. **{VSS 238.1}**

Ukali Hausaidii—Hubiri Ukweli, lakini epuka maneno yanayoonyesha roho ya ukali/hasira, kwa maana maneno ya namna hiyo hayawezi kumsaidia wala kumwangazia mtu yeyote. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 575–576. **{VSS 238.2}**

Athari ya Tone Moja la Uchungu—Kila mahubiri unayohubiri na kila makala unayoandika yanaweza kuwa ya Kweli kabisa; lakini tone moja la uchungu ndani yake litakuwa sumu kwa msikilizaji au msomaji. Kwa sababu ya tone hilo la sumu, mtu mmoja anaweza kuyaacha maneno yako yote mazuri na yanayokubalika, huku mwingine akilifurahia na kulipokea jambo hilo baya kwa sababu anapenda maneno makali kama hayo. Ataufuata mfano wako na kuzungumza kama unavyozungumza

wewe, na hivyo uovu utaongezeka zaidi. —[Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 6, uk. 123. **{VSS 238.3}**

Ulimi Wetu Kama Kalamu ya Mwandishi Mahiri—Jihadhari usije ukatoa maneno ya kushutumu hata mara moja. Tunahitaji Roho Mtakatifu wa Mungu awe uzima na sauti yetu. Ulimi wetu unapaswa kuwa kama kalamu ya mwandishi aliye tayari kuandika, kwa sababu Roho wa Mungu ananena kupitia chombo cha kibinadamu. Unapotumia kejeli na maneno makali yanayoumiza, umechanganya jambo fulani kutoka kwako mwenyewe, nasi hatutaki mchanganyiko wa namna hiyo. —[Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti](#), uk. 172. **{VSS 239.1}**

Kuwa Macho Kila Wakati—Wahubiri vijana, pamoja na wale waliowahi kuwa wahudumu lakini wamekuwa wakorofi, wajeuri na wakali katika mwenendo wao, wakitumia katika mazungumzo yao maneno yasiyo ya kiasi na yasiyo safi, hawafai kushiriki katika kazi hii mpaka watakapotoa ushahidi wa mabadiliko kamili. Neno moja lisilofikiriwa na bila hekima linaweza kusababisha madhara makubwa kuliko faida ambayo mfululizo wa mikutano yao unaweza kuleta. Kwa njia hiyo wanashusha kiwango cha Ukweli, ambacho kinapaswa kuinuliwa daima, na kukiweka chini mbele ya jamii. Waongofu wao kwa kawaida hawafikii kiwango cha juu zaidi ya kile kilichowekwa mbele yao na wahudumu hao. Watu wanaosimama kati ya wanadamu walio hai na wafu wanapaswa kuwa sahihi kabisa katika maisha yao. Mchungaji hapaswi kulegeza uangalifu wake hata kwa muda mfupi, kwa maana anafanya kazi ya kuwainua wengine kwa kuwapeleka kwenye kiwango cha Ukweli. Hebu aweze kuwaonyesha wengine kwamba Ukweli umefanya kazi ndani yake. Anapaswa kutambua uovu wa maneno ya uzembe, ujeuri, lugha chafu, ukali, na udhalilishaji, na kuyaondoa kabisa pamoja na kila jambo la namna hiyo; kwa maana asipofanya hivyo, waongofu wake wataiga mwenendo wake. —[Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 1, uk. 445–446. **{VSS 239.2}**

Milango Iliyofungwa na Kufuli—Kila mtu na akumbuke kwamba hatupaswi kwa namna yoyote kujitafutia au kualika mateso au kuchochea upinzani. Hatupaswi kutumia maneno makali na yenye kukata; maneno hayo yaondolewe katika kila makala tunayoandika na kila hotuba tunayotoa. Liacheni Neno la Mungu likate na kukemea; wanadamu wenye mipaka wajifiche na kukaa ndani ya Yesu Kristo, na

Roho wa Kristo aonekane katika yote. Kila mtu awe mwangalifu katika maneno yake, ili wasiwaweke wale wasio wa imani yetu katika upinzani mkali dhidi yetu na kumpa Shetani nafasi ya kutumia maneno yasiyofikiriwa ili kuziba njia yetu. “*Msifanye jambo lolote kabla ya wakati wake.*” Mungu atakapotoa ujumbe mkali na wa karibu na unaopenya, huo utakuwa ni kazi Yake wala hautachochewa na msukumo wa wanadamu wenye mipaka. Mwanadamu anapotumia upanga wenye makali kuwili kwa kukata na kuchoma kwa msukumo wake mwenyewe, ataziba njia yetu kiasi kwamba tutakutana na milango iliyofungwa na kufuli dhidi yetu. — *Manuscript 95, 1894.* {VSS 240.1}

Kutotaja Madai ya Wapinzani—Roho Mtakatifu atalifikisha moyoni neno linalosemwa kwa upendo. Lakini ieleweke kwamba hakuna faida inayopatikana pale ambapo sauti au kalamu vinaonyesha ukali, au hata vinapowasilisha Ukweli kwa namna ya ukali. Tupilia mbali na hisia kali za kibinadamu, ili Ukweli usieleweke vibaya, usitafsiriwe vibaya, wala usipotoshwe. Ukweli utakuwa na nguvu ya kuhuisha unaposemwa chini ya ushawishi kamili wa neema ya Kristo. Mpango wa Mungu ni kuufikia moyo kwanza. Sema Ukweli na umruhusu Yeye aendelee nguvu ya matengenezo na kanuni yake; lakini tusifanye kazi kwa kufuata msukumo wetu binafsi. {VSS 240.2}

Ni jambo gani jema linaloweza kutimizwa kwa roho zilizo gizani kwa kuwakemea kwa shutuma kali? Wale wasio na maarifa ya Ukweli, waliopofushwa na kupotoshwa katika hukumu zao, hawaelewi maana yake. Sema Ukweli kwa upendo. Ruhusu upole wa Kristo uingie moyoni. Usirejeele yale yanayosemwa na wapinzani, bali sema Ukweli pekee— “*Imeandikwa.*” Ukweli utagusa moyo kwa kina na haraka. Usiruhusu roho yako binafsi na tamaa zako zichanganywe na ukweli kama moto wa kawaida unavyochanganywa na mwali mtakatifu. Ufunue Neno waziwazi katika uzito wake wote. {VSS 241.1}

Wengi ambao sasa ni wapinzani wakali wa Ukweli wanafuata kile wanachoamini kwa uaminifu kuwa ni wajibu wao, lakini bado wataiona Kweli na kuwa watetezi wake wenye nguvu. Wale ambao sasa wanawadhihaki na kuwaonyesha roho ya ukali na dharau wataanguka katika majaribu, wataleta aibu kwa kazi ya Mungu, na kusababisha kupotea kwa roho kwa sababu ya kutokuwa kwao waangalifu. Wengi wanaoingia katika kazi wakati wa mwito wa saa ya kumi

na moja, kwa neema ya Kristo watawasilisha Kweli kwa namna ambayo watahesabiwa kuwa wa kwanza. **{VSS 241.2}**

Sisi hatupaswi kusema mambo yanayokinzana. Kazi yetu ni kupeleka nuru na kupandikiza mawazo katika roho ya upole na utegemezi kwa Mungu. Hebu tujitahidi kuwa washindi ili tupokee thawabu ya washindi. Fanyeni yote mnayoweza kuakisi nuru na kuwaleta watu kwenye ujuzi wa Ukweli kama ulivyo katika Yesu; lakini jipusheni kusema maneno yanayokera, yenye kuchokoz na kuchochea. Uwasilisheni ukweli katika urahisi wake, kwa maana lazima ushuhudiwe mbele ya wanadamu kwa kuwa unahusu maslahi yao ya milele. —*Letter 36*, 1895. **{VSS 241.3}**

Silaha za Mabishano Ziwekwe Kando—Silaha za mabishano/malumbano na roho ya kushindana lazima ziwekwe kando. Ikiwa tunataka kuwa kama Kristo, lazima tuwafikie watu walipo. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 249. **{VSS 242.1}**

Mabishano Yasiyofaa—Tunao ujumbe wa Ukweli wenye uzito mkubwa kuliko ujumbe mwingine wowote uliowahi kupeleka ulimwenguni. Ukweli huu unazidi kuheshimiwa na wasioamini kwa sababu hauwezi kupingwa. Kwa sababu ya jambo hili, vijana wetu hujiamini kupita kiasi na kujikweza au kujigamba. Wanachukua kweli zilizofafanuliwa na watu wengine, na bila kujifunza wala kuomba kwa bidii hukutana na wapinzani na kuingia katika mashindano, wakitumia maneno makali na kejeli, huku wakijidanganya kwamba wanafanya kazi ya mhudumu wa Injili. Ili kufaa kwa kazi ya Mungu, watu hawa wanahitaji uongofu kamili kama ule ambao Paulo alipata. Wachungaji wanapaswa kuwa wawakilishi hai wa Ukweli wanaouhubiri. Wanapaswa kuwa na kiwango cha juu zaidi cha maisha ya kiroho, yanayoambatana na ushahidi mkubwa zaidi. —*Shuhuda ka Kanisa*, juz. 4, uk. 446. **{VSS 242.2}**

Mabishano Zaidi, Upinzani Zaidi—Mara nyingi, unapojitahidi kuwasilisha Ukweli, upinzani utaibuka; lakini ukijaribu kuukabili upinzani huo kwa mabishano, utaongeza upinzani zaidi, na huwezi kumudu kufanya hivyo. Shikilia msimamo wa Ukweli unaouhubiri. —*Shuhuda ka Kanisa*, juz. 9, uk. 147. **{VSS 242.3}**

Mipaka ya Mijadala—Kamwe usiingie katika mijadala ambao mambo mengi sana yako hatarini, ukitegemea uwezo wako wa kujibu mabishano/hoja zenye nguvu. Ikiwa hauwezi kuepuka kuingia katika pambano hilo, ingia ukiwa na imani thabiti katika Mungu na ukiwa na roho ya unyenyekevu, yaani roho ileile ya Yesu, ambaye amekuagiza wewe ujifunze Kwake kwa sababu Yeye ni mpole na mnyenyekevu moyoni. Kisha, ili kumtukuza Mungu na kuonyesha tabia ya Kristo, usitumie kamwe njia zisizo halali ili kupata ushindi dhidi ya mpinzani wako. Weka kando kejeli, kushushua watu na mchezo wa maneno. Kumbuka kwamba unapambana si tu na mwanadamu, bali pia na Shetani pamoja na malaika zake. —[Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 1, uk. 626. {VSS 242.4}

Hakuna Dalili ya Kujitosheleza Nwebtewe—Usiseme neno wala usifanye tendo lolote litakalowathibitishia wengine katika kutokuamini. {VSS 243.1}

Ikiwa mtu yeyote atajaribu kuwavuta watendakazi katika mabishano au mijadala kuhusu masuala ya kisiasa au mambo mengine, msikubali kushawishiwa wala kuchochewa na changamoto hiyo. Endelezeni kazi ya Mungu kwa uthabiti na nguvu, lakini katika upole wa Kristo na kwa utulivu kadiri iwezekanavyo. Msimruhusu mwanadamu yeyote asikike akijisifu, wala msionyeshe dalili yoyote ya kujitegemea kupita kiasi au kujiona mnatosha wenyewe. Acha ionekane kwamba Mungu ametuita tushughulikie amana takatifu; hubirini Neno, iweni wenye bidii, dhati, wenye juhudi, na wenye moyo wa dhati. —[Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 6, uk. 122. {VSS 243.2}

Wachungaji Wenye Kupenda Mabishano Si Wachungaji Wema—Baadhi ya wahudumu ambao wamekuwa katika kazi ya kuhubiri Ukweli wa sasa kwa muda mrefu wamefanya makosa makubwa katika huduma zao. Wamejizoeza na kujielimisha kuwa walumbanaji/wapiganaji katika hoja. Wamejifunza kwa kina masuala yenye mabishano kwa kusudi la kujadiliana, na hupenda kutumia mada hizi walizoziaandaa katika mijadala. Ukweli wa Mungu ni wazi, dhahiri, na wenye kuthibitisha. Una upatanifu ndani yake, na unapolinganishwa na kosa, huangaza kwa uwazi na uzuri. Uthabiti wake hujidhihirisha kwa dhamiri ya kila moyo usiojawa na chuki. Wahubiri wetu huwasilisha hoja kuhusu Kweli ambazo tayari zimeandaliwa kwa ajili yao, na ikiwa hakuna vizuizi, Ukweli hushinda. Lakini nimeonyeshwa kwamba mara nyingi binadamu aliye chombo dhaifu hujichukulia sifa kwa ushindi uliopatikana, na watu ambao ni wa kidunia zaidi kuliko kuwa wa kiroho humsifu na

kumheshimu huyo binadamu ambaye ni chombo tu badala ya kuinua Ukweli wa Mungu ambao umeshinda kupitia kwake. **{VSS 243.3}**

Wale wanaopenda kujihusisha katika mijadala mara nyingi hupoteza hali yao ya kiroho. Hawamtegemei Mungu kama wanavyopaswa. Huandaa hoja za Ukweli kana kwamba ni mjeledi wa kumpiga mpinzani. Hisia za mioyo yao ambayo **haijatakaswa zimeandaa maneno makali na yenye kuchoma ili kuyatumia kama mshipi wa kumkera** na kumchochea mpinzani wao. Roho wa Kristo hana nafasi katika mwenendo huu. Ingawa mhubiri huyo ana hoja zenye nguvu za kuthibitisha Ukweli, mara nyingi huanza kufikiri kwamba ana nguvu za kutosha kumshinda mpinzani wake, na Mungu huachwa nje ya jambo hilo. Baadhi ya wachungaji wamefanya mijadala kuwa kazi yao kuu. Wanapokuwa katikati ya msisimko unaosababishwa na mjadala, huonekana kupata kupata nguvu mpya kihisia, nao hujihisi kuwa imara, na hunena kwa nguvu. Kisha atika msisimko huo, mambo mengi hupokelewa na watu kana kwamba ni sahihi, ingawa kwa Kweli ni makosa makubwa na ni aibu kwa mtu aliyetamka maneno yasiyofaa kwa mhudumu wa Kikristo. **{VSS 244.1}**

Mambo haya yana ushawishi mbaya kwa wahudumu wanaoshughulikia Kweli takatifu na zilizo kuu—Kweli ambazo zinapaswa kuwa harufu ya uzima iletayo uzima au harufu ya mauti iletayo mauti kwa wale wanaozisikia. Kwa kawaida, ushawishi wa mijadala kwa wahudumu wetu huwa unawafanya wajitosheleze na kujiona kuwa wakuu katika mawazo yao wenyewe. Lakini si hayo tu. Wale wanaopenda mabishano hawafai kuwa wachungaji wa kundi la Mungu. Wameizoeza akili yao kukabiliana na wapinzani na kusema maneno ya kejeli, hivyo hushindwa kushuka na kufikia mioyo ya watu wanaoteseka na wanaohitaji faraja. **{VSS 245.1}**

Pia wamejikita sana katika hoja za mabishano kiasi kwamba wamepuuza mambo ya kivitendo ambayo kundi la Mungu linayahitaji-mtino wa maisha ya kila siku. Wana maarifa machache kuhusu mafundisho ya Kristo yanayogusa maisha ya kila siku ya Mkristo, na hawana shauku kubwa ya kuyachunguza. Wameinuka juu ya urahisi wa kazi hiyo. Walipokuwa wadogo machoni pao wenyewe, Mungu aliwasaidia; malaika wa Mungu waliwahudumia na kufanya kazi zao kuwa na mafanikio makubwa katika kuwashawishi wanaume na wanawake kuupokea Ukweli. Lakini katika kuzoeza akili zao kwa ajili ya mabishano, mara nyingi huwa

wakali na wasio na upole. Wanapoteza shauku na huruma nyororo ambayo inapaswa kuambatana daima na kazi ya mchungaji wa Kristo. {VSS 254.2}

Wahudumu wanaopenda mabishano au [debate] kwa kawaida hawana sifa za kusaidia kundi la Mungu katika maeneo ambayo linahitaji msaada mkubwa zaidi. Kwa kuwa wamepuuza dini ya vitendo katika mioyo na maisha yao wenyewe, hawawezi kuifundisha kwa kundi. Isipokuwa kuwe na msisimko wa mjadala, hawajui jinsi ya kufanya kazi. Wanapojaribu kuzungumza, huonekana hawajui jinsi ya kuwasilisha somo linalofaa kwa wakati huo. Wakati wanapaswa kuwasilisha somo litakalolilisha kundi la Mungu na kugusa mioyo yao, wao hurudi kwenye mambo yale yale ya zamani yaliyopangwa na kukaririwa [stereotyped], na kutoa hoja zilizopangwa ambazo ni kavu na zisizovutia. Hivyo, badala ya kuleta nuru na uzima, huleta giza kwa kundi la Mungu na pia kwa nafsi zao wenyewe. —[Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 3, uk. 215–216. {VSS 244.3}

SURA YA 44—UFUPI

Mahubiri Mafupi Zaidi, Huduma Zaidi—Mahubiri marefu hayana manufaa makubwa katika kutenda mema, kwa sababu msemaji na msikilizaji huchoka; hivyo hotuba zinapaswa kufupishwa ili nguvu za mwili na akili za mhudumu zihifadhiwe kwa ajili ya kazi ya huduma, na kwa njia hiyo kazi kubwa zaidi iweze kutimizwa. —*The Review and Herald*, Septemba 2, 1890. {VSS 247.1}

Matokeo Makubwa Mara Kumi Zaidi—Ikiwa wahudumu wetu wangetoa mahubiri mafupi yanayolenga jambo kuu, kisha wawafundishe ndugu na dada kufanya kazi na kuwakabidhi wajibu huo, wachungaji wenyewe wangeepuka uchovu wa kupita kiasi; watu wangepata nguvu za kiroho kupitia juhudi

wanazofanya, na matokeo yangukuwa makubwa mara kumi zaidi kuliko yale yanayoonekana sasa. —*The Signs of the Times*, Mei 17, 1883. {VSS 247.2}

Mahubiri Yapunguzwe Kwa Nusu—Wahudumu hutumia muda mwingi sana katika kuhubiri na hivyo huchosha nguvu zao za mwili; ni mahubiri mengi marefu yanayowachosha watu, na nusu ya chakula cha Injili kinachowasilishwa kingekuwa na manufaa makubwa zaidi kuliko wingi wote unaotolewa. —

Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti uk. 658. {VSS 247.3}

Viungo vya Mwili Huchoka Kwa Hotuba Ndefu—Kuna jambo moja ambalo ningependa kuwaonya nalo: ninapozungumza mbele ya kusanyiko, sipaswi kuzungumza kwa muda mrefu sana kwa wakati mmoja, kwa maana kufanya hivyo huweka mzigo mkubwa juu ya viungo nyeti vinavyohusika katika kazi hiyo. Nimelazimika kujiwekea ahadi kwamba sitazungumza muda mrefu sana, kwa sababu ninajua kwamba nikifanya hivyo, tumbo, mapafu, na figo vitachoka kupita kiasi, na matokeo yake yatakuwa mateso. —*Letter 75*, 1904. {VSS 247.4}

Uvumba Unaopendeza Kwa Mungu—Nguvu na mwanga wa ukweli na vionekane katika maneno yanayofaa; eleza furaha na shukrani vinavyotoka moyoni unapoyaona juhudi za nafsi yako zikizaa matunda katika uongofu wa wenye dhambi. Lakini unapozungumza na watu, kumbuka kusimama kwa wakati unaofaa; usijichoshe kiasi cha kupata msongo wa mawazo na kudhoofika, kwa sababu kazi utakayohitaji kufanya zaidi ya kuhubiri inahitaji busara na uwezo. Kazi hii itakuwa chombo chenye nguvu cha kuleta mema, kama uvumba wa kupendeza unaoinuka juu, mbele za Mungu. —*Special Testimonies*, Series A, 7:12. {VSS 248.1}

Akiba ya Nguvu za Kimwili na Kiakili—Kamwe usitumie nguvu zako zote katika hotuba ndefu na yenye kuchosha kiasi kwamba usibaki na akiba ya nguvu za mwili na akili za kukutana na watu wanaouliza maswali, kuondoa mashaka yao kwa uvumilivu, na kuimarisha imani yao. Onyesha wazi kwamba tunashughulikia hoja nzito ambazo unajua haziwezi kupingwa; fundisha kwa mafundisho na kwa mfano kwamba Ukweli ni wa thamani, kwa kuwa huleta nuru katika ufahamu na ujasiri moyoni. Dumisha uso wenye furaha; utafanya hivyo ikiwa utawasilisha Ukweli kwa upendo. Daima kumbuka kwamba masilahi ya milele yako hatarini, na uwe tayari kufanya kazi binafsi kwa ajili ya wale wanaohitaji msaada. {VSS 248.2}

Kwa lugha rahisi na iliyo wazi, mwambie kila mtu kile anachopaswa kufanya ili aokolewe. —*Special Testimonies*, Series A, 7:8. {VSS 249.1}

Mahubiri Marefu Ni Mzigo kwa Mhubiri na Wasikilizaji

Wale watakaokuwa vinywa vya Mungu wanapaswa kutambua kwamba midomo yao imeguswa kwa kaa la moto kutoka madhabahuni, na wanapaswa kuwasilisha Ukweli kwa udhihirisho wa Roho; lakini mahubiri marefu huwa mzigo kwa msemaji na pia kwa wasikilizaji wanaolazimika kukaa kwa muda mrefu. Nusu tu ya mambo yanayowasilishwa yangekuwa na manufaa makubwa zaidi kwa msikilizaji kuliko wingi mkubwa wa mambo yanayotolewa na msemaji. Mambo yanayosemwa katika saa ya kwanza huwa na thamani kubwa zaidi ikiwa mahubiri yangeishia hapo, kuliko maneno yanayoongezwa katika nusu saa nyingine, kwa sababu mambo yaliyokwisha kuwasilishwa huzikwa chini ya wingi wa maneno yanayofuata. {VSSsw 249.2}

Jambo hili limeonyeshwa kwangu tena na tena kwamba wachungaji wetu wamekuwa wakifanya makosa kwa kuzungumza muda mrefu kiasi cha kufifisha mvuto wa kwanza wenye nguvu uliowapata wasikilizaji. Kiasi kikubwa sana cha mambo huwasilishwa ambacho, hawawezi kukitunza akilini wala kukielewa vizuri; hivyo kila kitu huonekana kuwa kimechanganyika.—*Shuhuda kwa Wachungaji na Watendakazi wa Injili*, uk. 256. {VSSsw 249.3}

Mahubiri Mafupi na Muda wa Ushuhuda—Huduma ya kuhubiri kwa kawaida inapaswa kuwa fupi, ili wale wanaompenda Mungu wapate nafasi ya kueleza shukrani zao na kumsifu. Maombi na sifa zinazotolewa kwa Mungu na watoto Wake wanaoamini humheshimu na kulitukuza Jina Lake. —*Manuscript 32a*, 1894. {VSSsw 249.4}

Ujumbe Mfupi, Unaorudiwa Mara kwa Mara—Ujumbe wa wakati huu unapaswa kuwasilishwa, si kwa mahubiri marefu na yenye kuchosha, bali kwa mazungumzo mafupi yanayolenga moja kwa moja jambo kuu au pointi. Mahubiri marefu huchosha nguvu za msemaji na huvuta sana uvumilivu wa wasikilizaji. Ikiwa msemaji anatambua umuhimu wa ujumbe wake, anapaswa kuwa mwangalifu sana asije akatumia nguvu zake za mwili kupita kiasi na kuwapa watu mambo mengi zaidi ya yale wanayoweza kuyakumbuka. {VSSsw 250.1}

Usifikiri kwamba kwa sababu umepitia somo fulani mara moja, wasikilizaji wako watakuwa wamehifadhi katika akili zao kila kitu ulichowasilisha. Kuna hatari ya kutoka haraka sana kutoka hoja moja kwenda nyingine. Toa mafundisho mafupi kwa lugha iliyo wazi na rahisi, na yarudie mara kwa mara. Mahubiri mafupi hukumbukwa vizuri zaidi kuliko mahubiri marefu. Wahubiri wetu wanapaswa kukumbuka kwamba masomo wanayowasilisha yanaweza kuwa mapya kwa baadhi ya wasikilizaji wao; kwa hiyo hoja kuu zinapaswa kurudiwa tena na tena. — *Watendakazi wa Injili*, uk. 167–168. {VSSsw 250.2}

Kupotea kwa Shauku ya Dini—Hotuba ndefu na maombi marefu yenye kuchosha huleta madhara makubwa kwa shauku ya mambo ya kiroho/dini na hushindwa kuleta usadikisho katika dhamiri za watu. Tabia hii ya kuzungumza kwa muda mrefu mara nyingi hupunguza shauku ya mambo ya kiroho ambayo ingeweza kuzaa matokeo makubwa. — [Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 4, uk. 261. {VSS 250.3}

Kidogo Kidogo kwa Wakati Mmoja—Uwasilisheni Ukweli kwa watu kwa kuzingatia umuhimu wake halisi na utakatifu wake, na jihadharini msiwape sehemu kubwa sana katika hotuba moja; kwa maana mkifanya hivyo, mambo hayo yatapotea kutoka kwao. Hotuba ndefu hupunguza ufanisi wa kazi yenu. Kwa wale wasiojua Ukweli, mafundisho yenu ni mapya na magumu kuyaelewa, na hawawezi kuyafahamu kwa urahisi. Kuna hatari ya kumimina katika akili zao wingi wa mambo ambayo hawawezi kuyaelewa wala kuyachanganua/kuyameng’anya vizuri. “*Lakini Neno la Bwana lilikuwa kwao: amri juu ya amri, amri juu ya amri; mstari juu ya mstari, mstari juu ya mstari; hapa kidogo na pale kidogo.*” Tunapaswa kujifunza namna Yeye alivyofundisha. Tunayo ushuhuda muhimu na wa hakika kabisa kwa ajili ya ulimwengu, na tunapaswa kuwapa watu mahubiri mafupi kwa lugha rahisi na iliyo wazi. Msifikiri kwamba kwa sababu mmepitia somo fulani mara moja, mnaweza kuendelea kwenye mambo mengine na wasikilizaji wakabaki na kila kitu kilichowasilishwa. — *Special Testimonies*, Series A 7:6–7. {VSSsw 250.4}

Kutilia Mkazo Zaidi Usomaji wa Biblia—Epukeni mahubiri marefu. Watu hawawezi kuhifadhi hata nusu ya mambo wanayosikia katika mahubiri hayo. Toeni mafundisho mafupi na masomo mengi zaidi ya Biblia. Huu ndio wakati wa kuweka kila jambo wazi kabisa kama alama za barabarani zinazomwongoza msafiri. — [Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti](#), uk. 439. {VSSsw 251.1}

Ngano Safi Iliyopepetwa Vizuri—Hubiri Ukweli kwa urahisi wake, lakini mahubiri yako yawe mafupi. Zingatia kwa uthabiti mambo machache muhimu. Wapatie watu ngano safi iliyopepetwa vizuri na kuondolewa makapi yote. Usiruhusu mahubiri yako yajumuishe mambo mengi kiasi kwamba udhaifu uonekane badala ya hoja imara. Uwasilishe Ukweli kama ulivyo katika Yesu, ili wale wanaosikia wapate mvuto bora kabisa. —*Shuhuda kwa Wachungaji na Watendakazi wa Injili*, uk. 310. {VSSsw 251.2}

Athari ya Maneno Makavu—Wengi hufanya kosa katika kuhubiri kwa kutosimama wakati shauku bado iko juu. Huendelea kuzungumza mpaka ile hamu iliyokuwa imeamka katika akili za wasikilizaji inapotea, na watu huchoshwa kabisa na maneno yasiyo na uzito wala mvuto maalumu. Simama kabla hujafikia hatua hiyo. Simama/stop wakati huna jambo la muhimu zaidi la kusema. Usiendelee kutumia maneno makavu ambayo huamsha tu upinzani na hayalainishi moyo. Unapaswa kuwa na uhusiano wa karibu sana na Kristo kiasi kwamba maneno yako yaweze kuyeyusha na kupenya hadi moyoni. Mazungumzo matupu pekee hayatoshi kwa wakati huu. Hoja ni nzuri, lakini kunaweza kuwa na hoja nyingi mno na kuwa na upungufu wa Roho na uzima wa Mungu. —[Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 3, uk. 419. {VSSsw 252.1}

Maandalizi Bora, Mahubiri Mafupi Zaidi—Mahubiri yanayowasilisha Ukweli wa sasa huwa na mambo mengi muhimu; na ikiwa yatafanyiwa tafakari kwa makini kabla ya kuwasilishwa kwa watu, yakafupishwa bila kujumuisha eneo kubwa mno, na ikiwa Roho wa Bwana ataambatana na maneno hayo, hakuna mtu atakayeachwa gizani wala atakayekuwa na sababu ya kulalamika kwamba hakulishwa kiroho. Maandalizi, kwa upande wa mhubiri na msikilizaji pia, yana mchango mkubwa katika matokeo yatakayopatikana. {VSSsw 252.2}

Hapa nitanukuu maneno machache yaliyonifikia hivi karibuni: “*Daima ninaweza kujua kutokana na urefu wa mahubiri ya Cannon kama amekuwa mbali na nyumbani kwa muda wa wiki hiyo,*” alisema mmoja wa washiriki wake. “*Anapoyafanyia maandalizi ya kutosha, mahubiri yake huwa na urefu wa wastani, lakini ni vigumu sana kwa wasikilizaji wake kusahau mafundisho yaliyomo ndani yake; lakini anapokosa muda wa maandalizi, mahubiri yake huwa marefu kupita kiasi, na vilevile huwa vigumu kupata jambo lolote kutoka humo litakalobaki katika kumbukumbu.*” {VSSsw 252.3}

Mhudumu mwingine mwenye uwezo aliulizwa ni muda gani kwa kawaida alikuwa akihubiri. Akajibu: *“Ninapojitayarisha kwa ukamilifu, nusu saa; ninapokuwa nimejitayarisha kwa kiasi fulani, saa moja; lakini ninapoingia madhabahuni bila maandalizi ya awali, naweza kuendelea kuzungumza muda wowote utakaotaka; kwa kweli, sijui hata ni lini ninapaswa kuacha.”* {VSSw 253.1}

Hapa kuna kauli nyingine yenye nguvu: *“Mchungaji mzuri,”* asema mwandishi mmoja, *“anapaswa kuwa na mkoba wake uliojaa mkate wa kutosha, na mbwa wake awe chini ya uthibiti wake. Mbwa huyo ni bidii yake, ambayo anapaswa kuiongoza, kuipanga, na kuidhibiti. Mkoba wake uliojaa mkate ni akili yake iliyojaa maarifa yenye manufaa; naye anapaswa kuwa tayari daima kuwapa kundi lake chakula cha kiroho.”*—*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 175–176. {VSSw 253.2}

Matumizi Yasiyo ya Lazima ya Nguvu za Uhai—Baadhi huomba kwa muda mrefu sana na kwa sauti kubwa sana, jambo ambalo huchosha sana nguvu zao dhaifu na kutumia bila sababu nguvu zao za uhai; wengine mara nyingi huongeza urefu wa mahubiri yao kwa theluthi moja au nusu zaidi ya muda unaopaswa kutumika. Kwa kufanya hivyo, wao huchoka kupita kiasi, shauku ya watu hupungua kabla mahubiri hayajaisha, na mambo mengi hupotea kwa sababu wasikilizaji hawawezi kuyahifadhi. Nusu ya yale yaliyosemwa yangukuwa bora zaidi kuliko kusema mengi zaidi; na ingawa mambo yote yaliyowasilishwa yanaweza kuwa muhimu, mafanikio yangukuwa makubwa zaidi ikiwa maombi na mazungumzo yangukuwa mafupi zaidi. Matokeo yangepatikana bila kuwachosha watu kupita kiasi. Wanatumia bila sababu nguvu zao na uwezo wao wa kimwili, ambao kwa ajili ya maendeleo ya kazi ya Mungu ni muhimu sana kuahifadhi; kwa maana ni juhudi ndefu zinazoendelea baada ya kufikia hatua ya kuchoka ndizo zinazodhoofisha na kuvunja nguvu. — [Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 2, uk. 116–117. {VSS 253.3}

Maombi Marefu Si Sehemu ya Injili—Maombi marefu yanayofanywa na baadhi ya wahudumu yamekuwa kushindwa kukubwa. Kuomba kwa muda mrefu kupita kiasi, kama wengine wanavyofanya, si jambo linalofaa; kwa maana huchosha koo na viungo vya sauti, kisha wao hulalamika kwamba wamechoka kwa sababu ya kazi

ngumu. Wanajiumiza wenyewe bila sababu ya msingi. Wengi huhisi kwamba kuomba huathiri vibaya viungo vya sauti kuliko kuzungumza; jambo hili hutokana na mkao usio wa kawaida wa mwili na namna ya kuinamisha kichwa wakati wa kuomba. Wanaweza kusimama na kuzungumza bila kupata madhara hayo. Mkao wa mwili wakati wa kuomba unapaswa kuwa wa kawaida kabisa. Maombi marefu huchosha na hayapatani na Injili ya Kristo. Nusu saa au hata robo saa ni muda mrefu mno; dakika chache zinatoshia kumweleza Mungu mahitaji yako na kumwambia unachotaka, na unaweza kuwashirikisha watu katika maombi hayo bila kuwachosha wala kupunguza shauku yao katika ibada na maombi. Badala yake, wanaweza kuburudishwa na kutiwa nguvu badala ya kudhoofishwa. {VSS 254.1}

Wengi wamekosea katika ibada zao kwa kufanya maombi marefu na mahubiri marefu kwa sauti ya juu, kwa nguvu za kulazimisha, kwa mkazo usio wa kawaida, na kwa namna ya kuzungumza isiyo ya asili. Mhudumu amejichosha bila sababu na amewatesa watu kwa juhudi ngumu zisizo za lazima. Wahudumu wanapaswa kuzungumza kwa namna itakayowafikia na kuwagusa watu. Mafundisho ya Kristo yalikuwa yenye mvuto na uzito; sauti Yake ilikuwa yenye kupendeza na ya muziki. Je, nasi hatupaswi, kama Kristo, kujifunza kuwa na mvuto katika sauti zetu? — [Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 2, uk. 617. {VSS 254.2}

Hali Maalumu ya Maombi ya Hadharani—Maombi yanayotolewa na wahudumu kabla ya mahubiri yao mara nyingi huwa marefu na yasiyofaa kwa sababu hujumuisha mfululizo wa mambo mengi ambayo hayahusiani na mahitaji ya tukio hilo wala mahitaji ya watu. Maombi ya namna hiyo yanafaa zaidi kufanywa faraghani, lakini hayapaswi kutolewa hadharani, kwa sababu wasikilizaji huchoka na kutamani mhudumu amalize. Ndugu zangu, ambataneni na watu pamoja nanyi katika maombi yenu; nendeni kwa Mwokozi wenu kwa imani, mwambieni kile mnachohitaji katika wakati huo, na mruhusu nafsi yako imwendee Mungu kwa shauku kubwa ikitamani baraka inayohitajika wakati huo. — [Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 5, uk. 201. {VSS 255.1}

Maombi Marefu Faraghani, Maombi Mafupi Hadharani—Maombi marefu huwafanya wale wanaosikiliza wachoke na hayawaandai watu kupokea mafundisho yatakayofuata. {VSS 255.2}

Mara nyingi, sababu ya maombi marefu na yenye kuchosha yanayotolewa hadharani ni kupuuzwa kwa maombi ya faragha. Kwa hiyo, wahudumu wasijaribu

katika maombi yao kuorodhesha majukumu waliyoyapuuza kwa juma zima, wakitumaini kufidia uzembe wao na kutuliza dhamiri zao, kwa maana maombi ya namna hiyo mara nyingi husababisha kuwashusha wengine katika kiwango cha chini cha maisha ya kiroho.—*Watendakazi wa Injili*, uk. 176. **{VSS 255.3}**

Kwa Watoto, Kurudia Mara kwa Mara Ni Bora Kuliko Urefu—Wale wanaowafundisha watoto wanapaswa kuepuka maelezo marefu na yanayochosha, kwa sababu maelezo mafupi yanayolenga moja kwa moja jambo kuu huwa na ushawishi mzuri. Ikiwa kuna mengi ya kusema, yafidie kwa kuyasema mara nyingi zaidi, kwa kuwa maneno machache yenye kuvutia yanayotolewa mara kwa mara huwa na manufaa zaidi kuliko kusema kila kitu kwa wakati mmoja. Hotuba ndefu huwa mzigo kwa akili changa za watoto, na maneno mengi sana yanaweza kuwafanya hata wachukie mafundisho ya kiroho, kama vile kula kupita kiasi kunavyolemea tumbo na kupunguza hamu ya chakula, hata kufikia hatua ya kuchukia chakula. Vivyo hivyo, akili za watu zinaweza kujazwa kupita kiasi kwa wingi wa maneno. Kazi kwa ajili ya kanisa, lakini hasa kwa ajili ya vijana, inapaswa kufanywa mstari kwa mstari, amri juu ya amri, hapa kidogo na pale kidogo. Zipeni akili zao muda wa kuyachakata na kuyafahamu Kweli mnazowalisha, kwa sababu watoto wanapaswa kuvutwa kuelekea mbinguni si kwa haraka wala kwa nguvu, bali kwa upole mkubwa. —[Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 2, uk. 420. **{VSS 256.1}**

Uboru Bora Pekee—Mwalimu, ondoa katika mazungumzo yako kila jambo lisilo la kiwango cha juu na bora kabisa, na waweke mbele wanafunzi mambo yale tu yaliyo ya msingi na ya lazima. Kamwe daktari, mchungaji, au mwalimu hapaswi kurefusha mazungumzo yake kiasi kwamba mambo ya msingi yasahaulike katika maelezo marefu yasiyo na manufaa yoyote, kwa sababu jambo hilo linapotokea, akili huzidiwa na wingi wa maneno ambayo haiwezi kuyahifadhi. Kwa hiyo, mazungumzo yanayotolewa yanapaswa kuwa mafupi na yenye kulenga moja kwa moja jambo kuu. —**Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi**, uk. 403. **{VSS 256.2}**

Maneno Machache na Yaliyochaguliwa Vizuri ya Walimu—Walimu, kutaneni na madarasa yenu, ombeni pamoja nao, na wafundisheni wanafunzi jinsi ya kuomba. Mioyo yao iwe laini, na maombi yao yawe mafupi na rahisi, lakini yenye bidii.

Maneno yenu yawe machache na yaliyochaguliwa vizuri, ili wajifunze kutoka katika midomo yenu na mfano wenu kwamba Ukweli wa Mungu lazima ukitie mizizi ndani ya mioyo yao; vinginevyo, hawawezi kusimama mbele ya majaribu. Tunatamani kuona madarasa yote ya vijana yakimgeukia Mungu na kukua kuwa washiriki wenye manufaa katika kanisa.—*Mashauri Kuhusu Kazi ya Shule ya Sabato*, uk. 125. {VSS 256.3}

SURA YA 45—KASI NA TONI YA SAUTI

Kurekebisha Kuzungumza kwa Haraka—Kuzungumza kwa haraka ni kasoro inayoweza na inayopaswa kurekebisha. Mwalimu anapaswa kujifunza kila siku katika shule ya Kristo ili aweze kuzungumza kwa namna itakayoweka mvuto bora na wa kudumu zaidi kwa wasikilizaji wake; kwa kuwa akiwa mlinzi aliyewekwa kusimamia Ukweli, anapaswa kulinda kwa uaminifu hazina takatifu alizokabidhiwa. Hatakiwi kukusanya idadi ndogo tu ya kweli za juu juu, bali anapaswa kuununua ule “uwanja” wote ili aweze kumiliki hazina iliyomo ndani yake. Anapaswa kutafuta

kuboresha mbinu zake za kazi na kutumia kwa ufanisi mkubwa viungo vyake vya usemi. Ikiwa maneno ya Ukweli yana umuhimu wa kutosha kusemwa mbele ya kusanyiko, basi yana umuhimu wa kutosha kusemwa kwa uwazi na kwa kueleweka. Uongozi wa Roho wa Mungu hauwezi kamwe kumwongoza mtu kuzungumza kwa namna isiyoeleweka; kwa maana Roho huchukua mambo ya Mungu na kuyawasilisha kwa watu kupitia chombo cha kibinadamu. Kwa hiyo, maneno hayo yanapaswa kutoka midomoni mwetu kwa namna iliyo bora kabisa iwezekanavyo. —*Kazi ya Kusini-ya Watu weusi-Watumwa*, Oktoba 27, 1903. {VSS 258.1}

Makosa ya Kiwango cha Sauti na Kasi ya Kuzungumza—Bwana anakusudia kwamba kila mhudumu afikie ukamilifu katika kazi yake kwa kushinda kila jambo linaloweza kupunguza ushawishi wake katika sauti, mkao wa mwili, au namna ya kuwasilisha ujumbe. Hili ni jukumu lake kufanya, kwa maana Kristo amesema: *“Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.”* (Mathayo 5:48) {VSS 258.2}

Ni jambo la kawaida kutarajia mafanikio makubwa zaidi kutoka kwa huduma ya mtu ambaye namna yake ya kuzungumza na sauti yake vinavutia kuliko kutoka kwa mtu ambaye mwenendo wake wa kuwasilisha ujumbe haupendezi. Watu wawili wanaweza kutumia Maandiko yale yale na kutoa ushuhuda kamili wa Injili; lakini mmoja wao, kwa sababu amekuwa mwangalifu kurekebisha matamshi yake yenye kasoro na kujifunza kuitawala sauti yake bila kuipandisha kwenye mlilo wa juu kupita kiasi, anaweza kuwa mtenda kazi mwenye mafanikio makubwa. Mwingine anaweza kuwa na maarifa ya Neno la Mungu, lakini akaacha kwa wasikilizaji wake mguso wa hisia isiyopendeza kwa sababu anaonekana kuwa na msisimko kupita kiasi; hivyo wote wanaomsikia hutamani atulie na kuzungumza kwa bidii, lakini kwa utulivu na bila msisimko usio wa lazima. {VSS 259.1}

Kwa kuzungumza kwa sauti ya juu sana, msemaji hupunguza kwa kiasi kikubwa ufanisi wa huduma yake. Wengine huzungumza kwa sauti ya chini sana kiasi kwamba maneno yao hayasikiki vizuri; wengine tena huzungumza kwa haraka sana, wakikimbiza neno moja juu ya jingine, na hivyo nusu ya yale wanayosema hupotea kwa sababu msikilizaji hawezi kuyapokea na kuyaelewa maneno yenye thamani yanayotoka midomoni mwao. Hizi ni kasoro zinazopaswa kushindwa. {VSS 259.2}

Inapaswa kujengwa tabia ya kuzungumza polepole, lakini kwa dhati na bidii na kwa uzito, huku kukiwa na uhakika wote ambao Neno la Mungu linaweza kutoa. Kwa njia hiyo, msikilizaji atafaidika na kila sentensi, kwa sababu kila neno litasemwa kwa uwazi na litaacha mvuto wake katika akili za wasikilizaji. Kuzungumza kwa haraka na kupandisha sauti katika kiwango cha juu ni kasoro ambayo kila mtu anapaswa kuishinda ikiwa anataka kutoa ujumbe wa Mungu kwa namna itakayoweka mvuto bora zaidi kwa ulimwengu na kupata kibali. Liruhusu Neno la Mungu litoke kama harufu ya uzima iletayo uzima. {VSS 259.3}

Ikiwa watumishi wa Mungu watalifikiria jambo hili kwa busara, wakijitia chini ya uongozi wa akili timamu na hukumu nzuri, wataona kwamba kasoro hizi hazipaswi kuendelea kuwepo. Watatambua kwamba kasoro hizo zinaweza kushindwa, na kwamba juhudi zao mimbarani zitakuwa na faida kubwa zaidi kwa wasikilizaji na zitawachosha wao wenyewe kwa kiwango kidogo zaidi. Kila mhudumu anapaswa kukumbuka kwamba anawapa watu ujumbe ambao Mungu amemkabidhi, na kwamba ujumbe huo unahusisha masuala ya milele.—*Manuscript 4*, 1897. {VSS 260.1}

Kweli Iliyopunguzwa Thamani—Iseme Kweli kwa upendo na kwa kuwahurumia wale wanaoiacha Kweli na kugeukia hekaya za kubuni. Kumbuka kwamba Bwana Yesu Yupo katika mikutano yenu. Anataka mdhihirishe heshima, utulivu na utengemano wa roho. Unapokimbiza neno moja mara baada ya jingine, nusu ya nguvu ya hotuba yako hupotea.—[Letter 8, 1894](#). {VSS 260.2}

Maagizo ya Mungu kwa Ellen White Kuhusu Sauti—Nina maneno ya tahadhari kwa ajili yako, ambayo ninayarudia kwako wakati wa usiku. Nilikuwa nikisema hivi: “Nina ujumbe kwa ajili yako kutoka kwa Bwana. Vitunze na viendeleze viungo vyako vya sauti. Hili ni fursa yako na wajibu wako. Sauti ni hazina yenye thamani sana. Mara nyingi wewe huzungumza kwa haraka mno. Maneno yanajazana na kusongana kwa haraka sana, neno likifuatana na neno, na usemi wako hukosa uwazi na utamkaji ulio dhahiri unaopaswa kuwa nao.” {VSS 260.3}

Kwa kuwa unazungumza mbele ya makusanyiko makubwa kama unavyofanya, ni wajibu wako kuvipatia viungo vyako vya sauti mapumziko yote yanayowezekana. Unapozungumza, vuta pumzi ndefu na za kina. Tumia misuli ya tumbo, na kwa njia hiyo uhamishie misuli hiyo mzigo ambao sasa unaweka kwenye koo na mapafu. {VSS 261.1}

Bwana hataki uviharibu viungo vyako vya sauti kwa kuvitumia kwa mkazo mkubwa kwa muda mrefu bila mapumziko. Maneno yako yatakuwa na nguvu zaidi ikiwa utavuta hewa zaidi ndani ya mapafu yako na kusema maneno machache zaidi. Unapozungumza, unahitaji kutenga muda wa kuvuta pumzi ndefu na za kina. Tumia misuli ya tumbo katika tendo hilo. Simama wima, vuta pumzi kwa kina, na tamka maneno yako kwa nguvu kadiri unavyotaka. **{VSS 261.2}**

Nilifundishwa somo hili wakati koo langu na mapafu yangu yalikuwa yameathirika sana kiasi kwamba sikuweza kupumua bila kuteseka. Hakuna rafiki yeyote wa kibinadamu aliyeniambia la kufanya ili kuboresha hali hiyo; lakini Mmisionari Mkuu wa Tiba, ninayempenda na kumtii, aliniambia nilichopaswa kufanya. Maagizo niliyopewa, nami ninawapa ninyi. Umuhimu wa mafunzo ya sauti ulisisitizwa sana kwangu, na tangu wakati huo nimejaribu kuwasisitizia wengine umuhimu huo. Wachungaji wetu na wazungumze polepole, wakivuta pumzi ndefu na za kutosha, na sauti zao zitakuwa na mdundo wa kimuziki ambao sasa unasikika katika sauti za watu wachache tu, kwa sababu ni vigumu kuacha mazoea mabaya na kuyabadilisha kwa mazoea mema. **{VSS 261.3}**

Mungu anataka watenda kazi Wake wavitunze viungo vyao vya sauti kwa uangalifu wa pekee, kama zawadi yenye thamani kutoka Kwake. Viungo hivi havipaswi kuvinyanyasa wa kuvitumia kupita kiasi wala kulazimishwa kufanya kazi kupita kiwango vinachoweza kustahimili. Uangalifu mkubwa unapaswa kuonyeshwa katika kuvitumia. Ndipo hotuba zitakazotolewa zitakuwa na mvuto zaidi, na wale wanaozungumza watawezesha kufanya kazi zaidi kwa ajili ya Bwana. Wapo watu ambao wamekwenda kaburini kwa sababu hawakujitahidi kupatana na sheria za asili katika matumizi ya viungo vyao vya sauti. **{VSS 261.4}**

Bwana anataka wajumbe Wake walinde kwa uangalifu mkubwa afya na nguvu zao. Hawapaswi kuharibu viungo vyao walivyopewa na Mungu kwa kuvitumia vibaya. Kiungo kimoja hakipaswi kutiwa mkazo kupita kiasi, wala kubebeshwa mzigo wa matumizi mabaya ambao utasababisha ugonjwa na kufupisha kipindi ambacho watenda kazi wanaweza kuwa na manufaa. **{VSS 262.1}**

Bwana anataka mboreshe usemi wenu kwa kuweka mzigo mahali unapopaswa kuwa, yaani, kwenye misuli ya kifua na tumbo. Koo ni njia tu ya kupitishia maneno. Zungumza polepole na vuta pumzi kwa kina. Hili litawawezesha kutamka maneno yenu kwa uwazi na kwa nguvu ya kutosha ya sauti, huku koo na

mapafu yenu, badala ya kuathirika, yakiimarishwa ili kustahimili mwelekeo wa kupata kifua kikuu. **{VSS 262.2}**

Ni fursa yako kujifunza mafunzo ya sauti, ikiwa inawezekana. Mafunzo ya sauti ni somo linalopaswa kupewa nafasi katika kila taasisi ya kuwaelimisha vijana. Somo hili ni muhimu hasa kwa wale wanaojiandaa kutumika kama walimu au wahudumu. Katika kila eneo la masomo, umuhimu wa kuzungumza polepole na kwa uwazi, na wa kuweka mzigo kwenye misuli ya tumbo, unapaswa kusisitizwa. Mafunzo haya yanapaswa kufanywa kuwa eneo maalumu katika kila shule. Wanafunzi wanapaswa kufundishwa kusimama wima, kuvuta pumzi kwa kina, na kuweka msisitizo unaofaa kwenye maneno na sentensi muhimu.... **{VSS 262.3}**

Yatafakarini mapendekezo haya. Yapeni uangalifu unaostahili, kwa maana ili kuhifadhi maisha yenu mwahitaji mfanye hivyo. Mwanadamu anapaswa kufanya yote yaliyo katika uwezo wake ili kuhifadhi afya na nguvu zake. Mhudumu wa Injili anapaswa kuyatunza kwa uangalifu wa pekee viungo vya usemi, akilinda koo kwa kila namna inayowezekana, ili lisije likawashwa au kukerwa. Ni lazima atenge muda wa kupumzika. Ndipo viungo vyake vya sauti havitatumiwa kupita kiasi kiasi cha kuathirika kwa ugonjwa usioweza kutibiwa. **{VSS 263.1}**

Ni lazima nikusihi utumie busara. Unazungumza kwa haraka, na koo lako pamoja na mapafu yako huchoka na kuwashwa/kukwaruzika. Mzee D alikuwa mtu mwenye uwezo mkubwa. Nilijitahidi kadiri niwezavyo kumshawishi aitunze afya yake, lakini hakufuata ushauri wangu. Alisema kwamba hangeweza kufurahia uhuru wa kuzungumza ikiwa angefuata kanuni alizojua kuwa muhimu kwa afya ya viungo vyake vya sauti. Nguvu ya mazoea ilikuwa kubwa sana kiasi kwamba hakubadilika. Alipokuwa akifa, aliomba mume wangu na mimi tuje kumwombea. Tulipokuwa pamoja naye, alisema: “Ee, Dada White, nisingekuwa nakufa sasa kama ningetii maonyo uliyonipa.”—[Letter 367, 1904](#). **{VSS 263.2}**

Kelele na Haraka Si Ushahidi wa Uwepo wa Mungu—Baadhi ya wahudumu wameangukia katika kosa la kudhani kwamba hawawezi kuzungumza kwa uhuru isipokuwa wapandishe sauti zao hadi kwenye toni ya juu na wazungumze kwa sauti kubwa na kwa haraka. Watu kama hao wanapaswa kuelewa kwamba kelele na kuzungumza kwa sauti ya juu na kwa haraka si ushahidi kwamba nguvu za Mungu zipo. Si nguvu ya sauti dniyo inayofanya athari ya kudumu. Wahudumu wanapaswa kuwa wanafunzi wa Biblia na kujipatia kwa kina sababu za imani na

tumaini letu; kisha, wakiwa na udhibiti kamili wa sauti zao na hisia zao, wanapaswa kuwasilisha sababu hizo kwa namna ambayo watu wanaweza kuzipima kwa utulivu na kuamua kwa kuzingatia ushahidi uliotolewa. Na wahudumu wanapohisi nguvu ya hoja wanazowasilisha katika mfumo wa Ukweli wenye uzito na unaowajaribu watu, watakuwa na bidii na umakini unaolingana na maarifa.—[Shuhuda ka Kanisa 1:645](#). {VSS 263.3}

Uuvvio wa Uongo—Baadhi yao wanaonekana kufikiri kwamba ni lazima waendeleo kuzungumza kwa kasi bila kusita, la sivyo watapoteza uvuvio walio nao na watu nao watapoteza uvuvio huo. Ikiwa huo ndio uvuvio, basi waache waupoteze uvuvio huo; na ni afadhali wauache mapema iwezekanavyo.—

[Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, 670](#). {VSS 264.1}

Kuvuruga Umakini kwa Vitendo vya Mwili—Pia kuna wahudumu wenye ushupavu wa kupindukia, ambao wanapojaribu kumhubiri Kristo, hupiga kelele, hupaza sauti, huruka-ruka huku na huko, na kugonga-gonga meza iliyo mbele yao, kana kwamba mazoezi hayo ya mwili yana manufaa yoyote [roudy, boisterious]. Vitendo kama hivyo haviziipika nguvu zaidi Kweli zinazotamkwa; bali, kinyume chake, huwachukiza wanaume na wanawake wenye uamuzi wa busara na mitazamo ya juu. Ni wajibu wa watu wanaojitoa katika huduma kuacha kila aina ya ukorofi na tabia ya makelele nje ya mimbari, angalau.—[Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, 640](#). {VSS 264.2}

Sauti ya Kunung'unika Si Ushahidi wa Unyenyekevu—Kuna kundi lingine linalowahutubia watu kwa sauti kunungunika [whining]. Mioyo yao haijalainishwa na Roho wa Mungu, nao hudhani kwamba lazima waache athari fulani kwa watu kwa kuonekana wanyenyekevu. Mwenendo huo hauinui huduma ya Injili, bali huishusha na kuidhalilisha. Wahudumu wanapaswa kuwasilisha Kweli ikiwa na joto linalotoka katika utukufu wa Mungu. Wanapaswa kuzungumza kwa namna inayomwakilisha Kristo ipasavyo na kuhifadhi heshima inayowastahili wahudumu Wake.—[Shuhuda ka Kanisa 2:617](#). {VSS 264.3}

Maombi Yasiyosikika Humfurahisha Shetani—Katika mikutano ya kijamii kuna hitaji maalumu la kutamka maneno kwa uwazi na kwa kueleweka ili wote waweze kusikia ushuhuda unaotolewa na kunufaika nao, kwa sababu shida huondolewa na msaada hutolewa wakati watu wa Mungu wanaposimulia uzoefu wao katika mikutano hiyo; lakini mara nyingi ushuhuda hutolewa kwa matamshi yenye kasoro na yasiyoeleweka vizuri kiasi kwamba haiwezekani kupata wazo sahihi la kile kinachosemwa, na kwa sababu hiyo baraka nyingi hupotea. **{VSS 265.1}**

Wale wanaoomba na wale wanaozungumza wanapaswa kutamka maneno yao kwa usahihi na kuzungumza kwa sauti iliyo wazi, inayoeleweka na yenye mpangilio unaofaa, kwa maana maombi yakitolewa kwa namna inayofaa huwa ni nguvu ya kutenda mema na ni mojawapo ya njia ambazo Bwana hutumia kuwafikishia watu hazina za thamani za Ukweli; lakini mara nyingi maombi hayafikii kusudi lake kwa sababu ya udhaifu wa sauti za wale wanaoomba. Shetani hufurahi wakati maombi yanayotolewa kwa Mungu hayasikiki vizuri; kwa hiyo, watu wa Mungu wajifunze namna ya kuzungumza na kuomba kwa njia itakayowakilisha kwa usahihi kweli kuu walizo nazo. Acha ushuhuda unaotolewa na maombi yanayotolewa yawe wazi na yenye kueleweka, ili kwa njia hiyo Mungu atukuzwe. —[Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 6, uk. 382. **{VSS 265.2}**

Uwazi Katika Kusoma Hadharani—Ni jambo la muhimu kwamba wanafunzi wafundishwe kusoma kwa sauti iliyo wazi na yenye kueleweka, kwa sababu tumekuwa tukisikitishwa mara nyingi tunapohudhuria mikutano ya konferensi, mikutano ya jumuiya za machapisho, na mikutano mbalimbali ambapo taarifa zimesomwa kwa sauti iliyokaribia kutosikika, kwa kusitasita, au kwa sauti iliyofifia na isiyoeleweka. Nusu ya mvuto wa mkutano hupotea wakati washiriki wanapotekeleza wajibu wao kwa namna ya kutojali na isiyo na nguvu; hivyo wanapaswa kujifunza kuzungumza kwa namna itakayowajenga wale wanaowasikiliza. Hebu kila mtu anayehusika katika kazi ya umisionari anapaswa kujitayarisha kuzungumza kwa njia iliyo wazi, kujipatia stahiki, yenye mvuto, na kutamka maneno yake kwa ukamilifu. —**Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi**, uk. 246–247. **{VSS 265.3}**

Msemaji wa Mungu—Yeye anayekubali nafasi ya kuwa msemaji wa Mungu anapaswa kuona kuwa ni jambo la muhimu sana kuwasilisha Ukweli kwa neema na hekima anayoweza kuzipata kupitia mafunzo ya akili, na kwa namna ambayo Ukweli hautapoteza chochote kutokana na jinsi anavyowasilisha; kwa hiyo, mtu yeyote asidhani kuwa ni jambo dogo kuzungumza kwa sauti nzito isiyoeleweka na kwa namna isiyo na ustadi, au kuinua sauti katika kiwango cha juu kisicho cha kawaida kisha kuzungumza kwa sauti kubwa na kwa muda mrefu kiasi cha kutumia vibaya viungo vya usemi alivyokabidhiwa na Mungu na hivyo kujifanya asikubalike mbele ya watu. —*Manuscript 67*, 1895. {VSS 266.1}

Ukweli Usipotoshwe kwa Matamshi Yenye Kasoro—Uwezo wa kuzungumza kwa uwazi na kueleweka, kwa sauti kamili na yenye mvuto, ni wa thamani katika kila aina ya kazi, na sifa hii ni ya lazima kwa wale wanaotamani kuwa wahudumu, wainjilisti, wafanyakazi wa Biblia, au wauzaji wa vitabu. Wale wanaopanga kuingia katika maeneo haya ya kazi wanapaswa kufundishwa kutumia sauti zao kwa namna ambayo wanapozungumza na watu kuhusu Ukweli wataweka mvuto thabiti wa mema, kwa sababu Ukweli haupaswi kuharibiwa kwa kuwasilishwa kupitia matamshi yenye kasoro. —[Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 6, uk. 380. {VSSw 266.2}

Namna ya Kuzungumza kwa Wafanyakazi Wote—Watendakazi wote, iwe wanahubiri madhabahuni au wanatoa masomo ya Biblia, wanapaswa kufundishwa kuzungumza kwa njia iliyo wazi na yenye kuonyesha maana. —[Enendeni](#)

[Mtandaoni Kote-Uinjilisti](#), uk. 665. {VSSw 267.1}

Ujasiri Mtakatifu Katika Maombi—Ninaumia ninapona jinsi kipawa cha usemi kinavyothaminiwa kwa kiwango kidogo sana, kwa sababu katika kusoma Biblia, kushiriki katika maombi, na kutoa ushuhuda katika mikutano, ni jambo la muhimu kiasi gani kutamka maneno kwa uwazi na kueleweka! Ni kiasi gani kinachopotea katika ibada za familia wakati yule anayetoa maombi anainamisha uso wake chini na kuzungumza kwa sauti ya chini na dhaifu! Lakini mara tu ibada ya familia inapomalizika, wale ambao hawakuweza kuzungumza kwa sauti ya kutosha kusikika wakati wa kuomba mara nyingi wanaweza kuzungumza kwa sauti iliyo wazi na yenye kueleweka, na hakuna ugumu wowote wa kusikia wanachosema. Maombi yanayotolewa kwa namna hiyo yanafaa kwa maombi ya faragha, lakini hayajengi katika ibada za familia au ibada za hadharani, kwa sababu wale waliokusanyika

wasiposikia kinachosemwa hawawezi kusema *Amina*. Karibu kila mtu anaweza kuzungumza kwa sauti inayosikika katika mazungumzo ya kawaida; kwa hiyo, kwa nini wasizungumze kwa namna hiyo wanapoitwa kutoa ushuhuda au kuomba? **{VSS 267.2}**

Tunapozungumza mambo ya Mungu, kwa nini tusizungumze kwa sauti iliyo wazi na kwa namna itakayoonyesha kwamba tunajua tunachokisema na kwamba hatuoni aibu kusimama upande wetu? Kwa nini tusiombe kana kwamba tuna dhamiri safi isiyo na kosa na tunaweza kufika kwenye kiti cha neema kwa unyenyekevu, lakini pia kwa ujasiri mtakatifu, tukiinua mikono mitakatifu bila hasira wala mashaka? Msiiname vichwa vyenu chini na kufunika nyuso zenu kana kwamba kuna jambo mnalotaka kulificha; bali inueni macho yenu kuelekea Patakatifu pa mbinguni, ambako Kristo Mpatanishi wenu anasimama mbele za Baba ili kuwasilisha maombi yenu, yakiwa yamechanganywa na Stahiki na sifa Zake Mwenyewe na haki Yake isiyo na doa, kama uvumba wenye harufu nzuri. —**Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi**, uk. 241. **{VSS 267.3}**

SURA YA 46—VISA NA UCHESHI

Ucheshi Usiofaa Katika Huduma—Mhudumu wa Mungu hapaswi kusema maneno yatakayochochea mzaha au kuleta hali ya kutojali mambo matakatifu, kwa maana sisi tumenunuliwa kwa gharama kubwa sana, yaani kwa dhabihu kuu ya Mwana wa pekee wa Mungu. —*Manuscript 19*, 1910. {VSS 269.1}

Mhudumu wa Injili anayefanya kazi pamoja na Mungu anapaswa kujifunza kila siku katika shule ya Kristo; kwa hiyo, kutoka midomoni mwake hayapaswi kutoka maneno mepesi au yasiyo na uzito, kwa maana yeye ni balozi wa Kristo anayebeba ujumbe wa Mungu kwa roho zinazopotea. Kila mzaha, utani, maneno ya kijuujuu, na mwenendo wa kutojali mambo matakatifu ni mambo yanayoumiza kwa mwanafunzi wa Kristo anayebeba msalaba. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 206–207. {VSS 269.2}

Neno la Mungu linakataza kabisa kila aina ya maneno mepesi na mazungumzo yasiyo na maana. Mazungumzo ya mhudumu yanapaswa kuelekezwa katika mambo ya mbinguni, na maneno yake yanapaswa kutiwa ladha ya neema. —*Shuhuda ka Kanisa*, juz. 2, uk. 338. {VSS 269.3}

Mfano Unaostahili kwa Vijana—Wahudumu wanapaswa kuwawekea vijana mfano unaostahili unaolingana na wito wao mtakatifu. Wanapaswa kuondoa kila aina ya ukorofi, mzaha, na mwenendo usiofaa, wakikumbuka daima kwamba wao ni waelimishaji; na kwamba, wawe wanataka au hawataki, maneno na matendo yao huwa kwa wale wanaokutana nao harufu ya uzima iletayo uzima au ya mauti iletayo mauti. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 126. {VSS 269.4}

Heshima Katika Madhabahu Takatifu-Decorum—Mhudumu anaweza kufanya nini bila Kristo? Hakika, hakuna kitu. Kwa hiyo, ikiwa yeye ni mtu wa mzaha na asiyejali mambo matakatifu, hayuko tayari kutekeleza wajibu ambao Bwana amemkabidhi. Kristo amesema: *“Pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo*

lote.” Kwa hiyo, maneno mepesi yanayotoka midomoni mwake, visa visivyo na uzito, na kauli zinazolenga kuwafanya watu wacheke, yote hayo yanahukumiwa na Neno la Mungu na hayafai kabisa katika madhabahu takatifu. —Shuhuda kwa Wachungaji na *Watendakazi wa Injili*, uk. 142. {VSS 270.1}

Hakuna Misemo Isiyo ya Kistaarabu—Mchungaji anapaswa kujitenga na kila msukosuko usio wa lazima wa mambo ya kidunia, ili aweze kujitoa kikamilifu kwa wito wake mtakatifu. Anapaswa kuwa mtu wa maombi mengi na kujitia chini ya nidhamu ya Mungu, ili maisha yake yaonyeshe matunda ya kujitawala nafsi kwa kweli. Lugha yake inapaswa kuwa sahihi; misemo ya mitaani, maneno ya hovyovy, au kauli zisizo na heshima hazipaswi kutoka kinywani mwake. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 145. {VSS 270.2}

Wakiwa Wawakilishi wa Kristo—Wachungaji wanapaswa kuwa waangalifu sana, hasa wanapokuwa mbele ya vijana. Hawapaswi kutumia usemi mwepesi, kufanya masihara wala kutania, bali wanapaswa kukumbuka kwamba wanamwakilisha Kristo na kwamba wanapaswa kuonyesha maisha ya Kristo kwa mfano wao. —[Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 1, uk. 380–381. {VSS 270.3}

Hakuna Utani Madhabahuni—Mhudumu ambaye yuko tayari kushiriki katika mazungumzo yasiyo na maana, kufanya mzaha, na kucheka ovyo, haelewi wajibu mtakatifu unaomkabili. Na ikiwa kutoka katika hali hiyo ataingia madhabahuni, Bwana hawezi kusimama pamoja naye ili kumbariki. Hotuba zenye maneno yaliyopambwa kwa ustadi pekee hazitoshi kuilisha roho ya mtoto wa Mungu mwenye njaa ya kiroho. —*The Review and Herald*, Juni 23, 1891. {VSS 270.4}

Maneno Yenye Ladha ya Neema—Mazungumzo mepesi na utani yaondolewe katika usemi wa mhudumu; bali maneno yake yajazwe neema. Mwanga na upendo wa Yesu uangaze katika mfano wake na mafundisho yake, ili roho zipate kushindwa na kuvutwa kwa ajili ya Bwana. —*The Review and Herald*, Aprili 5, 1892. {VSS 271.1}

Matumizi Mabaya ya Injili—Baadhi ya watu wanaosimama madhabahuni huwafanya wajumbe wa mbinguni waliopo katika kusanyiko kuona aibu. Injili ya thamani kubwa, ambayo iligharimu sana kuifikisha kwa ulimwengu, inatumiwa vibaya. Kuna mazungumzo ya kawaida yasiyo na thamani, mikao na mienendo ya kuchekesha isiyofaa, pamoja na matumizi yasiyofaa ya sura na mwili. Kwa wengine

kuna kuzungumza kwa haraka sana, na kwa wengine kuna matamshi mazito yasiyoeleweka. —Shuhuda kwa Wachungaji na *Watendakazi wa Injili*, uk. 339. **{VSS 271.2}**

Maneno ya Kawaida Yaliyobuniwa na Wanadamu—Ujumbe wa Ukweli unapaswa kulindwa kabisa dhidi ya maneno ya kawaida yasiyo na uzito na ya bei rahisi yaliyobuniwa na wanadamu. Kwa kufanya hivyo, mvuto wenye nguvu utaonekana katika mioyo ya watu. Wahudumu wasijidanganye kwamba lazima walete jambo jipya na la kushangaza, au kwamba maneno mepesi na yasiyo na thamani yatawapa ushawishi. Wahudumu wanapaswa kuwa vinywa vya Mungu, hivyo wanapaswa kuondoa katika usemi wao kila kauli ya bei rahisi-ovyo/cheap au ya kawaida. Wanapaswa kuwa waangalifu wasije wakajaribu kuwafanya watu wacheke wakati wa mahubiri yao na hivyo kumvunjia Mungu heshima. **{VSS 271.3}**

Ujumbe wetu ni wa dhati na mtakatifu, kwa hiyo tunapaswa kukesha katika maombi. Maneno yanayosemwa yanapaswa kuwa ya aina ambayo kupitia hayo Mungu anaweza kufanya mvuto katika mioyo na akili za watu. Wahudumu wa Injili wanapaswa kutakaswa kwa njia ya Ukweli. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 211. **{VSS 272.1}**

Katika Eneo la Adui—Mara mhubiri anaposhuka kutoka katika nafasi ya heshima ambayo mhudumu anapaswa kuishikilia daima, na kugeukia mambo ya kuchekesha ili kumfanya mpinzani wake acheke, au anapotumia kejeli, ukali, na maneno ya kudharau, anafanya jambo ambalo Mwokozi wa ulimwengu hakuthubutu kufanya; kwa maana anajiweka katika eneo la adui. —*Shuhuda ka Kanisa*, juz. 3, uk. 220. **{VSS 272.2}**

Chakula Safi Bila Makapi—Kuhubiri Neno kunapaswa kugusa akili na kutoa maarifa, lakini kunapaswa kufanya zaidi ya hayo; maneno ya mchungaji yanapaswa kufikia mioyo ya wasikilizaji. Lengo la mahubiri si kuwaburudisha watu. Baadhi ya wachungaji wamezoea kutumia mtindo wa mahubiri ambao hauna ushawishi bora. Wamekuwa na desturi ya kuingiza visa/anecdotes mbalimbali katika mahubiri yao, lakini mvuto unaobaki kwa wasikilizaji kutokana na mtindo huo si harufu ya uzima iletayo uzima. Wahudumu hawapaswi kuleta hadithi za kuchekesha katika mahubiri yao. Watu wanahitaji chakula safi cha kiroho, kilichosafishwa kabisa na makapi.

Paulo alimpa Timotheo agizo hili: **“Lihubiri Neno.”** Hilo ndilo agizo letu pia. {VSS 272.3}

Mhudumu anayechanganya simulizi ya hekaya na mahubiri yake anatumia moto wa kigeni. Mungu anakerwa, na kazi ya Ukweli inadharauliwa, wakati wawakilishi Wake wanaposhuka hadi kutumia maneno mepesi na yasiyo na uzito au ya ovyo.

—*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 211. {VSSw 273.1}

Ndugu zangu, Mwokozi wetu anawataka muwe waangalifu katika namna mnavyomshuhudia Yeye. Mnapaswa kwenda ndani zaidi na zaidi katika kujifunza Neno la Mungu, kwa kuwa mnayo nafasi ya kukutana na watu wenye aina mbalimbali za fikra; hivyo, mnapofundisha Kwenye Neno takatifu, mnapaswa kuonyesha bidii, heshima, na unyenyekevu. Ondoeni simulizi la hadithi lisilo la lazima katika mahubiri yenu na lihubirini Neno; ndipo mtakapokuwa na miganda mingi zaidi ya kumletea Bwana. Kumbukeni kwamba katika wasikilizaji wenu wapo watu wanaosumbuliwa daima na majaribu; wengine wanapambana na mashaka, wakiwa karibu kufikia kukata tamaa na kupoteza tumaini. Mwombeni Mungu awasaidie kusema maneno yatakayowatia nguvu ili waweze kusimama imara katika mapambano yao. —*The Review and Herald*, Desemba 22, 1904. {VSSw 273.2}

Visa Visivyohusiana na Ujumbe—Wahudumu hawapaswi kufanya kuwa desturi kusimulia visa visivyohusiana na ujumbe katika mahubiri yao, kwa sababu jambo hilo hupunguza nguvu ya Ukweli unaowasilishwa; kwa maana kusimulia visa vifupi vyenye kuchekesha au matukio yanayowafanya wasikilizaji wacheke au kuwafanya wayachukulie mambo kwa wepesi kunastahili kukemewa vikali. Ukweli unapaswa kuvalishwa lugha safi, yenye heshima, na yenye hadhi, na mifano inayotumiwa inapaswa kuwa ya aina hiyo hiyo. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 166. {VSSw 273.3}

Mifano ya Kuchekesha—Mhudumu wa Injili hapaswi kupuuza mwenendo wake; kwa sababu ikiwa yeye ni mwakilishi wa Kristo, tabia yake, mjongeo wa viungo vya mwili, mkao wake wa mwili, na ishara zake vinapaswa kuwa vya namna ambavyo havitamchukiza mtazamaji. Wahudumu wanapaswa kuwa na ustaarabu na adabu, wakiacha kila mwenendo usio na staha, mikao isiyofaa, na ishara zisizostahili; badala yake wajenge ndani yao hadhi ya unyenyekevu. Wanapaswa kuvaa kwa namna inayolingana na heshima ya nafasi yao, na maneno yao yanapaswa kuwa matakatifu, yenye uzito, na yaliyochaguliwa vizuri katika kila hali.

Nimeonyeshwa kwamba ni kosa kutumia maneno makali yasiyo na heshima, kusimulia visa kwa kusudi la kuwaburudisha watu au kuwachekesha, au kutumia mifano ya kuchekeka ili kuwafanya watu wacheke; kwa sababu kejeli, kushushua na kucheza na maneno ya mpinzani havipatani na utaratibu wa Mungu. —[Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 1, uk. 648–649. {VSS 273.4}

Hadithi za Kuburudisha—Ndugu yangu, unahitaji kuchunguza kwa makini zaidi mahubiri unayowasilisha kwa watu, kwa maana kusudi la kazi yako ya huduma si kuwaburudisha watu, wala si kutoa taarifa pekee au kushawishi akili tu. Kuhubiri Neno la Mungu kunapaswa kugusa akili na kutoa maarifa, lakini kunahusisha jambo kubwa zaidi ya hayo; moyo wa mhudumu lazima ufikie na kugusa mioyo ya wasikilizaji.

Baadhi wamezoea mtindo wa mahubiri usio na ushawishi unaofaa, kwa kuwa wamepunguza thamani ya mahubiri yao kwa kuingiza visa mbalimbali. Mvuto unaoachwa kwa wasikilizaji kwa njia hiyo si harufu ya uzima iletayo uzima. Hupaswi kuleta hadithi/anecdotes za kuchekeka katika mahubiri yako, kwa sababu watu wanahitaji chakula safi cha kiroho, kilichosafishwa kabisa kutoka kwa kila kitu kisicho na manufaa ya kiroho. “*Lihubiri Neno*,” ndilo agizo ambalo Paulo alimpa Timotheo, na hilo ndilo agizo lako pia. —*Letter 61*, 1896. {VSS 274.1}

Hakuna Wachekeka/clowns Madhabahuni—Nilikuonya dhidi ya mwenendo wa ucheshi na maigizo katika madhabahu au mbele ya watu. Je, wakati mwingine huleti aina hii ya uigizaji katika madhabahu takatifu? Kwa kufanya hivyo unawapendeza na kuwavutia watu wa ulimwengu. Je, hilo ni ushahidi kwamba una uchaji wa kina wa kiroho, uliotakaswa kwa Mungu kupitia Roho Wake? —*Letter 9*, 1889. {VSS 275.1}

SURA YA 47—MIFANO NA VIFAA VYA KUONEKANA

Lugha Safi na Yenye Heshima—Kweli inapaswa kuvikwa lugha safi na yenye heshima/uungwana; na mifano inayotumiwa inapaswa kuwa ya aina hiyo hiyo.— [Watendakazi wa Injili, 166] **{VSS 276.1}**

Mifano Inayojieleza Wenyewe—Ingekuwa jambo jema ikiwa wachungaji wanaofanya kazi katika Neno au mafundisho wangeweza kwenda mashambani na kutumia sehemu ya siku katika mazoezi ya kimwili pamoja na wanafunzi, kwa sababu wangeweza kufanya kama Kristo alivyofanya, yaani kutumia masomo kutoka katika maumbile kueleza na kufafanua Kweli za Biblia. —*Misingi ya Elimu kwa Kila Mwanadamu*, uk. 325. **{VSS 276.2}**

Kufundisha Kwa Kutumia Mifano—Katika mafundisho ya Kristo yaliyotolewa kwa njia ya mifano, tunaona kanuni ileile iliyodhihirishwa katika utume Wake kwa ulimwengu. Ili tupate kufahamu tabia na maisha Yake ya Kiungu, Kristo alitwaa asili yetu ya kibinadamu na akaishi miongoni mwetu. Uungu ulifunuliwa katika ubinadamu, na utukufu usioonekana ulidhihirishwa kupitia umbo la kibinadamu linaloonekana. Kwa njia hiyo, wanadamu waliweza kujifunza mambo yasiyojulikana kupitia yale yanayojulikana; mambo ya mbinguni yalifunuliwa kupitia mambo ya duniani; na Mungu alidhihirishwa katika mfano wa wanadamu. Ndivyo ilivyokuwa katika mafundisho ya Kristo, ambapo mambo yasiyojulikana yalielezwa kwa kutumia yale yanayojulikana, na Kweli za Kiungu zilifafanuliwa kwa kutumia mambo ya duniani ambayo watu walikuwa wameyazoea sana. **{VSS 276.3}**

Maandiko yanasema: *“Hayo yote Yesu aliwaambia makutano kwa mifano; wala pasipo mfano hakuwaambia Neno; ili litimie Neno lililonenwa na nabii, akisema, Nitafumbua kinywa Changu kwa mifano, Nitayatamka yaliyositirika tangu awali.”* (Mathayo 13:34, 35) Mambo ya asili/nature yalikuwa njia ya kueleza mambo ya kiroho, kwa kuwa vitu vya asili pamoja na uzoefu wa maisha ya wasikilizaji Wake vilihusishwa na Jweli za Neno lililoandikwa. Kwa njia hiyo, akiwavuta watu kutoka katika ufalme wa asili kwenda katika ufalme wa kiroho, mifano ya Kristo ikawa viungo katika mnyororo wa Ukweli unaomunganisha mwanadamu na Mungu, na dunia na mbingu. —*Mifano ya Masihi*, uk. 17–18. **{VSS 277.1}**

Matumizi ya Maandiko—Bwana anataka mjifunze jinsi ya kutumia “wavu wa Injili,” kwa sababu wengi wanahitaji kujifunza ustadi huu. Ili mpate kufanikiwa katika kazi yenu, matundu ya wavu wenu, yaani matumizi ya Maandiko, yanapaswa kuwa ya karibu na yenye kushikilia Kweli, huku maana yake ikiwa rahisi kutambulika. Kwa hiyo, jitahidini kutumia wavu huo kwa ufanisi mkubwa, mkilenga moja kwa moja kwenye jambo kuu na kutumia mifano inayojieleza yenyewe. Kwa maana hata mtu akiwa na maarifa makubwa kiasi gani, hayana faida ikiwa hawezi kuyawasilisha kwa wengine. —**Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi**, uk. 253. {VSS 277.2}

Mifano Kwa Kila Mtu—Walimu, kumbukeni kwamba Bwana Ndiye nguvu yenu. Jitahidini kuwapa wanafunzi mawazo ambayo yatakuwa kwao harufu ya uzima iletayo uzima. Fundisheni kwa kutumia mifano, na mwombeni Mungu awape maneno ya kusema ambayo kila mtu ataweza kuyaelewa. —**Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi**, uk. 254. {VSS 277.3}

Watoto Katika Ufahamu—Mwalimu anapaswa daima kulenga urahisi na ufanisi katika ufundishaji wake. Anapaswa kutumia kwa kiasi kikubwa mifano na vielelezo katika kufundisha, na hata anaposhughulika na wanafunzi wakubwa, anapaswa kuwa mwangalifu kufanya kila maelezo yawe wazi na yenye kueleweka, kwa sababu wanafunzi wengi ambao wameendelea kwa umri [watu wazima] bado ni watoto katika ufahamu. —*Elimu*, uk. 233. {VSS 278.1}

Uwezo wa Watoto Kuelewa—Katika yote ambayo wanadamu wameandika, ni wapi kunaweza kupatikana jambo lenye kushika moyo na kuamsha shauku ya watoto wadogo kama hadithi za Biblia? Katika simulizi hizi rahisi, kanuni kuu za sheria ya Mungu zinaweza kufafanuliwa wazi. Kwa hiyo, kupitia mifano inayofaa zaidi kwa uwezo wa mtoto kuelewa, wazazi na walimu wanaweza kuanza mapema sana kutimiza agizo la Bwana kuhusu maagizo Yake: “Nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii na uadilifu, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na

utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo.” (Kumbukumbu la Torati 6:7)—

Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi, uk. 181. {VSS 278.2}

Heshima ya Neno la Mungu—Mifano mingi inayotumiwa haina ushawishi unaofaa; badala yake, inapunguza heshima takatifu ambayo inapaswa kudumishwa daima katika kuwasilisha Neno la Mungu kwa watu. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 209. {VSS 278.3}

Kondoo Wenye Njaa—Kuna watu wanaosimama madhabahuni kama wachungaji, wakidai kuwalisha kondoo wa Mungu, wakati kondoo hao wanakufa njaa kwa kukosa mkate wa uzima. Kuna mahubiri marefu yanayojazwa kwa kiasi kikubwa na masimulizi ya visa mbalimbali, lakini mioyo ya wasikilizaji haiguswi. Hisia za baadhi yao zinaweza kuchochewa na hata kumwaga machozi machache, lakini mioyo yao haijavunjika. Bwana Yesu amekuwa katika mikutano ambayo mahubiri hayo yaliwasilishwa, lakini maneno yaliyosemwa hayakuwa na umande wala mvua ya mbinguni. Yalionyesha kwamba wale watiwa-mafuta wanaotajwa na Zekaria (tazama sura ya 4) hawakuwa wamewahudumia ili nao waweze kuwahudumia wengine. Wakati watiwa-mafuta wanapojimimina kupitia mifereji ya dhahabu, mafuta ya dhahabu hutiririka kutoka kwao kwenda katika mabakuli ya dhahabu, kisha kwenda katika taa, yaani makanisa. Hii ndiyo kazi ya kila mtumishi wa Kweli na aliyejitolea wa Mungu aliye hai. {VSS 278.4}

Bwana Mungu wa mbinguni hawezi kukubali mengi yanayoletwa madhabahuni na wale wanaodai kusema Neno la Bwana, kwa sababu hawatoi mawazo yatakayokuwa baraka kwa wasikilizaji; badala yake, wanawawekea watu chakula cha bei rahisi sana cha kiroho. —*Shuhuda kwa Wachungaji na Watendakazi wa Injili*, uk. 336–337. {VSS 279.1}

Moto wa Kigeni—Mhudumu anapoweka visa katika mahubiri yake, anatumia moto wa kigeni, kwa sababu anakutana na watu wa aina mbalimbali za fikra ambao wanahitaji kufikiwa kwa uangalifu. Kwa hiyo, anaposhughulika na Neno takatifu, anapaswa kuonyesha unyofu, bidii, heshima, na kicho. Asiruhusu mtu yeyote kupata picha kwamba yeye ni mhubiri wa bei rahisi au hovyoyoyote na wa juu juu. Anapaswa kuondoa masimulizi ya visa katika mahubiri yake na kulihubiri

Neno, kwa sababu angekuwa na miganda mingi zaidi ya kumletea Bwana ikiwa daima angehubiri Neno. Wahudumu wanapaswa kutambua kwamba hawajui kwa kina hitaji kubwa na shauku ya nafsi za watu, kwa kuwa wengine wanapambana na mashaka wakiwa karibu kufikia kukata tamaa na kupoteza tumaini. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 210. {VSS 279.2}

Matumizi ya Vifaa vya Kuonekana-Visual aids—Kwa kutumia chati, alama, na vielelezo vya aina mbalimbali, mhudumu anaweza kuifanya Kweli ionekane wazi na kwa usahihi zaidi; na hii ni msaada unaopatana na Neno la Mungu. —*Shuhuda ka Kanisa*, juz. 9, uk. 142. {VSS 280.1}

Masomo Kwa Kutumia Vitu Katika Shule ya Sabato—Shule zetu za Sabato zinapaswa kufanywa zivutie zaidi, kwa sababu katika miaka ya hivi karibuni shule za serikali au umma zimeboresha sana mbinu zao za kufundisha. Masomo kwa kutumia vitu halisi, picha, na mbao za kuandikia hutumiwa kufanya masomo magumu yaeleweke kwa akili za vijana. Vivyo hivyo, Kweli ya sasa inaweza kurahisishwa na kufanywa yenye kuvutia sana kwa akili changa na hai za watoto. —*Mashauri kuhusu Kazi ya Shule ya Sabato*, uk. 114. {VSS 280.2}

Kufundisha Kumbukumbu—Matumizi ya masomo kwa kutumia vitu halisi, mbao za kuandikia, ramani, na picha yatasaidia kueleza masomo haya, yaani visa vya Biblia, na kuyafanya yakumbukwe vizuri. Kwa hiyo, wazazi na walimu wanapaswa daima kutafuta mbinu bora zaidi za kufundisha. —*Elimu*, uk. 186. {VSS 280.3}

Chati Katika Uwasilishaji wa Ukweli—Nimeagizwa kwa uwazi na kwa hakika kwamba chati zinapaswa kutumiwa katika kuwasilisha Ukweli, na vielelezo hivi vinapaswa pia kufanywa kuwa na mvuto zaidi kwa kutumia maneno yanayoonyesha umuhimu wa utii. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 203. {VSS 280.4}

Kutumia Neno na Vielelezo—Matumizi ya chati yanafaa sana katika kueleza unabii unaohusu mambo ya zamani, ya sasa, na yajayo; hata hivyo, tunapaswa kufanya kazi yetu iwe rahisi na yenye gharama nafuu kadiri iwezekanavyo, kwa

sababu uUkweli unapaswa kuelezwa kwa urahisi na kwa namna inayoeleweka. —

Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, uk. 203. {VSS 280.5}

Njia ya Kudumisha Umakini—Ndugu S ni mwinjilisti mwenye hekima na uwezo mzuri wa kufundisha, anayezungumza kwa urahisi kama mtoto, na kamwe haingizi maneno ya kudharau au kubeza katika mahubiri yake. Anahubiri moja kwa moja kutoka katika Neno la Mungu, akiliruhusu Neno lenyewe lizungumze kwa watu wa kila daraja. Hoja zake zenye nguvu zinatokana na maneno ya Agano la Kale na Agano Jipya; hatafuti maneno yatakayowavutia watu kwa kuonyesha elimu yake, bali anajitahidi kulifanya Neno la Mungu lizungumze moja kwa moja kwao kwa matamshi yaliyo wazi na yanayoeleweka. Ikiwa mtu yeyote anakataa kuupokea ujumbe huo, basi analikataa Neno lenyewe. {VSS 281.1}

Ndugu S anazungumzia kwa namna ya pekee unabii unaopatikana katika vitabu vya Danieli na Ufunuo, akiwa na vielelezo vikubwa vya wanyama waliotajwa katika vitabu hivyo ambavyo huvitumia kwa wakati unaofaa ili kufafanua mambo anayoyaeleza. Hakuna neno hata moja la kizembe au lisilo la lazima linalotoka midomoni mwake; badala yake, anazungumza kwa nguvu na kwa uzito. Wengi wa wasikilizaji wake hawajawahi kusikia mahubiri yenye uzito wa namna hiyo hapo awali, na hawaonyeshi roho ya mzaha au kutojali, bali hofu na kicho kitakatifu huonekana kutawala mioyo yao. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 204–205. {VSS 281.2}

Vielelezo vya Wanyama wa Kinabii Vyenye Ukubwa Halisi—Mzee S anachochea mwitikio mzuri kupitia mikutano yake, kwa kuwa watu wa aina mbalimbali huja kusikiliza na pia kuona vielelezo vya ukubwa halisi vya wanyama wa kinabii wa kitabu cha Ufunuo alivyovitayarisha. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 205. {VSS 281.3}

Vielelezo Vyenye Nguvu ya Kushawishi—Nimefurahishwa na namna ambavyo ndugu yetu [Mzee S] ametumia ubunifu na ustadi wake katika kuandaa vielelezo

vinavyofaa kwa mada zinazowasilishwa, yaani vielelezo vyenye uwezo mkubwa wa kushawishi; na mbinu kama hizi zitatumika zaidi na zaidi katika kazi hii ya mwisho. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 205. {VSS 282.1}

Mbinu za Kutumia Vielelezo—Watendakazi wa Mungu wanapaswa kuonyesha ustadi na vipawa walivyopewa, na kubuni njia mbalimbali ambazo kupitia hizo wataweza kuwasilisha nuru kwa wale walio karibu na pia kwa wale walio mbali. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 206. {VSS 282.2}

SURA YA 48—UWASILISHAJI WA HOTUBA ZA UFASAHU NA MAONYESHO YA KIMAIGIZO

Hotuba za Kuvutia Bila Kina Ni Kama Shaba Iliayo—Maisha yaliyofanywa upya kwa neema ya Mungu na yaliyofichwa pamoja na Kristo ndani ya Mungu yana ufasaha unaodhihirika katika urahisi na unyenyekevu wake; kwa hiyo, hotuba na mazungumzo yanayotolewa na watu wanaoonekana kuwa wasomi ni kama shaba iliayo na upatu uvumao mbele za Mungu yakilinganishwa na maneno yanayotoka moja kwa moja katika moyo uliosafishwa kwa imani katika Kristo kama Mwokozi

binafsi. Wale walio na ufasaha unaokubalika mbele za Mungu, wako tayari kutembea katika njia za unyenyekevu, ingawa hawathaminiwi na wale wanaojitahidi daima kutafuta ukuu na ambao hawana ufahamu wa maana ya kutembea katika kujitiisha kwa unyenyekevu chini ya mapenzi na njia ya Mungu. Lakini Mungu asema: ***“Mtu huyu ndiye nitakayemwangalia, mtu aliye mnyonge, mwenye roho iliyopondeka, atetemekaye asikiapo Neno Langu.”*** (Isaya 66:2) —*Manuscript 176, 1899. {VSS 283.1}*

Wahudumu, Siyo Waigizaji/Actors—Isipokuwa watu waongozwe kuithamini kweli kama hazina ya thamani na kuipokea kama kitu kitakachoitakasa nafsi, hakuna faida ya kudumu inayoweza kupatikana; kwa maana mtu anayewasilisha maneno ya kuvutia kwa ustadi mkubwa wa usemi anaweza kuwafanya watu wasahau Ukweli uliochanganywa ndani ya hotuba yake. Baada ya msisimko huo kupita, itaonekana kwamba Neno la Mungu halikupandikizwa katika akili zao wala hawakuongezewa ufahamu wa kweli. Watu wanaweza kuondoka kanisani wakisifu uwezo wa hotuba wa mhubiri aliyewahubiria, lakini wasiguswe na Ukweli wala wasiletwe karibu zaidi na hatua ya kufanya uamuzi. Wanaweza kuizungumzia mahubiri hayo kama wanavyozungumzia mchezo wa kuigiza na kumzungumzia mhudumu kama wanavyomzungumzia mwigizaji wa ukumbi wa michezo; kisha wanaweza kurudi tena kusikiliza aina hiyo hiyo ya hotuba, lakini wakaondoka tena bila kuguswa wala kulishwa kiroho. **{VSS 283.2}**

Kwa hiyo, watu hawapaswi kuhamasishwa kuthamini maonyesho ya ufasaha wa maneno, kwa sababu mtindo huu wa mahubiri una athari ileile akilini kama kusoma hadithi yenye kulisimua; huleta msisimko wa muda mfupi, lakini haubadilishi tabia. Ushawishi wa aina hii ya mahubiri umeonekana wazi katika matokeo yake, kwa kuwa watu huvutiwa na mhubiri mwenyewe na kudhani kwamba hakuna mwingine anayelingana naye; lakini nimeonyeshwa kwamba, kama ilivyokuwa -----, ndivyo ilivyo katika sehemu nyingine, kwamba hakuna msingi imara unaowekwa kwa ajili ya kuanzishwa kwa kanisa. Mhudumu huyo anapoondoka, wale walioonekana kuipokea Kweli huonyesha wazi kwamba hawakuwa wameunganishwa na Kristo, bali walikuwa wamefungamana na mwanadamu; Kristo alikuwa mgeni kwao, nao hawakumjua, hivyo wakaacha ushirika Wake na hawakutembea naye tena. **{VSS 284.1}**

Wajumbe wa Mungu wanapaswa kupeleka kwa ulimwengu ulioanguka ujumbe wa mwisho, mzito, na wa kujaribu wa rehema; kwa hiyo, ikiwa mhudumu anajionyesha mwenyewe, anajiweka kati ya ujumbe na watu. Ikiwa anajifunza kuwasilisha ukweli kwa mtindo maalumu unaolenga kujionyesha, anaweza kuifanya kazi yake isiwe na matokeo na hatimaye kuifanya ipoteze nguvu, kwa sababu Roho Mtakatifu hafanyi kazi pamoja na juhudi za namna hiyo. Matokeo yake ni kwamba watu huchochewa kumtazama na kumtukiza mhudumu badala ya kumwona Yesu, na hivyo mwanadamu huingia mahali pa Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka. Mhudumu anaweza kuhubiri hotuba inayopaa juu kana kwamba inafika mawinguni na nyotani, lakini ikaacha bila mvuto wa kudumu katika mioyo ya wasikilizaji wake; kwa maana ikiwa usadikisho wa Kweli haujaingia moyoni, muda na mali vilivyotumika havijazaa matokeo. Kuna faida gani watu kumheshimu sana mhudumu ikiwa hawathamini Kweli inayookoa na inayowajaribu? **{VSS 284.2}**

Roho Mtakatifu Ndiye anayepaswa kufanya kazi ndani ya mwanadamu, wala mwanadamu hapaswi kujaribu kumtumia Roho Mtakatifu kwa mipango yake mwenyewe, kwa sababu Roho Mtakatifu si mtumishi wa mwanadamu bali ni nguvu inayotawala. Yeye huifanya Kweli ing'ae katika kila akili na hunena kupitia kila mahubiri ambayo mhudumu amejisalimisha kwake; hutembea pamoja na nafsi katika njia ya maisha na huzungumza kupitia binadamu ambaye ni chombo, akitoa mazingira ya kiroho yanayomzunguka mtu na kuzungumza na wasiotubu kupitia maneno ya maonyo. —*Letter 29, 1895.* **{VSS 285.1}**

Watu wa Maombi Ni Watu wa Nguvu—Hatutafuti wahubiri wenye ufasaha mkubwa wa maneno pekee, bali tunahitaji watendakazi wanyenyekevu, waadilifu, na wenye bidii, watu wenye imani ya kitoto katika nguvu iliyo kuu kuliko wao; kwa maana watu wa maombi, wanaomtafuta Bwana kwa mioyo iliyonyenyekea na iliyopondeka, ndio watu wenye nguvu. —*Letter 146, 1903.* **{VSS 285.2}**

Ufasaha wa Hotuba Unaweza Kuwa Mtego—Ni Kweli iliyowekwa ndani ya nafsi ndiyo inayomfanya mtu kuwa mtu wa Mungu. Umbuji/Ufasaha wa hotuba, ingawa unaweza kuwafurahisha watu wa aina fulani, unaweza kuwa mtego kwa yule anayeutumia na pia kwa kanisa. **{VSS 286.1}**

Kwa hiyo, wasiwasi wetu haupaswi kuwa kupata mchungaji atakayewafurahisha watu kwa hotuba nzuri na ustadi wa usemi ili kupata sifa na

makofi, bali kupata watu wanaofanya kazi pamoja na Mungu, watu wanaojitahidi kujionyesha kuwa wamekubaliwa na Mungu. —*Manuscript 1a, 1890.* {VSS 286.2}

Ufasaha wa Kufikirika—Mhudumu anaweza kupaa juu sana katika maelezo ya kishairi na mawasilisho ya kubuni yanayofurahisha hisia na kulisha mawazo, lakini yasiguse uzoefu wa kawaida wa maisha wala mahitaji ya kila siku, na hivyo kushindwa kuyafikisha moyoni mafundisho yale yenye umuhimu mkubwa wa kiroho. Mahitaji ya sasa na majaribu yanayowakabili watu yanahitaji msaada na nguvu ya wakati huo—yaani imani itendayo kazi kwa upendo na kuitakasa nafsi; si maneno yasiyo na ushawishi wa Kweli katika mwenendo wa kila siku wa Ukristo wa vitendo. {VSS 286.3}

Mchungaji anaweza kudhani kwamba kwa ufasaha wake wa kubuni amefanya kazi kubwa katika kuwalisha kundi la Mungu. Wasikilizaji wanaweza kufikiri kwamba hawajawahi kusikia mada nzuri kama hizo hapo awali, wala kuona Kweli ikivishwa kwa lugha yenye uzuri wa namna hiyo; na wanapomwona Mungu akiwakilishwa katika ukuu Wake, wanaweza kujazwa na msisimko mkubwa wa hisia. Lakini tunapofuatilia chanzo hadi matokeo ya msisimko huo unaosababishwa na mawasilisho hayo ya kubuni, tunaona kwamba ingawa huenda kulikuwa na Kweli ndani yake, mara nyingi si chakula kitakachowatia nguvu kwa ajili ya mapambano ya kila siku ya maisha. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 182. {VSS 286.4}

Kanuni Chache Rahisi—Nimeonyesha kwamba wahudumu wetu walikuwa wakijiletea madhara makubwa kwa sababu ya kutokuwa waangalifu katika matumizi ya viungo vyao vya sauti. Usikivu wao ulielekezwa kuzigantiaa jambo hili muhimu, na maonyo pamoja na maagizo walipewa kupitia Roho wa Mungu. Ilikuwa wajibu wao kujifunza namna bora zaidi ya kutumia viungo hivyo. Sauti, ambayo ni zawadi kutoka mbinguni, ni uwezo wenye nguvu kwa ajili ya mema, na ikiwa haitatumiwa vibaya, itamtukuza Mungu. Kilichohitajika tu ni kujifunza na kufuata kwa uaminifu kanuni chache rahisi; lakini badala ya kujielimisha wenyewe, jambo ambalo wangeweza kulifanya kwa kutumia akili ya

kawaida na mazoezi kidogo, waliamua kuajiri mwalimu wa ufasaha wa usemi. {VSS 287.1}

Matokeo yake yakawa kwamba wengi waliokuwa wakihihi kuwa Mungu alikuwa amewapa kazi ya kuwafundisha wengine Kweli walivutwa na kushikwa na tamaa kubwa ya kujifunza ufasaha wa usemi. Walihitaji tu kukabiliwa na jaribu hili ndipo walipoanza kuvutiwa na jambo hilo jipya. Shauku hiyo ikawachukua vijana wengi na baadhi ya wahudumu; wakaacha maeneo yao ya kazi, na kila kitu katika shamba la Bwana kikapuuzwa, wakatumia fedha zao na muda wao wa thamani kuhudhuria shule za ufasaha wa usemi. Walipomaliza mafunzo hayo, ibada na dini vilikuwa vimetenganishwa nao, na mzigo wa kuokoa nafsi ukawaondoka kama mtu anavyovua vazi. Walikuwa wamekubali mapendekezo ya Shetani, naye aliwaongoza mahali alipotaka. {VSS 287.2}

Baadhi yao walijiweka kuwa walimu wa ufasaha wa usemi [Elocution], ingawa hawakuwa na busara wala uwezo wa kutosha. Walijifanya kuwa wa kuvutia mbele ya watu, lakini wakawa kero kwa jamii kwa sababu hawakutumia vizuri maarifa waliyokuwa wamejifunza. Maonyesho yao yalikosa heshima na akili timamu; na matendo hayo yakafunga mlango wa ushawishi wao wa baadaye kama watu waliokusudiwa kupeleka ujumbe wa Kweli kwa ulimwengu. Huo ulikuwa mpango wa Shetani. Ni jambo jema kuboresha uwezo wa kuzungumza, lakini kutumia muda na fedha nyingi katika jambo hili moja pekee na kulifanya kuwa jambo kuu linaiteka akili ni kwenda katika kupita kiasi na kuonyesha udhaifu mkubwa. {VSS 288.1}

Vijana wanaojiita washika Sabato walijiongezea jina la “profesa” na kuliudhi jamii kwa mambo wasiyoyaelewa vizuri. Wengi wao walipotosha nuru ambayo Mungu alikuwa amewapa. Hawakuwa na usawaziko wa akili. Ufasaha wa usemi ukawa neno la dharau [Elocution], kwa sababu uliwafanya watu wajihusishe na kazi ambayo hawakuweza kuifanya kwa hekima na ukawaharibu kwa ajili ya kazi ambayo, kama wangejitahidi kuifanya kwa unyenyekevu, kiasi, na hofu ya Mungu, wangekuwa na mafanikio makubwa. Vijana hao wangepoteza kuwa na manufaa katika kazi ya umishonari kama wainjilisti wa vitabu, wahudumu wasaidizi, au watenda kazi wanaojaribiwa kwa ajili ya huduma ya injili, wakifanya kazi yenye thamani kwa wakati huu na kwa umilele. Lakini walichanganyikiwa na tamaa ya kuwa walimu wa ufasaha wa usemi-Elocution, naye Shetani akasimama akicheka kwa

sababu aliwanasa katika mtogo aliokuwa amewawekea.—[Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 4, uk. 604–606. {VSS 288.2}

Ufasaha Hata wa Ulimi Unaosita—Vito vingi vya thamani vya Kweli mara nyingi hupoteza nguvu kwa sababu ya ustadi wa maneno yanayotumiwa kuvieleza, wakati nguvu ya Roho wa Mungu inapokosekana; kwa maana maneno yenye mvuto pekee hayawezi kuchukua nafasi ya nguvu ya kiroho inayotoka kwa Mungu. Kristo aliwasilisha Kweli kwa urahisi, naye hakuwafikia watu wenye vyeo vya juu pekee, bali pia watu wanyenyekevu kabisa duniani. Mchungaji ambaye ni balozi wa Mungu na mwakilishi wa Kristo duniani, anayejinyenyekeza ili Mungu atukuzwe, atakuwa na sifa ya Kweli ya ufasaha. Ucha Mungu wa kweli, uhusiano wa karibu na Mungu, pamoja na uzoefu wa kila siku ulio hai katika kumjua Kristo, vitamfanya hata ulimi unaogugumia uwe na ufasaha. —[Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 4, uk. 314. {VSS 289.1}

Matumizi ya Moto wa Kawaida—Baadhi ya wachungaji hufanya kosa la kudhani kwamba mafanikio yanategemea kuvuta makundi makubwa ya watu kwa maonyesho ya nje, kisha kuwasilisha ujumbe wa Kweli kwa mtindo wa kimaigizo; lakini kufanya hivyo ni kutumia moto wa kawaida badala ya moto mtakatifu uliowashwa na Mungu. Bwana hatukuzwi kwa njia hiyo ya kufanya kazi, kwa maana kazi Yake haitakamilishwa kwa matangazo ya kushangaza wala kwa maonyesho ya gharama kubwa, bali kwa kufuata mbinu zinazofanana na zile za Kristo. — *Watendakazi wa Injili*, uk. 383. {VSS 289.2}

SURA YA 49—HATARI YA HISIA ZILIZOZIDI KIASI

Kushawishiwa na Neno la Mungu, Siyo Hisia—Ni kupitia Neno la Mungu—si kupitia hisia wala msisimko—ndipo tunapaswa kuwashawishi watu kuitii Kweli. Juu ya jukwaa/msingi wa Neno la Mungu tunaweza kusimama salama, kwa maana Neno lililo hai limejaa ushahidi, na nguvu ya ajabu huambatana na kutangazwa kwake katika ulimwengu wetu. —*Selected Messages*, juz. 3, uk. 375. {VSS 290.1}

Mahubiri Yanayochochea Hisia—Ikiwa mahubiri yana mwelekeo wa kuchochea hisia, yataathiri hisia za watu, lakini hayataigusa mioyo wala dhamiri zao. Mahubiri ya namna hiyo hayaleti faida ya kudumu; badala yake, mara nyingi huwavutia watu na kuwafanya wampende na kumpendelea mhubiri anayewafurahisha. Watu hao husahau kwamba Mungu amesema: “*Mwacheni mwanadamu ambaye pumzi yake i katika mianzi ya pua yake.*” Isaya 2:22 —[Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 5, uk. 301. {VSS 290.2}

Kumtumaini Mungu, Siyo Mwanadamu—Ninaumia sana moyoni ninapoona ukosefu mkubwa wa utambuzi miongoni mwa watu wetu ambao wamepokea nuru kubwa namna hii. Wanasikiliza mahubiri yanayochochea hisia zao, na mawazo ya mioyo yao huwa: “**Tupeni daima huduma ya mtu huyu; anagusa mioyo yetu, anatufanya tuhisi.**” Wanamsahau Mungu, na badala yake wanamsifu na kumtukuza mwanadamu, jambo linalomletea madhara yeye mwenyewe na pia kuleta madhara kwa nafsi zao. Ni lini wale wanaodai kuamini Kweli wataacha kumtegemea mwanadamu ambaye pumzi yake iko puani mwake? Ni lini watakapomtumaini Mungu na kumfanya kuwa kile Alichu—yaani yote katika yote? —*Letter 8, 1889*. {VSS 290.3}

Maamuzi Yanayotokana na Msukumo wa Muda Hayadumu—Katika huduma kuna watu wanaoonekana kufanikiwa kwa kutumia ushawishi wa kibinadamu juu ya akili za watu. Wachezea hisia za wasikilizaji wao wapendavyo, wakiweza kuwafanya walie na baada ya dakika chache kuwafanya wacheke. Chini ya kazi ya namna hii, wengi huchochewa na msukumo wa muda mfupi kumkiri Kristo, na hudhaniwa kwamba uamsho mkubwa umetokea; lakini jaribu linapokuja, kazi hiyo haidumu. Hisia huchochewa, na wengi husombwa na mkondo unaoonekana kuelekea mbinguni; lakini wanapokutana na mkondo mkali wa majaribu, hurudi nyuma haraka kama mti uliobebwa na maji. Mtendakazi hujidanganya mwenyewe, naye huwapotosha wasikilizaji wake. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 382. {VSS 291.1}

Akili ya Kweli Katika Kuhubiri—Mtu anaweza kuhubiri kwa nguvu na msisimko mkubwa kiasi cha kufurahisha masikio ya watu, lakini bila kuwasilisha wazo jipya wala maarifa ya Kweli katika akili zao. Athari na miguso inayopatikana kupitia mahubiri ya namna hiyo hudumu kwa muda mfupi tu—yaani kwa muda ambao sauti ya mhubiri inasikika. Baada ya kuchunguza matunda ya kazi hiyo, hupatikana machache sana. —[Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 1, uk. 447. {VSS 291.2}

Matumizi Yasiyo ya Kawaida ya Sauti—Baadhi ya watu huinua sauti zao kufikia kiwango kisicho cha kawaida wanapozungumza madhabahuni [unnatural key], huku wengine wakizungumza kwa haraka sana kiasi kwamba watu hawawezi kusikia wanachosema. Hali hii huleta madhara kwao wenyewe na kwa wasikilizaji wao, kwa sababu matumizi hayo yasiyo ya kawaida ya sauti huathiri vibaya viungo vyao vya sauti. Kwa kufanya hivyo, wanamaliza nguvu zao bila sababu na kufanya juhudi zao ziwe zenye kuchosha kwa wasikilizaji wao. Wanapaswa kujifunza kujitawala, kwa kuwa sifa hii ni muhimu sana kwao kama mabalozi wa Kristo, na kushinda mazoea yao mabaya. Iwapo watafanya hivyo, wataweza kuacha mvuto mzuri katika akili za wasikilizaji wao na kuifanya kazi ya kuhubiri Kweli iwe yenye kuvutia zaidi. —*The Review and Herald*, Oktoba 28, 1890. {VSS 291.3}

Nguvu Bila Kuchochea Hisia Kupita Kiasi—Mungu anataka wote watende kwa utulivu na kwa busara, wakichagua maneno yao kwa kupatana na Kweli imara ya wakati huu, ambayo inapaswa kuwasilishwa akilini bila kuchanganywa na mambo ya kihisia kadiri iwezekanavyo, huku bado ikiwa na nguvu na uzito unaostahili kuwa nayo. Tunapaswa kujilinda dhidi ya kuleta hali za kupita kiasi na pia dhidi ya kuwahamasisha wale ambao huenda wakaangukia katika misimamo mikali—ama kuwa katika moto au katika maji. {VSS 292.1}

Ninawasihi muondoe katika mafundisho yenu kila kauli iliyopitiliza, kila jambo ambalo watu wasio na usawaziko wa akili na wale wasio na uzoefu wanaweza kulichukua na kuligeuza kuwa harakati za kiholela na zisizokomaa. Ni muhimu kwenu kuwa waangalifu katika kila kauli mnayotoa, ili msije mkawaelekeza baadhi ya watu katika njia isiyo sahihi na kusababisha mkanganyiko ambao utahitaji kazi nyingi ya huzuni kuurekebisha. Kwa kufanya hivyo, nguvu na kazi ya watenda kazi zitaelekezwa katika maeneo ambayo Mungu hakusudii yaingiliwe. Mwelekeo mmoja tu wa ushupavu wa kidini unaoonekana miongoni mwetu unaweza kufunga

Nhandi Masunga na Grace Momadi Masaka-Jersey 2026 July

milango mingi dhidi ya kanuni thabiti za Kweli. —Shuhuda kwa Wachungaji na Watendakazi wa Injili, uk. 227–228. **{VSS 292.2}**

SURA YA 50—KUSIKIKA, LAKINI SI KWA KUPAZA SAUTI

Kuchosha Viungo vya Sauti—Kutokana na nuru niliyopewa, huduma ya injili ni wadhifa mtakatifu na wa juu sana; kwa hiyo, wale wanaokubali nafasi hii wanapaswa kuwa na Kristo mioyoni mwao na kuonyesha shauku ya Kweli ya kumwakilisha kwa kustahili mbele ya watu katika matendo yao yote, mavazi yao, usemi wao, na hata namna yao ya kuzungumza. Wanapaswa kuzungumza kwa heshima na kicho. **{VSS 294.1}**

Baadhi ya watu hugaribu mvuto mzito ambao huenda walikuwa wameujenga mbele ya watu kwa kuinua sauti zao kufikia kiwango cha juu sana, wakipaza sauti na kupiga kelele zinazofanana na sauti ‘haloooo’ wanapowasilisha Kweli-kama wanaotaka kupata usikivu wa watu au wale wanaowaita mbwa ili wapate usikivu wao. Ukweli unapowasilishwa kwa namna hiyo, hupoteza sehemu kubwa ya utamu wake, nguvu yake, na uzito wake. Lakini ikiwa sauti itarekebisha vizuri, ikiwa itakuwa na uzito na kupangwa kwa namna inayoonyesha hisia ya kina, na sikitiko, italeti mvuto mzuri zaidi. **{VSS 294.2}**

Hii ndiyo iliyokuwa namna Kristo alivyowafundisha wanafunzi Wake. Aliwajengea hisia ya uzito na heshima; alizungumza kwa namna iliyogusa mioyo yao ili kuleta hisia kama vile sikitiko nk. Lakini kupaza sauti kwa namna hiyo yenye nguvu nyingi kunaleta faida gani? Hakuleti kwa watu mtazamo wa juu zaidi kuhusu kweli wala hakuwafanyi waipokee kwa kina zaidi. Badala yake, husababisha hali isiyopendeza kwa wasikilizaji na huchosha viungo vya sauti vya msemaji. Mlio wa sauti una nafasi kubwa katika kuathiri mioyo ya wale wanaosikia. **{VSS 294.3}**

Watu wengi ambao wangeweza kuwa watenda kazi wenye manufaa wanatumia vibaya nguvu zao za uhai na kuharibu mapafu yao pamoja na viungo vyao vya sauti kwa sababu ya namna wanavyozungumza. Baadhi ya wachungaji wamejenga mazoea ya kutamka maneno yao kwa haraka sana, kana kwamba wanakariri somo fulani, au yabidi warudie jambo fulani na wanataka kulimaliza kwa kasi iwezekanavyo. Hii siyo njia bora ya kuzungumza. Kwa uangalifu unaofaa, kila mhudumu anaweza kujizoeza kuzungumza kwa uwazi na kwa namna yenye mvuto, badala ya kubana maneno mengi kwa haraka bila kutoa nafasi ya kuvuta pumzi. Anapaswa kuzungumza kwa mwendo wa wastani ili watu waweze kuelewa na kuhifadhi mawazo yanayowasilishwa. Lakini ujumbe unapowasilishwa kwa haraka mno, watu hawawezi kuyashika mambo muhimu akilini mwao wala hawapati muda

wa kupokea mvuto unaopaswa kuwafikia; pia Kweli hukosa nafasi ya kugusa mioyo yao kama ambavyo ingefanya vinginevyo. **{VSS 295.1}**

Kuzungumza kwa kutumia koo pekee, huku maneno yakitolewa kutoka sehemu ya juu ya viungo vya sauti na kuvichosha kila wakati kwa kuvibana na kuvichokoza, siyo njia bora ya kuhifadhi afya wala kuongeza ufanisi wa viungo hivyo. Mnapaswa kuvuta pumzi kwa kina na kuruhusu nguvu ya sauti itoke katika misuli ya tumbo. Mapafu yanapaswa kuwa njia ya kupitishia hewa tu, lakini msiyategemea kufanya kazi yote. Mkitoa maneno kutoka ndani kabisa kwa kuishugulisha misuli ya tumbo, mtaweza kuzungumza mbele ya maelfu ya watu kwa urahisi uleule mnaoweza kuzungumza mbele ya watu kumi. **{VSS 295.2}**

Baadhi ya wahubiri wetu wanajichosha na kujidhuru kwa maombi marefu yasiyo na lazima na kuzungumza kwa sauti kubwa sana, wakati sauti ya chini ingelea mvuto na mguso bora zaidi na kuwaokoa nguvu zao. Sasa, mnapoendelea kupuuza sheria za maisha na afya na kufuata msukumo wa wakati huo, msimlaumu Mungu ikiwa mtaanguka na kudhoofika. —[Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 2, uk. 615–616. **{VSS 295.3}**

Maombi Yanayosikika na Wote—Kwa wale wanaopanga kuingia katika kazi ya Mungu kama wahudumu, ningesema: Jitahidini kwa kuazimia kufikia ukamilifu katika usemi. Mwombeni Mungu awasaidie kufikia lengo hili kuu. Mnapoomba mbele ya kusanyiko, kumbukeni kwamba mnazungumza na Mungu, na kwamba Yeye anatamani mzungumze kwa namna ambayo wote waliopo waweze kusikia na kuunganisha maombi yao pamoja na yenu. Maombi yanayotolewa kwa haraka kiasi kwamba maneno yanachanganyika hayamtukuzi Mungu wala hayana manufaa kwa wasikilizaji. Wachungaji na wote wanaoongoza maombi ya hadhara wanapaswa kujifunza kuomba kwa namna ambayo Mungu atatukuzwa na wasikilizaji watabarikiwa. Wahubiri wanapaswa kuzungumza polepole, kwa uwazi, na kwa sauti inayoweza kusikika na wote, ili watu waweze kuungana kusema: “**Amina.**” —[Shuhuda ka Kanisa](#), juz. 6, uk. 383. **{VSS 296.1}**

Kuzungumza kwa Sauti Kubwa Ni Hatari kwa Afya—*[Mazungumzo yasiyopangwa wakati wa hotuba ya Ellen G. White kwa Kamati ya Konferensi Kuu huko Lake Goguwac, Michigan, Julai 14, 1890.]* Mzee Farnsworth alisema: “Je, Dada White, wewe hufikirii kwamba wahudumu wetu wengi wamepata madhara makubwa kwa sababu ya namna yao ya kuzungumza?” **{VSS 296.2}**

Ellen White akajibu: “Naam, hakika; nimeona jambo hili mara nyingi sana. Mume wangu aliwahi kuingia katika mazoea ya kuinua sauti yake sana wakati mwingine, na ilionekana kana kwamba hangeweza kuacha tabia hiyo. Pia kuna ndugu mmoja huko Texas, Ndugu A, ambaye anadhoofika na kufa polepole kana kwamba amejitokea kisu kooni mwake. Tangu nilipokuja hapa nimekuwa nikifikiria jambo hilo, na lazima nimwandikie.” {VSS 297.1}

Mzee Kilgore akasema: “Ameshakwisha kuambiwa kuhusu jambo hilo.” {VSS 297.2}

Mzee Farnsworth akaongeza: “Wapo wengi kama hao kila mahali na katika kila konferensi.” {VSS 297.3}

Ellen White akaendelea kusema: “Katika siku zangu za ujana nilikuwa nikizungumza kwa sauti kubwa sana. Bwana alinionesha kwamba singeweza kuleta mvuto unaofaa kwa watu kwa kuinua sauti yangu kufikia kiwango kisicho cha kawaida. Ndipo Kristo aliwasilishwa mbele yangu, pamoja na namna Yake ya kuzungumza. {VSS 297.4}

Kulikuwa na utamu wa pekee katika sauti Yake. Sauti Yake, kwa namna ya polepole na yenye utulivu, iliwafikia wale waliomsikiliza. Maneno Yake yaliingia moyoni mwao, na waliweza kuelewa alichokuwa akisema kabla hajaanza sentensi iliyofuata.” —*Manuscript 19b, 1890.* {VSS 297.5}

SURA YA 51—USTAARABU NA UZITO WA MWENENDO

[Refinement and Solemnity of Demeanor]

Hakuna Haja ya Maonyesho ya Kusisimua au Miondoko Mikali—Bwana anakuita ufanye maboresho makubwa na ya wazi katika namna yako ya kuwasilisha Kweli, kwa maana huna haja ya kutumia mbinu za kuisimua hisia za watu; bali unapaswa kulihubiri Neno kama Kristo, Mwana wa Mungu, alivyolihubiri. Miondoko yenye utata ya mwili na ishara zilizopitiliza zisizo za kiungwana hupunguza kwa kiasi kikubwa mvuto ambao Kweli ingeweza kuleta katika mioyo ya wanadamu na hudhoofisha nguvu ya udhihirisho wa Roho wa Mungu. Vitendo hivyo huondoa hisia ya utakatifu na uzito wa Neno la Mungu ambao malaika watakatifu wanatamani uwekwe katika akili za wanadamu. —

Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, uk. 184. {VSS 298.1}

Ishara Zenye Utata na Zisizo na Adabu/Uungwana—Ishara zisizo za kawaida au tata, zisizo na mpangilio, na zisizo za kiungwana hazipaswi kuvumiliwa katika maisha ya kawaida; sembuse katika kazi iliyo takatifu zaidi ya huduma ya injili. Mchungaji anapaswa kukuza neema, adabu, na ustaarabu wa mwenendo wake, na anapaswa kujiendesha kwa utulivu na heshima inayolingana na wito wake mkuu. Uzito wa kiroho pamoja na mamlaka ya Kiungu iliyochanganyika na upole vinapaswa kuwa sifa zinazomtambulisha yule anayefundisha Kweli ya Mungu.[Mifano ni kuruka-ruka, kukonyeza, kugombeza watu, na mengine mengi, tafadhali orodhesha] —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 640. {VSS 298.2}

Awkward and Uncouth Gestures—Awkward and uncouth gestures are not to be tolerated in the common walks of life; how much less, then, are they to be endured in the most sacred work of the gospel ministry. The minister should cultivate grace, courtesy, and refinement of manner. He should carry himself with a quiet dignity becoming his elevated calling. Solemnity, a certain godly authority, mingled with meekness, should characterize the demeanor of him who is a teacher of God's truth.—*Evangelism*, 640.

Awkward and Uncouth Gestures in Preaching

In preaching, **“awkward and uncouth gestures”** are nonverbal actions that are clumsy, unrefined, or inappropriate for the solemn and sacred nature of the ministry. According to *The Voice in Speech and Song* (1888), such gestures are **not to be tolerated in the gospel ministry** because they detract from the dignity, authority, and spiritual weight of the message

What They Are

These gestures are movements of the body—especially the hands, arms, or posture—that:

Lack grace, courtesy, or refinement in their execution

Are **unnatural, overly dramatic, or mechanically forced**, making the preacher appear self-conscious or “performing” rather than genuinely engaged

Contradict or distract from the message, such as mismatched hand movements that don’t align with the words spoken

Are **visually jarring or sensational**, drawing attention to the preacher’s manner rather than the truth being proclaimed

Examples include:

Excessive, violent gesticulations that overshadow the message

Repetitive, mechanical hand motions that create “visual noise”

Awkward postures or awkward hand positions (e.g., “fig leaf” clasping, “T-Rex” stance) that signal discomfort or artificiality

-

Why They Are Problematic

The 19th-century homiletic source warns that such gestures:

-

Lessen the force of the demonstration of the Spirit of God

-

- **Efface the solemn impressions** about God's Word that the ministry is meant to make
- Undermine the preacher's **godly authority** and **meekness**, which should characterize the teacher of Scripture
- Modern homiletics agrees: gestures should be **purposeful, congruent with the message, and natural**. When they are awkward or uncouth, they distract the audience, reduce credibility, and shift focus from the message to the preacher's manner
How to Avoid Them
- **Align gestures with your words** so they reinforce, not contradict, the message
Cultivate grace and dignity in your demeanor, avoiding sensationalism
Be natural and specific—gestures should grow from genuine engagement with the thought, not be “performed”
Use stillness strategically to give weight to key points

In short: In preaching, awkward and uncouth gestures are those that are clumsy, unnatural, or inappropriate for the sacred context, and they should be avoided because they undermine both the message and the minister's authority

Usiwe Kivuli cha Mtu Yeyote—Wahudumu hawapaswi kamwe kuiga ishara, mazoea, mkao, mwelekeo, mionekano ya uso, mwondoko, au sauti ya mtu mwingine; wala hawapaswi kuwa kivuli cha mtu yeyote katika mawazo yao, hisia zao, au katika kupanga na kutekeleza kazi kwa ujumla. Ikiwa Mungu amekufanya kuwa mchungaji wa kundi Lake, amekupa pia sifa na uwezo unaohitajika ili kufanya kazi hiyo. Kristo anasema: **“Wala msimwite mtu baba duniani; maana Baba yenu ni Mmoja, aliye wa mbinguni.”** (*Mathayo 23:9*) Kila mtu na achukue Biblia yake na kujiweka katika ushirika wa Kiungu pamoja na Mwalimu Mkuu, kwa maana Mungu Ndiye chanzo cha maarifa yote na hekima. —*Manuscript 104, 1898. {VSS 299.1}*

Kila Mtu Avai Silaha Zake Mwenyewe—Tunapungukiwa pia katika jambo jingine, yaani, kwamba watu wenye uwezo wa kufanya kazi hawajaunganishwa katika huduma pamoja na wale wasio na uzoefu ili wawasaidie kupata uzoefu ulio katika njia sahihi. Watu wasio na uzoefu hawapaswi kutumwa peke yao, bali wanapaswa kusimama karibu na wachungaji wakubwa na wenye uzoefu ili waweze kufundishwa na kuongozwa. Wanapaswa kuwaambia: “Hupaswi kuiga ishara zangu wala sauti yangu, kiasi kwamba watu wasijue kama ni wewe unayezungumza au ni mimi ninayezungumza. Unapaswa kusimama ukiwa umevaa silaha zako mwenyewe, ukiwa na tabia yako mwenyewe iliyotakaswa na Mungu. Usichukue tabia yangu, wala ishara zangu, wala sauti yangu, wala matamshi au mionekano yangu ya usemi, wala maneno yangu.” —*Manuscript 19b, 1890. {VSS 299.2}*

SURA YA 53—USHAHIDI HALISI WA MAHUBIRI

Ushahidi wa Maisha ya Kumcha Mungu—Haitoshi kutetea kweli kwa hoja pekee; ushahidi wenye nguvu zaidi wa thamani yake unaonekana katika maisha ya kumcha Mungu. Bila ushahidi huo, hata kauli zilizo wazi na zenye kushawishi zaidi zitakosa uzito na nguvu ya kushinda, kwa maana nguvu yetu iko katika kuunganishwa na Mungu kupitia Roho Wake Mtakatifu. Uasi humtenga mwanadamu na ukaribu huu mtakatifu pamoja na Chanzo cha nguvu na hekima yetu. —*The S.D.A. Bible Commentary*, juz. 2, uk. 998. {VSS 301.1}

Mahubiri ya Unafiki—Kuhubiri jambo ambalo hatulitekelezi katika maisha yetu ni kuwathibitishia wenye dhambi waendeleo katika hali yao ya kutokutubu. Maonyo ya dhati na bidii zaidi ya kutembea katika nuru hayatakuwa na matokeo, ikiwa msemaji mwenyewe anapuuza kufuata nuru ambayo Kristo amempa. —*The Review and Herald*, Juni 20, 1882. {VSS 301.2}

Uimara wa Tabia—Wale wanaofanya kazi kwa ajili ya Kristo wanapaswa kuwa wanaume na wanawake wenye busara kubwa, ili wale wasioelewa mafundisho yao waongozwe kuwaheshimu na kuwaona kuwa watu wasio na ushupavu wa kupindukia au kupitiliza, wasio na pupa wala matendo ya haraka yasiyo na hekima. Hotuba zao, mwenendo wao, na mazungumzo yao vinapaswa kuwa vya namna ambavyo vitawaongoza watu kufikia hitimisho kwamba wachungaji hawa ni watu wenye mawazo ya kina, wenye tabia thabiti, wanaomcha na kumpenda Baba yao wa mbinguni. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 170–171. {VSS 301.3}

Umuhimu wa Uzoefu Binafsi—Kila mchungaji wa kundi la Mungu anapaswa kutoa ushuhuda ulio wazi na wa uaminifu. Hali ya moyo inapaswa kuwa jambo letu la kwanza na la muhimu zaidi. “**Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.**” (*Warumi 10:10*) Lakini maneno pekee hayana thamani. Kuhubiri Neno halafu kuishi kinyume na Neno hilo hulifanya Neno la Mungu lipoteze nguvu yake katika maisha ya watu. Maarifa ya midomo, desturi, kaida na taratibu za kidini vina thamani ndogo ikiwa Kristo hakai ndani ya nafsi. {VSSw 302.1}

Tunapaswa kuilinda mioyo ya watu kama wale watakaotoa hesabu mbele za Mungu. Tunapaswa kumtakasa Bwana Mungu ndani ya mioyo yetu; ndipo tutakapokuwa wanaume na wanawake wa imani, maombi, na nguvu. Kuna kazi kubwa inayopaswa kufanywa. Moyo lazima ulindwe kwa uaminifu; vinginevyo kiburi na uasi vitatawala ndani yake. Maovu yaliyo nje yataamsha maovu yaliyo ndani, na nafsi itatangatanga katika ukungu wake yenyewe ulioumba, huku ikimlaumu mtu mwingine kwa matokeo ya mwenendo wake usio wa Kikristo. — *Manuscript 11, 1899. {VSSw 302.2}*

Kristo Kama Kitovu/Kituo Kikuu—Wale ambao hawajajitoa kikamilifu katika kazi ya Mungu wamejipotezea mambo mengi wao wenyewe, na hawajaweza kulifikishia kanisa kanuni sahihi za Ukristo. Ubinafsi haujafichwa ndani ya Kristo. Wale wanaoshughulika na mambo matakatifu hawajakua katika neema wala katika ujuzi wa Kweli za kina za Neno la Mungu ili kufikia kimo kamili cha wanaume na wanawake katika Kristo Yesu. Wamepunguka katika kipimo cha Mungu. Baadhi yao wamehubiri madhabahuni, lakini wameshindwa kuwafikia watu kwa sababu hawakuwa na nguvu ya utakaso ya Kristo ndani ya mioyo yao. Hawajawa na uhusiano wa karibu binafsi na watu, na kwa hiyo hawajapata manufaa ambayo wangeweza kupata. Si wote waliomwasilisha Kristo kama Kituo Kikuu ambacho wote wanapaswa kukifikia, wakitambua kwamba Yeye Ndiye Mwanzilishi na Mkamilishaji wa ukombozi wao, na kwamba Yeye Ndiye yote katika yote. Matokeo ya kazi yao yanaonyesha wazi kwamba hawakuwa na uzoefu wa kina wa kibinafsi waliopaswa kuwa nao; bali walihitaji uchaji Mungu wa ndani zaidi na kujitoa kusiko na ubinafsi katika kazi hiyo. —*Manuscript 12, 1891. {VSS 302.3}*

Kushindwa Kulitenda Neno—Matendo huzungumza kwa sauti kubwa kuliko maneno. Mahubiri yanayotolewa madhabahuni hupingwa na mahubiri yanayotolewa kupitia maisha ya wale wanaodai kuwa watetezi wa Kweli. Ni kwa sababu ya kushindwa kuyatenda maneno ya Kristo ndipo laana inakuja juu ya makanisa yetu. Ikiwa Kristo haishi ndani ya chombo Chake cha kibinadamu, basi mazingira yanapokuwa mazuri kwa maendeleo ya tabia, sifa za Shetani zitaonekana. Maisha mema na yenye heshima ndiyo mahubiri yenye nguvu zaidi yanayoitetea imani ya Kikristo. Ikiwa tungeishi maisha ya namna hiyo, dhamiri zetu lazima ziamshwe na kuimarishwa kwa njia ya kuwasiliana daima na Neno la Mungu. Nafsi zetu lazima zizoe kiwango cha mbinguni, na tunapaswa kuepuka kila njia inayopotoka kutoka katika haki. —*Letter 71, 1895. {VSS 303.1}*

Kukua Daima Katika Neema—Isipokuwa kuwe na kukua daima katika neema, tutakosa maneno yanayofaa kwa kila wakati na kila hali. Sababu inayowafanya wahudumu wetu wengi wahubiri mahubiri yasiyo na nguvu na yasiyo na uhai ni kwamba wanaruhusu mambo mbalimbali ya kidunia yachukue muda wao na fikira zao. Zungumza na moyo wako mwenyewe, kisha zungumza na Mungu. Usipofanya hivyo, juhudi zako zitakuwa bure, kwa sababu zitakosa Kristo kutokana na haraka isiyotakaswa na mkanganyiko unaosababishwa na mambo ya kidunia. —*Manuscript 101, 1902.* {VSS 304.1}

Kuhubiri na Kutenda—Katika kipindi hiki, kila mhudumu wa Kristo anapaswa kuzingatia agizo ambalo Paulo alimpa Timotheo: *“Jitunze nafsi yako, na mafundisho yako. Dumu katika mambo hayo; maana kwa kufanya hivyo utajiokoa nafsi yako na wale wakusikiao pia.”* (1 Timotheo 4:16) Mhudumu anapaswa kuzingatia tabia yake, maneno yake, mwenendo wake, na mafundisho yake. Anapaswa kutenda kulingana na mafundisho anayoyahubiri; vinginevyo, yeye mwenyewe anahitaji kufundishwa kanuni za kwanza za mafundisho safi. {VSS 304.2}

Bwana amenipa ujumbe kwa ajili yako. Wahudumu wa injili wanapaswa kuusalimisha ubinafsi chini ya Kristo daima. Lakini katika hali yako ya sasa ya moyo, hujatii kikamilifu mapenzi wala uongozi wa Mungu. Ubinafsi—nafsi yako dhaifu na yenye hali ya kutokujiweza—unaonekana katika kila jambo. Wakati nafsi inapokufa, amani ya Kristo itautawala moyo. Kwa kuwa wewe ni mchungaji wa injili, una wajibu mtakatifu sana mbele za Mungu wa kuwa mwenye hekima; si kwa kujiona kuwa mwenye hekima katika mawazo yako mwenyewe, bali kwa kutafuta hekima itokayo kwa Mungu. {VSSsw 304.3}

Kila siku mielekeo ya kurithi kuelekea uovu itapigania kutawala. Kila siku unapaswa kupambana dhidi ya tabia zako zisizofaa, mpaka vitu vyote vinavyohitaji kutenganishwa nawe viondolewe. Ndipo utaweza kujichunguza kwa uaminifu na hekima, na kumjia Bwana kwa moyo uliotakaswa. Utaweza kuona mapema maovu yatakayotokea ikiwa hutabadilika kwa kuepuka chanzo kinachosababisha matokeo hayo. {VSSsw 304.4}

Sasa kuliko wakati mwingine wowote, unahitaji kuelewa nguvu inayotiisha, inayolainisha, itawalayo, na ibadilishayo ya tabia ya Kweli inayofanana na Kristo.

Unahitaji kuelewa vita tunavyopigana. Nguvu ya maisha matakafu ina thamani kubwa zaidi kuliko hotuba zote za mafundisho. **{VSSw 305.1}**

Tunapaswa sasa kuliko wakati mwingine wowote kuomba kwa moyo na kwa sauti kwamba Roho wa Kristo atutumie katika huduma Yake kwa njia ya utakaso wa Roho. Tunapaswa kuomba ili, kwa kushirikiana na watenda kazi wenzetu, tujenge ufalme wa Mungu. Hatupaswi kamwe kuridhika na hali tuliyo nayo, bali tunapaswa kusonga mbele daima, tukitafuta bidii kubwa zaidi na juhudi yenye nguvu zaidi. Tamaa kuu ya mioyo yetu inapaswa kuwa kuhesabiwa miongoni mwa watu wa Mungu walio wapole na wanyenyekevu. Ndipo tutaweza kutafuta nafsi na kuzipata kwa ajili ya Kristo. **{VSSw 305.2}**

Wale wanaohudumu kwa Neno na mafundisho lazima kwanza wawe washiriki wa matunda ya Roho. Kumbuka jambo hili. Tawala tabia yako, ndipo amani na kuridhika vitapata nafasi katika nafsi yako. Ikiwa unatamani moyo wako ujazwe na upendo wa Mungu, kuza roho ya shukrani kwa ajili ya fursa isiyoelezeka ya kujua Kweli. Ukiacha kujitazama mwenyewe na kumtazama Kristo, utabadilishwa kutoka utukufu hadi utukufu, kutoka tabia moja hadi tabia nyingine, na utafurahia upendo Wake wa ukombozi. **{VSSw 305.3}**

Hatuna muda wa kuwa na wasiwasi, kufadhaika na kujisumbua kwa ajili yetu wenyewe wala muda wa kutazama upande wa giza. Kuna nafsi zinazopaswa kuokolewa. Tunapaswa kuishi ndani ya Kristo, na Kristo lazima akae ndani yetu; vinginevyo tutahubiri na kufanya kazi bure. Wale walio ndugu katika imani wanapaswa kusimama pamoja katika umoja, wakijitahidi kutimiza ombi la Kristo kwa Baba Yake. Hebu tuache wasiwasi na kujisumbua. Acheni kuondoa wivu wote na mashaka mabaya. Acheni tumvae Kristo na kutembea katika nuru ya Jua la Haki. Hubiri Neno. Liishi Neno. Ndipo roho zitakapoongolewaa. **{VSSw 305.4}**

Kwa sasa hali yako ya kiroho ni kikwazo katika juhudi zako bora. Tunayo kweli tukufu zaidi ambazo zimewahi kutolewa kwa wanadamu. Je, tunazitendeaje? Ukiwa ndani ya Kristo, ukiwa umefia nafsi, fungua kinywa chako, Naye Mungu atakijaza. Kristo atagusa mioyo ya wasikilizaji wako. **{VSSw 306.1}**

Kushirikiana na Mungu maana yake ni kumruhusu Mungu kushirikiana nasi. Kushirikiana na ndugu zetu huwapa nafasi wote wanaofanya kazi ya Mungu kusimama pamoja. Ushirikiano unahitajika sana sasa. Usitafute nafasi ya juu zaidi;

kwa maana ukifanya hivyo, utapewa nafasi ya chini zaidi. Uwe na ujasiri katika Bwana. Lakini usifikiri kwamba wewe ndiye chombo pekee ambacho kupitia hicho Mungu atafanya kazi. Kwa ajili ya Kristo, fanya lililo bora zaidi bila kusema neno lolote la kutokuwa na shukrani kwa Mungu au kwa ndugu zako. Ndipo Bwana atakubariki. Hatuna hata muda mfupi au sekunde ya kupoteza kwa majuto au kulaumiana. {VSSsw 306.2}

Usiwapelekee wanadamu shida zako, kwa maana huenda hawana hekima kubwa kuliko wewe mwenyewe. Zile shida zako kwa Yeye anayesikia na kujibu maombi. Fanya kazi, fanya kazi kwa ajili ya nafsi hii dhaifu na ile nafsi dhaifu. Ondoa kichwa chako katika vitabu na mkono wako katika kuandika kwa muda; tafuta wokovu wa wale walio tayari kupotea. Kwa dhati na bidii kubwa namna gani tunapaswa kujitoa katika kazi ya kuokoa nafsi, kama watu watakaotoa hesabu mbele za Mungu. — *Letter 119, 1900.* {VSSsw 306.3}

Athari ya Upendo wa Yesu Katika Moyo wa Mhubiri—Kumekuwa na mahubiri mazima yaliyokuwa makavu na yasiyo na Kristo, ambapo jina la Yesu limetajwa kwa shida sana au halikutajwa kabisa. Moyo wa msemaji haujaguswa wala kuyeyushwa na upendo wa Yesu. Badala yake, amejikita katika nadharia kavu. Hakuna mvuto au mguso mkubwa unaozalishwa. Msemaji hana upako wa kiungu; basi ataweze kugusa mioyo ya watu? Tunapaswa kutubu na kubadilishwa—naam, mhubiri mwenyewe anapaswa kwanza kubadilishwa. Watu wanapaswa kuinuliwa mbele yao Kristo, na wanapaswa kusihiwa: “*Tazameni, mkaishi.*” — *Selected Messages, Kitabu cha 3, uk. 184.* {VSSsw 307.1}

Tabia Kama Kielelezo cha Maneno ya Mwalimu—Mamlaka yenye heshima inahitajika kwa mwalimu; vinginevyo atakosa uwezo unaomfanya awe mwalimu mwenye mafanikio. Watoto hutambua haraka udhaifu au kasoro yoyote katika tabia ya mwalimu. Mwenendo wa mwalimu huwaachia mvuto fulani. Maneno anayosema mwalimu hayatawapa wanafunzi umbo linalofaa isipokuwa waone katika tabia yake mfano wa kile anachofundisha. — **Mashauri kuhusu Kazi ya Shule ya Sabato, uk. 98.** {VSSsw 307.2}

Mwenendo na Uso na Mijongo ya Mwalimu [deportment] na Heshima ya Mwanafunzi kwa Mungu—Yeye anayekubali jukumu la kuwa mwalimu, hata kama hajahitimu kikamilifu, akitambua uzito wa nafasi yake, atafanya kila juhudi kujifunza. Atakuza heshima, furaha, na uthabiti. Mwenendo wake unapaswa kuwa

Nhandi Masunga na Grace Momadi Masaka-Jersey 2026 July

wa namna ambayo darasa lake litafundishwa kuwa na mawazo matakatiifu na heshima kwa Mungu. Ingawa mawazo yanaweza kuwasilishwa kwa urahisi, lugha inayotumika kuzungumza juu ya Mungu, Kristo, mateso Yake, na ufufuo Wake—ikiwa mambo hayo ni halisi moyoni mwa mwalimu—inapaswa kuinua mawazo ya wanafunzi juu ya mambo ya duniani na kuwafanya wahisi kwamba wako mbele za Yeye Aliye Mkuu na asiye na mwisho. — **Mashauri kuhusu Kazi ya Shule ya Sabato, uk. 97. {VSS 307.3}**

SURA YA 54—KRISTO NDIYE JUMLA NA KIINI

Utukufu wa Mungu Aliyefanyika Mwili—Ikiwa Yesu angekuwa jumla na kiini cha kila mahubiri, wenye dhambi wangepaswa mioyoni mwao na kuhukumiwa kwa nuru ya Kweli, na kupitia ujumbe unaowasilishwa wangepaswa kile wanachopaswa kufanya ili wapate wokovu. Kwa hiyo, mwinue Kristo, Mtu wa Kalvari, juu zaidi na zaidi. Ni nani awezaye kueleza utukufu wa Mungu aliyefanyika mwili? Ni lugha gani inayoweza kueleza kwa ukamilifu ukuu na utukufu huo? Hakika, si wale walioelimika katika hekima ya ulimwengu huu pekee ndio wenye ufasaha wa kweli. —**Ellen G. White, Manuscript 176, 1899. {VSSw 311.1}**

Msingi wa Injili—Mahubiri ya kinadharia yana umuhimu wake, kwa sababu huwasaidia watu kuona mnyororo wa Kweli, kiungo baada ya kiungo, unaoungana na kuunda umoja mkamilifu. Hata hivyo, hakuna mahubiri yanayopaswa kutolewa bila kumweka Kristo na Kristo aliyesulubiwa kuwa msingi mkuu wa injili, kwa maana Yeye Ndiye kiini cha tumaini la wokovu. —**Ellen G. White, Watendakazi wa Injili, uk. 158. {VSS 311.2}**

Mfano Halisi na wa Kweli kwa Wahudumu—Je, wahudumu wetu hawatawapaswa kwa maombi ya dhati ili wapate upako mtakatifu, ili wasilete katika huduma yao mambo yasiyo ya muhimu wala yasiyokuwa na manufaa katika wakati huu wa maana? Hawapaswi kuingiza katika kazi yao mambo yale yanayoweza kusikika katika makanisa mengine ya madhehebu mbalimbali. Badala yake, wanapaswa daima kumweka mbele ya wasikilizaji wao Kristo Mwokozi aliyeinuliwa, ili kuwazuia waongofu wao wasimgande mwanadamu, kubeba sura yake, au kuiga njia zake katika mazungumzo na mwenendo wao. Bwana ana watenda kazi wa aina mbalimbali, ambao anawatumia kuwafikia watu kwa njia tofauti. Njia za mtu mmoja hazipaswi kuonekana kuwa kamilifu kiasi cha kupokelewa kama njia pekee yake katika kusanyiko lolote. Kristo Ndiye Mfano wetu mkuu. —**Ellen G. White, Manuscript 21a, 1894. {VSS 311.3}**

Mafundisho Rahisi ya Kristo—Kwa Jina la Yesu Kristo, ninatoa wito kwa kanisa ambalo limewekwa kuwa mtunzaji wa kweli kuu na za thamani. Mungu amelipa kanisa hazina hizi si ili zikusanywe na kufichwa kwa ulafi, wala kuzikwa ardhini, bali ili zigawanywe kwa wengine, ili wengine nao wapate kubarikiwa na kutajirika pamoja nasi. Basi, tutafanyaje kazi? Walei pamoja na wahudumu wanapaswa kufuata mfano wa Kristo na kukutana na watu pale walipo. Nawasihi mfanye kazi kwa njia ya Neno na mafundisho; msizidishe ugumu wa kazi hii wala kupita

kiwango cha uelewa wa watu wa kawaida kiasi kwamba washindwe kuwafuata. Na hata wakifanikiwa kuwafuata, wasije wakakosa kupata manufaa na baraka zinazokusudiwa. Fundisheni mafundisho sahili/rahisi ya Kristo. Simulieni kisa chenye kugusa moyo ya maisha Yake ya kujikana nafsi na kujitoa sadaka/dhabihu. Waelezeni juu ya kujinyenyekeza Kwake, kifo Chake, ufufuo Wake, na kupaa Kwake mbinguni, pamoja na huduma Yake ya kuwaombea katika nyua/mahakama za Mungu. Waambieni kwamba: ***“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.”*** (Yohana 3:16) — *Manuscript 38, 1894.* {VSS 312.1}

Lishe ya Kiroho—Miongoni mwa wote wanaodai kuwa Wakristo, Waadventista wa Sabato wanapaswa kuwa wa kwanza kabisa kumwinua Kristo mbele ya ulimwengu. Wahudumu/wachungaji wetu wanapaswa daima kuwa tayari kuwaelekeza wanaume na wanawake kwa Kristo, Yeye aliyesema Mwenyewe: ***“Mimi Ndimi Chakula cha uzima.”*** Kwa hiyo, wale wanaohudumia mahitaji ya kiroho ya watu wanapaswa kuwasomea Maneno ya Kristo: ***“Mimi Ndimi chakula chenye uzima kilichoshuka kutoka mbinguni; mtu akila chakula hiki, ataishi milele. Na chakula nitakachotoa Mimi ni mwili Wangu, kwa ajili ya uzima wa ulimwengu.”*** Yohana 6:51 {VSS 313.1}

Mara nyingi watu hupewa mahubiri yasiyo na Mkate wa Uzima, yaani chakula muhimu kwa ukuaji wa kiroho, kwa sababu wale ambao hawajaupata mkate huo wa kiroho hawawezi kuwagawia wengine kile ambacho wao wenyewe hawajakipokea; lakini wale ambao wamekuwa wakijilisha wenyewe kwa Mkate wa Uzima wataweza kuwagawia wengine kwa wingi. {VSS 313.2}

Nimehisi huzuni kubwa nilipowaona wahudumu wakitembea na kufanya kazi katika mwanga wa cheche walizowasha wenyewe, yaani, wachungaji ambao hawakuwa wakipokea lishe ya kiroho kutoka kwa Kristo, aliye Mkate wa Uzima. Nafsi zao wenyewe zilikuwa zimekosa mana ya mbinguni kama vile vilima vya Gilboa vilivyokosa umande na mvua, kwa sababu katika mioyo yao Kristo hakuwa Uwepo unaodumu. Basi, wangewezaje kusema kwa uelewa wa kweli au akili mahiri juu Yake ambaye hawakuwa wamemjua kwa uzoefu binafsi? —*Manuscript 21, 1891.* {VSS 313.3}

Mafundisho ya Vitendo Pamoja na Unabii—Maneno machache yenye nguvu kuhusu jambo fulani la mafundisho yataimarisha Ukweli huo akilini kwa uthabiti

zaidi kuliko kuwasilisha wingi wa mambo ambayo hayatoi jambo lolote lililo wazi na bayana katika akili za wale wasiojua imani yetu. Kwa hiyo, mafundisho ya vitendo ya Kristo yanapaswa kuingizwa pamoja na unabii, huku daima kukiwa na mvuto unaolainisha moyo na unaotawala wa Roho wa Mungu juu ya mioyo yetu wenyewe. Pia, kujikana nafsi na mateso ya Kristo vinapaswa kuonekana katika kazi zetu, na upendo mkuu ambao ametupenda nao unapaswa kudhihirika katika juhudi zetu zote. —*Letter 48, 1886.* {VSS 313.4}

Kristo Ndani ya Moyo—Mahubiri yenye Kristo kidogo sana na haki Yake kidogo sana hutolewa madhabahuni, nayo huwa ni mahubiri yasiyo na Kristo. Kwa sababu hiyo, kuhubiri kwa udhihirisho wa Roho ni jambo lisilowezezekana kabisa kwa wale ambao hawana Kristo. Mahubiri yao huwa dhaifu, matupu, na yasiyo na lishe ya kiroho, kwa kuwa hawana Kristo wa kwenda Naye katika maisha yao binafsi. Badala yake, wamejaa majivuno na majigambo, kiburi, na kujithamini; wakisema mabaya juu ya mambo wasiyoyafahamu kwa kweli, na huonyesha kutokuwa na subira kwa kila jambo lisiloendana na mtazamo wao. Hata hudhihaki na kukejeli mambo matakatifu, kwa sababu hawaelewi kwamba mambo ya kiroho hutambuliwa kwa njia ya kiroho. Kwa kupotosha na kugeuza Kweli kuwa uongo, wanajidhalilisha wenyewe. —*Manuscript 15, 1886.* {VSS 314.1}

Nguvu ya Roho—Lengo letu halipaswi kuwa kuzungumza tu juu ya mambo mazuri yanayofurahisha masikio na kuvuta usikivu wa watu, bali tunapaswa kumtangaza Kristo na Kristo aliyesulubiwa, ili nafsi zilizokufa katika makosa na dhambi ziogope, zichochewe, na kuhuishwa. Wale wanaotafuta kuwafundisha wengine wanapaswa kwanza kubadilishwa/kuongolewa kwa Kristo; wanapaswa kumsihi Mungu awajaze Roho Wake Mtakatifu kabla hawajamwinua Kristo kuwa tumaini pekee la mwenye dhambi. Maneno yaliyopambwa sana, hadithi za kuvutia, mifano ya kuchekesha, na visa mbalimbali haviwezi kumshawishi mwenye dhambi, kwa sababu watu husikiliza maneno kama hayo kama wanavyosikiliza wimbo mtamu, na watenda kazi huvuna masuke machache sana katika ghala la Mungu. Kwa hiyo, ujumbe ambao mwenye dhambi anapaswa kuusikia ni huu: ***“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.”*** (Yohana 3:16) Na Kweli itaunyenyekeza na kuufanya moyo wa mwalimu kuwa laini, kwa sababu ataona umuhimu wake wa vitendo katika maisha yake. —*Manuscript 12, 1891.* {VSS 314.2}

Dawa ya Uzima Itokayo Msalabani—Msalaba, yaani msalaba wa Kalvari, unapowasilishwa tena na tena na kuelezwa kwa uwazi katika kila mahubiri, utakuwa dawa ya kuponya maisha na utafunua uzuri pamoja na ubora wa wema. Hata hivyo, wale wanaobishana kuhusu uhalisi wa Maandiko na kuhoji mamlaka ya ufunuo wa Mungu hawataathiriwa na ujumbe huo. —*Manuscript 20, 1893.* {VSS 315.1}

Yesu Ndani ya Mahubiri— “*Na uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe, Mungu wa pekee wa Kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.*” (Yohana 17:3) Neno la milele lilifanyika mwili na kukaa kwetu, na mada hii itashinda hali ya kutokuamini; lakini kwa huzuni kubwa, Yesu ameondolewa katika mahubiri mengi sana yaliyotolewa na wahudumu wa Waadventista wa Sabato. Kwa nini? Ni kwa sababu wahudumu hao hawakuwa na Yesu akikaa ndani ya mioyo yao kwa imani, wala hawakuwa wamevikwa haki ya Kristo. —*Manuscript 16, 1890.* {VSS 315.2}

SURA YA 55—AHADI YA ROHO MTAKATIFU

Matokeo ya Kunyamaza Kuhusu Jambo Hili—Muda mfupi kabla ya kuwaacha wanafunzi Wake na kwenda katika makao ya mbinguni, Yesu aliwatia moyo kwa ahadi ya Roho Mtakatifu. Ahadi hii ni yetu kama ilivyokuwa yao; lakini ni mara chache sana inapowasilishwa kwa watu na kufundishwa katika kanisa. Kwa sababu ya ukimya huu kuhusu jambo hili muhimu sana, ni ahadi gani nyingine ambayo tunaifahamu kwa uchache zaidi katika uzoefu wake wa vitendo kuliko ahadi hii kuu

ya kipawa cha Roho Mtakatifu, ambaye kupitia Kwake nguvu na ufanisi hutolewa kwa kazi zetu zote za kiroho? Ahadi ya Roho Mtakatifu hutajwa kwa kupita katika mahubiri, huguswa kwa kifupi tu hapa na pale kwa bahati, na hapo ndipo jambo hilo huishia. Unabii umepewa nafasi kubwa, mafundisho yamefafanuliwa, lakini kile ambacho ni cha lazima kabisa kwa kanisa ili likue katika nguvu na ufanisi wa kiroho, ili mahubiri yaweze kuambatana na usadikisho wa mioyo, na ili nafsi zibadilishwe kwa Mungu, kwa kiasi kikubwa kimepuuzwa katika juhudi za huduma. — *Manuscript 12, 1891.* {VSS 317.1}

Umuhimu wa Kuwasilisha Roho Mtakatifu Katika Kila Hubiri—Roho Mtakatifu anapaswa kuwasilishwa katika kila mahubiri. Ni kauli za ajabu jinsi gani ambazo Kristo amezitoa kuhusu Mwakilishi Wake kwa ulimwengu! Hili ndilo somo la kutia moyo linalopaswa kuwekwa daima mbele ya watu. Tunapofahamu kazi na huduma ya Roho Mtakatifu, tutapokea baraka zote zinazopatikana kupitia Kwake. Yeye atatufanya kuwa wakamilifu ndani ya Kristo. —*Manuscript 8, 1898.* {VSS 317.2}

Chanzo cha Ukame wa Kiroho—Wahudumu wanaohubiri Kweli ya wakati huu watakiri umuhimu wa ushawishi wa Roho wa Mungu katika kuwashawishi watu kuhusu dhambi na katika kuleta uongofu wa nafsi; na ushawishi huu lazima uambatane na kuhubiriwa kwa Neno. Lakini hawatambui umuhimu wake kwa kiwango cha kutosha ili wawe na ufahamu wa kina na wa vitendo kuhusu jambo hilo. Upungufu wa neema na nguvu ya ushawishi wa Mungu kupitia Kweli katika mioyo yao wenyewe huwazuia kutambua mambo ya kiroho na kuwafanya washindwe kuonyesha umuhimu wake halisi kwa kanisa. Kwa hiyo, wanaendelea katika huduma yao wakiwa dhaifu/mbilikimo na wamepungukiwa katika ukuaji wa kiroho, kwa sababu katika huduma zao wana dini ya kisheria. Nguvu ya neema ya Mungu haionekani kwao kuwa hitaji hai, lenye matokeo, na kanuni inayodumu katika maisha. —*Manuscript 27, 1889.* {VSS 318.1}

SURA YA 56—KWELI YA MILELE

Umuhimu wa Mahubiri Mapya—Kuifahamu kwa kina Kweli za Maandiko humpa mwalimu wa Kweli sifa zinazomwezesha kuwa mwakilishi wa Kristo; kwa maana roho ya mafundisho ya Mwokozi humpa nguvu na uwazi katika mafundisho yake na katika maombi yake. Ushuhuda wake hautakuwa mwembamba wala usio na uhai, wala hatarudia tena na tena mahubiri yale yale aliyoyazoea, kwa kuwa akili yake itakuwa wazi daima kupokea mwangaza mpya kutoka kwa Roho Mtakatifu. — *Watendakazi wa Injili, uk. 252. {VSSsw 319.1}*

Wahubiri Waliobadilishwa—Wakati watu wanapobadilishwa Kweli, mabishano/migogoro na mijadala isiyo ya lazima hukoma; ndipo Kweli iliyo wazi na inayochunguza moyo hutangazwa na midomo iliyoguswa kwa kaa la moto kutoka madhabahuni pa Mungu. —*Ellen G. White, The Review and Herald, Februari 21, 1899. {VSSw 319.2}*

Uwasilishaji Wazi wa Kweli—Kila mahali kuna mioyo inayomlilia Mungu aliye hai, lakini katika makanisa yametolewa mahubiri yasiyotosheleza nafsi zenye njaa ya kiroho, kwa sababu katika mahubiri hayo hakuna udhihirisho wa nguvu za Mungu unaogusa akili na kuleta mng’ao wa kiroho ndani ya nafsi. Wasikilizaji hawawezi kusema: *“Je! Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani, na kutufunulia Maandiko?”* (Luka 24:32) Mafundisho mengi yanayotolewa hayana nguvu ya kumwamsha mkosaji wala kuleta usadikisho wa dhambi moyoni. Kwa hiyo, watu wanaokuja kusikiliza Neno la Mungu wanahitaji uwasilishaji wa Kweli ulio wazi, wa moja kwa moja, na usio na kificho. — *Shuhuda kwa Kanisa, juz. 6, uk. 53. {VSS 319.3}*

Wito kwa Watu Wenye Nafasi za Juu—Watu wenye nafasi za juu za uaminifu katika ulimwengu wataguswa na kuchangamshwa na pia kuvutiwa na maelezo ya Kweli yaliyo wazi, ya moja kwa moja, na yanayotegemea Maandiko. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, uk. 557. {VSS 320.1}*

Sauti Kama Tarumbeta—Mhudumu wa Kweli wa injili hatasimama mbele ya watu ili kusema maneno laini ya kuwafurahisha wala kupaza sauti akisema, *“Amani na usalama,”* kwa sababu anatambua hatari zinazotishia nafsi na hivyo huiwasilisha kweli kama ilivyo ndani ya Yesu. Kweli hutoka midomoni mwake ikiwa wazi, dhahiri, na thabiti, kana kwamba anaamini kwa moyo wote kwamba maneno anayosema yatakuwa **harufu ya uzima iletayo uzima au ya mauti iletayo mauti**. Maneno ya mhudumu anayejua kwamba anaye Roho na nguvu za Mungu yataamsha dhamiri za wasikilizaji wake. — *The Review and Herald, Machi 29, 1906. {VSS 320.2}*

Athari za Mahubiri Yenye Maneno Laini—Watumishi wa Mungu wanapaswa kuinua sauti zao kama tarumbeta na kuwaonyesha watu makosa yao. Mahubiri yenye maneno laini yanayotolewa mara nyingi, hayatoi mvuto wa kudumu, kwa sababu mioyo ya watu haiguswi au kukatwa kwa kina; kwani Kweli zilizo wazi na zenye

nguvu za Neno la Mungu hazijawekwa mbele yao. — *Watendakazi wa Injili, uk. 149. {VSS 320.3}*

Habari Njema ya Wokovu—Matumizi ya juu zaidi ya uwezo wa kusema ni kuwasilisha kweli ya Mungu; kwa hiyo, mahali popote wasikilizaji wanapokuwa na bila kujali aina ya watu wanaounda kusanyiko hilo, mshuhudiaji wa Kristo anapaswa kusema Kweli iliyo wazi na isiyopambwa kwa hila. Anapaswa kuwahudumia wasikilizaji wake kwa neema, na maneno yake yanapaswa kupatana na mafundisho ya Kristo. Nafsi iliyobadilishwa Kweli itakuwa na midomo iliyoguswa na moto mtakatifu wa utakaso, na kwa kila mtu anayekutana naye itatafuta nafasi ya kuzungumza habari njema ya wokovu. Kwa sababu anaamini, atasema yale yaliyojaa moyoni mwake; atasimama kama mnenaji wa Mungu, akizungumza na wanadamu Maneno ya uzima na wokovu. —*Letter 222, 1907. {VSS 320.4}*

Mana Mpya—Umehangaika sana kuwasilisha mawazo ambayo yangeleta utukufu kwako mwenyewe, ukifikiri kwamba ni lazima uzungumzie mada ambazo hazitoi mwanga kwa akili kuhusu Kweli muhimu wala hazifanyi njia ya wokovu kuwa wazi zaidi. Kwa ajili ya Kristo, shikilia jambo kuu. Katika kila mahubiri vunja mkate wa uzima, wasilisha mana mpya, weka mbele ya nafsi wajibu mtakatifu ambao Mungu ameuweka juu yao, na elekeza fikira zao katika mambo ya milele. Waelekeze watu kwenye maswali ya msingi na uwaongoze kufikia uamuzi, ukiwauliza: **“Mtafanya nini?”** Shirikiana na mawakala wa mbinguni. Unaporuhusu akili yako iondoke katika njia zilizo wazi za Kweli na kushughulishwa na mada zinazopendeza mawazo yako mwenyewe, unapoteza muda tu; kwa sababu Roho Mtakatifu hafanyi kazi pamoja nawe katika hali hiyo, na hivyo unafanya kosa. — *Letter 29, 1895. {VSS 321.1}*

Ubinafsi Uwekwe Pembeni—Katika sura ya kwanza ya Waraka wa Kwanza kwa Wakorintho, Paulo ametupatia mafundisho ambayo kila mtenda-kazi wa Kweli anapaswa kuyasoma, hasa maneno haya: **“bali sisi tunamhubiri Kristo, aliyesulibiwa; kwa Wayahudi ni kikwazo, na kwa Wayunani ni upuzi; bali kwao waitwao, Wayahudi kwa Wayunani, ni Kristo, nguvu ya Mungu, na hekima ya Mungu. Kwa sababu upumbavu wa Mungu una hekima zaidi ya wanadamu, na udhaifu wa Mungu una nguvu zaidi ya wanadamu.”** (1 Wakorintho 1:23–25) Hili ni somo lenye umuhimu wa pekee kwa kila mtenda kazi katika shamba la Bwana. Hakutakuwa na kazi thabiti ikiwa watu watahubiri ili kufurahisha masikio ya

wasikilizaji, huku Kweli ikiwa haijawekwa wazi kwa namna itakayowaleta kwenye msalaba wa Yesu Kristo. Mjumbe wa Mungu anapaswa kuwasilisha Kweli za milele kwa uwazi na kuwaonyesha watu hatari inayowakabili wanapopuuzia maslahi ya milele. Wakati ubinafsi ukiwekwa pembeni, Yesu Kristo anapaswa kuinuliwa na kutukuzwa daima. **{VSSsw 322.1}**

*“Maana, ndugu zangu, angalieni mwito wenu, ya kwamba si wengi wenye hekima ya mwilini, si wengi wenye nguvu, si wengi wenye cheo walioitwa; bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu; tena Mungu alivichagua vitu vinyonge vya dunia na vilivyodharauliwa, naam, vitu ambavyo haviko, ili avibatilishe vile vilivyoko; mwenye mwili awaye yote asije akajisifu mbele za Mungu. Bali kwa Yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu Hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi; kusudi, kama ilivyoandikwa, Yeye aonaye fahari na aone fahari juu ya Bwana.” (1 Wakorintho 1:26–31; 1 Wakorintho 2:1–3; 2 Timotheo 2:14) **{VSSsw 322.2}***

*“Basi, ndugu zangu, mimi nilipokuja kwenu, sikuja niwahubiri siri ya Mungu kwa ufasaha wa maneno, wala kwa hekima. Maana naliazimu nisijue neno lolote kwenu ila Yesu Kristo, Naye amesulibiwa. Nami nalikuwako kwenu katika hali ya udhaifu na hofu na matetemeko mengi.” 1 Wakorintho 2:1-3 **{VSSsw 323.1}***

Mtume aliogopa kwamba kazi yake ingesimama katika hekima ya wanadamu badala ya nguvu za Mungu, na hivyo juhudi zake zingekuwa kazi isiyozalisha mavuno. Kwa hiyo, tahadhari ya pekee inapaswa kutolewa kwa maneno haya ya mtume: **“Uwakumbushe mambo hayo, ukiwaonya machoni pa Mungu, wasiwe na mashindano ya maneno, ambayo hayana faida, bali huwaharibu wasikiao.”** (2 Timotheo 2:14) **{VSSsw 323.2}**

Mhudumu wa injili haagizwi kamwe kujitahidi kuwa mhubiri mwenye ustadi wa kujionyesha au mzungumzaji maarufu, bali anaagizwa: **“Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali Neno la Kweli. Jiepushe na maneno yasiyo na maana, ambayo si ya dini; kwa kuwa wataendelea zaidi katika maovu.”** (2 Timotheo 2:15, 16). Je, kila mjumbe wa Mungu atazingatia maneno haya? —*Manuscript 29, 1893.* **{VSSsw 323.3}**

Nuru Mpya na Mawazo Mapya—Baadhi ya wahudumu wetu wana mkusanyiko wa mahubiri wanaoutumia bila mabadiliko mwaka baada ya mwaka; wanatumia vielelezo vilevile, mifano ileile, na karibu maneno yaleyale mara kwa mara. Kwa kufanya hivyo, wameacha kuwa wanafunzi; maendeleo yao yamekoma, na wanalelemewa na mzigo wa mahubiri machache yaliyokaririwa, jambo linalosababisha akili zao kudumaa. Lakini mwanafunzi anayejifunza daima atapata nuru mpya, mawazo mapya, na vito vipya vya Kweli, naye atavipokea kwa shauku. Injili haiwezi kufundishwa wala kuwakilishwa ipasavyo mbele ya wasioamini na wale ambao wameacha kuwa wanafunzi, kana kwamba wamefikia mwisho wa utafiti wao wa Maandiko; kwa sababu kwa namna wanavyolishughulikia Neno la Mungu wanaleta aibu juu ya Kweli. Ikiwa watu wanapata nafasi ya kusikilizwa na umma, basi kiwango bora kabisa cha mahubiri kinahitajika, kwa sababu hadithi za kubuni zinazopendeza huwasilishwa na midomo yenye ufasaha. —*Letter 33, 1886.* {VSSw 323.4}

Kusoma Maandiko Dhidi ya Makisio na Hadithi za Kubuni—Hubiri Neno. Huenda mkawa na akili zenye uwezo wa kubuni mawazo mengi, na huenda mkawa na wabobezi wakubwa kama walivyokuwa walimu wa Kiyahudi katika kuanzisha nadharia mpya; lakini Kristo alisema juu yao: “*Nao waniabudu bure, Wakifundisha mafundisho Yaliyo maagizo ya wanadamu.*” (*Mathayo 15:9*). Walileta mbele ya watu mapokeo, makisio, na hadithi za kubuni za kila aina, na taratibu pamoja na desturi walizoziamuru ziliwafanya watu washindwe kutambua kama walikuwa wakishika Neno la Mungu au walikuwa wakifuata mawazo ya wanadamu. {VSSw 324.1}

Shetani hufurahi sana anapoweza kuchanganya akili za watu kwa njia hiyo. Kwa hiyo, wahudumu wasihubiri mawazo yao wenyewe yaliyobuniwa, bali wanapaswa kuyachunguza Maandiko kwa dhati bidii, wakiwa na ufahamu wa kina na kicho kwamba ikiwa watafundisha kuwa ni mafundisho mambo ambayo hayapatikani katika Neno la Mungu, watakuwa kama wale wanaowakilishwa katika sura ya mwisho ya kitabu cha Ufunuo. —*Letter 207, 1899.* {VSSw 324.2}

SURA YA 57—KWELI ZINAZOPIMA

Kweli kwa Ajili ya Wakati Huu—Katika mahubiri yetu ya mafundisho tunapaswa kukazia au kukita katika ile Kweli kama ilivyo ndani ya Yesu, na kuiwasilisha Kweli ya wakati huu kama ujumbe muhimu kutoka ulimwengu mwingine. Tunapaswa kumwinua Kristo, Mtu wa Kalvari, na kuja kwa kujitoa wakfu katika mahali patakatifu zaidi, tukiendelea katika uzoefu wa utakatifu wa juu zaidi. Hubiri Kweli kwa nguvu ya Mungu itokayo mbinguni; acha Kweli ishike sehemu ya kiroho ya utu wetu wenyewe, ndipo mkondo wa nguvu ya Mungu utakapowasilishwa kwa wale tunaowahutubia. Kumbuka kwamba tunahitaji kuwa na imani iliyoongezeka, kwa maana imani yetu ni ndogo sana. Kitu kinachoweza kutupatia msaada unaohitajika katika wakati wa hatari ni kuifahamu Kweli kwa uelewa wa kina kama ilivyo ndani ya Yesu. Tunauhitaji utu Wake- Asili Yake-His nature; yaani, vipawa vyetu vyote, uwezo wetu wote, na nguvu zetu zote viimarishwe na kuhuishwa kwa Roho wa Kristo. —*Letter 230, 1899.* {VSSw 325.1}

Ujumbe wa Malaika wa Tatu—Kweli ya wakati huu, yaani ujumbe maalumu uliopewa ulimwengu wetu, ambao ni ujumbe wa malaika wa tatu, unajumuisha eneo kubwa lenye hazina za mbinguni. Hakuna mtu anayeweza kujitetea kwa kusema: “Sitaendelea tena kushughulika na ujumbe huu maalumu; nitamhubiri Kristo.” Kwa maana hakuna mtu anayeweza kumhubiri Kristo na kuwasilisha kweli kama ilivyo ndani ya Yesu isipokuwa awasilishe zile Kweli zinazopaswa kuwekwa mbele ya watu katika wakati huu, hasa wakati ambapo matukio muhimu yanaendelea kutokea. —*Manuscript 33, 1897.* {VSSw 325.2}

Kweli Zinazofahamika Kwanza—Yesu alipokuwa akizungumza mbele ya Mafarisayo na Masadukayo alitumia mifano, akificha uwazi wa Kweli chini ya alama na mafumbo, kwa sababu wangetumia vibaya Kweli alizowaeleza; lakini kwa wanafunzi Wake alisema waziwazi. Tunapaswa kujifunza kutoka katika njia ya Kristo ya kufundisha na kuwa waangalifu tusije tukawanyima watu nafasi ya [au kukata masikio] kuelewa kwa kuwasilisha Kweli ambazo -, kwa sababu hazijaelezwa kikamilifu, bado hawako tayari kuzipokea. {VSSw 326.1}

Kweli ambazo tunafanana nazo na watu wengine zinapaswa kufundishwa kwanza, na imani ya wasikilizaji ijengwe; kisha, kadiri watu wanavyoongozwa hatua kwa

hatua, tunaweza kuendelea kuwafundisha mambo mengine muhimu. Hekima kubwa inahitajika katika kuwasilisha Kweli zisizopendwa mbele ya watu wenye chuki au mawazo yaliyokwisha kujengwa, kwa njia ya uangalifu na busara, ili tupate nafasi ya kufikia mioyo yao. Mijadala mara nyingi huwaweka mbele ya watu wasio na mwanga kuhusu msimamo wetu na wasiojua Kweli za Biblia mkusanyiko wa hoja zilizotengenezwa kwa ustadi na kupangwa kwa uangalifu ili kufunika mambo yaliyo wazi ya Kweli. Baadhi ya watu wamejifanya kazi yao kufunika kauli zilizo wazi za Kweli katika Neno la Mungu kwa nadharia zao za udanganyifu, ambazo huzifanya zionekane kuwa za kushawishi kwa wale ambao hawajachunguza mambo hayo wenyewe. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 3, uk. 426. {VSS 326.2}

Hoja Zenye Msingi Imara—Ni muhimu kwamba tunapotetea mafundisho tunayoyaona kuwa nguzo kuu za imani yetu, tusijiruhusu kamwe kutumia hoja ambazo hazina msingi thabiti kabisa. Huenda hoja hizo zikamfunga mdomo mpinzani, lakini haziliheshimu kweli. Tunapaswa kuwasilisha hoja zenye msingi imara ambazo hazitawanyamazisha wapinzani wetu tu, bali pia zitastahimili uchunguzi wa karibu na wa kina zaidi. Kwa wale waliozoeza akili zao katika mijadala ya mapambano kuna hatari kubwa ya kutolishughulikia Neno la Mungu kwa haki na usawa. Tunapokutana na mpinzani, juhudi yetu kuu inapaswa kuwa kuwasilisha mambo kwa namna itakayouamsha usadikisho katika akili yake, badala ya kutafuta tu kumpa mwamini ujasiri wa kushinda mjadala. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 5, uk. 708. {VSS 327.1}

Udhihirisho wa Roho—Kazi yetu katika wakati huu haipaswi kufanywa kwa maneno ya kuvutia yanayotokana na hekima ya kibinadamu, kama yale yaliyotumiwa na wasemaji wa kipagani waliotafuta kupata sifa kutoka kwa watu, bali tunapaswa kusema kwa udhihirisho wa Roho na kwa nguvu ambayo Mungu pekee anaweza kuitoa. Kweli zinazopima watu katika wakati huu zinapaswa kutangazwa na watu ambao midomo yao imeguswa na kaa la moto kutoka madhabahuni pa Mungu, kwa maana mahubiri ya namna hiyo yatakuwa tofauti kabisa na mahubiri yanayosikika kwa kawaida. —*The S.D.A. Bible Commentary*, juz. 6, uk. 1084. {VSS 327.2}

Mkate kwa Wenye Njaa—Nafsi nyingi zina njaa ya Mkate wa Uzima, na kilio chao ni: “Nipeni mkate; msinipatie jiwe. Ninachotaka ni mkate.” Kwa hiyo, walisheni nafsi hizi zinazokufa na zenye njaa. Wahudumu wetu wakumbuke kwamba chakula

kigumu zaidi hakipaswi kupewa watoto wachanga ambao bado hawajajua kanuni za kwanza za Kweli tunazoziamini, kwa sababu katika kila kizazi Bwana amekuwa na ujumbe maalumu kwa watu wa wakati huo; vivyo hivyo, sisi tuna ujumbe kwa watu wa kizazi hiki. Hata hivyo, ingawa tuna mambo mengi ya kusema, huenda tukalazimika kuyazuia baadhi yake kwa muda, kwa sababu watu bado hawajajitayarisha kuyapokea. {VSS 327.3}

Wakati mahubiri yanapotolewa, watu wanaweza kusikiliza kwa shauku, lakini mambo hayo yanaweza kuwa mageni na mapya kabisa kwao, na Shetani huwa tayari kuingiza katika akili zao mawazo mengi yasiyo ya Kweli; adui atatafuta kupotosha na kuwakilisha vibaya maneno ya mhubiri. Basi tufanye nini? Mahubiri yanayoeleza sababu za imani yetu yanapaswa kuchapishwa katika vijitabu vidogo na kusambazwa kwa upana iwezekanavyo, ili kwa njia hiyo uongo na upotoshaji ambao adui wa Kweli hujitahidi kueneza daima utafunuliwa katika hali yake halisi, na watu wapate nafasi ya kujua kwa usahihi kile mhudumu alichosema. Wale wanaoingiza chachu ya Kweli katikati ya wingi wa nadharia na mafundisho ya uongo wanapaswa kutarajia upinzani, kwa sababu mashambulizi ya Shetani yataelekezwa dhidi ya wale wanaotetea Kweli, na wabebaji wa bendera ya kweli watakutana na dhihaka nyingi pamoja na maneno ya kudharau ambayo ni magumu kuvumilia. {VSS 328.1}

Kwa hiyo, ujumbe wa onyo unapaswa kutolewa katika njia kuu na njia ndogo; miji inapaswa kufanyiwa kazi, si kuhubiriwa tu, bali lazima kuwepo na kazi ya nyumba kwa nyumba. —*Manuscript 95, 1894.* {VSS 328.2}

Uzuri wa Kimaadili wa Kweli Zinazopimwa—Unapoanza kazi katika eneo jipya la misheni, uwe mwangalifu kwamba udhaifu wako usije ukainuliwa kuwa sifa njema na hivyo kuzuia kazi ya Mungu, kwa maana tunawaletea watu Kweli zinazopima maisha yao. Katika kila hatua ya kazi yetu, Kweli hizo zinapaswa kuinuliwa ili zionekane katika uzuri wake wa kimaadili mbele ya wale tunaowahudumia; kwa hiyo, usiizunguke Kweli kwa sifa za pekee za tabia yako mwenyewe wala kwa mtindo wako binafsi wa kufanya kazi. —*Letter 12, 1887.* {VSS 328.3}

Ujumbe wa Malaika Watatu—Ni fursa yetu kutarajia mambo makubwa, hata udhihirisho wa Roho wa Mungu, kwa maana hii ndiyo nguvu itakayousadikisha na kuugeza moyo wa mwanadamu. Ujumbe wetu ni ujumbe unaohusu uzima na mauti, hivyo tunapaswa kuufanya ujumbe huu uonekane jinsi ulivyo—yaani, nguvu kuu ya

Mungu; ndipo Bwana atauwezesha kutimiza kusudi lake. Tunapaswa kuuwasilisha kwa nguvu yake yote yenye kushawishi, kwa kuwa ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili umefungamana na ujumbe wa malaika wa tatu, na nguvu ya kutangaza ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili inapaswa kujikita katika ujumbe wa malaika wa tatu. —*Letter 209, 1899.* {VSS 329.1}

Ujumbe Unaopima Watu—Kila mahubiri ambayo hayaangazii nafsi wala hayajibu swali: “Nifanye nini ili niokolewe?” yanapaswa kuondolewa katika mpango wenu. Hubirini ujumbe wa malaika wa tatu unaopima watu, kwa maana ni jambo la lazima kwamba wahudumu wetu wahubiri Kweli inayohusiana moja kwa moja na ujumbe wa wakati huu na wawasilishe mada hizo kwa lugha rahisi na inayoeleweka zaidi. Swali la “*Je, Nifanye nini ili niokolewe?*” pamoja na *haki ya Kristo* ni mada zenye umuhimu mkubwa kwa watu. —*Letter 29, 1895.* {VSS 329.2}

Umuhimu wa Kweli ya Sabato—Sabato ya amri ya nne ndiyo kipimo cha wakati huu; kwa hiyo, kila jambo linalohusiana na kumbukumbu hii kuu linapaswa kuwekwa mbele ya watu. —*Letter 207, 1899.* {VSS 330.1}

Kipimo kwa Wakati Huu—Ninawaandikia barua hii kuwaambia mambo machache ndugu zangu wahudumu. Mnapokuwa na kusanyiko mbele yenu kwa muda wa majuma mawili tu, msiahirishe kuwasilisha suala la Sabato, ambalo ndilo jambo halisi na la msingi, mkifikiri kwamba mnajiandalia njia kwa kuanza na mambo mengine. Hivyo ndivyo kosa lilivyofanyika huko Ballarat na Maitland. Sabato iliguswa, lakini haikuwekwa kuwa jambo kuu, yaani kipimo cha wakati huu. {VSS 330.2}

Inueni kiwango cha Mungu, yaani amri za Mungu na imani ya Yesu. Fanyeni jambo hili kuwa kiini cha kila kitu, kisha kwa hoja zenu zenye nguvu lilindeni na kulijengea msingi imara ili liwe na nguvu zaidi. —*Letter 209, 1899.* {VSS 330.3}

Sababu ya Kuchujwa kwa Watu wa Mungu—Niliuliza maana ya kuchujwa nilikokuwa nimeona, nami nikaonyesha kwamba kungetokana na Shuhuda ya wazi inayotokana na shauri la Shahidi wa Kweli kwa Walaodikia. Shuhuda hii itakuwa na athari moyoni mwa mpokeaji na utamwongoza kuinua kiwango na kutoa kweli iliyo wazi. Hata hivyo, baadhi ya watu hawatastahimili Shuhuda hiyo ya wazi; watauinukia na kuupinga, na jambo hilo ndilo litakalosababisha kuchujwa miongoni mwa watu wa Mungu. —*Maandiko ya Awali*, uk. 270. {VSS 330.4}

Ufunuo wa Yohana—Yohana alifunuliwa matukio yenye kuvutia sana na yenye umuhimu mkubwa katika uzoefu wa kanisa. Aliona hali, hatari, mapambano, na ukombozi wa mwisho wa watu wa Mungu. Aliandika ujumbe wa mwisho ambao unapaswa kukamilisha mavuno ya dunia, ama kama miganda ya kuwekwa katika ghala la mbinguni, au kama kuni kwa moto wa uharibifu. Mambo yenye umuhimu mkubwa yalifunuliwa kwake, hasa kwa ajili ya kanisa la mwisho, ili wale watakaogeuka kutoka katika kosa na kuingia katika Kweli wafundishwe kuhusu hatari na mapambano yaliyo mbele yao. Hakuna mtu anayepaswa kubaki gizani kuhusu mambo yatakayokuja juu ya dunia. —*Pambano Kuu*, uk. 341–342. {VSS 330.5}

Ushuhuda wa Kristo—Bwana alimfunulia Yohana mambo ambayo aliona yangekuwa muhimu kwa watu Wake katika siku za mwisho, na mafundisho aliyoyatoa yanapatikana katika kitabu cha Ufunuo. Wale watakaokuwa watenda kazi pamoja na Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo wataonyesha shauku kubwa katika kweli zinazopatikana katika kitabu hiki. Kwa kalamu na kwa sauti watajitahidi kueleza wazi mambo ya ajabu ambayo Kristo alikuja kutoka mbinguni kuyafunua. {VSS 331.1}

Ujumbe mzito uliotolewa kwa mpangilio wake katika kitabu cha Ufunuo unapaswa kuchukua nafasi ya kwanza katika mawazo ya watu wa Mungu, na hakuna jambo jingine linalopaswa kuruhusiwa kuteka fikira zao. {VSS 331.2}

Muda wa thamani unapita kwa haraka, na kuna hatari kwamba wengi watanyang'anywa muda ambao ulipaswa kutumika kutangaza ujumbe ambao Mungu ameutuma kwa ulimwengu ulioanguka. Shetani hufurahi kuona akili za watu zikigeuzwa kutoka katika kujifunza kweli zinazohusiana na mambo ya milele. {VSS 331.3}

Ushuhuda wa Kristo, ambao ni ushuhuda wenye uzito mkubwa sana, unapaswa kutolewa kwa ulimwengu. Katika kitabu chote cha Ufunuo kuna ahadi za thamani zinazoinua moyo, lakini pia kuna maonyo yenye uzito mkubwa sana. Je, wale wanaodai kuwa wanajua Kweli hawatasoma ushuhuda ambao Kristo alimpa Yohana? Hapa hakuna makisio wala udanganyifu wa kisayansi; hapa kuna Kweli zinazohusu ustawi wetu wa sasa na wa milele. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 8, uk. 301–302. {VSSw 332.1}

Danieli na Ufunuo—Wale wanaokubali nafasi za ualimu wanapaswa kuthamini zaidi na zaidi mapenzi yaliyofunuliwa ya Mungu ambayo yamewasilishwa kwa uwazi na kwa nguvu katika vitabu vya Danieli na Ufunuo. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 6, uk. 131. {VSSsw 332.2}

Kusudi la Kitabu cha Ufunuo—Katika kitabu cha Ufunuo tunasoma kuhusu kazi maalumu ambayo Mungu anataka watu Wake waifanye katika siku hizi za mwisho. Amefunua sheria Yake na kutuonyesha Kweli ya wakati huu. Kweli hii inaendelea kufunuliwa hatua kwa hatua, na Mungu anakusudia tupate ufahamu juu yake ili tuweze kutofautisha kati ya mema na mabaya, kati ya haki na udhalimu. {VSSsw 332.3}

Ujumbe wa malaika wa tatu, ambao ni kweli kuu inayopima watu katika wakati huu, unapaswa kufundishwa katika taasisi zetu zote. Mungu anakusudia kwamba kupitia taasisi hizo onyo hili maalumu litolewe na miale angavu ya nuru iangaze kwa ulimwengu. Muda ni mfupi. Hatari za siku za mwisho ziko mbele yetu, kwa hiyo tunapaswa kukesha na kuomba, kujifunza na kuyazingatia mafundisho tunayopata katika vitabu vya Danieli na Ufunuo. {VSSsw 332.4}

Wakati Yohana alipotengwa na wale aliowapenda na kupelekwa katika kisiwa cha upweke cha Patmo, Kristo alijua mahali alipokuwa mtumishi Wake mwaminifu. Yohana alisema: *“Mimi Yohana, ndugu yenu na mwenye kushiriki pamoja nanyi katika mateso na ufalme na subira ya Yesu Kristo, nalikuwa katika kisiwa kiitwacho Patmo, kwa ajili ya Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu. Nalikuwa katika Roho, siku ya Bwana; nikasikia sauti kuu nyuma yangu, kama sauti ya baragumu.”* Ufunuo 1:9-10 {VSSsw 333.1}

Siku ya Bwana ni siku ya saba, yaani Sabato ya uumbaji. Katika siku ambayo Mungu aliitakasa na kuibariki, Kristo alimjulisha mtumishi Wake Yohana, kwa njia ya malaika Wake, mambo ambayo yangetokea kabla ya kufungwa kwa historia ya dunia, na anakusudia tupate ufahamu kuhusu mambo hayo. Si kwa bahati kwamba alisema: *“Heri yeye asomaye, na wao wayasikiao Maneno ya unabii huu, na kuyashika yaliyoandikwa humo; kwa maana wakati u karibu.”* (Ufunuo 1:9, 10; 1–3) Haya ndiyo mafundisho yanayopaswa kutolewa kwa uvumilivu. Masomo yetu yapaswe kuendana na siku tunazoishi, na mafundisho yetu ya dini yatolewe kulingana na ujumbe ambao Mungu anautuma. {VSSsw 333.2}

Tutalazimika kusimama mbele ya watawala na kujibu kuhusu uaminifu wetu kwa sheria ya Mungu, na kueleza sababu za imani yetu. Vijana wanapaswa kuelewa mambo haya. Wanapaswa kujua mambo yatakayotokea kabla ya kufungwa kwa historia ya dunia. Mambo haya yanahusu ustawi wetu wa milele; kwa hiyo walimu na wanafunzi wanapaswa kuyapa umakini zaidi. Kwa kalamu na kwa sauti, maarifa yanapaswa kutolewa ambayo yatakuwa chakula kwa wakati unaofaa, si kwa vijana tu, bali pia kwa watu wazima. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 6, uk. 127–129. {VSS 333.3}

Matukio Mazito ya Unabii—Hatari za siku za mwisho ziko juu yetu, na katika kazi yetu tunapaswa kuwaonya watu kuhusu hatari walizo nazo. Matukio mazito ambayo unabii umefunua yasipuuzwe. Ikiwa watu wetu wangukuwa wameamka hata kwa kiasi kidogo na kutambua ukaribu wa matukio yaliyoelezwa katika Ufunuo, kungetokea matengenezo katika makanisa yetu, na wengi zaidi wangeamini ujumbe huu. Hatuna muda wa kupoteza; Mungu anaitua tuwachungie watu kama wale watakaotoa hesabu. {VSS 334.1}

Tuendeleze kanuni mpya na kusesitiza Kweli iliyo wazi, kwa maana itakuwa kama upanga ukatao kuwili. {VSS 334.2}

Lakini tusiwe wepesi kuingia katika hali ya mabishano. Kutakuwa na nyakati ambapo tunapaswa kusimama na kuona wokovu wa Mungu. Acha Danieli aseme, acha Ufunuo useme, na uonyeshe lililo Kweli. Lakini kila upande wa mada unapowasilishwa, mwinulieni Yesu kuwa kitovu cha tumaini lote, “Mzizi na Mzao wa Daudi, na Nyota yenye kung’aa ya asubuhi.” —*Shuhuda kwa Wachungaji na Watendakazi wa Injili*, uk. 118. {VSS 334.3}

Hatari za Siku za Mwisho—Je, ndugu zetu watakumbuka kwamba tunaishi katikati ya hatari za siku za mwisho? Someni kitabu cha Ufunuo pamoja na kitabu cha Danieli, na fundisheni mambo haya. —*Shuhuda kwa Wachungaji na Watendakazi wa Injili*, uk. 115. {VSS 334.4}

SURA YA 58— KUJA KWA KRISTO HIVI KARIBUNI

Kuhubiri Injili—Mungu hatarajii watenda kazi Wake wajishughulishe na mambo madogo yasiyo na umuhimu; badala yake, wanapaswa kuhubiri Injili, na watagundua kwamba mahubiri mafupi huwa na matokeo makubwa zaidi. Katika kila mahali ambapo kazi inaanizishwa, bendera inapaswa kuinuliwa juu zaidi na zaidi. Ukweli kuhusu kuja kwa Kristo hivi karibuni unapaswa kutangazwa. Na watenda kazi wote, iwe wanahubiri madhabahuni au wanatoa mafundisho ya Biblia, wanapaswa kufundishwa kuzungumza kwa njia iliyo wazi, inayoeleweka, na yenye mvuto. —*Letter 200, 1903.* **{VSS 335.1}**

Maonyo ya Dhati—Nguvu hai ya Mungu lazima iambatane na ujumbe kuhusu kuja kwa Kristo mara ya pili, na hatupaswi kupumzika mpaka tuone nafsi nyingi zikiongoa na kuongozwa katika tumaini lenye baraka la kurudi kwa Bwana. Katika siku za mitume, ujumbe waliouhubiri ulifanya kazi halisi kwa kuwageuza watu kutoka katika ibada ya sanamu na kuwaongoza kumtumikia Mungu aliye hai; vivyo hivyo, kazi inayopaswa kufanywa leo ni ya Kweli na ujumbe huo bado una ukweli uleule, isipokuwa kwamba tunapaswa kuutoa kwa bidii zaidi kwa sababu kuja kwa Bwana kumekaribia zaidi. Ujumbe wa wakati huu ni wa hakika, rahisi kueleweka, na wenye umuhimu mkubwa sana; kwa hiyo, tunapaswa kutenda kama wanaume na wanawake wanaouamini ujumbe huo. Kusubiri, kukesha, kufanya kazi, kuomba, na kuuonya ulimwengu—hiyo ndiyo kazi yetu. —*The Review and Herald*, Novemba 13, 1913. **{VSS 335.2}**

Kweli ya Kikristo Inayotumika Katika Maisha—Kweli za unabii zimefungamana pamoja, na tunapozichunguza huunda mkusanyiko wenye upatanifu wa kweli za Kikristo zinazotumika katika maisha ya kila siku; kwa hiyo, mahubiri yote tunayoyatoa yanapaswa kuonyesha wazi kwamba tunangojea, tunafanya kazi, na tunaomba kwa ajili ya kuja kwa Mwana wa Mungu. Kuja Kwake ndilo tumaini letu, na tumaini hili linapaswa kuhusishwa na maneno yetu

yote, matendo yetu yote, mahusiano yetu yote, na ushirika wetu wote na wengine.

—*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 220. {VSS 336.1}

Kuja Mara ya Pili, Mada ya Kudumu—Kuja mara ya pili kwa Mwana wa Adamu kunapaswa kuwa mada ya ajabu inayowekwa mbele ya watu daima, na jambo hili halipaswi kamwe kuachwa katika mahubiri yetu. Mambo ya milele yanapaswa kuwekwa mbele ya ufahamu wa watu, na mvuto wa dunia utaonekana jinsi ulivyo hasa—yaani, usio na maana na wa kupita kama ubatili. Kwa hiyo, tutafanya nini na ubatili wa dunia, sifa zake, utajiri wake, heshima zake, au starehe zake? —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 220. {VSS 336.2}

SURA YA 59—NJIA YA WOKOVU

Mzigo wa Kila Mahubiri—Sayansi ya wokovu inapaswa kuwa mzigo wa kila mahubiri, mada ya kila wimbo, na jambo linalomiminwa katika kila ombi, huku hakuna jambo lolote linalopaswa kuingizwa katika mahubiri ya Neno litakalochukua nafasi ya Kristo, ambaye Ndiye Neno na nguvu ya Mungu. Jina Lake, ambalo ndilo Jina pekee lililopewa chini ya mbingu ambalo kwa hilo tunaweza kuokolewa, linapaswa kuinuliwa katika kila mahubiri, na kutoka Sabato hadi Sabato tarumbeta ya walinzi inapaswa kutoa sauti iliyo wazi na isiyo na mashaka. Kristo ndiye kiini cha maarifa na ufasaha wa Injili, na wahudumu Wake wanapaswa kulihubiri Neno la uzima kwa kuwasilisha tumaini kwa wenye kutubu, amani kwa walio na huzuni na waliokata tamaa, pamoja na neema, ukamilifu, na nguvu kwa waaminio. — *Manuscript 107, 1898.* {VSS 337.1}

Mwana-Kondoo wa Mungu—Kamwe mahubiri yoyote hayapaswi kutolewa, wala mafundisho yoyote ya Biblia katika eneo lolote hayapaswi kutolewa, bila

kuwaelekeza wasikilizaji kwa **“Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu.”** —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 6, uk. 54. {VSS 337.2}

Wokovu Katika Urahisi Wake—Katika kila kusanyiko kuna nafsi zisizoridhika ambazo kila Sabato hutamani kusikia jambo la wazi linaloeleza jinsi wanavyoweza kuokolewa na jinsi wanavyoweza kuwa Wakristo; kwa hiyo jambo la muhimu zaidi ambalo wanahitaji kulijua ni hili: Mwenye dhambi anawezaje kusimama mbele za Mungu? Hivyo, njia ya wokovu inapaswa kuwekwa mbele yao kwa urahisi na uwazi, kama vile ambavyo ungemweleza mtoto mdogo, huku Yesu akiinuliwa kuwa tumaini pekee la mwenye dhambi. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*

, uk. 350. {VSS 337.3}

Kuitumia Kweli Moyoni—Ni jambo la hakika kwamba mada mpya na zenye kushangaza hazipaswi kuwasilishwa kwa watu kwa urefu usio wa lazima; bali katika kila hotuba inayotolewa, kuwe na matumizi ya Kweli yanayogusa moyo, ili kila atakayesikia aweze kuelewa na wanaume, wanawake, pamoja na vijana waweze kufanywa kuwa hai kwa Mungu. —*Shuhuda kwa Wachungaji na Watendakazi wa Injili*, uk. 258. {VSS 338.1}

Umuhimu wa Mabadiliko ya Moyo—Wakati mwingine wanaume na wanawake huamua kuikubali kweli kwa sababu ya uzito wa ushahidi uliowasilishwa, lakini bado hawajabadilishwa; kwa hiyo kazi ya mhudumu haijakamilika mpaka awasisitize wasikilizaji wake umuhimu wa kuwa na mabadiliko ya moyo. Katika kila mahubiri, maombi ya dhati yanapaswa kutolewa kwa watu ili waache dhambi zao na wamgeukie Kristo. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 159. {VSS 338.2}

Kimbilio Katika Kristo—Mhudumu aliyejifunza kutoka kwa Kristo daima atatambua kwamba yeye ni mjumbe wa Mungu, aliyeagizwa na Mungu kufanya kazi yenye matokeo kwa wakati huu na kwa umilele; kwa hiyo lengo lake halipaswi kuwa kujivutia mwenyewe, elimu yake, au uwezo wake, bali kusudi lake lote linapaswa kuwa kuwaongoza wenye dhambi katika toba na kuwaelekeza, kwa

mafundisho na mfano wake, kwa Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Ubinafsi wake unapaswa kufichwa ndani ya Kristo, na watu wa namna hiyo watazungumza wakiwa na ufahamu kwamba wana nguvu na mamlaka kutoka kwa Mungu, wakiwa vyombo vya sauti Yake. Mahubiri yao yatakuwa na bidii na msisitizo wa ushawishi utakaowaongoza wenye dhambi kuona hali yao ya kupotea na kukimbilia katika Kristo kama kimbilio lao. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti*, uk. 134. {VSS 338.3}

Hatua za Uongofu—Wahudumu wanapaswa kuiwasilisha Kweli kwa njia iliyo wazi na rahisi, kwa sababu miongoni mwa wasikilizaji wao kuna wengi wanaohitaji maelezo rahisi kuhusu hatua zinazohitajika katika uongofu, kwani umati mkubwa wa watu una uelewa mdogo zaidi kuhusu jambo hili kuliko inavyodhaniwa. Hata miongoni mwa wahitimu wa vyuo, wasemaji wenye ufasaha, viongozi wenye uwezo, na watu walio katika nafasi za juu za uwajibikaji, wapo wengi ambao wameelekeza uwezo wao katika mambo mengine na kupuuza mambo yenye umuhimu mkubwa zaidi. Watu wa namna hiyo wanapokuwa sehemu ya kusanyiko, mara nyingi mhubiri hujitahidi kutumia uwezo wake wote kutoa mahubiri yenye kiwango cha kielimu, lakini hushindwa kumfunua Kristo; haonyeshi kwamba dhambi ni kuivunja sheria ya Mungu, wala haelezi wazi mpango wa wokovu. Jambo ambalo lingegusa mioyo ya wasikilizaji wake lingekuwa ni kuwaelekeza kwa Kristo anayekufa ili kuleta ukombozi karibu nao. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 170. {VSS 339.1}

Ondoleo la Dhambi Kupitia kwa Kristo—Maombi ya moja kwa moja yanapaswa kutolewa, na daima mhubiri anapaswa kukumbuka kwamba yeye ni chombo tu; kwa sababu ni Roho Mtakatifu anayegusa mioyo ya watu wa hali zote—walio juu na walio chini, wenye heshima kubwa na wale waliotelekezwa kabisa. Neno linapaswa kuhubiriwa kwa urahisi na uwazi, huku wanadamu wakielezwa kwamba wao ni wenye dhambi walio katika hatari ya kupoteza nafsi zao. Tofauti zote za hadhi zinapaswa kupuuzwa, kwa maana wote wanahitaji Kweli ileile; wote wanamhitaji Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka, aliyekufa ili wapate kuokolewa. {VSS 339.2}

Lihubiri Neno la Mungu kama njia ambayo kwayo imani takatifu na tabia safi vinaweza kupatikana. Toeni wokovu kamili na wa bure, si kana kwamba unatoka

kwenu wenyewe, bali unatoka kwa Kristo. Waonyesheni wasikilizaji wenu hitaji la kurudi katika uaminifu wao kwa Mungu kwa njia ya toba na imani, kwa maana wote wako katika kiwango kimoja; wote wamehukumiwa sawasawa na kipimo hicho kikuu cha haki ya maadili. Tangazeni ondoleo la dhambi kupitia kwa Kristo, ambaye Ndiye Mchukuaji pekee wa dhambi na Msameheaji pekee wa dhambi; tangazeni msamaha wa dhambi kwa njia ya toba mbele za Mungu na imani katika Kristo, Naye Mungu atathibitisha ushuhuda wenu. Kwa uhakika wote mnaweza kutangaza njia ambayo kwayo tabia takatifu inaweza kupatikana, kama Henoko alivyoipata, yaani, kupitia kwa Yesu Kristo. **{VSS 340.1}**

Kila mjumbe wa Mungu anaweza kutangaza msamaha na ondoleo la dhambi kwa jina la Kristo, ambaye alikufa ili kumkomboa mwenye dhambi. Kibali kamili cha Bwana huja kwa wale wanaomtafuta kwa moyo wote na walio tayari kumfuata katika kufanya mapenzi ya Mungu, wakimtawaza Kristo moyoni na kupandikiza sifa Zake ndani ya maisha yao ya kila siku. Watu hao wana msukumo unaowatawala, yaani, upendo mkuu kwa Kristo Mwokozi wetu, ambao huleta hata mawazo yao yote chini ya utii Wake. —*Manuscript 138, 1897.* **{VSS 340.2}**

Kweli Zinazousadikisha na Kuongoa—Katika kila kusanyiko kuna nafsi ambazo Roho wa Bwana anazifanyia kazi, nazo zinahitaji msaada ili ziweze kuelewa kile wanachopaswa kufanya ili ziokolewe. Mara nyingi umewasilisha mbele yao picha kuu za kiroho ambazo hawakuweza kuzielewa; kwa sababu wale wenye uwezo mkubwa wa kufikirika wanaweza kufahamu mawazo hayo ya juu, lakini kwa wengi mahubiri ya namna hiyo huwa kama lugha ya kigeni isiyoeleweka. Kwa hiyo, zingatia zaidi Kweli zinazousadikisha na kuongoa nafsi, kwa maana Mungu anafanya kazi katika hema la mikutano, awepo wachache au wengi. **{VSS 340.3}**

Kutoka katika midomo ya Kweli na ya unyenyekevu unapaswa kutoa ombi kwamba Mungu akuongoze kuwapa kila mtu sehemu yake ya chakula kwa wakati unaofaa, na akupe msaada ili usizidi mipaka ya urahisi wa Injili kwa kukazia mada unazozipenda ambazo hazitaangazia dhamiri zilizotiwa giza, wala kuwasadikisha watu kuhusu dhambi, haki, na hukumu ijayo. Kwa njia iliyo wazi na maalumu, waeleze wasikilizaji wako kile wanachopaswa kufanya ili waokolewe; waongoze katika njia za kweli na utakatifu. Kama mchungaji anavyoliongoza kundi lake malishoni, waongoze mahali watakapokunywa maji ya wokovu. —*Letter 29, 1895.* **{VSS 341.1}**

Kujitoa Wakfu Bila Masharti—Wakati fulani uliopita niliandika katika shajara yangu maneno haya: “Ilionekana kana kwamba tulikuwa tumekusanyika katika mkutano. Mmoja mwenye mamlaka alikuwepo, naye alisema: ‘Waambie wahudumu na wainjilisti: Endeleeni na kazi kwa hali ya kweli ya kiroho. Tumia matumizi ya moja kwa moja yanayofanywa katika Neno la Mungu, ili matokeo yasiwe tu msisimko wa hisia za huruma ambao utatoweka mara tu msukumo huo utakapoondoka.’” Nimeagizwa kusema kwamba wote wanaotambua hitaji lao wanaweza kusaidiwa. Kwa hiyo, kila hatua inayochukuliwa iwe hatua ya kusonga mbele kuelekea uongofu wa Kweli na kujitoa wakfu bila masharti kwa moyo, akili, nafsi, na nguvu zote katika huduma ya Bwana. Kila jambo linalofanyika lielekee katika matengenezo ya Kweli ya mawazo, maneno, matendo, na ujenzi wa tabia. Kweli itambuliwe kuwa tofauti na uongo. Usimruhusu adui akuongoze kuchanganya mifano isiyo sahihi katika muundo wa kazi yako. Dumisheni upendo wa Kristo ukiwa mbele ya watoto na vijana, na warudieni mara nyingi mafundisho Yake rahisi. —*Letter 111, 1904.* {VSS 341.2}

Utii kwa Wazazi na kwa Mungu—Wafundisheni vijana kwamba dhambi katika kila jambo imeelezwa katika Maandiko kuwa ni “**kuivunja sheria**” (1 Yohana 3:4), na wafundisheni kwa lugha rahisi kwamba wanapaswa kuwatii wazazi wao na kumtolea Mungu mioyo yao. —*Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi*, uk. 169. {VSS 342.1}

Malaria ya Kiroho—Mielekeo isiyotii, inayodhalilisha, na tamaa mbaya haviwezi kutawala katika moyo unaoongozwa na Roho wa Kristo, lakini wapo wengi ambao hawajawahi kujitoa kikamilifu bila masharti kwa Yesu Kristo, wakisalimisha mapenzi yao na njia zao Kwake. {VSSw 342.2}

Katika huduma ya Neno kunapaswa kuwepo mafundisho mengi zaidi kuhusu uongofu wa kweli kuliko hoja za mafundisho ya kidini, kwa maana ni rahisi zaidi na ni jambo la kawaida kwa moyo ambao hauko chini ya utawala wa Roho wa Kristo kuchagua mada za mafundisho kuliko mambo ya utendaji wa maisha. Kuna mahubiri mengi yanayotolewa bila Kristo, ambayo hayakubaliki kwa Mungu zaidi ya sadaka ya Kaini, kwa sababu hayapatani na Mungu. {VSSw 342.3}

Bwana anakuita, ndugu yangu, uache kazi hii, uondoke katika kuta za Sayuni, au uwe mtu aliyebadilishwa. Wakati moyo wako mwenyewe utakapokuwa umetakaswa kwa njia ya Kweli, hautakuwa na uchafu wa kimaadili ndani yake. Hapo itahitaji upinzani mkubwa sana kutoka kwako dhidi ya mawazo yasiyo matakatifu, kwa sababu nafsi yako imechafuliwa na malaria ya kiroho. Umevuta hewa ya kishetani, na hujawa mtu anayekubalika mbele za Mungu. Wakati akili yako ilipaswa kukua, mawazo yako kuinuliwa, na mipango pamoja na kazi zako kupanuliwa, umekuwa ukipungua zaidi na zaidi katika ufanisi kama mtenda kazi, kwa sababu Mungu hayabariki juhudi zako. —*Letter 5, 1886.* {VSSsw 343.1}

SURA YA 60—UCHAJI WA MUNGU UNAOTUMIKA KATIKA MAISHA

Njia ya Kufikia Moyo—Wahudumu wangeveza kugusa mioyo ya watu wengi zaidi ikiwa wangezingatia zaidi uchaji wa Mungu unaoonekana katika maisha ya kila siku. Mara nyingi, juhudi zinapofanywa kuwasilisha Kweli katika maeneo mapya, mahubiri yanayotolewa huwa yamejikita zaidi katika nadharia kuliko katika matumizi halisi ya maisha. {VSSsw 344.1}

Katika kila mahubiri, maombi ya dhati yanapaswa kutolewa kwa watu ili waache dhambi zao na kumgeukia Kristo. Dhambi zinazotawala jamii na anasa zinazopendwa katika siku zetu zinapaswa kukemewa, na uchaji wa Mungu unaoonekana katika mwenendo wa maisha unapaswa kusesitizwa. Mhudumu wa Kweli, akiwa ametambua moyoni umuhimu wa maneno anayoyasema, hawezi kujizuia kuonyesha kujali kwake kwa ajili ya wokovu wa nafsi za wale anaowahudumia. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 158–159. {VSSsw 344.2}

Mahali pa Uchaji wa Mungu Katika Kila Mahubiri—Hoja zenye kushawishi zaidi zinaweza kutolewa, lakini bado wenye dhambi wakaonekana kuwa mbali na

wokovu kama walivyokuwa hapo awali. Wahudumu hawapaswi kutoa mahubiri moja baada ya jingine yanayohusu mafundisho pekee; bali uchaji wa Mungu unaotumika katika maisha unapaswa kuwa sehemu ya kila mahubiri. —*Evangelism*, uk. 178. {VSS 344.3}

Usafi, Utakatifu, na Manufaa Katika Huduma—Usafi, utakatifu, na manufaa katika maisha na huduma vinapaswa kuwa mzigo wa kila mahubiri na mada ya kila ombi. —*Letter 27, 1888*. {VSS 344.4}

Hazina ya Mada za Kivitendo—Unapaswa kuwa mwangalifu na kujifunza ili uwe na hazina ya mada za kivitendo ambazo umefanya utafiti wake kwa kina na ambazo unaweza kuziwasilisha kwa watu kwa njia rahisi, yenye nguvu, na inayofaa kulingana na wakati na mahali wanapozihitaji. Hujajiandaa kikamilifu kutoka katika Neno lililoongozwa na Mungu kwa ajili ya kila tendo jema. Mara nyingi, kundi lilipohitaji chakula cha kiroho, uliwasilisha mada zenye hoja nyingi ambazo hazikufaa kwa wakati huo zaidi ya vile hotuba kuhusu mambo ya kitaifa ingefaa. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 3, uk. 228. {VSS 345.1}

Ufunuo Mpya wa Uchaji wa Mungu wa Kivitendo—Washiriki wa makanisa mbalimbali wana uelewa mdogo kuhusu Biblia, na mafundisho rahisi kuhusu uchaji wa Mungu unaotumika katika maisha huja kwao kama ufunuo mpya. Wanahitaji kufahamu Kweli ni nini. Msichague mada za kufikirika ambazo zinalenga tu kupendeza mawazo au kutosheleza udadisi wa watu. Wavunje watu mkate wa uzima. —*Letter 29, 1895*. {VSS 345.2}

Mtindo wa Maisha wa Kristo—Ingawa ujumbe huu haupatani na mielekeo ya asili ya mwanadamu, mhudumu lazima atangaze Kweli iliyo wazi ambayo itawafanya wasikilizaji wake washtuke; kwa maana anapaswa kuwaonyesha wale wanaopenda starehe kuliko kumpenda Mungu hatari na maangamizi yaliyo mbele yao, pamoja na hukumu inayowangojea wasiotubu. Kwa kuwa ujumbe huu haupendwi na wale wanaohitaji kuonywa wala haukubaliki kwa tamaa zao, wahudumu wanaagizwa kwa uzito kuwa waaminifu katika kuutangaza. Mhudumu atakutana na makosa ambayo yataonekana kana kwamba hayawezi kurekebisha. Atagundua dhambi zilizofichwa ambazo zinahitaji kufunuliwa wazi. Nabii asema: *“Piga kelele, usiache, Paza sauti yako kama tarumbeta; Uwahubiri watu Wangu kosa lao, Na nyumba ya Yakobo dhambi zao. Walakini wanitafuta kila siku; hupenda kujua*

njia Zangu; kama vile taifa waliotenda haki, wasioacha sheria ya Mungu wao.”
(Isaya 58:1, 2) {VSS 345.3}

Na tena: ***“Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa Kwake na kwa ufalme Wake; lihubiri neno, uwe tayari, wakati ukufaa na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho.”*** (2 Timotheo 4:1, 2) {VSSw 346.1}

Mhudumu hapaswi kujishughulisha na kusimulia hadithi za kuburudisha na kuchekeka [anecdotes], bali anapaswa kulihubiri Neno. ***“Wale wadumuo kutenda dhambi uwakemee mbele ya wote, ili na wengine waogope. Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, na mbele za malaika wateule, uyatende hayo pasipo kuhukumu kwa haraka; usifanye neno lo lote kwa upendeleo.”*** (1 Timotheo 5:20, 21) ***“bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi.”*** (1 Timotheo 4:12) ***“Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.”*** (2 Timotheo 2:15) {VSSw 346.2}

Tunapaswa kumtangaza Kristo kwa watu, tukifuata maneno ya mtume:

“Ambaye sisi tunamhubiri habari zake tukimwonya kila mtu, na kumfundisha kila mtu katika hekima yote, tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo. Nami najitaabisha kwa Neno lilo hilo, nikijitahidi kwa kadiri ya kutenda kazi kwake atendaye kazi ndani yangu kwa nguvu.” (Wakolosai 1:28, 29) Je, ilikuwa muhimu kwa Paulo kuwa na uzoefu huo? Soma kwa makini maneno yake, na uone kama ni salama kwa mhudumu yeyote wa Kristo kuishi chini ya kiwango chochote cha uchaji wa Mungu kuliko hicho. —*Letter 3, 1892.* {VSSw 346.3}

Mahubiri Rahisi, Yenye Maana, na Yenye Busara—Hakuna mtenda kazi anayepaswa kudhani kwamba wajibu wake ni kukemea tu, kuonyesha maovu yaliyopo, na kuishia hapo. Kazi hiyo haileti manufaa yoyote, bali huwakatisha tamaa na kuwavunja moyo watu. Mahubiri rahisi, yenye maana, na yenye hekima yanapaswa kutolewa kwa makanisa, yakionyesha umuhimu wa kumtafuta Bwana katika maombi na kufungua mioyo kwa Nuru ya uzima. Mahubiri hayo yanapaswa kuwaongoza washiriki wa kanisa kushiriki katika kazi ya unyenyekevu kwa ajili ya Mungu. Mungu amempa kila mtu kazi; na kila mtenda kazi anayeshiriki katika

huduma Yake amepewa sehemu ya kutekeleza katika kuwasilisha nuru na Kweli. —
Manuscript 95, 1907. {VSS 347.1}

Kufanywa Upya kwa Neema—Nimeazimia kuwaweka watu mbele ya Ukweli kwamba tunapaswa kuwa na umoja. Lazima tuache kabisa tabia ya kukosoana. Tunapaswa kuisisitiza kwamba sifa kuu inayowatofautisha Wakristo na watu wengine wote ni umoja uliopo kati yao na Bwana Yesu Kristo, unaodumishwa kwa imani inayotenda kazi kwa upendo na kuitakasa nafsi. Umoja huu na Kristo, yaani kuwa mmoja Naye, huleta umoja na upendo kati yetu sisi kwa sisi. Wakristo hufurahia kumheshimu Mungu kwa kutii amri Zake zote. Wakiwa wamefungwa pamoja na Kristo katika upendo, wanakuwa na upendo kwa wengine. {VSSw 347.2}

Tunapaswa kuzungumzia jambo hili zaidi kuliko tulivyofanya hapo awali. Mada ya neema Yake ifanyayo upya inaposisitizwa katika mahubiri itampendeza Bwana, na Roho Wake Mtakatifu ataingia katika mioyo ya wale wanaosikiliza. —
Letter 42, 1906. {VSS 348.1}

SURA YA 61—WANAUME NA WANAWAKE WA BIBLIA

Henoko

Mazungumzo Kuhusu Mambo ya Mbinguni—Kisa cha Henoko kiko mbele yetu. Kwa mamia ya miaka alitembea pamoja na Mungu. Aliishi katika kizazi kilichokuwa kimejaa uharibifu wa kimaadili, ambapo upotovu wa maadili ulikuwa umeenea kila mahali; hata hivyo, aliufundisha moyo wake kujitoa kwa Mungu na kupenda usafi. Mazungumzo yake yalihusu mambo ya mbinguni. Aliifundisha akili yake kuelekezwa katika njia hiyo, naye akawa na alama ya tabia ya Mungu ndani yake. Uso wake uliangazwa kwa nuru ile ing’ayo katika uso wa Yesu. —*Shuhuda kwa Kanisa*, juz. 2, uk. 122. {VSSw 351.1}

Mhubiri wa Haki—Matukio ya wakati ujao yalipofunuliwa mbele yake, Henoko akawa mhubiri wa haki, akiwasilisha ujumbe wa Mungu kwa wote waliokuwa tayari kusikia maneno ya onyo. Katika nchi ambako Kaini alikuwa ametafuta kujificha

kutoka katika uwepo wa Mungu, nabii wa Mungu alitangaza matukio ya ajabu aliyokuwa ameonyeshwa katika maono yake. Alisema: “*Tazama, Bwana Anakuja pamoja na watakatifu Wake elfu kumi, ili afanye hukumu juu ya wote, na kuwathibitisha wote wasiomcha Mungu kwa ajili ya matendo yao yote ya uovu waliyoyatenda.*” **{VSS 351.2}**

Nguvu ya Mungu iliyofanya kazi pamoja na mtumishi Wake iligusa mioyo ya wale waliosikia ujumbe huo. Baadhi yao walitii onyo hilo na kuacha dhambi zao; lakini umati mkubwa uliidharau na kuicheka ile habari ya kutisha. Watumishi wa Mungu wanapaswa kupeleka ujumbe kama huo kwa ulimwengu katika siku za mwisho, nao pia utapokelewa na wengi kwa kutokuamini na dhihaka. **{VSS 352.1}**

Kadiri miaka ilivyopita, wimbi la hatia ya mwanadamu lilizidi kuwa kubwa, na mawingu ya hukumu ya Mungu yakawa mazito zaidi na zaidi. Lakini Henoko, shahidi wa imani, aliendelea na njia yake, akiendelea kuonya, kusihi, na kufundisha, akijitahidi kugeuza wimbi la hatia na kuzuia utekelezaji wa hukumu. —*Watendakazi wa Injili*, uk. 52–53. **{VSS 352.2}**

Mkemeaji wa Dhambi—Henoko alikuwa mtu aliyekemea dhambi bila hofu. Alipowahubiria watu wa wakati wake kuhusu upendo wa Mungu uliodhihirishwa katika Kristo na kuwasihi waache njia zao mbaya, alikemea uovu uliokuwa umetawala na kuwaonya watu wa kizazi chake kwamba hukumu ingewapata hakika wale wanaovunja sheria ya Mungu. Ilikuwa Roho wa Kristo aliyesema kupitia kwa Henoko; na Roho huyo huonekana si katika maneno ya upendo, huruma, na maombi pekee, bali pia katika Ukweli mkali na unaopenya unaotolewa na watu watakatifu. Mungu huweka katika mioyo na midomo ya wajumbe Wake kweli zinazopaswa kutamkwa—Kweli kali na zenye kukata kama upanga wenye makali kuwili. —*Wazee wa Imani na Manabii*, uk. 86. **{VSS 352.3}**

Matunda ya Ujumbe Wake—Baada ya kutangaza ujumbe wake, daima aliambatana na baadhi ya wale waliolipokea onyo hilo hadi mahali pake pa faragha. Baadhi yao walikuwa washindi, nao wakafa kabla ya gharika kufika. Lakini wengine walikuwa wameishi muda mrefu sana chini ya ushawishi unaoharibu wa dhambi kiasi kwamba hawakuweza kuvumilia haki. —*The S.D.A. Bible Commentary*, juz. 1, uk. 1088. **{VSS 352.4}**

Yokebedi

Mwalimu wa Musa—Yokebedi alikuwa mwanamke mtumwa. Maisha yake yalikuwa ya hali ya chini, na mzigo wake ulikuwa mzito. Lakini mbali na Mariamu wa Nazareti, hakuna mwanamke mwingine ambaye kupitia kwake ulimwengu umepokea baraka kubwa kama hizo. Akijua kwamba mtoto wake angeondolewa kutoka katika uangalizi wake muda si mrefu na kuwekwa chini ya ulinzi wa watu wasiomjua Mungu, alijitahidi kwa bidii zaidi kuiunganisha nafsi ya mtoto wake na mambo ya mbinguni. Alitafuta kupanda ndani ya moyo wake upendo na uaminifu kwa Mungu. Na kazi hiyo ilikamilishwa kwa uaminifu. Kanuni hizo za Kweli zilizokuwa kiini cha mafundisho ya mama yake na somo la maisha yake, hakuna ushawishi wowote wa baadaye ulioweza kumfanya Musa azikane. —*Elimu*, uk. 61. **{VSS 353.1}**

Mwalimu kwa Ajili ya Mungu—Mungu alikuwa amesikia maombi ya mama huyo; imani yake ilikuwa imepata thawabu. Kwa shukrani kubwa aliingia katika jukumu lake jipya la kumlea mtoto wake katika hali ya usalama na furaha. Alitumia kwa uaminifu nafasi aliyokuwa nayo kumlea mtoto wake kwa ajili ya Mungu. Alikuwa na uhakika kwamba mtoto huyo alikuwa ameokolewa kwa ajili ya kazi kubwa, na alijua kwamba muda si mrefu angelazimika kumkabidhi kwa binti Farao, mama yake wa kifalme wa kumlea, ambako angezungukwa na mazingira ambayo yangemwelekeza mbali na Mungu. Hali hiyo ilimfanya awe makini zaidi na mwenye bidii zaidi katika mafundisho yake kuliko alivyokuwa kwa watoto wake wengine. Alijitahidi kuujaza moyo wake kwa hofu ya Mungu, pamoja na upendo kwa Kweli na haki, na aliomba kwa bidii kwamba aweze kulindwa dhidi ya kila ushawishi unaoweza kumharibu. Alimwonyesha upumbavu na dhambi ya ibada ya sanamu, na tangu utotoni alimfundisha kuinama na kuomba kwa Mungu aliye hai, ambaye pekee angeweza kumsikia na kumsaidia katika kila hali ngumu. **{VSSw 353.2}**

Alimlea mtoto huyo kwa muda mrefu kadiri alivyoweza, lakini alilazimika kumtoa alipokuwa na umri wa karibu miaka kumi na miwili. Kutoka katika nyumba yake ya kawaida, alipelekwa katika jumba la kifalme kwa binti Farao, “akawa mwanawe.” Hata hivyo, hata huko hakupoteza athari na kumbukumbu alizopokea utotoni. Mafundisho aliyojifunza akiwa kando ya mama yake hayangeweza kusahaulika. Yalikuwa ngao dhidi ya kiburi, kutokuamini, na maovu yaliyostawi katikati ya fahari ya ikulu. **{VSSw 354.1}**

Ushawishi wa mwanamke huyo mmoja Mwebrania ulikuwa na matokeo makubwa kiasi gani, naye akiwa mhamishwa huko uhamishoni na mtumwa! Maisha yote ya baadaye ya Musa, pamoja na kazi kuu aliyotimiza kama kiongozi wa Israeli, yanathibitisha umuhimu wa kazi ya mama Mkristo. —*Wazee wa Imani na Manabii*, uk. 243–244. {VSSw 354.2}

Wanawake Waaminifu Kama Akina Mama—Kwa namna ya pekee, wajibu mkubwa umewekwa juu ya mama. Yeye Ndiye ambaye kupitia damu yake mtoto hulishwa na ambaye kupitia mwili wake mtoto hujengwa; lakini pia humjengea mtoto ushawishi wa kiakili na kiroho unaosaidia kuunda akili na tabia yake. Alikuwa Yokebedi, mama Mwebrania, ambaye akiwa imara katika imani *“hakiuogopa amri ya mfalme”* (*Waebrania 11:23*), naye ndiye aliyemzaa Musa, mkombozi wa Israeli. Alikuwa Hana, mwanamke wa maombi, kujitoa mhanga, na msukumo wa mbinguni, aliyemzaa Samweli, mtoto aliyefundishwa na Mungu, mwamuzi asiye na upendeleo wala ufasadi, na mwanzilishi wa shule takatifu za Israeli [schools of prophets]. Alikuwa Elizabeti, ndugu wa karibu na mwenye roho inayofanana na Mariamu wa Nazareti, ambaye alikuwa mama wa mjumbe wa Mwokozi. —*Huduma ya Uponyaji*, uk. 372. {VSSw 354.3}

Musa

Maneno Yenye Ufasaha—Maisha ya Musa yalitawaliwa na upendo mkuu kwa Mungu. Uchaji wake wa Mungu, unyenyekevu wake, na uvumilivu wake vilimpa ushawishi mkubwa mbele ya kutaniko la Israeli. Bidii yake na imani yake kwa Mungu vilizidi za mtu mwingine yeyote duniani. Mara nyingi alikuwa akizungumza na watu wake kwa maneno yenye ufasaha mkubwa yaliyogusa na kuchochea mioyo yao. Hakuna mtu aliyejua vizuri kuliko yeye jinsi ya kugusa mioyo ya watu. Aliongoza mambo yote yaliyohusiana na masuala ya kidini ya watu kwa hekima kubwa. —*Spiritual Gifts*, juz. 3, uk. 57. {VSS 355.1}

Mfalme Sauli

Ufasaha na Hekima—Sauli alipolikaribia kundi lile la manabii, Roho wa Bwana akamjia pia, naye akajiunga nao katika nyimbo zao za sifa na kutoa unabii pamoja nao. Alizungumza kwa ufasaha mkubwa na hekima nyingi, naye akashiriki katika huduma hiyo kwa bidii kiasi kwamba wale waliomjua walishangaa na kusema: *“Ni*

nini hilo lililompata mwana wa Kishi? Je! Sauli pia yumo miongoni mwa manabii?” 1 Samweli 10:11 —Wazee wa Imani na Manabii, uk. 610. {VSS 355.2}

Abigaili

Wema na Amani—Uchaji wa Mungu wa Abigaili, kama harufu nzuri ya ua, ulijidhihirisha bila yeye kutambua, katika uso wake, maneno yake, na matendo yake. Roho wa Mwana wa Mungu alikuwa akikaa ndani ya moyo wake. Maneno yake, yaliyotiwa neema na yaliyojaa wema na amani, yalieneza ushawishi wa mbinguni. Hisia bora zaidi ziliamshwa ndani ya Daudi, naye akatetemeka alipofikiria matokeo ambayo yangetokana na kusudi lake la pupa na lisilo la busara. *“Heri wapatanishi; maana hao wataitwa wana wa Mungu.” (Mathayo 5:9)* Laiti kungekuwa na wanawake wengi zaidi kama mwanamke huyu wa Israeli, ambao wangeweza kutuliza hisia zilizochokozwa, kuzuia misukumo ya pupa, na kukomesha maovu makubwa kwa maneno ya hekima yenye utulivu na yaliyoelekezwa kwa usahihi. —*Wazee wa Imani na Manabii, uk. 667. {VSS 356.1}*

Eliya

Sauti Wazi Kama Ya Tarumbeta—Akiitazama kwanza madhabahu ya Yehova iliyobomolewa, kisha umati wa watu, Eliya akapaza sauti yake kwa uwazi na nguvu kama ya tarumbeta, akisema: *“Mtasitasita kati ya mawazo mawili hata lini?”* —*Manabii na Wafalme, uk. 147. {VSS 356.2}*

Wana wa Israeli

Wajibu wa Wazazi—Mungu aliwaamuru Waebrania kuwafundisha watoto wao maagizo Yake na kuwajulisha yote aliyowatendea watu Wake. Nyumba na shule vilikuwa kitu kimoja. Badala ya watoto kufundishwa na watu wasiowafahamu, mioyo yenye upendo ya baba na mama ilipaswa kuwapa mafundisho. Mawazo kuhusu Mungu yalikusishwa na matukio yote ya maisha ya kila siku nyumbani. Matendo makuu ya Mungu katika kuwaokoa watu Wake yalisimuliwa kwa ufasaha na kwa kicho na heshima. Kweli kuu kuhusu majaliwa ya Mungu na maisha yajayo ziliwekwa katika akili changa. Watoto walifundishwa kuyatambua yaliyo ya Kweli, mema, na mazuri. *{VSS 356.3}*

Kwa kutumia mifano na alama, mafundisho yaliyotolewa yalifafanuliwa, na hivyo yakazama kwa nguvu zaidi katika kumbukumbu. Kupitia mifano hii yenye uhai na yenye kuvutia fikira, mtoto, karibu tangu utoto wake, aliingizwa katika siri, hekima, na matumaini ya mababu zake; naye akaongozwa katika namna ya kufikiri, kuhisi, na kutazamia mambo yaliyovuka mipaka ya vitu vinavyoonekana na vya muda mfupi, kuelekea mambo yasiyoonekana na ya milele. —*Misingi ya Elimu kwa Kila Mwanadamu*, uk. 95. {VSS 357.1}

Yohana Mbatizaji

Ufasaha Safi wa Kiasili—Sauti ya Yohana ilipazwa kama tarumbeta. Agizo lake lilikuwa: *“Uwahubiri watu Wangu kosa lao, Na nyumba ya Yakobo dhambi zao.”* (Isaya 58:1). Hakuwa amepata elimu ya kibinadamu; bali Mungu na asili vilikuwa vyanzo vya mafundisho yake. Hata hivyo, alihitajika mtu wa kutengeneza njia mbele ya Kristo, mtu aliyekuwa na ujasiri wa kutosha kuinua sauti yake kama manabii wa zamani, akiita taifa lililopotoka litubu. {VSS 357.2}

Kwa hiyo, watu walitoka pande zote kwenda nyikani kumsikiliza. Wavuvi wasio na elimu na wakulima walifika kutoka nchi zilizowazunguka na kutoka maeneo ya karibu na ya mbali. Askari wa Kirumi kutoka ngome za Herode walikuja kusikia ujumbe wake, na wakuu wa kijeshi walifika wakiwa wamejifunga panga zao kiunoni, tayari kukomesha jambo lolote lililoonekana kuwa vurugu au uasi. Wakusanyaji wa kodi wenye tamaa walikuja kutoka maeneo ya jirani, na kutoka Baraza la Sanhedrini walitoka makuhani na viongozi wa dini waliovaa tefillin (vifuko vya maandiko ya Sheria vilivyovaliwa na Wayahudi). Wote walimsikiliza kwa makini kana kwamba walikuwa wamevutwa kabisa na nguvu ya maneno yake; na wote waliondoka wakiwa wameguswa moyoni. Hata Mafarisayo, Masadukayo, na wale waliokuwa na dharau baridi na mioyo migumu katika kizazi hicho waliondoka huku dharau yao ikiwa imeondoka, na mioyo yao ikiwa imeguswa sana na utambuzi wa dhambi zao. Hakukuwa na mabishano marefu wala nadharia tata zilizofumwa kwa ustadi na kuwasilishwa kwa mpangilio wa “kwanza,” “pili,” na “tatu”; bali ufasaha safi wa kiasili ulidhihirishwa katika sentensi fupi, ambapo kila neno lilikuwa limebeba uhakika na Ukweli wa uzito wa maonyo makuu yaliyotolewa. {VSS 357.3}

Yohana Mbatizaji alikabiliana na dhambi kwa ukemezi wa wazi miongoni mwa watu wa kazi za kawaida na miongoni mwa watu wenye vyeo vya juu. Aliwatangaza wafalme na wakuu Ukweli, iwe walikuwa tayari kuusikia au kuukataa. — *Jumbe Teule, Juzuu ya 2, uk. 148, 149.* {VSS 358.1}

Nguvu ya Maneno Yake—Lengo la Yohana lilikuwa kuwashangaza na kuwaamsha watu, na kuwafanya watetemeke kwa sababu ya uovu wao mkubwa. Kwa unyenyekevu na uwazi, alionyesha makosa na uhalifu wa wanadamu. Nguvu ya pekee iliambatana na maneno yake, na ingawa watu hawakupenda kusikia hukumu dhidi ya maisha yao yasiyo matakatifu, hawakuweza kuyapinga maneno yake. Hakumsifia mtu yeyote wala hakukubali kusifiwa na mtu yeyote. Watu, kana kwamba walikubaliana kwa pamoja, walimwendea wakitubu na kukiri dhambi zao, naye akawabatiza katika Mto Yordani. {VSS 358.2}

Wafalme na watawala walifika nyikani kumsikiliza nabii huyo, nao waliguswa na kusadikishwa kwa kina alipokuwa akionyesha bila woga dhambi zao binafsi. Ufahamu wake wa tabia na uwezo wake wa kuona mambo ya kiroho ulitambua makusudi na mioyo ya wale waliokuja kwake. Bila woga aliwaambia matajiri na maskini, watu wenye heshima na watu wa hali ya chini, kwamba bila kutubu dhambi zao na kupata toba/mgeuko wa kweli wa maisha, hata kama wangedai kuwa wenye haki, wasingeweza kufurahia kibali cha Mungu wala kushiriki katika ufalme wa Masihi, ambaye ujio Wake alikuwa akiutangaza. {VSS 359.1}

Kwa roho na nguvu ya Eliya, Yohana alikemea upotovu wa Wayahudi na kuinua sauti yake dhidi ya dhambi zao zilizokuwa zimeenea. Mahubiri yake yalikuwa wazi, yenye kulenga moja kwa moja, na yenye kushawishi. — *The Review and Herald, Januari 7, 1873.* {VSS 359.2}

Sauti Yenye Nguvu na Msisitizo—Bila kutumia mabishano marefu au nadharia zilizotungwa kwa ustadi, Yohana alitangaza ujumbe wake. Sauti yake ilikuwa ya kushtua na yenye msisitizo, lakini pia ilikuwa imejaa tumaini. Kutoka nyikani ilisikika sauti yake: *“Tubuni; kwa maana ufulme wa mbinguni umekaribia.”* (*Mathayo 3:2*). Kwa nguvu mpya na isiyo ya kawaida, maneno haya yaliwagusa watu. Taifa lote lilitikiswa, na makundi makubwa ya watu yalimiminika nyikani. — *Shuhuda kwa Kanisa, Juzuu ya 8, uk. 332.* {VSS 359.3}

Mzigo wa Utume Wake—Akiwa na ufahamu uliotiwa nuru na Roho wa Mungu, Yohana alichunguza tabia za wanadamu ili aweze kuelewa jinsi ya kugusa mioyo yao kwa ujumbe wa mbinguni. Mzigo wa utume wake ulikuwa juu yake. Katika upweke, kwa kutafakari na kwa maombi, alitafuta kuiimarisha nafsi yake kwa ajili ya kazi ya maisha iliyokuwa mbele yake. — *Tumaini la Vizazi Vyote*, uk. 102. {VSS 359.4}

Sauti Kama ya Tarumbeta—Yohana alikuwa amehubiri kuhusu ujio wa Masihi. Kwa sauti kama ya tarumbeta, maneno ya mtangulizi wa Kristo yalikuwa yamevuma masikioni mwao. — *The Review and Herald*, Februari 13, 1900. {VSS 360.1}

Mmoja wa Manabii Wakuu Zaidi—Kristo alimtaja Yohana Mbatizaji kuwa mmoja wa manabii wakuu zaidi, na aliwaonyesha wasikilizaji wake kwamba walikuwa wamepewa ushahidi wa kutosha kwamba Yohana alikuwa mjumbe kutoka kwa Mungu. Maneno ya mhubiri huyo wa nyikani yalikuwa na nguvu; aliwasilisha ujumbe wake bila woga wala kuyumba, aliwakemea dhambi makuhani na watawala, na kuwaagiza wafanye matendo yanayostahili ufalme wa mbinguni. — *Mifano ya Masihi*, uk. 278. {VSS 360.2}

Mariam, Mama wa Yesu

Mwalimu wa Mtoto Yesu—Mtoto Yesu hakufundishwa katika shule za masinagogi, bali mama yake Ndiye aliyekuwa mwalimu Wake wa kwanza miongoni mwa wanadamu. Kupitia mafundisho aliyopokea kutoka kwa mama yake na kutoka katika magombo ya manabii, alijifunza Kweli za mbinguni. — *Tumaini la Vizazi Vyote*, uk. 70. {VSS 360.3}

Mafundisho Akiwa Kwenye Magoti ya Mama Yake—Kuanzia utotoni, katika ujana wake, hadi maisha yake ya utu uzima, Yesu alijifunza Maandiko. Akiwa mtoto mdogo, kila siku alikaa karibu na mama yake, akifundishwa kutoka katika magombo ya manabii. — *Elimu*, uk. 185. {VSS 360.4}

Mitume

Usemi Rahisi, Sahihi, na Wazi—Mitume na wenzao walikuwa watu wasio na elimu rasmi ya kibinadamu; hata hivyo, kwa kumiminwa kwa Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste, usemi wao, iwe walizungumza lugha yao ya asili au lugha ya

kigeni, ulifanywa kuwa safi, rahisi, na sahihi katika maneno na matamshi. —

Tumaini za Vizazi Vyote, uk. 821. {VSS 361.1}

Kweli Zilizotukuka—Tangu wakati huu [Pentekoste] na kuendelea, lugha ya wanafunzi ilikuwa safi, rahisi, na sahihi katika maneno na matamshi, iwe walizungumza lugha yao ya asili au lugha ya kigeni. Watu hawa wanyenyekevu, ambao hawakuwa wamejifunza kamwe katika shule za manabii, waliwasilisha kweli zilizotukuka na safi kiasi kwamba ziliwashangaza wale waliowasikia. — *Kisa cha Wokovu*, uk. 246. {VSS 361.2}

Maneno Kama Mishale Mikali—Hoja za mitume, ingawa zilikuwa wazi na zenye kushawishi, zisingeweza peke yake kuondoa chuki iliyokuwa imedumu licha ya ushahidi mwingi uliokuwa umetolewa. Lakini Roho Mtakatifu alizifikisha hoja hizo mioyoni mwa watu kwa nguvu ya kimungu. Maneno ya mitume yalikuwa kama mishale mikali kutoka kwa Mwenyezi Mungu, yakiwathibitishia wanadamu hatia yao kubwa ya kumkataa na kumsulubisha Bwana wa utukufu. — *Matendo ya Mitume*, uk. 45. {VSSsw 361.3}

Mashujaa wa Imani—Wanafunzi walikuwa watu wanyenyekevu tu, wasio na mali wala silaha nyingine isipokuwa Neno la Mungu; hata hivyo, kwa nguvu ya Kristo walitoka kwenda kusimulia habari ya ajabu ya hori na msalaba, na kushinda upinzani wote. Bila heshima wala kutambuliwa kwa kibinadamu, walikuwa mashujaa wa imani. Kutoka midomoni mwao zilitoka maneno yenye ufasaha wa kimungu yaliyoutikisa ulimwengu. — *Matendo ya Mitume*, uk. 77. {VSS 361.4}

Wahubiri wa Mungu Muumba—Mitume walijitahidi kuwafundisha waabudu sanamu hao kumjua Mungu Muumba na Mwanawe, Mwokozi wa wanadamu. Kwanza walielekeza fikira zao kwenye kazi za ajabu za Mungu—jua, mwezi, na nyota; mpangilio mzuri wa majira yanayojirudia; milima mikubwa iliyofunikwa na theluji; miti mirefu; na maajabu mengine mbalimbali ya asili yaliyodhihirisha ustadi uliopita uwezo wa mwanadamu kuelewa. Kupitia kazi hizi za Mungu Muumba, mitume waliongoza akili za watu wa mataifa kumtafakari Mtawala wa ulimwengu. {VSS 362.1}

Baada ya kuweka wazi kweli hizi za msingi kuhusu Muumba, mitume waliwaeleza watu wa Listra kuhusu Mwana wa Mungu, aliyekuja kutoka mbinguni

kuja katika ulimwengu wetu kwa sababu aliwapenda wanadamu. — *Matendo ya Mitume, uk. 180. {VSS 362.2}*

Ujumbe Wazi na Rahisi—Watendakazi wa injili huko Korintho walitambua hatari kubwa zilizokuwa zikitishia roho za wale waliokuwa wakiwahudumia; na kwa kutambua wajibu mkubwa uliokuwa juu yao, waliwasilisha Kweli kama ilivyo katika Yesu. Ujumbe wao ulikuwa wazi, rahisi, na thabiti—harufu ya uzima iletayo uzima, au ya mauti iletayo mauti. Si kwa maneno yao tu, bali pia katika maisha yao ya kila siku, injili ilidhihirishwa. — *Matendo ya Mitume, uk. 249. {VSS 362.3}*

Unyenyekevu na Uwazi—Walikuwa wamewasilisha Kweli kwa unyenyekevu na uwazi, wakisali ili mioyo ya watu ishawishike na ibadilishwe. Pia walijitahidi kuweka mwenendo wao katika upatano na mafundisho yao, ili Kweli waliyowasilisha ijipendekeze kwa dhamiri ya kila mwanadamu. — *Matendo ya Mitume, uk. 330. {VSS 362.4}*

Ujasiri na Nguvu—Watu walishangazwa na ujasiri wa wanafunzi. Walidhani kwamba, kwa kuwa walikuwa wavuvi wasio na elimu, wangeshindwa na aibu watakapokabiliana na makuhani, waandishi, na wazee. Lakini walitambua kwamba walikuwa wamekuwa pamoja na Yesu. Mitume walizungumza kama Yesu alivyokuwa amesema, kwa nguvu yenye ushawishi iliyowanyamazisha wapinzani wao. — *Kisa cha Wokovu, uk. 252. {VSS 363.1}*

Yohana Mtume

Mtenda Kazi Mwaminifu na Mwenye Bidii—Baada ya kupaa kwa Kristo, Yohana alidhihirika kuwa mtenda kazi mwaminifu na mwenye bidii kwa ajili ya Bwana. Pamoja na wanafunzi wengine, alishiriki katika kumiminwa kwa Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste, na kwa bidii mpya na nguvu mpya aliendelea kuwatangazia watu maneno ya uzima, akitafuta kuelekeza mawazo yao kwa Yule asiyeonekana. Alikuwa mhubiri mwenye nguvu, mwenye shauku, na aliyejitoa kwa dhati katika kazi yake. Kwa lugha nzuri na sauti yenye mvuto wa pekee, alieleza maneno na matendo ya Kristo, akizungumza kwa namna iliyogusa mioyo ya wale waliomsikia. Unyenyekevu wa maneno yake, nguvu tukufu ya Kweli alizozitangaza, na bidii iliyotawala mafundisho yake vilimfungulia njia ya kuwafikia watu wa kila tabaka. — *Matendo ya Mitume, uk. 546. {VSS 363.2}*

Hakukuwa na Mabishano—Kama shahidi wa Kristo, Yohana hakujihusisha na mabishano wala mijadala yenye kuchosha. Alitangaza yale aliyoyajua, yale aliyoyaona na kuyasikia. — *Matendo ya Mitume*, uk. 555. {VSS 364.1}

Kuweka Mkazo kwenye Habari ya Injili—Imani ya Wakristo ilipoonekana kuyumba kutokana na upinzani mkali waliolazimika kukabiliana nao, mtumishi wa Yesu mzee na aliyethibitishwa kwa uzoefu alirudia kwa nguvu na ufasaha habari ya Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka. — *Matendo ya Mitume*, uk. 568. {VSS 364.2}

Urahisi wa Lugha—Aliposhuhudia juu ya neema ya Mwokozi, lugha yake rahisi ilikuwa na ufasaha uliotokana na upendo uliokuwa umejaza nafsi yake yote. Hakuwa na mashaka wala mashuku yoyote. Hakujihusisha na mabishano wala mijadala yenye kuchosha. — *Manuscript 8a*, 1888. {VSS 364.3}

Mhubiri Mwenye Nguvu—Maisha ya mtume yalikuwa katika upatano na mafundisho yake. Upendo uliokuwa ukiwaka moyoni mwake kwa Kristo ulimchochea kufanya kazi kwa bidii kubwa na bila kuchoka kwa ajili ya wanadamu wenzake, hasa kwa ajili ya ndugu zake katika kanisa la Kikristo. Alikuwa mhubiri mwenye nguvu, mwenye shauku, na aliyejitoe kwa dhati, na maneno yake yalibeba nguvu ya usadikisho. — *The Review and Herald*, Februari 15, 1881. {VSS 364.4}

Uwazi Mbele ya Mahakama ya Mfalme—Kwa sababu hiyo, Yohana aliitwa kwenda Rumi ili kuhukumiwa kwa ajili ya imani yake. Huko mbele ya mamlaka, mafundisho ya mtume yalipotoshwa. Mashahidi wa uongo walimshtaki kuwa alikuwa akifundisha mafundisho ya uzushi na uchochezi wa uasi. Kupitia mashtaka hayo, maadui zake walitumaini kusababisha kifo cha mwanafunzi huyo. {VSS 364.5}

Yohana alijitetea kwa uwazi na kwa hoja zenye kushawishi, kwa unyenyekevu na uaminifu mkubwa kiasi kwamba maneno yake yalikuwa na athari kubwa. Wasikilizaji wake walishangazwa na hekima na ufasaha wake. Lakini kadiri ushuhuda wake ulivyozidi kushawishi, ndivyo chuki ya wapinzani wake ilivyozidi kuongezeka. Mfalme Domitian alijawa na hasira. Hakuweza kupinga hoja za mtetezi mwaminifu wa Kristo wala kushindana na nguvu iliyoambatana na ushuhuda wake wa Kweli; hata hivyo, aliamua kuinyamazisha sauti yake. — *Matendo ya Mitume*, uk. 569, 570. {VSS 365.1}

Ushawishi wa Roho Mtakatifu—Unyenyekevu wa maneno yake, nguvu tukufu ya kweli alizozitangaza, na bidii ya kiroho iliyotawala mafundisho yake vilimpa nafasi ya kuwafikia watu wa kila tabaka. Hata hivyo, hata waamini hawakuweza kuelewa kikamilifu siri takatifu za Kweli za Mungu zilizofunuliwa katika mahubiri yake. Alionekana kuwa amejazwa daima na Roho Mtakatifu. Alitafuta kuinua mawazo ya watu ili waweze kufahamu mambo yasiyoonekana. Hekima aliyokuwa nayo katika kuzungumza ilisababisha maneno yake kushuka kama umande, yakilainisha na kutawala mioyo ya watu. — *The Review and Herald, Februari 15, 1881.* {VSS 365.2}

Petro

Kuwafikia Wasikilizaji Wake—Kwa uwazi na nguvu, Petro alitoa ushuhuda kuhusu kifo na ufufuo wa Kristo: “*Enyi waume wa Israeli, sikilizeni maneno haya:* {VSS 365.3}

Yesu wa Nazareti, mtu aliyedhihirishwa kwenu na Mungu kwa miujiza na ajabu na ishara, ambazo Mungu alizifanya kwa mkono wake kati yenu, kama ninyi wenyewe mnavyojua; mtu huyu alipotolewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa, na kwa kujua kwake tangu zamani, ninyi mkamsulibisha kwa mikono ya watu wabaya, mkamwua; ambaye Mungu alimfufua, akiufungua uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao.” Matendo 2:22-24 {VSS 366.1}

Petro hakurejelea mafundisho ya Kristo ili kuthibitisha hoja yake, kwa sababu alijua kwamba chuki ya wasikilizaji wake ilikuwa kubwa kiasi kwamba maneno yake kuhusu jambo hilo yasingelea matokeo yoyote. Badala yake, aliwaeleza kuhusu Daudi, ambaye Wayahudi walimwona kuwa mmoja wa wazee wa imani wa taifa lao. — *Matendo ya Mitume, uk. 41.* {VSS 366.2}

Kristo Kama Mfano Wake—Utetezi huu wa ujasiri uliwashangaza viongozi wa Kiyahudi. Walidhani kwamba wanafunzi wangetiwa hofu na kuchanganyikiwa waliposimama mbele ya Sanhedrini. Lakini badala yake, mashahidi hawa walizungumza kama Kristo alivyokuwa amesema, kwa nguvu ya ushawishi iliyowanyamazisha wapinzani wao. Hakukuwa na dalili yoyote ya hofu katika sauti ya Petro alipomtangaza Kristo kwa kusema: “*Yeye Ndiye Jiwe lile lililodharauliwa na ninyi waashi, nalo limewekwa kuwa jiwe kuu la pembeni.” Matendo ya Mitume 4:11 {VSS 366.3}*

Hapa Petro alitumia mfano wa usemi uliokuwa wa kawaida kwa makuhani na ambao waliuelewa vizuri. — *Matendo ya Mitume*, uk. 63, 64. {VSS 366.4}

Stefano

Mtetezi wa Kweli—Stefano, aliyekuwa wa kwanza miongoni mwa mashemasi saba, alikuwa mtu mwenye uchaji mkubwa kwa Mungu na imani pana. Ingawa alizaliwa akiwa Myahudi, alizungumza lugha ya Kigiriki na alifahamu desturi na mienendo ya Wayunani. Kwa hiyo, alipata nafasi ya kuhubiri injili katika masinagogi ya Wayahudi waliokuwa wakizungumza Kigiriki. Alikuwa mwenye bidii sana katika kazi ya Kristo, na alitangaza imani yake kwa ujasiri. Marabi wasomi na walimu wa sheria walijadiliana naye hadharani, wakitajia kwa uhakika kupata ushindi rahisi. Lakini *“lakini hawakuweza kushindana na hiyo hekima na huyo Roho aliyesema naye.”* **Matendo ya Mitume 6:10** Hakuzungumza kwa nguvu ya Roho Mtakatifu pekee tu, bali ilikuwa wazi kwamba alikuwa mwanafunzi wa unabii na mjuzi katika mambo yote ya sheria. Alitetea kwa ustadi Kweli alizofundisha, na aliwashinda kabisa wapinzani wake. — *Matendo ya Mitume*, uk. 97. {VSS 366.5}

Sauti Wazi na Yenye Kuvutia—Stefano alipoulizwa kuhusu Ukweli wa mashtaka yaliyokuwa yametolewa dhidi yake, alianza utetezi wake kwa sauti iliyo wazi na yenye kusisimua, iliyosikika katika ukumbi wa baraza. Kwa maneno yaliyolivutia na kuliteka kusanyiko lote, aliendelea kusimulia historia ya watu wateule wa Mungu. — *Matendo ya Mitume*, uk. 99. {VSS 367.1}

Hekima na Nguvu—Kwa nguvu itokayo juu, Stefano aliwakemea makuhani na wazee waliokuwa hawamwamini Mungu, na akamtukuza Yesu mbele yao. Hawakuweza kushindana na hekima na nguvu vilivyoambatana na maneno yake. — *Maandiko ya Awali*, uk. 197. {VSS 367.2}

Paulo

Maagizo Kutoka kwa Mungu—Paulo hakwenda katika makanisa kama mzungumzaji aliyetegemea ufasaha wa kibinadamu au kama mwanafalsafa wa kisayansi. Hakutafuta tu kufurahisha masikio ya watu kwa maneno na misemo iliyopambwa. Kwa urahisi wenye ufasaha, alitangaza mambo yale aliyofunuliwa. Aliweza kuzungumza kwa nguvu na mamlaka, kwa sababu mara nyingi alipokea maagizo kutoka kwa Mungu katika maono. — *The S.D.A. Bible Commentary*, Juzuu ya 6, uk. 1084. {VSS 367.3}

Uwezo Mzuri wa Kufikiri—Paulo aliweza kujenga hoja kwa uwazi wa ajabu, na kwa hoja zake kali pamoja na kejeli zake zenye nguvu aliweza kumdhoofisha mpinzani wake. Alikuwa msemaji mwenye ufasaha na mkosoaji mkali; akiwa na kusudi thabiti na ujasiri usiotetereka, Paulo alikuwa na sifa hasa zilizohitajika katika kanisa la kwanza. — *Matendo ya Mitume, uk. 124. {VSS 368.1}*

Maisha Yake Yalikuwa Mfano—Paulo alibeba pamoja naye hali ya mbinguni popote alipokwenda. Wote waliokuwa na uhusiano naye walihisi ushawishi wa umoja wake na Kristo. Ukweli kwamba maisha yake mwenyewe yalidhihirisha Kweli aliyokuwa akiitangaza ulipa mahubiri yake nguvu ya usadikisho. Hapo ndipo palipo na nguvu ya Kweli. Ushawishi wa maisha matakatifu unaojitokeza bila kulazimishwa wala kujifanya ndiyo mahubiri yenye ushawishi mkubwa zaidi yanayoweza kutolewa kwa ajili ya Ukristo. Hoja, hata ikiwa haziwezi kupingwa, zinaweza kusababisha upinzani tu; lakini mfano wa maisha ya utauwa una nguvu ambayo haiwezekani kuipinga kabisa. — *Watendakazi wa Injili, uk. 59. {VSS 368.2}*

Maombi Yenye Hekima, Uelewa, na Ushawishi—Mikono yake iliyochoka kwa kazi, alipoionyesha mbele ya watu, ilishuhudia kwamba hakumtegemea mtu yeyote kwa ajili ya mahitaji yake. Hakudhani kwamba hali hiyo ilipunguza nguvu ya maombi yake ya kugusa moyo—maombi yenye hekima, uelewa, na ufasaha mkubwa kuliko ya mtu mwingine yeyote aliyewahi kushiriki katika huduma ya Kikristo. — *The S.D.A. Bible Commentary, Juzuu ya 6, uk. 1064. {VSS 368.3}*

Njia ya Kufundisha Hatua kwa Hatua—Paulo hakuwakaribia Wayahudi kwa namna ambayo ingeamsha chuki na upendeleo wao. Mwanzoni hakuliwaambia kwamba walipaswa kumwamini Yesu Mnazareti; bali alizungumzia unabii uliomhusu Kristo, utume Wake, na kazi Yake. Hatua kwa hatua aliwaongoza wasikilizaji wake, akiwaonyesha umuhimu wa kuiheshimu sheria ya Mungu. Aliipa sheria ya ibada ya Kiyahudi heshima inayostahili, akionyesha kwamba Kristo ndiye aliyeanzisha mfumo wa ibada ya Kiyahudi na huduma ya dhabihu. Kisha aliwaongoza hadi kwenye kuja kwa kwanza kwa Mkombozi, na akaonyesha kwamba katika maisha na kifo cha Kristo kila jambo lililotabiriwa katika huduma ya dhabihu lilikuwa limetimizwa. **{VSS 369 .1}**

Kwa watu wa mataifa, Paulo aliwafikia kwa kumtukuza Kristo kwanza, kisha akawaonyesha mahitaji ya lazima ya sheria. Aliwaonyesha jinsi nuru iliyotoka katika

msalaba wa Kalvari ilivyotoa maana na utukufu kwa mfumo wote wa ibada ya Kiyahudi. **{VSS 369.2}**

Hivyo, mtume alibadilisha namna yake ya kufanya kazi, akiunda ujumbe wake kulingana na mazingira aliyokuwa nayo. Baada ya kufanya kazi kwa uvumilivu, alifanikiwa kwa kiwango kikubwa; hata hivyo, bado kulikuwa na wengi ambao hawakusadikishwa. — *Watendakazi wa Injili, uk. 118.* **{VSS 369.3}**

Lugha ya Unyenyekevu—Kuna tofauti kubwa kati ya madai ya kujisifu na kujihesabia haki ya wale wanaodai kuwa hawana dhambi, na lugha ya unyenyekevu ya mtume. Hata hivyo, ilikuwa usafi na uaminifu wa maisha yake mwenyewe uliotoa nguvu kwa maonyo yake kwa ndugu zake. — *Maisha Yaliyotakaswa, uk. 86.* **{VSS 369.4}**

Namna Yenye Nguvu—Roho wa Mungu alipokuwa juu yake, Paulo aliwaongoza wasikilizaji wake kwa uwazi na nguvu kupitia unabii hadi wakati wa kuja kwa kwanza kwa Kristo, akiwaonyesha kwamba Maandiko yalikuwa yametimia kuhusu mateso, kifo, na ufufuo Wake. — *Maandiko ya Awali, uk. 201, 202.* **{VSS 370.1}**

Hoja Zenye Kushawishi—Miongoni mwa wale waliokutana na Paulo sokoni walikuwa “wanafalsafa fulani wa Waepikureo na Wastoiko.” Hata hivyo, wao na wengine wote waliokutana naye waliona haraka kwamba alikuwa na hazina ya maarifa iliyokuwa kubwa kuliko yao. Uwezo wake wa kiakili uliwafanya wasomi wamheshimu; huku hoja zake zenye bidii, zenye mantiki, na nguvu ya usemi wake ilivuta usikivu wa wasikilizaji wote. Wasikilizaji wake walitambua kwamba hakuwa mwanafunzi asiye na uzoefu, bali alikuwa na uwezo wa kukabiliana na watu wa kila tabaka kwa hoja zenye kushawishi katika kutetea mafundisho aliyoyafundisha. Hivyo, mtume alisimama bila woga, akikabiliana na wapinzani wake katika uwanja wao wenyewe, akilinganisha mantiki kwa mantiki, falsafa kwa falsafa, na ufasaha kwa ufasaha. **{VSS 370.2}**

Wapinzani wake wapagani walimkumbusha juu ya hatima ya Socrates, ambaye kwa sababu ya kufundisha juu ya miungu ya kigeni alihukumiwa kifo; nao walimshauri Paulo asihatarishe maisha yake kwa njia hiyo hiyo. Lakini mahubiri ya mtume yaliwavuta watu kwa makini, na hekima yake isiyo na majivuno iliwafanya wamheshimu na kumstaajabia. — *Matendo ya Mitume, uk. 235, 236.* **{VSS 370.3}**

Kushindwa kwa Ufasaha na Mantiki Pekee—Ilikuwa desturi ya Paulo kutumia mtindo wa usemi wenye ufasaha katika mahubiri yake. Alikuwa mtu aliyestahili kusimama mbele ya wafalme, watu wakuu, na wasomi wa Athene. Uwezo wake mkubwa wa kiakili mara nyingi ulimsaidia katika kuandaa njia kwa ajili ya injili. Alijaribu kufanya hivyo huko Athene, akikutana na ufasaha kwa ufasaha, falsafa kwa falsafa, na mantiki kwa mantiki; lakini hakufanikiwa kupata mafanikio aliyokuwa ameyatarajia. — *The S.D.A. Bible Commentary, Juzuu ya 6, uk. 1084.*
{VSS 371.1}

Uwasilishaji Rahisi wa Kristo—Uzoefu wa mtume Paulo alipokutana na wanafalsafa wa Athene una somo muhimu kwetu. Alipowasilisha injili mbele ya mahakama ya Areopago, Paulo alikabiliana na mantiki kwa mantiki, sayansi kwa sayansi, na falsafa kwa falsafa. Wasikilizaji wake wenye hekima zaidi walishangazwa na kunyamazishwa, na hakuna mtu aliyeweza kupinga maneno yake. Hata hivyo, juhudi hiyo haikuzaa matunda mengi. Ni watu wachache tu walioongozwa kuikubali injili. Tangu wakati huo, Paulo alibadili namna yake ya kufanya kazi. Aliepuka hoja tata na mjadala mirefu kuhusu nadharia, bali kwa unyenyekevu aliwaelekeza wanaume na wanawake kwa Kristo kama Mwokozi wa wenye dhambi. **{VSS 371.2}**

Alipowaandikia Wakorintho kuhusu kazi yake miongoni mwao, alisema: *“Basi, ndugu zangu, mimi nilipokuja kwenu, sikuja niwahubiri siri ya Mungu kwa ufasaha wa maneno, wala kwa hekima. Maana naliazimu nisijue neno lo lote kwenu ila Yesu Kristo, Naye amesulibiwa. Nami nalikuwako kwenu katika hali ya udhaifu na hofu na matetemeko mengi. Na neno langu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na za nguvu, ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu.”* (1 Wakorintho 2:1-5) — *Huduma ya Uponyaji, uk. 214, 215.*
{VSS 371.3}

Hoja Zenye Kina—Ukweli wa jambo hilo ni kwamba Paulo alikuwa mtu mwenye elimu kubwa, na hekima yake pamoja na mwenendo wake viliwavutia wasikilizaji wake. Watu wenye elimu walifurahia maarifa yake, na wengi wao walimwamini Yesu. Aliposimama mbele ya wafalme na makusanyiko makubwa, alitoa maneno yenye ufasaha uliowavutia wote waliomsikia. Jambo hili liliwakasirisha sana makuhani na wazee. Paulo aliweza kwa urahisi kuingia katika hoja za kina, na kwa

kuinua mawazo ya watu hadi kwenye viwango vya juu vya fikira, aliwaongoza kutafakari utajiri mkuu wa neema ya Mungu na kuwaeleza upendo wa ajabu wa Kristo. Kisha, kwa unyenyekevu, alishuka hadi kufikia ufahamu wa watu wa kawaida na kwa namna yenye nguvu aliwasimulia uzoefu wake binafsi, jambo lililochoea ndani yao hamu kubwa ya kuwa wanafunzi wa Kristo. — *Maandiko ya Awali, uk. 206, 207. {VSS 372.1}*

Nguvu ya Uumbaji ya Mungu wa Kweli—Watu walivutiwa sana na jinsi Paulo alivyoeleza kwa bidii na mantiki sifa za Mungu wa Kweli—nguvu zake za uumbaji na uwepo wa uongozi wake mkuu juu ya viumbe vyote. Kwa ufasaha wenye bidii na msukumo, mtume alisema: *“Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, yeye, kwa kuwa ni Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono; wala hatumikiwi kwa mikono ya wanadamu kana kwamba anahitaji kitu cho chote; kwa maana Ndiye anayewapa wote uzima na pumzi na vitu vyote.”* Matendo ya Mitume 17:24-25 — *Matendo ya Mitume, uk. 238. {VSS 372.2}*

Busara kwa Wasikilizaji wa Mataifa—Maneno ya Paulo yana hazina kubwa ya maarifa kwa ajili ya kanisa. Alikuwa katika mazingira ambayo angeweza kusema jambo lolote ambalo lingewakasirisha wasikilizaji wake wenye majivuno na kumwingiza katika matatizo. Kama mahubiri yake yangekuwa shambulio la moja kwa moja dhidi ya miungu yao na watu mashuhuri wa mji huo, angeweza kukabiliwa na hatima kama ya Socrates. Lakini kwa busara iliyotokana na upendo wa Mungu, aliwaondoa kwa uangalifu mawazo yao kutoka kwa miungu ya kipagani na kuwaelekeza kwa Mungu wa kweli, ambaye walikuwa hawamjui. — *Matendo ya Mitume, uk. 241. {VSS 373.1}*

Kristo Alikuwa Kiini cha Mawazo Yake—Maneno ya Paulo yalisemwa kwa uzito mkubwa na kwa moyo wa dhati, kiasi kwamba wasikilizaji wake hawakuweza kushindwa kutambua kwamba alimpenda kwa moyo wake wote Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka. Walitambua kwamba mawazo yake yalikuwa yamejikita ndani ya Kristo na kwamba maisha yake yote yalikuwa yamefungamana na Bwana wake. Maneno yake yalikuwa na mvuto mkubwa kiasi kwamba ni wale tu waliokuwa wamejaa chuki kali dhidi ya dini ya Kikristo ndio walioweza kubaki bila kuguswa nayo. — *Matendo ya Mitume, uk. 247, 248. {VSS 373.2}*

Mafundisho Yenye Mantiki na Yanayotekelezeka—Paulo alikuwa msemaji mwenye ufasaha/umbuji. Kabla ya uongofu wake, mara nyingi alijitahidi kuwavutia wasikilizaji wake kwa matumizi ya usemi wa hali ya juu. Lakini baada ya kumjua Kristo, aliacha mtindo huo. Badala ya kutumia maelezo ya kishairi na mifano ya kubuni ambayo ingeweza kufurahisha hisia na kuchochea mawazo, lakini isiiguse uzoefu wa kila siku wa maisha, Paulo alitumia lugha rahisi kuifikisha mioyoni mwa watu kweli ambazo zilikuwa za umuhimu mkubwa. Maelezo ya kubuni kuhusu kweli yanaweza kusababisha msisimko mkubwa wa hisia; lakini mara nyingi kweli zinapowasilishwa kwa namna hiyo hazitoi chakula cha kiroho kinachohitajika ili kumtia nguvu na kumwezesha mwamini kukabiliana na mapambano ya maisha. Kwa hiyo, mahitaji ya haraka na majaribu ya sasa ya roho zinazopambana lazima yashughulikiwe kwa mafundisho yenye msingi imara, yanayotekelezeka, na yanayohusu kanuni za msingi za Ukristo. — *Matendo ya Mitume*, uk. 251, 252. {VSS 373.3}

Injili katika Usahili Wake—Katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu ambacho Paulo alikaa Korintho, kwa makusudi aliwasilisha Injili kwa usahili wake. “*Basi, ndugu zangu, mimi nilipokuja kwenu, sikuja niwahubiri siri ya Mungu kwa ufasaha wa maneno, wala kwa hekima. Na neno langu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na za nguvu, ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu.*” 1 Wakorintho 2:1, 4-5 {VSS 374.1}

Paulo alilazimika kurekebisha namna yake ya kufundisha kulingana na hali ya kanisa. “*Lakini, ndugu zangu, mimi sikuweza kusema nanyi kama na watu wenye tabia ya rohani, bali kama na watu wenye tabia ya mwilini, kama na watoto wachanga katika Kristo.*” 1 Wakorintho 3:1 {VSS 374.2}

Dini Yake Haikuwa Ukiri wa Maneno Tu—Mwenendo wake, ushawishi wake, na kukataa kwake kujifurahisha nafsi, vilipaswa kuonyesha kwamba dini yake haikuwa ukiri wa maneno tu, bali ilikuwa uhusiano wa kila siku na Mungu, ulio hai. Lengo moja aliliweka daima mbele yake, na alijitahidi kwa dhati kulifikia—“**haki ipatikanayo kwa imani katika Mungu.**”—[Philippians 3:9]. *Matendo ya Mitume*, 314. {VSS 374.3}

Nguvu ya Ushawishi—Kwa nguvu ya kushawishi, mtume aliwasilisha ukweli mkuu wa ufufuo. —*Matendo ya Mitume*, 320. {VSS 375.1}

Usemi Wazi—Mtume, kwa namna thabiti na yenye kuvutia sana, alijitahidi kurekebisha mawazo na desturi za uongo na zenye hatari zilizokuwa zimeenea katika kanisa la Korintho. Alizungumza kwa uwazi, lakini kwa upendo kwa ajili ya nafsi zao.—*Matendo ya Mitume*, [321](#). {VSS 375.2}

Mwenendo wa Utulivu na Kujitawala—Katikati ya ghasia [Tazama [Matendo 21:33-40](#)], mtume alikuwa mtulivu na mwenye kujitawala. Akili yake ilikuwa imemtegemea Mungu, naye alijua kwamba malaika wa mbinguni walikuwa wamemzunguka. Hakutaka kuondoka hekaluni bila kufanya jitihada ya kuwaeleza ndugu zake wa taifa lake ukweli. Alipokuwa karibu kupelekwa ndani ya ngome, alimwambia jemadari, “*Nina ruhusa nikuambie neno? Naye akasema, Je! Unajua Kiyunani? Wewe si yule Mmisri ambaye kabla ya siku hizi aliwafitinisha wale watu elfu nne, walioitwa Wauaji, akawaongoza jangwani? Paulo akasema, Mimi ni mtu wa Kiyahudi, mtu wa Tarso, mji wa Kilikia, mwenyeji wa mji usiokuwa mnyonge. Nakuomba, nipe ruhusa niseme na wenyeji hawa.*” *Matendo ya Mitume 21:37-39* {VSS 375.3}

Ombi hilo lilikubaliwa na “**Paulo akasimama madarajani, akawapungia mkono wale wenyeji**” *Matendo ya Mitume 21:40* Ishara hiyo ilivuta usikivu wao, na mwenendo wake ukawafanya wamheshimu. —[*Matendo ya Mitume*, 408] {VSS 376.4}

Uzoefu Binafsi—Kama angejaribu kubishana na wapinzani wake, wangekataa kwa ukaidi kusikiliza maneno yake; lakini aliposimulia uzoefu wake, simulizi hiyo ilikuwa na nguvu ya kushawishi ambayo, kwa muda huo, ilionekana kulainisha na kutuliza mioyo yao. —[*Matendo ya Mitume*, 409] {VSS 376.1}

Unyoofu Ulio Dhahiri—Kwa unyoofu na uwazi, alieleza kusudi la ziara yake huko Yerusalemu, pamoja na mazingira ya kukamatwa kwake na kushtakiwa kwake.... Mtume huyo alizungumza kwa dhati na kwa unyoofu ulio wazi, na maneno yake yalikuwa na nguvu kubwa ya ushawishi. —[*Matendo ya Mitume*, 421] {VSS 376.2}

Utetezi Wazi Mbele ya Agripa—Kwa uwazi na nguvu, Paulo alieleza mbele ya Agripa matukio makuu yaliyohusiana na maisha ya Kristo duniani. —[*Matendo ya Mitume*, 436] {VSS 376.3}

Adabu ya Kweli—Mtazameni Paulo alipokuwa akisimamishwa mbele ya watawala. Hotuba yake mbele ya Agripa ni mfano wa uungwana/adabu ya kweli pamoja na ufasaha wenye uwezo mkubwa wa kushawishi. — *Huduma ya Uponyaji*, uk. 489, 490. {VSS 376.4}

Tahadhari na Wema—Hakutaja lolote kuhusu mateso aliyoyapata kutoka kwa Wayahudi, wala kuhusu njama zao za mara kwa mara za kumuua. Maneno yake yalitambulishwa na tahadhari na wema. Alisimulia uzoefu wake mwenyewe na akawasilisha hoja kutoka katika Maandiko ya Agano la Kale kwa unyenyekevu, uaminifu, na nguvu. — *Matendo ya Mitume*, uk. 450, 451. {VSS 376.5}

Kama Sauti Kutoka Mbinguni—Kwa ufasaha na nguvu iliyopita uwezo wa kibinadamu, Paulo aliwasilisha kweli za injili. Aliwaelekeza wasikilizaji wake kwenye dhabihu iliyotolewa kwa ajili ya wanadamu walioanguka, akitangaza kwamba thamani isiyo na kikomo ilikuwa imelipwa kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu. {VSS 377.1}

Hivyo ndivyo mtetezi wa kweli alivyowasilisha hoja yake. Akiwa mwaminifu katikati ya wasio waaminifu na mtiifu katikati ya wasiotii, alisimama kama mwakilishi wa Mungu, na sauti yake ilikuwa kama sauti kutoka mbinguni. Hakukuwa na hofu, huzuni, wala kuvunjika moyo katika maneno yake au katika sura yake. {VSS 377.2}

Wengi waliomtazama siku hiyo “*waliona uso wake kama uso wa malaika.*” (*Matendo 6:15*). {VSS 377.3}

Kamwe kabla ya hapo kusanyiko hilo halikuwa limesikia maneno kama hayo. Maneno yake yaligusa nyuzi za mioyo hata ya wale waliokuwa wamefanywa wagumu zaidi. Kweli iliyo wazi na yenye kushawishi ilianguka makosa na uongo. — *Matendo ya Mitume*, uk. 495, 496. {VSS 377.4}

Timotheo

Mafundisho ya Nyumbani—Baba yake Timotheo alikuwa Myunani, naye mama yake alikuwa Myahudi. Tangu utotoni mwake alikuwa ameyajua Maandiko. Ucha Mungu aliouona katika maisha yao ya nyumbani ulikuwa wa kweli na wenye busara. Imani ya mama yake na bibi yake katika Maandiko matakatifu ilikuwa kwake

ukumbusho wa kudumu wa baraka inayopatikana katika kufanya mapenzi ya Mungu. Neno la Mungu lilikuwa kanuni ambayo kwayo wanawake hawa wawili wacha Mungu walimwongoza Timotheo katika maisha yake. Nguvu ya kiroho ya mafundisho aliyopokea kutoka kwao ilimsaidia kuwa safi katika usemi na kutobadilishwa na ushawishi wa uovu uliomzunguka. Hivyo, wale waliokuwa walimu wake nyumbani walishirikiana na Mungu katika kumwandaa kubeba majukumu mazito. **{VSS 377.5}**

Paulo aliona kwamba Timotheo alikuwa mwaminifu, thabiti, na mkweli, naye akamchagua kuwa mwenzake katika kazi na safari. Wale waliomfundisha Timotheo wakati wa utoto wake walipata thawabu kwa kuona mwana waliyemlea akiunganishwa katika ushirika wa karibu na mtume mkuu. Timotheo alikuwa kijana tu alipochaguliwa na Mungu kuwa mwalimu; lakini misingi ya tabia yake ilikuwa imejengwa imara kupitia elimu yake ya awali, kiasi kwamba alifaa kuchukua nafasi yake kama msaidizi wa Paulo. Ingawa alikuwa kijana, aliyabeba majukumu yake kwa unyenyekevu wa Kikristo. — *Matendo ya Mitume, uk. 203, 204.* **{VSS 378.1}**

SURA YA 62—WANAMATENGENEZO WA ZAMA ZA KATI

Wycliffe

Mwalimu na Mhubiri Hodari—Wycliffe alikuwa mwalimu hodari na mwenye bidii, pia alikuwa mhubiri mwenye ufasaha. Maisha yake ya kila siku yalikuwa ushuhuda hai wa kweli alizokuwa akihubiri. Maarifa yake ya Maandiko, nguvu ya hoja zake, usafi wa maisha yake, pamoja na ujasiri na uadilifu wake usioyumba, vilimpatia heshima na imani ya watu wengi. — *Pambano Kuu, uk. 81.* **{VSS 379.1}**

Kutokuwa na Hofu—Wycliffe alikata rufaa kutoka kwa sinodi kwenda kwa Bunge. Bila hofu alilishitaki tabaka la viongozi wa kanisa mbele ya baraza la taifa, akidai

kufanyika kwa matengenezo dhidi ya maovu makubwa yaliyokuwa yameidhinishwa na kanisa. Kwa nguvu yenye kushawishi alifunua jinsi mamlaka ya kipapa yalivyokuwa yamejinyakulia madaraka yasiyostahili na jinsi yalivyokuwa yamejaa uovu na ufisadi. — *Pambano Kuu*, uk. 89. {VSS 379.2}

Ujasiri na Unyenyekevu—Kwa ujasiri, Wycliffe alisimamia mafundisho yake na kuyakanusha mashtaka ya watesi wake. Akiweka kando masilahi yake binafsi, cheo chake, na hata mazingira aliyokuwamo wakati huo, aliwaita wasikilizaji wake wasimame mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu, akazipima hoja zao za upotoshaji na udanganyifu kwa mizani ya kweli ya milele. — *Pambano Kuu*, uk. 90. {VSS 379.3}

Huss

Mhubiri wa Neno la Mungu—Hata hivyo, ilikuwa katika uwanja mwingine ndipo Huss alianza kazi ya matengenezo. Miaka kadhaa baada ya kuwekwa wakfu kuwa kuhani, aliteuliwa kuwa mhubiri wa Kanisa la Bethlehemu. Mwanzilishi wa kanisa hilo alikuwa amesisitiza kwamba jambo la muhimu sana lilikuwa kuhubiri Maandiko kwa lugha ya watu. Licha ya upinzani wa Rumi dhidi ya desturi hiyo, haikuwa imekomeshwa kabisa katika Bohemia. Hata hivyo, kulikuwa na ujinga mkubwa kuhusu Biblia, na maovu mabaya zaidi yalikuwa yameenea miongoni mwa watu wa tabaka zote. Kwa hiyo, Huss aliyakemea maovu hayo bila kuyafumbia macho, akilitumia Neno la Mungu kuthibitisha kanuni za Kweli na usafi alizokuwa akifundisha. — *Pambano Kuu*, uk. 99. {VSS 380.1}

Jerome

Uwazi na Nguvu—Maneno ya Jerome yaliwashangaza na kuwavutia hata maadui zake. Kwa mwaka mzima alikuwa amefungwa gereza, bila fursa ya kusoma wala kuona, huku akiteseka sana kimwili na kuwa katika dhiki kubwa ya kiakili. Hata hivyo, hoja zake ziliwasilishwa kwa uwazi na nguvu kana kwamba alikuwa amepata nafasi ya kutosha ya kujifunza bila usumbufu wowote. — *Pambano Kuu*, uk. 112, 113. {VSS 380.2}

Luther

Bidii ya Dhati—Luther aliwekwa wakfu kuwa kuhani/kasisi, kisha akaitwa kutoka **katika monasteri** (nyumba ya watawa) kuwa mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Wittenberg. Huko alijitosa katika kujifunza Maandiko katika lugha zake za asili. Akaanza kufundisha Biblia, na Kitabu cha Zaburi, Injili, na Nyaraka zikafunguliwa kwa uelewa wa makundi makubwa ya wasikilizaji waliofurahia mafundisho yake. Alikuwa hodari katika Maandiko, na neema ya Mungu ilikuwa juu yake. Ufasaha wake uliwavutia wasikilizaji wake; uwazi na nguvu alizotumia kuwasilisha Kweli ziliwashawishi na kuwasadikisha, na bidii yake ya dhati iligusa mioyo yao. — *Kisa cha Wokovu, uk. 341.* {VSS 381.1}

Msimamo Usio na Hofu—Unyenyekevu wenye nguvu wa maneno yake, msimamo wake usio na hofu, macho yake yaliyotulia alipokuwa akizungumza, na azimio lisiloyumba lililoonekana katika kila neno na tendo lake, vililiacha kusanyiko lote na hisia kubwa. Ilikuwa wazi kwamba hangeweza kushawishiwa kwa ahadi wala kutishwa kwa vitisho ili akubali amri ya Roma. {VSS 381.2}

Kristo alinena kupitia ushuhuda wa Luther kwa nguvu na utukufu uliowajaza marafiki na maadui wake hofu na mshangao. — *Kisa cha Wokovu, uk. 348.* {VSS 381.3}

Chombo Teule cha Mungu—Luther alikuwa chombo teule cha Mungu cha kulivua Kanisa la Upapa vazi la unafiki na kufichua upotovu wake. Aliinua sauti yake kwa bidii, na kwa nguvu za Roho Mtakatifu akakemea dhambi zilizokuwa zikitendwa na viongozi wa watu. — *Shuhuda kwa Kanisa, Juzuu ya 1, uk. 372.* {VSS 381.4}

Nguvu ya Utulivu na Heshima—Nguvu ya Luther iliyodhihirishwa kwa utulivu na heshima iliwaabisha maadui zake na kulipiga upapa pigo kubwa sana. — *Shuhuda kwa Kanisa, Juzuu ya 1, uk. 373.* {VSS 382.1}

Maneno Yenye Ukuu—Sala ya Luther ilijibiwa. Ujasiri na imani yake vilirejea alipokutana na maadui zake. Akiwa mpole kama mwana-kondoo, alisimama akiwa amezungukwa na wakuu wa dunia waliomtazama kama mbwa-mwitu wenye hasira, wakitumaini kumtisha kwa mamlaka na ukuu wao. Lakini alikuwa ameshikamana na nguvu za Mungu, wala hakuogopa. Maneno yake yalitamkwa kwa ukuu na nguvu kiasi kwamba maadui zake hawakuweza kufanya lolote dhidi yake. {VSS 382.2}

Utulivu wake ulitofautiana sana na hasira na ghadhabu zilizoonyeshwa na wale waliojiita watu wakuu. Hawakuweza kumlazimisha kuikana Kweli. Kwa

unyenyekavu wa heshima na uthabiti wa utulivu, alisimama imara kama mwamba. — *Shuhuda kwa Kanisa, Juzuu ya 1, uk. 374, 375. {VSS 382.3}*

Ufafanuzi Wenye Nguvu—Katika mahojiano yaliyofuata, Luther aliwasilisha maelezo yaliyo wazi, mafupi, na yenye nguvu kuhusu mafundisho yake, akiyaunga mkono kikamilifu kwa nukuu nyingi kutoka katika Maandiko. — *Pambano kuu, uk. 136. {VSS 382.4}*

Umakini na Bidii ya Dhati—Uzito na bidii ya dhati iliyodhihirika katika maneno yake vilimpa nguvu ambayo hata maadui zake hawakuweza kuipinga kabisa. — *Pambano Kuu, uk. 154. {VSS 382.5}*

Busara na Heshima—“Kwa sababu hiyo, ninakusihi, Ee Mfalme Mkuu, kwa unyenyekevu wote, uniruhusu nipate muda ili nijibu bila kwenda kinyume na Neno la Mungu.” *{VSS 383.1}*

Kwa ombi hilo, Luther alitenda kwa busara. Mwenendo wake ulilithibitisha kusanyiko kwamba hakutenda kwa hasira wala kwa msukumo wa ghafla. Utulivu wake na uwezo wake wa kujitawala, ambao haukutarajiwa kwa mtu aliyejulikana kwa ujasiri na kutokubali maridhiano, viliongeza nguvu yake na baadaye vikamwezesha kujibu kwa busara, uthabiti, hekima, na heshima. Jambo hilo liliwashangaza na kuwavunja moyo wapinzani wake, huku likikemea jeuri na kiburi chao. — *Pambano Kuu, uk. 156. {VSS 383.2}*

Maandalizi Makini ya Utetezi Wake—Akiwa ameweka mawazo yake kwa Mungu, Luther alijiandaa kwa pambano lililokuwa mbele yake. Alitafakari mpangilio wa majibu yake, akachunguza sehemu mbalimbali za maandishi yake mwenyewe, na akakusanya ushahidi unaofaa kutoka katika Maandiko Matakatifu ili kuunga mkono msimamo wake. — *Pambano Kuu, uk. 157. {VSS 383.3}*

Sauti ya Unyenyekevu—Kisha afisa wa mfalme alimtaka atoe uamuzi wake kuhusu ikiwa alikuwa tayari kuyakana mafundisho yake. Luther akajibu kwa sauti ya utulivu na unyenyekevu, bila ukali wala hasira. Mwenendo wake ulikuwa wa kiasi na wenye heshima; hata hivyo, alionyesha ujasiri na utulivu wa ndani uliolishangaza kusanyiko lote. — *Pambano Kuu, uk. 158. {VSS 383.4}*

Ujasiri na Uthabiti—Ujasiri na uthabiti aliouonyesha wakati huo, pamoja na nguvu na uwazi wa hoja zake, uliwashangaza watu wa pande zote. — *Pambano Kuu, uk. 160, 161. {VSS 383.5}*

Mbele za Mungu—Viongozi wa upapa walikasirishwa kwa kuona kwamba mamlaka yao, yaliyowafanya wafalme na wakuu kutetemeka, yalidharauliwa na mtawa mnyenyekevu. Walitamani kumfanya ahisi ghadhabu yao kwa kumtesa hadi kufa. Lakini Luther, akitambua hatari iliyokuwa mbele yake, aliwahutubia wote kwa heshima na utulivu wa Kikristo. Maneno yake hayakuwa na kiburi, hasira, wala upotoshaji. Alijisahau mwenyewe, akawasahau hata wakuu waliomzunguka, na akatambua tu kwamba alikuwa mbele za Yule aliye mkuu zaidi kuliko mapapa, maaskofu wakuu, wafalme, na watawala. Kristo alinena kupitia ushuhuda wa Luther kwa nguvu na utukufu uliowajaza marafiki na maadui wake hofu na mshangao. **{VSS 384.1}**

Mteule Frederick alikuwa akisubiri kwa hamu kuu kumwona Luther akisimama mbele ya Baraza la Dola, na kwa hisia nyingi alisikiliza hotuba yake. Kwa furaha na fahari alishuhudia ujasiri, uthabiti, na utulivu wake, akaazimia kusimama imara zaidi katika kumtetea. — *Pambano Kuu, uk. 161, 162.* **{VSS 384.2}**

Hoja Zilizo Wazi—Tofauti kati ya wabishi hao wawili—Oekolampadio na Eck—haikukosa kuleta athari. Hoja za Mtengenezaji huyo wa Matengenezo, zilizokuwa tulivu, wazi, na zilizowasilishwa kwa upole na unyenyekevu, zilivutia akili za wale waliokerwa na madai ya majivuno na makelele ya Eck. — *Pambano Kuu, uk. 184.* **{VSS 384.3}**

Akina Wesley na Whitefield

Kuhesabiwa Haki na Kufanywa Upya—Maisha ya Wesley yalijitolea kikamilifu kuhubiri Kweli kuu alizokuwa amezipokea—kuhesabiwa haki kwa njia ya imani katika damu ya Kristo iliyomwagika kwa ajili ya upatanisho, na nguvu ya Roho Mtakatifu ya kuufanya moyo kuwa mpya, ili uzae matunda katika maisha yanayopata na mfano wa Kristo. **{VSS 384.4}**

Whitefield na akina Wesley walikuwa wameandaliwa kwa kazi yao kupitia uzoefu mrefu na mgumu wa kutambua hali yao wenyewe ya kupotea. Ili waweze kuvumilia magumu kama askari wema wa Kristo, walipitia tanuru la majaribu ya dhihaka, kejeli, na mateso, wakiwa chuoni na hata walipoanza huduma yao. **{VSS 385.1}**

Kwa kuwa walikuwa washiriki wa Kanisa la Anglikana, walishikamana kwa dhati na taratibu zake za ibada. Hata hivyo, Bwana alikuwa amewaonyesha katika

Neno Lake kiwango cha juu zaidi. Roho Mtakatifu aliwasukuma kumhubiri Kristo, naye aliyesulubiwa. Nguvu za Aliye Juu ziliandamana na kazi yao. Maelfu ya watu walishawishika kuhusu dhambi zao na kuongoka kwa Kweli. Ilikuwa lazima kondoo hawa walindwe dhidi ya mbwa-mwitu wakali. Wesley hakuwahi kufikiria kuanzisha dhehebu jipya; badala yake, aliwapanga waumini hao katika ushirika uliojulikana kama **Methodist Connection**. — *Pambano Kuu, uk. 256, 257. {VSS 385.2}*

Injili ya Neema ya Mungu—Hivyo, alipokuwa akihubiri injili ya neema ya Mungu, John Wesley, kama Bwana wake, alitafuta “kuitukuza sheria na kuifanya iheshimike.” Aliitekeleza kwa uaminifu kazi aliyokabidhiwa na Mungu, na matokeo aliyobarikiwa kuyaona yalikuwa ya utukufu. Mwishoni mwa maisha yake marefu ya zaidi ya miaka themanini, ambayo zaidi ya nusu karne aliitumia katika huduma ya kuhubiri kutoka mahali hadi mahali, idadi ya wafuasi wake waliotambulika ilifikia zaidi ya nusu milioni. Hata hivyo, idadi ya watu ambao kupitia huduma yake waliinuliwa kutoka katika uharibifu na udhalili wa dhambi na kuingia katika maisha yaliyo bora na safi zaidi, pamoja na wale ambao kwa mafundisho yake walipata uzoefu wa kina na wa utajiri zaidi wa kiroho, haitajulikana kamwe mpaka familia yote ya waliokombolewa ikusanywe katika ufalme wa Mungu. Maisha yake yanatoa somo lenye thamani isiyokadirika kwa kila Mkristo. Laiti imani, unyenyekevu, bidii isiyochoka, kujikana nafsi, na kujitolea kwa mtumishi huyu wa Kristo vingedhihirishwa pia katika makanisa ya leo! — *Pambano Kuu, uk. 264. {VSS 385.3}*

Watu Wanyenyekevu wa Nyakati za Matengenezo

Hoja Rahisi na Zilizo Wazi—Kwa hoja, hila za mabishano, mapokeo ya mababa wa kanisa, na mamlaka ya kanisa, wengi walijaribu kuipinga Kweli. Watetezi wa kweli walilazimika kurejea kwenye Biblia zao ili kuthibitisha uhalali wa amri ya nne. Watu hao wanyenyekevu, wakiwa wamejihami kwa Neno la Kweli pekee, walikabiliana na mashambulizi ya wasomi ambao, kwa mshangao na hasira, waligundua kwamba ufasaha wao wa mabishano na hoja zao za ujanja haukuwa na nguvu mbele ya hoja rahisi, za moja kwa moja, na zenye msingi wa Maandiko

zilizotolewa na watu waliokuwa na ujuzi mkubwa wa Maandiko kuliko wa mbinu za mabishano za shule. —*Pambano Kuu*, uk. 455. {VSS 386.1}

SURA YA 63—WAANZILISHI WA KIADVENTISTA

William Miller

Lugha ya Kweli—Mahubiri ya Bw. Miller hayakuwa ya maneno yaliyopambwa wala ya ufasaha wa kisanaa. Badala yake, aliwasilisha Ukweli kwa lugha rahisi na kwa hoja zenye nguvu zilizowaamsha wasikilizaji wake kutoka katika hali yao ya kutojali. Kadiri alivyoendelea kuhubiri, aliunga mkono kauli na mafundisho yake kwa uthibitisho wa Maandiko. Maneno yake yaliambatana na nguvu ya usadikisho, kiasi kwamba yalionekana kuwa ni lugha ya kweli. {VSS 387.1}

Alikuwa msemaji mwenye kuvutia, na maonyo yake, kwa wale waliodai kuwa Wakristo na kwa wale ambao hawakuwa wametubu, yalikuwa yenye kufaa na yenye nguvu. Wakati mwingine mikutano yake ilitawaliwa na hali ya uzito mkubwa, kiasi cha kuwagusa sana waliohudhuria. Hisia ya ukaribu wa mgogoro mkuu wa matukio ya wanadamu, iligusa kwa kina akili za umati wa wasikilizaji. — *Life Sketches of Ellen G. White*, uk. 27. {VSS 387.2}

James White

Ujasiri katika Kutenda na Kunena—Mungu Ndiye anayestahili utukufu kwa sababu ya uaminifu usioyumba na ujasiri wa hali ya juu ambao mume wangu aliunyesha katika kuitetea haki na kukemea uovu. Uthabiti na msimamo wa namna hiyo ulihitajika sana mwanzoni mwa kazi hii, na umeendelea kuhitajika kadiri kazi ilivyoendelea hatua kwa hatua. Daima alisimama kuitetea Kweli bila kulegeza hata kanuni moja ili kumpendeza hata rafiki yake wa karibu zaidi. Alikuwa na tabia ya

hisia kali, jasiri na asiyeogopa katika kutenda na kunena. Hali hiyo mara nyingi ilimwingiza katika matatizo ambayo angeweza kuyaepuka. Hata hivyo, mara nyingi alilazimika kusimama imara zaidi, kuwa na msimamo thabiti zaidi, na kusema kwa bidii na ujasiri zaidi, kwa sababu ya tofauti kubwa ya tabia kati yake na watu walioshirikiana naye katika kazi. — *Life Sketches of Ellen G. White*, uk. 243. {VSS 387.3}

Uwazi wa Fikra—Baada ya Mungu kutujaribu na kututhibitisha katika tanuru la mateso, alimwinua mume wangu na kumpa uwazi mkubwa zaidi wa fikra pamoja na uwezo mkubwa zaidi wa kiakili wa kupanga na kutekeleza kazi kuliko alivyokuwa nao kabla ya mateso hayo. Mume wangu alipoutambua udhaifu wake mwenyewe na kutembea katika kumcha Mungu, ndipo Bwana alipokuwa nguvu zake. Alikuwa mwepesi wa kusema na kutenda, na kwa njia hiyo alisukuma mbele mageuzi ambayo, la sivyo, yangesuasua. Pia alitoa kwa ukarimu michango mingi, akiogopa kwamba mali yake ingeweza kuwa mtego kwake. — *Life Sketches of Ellen G. White*, uk. 244. {VSSw 388.1}

Nuru ya Thamani ya Kweli kwa Ajili Yake Mwenyewe—Mungu ameruhusu nuru ya thamani ya kweli iangaze juu ya Neno Lake na kuangaza akili ya mume wangu. Kwa njia ya mahubiri na maandishi yake, anaweza kuwaakisia wengine miale ya nuru itokayo mbele za Yesu. — *Shuhuda kwa Kanisa, Juzuu ya 3*, uk. 502. {VSSw 388.2}

Nuru Kubwa Zaidi kwa Ajili ya Wengine—Nilionyeshwa kwamba, kwa namna fulani, uhusiano wa mume wangu na watu wa Mungu ulikuwa sawa na ule wa Musa kwa Waisraeli. Kama walivyokuwapo walionung'unika dhidi ya Musa wakati wa nyakati za majaribu, ndivyo pia walivyokuwapo walionung'unika dhidi yake. Mungu pia alimpa mume wangu nuru kubwa kuhusu mafundisho ya Biblia, si kwa ajili yake mwenyewe tu, bali pia kwa ajili ya wengine. Niliona kwamba mambo haya yanapaswa kuandikwa na kutangazwa, na kwamba nuru mpya ingeendelea kuangaza juu ya Neno la Mungu. — *Shuhuda kwa Kanisa, Juzuu ya 3*, uk. 85. {VSSw 389.1}

Chombo cha Mungu kwa Ajili ya Kukemea—Mume wangu aliposimama kando yangu kunitegemeza katika kazi yangu na kutoa ushuhuda wa wazi uliopatana na kazi ya Roho wa Mungu, wengi walidhani kwamba yeye binafsi ndiye aliyekuwa akiwajeruhi. Lakini ukweli ni kwamba Bwana ndiye aliyemtika mzungu huo, na kupitia kwa mtumishi Wake alikuwa akiwakemea na kuwavuta ili watubu makosa

yao na kupata kibali cha Mungu. — *Shuhuda kwa Kanisa, Juzuu ya 3, uk. 261.*
{VSSsw 389.2}

Ushawishi wa Maandishi Yake —Mume wangu amefanya kazi bila kuchoka ili kuikuza huduma ya uchapishaji hadi kufikia hali yake ya sasa ya mafanikio. Niliona kwamba ndugu zake walikuwa na upendo na huruma nyingi zaidi kwake kuliko alivyodhani. Walikuwa wakilisoma gazeti kwa hamu wakitafuta kuona kama kulikuwa na jambo lolote lililoandikwa na yeye. Maandishi yake yalipokuwa na sauti ya matumaini na maneno ya kutia moyo, mioyo yao ilijawa na faraja, na wengine hata walilia kwa furaha ya upole. Lakini maandishi yake yalipoonyesha huzuni au majonzi, nyuso za ndugu na dada zake zilijawa na huzuni walipokuwa wakiyasoma, na roho iliyodhihirishwa katika maandishi yake iliakisiwa pia ndani yao. — *Shuhuda kwa Kanisa, Juzuu ya 3, uk. 96–97.* **{VSSsw 389.3}**

W. W. Prescott

Chanzo cha Mafanikio—Ninajua kwamba tangu alipofika mahali hapa amepokea kumiminwa kwa Roho Mtakatifu; midomo yake imeguswa na kaa la moto lililotoka madhabahuni. Tunajua na tunaweza kuitambua sauti ya Mchungaji wa Kweli. Kweli imemiminwa kutoka katika midomo ya mtumishi wa Mungu kwa namna ambayo watu hawakuwa wamewahi kuisikia hapo awali. Wasioamini hushtuka, nyuso zao zikibadilika rangi, na kusema, “Mtu huyu amevuviwa na Mungu.” Watu hawazunguki-zunguki ovyo katika eneo la mkutano, bali huingia mara moja ndani ya hema na kusikiliza kana kwamba wameshikiliwa na nguvu isiyoonekana.
{VSSsw 390.1}

Kila siku baadhi ya watendakazi wetu huenda katika vitongoji wakiwa na nakala za *Bible Echoes*, matangazo, na mialiko ya kuwaalika watu kuhudhuria mikutano ambako mambo ya ajabu yanafunuliwa kutoka katika Neno la Mungu. Bwana anaendelea kumimina nuru mpya, yenye thamani kama dhahabu, ndani ya akili na katika hekalu la nafsi. Sijawahi kusikia Neno la Mungu likihubiriwa kwa bidii na nguvu kama nilivyosikia hapa. Ninajua kwamba jambo hili linawezekana tu kwa sababu ya nguvu ya Mungu inayotenda kazi kupitia kwa chombo chake cha kibinadamu. Wengi wamekuwa wakisema kwamba hakuna aina yoyote ya vurugu katika eneo la mkutano. Kila ninapoingia kambini, ninafikiri kwamba malaika wa Mungu wapo hapo. — *Letter 82, 1895.* **{VSSsw 390.2}**

Mjumbe wa Mungu wa Nyakati Zetu

Hotuba ya Kwanza (Poland, Maine, 1845) —Kwa muda wa miezi mitatu, koo langu na mapafu yangu yalikuwa yamesumbuliwa na ugonjwa kiasi kwamba niliweza kuzungumza kidogo tu, tena kwa sauti ya chini na ya kukwaruza. Katika tukio hili, nilisimama katika mkutano na kuanza kuzungumza kwa sauti ya kunong’ona. Niliendelea hivyo kwa takribani dakika tano, ndipo maumivu na kizuizi vilipoondoka; sauti yangu ikawa wazi na yenye nguvu, nami nikazungumza kwa urahisi na uhuru kamili kwa karibu saa mbili. Baada ya ujumbe wangu kumalizika, sauti yangu ilipotea tena hadi niliposimama mbele ya watu kwa mara nyingine; ndipo urejesho ule wa ajabu ulirudiwa tena. Nilikuwa na uhakika wa kudumu kwamba nilikuwa nikifanya mapenzi ya Mungu, na niliona matokeo makubwa yakifuatana na juhudi zangu. — *Life Sketches of Ellen G. White*, uk. 72, 73. {VSSsw 391.1}

Nguvu Kutoka kwa Bwana—Siku ya Sabato nilikuwa dhaifu sana. Baada ya kuzungumza na watu, nilichoka kiasi kwamba nilikaribia kuzimia. Watu walisema kwamba hawakuwa wamewahi kuniona katika hali mbaya kama ile. Nilipoteza kilo kumi na tano za uzito wa mwili ndani ya majuma matatu. Jumapili nilimsihi Bwana anipe nguvu ili niweze kutoa ushuhuda wangu kwa watu, nami nikaamini. Nilipanda jukwaani nikiwa dhaifu sana, nikazungumza kwa saa moja na nusu, kisha niliposhuka nilikuwa na nguvu nyingi zaidi kuliko nilivyokuwa nilipopanda, na niliendelea kuwa na nguvu zile nilizopewa katika tukio hilo. {VSSsw 391.2}

Nimepokea hivi karibuni ombi kutoka kwa watu mashuhuri zaidi wa Dunlap—mabenki, wahudumu wa dini, na wafanyabiashara—la kurudia hotuba yangu niliyotoa Jumapili chini ya hema kuhusu suala la kiasi katika kanisa la Congregational. — *Letter 22, 1879*. {VSSsw 392.1}

Nguvu Kupitia Roho Mtakatifu—Nilipotarajiwa kuzungumza mbele ya watu wengi, nyakati fulani nilihisi kwamba haingewezekana kwangu kusimama siku baada ya siku mbele ya makusanyiko makubwa. Lakini nilijitahidi kujiweka kimwili katika uhusiano unaofaa na Mungu. Kisha nilimwambia: “Bwana, nimefanya yote ninayoweza kufanya, nikitumia njia ulizonipa Wewe Mwenyewe, na sasa naomba baraka maalumu ambayo Wewe pekee unaweza kunipa ili kuniimarisha.” Kwa hatua za kutetemeka niliingia jukwaani ili kuzungumza mbele ya maelfu ya watu

waliokusanyika; lakini mara tu niliposimama mbele ya kusanyiko, Roho wa Mungu alikuja juu yangu daima kwa nguvu ya kunitia nguvu. {VSSsw 392.2}

Mara nyingi nilimwambia mume wangu alipokuwa pamoja nami: “Laiti ningekuwa na uhakika kabla ya kuanza, ingekuwa msaada mkubwa kwangu.” Naye alinijibu: “Mungu hajawahi kushindwa kukubariki wakati unapoinuka kuzungumza; kwa hiyo, bila kujali hisia zako, lazima umtumaini Yeye, ukiitegemeza nafsi yako isiyo na msaada juu ya ahadi Zake.” Nimejitahidi kufanya hivyo. Nimejifunza kwamba ni lazima tufanye sehemu yetu, tukishirikiana na Mungu. Yeye hutoa nguvu kwa kila wajibu. — *Manuscript 8a, 1888.* {VSSsw 392.3}

Sauti Aliyopewa na Mungu—Nilipokuwa na umri wa karibu miaka kumi na moja tu, nilimsikia mhudumu wa injili akisoma simulizi la Petro alipofungwa gerezeni, kama lilivyoandikwa katika kitabu cha Matendo ya Mitume. Alilisoma kwa namna yenye kuvutia sana kiasi kwamba maelezo yote ya simulizi hilo yalionekana kana kwamba yalikuwa yakipita mbele ya macho yangu kwa uhalisia wake. Hisia kubwa iliyojengwa moyoni mwangu ilikuwa ya kina sana kiasi kwamba sijawahi kuisahau. {VSSsw 392.4}

Miaka michache baadaye, nilipokuwa nikizungumza katika mikutano mikuu, nilikutana tena na mtu huyo. Baada ya kumaliza hotuba yangu, aliniuliza: “Ulipata wapi sauti hiyo ya ajabu?” Nilimjibu kwamba Bwana ndiye aliyenipa. Nilipoanza huduma yangu ya hadhara, sikuwa na sauti isipokuwa niliposimama mbele ya makusanyiko ili kuzungumza. Wakati mwingine sikuweza kusema zaidi ya kunong’ona. Kisha nikaongeza: “Mara nyingi nimekumbuka yale uliyowaambia watu ulipoulizwa jinsi ulivyokuwa mhudumu wa injili. Uliwaambia kwamba rafiki zako walisema usingeweza kuwa mhudumu kwa sababu hukuweza kuzungumza vizuri; lakini ukaenda peke yako msituni na kuzungumza na miti. Pia ulipokuwa ukiendesha ng’ombe, uliendelea kuzungumza nao kana kwamba ulikuwa katika mkutano. Uliwaambia kwamba hiyo ndiyo njia uliyotumia kujifunza kuzungumza hadharani.” — *Manuscript 91, 1903.* {VSSsw 393.1}

Msaada wa Mungu Katika Kuzungumza—Siku iliyofuata nilikuwa mgonjwa na dhaifu sana. Mafua yalikuwa yameshika mwili wangu kwa nguvu. Nilikuwa na mashaka ikiwa ningeweza kuzungumza siku iliyofuata. Hata hivyo, nilikubali ndugu kupanga muda wa mimi kuzungumza na watu siku ya Sabato asubuhi. Nilimtegemea Bwana kabisa, kwa maana nilijua kwamba pasipo Yeye kuwa msaidizi wangu,

nisingeweza kusema zaidi ya maneno machache. Koo langu na kichwa changu vilikuwa vikisumbuliwa sana. Nilikuwa nimekuwa na sauti ya kukwaruza kiasi kwamba nilishindwa karibu kabisa kuzungumza kwa sauti kubwa. {VSSsw 393.2}

Asubuhi ya Sabato sikuwa nimepata nafuu. Wakati uliopangwa ulipofika, nilikwenda kwenye kanisa na nikalikuta limejaa watu. Niliogopa kwamba ningeshindwa, lakini nilianza kuzungumza. Mara tu nilipoanza kuzungumza, nilipewa nguvu. Mkwaruzo wa sauti uliondoka, nami nikazungumza bila shida kwa karibu saa moja. Ugonjwa wangu ulionekana kutoweka, na akili yangu ikawa wazi. Mara tu nilipomaliza kuzungumza, ukwaruzo wa sauti ulirudi tena, nami nikaanza kukohoa na kupiga chafya kama hapo awali. {VSSsw 394.1}

Kwangu mimi, uzoefu huu ulikuwa ushahidi dhahiri wa msaada wa Mungu. — *The Review and Herald, Julai 19, 1906.* {VSS 394.2}

Mahubiri Marefu ya Ellen White—(*Sehemu hii pamoja na inayofuata ni sehemu ya mazungumzo yasiyopangwa yaliyofanyika wakati Ellen White alipokuwa akizungumza na Konferensi Kuu huko Lake Goguwac, Michigan, tarehe 14 Julai 1890.*) **Mzee Underwood:** “Je, tunahubiri kwa muda mrefu sana?” {VSSsw 394.3}

Ellen White: “Ndiyo, kwa kweli; nami pia ninajihusisha katika jambo hili. Mimi pia huhubiri kwa muda mrefu sana.” {VSSsw 394.4}

W. C. White: “Niruhusu niulize swali. Je, tunapaswa kuchukua mfano wako kama kielelezo cha mtazamo wako kuhusu jambo hili?” {VSSsw 394.5}

Ellen White: “Naam, je, sikufanya ukiri wangu muda mfupi uliopita? Na je, sijawapa mfano? Najiona kuwa mwenye hali ya pekee katika jambo hili, lakini nafikiri hata katika hali hiyo ya pekee nimeenda mbali zaidi ya inavyopaswa. Lakini nitawaambia kwa nini najiona kuwa mwenye hali ya pekee. Nimewahi kuchukuliwa na mume wangu, nikabebwa hadi kwenye gari na kulazwa kwenye kiti, kisha nikapelekwa mahali pa mkutano. Nilikuwa nimeathiriwa na kupooza kwa majuma kadhaa, kiasi kwamba sikuweza hata kupanga maneno yangu vizuri ili kusema sentensi moja kwa usahihi. Hata hivyo, nilisimama mbele ya watu na kutoa ushuhuda wangu kwa unyoofo mkubwa. Roho wa Bwana alikuwa juu yangu. Kila mtu si mwenye hali hiyo ya pekee. Sasa, ninawezaje kujua ninapokwenda mbali sana? Nimefikishwa katika hali hiyo tena na tena. {VSSsw 394.6}

Sasa, ni mpaka gani ninapaswa kufikia? Nimechukua msimamo kwamba ikiwa Bwana atanipa mzigo wa ujumbe kwa kanisa la Battle Creek, nitawaambia; lakini nisipokuwa na mzigo huo, sina jambo jingine la kusema. Nilizungumza mara 21 katika kipindi cha siku hizo huko Battle Creek. Sikuzungumza kila siku, lakini siku fulani nilizungumza mara mbili. Hii ilikuwa kabla sijatoka huko; na sikupata mapumziko hadi jambo hilo liliposababisha ugonjwa huu mkubwa. Nilijua, na niliwaambia huko Fresno, kwamba nilikuwa napigana katika raundi yangu ya mwisho. Kisha katika mikutano ile ya faragha, kazi ilikuwa ngumu zaidi kuliko kuzungumza hadharani, kwa sababu nililazimika kuwaambia mambo ya moja kwa moja na mazito kama nilivyopaswa kuwaambia. {VSSw 395.1}

Sasa sijui kama swali lako limejibiwa au la; labda limekuwa kama mahubiri marefu—limekuwa refu kiasi kwamba umepoteza hoja kuu.” {VSSw 395.2}

Mzee White: “Sasa nimekuwa nikijiuliza kama mtu mmoja ana haki ya kuunda mwenendo wake kwa kufuata uzoefu wa mtu mwingine. Nimejiuliza kama si wajibu wetu kuunda mwenendo wetu kulingana na uzoefu wetu wenyewe.” {VSSw 395.3}

Ellen White: “Naam, imekuwa hivi. Nimekuwa mgonjwa na katika maumivu; lakini nataka kuwaambia kwamba hakuna wakati ninapopanga kwenda kuzungumza mbele ya watu ambapo, kabla ya muda huo kufika, sipambani na changamoto kubwa sana moyoni au udhaifu fulani unaofanya ionekane kana kwamba haiwezekani kwangu kusimama mbele ya watu. Lakini mara tu ninaposimama mbele ya watu, nahisi kwa hakika kwamba malaika wa Mungu wako karibu nami kana kwamba nimefungua macho yangu na kuwaona, kama nilivyowaona wakati Kristo aliponiponya. Ninaondolewa kabisa katika hali yangu ya kawaida na kuinuliwa juu ya uwezo wangu wa kibinadamu. Nahisi kana kwamba hukumu iko mbele yangu; kana kwamba ulimwengu wote wa mbinguni unaniangalia, na kana kwamba nina mambo haya ya kusema ambayo lazima niyaambie hata kama nitakufa hapo hapo jukwaani. Siamini kwamba ni wajibu wa wengine kufanya hivyo. Na kila siku ninahisi hivyo. Ni kwa sababu uhalisia mkuu wa umilele umewekwa wazi mbele yangu, na mara tu ninaposimama kwa miguu yangu, uhalisia huo mkuu unaonekana kunizunguka kama vazi.” — *Manuscript 19b, 1890.* {VSSw 395.4}

Sauti, Kiasi cha Sauti, na Kasi ya Kuzungumza—Mzee Farnsworth aliuliza: “Dada White, je, hudhani kwamba wahudumu wetu wengi wamepata madhara makubwa kwa sababu ya namna yao ya kuzungumza?” {VSSw 396.1}

Ellen White akajibu: “Ndiyo, kwa kweli; nimeona jambo hilo mara nyingi. Mume wangu wakati fulani alikuwa na mazoea ya kuinua sauti yake kwa nguvu sana, na ilionekana kana kwamba hangeweza kuachana na mazoea hayo. Pia kuna ndugu mmoja huko Texas, Ndugu A, ambaye anajiweka katika hatari ya kufa kana kwamba amejichoma kisu kooni mwake. Tangu nilipokuja hapa, nimekuwa nikifikiria jambo hilo, na ni lazima nimwandikie.” {VSSsw 396.2}

Mzee Kilgore akasema: “Ameshakwisha kuambiwa kuhusu jambo hilo.” {VSSsw 397.1}

Mzee Farnsworth akaongeza: “Watu wa namna hiyo wapo katika karibu kila konferensi.” {VSSsw 397.2}

Ellen White akaendelea kusema: “Katika siku zangu za ujana nilikuwa nikizungumza kwa sauti kubwa mno. Bwana alinionesha kwamba singeweza kutoa mvuto unaofaa kwa watu kwa kuinua sauti yangu kufikia kiwango kisicho cha kawaida. Ndipo Kristo alionyeshwa mbele yangu, pamoja na namna Yake ya kuzungumza. Kulikuwa na utamu wa pekee katika sauti Yake. Sauti Yake, iliyokuwa laini na yenye utulivu, iliwafikia wale waliomsikiliza; maneno Yake yaliingia moyoni mwao, na waliweza kuelewa alichosema kabla hajaanza sentensi iliyofuata. Wengine huonekana kudhani kwamba lazima wazungumze kwa kasi sana, la sivyo watapoteza msukumo na watu nao watapoteza msukumo huo. Ikiwa huo ndio wanaouita msukumo, basi ni afadhali upotee, na kadiri unavyopotea haraka ndivyo inavyokuwa bora zaidi. {VSSsw 397.3}

Nilipoandika makala kuhusu jambo hili nilipokuwa St. Helena, nilihisi kwamba wahudumu wetu walikuwa wakidhoofika, na kulikuwa na sababu iliyosababisha hali hiyo.”— Manuscript 19b, 1890. {VSSsw 397.4}

Ujumbe Kutoka kwa Roho wa Mungu—Ninapozungumza na watu, mara nyingi husema mambo ambayo sikuwa nimeyapanga mapema. Mara kwa mara Roho wa Bwana hunijia juu yangu. Huonekana kana kwamba ninatolewa katika hali yangu ya kawaida na kuinuliwa juu ya uwezo wangu wa kawaida; maisha na tabia za watu mbalimbali huonyeshwa wazi mbele ya akili yangu. —Ninaona makosa yao na hatari zinazowakabili, na nahisi nalazimika kusema mambo hayo ninayoonyeshwa. — Shuhuda kwa Kanisa, Juzuu ya 5, uk. 678. {VSSsw 397.5}

Ufunuo Kupitia Maono—Kabla sijasimama mbele ya watu kuzungumza, sina wazo lolote kwamba nitasema kwa uwazi kiasi hicho. Lakini Roho wa Mungu hunijia juu yangu kwa nguvu, nami siwezi kujizuia kusema maneno ninayopewa. Sithubutu kuficha hata neno moja la ushuhuda huo. Nasema maneno ninayopewa na Nguvu iliyo kuu kuliko nguvu za kibinadamu, na hata nikitaka, siwezi kufuta au kurejesha nyuma hata sentensi moja. {VSSsw 398.1}

Wakati wa usiku, Bwana hunipa maagizo katika mifano, kisha hunieleza maana yake. Hunipa ujumbe, nami siwezi kukataa kuuwasilisha kwa watu. Upendo wa Kristo, na ninaweza kusema pia, upendo kwa roho za wanadamu, hunisukuma, nami siwezi kunyamaza. — *Manuscript 22, 1890.* {VSSsw 398.2}

Mume na Mke Kama Timu ya Wahubiri—Mwanzoni nilianza kazi ya kuzungumza hadharani kwa woga na mashaka. Ikiwa nilikuwa na ujasiri wowote, nilipokea kutoka kwa Roho Mtakatifu. Ikiwa nilizungumza kwa uhuru na nguvu, ilikuwa ni kwa msaada niliopewa na Mungu. Mikutano yetu kwa kawaida iliendeshwa kwa namna ambayo sisi sote wawili tulishiriki. Mume wangu alitoa mahubiri kuhusu mafundisho ya msingi ya imani, kisha mimi nilifuata kwa maonyo marefu yaliyogusa mioyo ya kusanyiko. Kwa hiyo, mume wangu alipanda mbegu ya kweli, nami nikamwagilia maji; lakini Mungu Ndiye aliyetoa ukuaji. — *Shuhuda kwa Kanisa, Juzuu ya 1, uk. 75.* {VSSsw 398.3}

Maisha ya Kristo na Suala la Afya—Jioni baada ya Sabato, nilizungumza tena mbele ya idadi kubwa ya watu. Jumapili kanisa la Methodist lilifunguliwa. Baba alihubiri asubuhi, nami nikazungumza mchana kuhusu maisha, mateso, na ufufuo wa Kristo. Tangazo lilitolewa kwamba jioni ningezungumza ukumbini kuhusu suala la afya. Kabla ya muda wa kuanza kufika, ukumbi ulikuwa umejaa kupita kiasi, na watu wengi walikuwa wamesimama nje kwa sababu hawakuweza kuingia. Tulijikaza kupita katika njia ya kuingilia, lakini baadhi ya watu walihofia kwamba sakafu ingeweza kubomoka. Watu waliokuwa na ujuzi walihakikisha kwamba hakukuwa na hatari yoyote. {VSSsw 398.4}

Baadhi walipendekeza watu waende kwenye kanisa la Methodist, ambalo lilikuwa limefunguliwa kwa ajili yao na lilikuwa na nafasi nzuri zaidi pamoja na hewa ya kutosha. Walieleza kwamba tayari kulikuwa na watu wengi huko. Mtu mmoja alipaza sauti akisema: “*Wagawanyeni wahubiri.*” Baba yako akajibu kwamba asingethubutu kujaribu jambo hilo, kwa sababu aliogopa kwamba angekosa

sehemu yake ya wasikilizaji. Hatimaye watu wote walihamia kwenye kanisa la mikutano, ambalo lilikuwa limejaa, na viti vya ziada vikaandaliwa. Nilikuwa na kusanyiko lenye heshima na umakini mkubwa. Nilizungumza kwa saa moja na nusu kwa uhuru, na mkutano ukamalizika vizuri. Tuna mkutano mwingine uliopangwa kwa usiku huu. Ombi letu ni kwamba Bwana aende pamoja nasi na kutusaidia katika kazi yetu. — *Letter 17, 1870.* {VSSsw 399.1}

Mahubiri Kuhusu Wakolosai 1:24–29—Ndugu D. T. Bourdeau alizungumza katika mkutano wa asubuhi. Mchana nilizungumza na watu kutoka katika **Wakolosai 1:24–29**. Nilihisi udhaifu mkubwa kabla ya kwenda madhabahuni. Kwa bidii kubwa nilimsihi Mungu katika maombi anisaidie na kuwabariki watu kwa namna ya pekee. Roho wa Bwana alitulia juu yangu na juu ya watu waliokuwa wakisikiliza. Baada yangu walifuata wakalimani watatu—wa Kijerumani, Kifaransa, na Kidenishi—lakini jambo hilo halikunisumbua hata kidogo. Malaika wa mbinguni walikuwa katikati yetu. Nilibarikiwa katika kuzungumza, nao watu walibarikiwa katika kusikiliza. Ninaona kwamba ujumbe wangu uliwafanya watu hawa wa mataifa mbalimbali waathirike zaidi kuliko hata ndugu na dada zangu Waamerika. {VSSsw 399.2}

Baada ya mahubiri, tulikuwa na mkutano wa thamani sana. Ndugu zetu wa mataifa yote walieleza kwamba walibarikiwa sana na walimshukuru Mungu kwa neno lililonenwa. — *Letter 23, 1885.* {VSSsw 400.1}

Ujumbe Kuhusu Mathayo 9:28–30—Mada yangu ilikuwa kutoka katika **Mathayo 9:28–30**. Wengi katika kusanyiko walikuwa wanaume na wanawake wenye akili na elimu. Niliwasilisha Kweli kwa urahisi kiasi kwamba wazee na vijana waliweza kuelewa. Hii ndiyo ilikuwa namna ya Kristo kufundisha. Aliwafundisha watu kwa lugha rahisi. Hakutumia maneno makubwa ambayo watu wasio na elimu wasingeweza kuyaelewa. Hata mtu asiye na elimu, pamoja na mtoto mdogo kabisa, angeweza kuelewa maneno Yake. {VSSsw 400.2}

Yesu alisema huko Nazareti: “*Roho wa Bwana yu juu Yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa*” (Luka 4:18) Ni wahudumu wangapi wanaodai kuwa ni wahudumu wa Kristo wanaofuata mfano huu wa Mwalimu wetu wa Mungu? — *Manuscript 55, 1886.* {VSS 400.3}

Kuhubiri Mfano wa Talanta—Kulikuwa kumepangwa nizungumze Jumamosi alasiri, tarehe 7 Januari; lakini nilipokuwa nikisafiri maili tano kwenda kwenye mkutano huo, nilikuwa katika hali ya uchovu mkubwa kiasi kwamba nilijawa na hofu na kutetemeka, huku nikikabiliwa na majaribu mbalimbali. Kwa kuangalia hali yangu, ilikuwa vigumu sana kwangu kuweza kuhubiri, hivyo niliomba katika safari yote. Niliposimama kwenye jukwaa, Bwana alinipa uhakikisho kwamba alikuwa amemtuma malaika Wake kunitia nguvu, na hivyo sikuweza kuwa na shaka. Maneno haya yalionekana kusemwa kwangu: *“Uwe hodari katika Bwana; naam, uwe hodari.”* Sikuwahi kamwe kuhubiri kwa urahisi na uhuru mkubwa namna hiyo, bila kuzuiwa na udhaifu wa mwili. Wasikilizaji walisema kwamba sauti yangu ilikuwa safi na yenye mvuto, na kusanyiko lote lilitambua kwamba Roho na nguvu za Mungu zilikuwa juu yangu. {VSSsw 400.4}

Nilihubiri kwa muda wa saa moja kuhusu mfano wa talanta, nikikazia kwa namna ya pekee habari ya mtumishi mvivu aliyeficha talanta yake moja ardhini na kisha akaleta mbele ya bwana wake akiwa na malalamiko makali, akimtuhumu Mungu kuwa ni Bwana mkali. Kupitia chombo cha udongo, Bwana alizungumza na mioyo ya watu ikaguswa. Baadhi yao waliguswa sana. Miongoni mwa waliokuwepo alikuwa mchungaji mmoja wa Kanisa la Uingereza, aliyekuwa ametoka Tasmania pamoja na Ndugu Baker na Rousseau, ambaye alikuwa ameanza hivi karibuni kushika Sabato. — *Letter 23a, 1893.* {VSSsw 401.1}

Busara na Utakatifu—Bwana anakaribia kufanya kazi kwa nguvu zaidi miongoni mwetu, lakini kuna hatari ya kuruhusu misukumo yetu itupeleke mahali ambapo Bwana hataki twende; kwa hiyo hatupaswi kuchukua hatua yoyote ambayo baadaye tutalazimika kuirudia nyuma. Tunapaswa kusonga mbele kwa utulivu, kwa busara na kwa tahadhari, bila kutumia maneno yaliyotiwa chumvi wala kuruhusu hisia zetu zichochewe kupita kiasi. Tunapaswa kufikiri kwa utulivu na kufanya kazi bila msisimko wa kupita kiasi, kwa sababu kutakuwa na watu ambao huchocheka kwa urahisi na ambao watashika maneno yasiyolindwa vizuri, kisha kuyatumia kutoa kauli kali zinazoweza kuleta msisimko na hivyo kuzuia kazi ileile ambayo Mungu angependa kufanya. {VSSsw 401.2}

Kuna kundi la watu ambao daima wako tayari kwenda upande mwingine uliopitiliza; wao hutafuta jambo geni, la kushangaza na jipya. Lakini Mungu anataka sisi sote tutembe kwa utulivu na kwa kufikiri, tukichagua maneno yetu kwa

kupatana na ukweli thabiti wa wakati huu. Ukweli huo unapaswa kuwasilishwa bila msisimko wa kihisia kadiri iwezekanavyo, huku ukiendelea kubeba uzito na utakatifu unaostahili. Kwa hiyo, tunapaswa kujilinda dhidi ya kuleta hali za kupita kiasi na dhidi ya kuwahamasisha wale wanaopenda kwenda ama katika moto au katika maji (hatari). — *Letter 37, 1894.* {VSS 402.1}

Somo Kutoka kwa Roho Mtakatifu kwa Tukio Maalumu—Jumapili, tarehe 23 Juni 1895, nilizungumza chini ya hema huko Canterbury. Mkutano mkuu ulikuwa umeandaliwa, na watu wengi wa kwetu walikuwa wamehudhuria kutoka Ashfield, Sydney na Petersham. Baadhi ya watu waliokuwa bado hawajaamua kikamilifu kutii waliguswa na ukweli. Nilipoingia madhabahuni, sikuweza kuielekeza akili yangu kwenye somo lolote la kuzungumzia; lakini niliposimama tu, kila jambo likawa wazi, na somo nililopewa lilikuwa swali la yule mwanasheria kwa Kristo: “*Nifanye nini ili nipate uzima wa milele?*” {VSS 402.2}

Nguvu ya Mungu ilinijia, na ukweli wa Mungu uliwasilishwa kupitia chombo chake cha kibinadamu kwa uwazi na nguvu kubwa. Mzee Corliss alisema kwamba alikuwa amenisikia nikizungumza katika karibu kila hali kwa miaka arobaini iliyopita, lakini kwamba hili lilikuwa hubiri lenye nguvu zaidi kuwahi kunisikia nikitoa. Nilionekana kuinuliwa na kutolewa nje ya nafsi yangu; ilikuwa Roho wa Bwana aliyenijia, na jina Lake ndilo linalopaswa kupewa utukufu. Katika barua yangu inayofuata kwako, nitakupa kiini cha yale yaliyosemwa. {VSS 403.1}

Baada ya mahubiri hayo, tulitumia karibu saa moja katika mkutano wa kijamii. Ushuhuda ulitolewa ulikuwa mzuri sana, na mkutano ulifungwa ukiwa umeacha athari nzuri katika mioyo ya wale waliokuwa bado wakisita katika uamuzi wao wa kuikubali Kweli. — *Letter 28, 1895.* {VSS 403.2}

Ujumbe Kuhusu Mtini Usiozaa Matunda—Nimetoka sasa kwenye ibada iliyofanyika chini ya hema. Leo nimezungumza mara mbili; kwanza kwa karibu saa moja katika mkutano wa asubuhi wa saa sita na nusu, na tena alasiri hii. Kwa kawaida huzungumza Jumatano alasiri kwa sababu ni siku ya mapumziko, lakini wiki hii nilikubali kuzungumza Jumanne kwa sababu ilikuwa siku ya sherehe ya Cup Day. Hema lilikuwa limejaa kabisa; viti vya ziada viliwekwa, na baadhi ya watu walilazimika kusimama. {VSS 403.3}

Nilizungumza kuhusu mtini usiozaa matunda, nikitumia mfano huo kwa makanisa yasiyozaa matunda. Bwana alinipa uhuru wa kuzungumza mbele ya kusanyiko hilo kubwa. Kulikuwa mbele yangu watu wenye nyuso zenye heshima, na wengi wao, wanaume kwa wanawake, walilia. Hakuna hata mmoja aliyeondoka mahali pake; wote walisikiliza kwa umakini mkubwa. Bwana alinipa ujumbe kwa ajili ya watu hao, na ninajua kwamba Roho Mtakatifu alifanya kazi katika akili na mioyo yao. Sijawahi kuona katika mikutano yetu ya kambi hamu kubwa namna hii ya kusikia ukweli. **{VSSsw 403.4}**

Tayari nimezungumza mara kumi na mbili kwa zaidi ya saa moja kila mara, pamoja na mahubiri mafupi kadhaa. Uwepo wa Bwana uko juu ya kambi hii, na mioyo mingi imeguswa. — *Letter 82, 1895.* **{VSSsw 404.1}**

SURA YA 64—NGUVU YA WIMBO

Njia ya Elimu—Historia ya nyimbo za Biblia imejaa mafundisho kuhusu matumizi na manufaa ya muziki na nyimbo. Mara nyingi muziki umepotoshwa ili kutumika kwa madhumuni maovu, na hivyo kuwa mojawapo ya vyombo vinavyovutia sana vya majaribu. Lakini unapotumiwa kwa usahihi, muziki ni zawadi ya thamani kutoka kwa Mungu, iliyokusudiwa kuinua mawazo kuelekea mambo ya juu na yenye heshima, na kuhamasisha pamoja na kuinua roho. **{VSSsw 407.1}**

Kama vile wana wa Israeli walivyokuwa wakisafiri jangwani na kutiwa moyo katika safari yao kwa muziki wa nyimbo takatifu, ndivyo Mungu anavyowaalika watoto Wake leo wafurahishe maisha yao ya hija kwa nyimbo. Kuna njia chache zenye ufanisi mkubwa kuliko kurudia Maneno ya Mungu kwa njia ya kuimba ili kuyatia moyoni na kuyafanya yakumbukwe. Nyimbo za aina hiyo zina nguvu kubwa: zinaweza kutuliza tabia zisizo na nidhamu na zisizokuzwa; zinaweza kuamsha fikira na kuchochea huruma; zinaweza kuleta umoja katika matendo na kuondoa huzuni pamoja na hofu zinazodhoofisha ujasiri na kupunguza bidii. **{VSSsw 407.2}**

Nyimbo ni mojawapo ya njia zenye ufanisi mkubwa zaidi za kuzikazia Kweli za kiroho moyoni. Mara nyingi, kwa roho iliyolemewa na shida na iliyo karibu kukata tamaa, kumbukumbu humrudishia neno fulani la Mungu—labda ujumbe uliosahaulika kwa muda mrefu kutoka katika wimbo wa utotoni—na hapo majaribu hupoteza nguvu yake; maisha hupata maana na kusudi jipya, na ujasiri pamoja na furaha huwasilishwa kwa roho nyingine. **{VSSsw 407.3}**

Thamani ya nyimbo kama njia ya elimu haipaswi kamwe kupuuzwa. Nyimbo tamu na safi ziimbwe katika nyumba, na matokeo yake yatakuwa kupungua kwa maneno ya lawama na kuongezeka kwa furaha, tumaini na shangwe. Nyimbo ziimbwe shuleni, na wanafunzi watafutwa karibu zaidi na Mungu, kwa walimu wao, na kwa wenzao. **{VSSsw 408.1}**

Katika ibada za kidini, kuimba ni tendo la ibada kama lilivyo ombi. Kwa hakika, nyimbo nyingi ni maombi. Mtoto akifundishwa kutambua jambo hili, atazingatia zaidi maana ya maneno anayoyaimba na atakuwa tayari zaidi kupokea nguvu yake ya kiroho. — *Elimu, uk. 167, 168. {VSSw 408.2}*

Kipawa cha Kuimba—Usiku mmoja nilionekana kuwa katika mkutano wa mashauri ambako mambo haya—yaani, mahali pa kutoa ujumbe wa onyo na mafundisho—yalikuwa yakijadiliwa. Ndipo mtu mmoja mwenye sura ya uzito na heshima akasema: “Mnamsihi Bwana awainue wanaume na wanawake wenye vipawa ili wajitoe kwa ajili ya kazi hii. Mna vipawa miongoni mwenu ambavyo vinahitaji kutambuliwa.” Mapendekezo kadhaa yenye hekima yalitolewa, kisha maneno yafuatayo yalisemwa kwa maana hii: “Ninawavutia kutambua kipawa cha kuimba ambacho kinapaswa kukuzwa; kwa maana sauti ya mwanadamu katika kuimba ni mojawapo ya vipawa ambavyo Mungu amevikabidhi ili vitumike kwa utukufu Wake. Adui wa haki anathamini sana kipawa hiki katika huduma yake. Kile ambacho ni zawadi kutoka kwa Mungu, kilichokusudiwa kuwa baraka kwa roho za watu, kimepotoshwa, kimetumiwa vibaya, na kimegeuzwa kutumikia kusudi la Shetani. Kipawa hiki cha sauti ni baraka kinapowekwa wakfu kwa Bwana ili kitumikie kazi Yake. _____ ana kipawa, lakini hakithaminiwi. Nafasi yake inapaswa kuzingatiwa, na kipawa chake kitawavuta watu, nao watausikia ujumbe wa kweli.” — *Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, uk. 497, 498. {VSS 408.3}*

Uhusiano Hai na Mungu—Lazima kuwe na uhusiano hai na Mungu katika maombi; vivyo hivyo lazima kuwe na uhusiano hai na Mungu katika nyimbo za sifa na shukrani. — *Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, uk. 498. {VSS 409.1}*

Kufundisha Ulimi Kumsifu Mungu—Ikiwa mmeketi pamoja na Kristo katika mambo ya mbinguni, hamwezi kujizuia kumtukuza Mungu. Anzeni kuuzoeza ulimi wenu katika kumsifu Yeye, na kuifundisha mioyo yenu kumwambia Mungu kwa nyimbo za shangwe; na yule mwovu anapoanza kuleta hali ya giza na kukatisha tamaa juu yenu, imbeni sifa kwa Mungu. — *In Heavenly Places, uk. 95. {VSS 409.2}*

Msaada Katika Kushinda Majaribu—Sifa na shukrani zionyeshe kwa njia ya nyimbo. Tunapojaribiwa, badala ya kutoa maneno yanayotokana na hisia zetu, kwa imani tuinulie Mungu wimbo wa shukrani. Wimbo ni silaha ambayo tunaweza kuitumia daima dhidi ya kuvunjika moyo. Tunapoufungua moyo wetu kwa mwanga wa uwepo wa Mwokozi, tutapata afya na baraka Zake. — *Huduma ya Uponyaji, uk. 254. {VSS 409.3}*

Njia ya Kupata Ushindi Dhidi ya Adui—Niliona kwamba tunapaswa kuinuka kila siku na kudumisha ushindi dhidi ya nguvu za giza. Mungu wetu ni mkuu. Niliona kwamba kuimba kwa utukufu wa Mungu mara nyingi humfukuza adui, na kumsifu Mungu humrudisha nyuma na kutupatia ushindi. — *Manuscript 5, 1850. {VSS 409.4}*

Matokeo ya Nyimbo Takatifu—Baraka kuu zimepokelewa na wanadamu kwa kuitikia nyimbo za sifa. Ni mara ngapi katika uzoefu wa kiroho historia hii hurudiwa! Ni mara ngapi kupitia maneno ya nyimbo takatifu vyanzo vya toba na imani, tumaini, upendo na furaha hufunguliwa ndani ya moyo! — *Elimu, uk. 162. {VSS 410.1}*

Njia ya Kufanya Kazi Kuwa Ya Kufurahisha—Fanyeni kazi zenu ziwe za kufurahisha kwa kuziambatanisha na nyimbo za sifa. — *Mwongozo wa Malezi kwa Wazazi na Mtoto, uk. 148. {VSS 410.2}*

Wimbo Katika Nyumba—Asubuhi na jioni shirikianeni na watoto wenu katika ibada ya Mungu, mkisoma Neno Lake na kuimba sifa Zake. Wafundisheni kurudia sheria ya Mungu. Kuhusu amri hizo, wana wa Israeli waliagizwa: *“nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo.”* (Kumbukumbu la Torati 6:7) Kwa kufuata maagizo hayo, Musa aliwaelekeza wana wa Israeli kuweka maneno ya sheria katika mfumo wa nyimbo. **{VSS 410.3}**

Ikiwa ilikuwa muhimu kwa Musa kuyaweka maagizo ya Mungu katika nyimbo takatifu, ili watoto walipokuwa wakisafiri jangwani waweze kujifunza kuimba sheria hiyo mstari kwa mstari, basi ni muhimu kiasi gani wakati huu kuwafundisha watoto wetu Neno la Mungu! Tushirikiane katika kazi ya Bwana kwa kuwafundisha

watoto wetu kuzishika amri kwa uaminifu kamili. Tufanye kila tuwezalo ili nyimbo za sifa zisikike katika nyumba zetu, ili Mungu aweze kuja na kukaa nasi. — *Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, uk. 499. {VSS 410.4}*

Umoja wa Familia Katika Wimbo—Heri baba na mama wanaoweza kuwafundisha watoto wao Neno la Mungu lililoandikwa kwa kutumia vielelezo kutoka katika kurasa zilizo wazi za kitabu cha asili; wanaoweza kukusanyika chini ya miti yenye majani mabichi, katika hewa safi na yenye afya, ili kujifunza Neno la Mungu na kuimba sifa za Baba aliye juu. Kupitia ushirika wa namna hiyo, wazazi wanaweza kuwavuta watoto wao karibu na mioyo yao, na hivyo kuwaunganisha na Mungu kwa vifungo visivyoweza kuvunjika kamwe. — *Elimu, uk. 251. {VSS 411.1}*

Nyimbo za Watoto—Ibada ziwe fupi na zenye uhai, zilingane na tukio husika, na zibadilishwe mara kwa mara. Wote washiriki katika kusoma Biblia, wajifunze na kurudia mara nyingi sheria ya Mungu. Watoto watavutiwa zaidi ikiwa wakati mwingine wataruhusiwa kuchagua sehemu ya kusoma. Waulizeni maswali kuhusu walichosoma, na waruhusuni nao waulize maswali. Taja jambo lolote litakalosaidia kueleza maana yake. Ibada inapokuwa haijafanywa ndefu kupita kiasi, watoto wadogo washiriki katika maombi, na washiriki pia katika kuimba, hata kama ni mstari mmoja tu wa wimbo. — *Mwongozo wa Malezi kwa Wazazi na Mtoto, uk. 522. {VSS 411.2}*

SURA YA 65—UIMBAJI WA KRISTO

Kristo—Mshindi Juu ya Majaribu Katika Utoto Wake—Kristo alipokuwa mtoto kama watoto wengine hapa, alijaribiwa kutenda dhambi, lakini hakushindwa na majaribu hayo. Alipokuwa akikua, alijaribiwa pia, lakini nyimbo ambazo mama yake alikuwa amemfundisha kuziimba zilimjia akilini mwake, naye aliinua sauti yake katika sifa. Kabla wenzake hawajatambua kilichokuwa kimetokea, nao walikuwa wakiimba pamoja naye. Mungu anataka tutumie kila uwezo ambao Mbingu imetupatia ili kumpinga adui. — *Manuscript 65, 1901*. {VSS 412.1}

Kwa wimbo, Yesu katika maisha yake duniani alikabiliana na majaribu. Mara nyingi, wakati maneno makali na yenye kuumiza yaliposemwa dhidi yake, na wakati mazingira yaliyomzunguka yalipojaa huzuni, kutoridhika, mashaka au hofu yenye kukandamiza, sauti yake ilisikiwa ikiimba wimbo wa imani na furaha takatifu. — *Elimu, 166*. {VSS 412.2}

Kristo alishuka katika umaskini ili kutufundisha jinsi tunavyoweza kutembea kwa ukaribu na Mungu katika maisha yetu ya kila siku. Alitwaa asili ya kibinadamu ili aweze kuwahurumia mioyo yote. Aliweza kushiriki katika kazi ngumu, kubeba sehemu yake ya jukumu la kuitunza familia katika mahitaji yao, kuzoea uchovu, na bado hakuonyesha kukosa subira. Roho yake haikuwahi kujazwa sana na mahangaiko ya kidunia kiasi cha kukosa muda au mawazo kwa mambo ya mbinguni. Mara nyingi aliwasiliana na Mbingu kwa njia ya nyimbo. Watu wa Nazareti mara nyingi walisikia sauti yake ikiinuliwa katika maombi na shukrani kwa Mungu; na wale waliokuwa wakishirikiana naye, ambao mara nyingi walilalamika kwa sababu ya uchovu wao, walitiwa moyo na sauti tamu ya nyimbo iliyotoka katika midomo yake. — *The Review and Herald, October 24, 1899*. {VSS 412.3}

Mwanzoni mwa Siku—Asubuhi na mapema mara nyingi ilimkuta Yesu akiwa mahali pa faragha, akitafakari, akichunguza Maandiko, au akiomba. Kwa sauti ya kuimba aliukaribisha mwanga wa asubuhi. Kwa nyimbo za shukrani aliimarisha saa zake za kazi na kuwaletea furaha ya mbinguni wale waliokuwa wamechoka na waliokata tamaa.— *Huduma ya Uponyaji, 52*. {VSS 413.1}

Mara nyingi alionyesha furaha ya moyo Wake kwa kuimba zaburi na nyimbo za mbinguni. Mara nyingi wakaaji wa Nazareti walisikia sauti Yake ikiinuliwa katika sifa na shukrani kwa Mungu. Alifanya ushirika na Mbingu kupitia nyimbo; na

Nhandi Masunga na Grace Momadi Masaka-Jersey 2026 July

wenzake walipolalamika kwa uchovu uliotokana na kazi, walifarijika kwa sauti tamu iliyotoka katika midomo Yake. Sifa Zake zilionekana kuwafukuza malaika waovu na, kama uvumba wenye harufu nzuri, zilijaza mahali hapo manukato ya kiroho. Akili za wasikilizaji Wake zilihamishwa kutoka katika utumwa wa kidunia na kuelekezwa kwenye makao ya mbinguni. — *Tumaini la Vizazi Vyote*, 73, 74. {VSS 413.2}

SURA YA 66—MAFUNZO YA SAUTI NA UIMBAJI

Somo la Kila Shule—Ninafurahi kwamba kipengele cha muziki kimejumuishwa katika Shule ya Healdsburg. Katika kila shule, mafundisho ya uimbaji yanahitajika

sana. Kunapaswa kuwa na shauku kubwa zaidi katika mafunzo ya sauti kuliko inavyoonekana kwa ujumla sasa. Wanafunzi ambao wamejifunza kuimba nyimbo tamu za injili kwa sauti yenye mvuto, ulinganifu mzuri wa sauti na matamshi yaliyo wazi, wanaweza kufanya kazi kubwa kama wainjilisti wa nyimbo. Watapata fursa nyingi za kutumia kipawa ambacho Mungu amewapa, wakipeleka nyimbo na mwanga wa tumaini katika maeneo mengi ya upweke yaliyotiwa giza na dhambi, huzuni na mateso, wakiwambia wale ambao mara chache hupata fursa ya kushiriki ibada za kanisani. — *The Review and Herald, August 27, 1903.* {VSS 414.1}

Mpangilio Sahihi wa Sauti na Matamshi—Hakuna maneno yanayoweza kueleza kikamilifu baraka kuu inayopatikana katika ibada ya kweli. Wanadamu wanapoimba kwa roho na kwa ufahamu, wanamuziki wa mbinguni huunganisha sauti zao pamoja nao katika wimbo wa shukrani. Yeye ambaye ametupatia vipawa vyote vinavyotuwezesha kuwa watenda kazi pamoja na Mungu, anatarajia watumishi wake kuzilea sauti zao ili waweze kusema na kuimba kwa namna ambayo wote wanaweza kuelewa. Kinachohitajika si uimbaji wa sauti kubwa, bali ni upangaji sahihi wa sauti, matamshi yaliyo sahihi na usemi ulio wazi. Kila mmoja atenge muda wa kuiratibu/kuipalilia/kuilea sauti yake ili sifa za Mungu ziimbwe kwa sauti laini, safi na yenye mvuto, wala si kwa ukali na mlio mkali unaoudhi masikio. Uwezo wa kuimba ni kipawa kutoka kwa Mungu; kwa hiyo, utumike kwa utukufu Wake. — *Shuhuda kwa Kanisa, 9:143, 144.* {VSS 414.2}

Uzuri, Hisia na Nguvu—Muziki unaweza kuwa nguvu kubwa kwa ajili ya mema; hata hivyo, hatutumii kikamilifu sehemu hii ya ibada. Mara nyingi uimbaji hufanywa kwa msukumo wa ghafla au kwa ajili ya matukio maalumu, na wakati mwingine waimbaji huachwa waendeleo bila mpangilio au mwongozo unaofaa; hivyo muziki hupoteza athari yake inayostahili katika mioyo ya wale waliopo. Muziki unapaswa kuwa na uzuri, hisia na nguvu. Sauti ziinuliwe katika nyimbo za sifa na ibada. Ikiwezekana, tumieni msaada wa ala za muziki, na acha maelewano matukufu ya sauti yapae kwa Mungu kama sadaka inayokubalika. {VSS 415.1}

Lakini wakati mwingine ni vigumu zaidi kuwaadibisha waimbaji na kuwaweka katika mpangilio wa kazi kuliko kuboresha mazoea ya kuomba na kutoa mahubiri. Wengi wanataka kufanya mambo kwa mtindo wao wenyewe; wanapinga mashauriano na hawana subira wanapoongozwa. Mipango iliyokomaa vizuri

inahitajika katika huduma ya Mungu. Busara ya kawaida ni jambo la thamani katika ibada ya Bwana. — *Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti* 505. {VSS 415.2}

Sifa za Uimbaji Bora—Maboresho makubwa yanaweza kufanywa katika uimbaji. Baadhi ya watu hudhani kwamba kadiri wanavyoimba kwa sauti kubwa ndivyo wanavyotengeneza muziki bora zaidi; lakini kelele si muziki. Uimbaji mzuri unafanana na sauti ya ndege—ni wa upole na wenye miondoko mizuri ya sauti. {VSS 415.3}

Katika baadhi ya makanisa yetu nimesikia nyimbo za solo ambazo hazikufaa kabisa kwa ibada katika nyumba ya Bwana. Mivutano mirefu ya sauti na sauti za pekee zinazotumiwa katika uimbaji wa kimuziki wa jukwaani hazipendezi kwa malaika. Malaika hufurahia kusikia nyimbo rahisi za sifa zikiimbwa kwa sauti ya kawaida na ya asili. Nyimbo ambazo kila neno hutamkwa kwa uwazi, kwa sauti yenye upatanifu wa muziki, ndizo nyimbo ambazo malaika hujiunga nasi kuziimba. Wao hushiriki katika kiitikio kinachoimbwa kutoka moyoni kwa roho na ufahamu. — *Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, uk. 510*. {VSS 416.1}

Heshima na Kicho—Muziki wa wimbo, unaotolewa kutoka katika mioyo mingi kwa matamshi yaliyo wazi na dhahiri, ni mojawapo ya vyombo vya Mungu katika kazi ya kuokoa roho. Ibada yote inapaswa kufanywa kwa heshima na kicho, kana kwamba tuko mbele ya Bwana wa kusanyiko kwa namna inayoonekana. — *Shuhuda kwa Kanisa 5:493*. {VSS 416.2}

Muziki Kama Sehemu ya Ibada ya Mungu Mbinguni—Muziki ni sehemu ya ibada ya Mungu katika nyua za mbinguni. Tunapaswa kujitahidi katika nyimbo zetu za sifa kumkaribia Mungu kadiri iwezekanavyo kwa upatanifu wa wimbaji wa mbinguni. Mara nyingi nimehuzunika kusikia sauti zisizofundishwa vizuri, zilizopandishwa hadi kwenye kiwango cha juu kabisa, zikilia kwa nguvu maneno matakatifu ya baadhi ya nyimbo za sifa. Ni jambo lisilofaa jinsi gani sauti hizo kali na zinazokera kwa ibada takatifu na yenye furaha ya Mungu! Natamani kuziba

masikio yangu au kuondoka mahali hapo, nami hufurahi pale zoezi hilo linaloumiza linapomalizika. —*Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilist*, uk. 507, 508. {VSS 416.3}

SURA YA 67—MATUMIZI MABAYA YA SAUTI KATIKA MUZIKI

Vurugu za Kelele *Bedlam of Noise-Kelele kama za wendawazimu*—Mambo ambayo umeeleza kuhusu yaliyotokea Indiana, Bwana amenionyesha kwamba mambo kama hayo yangetokea karibu na kufungwa kwa muda wa rehema. Kila jambo lisilo na adabu na lisilo na mpangilio lingeonyeshwa wazi. Kungekuwa na makelele, mapigo ya ngoma, muziki na dansi. {VSS 417.1}

Uwezo wa kufikiri wa viumbe wenye akili ungechanganyikiwa kiasi kwamba wasingeweza tena kutegemewa kufanya maamuzi sahihi. Hali hiyo ingeitwa kuwa ni kazi ya Roho Mtakatifu. {VSS 417.2}

Roho Mtakatifu hajidhihirishi kamwe katika njia kama hizo wala katika vurugu hiyo ya kelele. Hii ni mbinu iliyobuniwa na Shetani ili kuficha hila zake za werevu za kuifanya Kweli safi, ya dhati, yenye kuinua, inayotukuza na kuitakasa mioyo kwa ujumbe wa wakati huu ionekane haina nguvu. Ni afadhali ibada ya Mungu isiunganishwe kabisa na muziki kuliko kutumia vyombo vya muziki kufanya kazi ambayo nilionyesha Januari iliyopita kwamba ingeletwa katika mikutano yetu mikubwa. Ukweli wa wakati huu hauhitaji mambo ya aina hiyo katika kazi ya kuongoa roho. Vurugu ya kelele hutikisa hisia na kupotosha jambo ambalo, likiongozwa kwa usahihi, lingeweza kuwa baraka. Nguvu za kishetani huungana na makelele na vurugu hizo zinazofanana na zile za wacheza dansi na wanywa pombe ili kuleta hali ya sherehe isiyo ya kiroho, na hali hiyo huitwa kuwa ni kazi ya Roho Mtakatifu [carnival au reverly]. {VSS 417.3}

Hakuna mtu anayepaswa kutiwa moyo wa kushiriki katika aina hii ya ibada. Ushawishi wa aina hiyo hiyo ulionekana baada ya kupita kwa mwaka 1844. Maonyesho kama hayo yalifanyika tena; watu walisimka na kuchochewa na nguvu waliyoidhani kuwa ilikuwa nguvu ya Mungu. —*Jumbe Teule* 2:36, 37. {VSS 418.1}

Mtego wa Shetani—Roho Mtakatifu hahusiki na mkanganyiko wa kelele na mchanganyiko wa sauti nyingi kama ule nilioonyeshwa Januari iliyopita. Shetani hufanya kazi katikati ya vurugu na makelele ya muziki huo ambao, ukiendeshwa

kwa usahihi, ungekuwa sifa na utukufu kwa Mungu. Adui hufanya athari yake kuwa kama sumu ya kuumwa na nyoka. {VSS 418.2}

Mambo yaliyotokea zamani yatatokea tena wakati ujao. Shetani ataugeuza muziki kuwa mtego kupitia namna unavyotumiwa. — *Jumbe Teule* 2:37, 38. {VSS 418.3}

Nyimbo Zinazowafanya Malaika Walie—Kumekuwa na aina ya mikusanyiko ya kijamii yenye tabia tofauti kabisa; mikusanyiko ya starehe ambayo imekuwa aibu kwa taasisi zetu na kwa kanisa. Mikusanyiko hiyo imekuwa ikichochea kiburi cha mavazi, kiburi cha mwonekano, kujifurahisha nafsi, vicheko vya kupita kiasi na mambo yasiyo na maana. Shetani hupokelewa humo kama mgeni wa heshima, naye huwatawala wale wanaoshiriki katika mikusanyiko hiyo. {VSSsw 418.4}

Nilionyeshwa tukio la kundi moja kama hilo, ambapo walikuwa wamekusanyika watu waliodai kuamini ukweli. Mmoja alikuwa ameketi kwenye chombo cha muziki, na nyimbo zilizokuwa zikiimbwa ziliwafanya malaika waliokuwa wakitazama wahuzunike na kulia. Kulikuwa na furaha, vicheko vya hovy ovyo, msisimko mwingi na aina fulani ya hali ya kuchochewa; lakini furaha hiyo ilikuwa ile ambayo Shetani pekee anaweza kuizalisha. Huu ni msisimko na upotovu wa akili ambao wote wanaompenda Mungu wanguonea aibu. Huwatayarisha washiriki wake kwa mawazo na matendo yasiyo matakatifu. Nina sababu ya kuamini kwamba baadhi ya wale walioshiriki katika tukio hilo walitubu kwa dhati baada ya kutambua aibu ya tendo na maonyesho hayo. — **Mashauri kwa Wazazi, Walimu na Wanafunzi**, *uk. 339*. {VSS 418.5}

Nyimbo za Kujifurahisha na Muziki Maarufu—Ninaingiwa na hofu ninapoonza kila mahali hali ya kujifurahisha isiyo na maana miongoni mwa vijana wanaodai kuamini Ukweli. Mungu haonekani kuwa katika mawazo yao. Akili zao zimejaa mambo yasiyo na maana, na mazungumzo yao yamekuwa maneno matupu na ya batili. Wana uwezo mkubwa wa kupendezwa na muziki, na Shetani anajua ni sehemu

zipi za akili anazopaswa kuchochea ili kuzihuisha, kuzishika na kuzivutia, kiasi kwamba Kristo hatamaniwi tena. Hamu ya kiroho ya nafsi ya kupata maarifa ya Mungu na kukua katika neema haipo. **{VSS 419.1}**

Nilionyesha kwamba vijana wanapaswa kuchukua msimamo wa juu zaidi na kulifanya Neno la Mungu kuwa mshauri na kiongozi wao. Majukumu makubwa yapo juu yao, lakini wanayachukulia kwa wepesi. Kuingizwa kwa muziki katika nyumba zao, badala ya kuwachochea kuwa watakatifu na wenye hali ya kiroho, kumekuwa njia ya kugeuza mawazo yao kutoka katika ukweli. Nyimbo zisizo na maana na muziki maarufu wa siku hizi huonekana kuwavutia. Vyombo vya muziki vimechukua muda ambao ulipaswa kutengwa kwa ajili ya maombi. **{VSS 419.2}**

Muziki, unapotumiwa kwa usahihi, ni baraka kubwa; lakini unapotumiwa vibaya, huwa laana yenye madhara makubwa. Huchochea hisia, lakini hauleti nguvu wala ujasiri ambao Mkristo anaweza kuupata mbele ya kiti cha neema pekee, anapomweleza Mungu mahitaji yake kwa unyenyekevu na kumwomba kwa machozi na maombi ya dhiti nguvu za mbinguni ili aimarishwe dhidi ya majaribu makali ya yule mwovu. Shetani anawateka vijana. Ni jambo gani linaweza kusemwa ili kuwasaidia kuvunja nguvu ya mvuto wake wa udanganyifu? Yeye ni mshawishi mwenye ustadi, anayewavuta kuelekea upotevu. — *Shuhuda kwa Kanisa 1:496, 497.* **{VSS 420.1}**

Ibada ya Muziki Kama Sanamu—Mambo ya milele yana uzito mdogo sana katika mawazo ya vijana. Malaika wa Mungu hulika machozi wanapoandika katika kumbukumbu maneno na matendo ya Wakristo wanaodai kumfuata Kristo. Malaika walikuwa wameizunguka nyumba ile. Vijana walikuwa wamekusanyika humo, na kulisikika sauti za muziki wa kuimba na wa vyombo. Wakristo walikuwa wamekusanyika hapo, lakini walikuwa wakisikiliza nini? Walikuwa wakisikiliza wimbo wa kijinga unaofaa ukumbi wa dansi. Tazameni malaika watakatifu wakikusanya nuru yao kwa karibu zaidi, na giza likiwafunika wale waliomo ndani ya nyumba hiyo. Malaika waliondoka mahali hapo. Huzuni ilionekana katika nyuso zao; walikuwa wakilia. Nimeona jambo hili likirudiwa mara nyingi katika makundi ya washika Sabato, hasa katika sehemu fulani. **{VSS 420.2}**

Muziki umechukua muda ambao ulipaswa kutengwa kwa ajili ya maombi. Muziki umekuwa sanamu ambayo baadhi ya Wakristo wanaodai kushika Sabato

huiabudu. Shetani hana pingamizi dhidi ya muziki ikiwa anaweza kuufanya kuwa njia ya kuingia katika akili za vijana. **{VSS 420.3}**

Kitu chochote kinachoweza kuondoa mawazo kwa Mungu na kutumia muda ambao ulipaswa kutolewa kwa huduma yake kitamtosheleza. Hutumia njia zenye ushawishi mkubwa zaidi kuwashikilia watu wengi katika hali ya kujidanganya yenye kupendeza, huku wakiwa wamepooza na nguvu zake. **{VSS 421.1}**

Muziki unapotumiwa vizuri ni baraka; lakini mara nyingi hufanywa kuwa mojawapo ya njia zinazovutia zaidi za Shetani za kunasa roho. Unapotumiwa vibaya, huwaongoza wale wasiotakaswa kwenye kiburi, majivuno na upumbavu. Unaporuhusiwa kuchukua nafasi ya ibada na maombi, huwa laana kubwa. **{VSS 421.2}**

Vijana hukusanyika ili kuimba, na, ingawa wanajitambulisha kuwa Wakristo, mara nyingi humvunjia Mungu heshima na kuidhalilisha imani yao kwa mazungumzo yao ya kipuuzi na uchaguzi wao wa muziki. Muziki mtakatifu hauendani na ladha yao. Nilielekezwa kwenye mafundisho yaliyo wazi ya Neno la Mungu, ambayo yamepuuzwa. Katika hukumu, maneno haya yote ya uvuvio yatawalaani wale ambao hawajayazingatia.—[Shuhuda kwa Kanisa 1:505, 506.](#) **{VSS 421.3}**

Starehe Zilizokatazwa—Ni tofauti kubwa jinsi gani kati ya matumizi ya muziki zamani na matumizi ambayo mara nyingi hufanywa leo! Ni wangapi wanaotumia kipawa hiki kujitukuza badala ya kumtukuza Mungu! Upendo wa muziki huwaongoza watu wasio waangalifu kuungana na wapenda dunia katika mikusanyiko ya starehe ambayo Mungu amekataza watoto Wake kwenda. Hivyo, kile ambacho ni baraka kubwa kinapotumiwa kwa usahihi huwa mojawapo ya njia zenye mafanikio makubwa ambazo Shetani hutumia kuigeuza akili kutoka katika wajibu na kuitoa katika kutafakari mambo ya milele. — *Wazee wa Imani na Manabii, uk. 594.* **{VSS 421.4}**

Tamaa ya Kujionyeshwa—Burudani za muziki ambazo, zikiendeshwa kwa usahihi, hazina madhara yoyote, mara nyingi huwa chanzo cha uovu. Katika hali ya sasa ya jamii, ambapo maadili yameshuka si tu miongoni mwa vijana bali pia miongoni mwa watu wazima wenye uzoefu, kuna hatari kubwa ya kuwa wazembe, kuwapa watu fulani upendeleo maalumu, na hivyo kusababisha husuda, wivu na mashaka mabaya.

Mara nyingi kipaji cha muziki huchochea kiburi na tamaa ya kujionyesha, na waimbaji huwa hawazingatii kwa kina ibada ya Mungu. Badala ya kuongoza mawazo ya watu kumkumbuka Mungu, mara nyingi husababisha wamsahau.

—[Letter 6a, 1890](#) {VSS 422.1}

Ushauri kwa Viongozi wa Muziki—Nilionyesha baadhi ya mazoezi yenu ya uimbaji, na nikawezeshwa kutambua hali za mioyo iliyokuwa miongoni mwa kundi hilo, huku wewe ukiwa kiongozi mkuu. Kulikuwa na wivu mdogo, husuda, mashaka mabaya na kusema vibaya juu ya wengine. Mungu anahitaji ibada inayotoka moyoni; ibada ya maumbo ya nje na huduma ya midomo pekee ni kama shaba iliayo na upatu uvumao. Uimbaji wenu unalenga kujionyesha badala ya kumsifu Mungu kwa roho na ufahamu. Hali ya moyo ndiyo inayofunua ubora wa dini ya mtu anayekiri kuwa mcha Mungu. —[Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, 507](#) {VSS 422.2}

Chaguo la Mungu Kuhusu Uimbaji—Uimbaji ni sehemu ya ibada ya Mungu katika mikutano ya kidini kama vile mahubiri yalivyo. Jambo lolote lisilo la kawaida au la kipekee linalokuzwa katika uimbaji huvuta mawazo ya watu na kuharibu hali ya uzito na utakatifu ambayo inapaswa kuambatana na muziki mtakatifu. Kitu chochote cha ajabu au kisicho cha kawaida katika uimbaji hupunguza uzito na utakatifu wa ibada ya kidini. {VSS 422.3}

Mazoezi ya mwili yafaa kidogo [Bodily exercise. Kila jambo linalohusiana kwa namna yoyote na ibada ya kidini linapaswa kuwa lenye heshima, lenye uzito, na lenye kuvutia kwa namna ya kutia kicho. Mungu hafurahishwi wakati wahudumu wanaodai kuwa wawakilishi wa Kristo wanapomwakilisha Kristo vibaya kwa kutumia vitendo vya ishara visivyofaa, ishara zisizo na staha na vitendo visivyo vya heshima. Mambo hayo huwafurahisha watazamaji wanaotafuta mambo ya ajabu, lakini hayainui akili wala mioyo ya wale wanaoyaona. {VSS 423.1}

Vivyo hivyo ndivyo ilivyo katika uimbaji. Baadhi ya waimbaji hutumia nguvu nyingi na kuinua sauti kupita kiasi. Sauti kali na yenye kelele huzifunika sauti laini na zenye mvuto zaidi. Jitihada hizo za mwili na sauti kali hazileti uzuri wa muziki

kwa wanaosikiliza duniani wala mbinguni. Uimbaji huo una kasoro na haukubaliki mbele za Mungu kama sauti laini, tamu na zilizosawazika za muziki zinavyokubalika. Hakuna maonyesho ya namna hiyo miongoni mwa kwaya za malaika. Nyimbo zao hazichoshi masikio; ni laini, zenye kupendeza na hutolewa bila kulazimisha nguvu za mwili.—[Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, 507](#) {VSS 423.2}

Ndugu S. hajui ni kwa kiasi gani watu wengi hushangazwa na kuchukizwa na mwenendo wake. Wengine hushindwa kujizuia kuwa na mawazo yasiyo matakatifu na hisia za mzaha wanapooona miondoko isiyo na ustaarabu inayofanywa wakati wa kuimba. Ndugu S. hujionyesha mwenyewe kupitia namna yake ya kuimba. Uimbaji wake hauna ushawishi wa kuituliza mioyo wala kugusa hisia za wasikilizaji. Wengi wamehudhuria mikutano na kusikiliza maneno ya Kweli yaliyohubiriwa madhabahuni, ambayo yamewagusa na kuwafanya wawe na hali ya unyenyekevu na tafakari; lakini mara nyingi namna ambavyo uimbaji umeendeshwa haijaongeza nguvu wala kuimarisha mvuto wa ujumbe uliowasilishwa. Miondoko ya mwili, kujikunja-jikunja, na jitihada za kulazimisha sauti zimeonekana kuwa hazifai kabisa kwa nyumba ya Mungu; zimekuwa kama jambo la kuchekesha, kiasi kwamba zimeondoa athari nzito iliyokuwa imejengwa katika akili za wasikilizaji. Wale wanaoamini Lweli hawaheshimiwi tena kama ilivyokuwa hapo awali, tangu kuanza kwa uimbaji.... {VSS 424.1}

Ndugu S. amefikiri kwamba kuimba ndiyo kazi kuu kuliko zote zinazopaswa kufanywa duniani, na kwamba namna yake ya kuimba ni kubwa na ya kuvutia sana. {VSS 424.2}

Uimbaji wako haupendezi hata kidogo kwa kwaya ya malaika. Hebu jifikirie ukiwa umesimama pamoja na kundi la malaika, ukiinua mabega yako, ukisisitiza maneno kwa nguvu, ukitikisa mwili wako, na kutumia sauti yako kwa kiwango cha juu kabisa. Ni aina gani ya tamasha na upatanifu ambao ungepatikana mbele ya malaika kwa maonyesho kama hayo? —[Manuscript 5, 1874](#). {VSS 424.3}

Muziki una asili ya mbinguni. Kuna nguvu kubwa ndani ya muziki. Ilikuwa muziki wa makundi ya malaika uliogusa mioyo ya wachungaji katika nyanda za Bethlehemu na kusambaa duniani kote. Kupitia muziki ndipo sifa zetu zinapanda

kwenda Kwake ambaye ni mfano kamili wa usafi na upatanifu. Ni kwa muziki na nyimbo za ushindi ndipo waliokombolewa watakapoingia hatimaye katika taji/thawabu isiyoharibika. {VSS 424.4}

Kuna jambo la pekee lenye utakatifu katika sauti ya mwanadamu. Upatanifu wake, pamoja na hisia zake tulivu na zenye msukumo wa mbinguni, huzidi kila chombo kingine cha muziki. Muziki wa maneno yanayotoka mdomoni ni mojawapo ya zawadi za Mungu kwa wanadamu; ni chombo kisichoweza kuzidiwa wala kulinganishwa wakati upendo wa Mungu unapojaza nafsi. Kuimba kwa roho na kwa ufahamu pia ni nyongeza kubwa katika ibada za kiroho katika nyumba ya Mungu. {VSS 425.1}

Lakini zawadi hii imechafuliwa namna gani! Ikiwa ingetakaswa na kusafishwa, ingefanya mema makubwa kwa kuvunja vizuizi vya chuki, ubaguzi na mioyo migumu isiyuamini; na ingekuwa njia ya kuleta roho kwa Kristo. Haitoshi tu kuelewa misingi ya uimbaji; bali pamoja na ufahamu na maarifa, lazima kuwepo na uhusiano wa karibu na mbingu kiasi kwamba malaika waweze kuimba kupitia sisi. {VSSw 425.2}

Sauti yako imesikika kanisani ikiwa kubwa sana na kali, ikiambatana na miondoko ya mwili isiyokuwa yenye uzuri wa heshima, kiasi kwamba sauti laini na tamu zaidi, zinazofanana na muziki wa malaika, hazikusikika. Umeimba zaidi kwa ajili ya wanadamu kuliko kwa ajili ya Mungu. {VSSw 425.3}

Kwa kuwa umeiinua sauti yako kwa nguvu kuliko kusanyiko lote, umeonekana kujali zaidi sifa na kuvutiwa na watu. Kwa kweli ulikuwa na mawazo makubwa kuhusu kipawa chako cha kuimba kiasi kwamba ulifikiria hata kwamba ulipaswa kulipwa kwa kutumia kipawa hicho. —[Manuscript 5, 1874](#). {VSSw 425.4}

Mwelekeo wa Kupindukia Katika Uimbaji—Uimbaji haupaswi kuruhusiwa kuondoa mawazo ya watu katika saa za ibada. Ikiwa kuna jambo linalopaswa kupuuzwa, basi iwe ni uimbaji. Mojawapo ya majaribu makubwa ya kizazi hiki ni kuyapa mazoezi ya muziki nafasi kubwa kupita kiasi, kiasi kwamba muziki unathaminiwa zaidi kuliko maombi. Roho nyingi zimepotea katika jambo hili. Wakati Roho wa Mungu anapoamsha dhamiri na kumshawishi mtu kuhusu dhambi, Shetani huleta wazo la kufanya mazoezi ya kuimba au kuanzisha shule za uimbaji

ambazo, zikiendeshwa kwa namna ya mzaha na kutokuwa na uzito, huondoa hali ya unyenyekevu na kuzima tamaa ya kuwa na Roho wa Mungu. Kwa njia hiyo, mlango wa moyo ambao ulikuwa karibu kufunguliwa kwa ajili ya Yesu hufungwa na kuzuiwa na kiburi na ukaidi; na mara nyingi haufunguki tena. {VSSw 426.1}

Kwa sababu ya majaribu yanayoambatana na mazoezi haya ya kuimba, wengi waliokuwa wameongoka kwa kweli wameongozwa kujitenga na Mungu. Wamechagua uimbaji badala ya maombi; wamechagua kuhudhuria shule za uimbaji badala ya mikutano ya kiroho, mpaka Kweli ikapoteza nguvu yake ya kutakasa mioyo yao. Uimbaji wa namna hiyo ni chukizo mbele za Mungu. —[The Review and Herald, July 24, 1883](#). {VSSw 426.2}

SURA YA 68—UIMBAJI UNAOMTUKUZA MUNGU

Muziki Mbinguni—Niliona uzuri wa mbingu. Niliwasikia malaika wakiimba nyimbo za shangwe kuu, wakimtolea Yesu sifa, heshima na utukufu. Ndipo niliweza kutambua kwa kiasi fulani upendo wa ajabu wa Mwana wa Mungu. —[Shuhuda kwa Kanisa 1:123](#). {VSS 427.1}

Malaika Wapiga Vyombo-Malaika wa Muziki wa Ala —Nimeonyeshwa utaratibu, utaratibu mkamilifu wa mbingu, nami nilivutiwa sana niliposikia muziki mkamilifu ulioko huko. Baada ya kutoka katika maono, uimbaji wa hapa duniani ulionekana kuwa mkali na usio na upatanifu. Niliwaona makundi ya malaika wakiwa wamesimama katika mpangilio wa mraba, kila mmoja akiwa na kinubi cha dhahabu. Mwishoni mwa kila kinubi kulikuwa na kifaa cha kukiweka sawa au kubadilisha sauti zake. Vidole vyao havikupita juu ya nyuzi kwa uzembe, bali viligusa nyuzi mbalimbali ili kutoa sauti tofauti. Kulikuwa na malaika mmoja aliyeongoza daima; alianza kwa kugusa kinubi na kutoa sauti ya kwanza, kisha wote wakaungana katika

muziki wenye utajiri na ukamilifu wa mbingu. Hauwezi kuelezwa kwa maneno. Ulikuwa ni mlio mtamu, wa mbinguni na wa Kiungu; huku kila uso ukiangaza kwa sura ya Yesu, uking'aa kwa utukufu usioelezeka. —[Shuhuda kwa Kanisa 1:146](#). {VSS 427.2}

Muziki Mtamu Wenye Sauti Zenye Upole—Acheni wale wanaoridhika na hali yao iliyodumaa na isiyokamilika katika mambo ya kiroho wahamishwe ghafla kwenda mbinguni na kwa muda mfupi kuona hali hiyo ya juu, takatifu na kamilifu inayodumu milele; kila nafsi ikiwa imejaa upendo, kila uso ukiangaza kwa furaha, na muziki wa kuvutia wenye sauti tamu ukiinuka kwa heshima kwa Mungu na Mwana-Kondoo. —[Shuhuda kwa Kanisa 2:266](#). {VSS 428.1}

Athari za Nyimbo kwa Lusifa—Malaika walikubali kwa furaha ukuu wa Kristo, wakamsujudia na kumiminia upendo na ibada yao. Lusifa naye alipiga magoti pamoja nao, lakini moyoni mwake kulikuwa na mapambano makali na ya ajabu. Ukweli, haki na uaminifu vilikuwa vinapambana dhidi ya wivu na husuda. Ushawishi wa malaika watakatifu ulionekana kwa muda kumvuta pamoja nao. Nyimbo za sifa zilipopaa kwa sauti tamu za maelfu ya sauti za furaha, roho ya uovu ilionekana kushindwa; upendo usioelezeka ulijaza nafsi yake yote, na moyo wake ukaungana na waabudu wasio na dhambi katika kumpenda Baba na Mwana. —[Wazee wa Imani na Manabii, 36, 37](#). {VSS 428.2}

Kwaya ya Malaika Wakati wa Kuzaliwa kwa Yesu—Ndipo muziki wa mbingu uliposikika kwa masikio ya wanadamu, na kwaya ya mbinguni ikarudi mbinguni baada ya kumaliza wimbo wao wa pekee na wa kukumbukwa milele. Mwanga ulitoweka polepole, lakini ndani ya mioyo ya wachungaji kulibaki picha angavu zaidi ambayo mwanadamu angeweza kuiona, pamoja na ahadi na uhakikisho wenye baraka wa kuja kwa Mwokozi wa wanadamu katika ulimwengu huu, jambo lililowajaza mioyo yao furaha na shangwe, iliyochanganyika na imani na upendo wa ajabu kwa Mungu. —[Maisha Yangu Leo, 363](#). {VSS 428.3}

Uimbaji Wakati wa Ufufuo wa Yesu—Yesu alipotoka kaburini, wale malaika wenye kung'aa waliinama chini kwa ibada, wakamsalimu kwa nyimbo za ushindi na shangwe. —[Maandiko ya Awali, 182](#). {VSS 429.1}

Roho Zilizokombolewa Ni Mada ya Nyimbo—Nafsi iliyokombolewa na kutakaswa kutoka katika dhambi, yenye nguvu zake zote bora zilizowekwa wakfu

kwa huduma ya Mungu, ina thamani kuu isiyoweza kupimika; na mbinguni, mbele za Mungu na malaika watakatifu, kuna furaha juu ya nafsi moja iliyokombolewa, furaha ambayo huonyeshwa katika nyimbo za ushindi mtakatifu. —[Steps to Christ, 126. {VSS 429.2}](#)

Katika Nyumba Zetu Mwangwi wa Nyimbo za Malaika—Mwokozi wetu anapotutuongoza hadi kwenye kizingiti cha Ukuu usio na mwisho, tukiwa tumeng’aa kwa utukufu wa Mungu, tunaweza kusikia mada za sifa na shukrani kutoka kwa kwaya ya mbinguni inayozunguka kiti cha enzi; na mwangwi wa wimbo wa malaika unapoanza kusikika katika nyumba zetu za duniani, mioyo yetu itavutwa karibu zaidi na waimbaji wa mbinguni. Ushirika na mbingu huanza hapa duniani. Hapa tunajifunza sauti kuu ya sifa za mbinguni. —[Elimu, 168. {VSS 429.3}](#)

Shukrani Ni Sauti Kuu ya Mbingu—Matatizo yatatokea ambayo yatajaribu imani na uvumilivu wako. Yakabili kwa ujasiri. Tazama upande wenye mwanga. Ikiwa kazi imezuiwa, hakikisha kwamba si kwa kosa lako, kisha endelea mbele ukifurahi katika Bwana. Mbingu imejaa furaha. Inasikika kwa sifa za Yeye aliyetoa dhabihu kubwa namna hiyo kwa ajili ya ukombozi wa wanadamu. Je, kanisa lililo duniani halipaswi kujazwa na sifa? Je, Wakristo hawapaswi kutangaza duniani kote furaha ya kumtumikia Kristo? Wale ambao mbinguni wataungana na kwaya ya malaika katika wimbo wao wa sifa, lazima wajifunze hapa duniani wimbo wa mbingu, ambao sauti yake kuu ni shukrani. —[Shuhuda kwa Kanisa 7:244. {VSS 429.4}](#)

Nyimbo za Mbingu—Wengi wanaojiita Wakristo hawajui lugha ya mbingu, wala hawafundishi akili zao ili ziwe tayari kuimba nyimbo za mbingu au kufurahia shughuli za kiroho ambazo zitashughulisha mawazo ya wote huko. —[Shuhuda kwa Kanisa 2:265. {VSS 430.1}](#)

Sifa kwa Mungu—“Yeye atoe sadaka ya sifa,” asema Muumba, “hunitukuza Mimi.” Wakaaji wote wa mbingu wanaungana katika kumsifu Mungu. Tujifunze sasa wimbo wa malaika ili tuweze kuuimba tutakapoungana na safu zao zenye kung’aa. Tuseme pamoja na mtunga zaburi: *“Nitamsifu Bwana muda ninaoishi, Nitamwambia Mungu wangu ningali ni hai “Watu na wakushukuru, Ee Mungu, Watu wote na wakushukuru.”* Zaburi 146:2, Zaburi 67:5 —[Wazee wa Imani na Manabii, 289, 290. {VSS 430.2}](#)

Ibada Katika Nyumba za Mbinguni—Muziki ni sehemu ya ibada ya Mungu katika nyua za mbinguni, nasi tunapaswa kujitahidi katika nyimbo zetu za sifa kukaribia kadiri iwezekanavyo upatanifu wa kwaya za mbinguni. Mafunzo sahihi ya sauti ni sehemu muhimu ya elimu, nayo hayapaswi kupuuzwa. —[The Signs of the Times, March 14, 1900](#). {VSS 430.3}

Nyimbo za Watakatifu na Malaika—Ikiwa watakatifu wataweka macho yao juu ya thawabu iliyo mbele yao na kumtukiza Mungu kwa kumsifu, malaika watapeleka habari hizo njema katika mji, na malaika walioko mjini watagusa vinubi vyao vya dhahabu na kuimba kwa sauti kuu, “Haleluya!” Nayo matao ya mbinguni yatasikika kwa nyimbo zao nzuri. —[Maandiko ya Awali, 39](#). {VSS 431.1}

Rehema Duniani, Muziki Mbinguni—Unapomfungulia mlango Kristo kwa kuwahudumia wenye uhitaji na wanaoteseka, unapowakaribisha malaika wasioonekana. Unaalika ushirika wa viumbe wa mbinguni. Wanaleta hali takatifu ya furaha na amani. Wanakuja wakiwa na sifa midomoni mwao, na mwitikio wa wimbo wao husikika mbinguni. Kila tendo la rehema hufanya muziki huko. Baba kutoka katika kiti chake cha enzi huwataja watenda kazi wasio na ubinafsi kuwa hazina zake za thamani zaidi. —[Tumaini za Vizazi Vyote, 639](#). {VSS 431.2}

Maandalizi kwa Ajili ya Mbingu—Kwa nafsi yenye unyenyekevu na imani, nyumba ya Mungu duniani ni lango la mbingu. Wimbo wa sifa, sala, na maneno yanayosemwa na wawakilishi wa Kristo ni njia alizoweka Mungu kwa ajili ya kuwaandaa watu kwa kanisa lililo juu, kwa ibada ya juu zaidi ambayo ndani yake hakitaingia chochote kilicho najisi. —[Shuhuda kwa Kanisa 5:491](#). {VSS 431.3}

SURA YA 69—WIMBO NI SEHEMU YA IBADA

Tendo la Ibada Kama Sala—Kuimba, kama sehemu ya ibada ya kidini, ni tendo la ibada sawa na sala. Moyo lazima uhisi roho ya wimbo huo ili uweze kuutoa kwa namna inayofaa.—[Wazee wa Imani na Manabii, 594](#). {VSS 432.1}

Maana ya Maneno Katika Nyimbo.—Kwa kuwa kuimba ni sehemu ya ibada ya kidini, ni tendo la kumwabudu Mungu sawa na sala; kwa kweli, nyimbo nyingi ni sala. Mtoto anapofundishwa kutambua jambo hili, atazingatia zaidi maana ya maneno anayoyaimba na atakuwa tayari zaidi kupokea nguvu yake. [Elimu, 168](#). {VSS 432.2}

Maandalizi kwa Ajili ya Kanisa Lililo Juu—Mungu ni mkuu na mtakatifu; kwa roho mnyenyekevu na mwenye kuamini, nyumba Yake duniani, yaani mahali ambapo watu Wake hukutana kwa ibada, ni kama lango la mbinguni. Wimbo wa sifa na maneno yanayonenwa na wahudumu wa Kristo ni njia zilizowekwa na Mungu za kuwaandaa watu kwa ajili ya kanisa lililo juu na ibada iliyo kuu zaidi. [The Youth's Instructor, October 8, 1896](#). {VSS 432.3}

Malaika Wakiwa Miongoni mwa Wasikilizaji Katika Kanisa Letu—Tukumbuke kwamba katika kila kusanyiko la watakatifu hapa duniani kuna malaika wa Mungu

wanaosikiliza ushuhuda, nyimbo na sala; pia tukumbuke kwamba sifa zetu zinaongezewa nguvu na kwaya za jeshi la malaika lililo juu. [Shuhuda kwa Kanisa 6:367](#). {VSS 432.4}

Dhamira ya Kila Wimbo—Sayansi ya wokovu inapaswa kuwa kiini cha kila mahubiri, mada ya kila wimbo, na iwe pia maudhui ya kila ombi linalotolewa mbele za Mungu. [Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, 502](#). {VSS 433.1}

Imbeni kwa Roho na kwa Ufahamu—Uovu wa ibada ya mazoea hauwezi kuelezewa kwa msisitizo wa kutosha, lakini hakuna maneno yanayoweza kueleza kikamilifu baraka kuu ya ibada ya kweli. Wanadamu wanapoimba kwa roho na ufahamu, waimbaji wa mbinguni huunganisha sauti zao na wimbo huo wa shukrani. Yeye aliyetupatia vipawa vyote vinavyotuwezesha kuwa watenda kazi pamoja na Mungu anatarajia watumishi Wake kuzipalilia/kuziratibu/kuzilea sauti zao ili waweze kusema na kuimba kwa namna ambayo wote wataweza kuelewa. Kinachohitajika si kuimba kwa sauti kubwa, bali ni matamshi yaliyo wazi, matamshi sahihi na utoaji wa maneno unaoeleweka. Kila mmoja anapaswa kutenga muda wa kuilea sauti yake ili sifa za Mungu ziimbwe kwa sauti laini na safi, si kwa ukali na mlio mkali unaokera masikio. Uwezo wa kuimba ni kipawa kutoka kwa Mungu; hivyo kitumike kwa utukufu Wake. [Shuhuda kwa Kanisa 9:143, 144](#). {VSS 433.2}

Uzuri wa Sauti Katika Uimbaji Sio Kila Kitu—Watu wengi huimba nyimbo nzuri katika mikutano, nyimbo zinazozungumzia mambo watakayofanya na wanayokusudia kutenda, lakini baadhi yao hawatendi hayo; hawaimbi kwa roho wala kwa ufahamu. Vivyo hivyo, katika kusoma Neno la Mungu, wengine hawapati faida kwa sababu hawaliingizi katika maisha yao wala hawalitekelezi. [Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, 508](#). {VSS 433.3}

Nyimbo za Ibada Zinazofaa kwa Tukio—Wale wanaofanya uimbaji kuwa sehemu ya ibada ya Mungu wanapaswa kuchagua nyimbo zenye muziki unaofaa kwa tukio husika; si nyimbo zenye huzuni kama za mazishi, bali nyimbo zenye furaha na

wakati huohuo zenye heshima na utulivu. Sauti inaweza na inapaswa kurekebisha, kulainishwa na kudhibitiwa. [Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, 508. {VSS 434.1}](#)

Nyimbo za Kusanyiko—Jambo lingine linalopaswa kupewa uangalifu katika mikutano yetu ya makambi na sehemu nyingine ni suala la uimbaji. Mhubiri hapaswi kuchagua wimbo wa kuimbwa kabla hajahakikisha kwamba wale watakaoimba wanafahamu wimbo huo. Mtu anayefaa anapaswa kuteuliwa kusimamia huduma hii, na wajibu wake uwe kuhakikisha kwamba nyimbo zinazochaguliwa zinaweza kuimbwa kwa roho na ufahamu. Kuimba ni sehemu ya ibada ya Mungu, lakini inapofanywa bila mpangilio na maandalizi, hakuliletei heshima kweli wala utukufu Mungu. Kunapaswa kuwepo na utaratibu na mpangilio katika jambo hili kama ilivyo katika kila sehemu nyingine ya kazi ya Bwana. Undeni kikundi cha waimbaji bora ambao sauti zao zinaweza kuongoza kusanyiko, kisha wote wanaotaka washirikiane nao. Wanaoimba wanapaswa kujitahidi kuimba kwa upatano na kutenga muda wa kufanya mazoezi ili kutumia kipawa hiki kwa utukufu wa Mungu. [The Review and Herald, July 24, 1883. {VSSw 434.2}](#)

Ibada ya Nyimbo kwa Kila Mtu—Katika mikutano haipaswi kuwepo jambo lolote la kuonekana kama maonyesho ya jukwaani. Uimbaji haupaswi kufanywa na watu wachache pekee; wote waliopo wanapaswa kutiwa moyo kushiriki katika huduma ya uimbaji. Wapo wenye kipawa maalumu cha kuimba, na kuna nyakati ambapo ujumbe maalumu unaweza kutolewa kupitia mwimbaji mmoja au kikundi kidogo, lakini kwa kawaida uimbaji unapaswa kushirikisha wengi. Uwezo wa kuimba ni kipawa chenye ushawishi ambacho Mungu anatamani kila mmoja akikuze na kukitumia kwa utukufu wa Jina Lake. [Shuhuda kwa Kanisa 7:115, 116. {VSSw 435.1}](#)

Uimbaji Mtamu na Rahisi—Mungu anawezaje kutukuzwa tunapotegemea kwaya ya kidunia inayolipwa kwa ajili ya kuimba? Tunapoyaona mambo haya kwa mtazamo sahihi, katika mikutano yetu tutakuwa na uimbaji mtamu na rahisi, na tutaalika kusanyiko lote kushiriki katika wimbo. Je, ikiwa miongoni mwao wapo watu ambao sauti zao si nzuri kama za wengine? Wakati uimbaji unapokuwa katika hali ambayo malaika wanaweza kuungana nao, utaleta mvuto mioyoni mwa watu

ambao hauwezi kuletwa na uimbaji wa midomo isiyotakaswa. [Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, 509.](#) {VSSsw 435.2}

Mvuto wa Uimbaji wa Kusanyiko—Katika mikutano inayofanyika, uimbaji haupaswi kupuuzwa. Mungu anaweza kutukuzwa kupitia sehemu hii ya ibada. Waimbaji wanapojitoa kwa huduma hii wanapaswa kukubaliwa, lakini fedha hazipaswi kutumiwa kuwalipa waimbaji. Mara nyingi uimbaji rahisi wa nyimbo za kiroho unaofanywa na kusanyiko huwa na mvuto ambao haupatikani hata katika uimbaji wa kwaya yenye ustadi mkubwa. [Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, 509](#) {VSSsw 435.3}

Ufalme wa Mungu Unazidi Taratibu za Nje—Taratibu na kaida za kidini haviwezi kuunda ufalme wa Mungu, kwa sababu sherehe huzidi kuwa nyingi na za kupindukia pale kanuni muhimu za ufalme wa Mungu zinapopotea; Kristo hataki taratibu na maadhimisho ya nje pekee, bali anatamani kupokea kutoka katika shamba Lake matunda ya utakatifu na kutokuwa na ubinafsi, yanayoonekana katika matendo ya wema, rehma na kweli. {VSSsw 436.1}

Mavazi ya kuvutia, uimbaji mzuri na muziki wa vyombo kanisani haviwezi kuleta nyimbo za kwaya ya malaika, kwa maana mbele za Mungu mambo hayo yanafanana na matawi ya mtini usiozaa yaliyokuwa na majani mengi ya kujionyesha bila matunda. Kristo anatafuta matunda, yaani kanuni za wema, huruma na upendo, ambazo ndizo kanuni za mbinguni; na kanuni hizo zinapoonekana katika maisha ya wanadamu, tunajua kwamba Kristo amefanyika ndani yao, akiwa tumaini la utukufu. Kusanyiko linaweza kuwa maskini zaidi katika nchi, bila muziki wala maonyesho ya nje, lakini ikiwa lina kanuni hizi, waumini wanaweza kuimba kwa sababu furaha ya Kristo imo ndani ya mioyo yao, na wanaweza kumtolea Mungu sadaka tamu ya sifa. [Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, 511, 512.](#) {VSSsw 436.2}

Huduma ya Uimbaji Si Tamasha—Nilionyeshwa kwamba ikiwa Mzee _____ angezingatia ushauri wa ndugu zake na kuacha kukimbilia kufanya juhudi kubwa za

kuvutia makusanyiko mengi, angekuwa na ushawishi mkubwa zaidi kwa mema na kazi yake ingekuwa na matokeo yenye nguvu zaidi. Anapaswa kuondoa katika mikutano yake kila kitu kinachofanana na maonyesho ya kimaigizo, kwa sababu sura hizo za nje haziongezi nguvu katika ujumbe anaouhubiri. Wakati Bwana atakapoweza kushirikiana naye, kazi yake haitahitaji kufanywa kwa gharama kubwa namna hiyo; hatakuwa na haja ya kutumia fedha nyingi katika kutangaza mikutano yake wala kutegemea sana mipango ya muziki. Sehemu hii ya huduma yake imekuwa ikiendeshwa zaidi kama tamasha la ukumbi wa maonyesho kuliko huduma ya uimbaji katika mkutano wa kidini. [Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti](#)

[.501.](#) {VSSsw 436.3}

Mapenzi ya Mungu Kuhusu Muziki—Mambo ya ziada yasiyo ya lazima yaliyoingizwa katika ibada yanapaswa kuepukwa kwa nguvu zote, kwa sababu muziki unakubalika mbele za Mungu pale tu moyo unapokuwa umetakaswa, kulainishwa na kufanywa mtakatifu kupitia matumizi yake sahihi. Hata hivyo, wengi wanaofurahia muziki hawajui maana ya kumwambia Bwana kwa mioyo yao, kwa kuwa mioyo yao imeelekezwa “kwa sanamu zao.” [Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, 512.](#) {VSSsw 437.1}

Kuondoa Mabaki Yasiyofaa Kanisani—Wakristo wanaodai kumfuata Kristo wanapofikia kiwango cha juu ambacho wana haki ya kufikia, urahisi wa Kristo utaonekana katika ibada zao zote, kwa sababu maumbo ya nje, taratibu na ustadi wa muziki si nguvu ya kanisa; hata hivyo, mambo haya yamechukua nafasi ambayo Mungu anapaswa kuwa nayo, kama ilivyokuwa katika ibada ya Wayahudi. {VSSsw 437.2}

Bwana amenifunulia kwamba wakati moyo unaposafishwa na kutakaswa, na washiriki wa kanisa wanaposhiriki asili ya Mungu, nguvu itatoka katika kanisa la waaminio wa kweli itakayozalisha wimbo ndani ya mioyo yao. Wanaume na wanawake hawatategemea tena muziki wa vyombo pekee, bali nguvu na neema ya

Mungu vitawapa utimilifu wa furaha. Kwa hiyo, kuna kazi inayopaswa kufanywa ya kuondoa mabaki yasiyofaa yaliyoingizwa kanisani; na ujumbe huu hauwahusu tu waumini wa kanisa la _____, bali kila kanisa lililofuata mfano wake. [Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, 512. {VSSsw 437.3}](#)

Urahisi Katika Huduma za Kidini—Watumishi wa kweli wanatambua thamani ya kazi ya ndani ya Roho Mtakatifu katika mioyo ya wanadamu, hivyo wanaridhika na urahisi katika huduma za kidini. Badala ya kufanya uimbaji maarufu kuwa jambo kuu, wao huipa nafasi ya kwanza kujifunza Neno la Mungu na kumtolea Mungu sifa kutoka moyoni. Zaidi ya mapambo ya nje, wanathamini mapambo ya ndani, yaani roho ya upole na utulivu, na vinywani mwao hamna hila. [Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, 502. {VSSsw 438.1}](#)

Kazi ya Roho Mtakatifu—Mioyo ya watu wengi duniani pamoja na washiriki wengi wa kanisa ina njaa ya Mkate wa Uzima na kiu ya maji ya wokovu. Ingawa wanapendezwa na huduma ya nyimbo, shauku yao kuu si nyimbo pekee wala hata maombi, bali wanataka kujua Maandiko yanavyosema: “Neno la Mungu linaniambia nini mimi?” Roho Mtakatifu anatenda kazi katika akili na mioyo yao, akiwaongoza kwenye Mkate wa Uzima, na wanapooni kila kitu kinachowazunguka kikibadilika, hisia za kibinadamu pamoja na mawazo kuhusu kile kinachounda dini hubadilika pia; hivyo wanakuja kusikiliza Neno kama lilivyoandikwa. [Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, 501. {VSSsw 438.2}](#)

Uwiano Sahihi Katika Mikutano ya Makambi—Maboresho yanaweza kufanywa katika namna tunavyoendesha mikutano ya makambi ili wote wanaohudhuria wapate huduma ya moja kwa moja zaidi. Kuna mikutano ya kijamii inayofanyika katika hema kubwa ambapo wote hukusanyika kwa ajili ya ibada, lakini mikutano hiyo huwa mikubwa kiasi kwamba ni wachache tu wanaoweza kushiriki, na wengi huzungumza kwa sauti ya chini kiasi kwamba wachache husikia. Katika baadhi ya

matukio muda mwingi umetumika katika kuimba; wimbo mrefu huimbwa kabla ya sala, mwingine mrefu baada ya sala, na nyimbo nyingi huingizwa katikati ya mkutano. Kwa njia hiyo, nyakati za thamani zimetumiwa vibaya, na si nusu ya matokeo mema yaliyoweza kupatikana kama nyakati hizo zingesimamiwa vizuri zaidi. [Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti](#). {VSS 439.1}

Uambatanishaji wa Vyombo vya Muziki—Katika huduma zetu za mikutano ya makambi kunapaswa kuwepo uimbaji pamoja na muziki wa vyombo, kwa sababu vyombo vya muziki vilitumika katika huduma za kidini nyakati za kale ambapo waabudu walimsifu Mungu kwa kinubi na matoazi; hivyo muziki unapaswa kuwa na nafasi katika huduma zetu kwa kuwa unaongeza mvuto katika ibada. [Shuhuda kwa Kanisa 6:62](#). {VSS 439.2}

Uangalifu Katika Huduma ya Uimbaji—Katika mikutano inayofanyika, wachaguliwe watu kadhaa kushiriki katika huduma ya uimbaji, na uimbaji huo uambatanishwe na vyombo vya muziki vinavyopigwa kwa ustadi. Hatupaswi kupinga matumizi ya vyombo vya muziki katika kazi yetu, bali sehemu hii ya huduma inapaswa kuendeshwa kwa uangalifu kwa sababu ni tendo la kumsifu Mungu kwa njia ya nyimbo. Uimbaji haupaswi kufanywa na watu wachache kila wakati; inapowezekana, kusanyiko lote lishiriki. [Watendakazi wa Injili, 357, 358](#). {VSS 439.3}

SURA YA 70—UIMBAJI KAMA NJIA YA USHUHUDA

Chombo cha Kuleta Wokovu—Mwimbiko wa nyimbo unaoinuliwa kutoka katika mioyo mingi kwa matamshi yaliyo wazi na yanayoeleweka ni mojawapo ya njia ambazo Mungu hutumia katika kazi ya kuokoa roho. [Shuhuda kwa Kanisa5:493](#). {VSS 441.1}

Nguvu ya Kuwavuta Watu kwa Kristo—Sauti ya mwanadamu ina mvuto wa pekee pamoja na uzuri wa kimuziki, na ikiwa mwanafunzi atafanya juhudi za dhiti, atajenga mazoea ya kuzungumza na kuimba ambayo yatakuwa chombo chenye nguvu cha kuwavuta watu kwa Kristo. [Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, 504](#). {VSS 441.2}

Vipawa Vinavyotoka kwa Mungu—Sauti yako, ushawishi wako na muda wako—vyote hivi ni vipawa kutoka kwa Mungu, na vinapaswa kutumiwa katika kazi ya kuongoza roho kwa Kristo. [Shuhuda kwa Kanisa 9:38](#). {VSSw 441.3}

Wainjilisti wa Uimbaji—Jioni moja, umati mkubwa ulikusanyika kanisani ili kusikiliza huduma ya muziki iliyowasilishwa na Ndugu Beardslee pamoja na wanafunzi wake. Uimbaji mzuri ni sehemu muhimu ya ibada ya Mungu, na ninafurahi kwamba Ndugu Beardslee anawafundisha wanafunzi ili waweze kuwa wainjilisti wa uimbaji. [Misingi ya Elimu kwa Kila Mwanadamu, 487](#). {VSSw 441.4}

Uimbaji Katika Ziara za Nyumbani—Jifunzeni kuimba nyimbo rahisi zaidi, kwa sababu nyimbo hizo zitawasaidia katika kazi ya nyumba kwa nyumba, na mioyo ya watu itaguswa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Kristo mara nyingi alisikika akiimba nyimbo za sifa, kwa kuwa kulikuwa na furaha moyoni Mwake. Tunajifunza kutoka katika Neno la Mungu kwamba kuna furaha miongoni mwa malaika wa mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja anayetubu, na kwamba Bwana hufurahia kanisa Lake kwa nyimbo. [Maisha Yangu Leo, 238](#). {VSSw 441.5}

Vijana Kuimba Kwa Ajili ya Watu wa Tabaka Zote—Enyi wanafunzi, tokeni katika njia kuu na njia za pembeni, mkijitahidi kuwafikia watu wa tabaka za juu na za chini. Ingieni katika nyumba za matajiri na maskini, na kila mpatao nafasi waulizeni: “*Je, mtafurahi tukiomba tuwaimbie? Tutafurahi kufanya huduma ya*

nyimbo pamoja nanyi.” Kisha mioyo inapolainishwa, njia inaweza kufunguka ili mtoe maneno machache ya sala kwa ajili ya baraka za Mungu. Wengi hawatakataa mwaliko huo. Huduma ya namna hii ni kazi halisi ya umisionari. Mungu anatamani kila mmoja wetu ageuzwe na ajifunze kushiriki kwa bidii katika kazi ya umisionari. Atatubariki tunapowahudumia wengine, na tutaona wokovu Wake. [The Review and Herald, August 27, 1903.](#) {VSSsw 442.1}

Huduma ya Uimbaji Wakati wa Safari—Siku ya Sabato tulikuwa na huduma ya uimbaji. Ndugu Lawrence, ambaye alikuwa mwanamuziki, aliongoza uimbaji huo, na abiria wote waliokuwa ndani ya gari walionekana kufurahia sana huduma hiyo; wengi wao walijiunga katika kuimba. {VSSsw 442.2}

Siku ya Jumapili tulikuwa tena na huduma ya uimbaji, kisha Mzee Corliss akatoa hotuba fupi akitumia maneno haya kama Andiko lake: *“Tazameni ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu.”* Abiria walisikiliza kwa makini na walionekana kufurahia ujumbe huo. {VSSsw 442.3}

Siku ya Jumatatu tuliendelea tena na uimbaji, na sote tulionekana kusogea karibu zaidi katika umoja. [Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, 503.](#) {VSSsw 443.1}

Malaika Kama Walimu wa Uimbaji—Wale walio na kipawa cha kuimba wanahitajika, kwa sababu uimbaji ni mojawapo ya njia zenye nguvu zaidi za kuingiza kweli za kiroho ndani ya moyo. Mara nyingi, kupitia maneno ya nyimbo takatifu, chemchemi za toba na imani zimefunguliwa ndani ya nafsi. Washiriki wa kanisa, vijana kwa wazee, wanapaswa kufundishwa kwenda mbele kutangaza ujumbe huu wa mwisho kwa ulimwengu. Ikiwa wataenda kwa unyenyekevu, malaika wa Mungu wataandamana nao, wakiwafundisha jinsi ya kuinua sauti katika sala, jinsi ya kuinua sauti katika nyimbo, na jinsi ya kutangaza ujumbe wa injili kwa wakati huu. [Maisha Yangu Loe, 238.](#) {VSSsw 443.2}

SURA YA 71—UIMBAJI KATIKA UZOEFU WA ISRAELI

Wimbo na Matukio ya Historia ya Mwanadamu—Muziki wa sifa ni hali ya mbinguni; na wakati mbingu inapogusana na dunia, huonekana muziki na nyimbo—*“shukrani na sauti ya nyimbo.”* (Isaya 51:3). {VSS 444.1}

Juu ya dunia mpya iliyoumbwa, ilipokuwa bado nzuri na isiyo na doa chini ya tabasamu la Mungu, “nyota za asubuhi ziliimba pamoja, nao wana wote wa Mungu walipiga kelele kwa furaha.” (*Ayubu 38:7*). Vivyo hivyo, mioyo ya wanadamu inapopatana na mbingu, imeitikia wema wa Mungu kwa sauti za sifa. Matukio mengi katika historia ya mwanadamu yamehusishwa na nyimbo. —[Elimu, 161](#). {VSS 444.2}

Kuvuka Bahari ya Shamu—Wimbo wa kwanza uliorekodiwa katika Biblia kutoka midomoni mwa wanadamu ulikuwa ule mlipuko mtukufu wa shukrani uliotolewa na majeshi ya Israeli katika Bahari ya Shamu. —[Elimu, 162](#). {VSS 444.3}

Miriamu Akiwa Kiongozi wa Kwaya—Kama sauti ya bahari kuu ilivyoinuka kutoka kwa umati mkubwa wa Israeli, ndivyo lilivyokuwa tendo hilo tukufu la sifa. (*Tazama Kutoka 15:1-16*). Wimbo huo uliimbwa tena na wanawake wa Israeli, huku Miriamu, dada yake Musa, akiwaongoza walipotoka wakiwa na matari na kucheza. Kilio cha furaha kilisikika mbali katika jangwa na bahari, na milima ikarudia maneno yao ya sifa: “**Mwimbieni Bwana, kwa maana ametenda mambo makuu kwa ushindi.**” —[Wazee wa Imani na Manabii, 288, 289](#). {VSS 444.4}

Wimbo wa Musa—Maneno haya (*yaani, wimbo wa Musa*) yalirudiwa kwa Israeli wote, yakawa wimbo uliokuwa ukiimbwa mara kwa mara kwa sauti kuu za muziki wa utukufu. Hii ilikuwa hekima ya Musa: aliwasilisha Kweli kwao katika mfumo wa wimbo, ili kupitia sauti tamu za muziki waweze kuizoea na kuihifadhi katika akili za taifa lote, vijana kwa wazee. Ilikuwa muhimu watoto wajifunze wimbo huo, kwa sababu ungezungumza nao kwa kuwaonya, kuwazuia, kuwakemea na kuwatia moyo. Ulikuwa kama mahubiri ya kudumu. —[Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, 496, 497](#). {VSS 445.1}

Nyimbo Kama Unabii—Ili kuzifanya Kweli hizi (*ambazo Musa alizitoa katika hotuba yake ya mwisho kwa wana wa Israeli kuhusu matokeo ya utii na kutokutii, yaani uchaguzi kati ya uzima na mauti*) ziingie kwa undani zaidi katika akili za watu wote, kiongozi huyo mkuu aliziweka katika mfumo wa mashairi matakatifu.

Wimbo huu haukuwa wa kihistoria tu, bali pia ulikuwa wa kinabii. Ulisimulia matendo makuu ya Mungu kwa watu wake katika siku zilizopita, na pia ulitangulia kuonyesha matukio makuu ya wakati ujao, yaani ushindi wa mwisho wa waaminifu Kristo atakapokuja mara ya pili katika nguvu na utukufu. Watu waliagizwa

kuuhifadhi moyoni huo mkusanyo wa historia ya kishairi na kuwafundisha watoto wao na wajukuu zao. Ulipaswa kuimbwa na kusanyiko wakati walipokusanyika kwa ibada, na pia kurudiwa na watu walipokuwa wakiendelea na kazi zao za kila siku. —[Wazee wa Imani na Manabii, 467, 468.](#) {VSS 445.2}

Amri za Mungu Katika Wimbo—Watu waliposafiri jangwani, mafundisho mengi ya thamani yaliwekwa katika akili zao kwa njia ya nyimbo. Wakati walipookolewa kutoka kwa jeshi la Farao, mkutano wote wa Israeli uliungana katika wimbo wa ushindi. Mbali katika jangwa na bahari ulisikika mwanzi wa wimbo wa furaha, na milima ikarudia sauti za sifa: *“Mwimbieni Bwana, kwa maana ametukuka sana.”* (Kutoka 15:21). Mara nyingi katika safari yao waliurudia wimbo huu, ukiwafariji mioyo yao na kuwasha imani ya wasafiri hao waliokuwa njiani. Amri zilizotolewa katika Sinai, pamoja na ahadi za kibali cha Mungu na kumbukumbu za matendo Yake makuu ya ukombozi, ziliwekwa kwa njia ya Kiungu katika mfumo wa wimbo na kuimbwa kwa ala za muziki, huku watu wakitembea kwa mpangilio na kuunganisha sauti zao katika sifa. {VSS 446.1}

Kwa njia hiyo, mawazo yao yaliinuliwa kutoka katika majaribu na shida za safari; roho yao ya kutotulia na ya vurugu ilitulizwa; kanuni za Kweli ziliwekwa katika kumbukumbu zao; na imani yao iliimarishwa. Ushirikiano katika tendo moja uliwafundisha utaratibu na umoja, na watu waliletwa karibu zaidi na Mungu na wao kwa wao. —[Elimu, 39.](#) {VSS 446.2}

Maneno ya Sheria Katika Muziki—Musa aliwaagiza Waisraeli kuyaweka maneno ya sheria katika mfumo wa muziki. Watoto wakubwa walipiga vyombo vya muziki, huku wadogo wakitembea kwa mpangilio wakiimba kwa pamoja wimbo wa amri za Mungu. Katika miaka iliyofuata, waliendelea kuyakumbuka maneno ya sheria ambayo walijifunza utotoni. {VSS 446.3}

Ikiwa ilikuwa muhimu kwa Musa kuyaweka maagizo katika wimbo mtakatifu ili watoto waweze kujifunza kuimba sheria mstari kwa mstari walipokuwa wakitembea jangwani, basi ni muhimu zaidi katika wakati huu kuwafundisha watoto wetu Neno la Mungu. Tufanye kila tuwezalo kufanya muziki katika nyumba zetu, ili Mungu aweze kuingia humo. —[Enendeni Mtandaoni Kote-Uinjilisti, 499, 500.](#) {VSS 447.1}

Nyimbo za Ukumbusho—Matendo ya Mungu kwa watu wake yanapaswa kurudiwa mara kwa mara. Ili wasisahau historia ya zamani, Mungu alimwamuru Musa kuyaweka matukio hayo katika mfumo wa wimbo, ili wazazi wawafundishe watoto wao. Tunapaswa mara nyingi kusimulia wema wa Mungu na kumsifu kwa matendo Yake ya ajabu. —[Shuhuda kwa Kanisa 6:364, 365](#). {VSS 447.2}

Muziki katika Shule za Manabii—Masomo makuu yaliyofundishwa katika shule hizi yalikuwa sheria ya Mungu pamoja na mafundisho aliyompa Musa, historia takatifu, muziki mtakatifu na mashairi. Akili iliyotakaswa ilitoa kutoka katika hazina ya Mungu mambo mapya na ya kale, na Roho wa Mungu alidhihirishwa katika unabii na nyimbo takatifu. —[Elimu, 47](#). {VSSw 447.3}

Melodi Takatifu kwa Wanafunzi—Sanaa ya melodi takatifu ilisitawishwa kwa bidii. Hakukuwa na ngoma za starehe zisizo na maana wala nyimbo za mzaha zilizomtukuza mwanadamu na kugeuza mawazo kutoka kwa Mungu; bali kulikuwa na zaburi takatifu na zenye uzito za kumsifu Muumba, zilizolitukuza Jina Lake na kusimulia matendo Yake ya ajabu. Hivyo, muziki ulifanywa kutumikia kusudi takatifu, yaani kuinua mawazo kuelekea mambo yaliyo safi, yenye heshima na yenye kuinua roho, na kuamsha ndani ya nafsi ibada na shukrani kwa Mungu. —*Misingi ya Elimu kwa Kila Mwanadamu*, [97, 98](#). {VSSw 447.4}

Muziki kwa Kusudi Takatifu—Muziki ulifanywa kutumikia kusudi takatifu; uliinua mawazo kuelekea mambo yaliyo safi, yenye heshima na yenye kuinua roho, na kuamsha ndani ya moyo ibada na shukrani kwa Mungu. Kuna tofauti kubwa kati ya matumizi ya zamani ya muziki na matumizi ambayo mara nyingi hufanywa leo. Wengi hutumia kipawa hiki kujitukuza wenyewe badala ya kumtukuza Mungu. Upendo wa muziki huwaongoza baadhi ya watu wasio na tahadhari kuungana na wapenda dunia katika mikusanyiko ya starehe ambako Mungu amewakataza watoto Wake kwenda. Kwa hiyo, kile ambacho ni baraka kubwa kinapotumiwa kwa usahihi, huwa mojawapo ya njia zenye mafanikio makubwa ambazo Shetani huzitumia kuvuta akili za watu mbali na wajibu na kutafakari mambo ya milele. —[Wazee wa Imani na Manabii, 594](#). {VSSw 448.1}

Zaburi za Daudi Zinazoendelea Kuwa Chanzo cha Msukumo—Ushirika wa Daudi na mazingira ya asili pamoja na Mungu haukuwa tu kwa ajili ya kujenga tabia yake na kuathiri maisha yake ya baadaye, bali pia kupitia zaburi za mwimbaji huyo mtamu wa Israeli, katika vizazi vyote vijavyo, ungechochea upendo na imani katika mioyo ya watu wa Mungu na kuwavuta karibu zaidi na moyo wa Mungu mwenye upendo, ambaye ndani Yake viumbe Vyake vyote vinaishi. —[Wazee wa Imani na Manabii, 642](#). {VSS 448.2}

Ibada ya Daudi Kupitia Nyimbo—Ufunuo wa kila siku wa tabia na ukuu wa Muumba wake uliujaza moyo wa Daudi kijana mshairi kwa ibada na furaha. Alipotafakari juu ya Mungu na kazi Zake, uwezo wa akili na moyo wake ulikua na kuimarika kwa ajili ya kazi yake ya baadaye. Kila siku aliingia katika ushirika wa karibu zaidi na Mungu. Mawazo yake yaliendelea kutafuta vina vipya vya kumtia moyo katika nyimbo zake na kuamsha muziki wa kinubi chake. Melodi tamu ya sauti yake ilipoenea hewani, ilisikiwa ikirudiwa na vilima kana kwamba vilikuwa vikijibu nyimbo za furaha za malaika huko mbinguni. —[Wazee wa Imani na Manabii](#). {VSS 448.3}

Muziki wa Mbinguni kwa Mfalme Sauli—Kwa mpango wa Mungu, Daudi, akiwa mpigaji stadi wa kinubi, aliletwa mbele ya mfalme. Melodi zake zenye ukuu na zilizoongozwa na mbingu zilileta matokeo yaliyokusudiwa. Huzuni nzito iliyokuwa imetanda juu ya akili ya Sauli kama wingu jeusi ilitoweka. —[Wazee wa Imani na Manabii, 643](#). {VSS 449.1}

Faraja Kupitia Muziki—Daudi alikuwa katika jumba la mfalme na alikuwa ameona majukumu makubwa ya ufalme. Aliona baadhi ya majaribu yaliyokuwa yakiikabili nafsi ya Sauli na akaelewa kwa kina baadhi ya mambo yaliyohusu tabia na mwenendo wa mfalme wa kwanza wa Israeli. Aliona utukufu wa ufalme ukiwa umefunikwa na kivuli kizito cha huzuni, na alijua kwamba nyumba ya Sauli, katika maisha yao ya faragha, haikuwa na furaha ya kweli. Mambo haya yote yalileta mawazo mazito kwa yule aliyekuwa ametiwa mafuta kuwa mfalme wa Israeli. Lakini alipokuwa amezama katika tafakari nzito na kusumbuliwa na mawazo ya wasiwasi, aligeukia kinubi chake na kutoa melodi zilizoinua akili yake kwa Mwanzilishi wa kila jambo jema; ndipo mawingu meusi yaliyokuwa yakifunika upeo wa maisha yake ya baadaye yalitoweka. —[Wazee wa Imani na Manabii, 644](#). {VSS 449.2}

Daudi Akiwa Kiongozi wa Nyimbo—Watu wa Israeli walimfuata kwa shangwe kuu na nyimbo za furaha, huku sauti nyingi zikiungana katika melodi pamoja na vyombo vya muziki; *“Daudi na nyumba yote ya Israeli wakacheza mbele za Bwana ... kwa vinubi, na vinanda, na matari, na pembe, na matoazi.”* [Tazama 2 Samweli 6]. —[Wazee wa Imani na Manabii, 704, 705. {VSS 450.1}](#)

Muziki katika Maandamano ya Sanduku la Agano—Maandamano ya ushindi yalipokaribia mji mkuu, yakifuata alama takatifu ya Mfalme wao asiyeonekana, wimbo mkubwa wa shangwe ulisikika ukiwataka walinzi waliokuwa juu ya kuta za mji wafungue malango ya mji mtakatifu: *“Inueni vichwa vyenu, enyi malango, Inukeni, enyi malango ya milele, Mfalme wa utukufu apate kuingia.”* Zaburi 24:7 Kundi la waimbaji na wapigaji vyombo vya muziki lilijibu kwa kuuliza: *“Ni nani Mfalme wa utukufu?”* Nalo kundi jingine likajibu: *“Bwana Mwenye nguvu, hodari, Bwana hodari wa vita.”* Zaburi 24:8 {VSSw 450.2}

Kisha mamia ya sauti yaliungana pamoja na kuinua wimbo wa ushindi: *“Inueni vichwa vyenu, enyi malango, Naam, viinueni, enyi malango ya milele, Mfalme wa utukufu apate kuingia.”* {VSSw 450.3}

Nayo sauti ya umati mkubwa, iliyokuwa kama *“mvumo wa maji mengi,”* ikasikika ikijibu kwa furaha: *“Bwana wa majeshi, Yeye Ndiye Mfalme wa utukufu.”* —[Wazee wa Imani na Manabii, 707, 708. {VSS 450.4}](#)

Nyimbo za Uzoefu wa Daudi—Zaburi ya hamsini na moja ni maelezo ya toba ya Daudi baada ya kupokea ujumbe wa kukemewa kutoka kwa Mungu. Katika wimbo huu mtakatifu uliokusudiwa kuimbwa katika mikusanyiko ya hadhara ya watu wake, mbele ya jumba la kifalme—mbele ya makuhani, waamuzi, wakuu na mashujaa wa vita—mfalme wa Israeli alisimulia dhambi yake, toba yake, na tumaini lake la kupata msamaha kupitia rehema za Mungu. Wimbo huo ungeendelea kuwa kumbukumbu ya kuanguka kwake kwa vizazi vijavyo. —[Wazee wa Imani na Manabi, 724, 725. {VSSw 451.1}](#)

Muziki Kama Njia ya Kuondoa Ibada ya Sanamu—Huduma ya nyimbo iliwekwa kuwa sehemu ya kawaida ya ibada ya kidini, na Daudi alitunga zaburi si kwa matumizi ya makuhani pekee katika huduma ya patakatifu, bali pia ili ziimbwe na watu wakati wa safari zao kwenda madhabahuni pa taifa katika sikukuu za kila mwaka. Ushawishi wa nyimbo hizo ulikuwa mkubwa sana kiasi kwamba ulisaidia

kulikomboa taifa kutoka katika ibada ya sanamu. Mataifa yaliyowazunguka, yalipoona ustawi wa Israeli, yaliongozwa kumfikiria Mungu wa Israeli kwa mtazamo mzuri, kwa sababu yaliona matendo makuu aliyowatendea watu Wake. — [Wazee wa Imani na Manabii, 711](#). {VSSw 451.2}

Nyimbo Katika Majaribu Makali—Ni hisia gani zilizokuwa moyoni mwa baba na mfalme aliyekuwa ametendewa vibaya sana katika hatari hii kubwa ya uasi wa Absalom? Alikuwa “*mtu hodari wa vita*,” mfalme ambaye neno lake lilikuwa sheria; lakini sasa alikuwa amesaliwa na mwana wake aliyempenda, aliyemlea na aliyemwamini bila busara. Alikuwa amedhulumiwa na kuachwa na raia waliokuwa wamefungwa kwake kwa vifungo vya heshima na uaminifu. Katika saa ya jaribu lake kuu, wakati giza lilipoonekana kumzunguka, Daudi aliweka moyo wake kwa Mungu, naye akaimba. Katika huzuni na mateso yake, alimtegemea Bwana aliyekuwa chanzo cha nguvu na tumaini lake. —[Zaburi 3:1-8](#).—[Wazee wa Imani na Manabii, 741, 742](#). {VSSw 451.3}

Muziki Kama Sehemu ya Mfumo wa Patakatifu—Wakati Sulemani alipolileta hekaluni sanduku takatifu lililokuwa na mbao mbili za mawe ambazo juu yake amri za Mungu za Amri Kumi ziliandikwa kwa kidole cha Mungu, alifuata mfano wa baba yake Daudi. Kila baada ya hatua sita walitoa dhabihu. Kwa nyimbo, muziki na sherehe kubwa, “*makuhani waliliingiza Sanduku la Agano la Bwana mahali pake*.” Walipotoka katika Patakatifu pa ndani, walichukua nafasi walizopewa. Waimbaji, yaani Walawi waliovaa mavazi meupe ya kitani, wakiwa na matoazi, vinubi na vinanda, walisimama upande wa mashariki wa madhabahu, pamoja nao walikuwepo makuhani mia moja na ishirini waliopiga tarumbeta. —[2 Mambo ya Nyakati 5:7, 12](#).—[Manabii na Wafalme, 38, 39](#). {VSS 452.1}

Nyimbo Katika Vita—*Yehoshafati alipokuwa akikabili tishio la maadui, aliinama kifudifudi mbele za Bwana, naye Yuda wote pamoja na wenyeji wa Yerusalemu wakaanguka mbele za Mungu wakimsujudia. Ndipo Walawi wa wana wa Wakohathi na wana wa Wakora wakasimama kumsifu Bwana, Mungu wa Israeli, kwa sauti kuu sana.* {VSS 452.2}

Asubuhi na mapema wakaondoka kwenda nyikani mwa Tekoa. Walipokuwa wakielekea vitani, Yehoshafati akawaambia: “*Nisikieni, enyi Yuda nanyi wenyeji wa Yerusalemu; mwaminini Bwana, Mungu wenu, ndivyo mtakavyothibitika; waaminini manabii Wake, ndivyo mtakavyofanikiwa.*” Kisha baada ya kushauriana

na watu, aliwaweka waimbaji wa Bwana watangulie mbele ya jeshi ili kumsifu Mungu kwa ajili ya uzuri wa utakatifu Wake. —[2 Mambo ya Nyakati 20:14-21](#). Waimbaji hao walitangulia mbele ya jeshi, wakiinua sauti zao kwa sifa kwa Mungu kwa sababu ya ahadi ya ushindi. {VSS 452.3}

Ilikuwa njia ya pekee ya kwenda vitani dhidi ya jeshi la adui—kumtukuza Bwana kwa nyimbo na kumwinua Mungu wa Israeli. Huu ulikuwa wimbo wao wa vita. Walikuwa na uzuri wa utakatifu. Ikiwa watu wa Mungu leo wangetumia muda mwingi zaidi kumsifu Mungu, tumaini, ujasiri na imani vingezidi kuongezeka. Je, jambo hilo lisingeimarisha mikono ya mashujaa wanaosimama leo kuitetea kweli? —[Manabii na Wafalme, 201, 202](#). {VSS 453.1}

Rekodi ya Nyimbo za Walawi Katika Kitabu cha Nehemia—Walawi, katika wimbo wao uliorekodiwa na Nehemia, waliimba wakisema: “*Wewe Ndiwe Bwana, Wewe peke yako; Wewe ulifanya mbingu, mbingu za mbingu, pamoja na jeshi lake lote, dunia na vyote vilivyomo, bahari na vitu vyote vilivyomo, Nawe unavihifadhi vitu hivi vyote*” [Nehemia 9:6](#).—[Wazee wa Imani na Manabiis, 115](#). {VSS 453.2}

Ulinzi wa Mungu kwa Israeli—Wimbo wa Walawi uliorekodiwa na Nehemia unaonyesha kwa uwazi jinsi Mungu alivyowatunza watu wa Israeli hata katika miaka yao ya kukataliwa na kufanywa mateka. Waliimba wakisema: “*Wewe kwa wingi wa rehema Zako hukuwaacha jangwani; nguzo ya wingu haikuwaondokea wakati wa mchana, ili kuwaongoza njiani; wala nguzo ya moto haikuondoka wakati wa usiku, ili kuwapa mwanga na kuwaonyesha njia watakayoiendea. Ukawapa na roho Yako mwema ili kuwaelimisha, wala hukuwanyima mana vinywani mwao, tena ukawapa maji kwa ajili ya kiu yao. Naam, muda wa miaka arobaini uliwaruzuku jangwani, wasihitaji kitu; nguo zao hazikuchakaa, wala miguu yao haikuvimba.*”—[Nehemia 9:19-21](#).—[Wazee wa Imani na Manabii, 406, 407](#). {VSS 453.3}

Sifa Katika Nyakati za Ezra—Katika nyakati za Ezra, baada ya ukuta wa Yerusalemu kujengwa upya, wakati wa Sikukuu ya Tarumbeta, kusanyiko kubwa la watu lilisimama huku likiinua mikono yao kuelekea mbinguni. Ndipo wakainua wimbo huu wa sifa: “*Na lihimidiwe Jina Lako tukufu, lililotukuka kuliko baraka zote na sifa zote. Wewe ndiwe Bwana, Wewe peke yako; Wewe ulifanya mbingu, mbingu za mbingu, pamoja na jeshi lake lote, dunia na vyote vilivyomo, bahari na vitu vyote vilivyomo, Nawe unavihifadhi vitu hivi vyote; na jeshi la mbinguni*

lakusujudu wewe.” —[Nehemia 9:5, 6](#). Baada ya wimbo huo wa sifa kumalizika, viongozi wa kusanyiko waliwasimulia watu historia ya Israeli, wakionyesha jinsi wema wa Mungu ulivyokuwa mkuu kwao na jinsi walivyokuwa wamemjibu kwa kutokuwa na shukrani. —[Manabii na Wafalme, 666](#). {VSS 454.1}

Nyimbo Katika Safari za Kwenda Yerusalemu—Safari ya kwenda Yerusalemu, wakati familia za Kiyahudi zilipokwenda kuhudhuria sikukuu, ilikuwa safari ya furaha kubwa. Walitembea kwa mtindo rahisi wa kifamilia wa kale, wakiwa katikati ya uzuri wa majira ya kuchipua, utajiri wa katikati ya kiangazi, au fahari ya vuli iliyokomaa. Wakiwa na sadaka za shukrani, walikwenda kukutana na Mungu katika maskani Yake takatifu; kuanzia mzee mwenye mvi hadi mtoto mdogo. Walipokuwa safarini, waliwasimulia watoto wa Kiebrania matukio ya zamani na hadithi ambazo wazee kwa vijana walizipenda sana. Nyimbo zilizowatia moyo wakati wa safari za jangwani ziliimbwa. Amri za Mungu ziliimbwa kwa sauti ya pamoja, na zikiwa zimeunganishwa na baraka za mazingira ya asili pamoja na ushirika mwema wa wanadamu, zilibaki milele katika kumbukumbu za watoto na vijana wengi. —[Elimu, 42](#). {VSS 454.2}

Muziki Katika Sikukuu ya Vibanda—Kwa nyimbo takatifu na shukrani, waabudu walisherehekea sikukuu hiyo. Muda mfupi kabla ya sikukuu hiyo ilikuwa Siku ya Upatanisho, ambapo baada ya watu kukiri dhambi zao, walitangazwa kuwa wamepatanishwa na Mungu. Hivyo, njia iliandaliwa kwa ajili ya furaha ya sikukuu. Waliimba kwa ushindi: *“Haleluya. Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema, Kwa maana fadhili Zake ni za milele.”*—[Zaburi 106:1](#). Aina mbalimbali za muziki, zikichanganyika na sauti za furaha za **Hosana**, ziliambatana na uimbaji wa pamoja. {VSS 455.1}

Hekalu lilikuwa kitovu cha furaha hiyo kuu. Hapa ndipo palipofanyika huduma zenye fahari za dhabihu. Pande zote mbili za ngazi nyeupe za marumaru za jengo takatifu, kwaya ya Walawi ilisimamia huduma ya nyimbo. Umati mkubwa wa waabudu, wakiwa wamebeba matawi ya mitende na mihadasi, uliungana katika wimbo huo na kurudia kiitikio. Kisha sauti hizo zikaendelea kusikika kutoka kwa waimbaji waliokuwa karibu na wale waliokuwa mbali, mpaka vilima vilivyoizunguka Yerusalemu vikajaa sauti za sifa kwa Mungu. {VSS 455.2}

Usiku ulipofika, hekalu na ua wake viliangaza kwa mwanga wa taa nyingi. Muziki, kupeperusha matawi ya mitende, sauti za furaha za Hosana, umati mkubwa

wa watu uliokuwa umeangaziwa na mwanga wa taa zilizoning'inizwa, mavazi ya makuhani na ukuu wa sherehe hizo, vyote vilifanya tukio lililowagusa sana mioyo ya waliolishuhudia. Hata hivyo, sherehe iliyovutia zaidi na iliyosababisha furaha kubwa zaidi ilikuwa ile iliyokumbusha tukio fulani katika safari ya jangwani. {VSS 455.3}

Alfajiri ilipoanza, makuhani walipiga tarumbeta zao za fedha kwa mlio mrefu na mkali. Tarumbeta hizo zilijibiwa na vilio vya furaha vya watu kutoka katika vibanda vyao, na sauti hizo zikasikika katika vilima na mabonde, zikitangaza mwanzo wa siku ya sikukuu. Kisha kuhani alichota maji kutoka mto Kidroni na kuyainua juu huku tarumbeta zikipigwa. Akapanda ngazi pana za hekalu kwa hatua za polepole na zenye mpangilio, akifuata mwendo wa muziki huku akiimba: *“Miguu yetu imesimama Ndani ya malango yako, Ee Yerusalemu.”*—[Zaburi 122:2](#). {VSS 456.1}

Alipeleka chombo cha maji madhabahuni palipokuwa katikati ya ua wa makuhani. Hapo palikuwa na mabakuli mawili ya fedha, huku kuhani akiwa amesimama kila upande. Maji yaliwekwa katika moja na divai katika lingine; kisha yaliyomo katika mabakuli hayo yalitiririka kupitia mfereji uliunganishwa na Kidroni na kuelekea Bahari ya Chumvi. Kitendo hiki cha kuonyesha maji yaliyowekwa wakfu kilikuwa mfano wa chemchemi iliyotoka mwambani kwa amri ya Mungu ili kukata kiu ya wana wa Israeli. Ndipo nyimbo za furaha zilisikika: *“Bwana YEHOVA ni nguvu zangu na wimbo wangu” “Basi, kwa furaha mtateka maji katika visima vya wokovu.”*—[Isaya 12:2, 3](#).—*Tumaini la Vizazi Vyote*, [448, 449](#). {VSS 456.2}

Wimbo Wakati Yesu Alipoingia Yerusalemu kwa Ushindi—Kutoka katika umati mkubwa uliokusanyika kuhudhuria Pasaka, maelfu walitoka kwenda kumpokea Yesu. Walimpokea kwa kupeperusha matawi ya mitende na kwa kuimba nyimbo takatifu za sifa. —*Tumaini la Vizazi Vyote*, [571](#). {VSS 456.3}

Sifa Katika Meza ya Bwana/Pasaka—Kabla ya kuondoka katika chumba cha juu, Mwokozi aliwaongoza wanafunzi Wake katika wimbo wa sifa. Sauti Yake

haikusikika katika nyimbo za huzuni au maombolezo, bali katika sauti za shangwe za nyimbo za sifa za Pasaka.—[Zaburi 117](#).—*Tumaini la Vizazi Vyote*, [672](#). {VSS 457.1}

SURA YA 72—WIMBO KATIKA UFUFUO NA KUPAA KWA KRISTO

Karibu ya Mbinguni kwa Bwana Aliyefufuka—Wakati wa ufufuo wa Kristo, wale askari waliokuwa wakilinda kaburi Lake waliona mwangaza wa malaika ukiangaza usiku huo, nao wakasikia wenyeji wa mbinguni wakiimba kwa furaha kuu na kwa sauti za ushindi. —*Tumaini la Vizazi Vyote*, [780](#) {VSS 458.1}

Nyimbo za Jeshi la Malaika—Wale askari waliokuwa wakilinda kaburi walimwona Yesu akitoka katika kaburi, nao wakamsikia akitangaza juu ya kaburi lililopasuka: *“Mimi Ndimi huo ufufuo, na uzima.”* Alipotoka kwa ukuu na utukufu, jeshi la malaika lilimsujudia Mkombozi kwa ibada na kumkaribisha kwa nyimbo za sifa. —*Tumaini la Vizazi Vyote*, [780](#) {VSSsw 458.2}

Sifa kwa Kristo Katika Kupaa Kwake—Mbingu yote ilikuwa ikingojea kumkaribisha Mwokozi katika makao ya kifalme ya mbinguni. Alipopaa, Kristo aliongoza njia, na kundi la mateka waliowekwa huru wakati wa ufufuo Wake lilimfuata. Jeshi la mbinguni, likiwa na shangwe, sauti za sifa na nyimbo za mbinguni, liliandamana na msafara huo wa furaha. {VSS 458.3}

Walipokaribia mji wa Mungu, malaika waliokuwa wakiwasindikiza walitoa mwito: *“Inueni vichwa vyenu, enyi malango; inueni juu, enyi milango ya milele, naye Mfalme wa utukufu ataingia.”* {VSS 458.4}

Kwa furaha, walinzi waliokuwa wakisubiri walijibu: *“Ni nani huyo Mfalme wa utukufu?”* Hawaitikia hivyo kwa sababu hawakumjua, bali kwa sababu walitamani kusikia jibu la sifa kuu: *“Bwana Mwenye nguvu na hodari, Bwana hodari katika vita. Inueni vichwa vyenu, enyi malango; naam, viinueni juu, enyi milango ya milele, Naye Mfalme wa utukufu ataingia.”* {VSS 459.1}

Tena ulisikika mwito: *“Ni nani huyo Mfalme wa utukufu?”* Kwa maana malaika hawachoki kulisikia jina Lake likitukuzwa. Malaika waliokuwa wakimsindikiza wakajibu: *“Bwana wa majeshi; Yeye Ndiye Mfalme wa utukufu.”* ([Zaburi 24:7–10](#)) {VSSsw 459.2}

Ndipo malango ya mji wa Mungu yakafunguliwa kwa upana, na umati wa malaika ukaingia kupitia malango hayo kwa mlio wa muziki wa furaha kuu. {VSSsw 459.3}

Kristo alimtolea Mungu mganda wa kwanza wa mavuno, pamoja na wale waliofufuliwa pamoja Naye, wakiwa wawakilishi wa umati mkubwa wa wale watakaotoka makaburini wakati wa kuja Kwake mara ya pili. Kristo Alimsogelea Baba, ambaye hufurahia juu ya mwenye dhambi mmoja anayetubu na kushangilia juu yake kwa nyimbo. {VSSsw 459.4}

Kwa furaha isiyoweza kusemwa, watawala, mamlaka na nguvu zilitambua ukuu wa Mfalme wa uzima. Jeshi la malaika lilimsujudia, huku sauti ya shangwe ikijaza nyua zote za mbinguni: *“Astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, kuupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka.”* ([Ufunuo 5:12](#)) {VSSsw 459.5}

Nyimbo za ushindi ziliungana na muziki wa vinubi vya malaika, hata mbingu ikaonekana kufurika kwa furaha na sifa. Upendo ulikuwa umeshinda. Aliyepotea alikuwa amepatikana. Mbingu ilijaa sauti zilizoinuka kwa utukufu mkuu zikisema: *“Baraka na heshima na utukufu na uweza una Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele.”* ([Ufunuo 5:13](#)) —*Tumaini la Vizazi Vyote, 832–835* {VSSsw 459.6}

SURA YA 73—WIMBO KATIKA PAMBANO KUU LA MWISHO

Wimbo wa Malaika Sasa— *“Atoaye dhabihu za kushukuru, Ndiye anayenitukuza”* asema Muumba (*Zaburi 50:23*). Wakazi wote wa mbinguni huungana katika kumsifu Mungu. Tujifunze sasa wimbo wa malaika, ili tupate kuuimba tutakapoungana na safu zao zenye kung’aa. Tuseme pamoja na mtunga-zaburi: *“Nitamsifu Bwana muda ninaoishi, Nitamwambia Mungu wangu ningali ni hai; Watu na wakushukuru, Ee Mungu, Watu wote na wakushukuru.”* (*Zaburi 146:2; 67:5*). —Wazee wa Imani na Manabii, uk. 289, 290. {VSSsw 461.1}

Katika Vivuli vya Dhiki—Katika mwanga kamili wa mchana na huku akisikia sauti za ndege wengine wakiimba, ndege aliyefungiwa ndani ya kizimba hawezi kuimba wimbo ambao bwana wake anataka ajifunze. Huokota sehemu ndogo ya wimbo huu na mlilo wa ule mwingine, lakini kamwe haujifunzi wimbo mmoja kamili na ulio timilifu. Lakini bwana wake hufunika kizimba hicho na kukiweka mahali ambapo ndege huyo atasikia wimbo mmoja anaapaswa kuimba. Katika giza, hujaribu tena na tena kuimba wimbo huo mpaka anapoujifunza kikamilifu, kisha huanza kuutoa kwa sauti yenye upatanifu mkamilifu. Baadaye ndege huyo hutolewa nje, na tangu wakati huo huweza kuimba wimbo huo hata akiwa katika mwanga. *Hivyo ndivyo Mungu anavyowafundisha watoto Wake. Yeye Ana wimbo anaotaka kutufundisha; nasi tunapojifunza huu wimbo katikati ya vivuli vya mateso, tutaweza kuuimba milele baadaye.* —Huduma ya Uponyaji, uk. 472. {VSSsw 461.2}

Tumaini Katika Mgogoro Mkuu wa Mwisho—Katikakati ya vivuli vinavyozidi kuwa vizito vya mgogoro mkuu wa mwisho wa dunia, nuru ya Mungu itaangaza kwa uangavu zaidi, na wimbo wa tumaini na imani utasikika kwa sauti iliyo wazi zaidi na yenye ukuu mkuu. —Elimu, uk. 166. {VSSsw 462.1}

Wimbo wa Ushindi Wakati wa Kuja kwa Kristo—Kupitia uwazi uliopo katika mawingu, wakati wa mwisho ambapo watu wa Mungu watakombolewa,

linaonekana nyota yenye mwangaza mkubwa ambao huongezeka mara nne zaidi kwa sababu ya tofauti yake na giza linaloizunguka. Nyota hiyo huleta ujumbe wa tumaini na furaha kwa waaminifu, lakini huleta ukali na ghadhabu kwa wavunjaji wa sheria ya Mungu. Wale walioita kila kitu kwa ajili ya Kristo sasa wako salama, wakiwa wamefichwa kana kwamba wako katika siri ya banda la Bwana. Wamejaribiwa, na mbele ya ulimwengu pamoja na wale waliodhihaki Kweli, wameonyesha uaminifu wao kwa Yeye aliyekufa kwa ajili yao. {VSSw 462.2}

Mabadiliko ya ajabu yamewapata wale walioshikilia uaminifu wao hata walipokabiliwa na kifo. Ghafla wamekombolewa kutoka katika utawala wa giza na wa kutisha wa wanadamu waliobadilishwa kuwa kama mashetani. Nyuso zao, ambazo muda mfupi uliopita zilikuwa zimepauka, zenye huzuni na hofu, sasa zinaangaza kwa mshangao, imani na upendo. Sauti zao zinainuka katika wimbo wa ushindi: *“Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, Msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso. Kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi, Ijapotetemeka milima moyoni mwa bahari. Maji yake yajapovuma na kuumuka, Ijapopepesuka milima kwa kiburi chake.”* (Zaburi 46:1–3). —Pambano Kuu, uk. 638, 639. {VSSw 462.3}

SURA YA 74—NYIMBO ZA WALIOKOMBOLEWA

Mwonekano wa Awali wa Mbinguni—Kisha nikaonyeshwa utukufu wa mbinguni na hazina iliyowekwa kwa ajili ya waaminifu. Kila kitu kilikuwa cha kupendeza na chenye utukufu. Malaika waliimba wimbo mtamu, kisha wakaacha kuimba na kuvua taji zao vichwani mwao, wakazitupa zikiwa zinameremeta chini ya miguu ya Yesu

mpendwa. Kwa sauti zao zenye kupendeza waliita kwa furaha: **“Utukufu, Haleluya!”** Niliungana nao katika nyimbo zao za kumsifu na kumheshimu Mwana-Kondoo; na kila nilipofungua kinywa changu ili kumsifu, nilihisi utukufu usioelezeka uliokuwa umenizunguka. —[Maandiko ya Awali, 66](#). {VSSsw 463.1}

Nyimbo za Watakatifu—Sisi sote tulipaza sauti tukisema: “Gharama yoyote kwa ajili ya kuipata Mbingu ni ndogo sana! Heaven is Cheap Enough” Kisha tukavipiga vinubi vyetu vya utukufu, na kufanya matao ya mbinguni yasikike kwa sauti ya shangwe. —[Maandiko ya Awali, 17](#). {VSSsw 463.2}

Nyimbo za Wana wa Mungu—Viumbe vyote vya asili, katika uzuri wake usio na kifani, vitamtolea Mungu sifa na ibada. Dunia itajazwa na nuru ya mbinguni. Nuru ya mwezi itakuwa kama nuru ya jua, na nuru ya jua itakuwa mara saba zaidi ya ilivyo sasa. Miaka itaendelea kupita katika furaha. Juu ya mandhari hiyo, nyota za asubuhi zitaimba pamoja, na wana wa Mungu watapiga kelele kwa shangwe, huku Mungu na Kristo wakiungana kutangaza: “dhambi haitakuwapo tena, wala mauti haitakuwapo tena.” [Huduma ya Uponyaji, 506](#). {VSSsw 463.3}

Kwaya ya Waliokombolewa na Malaika—Simama katika kizingiti cha milele na usikie makaribisho yenye neema yanayotolewa kwa wale ambao katika maisha haya walishirikiana na Kristo, wakiona kuwa ni pendeleo na heshima kuteseka kwa ajili Yake. Pamoja na malaika, watatupa taji zao chini ya miguu ya Mkombozi, wakisema: *“Astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, kuupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka.... heshima na utukufu na uweza una Yeye Aketiye juu ya kiti cha enzi, na Yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele.”* (Ufunuo 5:12, 13). {VSSsw 464.1}

Huko waliokombolewa watawasalimu wale waliowaelekeza kwa Mwokozi aliyeinuliwa. Wataungana katika kumsifu Yeye aliyekufa ili wanadamu waweze kupata uzima unaolingana na uzima wa Mungu. Mapambano yatakuwa yamekwisha; mateso yote na migogoro yote itakuwa imekoma. Nyimbo za ushindi zitajaza mbingu yote, huku waliokombolewa wakisimama kuzunguka kiti cha enzi cha Mungu. Wote watajiunga katika wimbo wa furaha: *“Anastahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, Ambaye ametukomboha kwa ajili ya Mungu.”* —[Huduma ya Uponyaji, 506, 507](#). {VSSsw 464.2}

Wimbo wa Musa na Mwana-Kondoo—Wimbo huu pamoja na ukombozi mkuu unaokumbuka, uliacha alama isiyoweza kufutika katika kumbukumbu ya watu wa Kiebrania. Tangu kizazi hadi kizazi, uliimbwa na manabii pamoja na waimbaji wa Israeli, ukishuhudia kwamba Yehova Ndiye nguvu na ukombozi wa wale wanaomtumaini. Hata hivyo, wimbo huu hauwahusu watu wa Kiyahudi pekee; bali unaelekeza mbele kwenye kuangamizwa kwa maadui wote wa haki na ushindi wa mwisho wa Israeli wa Mungu. Mtume Yohana katika kisiwa cha Patmo aliona umati mkubwa uliovikwa mavazi meupe, ambao *“walikuwa wamepata ushindi,”* wakisimama juu ya *“bahari ya kioo iliyochanganyika na moto,”* wakiwa na *“vinubi vya Mungu.”* Nao waliimba *“wimbo wa Musa, mtumishi wa Mungu, na wimbo wa Mwana-Kondoo.”* (Ufunuo 15:2, 3). **{VSSw 464.3}**

“Ee Bwana, kutukuza usitutukuze sisi, Bali ulitukuze Jina Lako, Kwa ajili ya fadhili Zako, Kwa ajili ya uaminifu Wako.” (Zaburi 115:1). Huo ndio uliokuwa moyo wa wimbo wa ukombozi wa Israeli, na huo ndio moyo unaopaswa kukaa ndani ya wote wanaompenda na kumcha Mungu. Katika kutuokoa kutoka katika utumwa wa dhambi, Mungu ametufanyia ukombozi mkuu kuliko ule aliowafanyia Waebrania walipovuka Bahari ya Shamu. Kama jeshi la Waebrania lilivyomsifu Bwana kwa moyo, nafsi na sauti, vivyo hivyo nasi tunapaswa kumsifu kwa ajili ya *“matendo Yake ya ajabu kwa wanadamu.”* Wale wanaotafakari rehema kuu za Mungu na wasiopuuzwa hata zawadi Zake ndogo, watajivika mshipi wa furaha na kufanya mioyoni mwao muziki wa sifa kwa Bwana. **{VSSw 465.1}**

Baraka za kila siku tunazopokea kutoka mkononi mwa Mungu, na zaidi ya yote kifo cha Yesu kilichofungua njia ya furaha na uzima wa milele kwetu, vinapaswa kuwa mada ya shukrani ya kudumu. Ni huruma kuu na upendo usio na kifani kiasi gani Mungu ametuonyesha sisi wenye dhambi waliopotea, kwa kutuunganisha Naye ili tuwe hazina Yake ya pekee! Ni dhabihu kubwa kiasi gani iliyotolewa na Mkombozi wetu ili tuweze kuitwa watoto wa Mungu! Tunapaswa kumsifu Mungu kwa tumaini lenye baraka lililowekwa mbele yetu katika mpango mkuu wa ukombozi, kwa urithi wa mbinguni na kwa ahadi Zake nyingi; tunapaswa kumsifu kwa sababu Yesu Yu hai ili atuombee. —**Wazee wa Imani na Manabii, 289.****{VSSw 465.2}**

Mfalme katika Uzuri Wake—Wale ambao, bila kujali mambo mengine yote, hujiweka mikononi mwa Mungu ili wawe na kufanya yote anayowataka,

watamwona Mfalme katika uzuri Wake. Watatazama mvuto Wake usio na kifani, na huku wakipiga vinubi vyao vya dhahabu, wataijaza mbingu yote kwa muziki wa utukufu na nyimbo za kumsifu Mwana-Kondoo. —[Evangelism, 503](#). {VSSw 466.1}

Nyimbo za Sifa za Waliobarikiwa—Malaika wanatazamia kwa hamu kubwa ushindi wa mwisho wa watu wa Mungu, wakati maserafi, makerubi, na *“elfu kumi mara elfu kumi, na maelfu kwa maelfu”* watakapongeza sauti zao katika nyimbo za wenye baraka na kusherehekea ushindi wa kazi ya upatanishi iliyofanikisha ukombozi wa mwanadamu. —[Maisha Yangu Leo, 307](#). {VSSw 466.2}

Mtende wa Mshindi na Kinubi Chenye Kung'aa—Katika kila mkono utawekwa mtende wa ushindi na kinubi kinachong'aa. Kisha malaika wakuu watakapotoa sauti ya kuongoza, kila mkono utapiga nyuzi za kinubi kwa ustadi, na kuamsha muziki mtamu wenye sauti zenye upatanifu mkubwa. Furaha isiyoweza kusemeka itaijaza kila moyo, na kila sauti itainuliwa katika sifa za shukrani: *“Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu Yake, na kutufanya kuwa ufalme, na makuhani kwa Mungu, Naye ni Baba Yake; utukufu na ukuu una Yeye hata milele na milele.”* (Ufunuo 1:5, 6). —[Pambano Kuu, 646](#). {VSSw 466.3}

Sauti za Muziki Mbinguni—Nabii alisikia sauti ya muziki huko, na wimbo wenye uzuri mkubwa kiasi kwamba, isipokuwa katika maono ya Mungu, hakuna sikio la mwanadamu lililowahi kuusikia wala akili ya mwanadamu kuufikiria. *“Na hao waliokombolewa na Bwana watarudi, watafika Sayuni wakiimba; na furaha ya milele itakuwa juu ya vichwa vyao; nao watapata kicheko na furaha, huzuni na kuugua zitakimbia.”* (Isaya 35:10). *“Furaha na kicheko zitaonekana ndani yake, kushukuru, na sauti ya kuimba.”* (Isaya 51:3). *“Waimbao na wachezao na waseme, Visima vyangu vyote vimo mwako.”* (Zaburi 87:7). *“Hawa watainua sauti zao, watapiga kelele; kwa sababu ya utukufu wa Bwana.”* (Isaya 24:14). —Manabii na Wafalme, [730](#). {VSS 467.1}

Wimbo wa Wale 144,000—Hawa ndio wale wanaosimama juu ya Mlima Sayuni pamoja na Mwana-Kondoo, wakiwa na Jina la Baba limeandikwa katika vipaji vya nyuso zao. Wanaimba wimbo mpya mbele ya kiti cha enzi; wimbo ambao hakuna mtu awezaye kuujifunza isipokuwa wale 144,000 waliokombolewa kutoka duniani. —Manabii na Wafalme, [591](#). {VSS 467.2}

Shangwe za Sifa katika Dunia Mpya—Juu ya kilele cha Mlima wa Mizeituni miguu Yake itasimama atakapokuja tena. Hatakuja tena kama Mtu wa huzuni, bali kama Mfalme mtukufu na mwenye ushindi. Atasimama juu ya Mlima wa Mizeituni, huku haleluya za Waebrania zikichanganyika na hosana za Mataifa, na sauti za waliokombolewa kama jeshi kubwa zikiongeza mwito wa ushindi: “*Mvikeni taji, Mfalme wa wote!*” —*Tumaini la Vizazi Vyote*, [830](#). {VSSsw 467.3}

Sifa Kutoka Sabato Moja Hadi Nyingine—Wakati kutakapokuwa na “*kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu.*” (*Matendo 3:21*), Sabato ya uumbaji, siku ambayo Yesu alipumzika katika kaburi la Yusufu, itaendelea kuwa siku ya pumziko na furaha. Mbingu na dunia vitaungana katika sifa, na “kutoka Sabato hata Sabato” (*Isaya 66:23*), mataifa ya waliokombolewa watasujudu katika ibada ya furaha kwa Mungu na Mwana-Kondoo. —*Tumaini la Vizazi Vyote*, [769, 770](#). {VSS 468.1}

Kwaya ya Milele ya Sifa—Miaka ya milele inapoendelea kupita, italeta mafunuo mengi zaidi yenye utukufu kuhusu Mungu na Kristo. Kadiri maarifa yatakavyoongezeka, ndivyo upendo, heshima na furaha vitakavyoongezeka. Kadiri wanadamu watakavyojifunza zaidi juu ya Mungu, ndivyo watakavyostaajabia zaidi tabia Yake. Yesu atakapowafunulia waliokombolewa utajiri wa ukombozi na mafanikio ya ajabu katika pambano kuu dhidi ya Shetani, mioyo yao itajawa na kujitoa kwa bidii zaidi. Kwa furaha isiyosemeka watapiga vinubi vyao vya dhahabu, na *elfu kumi mara elfu kumi pamoja na maelfu kwa maelfu ya sauti* zitaungana kuinua kwaya kuu ya sifa: {VSSsw 468.2}

“Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya nchi ya juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake, nalivisikia, vikisema, Baraka na heshima na utukufu na uweza una Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na Yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele.” (*Ufunuo 5:13*). {VSSsw 468.3}

Pambano kuu limekwisha. Dhambi na wenye dhambi hawapo tena. Ulimwengu wote umetakaswa. Mshindo mmoja wa upatanifu na furaha unarindima katika uumbaji wote mpana. Kutoka Kwake aliyeumba vitu vyote hutoka uzima,

Nhandi Masunga na Grace Momadi Masaka-Jersey 2026 July

nuru na furaha katika maeneo yote ya anga lisilo na mipaka. Kuanzia chembe ndogo kabisa hadi ulimwengu mkubwa zaidi, vitu vyote vilivyo hai na visivyo hai, katika uzuri usiofunikwa na kivuli chochote na furaha kamilifu, vinatangaza: ***“Mungu ni upendo.”*** — **Pambano Kuu. {VSSw 469.1}**